


# HISTORIA KUU YA AFRIKA.

Juzuu  
Lililofupishwa

III Afrika kuanzia Karne ya  
Saba hadi ya Kumi na Moja

MHARIRI I. HRBEK





Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (UNESCO)

---

Historia Kuu ya Afrika · III

---

# Afrika Kuanzia Karne ya Saba Hadi ya Kumi na Moja

---

MHARIRI I. HRBEK

---

Juzuu Lililofupishwa

TUKI . CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM . UNESCO

## Jina la Asili: GENERAL HISTORY OF AFRICA, VOL III

© UNESCO 1999

ISBN 9976 911 32 7

*Maelezo yaliyotolewa na uwasilishaji wa matini zote kwenye chapisho hili haumaanishi maoni yoyote yale kwa upande wa UNESCO kuhusu sheria ya nchi yoyote ile, mji au eneo au mamlaka yake, au kuwekea mipaka eneo lolote lile.*

*Waandishi wanahusika na uteuzi na uwasilishaji wa taarifa za kweli zilizopo kwenye kitabu hiki na kwa maoni yaliyoelezewa ndani, ambayo si lazima yawe yale ya UNESCO na hayalifanyi Shirika liwajibike.*

*Toleo la Tafsihi ya Kiswahili limechapishwa kwa msaada wa kifedha wa UNESCO.*

---

## Historia Kuu ya Afrika · III

---

# Afrika Kuanzia Karne ya Saba Hadi ya Kumi na Moja

---

### Toleo Lililofupishwa

#### UNESCO Historia Kuu ya Afrika

- Juzuu I**                    *Mbinu na Historia ya Awali ya Afrika*  
Mhariri **J. Ki-Zerbo**
- Juzuu II**                    Staarabu za Kale za Afrika  
Mhariri **G. Mokhtar**
- Juzuu III**                    Afrika kuanzia Karne ya Saba hadi ya Kumi na Moja  
Mhariri **I. Hrbek**
- Juzuu IV**                    Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Mbili hadi ya Kumi na Sita  
Mhariri **J. Ki-Zerbo na D.T. Niane**
- Juzuu V**                    Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Sita hadi ya Kumi na Nane  
Mhariri **B.A. Ogot**
- Juzuu VI**                    Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Tisa hadi Miaka ya 1880  
Mhariri **J.F. Ade Ajayi**
- Juzuu VII**                    Afrika Chini ya Utawala wa Kigeni 1880 - 1935  
Mhariri **A. Adu Boahen**

### Toleo Lisilofupishwa la Jalada Jepesi

- Juzuu VIII**                    Afrika Kuanzia 1935  
Mhariri **A.A. Mazrui**  
Mhariri **Msaidizi C. Wondji**




Toleo lililofupishwa la  
**HISTORIA KUU YA AFRIKA YA UNESCO**

**Limechapishwa na:**

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI)  
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam  
S.L.P. 35110  
Dar es Salaam, Tanzania

Pamoja na:  
UNESCO Publishing  
7 Place de Fontenoy, 75700, Paris

Kimchapwa na kuchapwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha  
Dar es Salaam, S.L.P. 35110, Dar es Salaam, Tanzania.




## YALIYOMO

|   |       |
|---|-------|
| Dibaji na Amadou -Mahtar M'Bow aliyekuwa Mkurugenzi wa UNESCO (1974-87)   | vii   |
| Wasifu wa Mradi na B.A. Ogot, aliyekuwa Mwenyekiti, Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika | xii   |
| Maelezo ya Wendo  | xv    |
| Wanakamati wa Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika                                       | xvi   |
| Orodha na Wasifu wa Waandishi waliochangia kwenye juzuu kuu   | xviii |
|   |       |
| 1 Afrika katika muktadha wa historia ya dunia   | 1     |
| 2 Majilio ya uislamu na ustawi wa himaya ya waislamu  | 15    |
| 3 Maendeleo ya uislamu na kuenea kwake Barani Afrika  | 29    |
| 4 Uisilamu kama Mfumo wa kijamii katika Afrika kuanzia karene ya saba   | 47    |
| 5 Watu wa Sudan: Miguro ya watu   | 59    |
| 6 Wabantu na kuenea kwao  | 71    |
| 7 Misri kuanzia utamalaki wa Waarabu hadi mwisho wa dola ya wafatimi (1171)   | 82    |
| 8 Nubia ya kikristo katika kilele cha ustaarabu wake  | 99    |
| 9 Kutamalakiwa kwa Afrika ya Kaskazini na ukinzani wa Waberiberi  | 114   |
| 10 Uhuru wa Maghrib   | 125   |

---

|    |  |     |
|----|--|-----|
| 11 | <i>Dhimu ya jungwa la Sahara na wana Sahara katika mahusiano kati ya Kaskazini na Kusini</i> | 142 |
| 12 | <i>Kutokea kwa Wafatini</i>  | 158 |
| 13 | <i>Wanoravi</i>  | 171 |
| 14 | <i>Biashara na njia za biashara katika Afrika Magharibi</i>                                  | 186 |
| 15 | <i>Ukanda wa Chad kama njia panda</i>  | 214 |
| 16 | <i>Ukanda wa Guinea: hali ya jumla</i>   | 224 |
| 17 | <i>Ukanda wa Guinea: Watu waishio kati ya mlima Kameruni na Cote d'Ivoire</i>                | 237 |
| 18 | <i>Watu wa Guinea ya juu: kati ya Cote d'Ivoire na Kasamansi</i>                             | 256 |
| 19 | <i>Pembe ya Afrika</i>   | 268 |
| 20 | <i>Mahusiano ya Ethiopia na nchi za Kiislamu</i>   | 276 |
| 21 | <i>Pwani ya Afrika Mashariki na Visiwa vya Ngazija</i>                                       | 283 |
| 22 | <i>Bara la Afrika Mashariki</i>  | 295 |
| 23 | <i>Afrika ya Kati hadi Kaskakazini ya Mto Zambezi</i>  | 304 |
| 24 | <i>Kusini mwa Afrika hadi kusini ya Mto Zambezi</i>  | 315 |
| 25 | <i>Bukini</i>  | 324 |
| 26 | <i>Diaspora ya Waafrika katika Bara la Asia</i>  | 334 |
| 27 | <i>Mahusiano kati ya kanda mbalimbali za Afrika</i>  | 345 |
| 28 | <i>Afrika kuanzia karne ya saba hadi ya kumi na moja: karne tano za ujenzi</i>               | 356 |
|    | <i>Bibliografia</i>  |     |
|    | <i>Faharasa</i>  |     |

---



## Dibaji

**AMADOU - MAHTAR M'BOW**

*Mkurugenzi Mkuu wa Zamani wa UNESCO (1974-1987)*

---

Kwa muda mrefu, aina zote za uzushi na kashfa zilificha historia halisi ya Afrika kwa dunia nzima. Jamii za Kiafrika zilionekana kama jamii zisizoweza kuwa na historia. Licha ya kazi muhimu zilizofanywa na waasisi kama Leo Frobenius, Maurice Delafosse na Arturo Labriola tangu miongo ya mwanzoni mwa karne hii, wataalamu wengi wasio Waafrika hawakuweza kuondoa fikra fulani za awali walizozishikilia na wakadai kwamba kukosekana kwa kumbukumbu za maandishi kulifanya isiwezekane kufanya utafiti wowote wa kisayansi wa jamii kama hizo.

Ingawa tenzi za *Iliad* na *Odyssey* kwa usahihi zilichukuliwa kama kumbukumbu muhimu za historia ya Ugiriki ya kale, mapokeo simulizi ya Kiafrika, ambayo ndiyo kumbukumbu za pamoja za watu yanayounganisha matukio mengi yenye kuonyesha inaisha yao, yanakataliwa kuwa hayana thamani. Kwa kuandika historia ya sehemu kubwa ya Afrika, kumbukumbu tu zilizotumika ni zile za kutoka nje ya bara. Matokeo yake ni kuwa kile walichoandika kilitoa sura ambayo sio ya njia halisi walizopita Waafrika, bali zile ambazo waandishi walifikiria kuwa pengine ndimo walimopita. Kwa kuwa Enzi za Kati za Ulaya mara nyingi ndizo zilizotumika kama kipimo, njia za uzalishaji, mahusiano ya kijamii na asasi za kisiasa zilitazamwa tu kwa kurejelea zama za Ulaya.

Kwa hakika, waandishi hao walikataa kuwachukulia Waafrika kama waumbaji wa tamaduni za asili ambazo zilichanua na kudumu kwa karne nyingi katika ruwaza walizozibuni na ambazo wanahistoria hawawezi kuzibaini isipokuwa pale tu watakapokubali kuachana na mawazo yao ya kashfa.

Zaidi ya hayo, bara la Afrika halikutazamwa hata kidogo kama eneo moja kihistoria. Kinyume chake, mkazo uliwekwa kwenye kila kitu kilichoelekea kuhalalisha wazo kwamba ingawanyiko ulikuwepo toka zama za kale, kati ya 'Afrika ya weupe' na 'Afrika ya Weusi', kila upande ukiwa haujui kuwa kuna watu wa upande mwingine. Mara nyingi Sahara ilielezwa kama eneo lisilopitika na hivyo kuzuia kuchanganyikana kwa makundi ya kimbari na watu au mabadilishano ya bidhaa, imani, desturi na mawazo baina ya jamii zilizozidi kukua katika kila upande wa jangwa. Mipaka iliyofungwa kabisa iliwekwa baina ya staarabu za Misri ya Kale na Unubi na ile ya watu wa kusini mwa Sahara.

Ni kweli kwamba historia ya Afrika kaskazini mwa Sahara imehusishwa kwa karibu

mno na ile ya nchi za bonde la Bahari ya Mediterani kuliko ilivyokuwa kwa historia ya Afrika Kusini mwa Sahara, lakini hivi sasa inafahamika zaidi kwamba staarabu mbalimbali za bara la Afrika, pamoja na tofauti zao za lugha na tamaduni, zinawakilisha, kwa kiasi kikubwa au kidogo, michepuo ya kihistoria ya makundi ya watu na jamii yanayounganishwa na mahusiano ya karibu yenye umri wa karne nyingi.

Jambo jingine ambalo halikutendea haki utafiti wa uhakika wa Afrika ya Kale ilikuwa ni tokezaji wa ubaguzi wa rangi, ikiwa ni pamoja na biashara ya utunwa na ukoloni, ambao ulizaa dharau na kutokuelewana na hata kupata mashiko kiasi kwamba hisia hizo kuvuruga hata dhana za msingi za uandikaji historia. Tokea wakati dhana za "mweupe" na "mweusi" zilipoanza kutumika kama vitambulisho vya jumla na wakoloni, ambao walichukuliwa kuwa watu wa daraja la juu, ilibidi Waafrika waliotawaliwa wapambane dhidi ya utunwa wa kiuchumi na wa kisaikolojia. Waafrika walitambuliwa kwa rangi ya ngozi zao, walifanywa kama bidhaa, walitayarishwa ili kufanya kazi ngumu na hatimaye, katika fikra za waliowatawala, waliishia kuashiria mbari ya *kinegro* ambayo ilibuni wa na kudaiwa kuwa mbari duni. Ruwaza hii ya utambulisho wa uwongo ilidhalilisha historia ya watu wa Afrika katika fikra za watu kufikia kiwango cha historia ya kimbari, ambamo ufahamu wa ukweli wa kihistoria na kitamaduni ulikuwa lazima upotoshwe.

Hali imebadilika vya kutosha tangu mwishoni nwa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia na hasa toka nchi za Kiafrika zipate uhuru na kuanza kushiriki kikamilifu katika maisha ya jumuiya ya kimataifa na katika mabadilishano ambayo ndiyo sababu ya kuwepo kwake. Idadi kubwa ya wanahistoria wamejitahidi kukabili utafiti wa Afrika kwa mtazamo thabiti, usiopendelea na wa wazi kwa kutumia - pamoja na tahadhari zote - kumbukumbu halisi ya Kiafrika. Kwa kutumia haki yao ya kuchukua jitihada za kihistoria, Waafrika wenyewe wameihisi haja kubwa ya kuanzisha upya ukweli wa kihistoria wa jamii zao kwenye misingi thabiti.

Katika muktadha huu, umuhimu wa majuzuu liaya nane ya *Historia Kuu ya Afrika*, ambayo UNESCO inachapisha unajieleza wenyewe.

Wataalamu kutoka kwenye nchi nyingi ambao wanashughulikia mradi huu walianza kwa kuweka misingi ya kinadharia na ya kimbinu kwa ajili ya *Historia* hii. Wamekuwa katika hali ngumu ya kuutilia shaka urahisishaji mno wa historia ya Afrika unaotokana na dhana ya wazo la upande mmoja na finyu kuhusu historia ya dunia na kuanzisha upya taarifa za kweli kila ilipolazimu na ilipowezekana. Wamejitahidi kuonyesha bayana data za kihistoria zinazotoa picha ya wazi kuhusu mabadiliko ya watu tofauti wa Afrika katika mandhari yao maalum ya kijamii na kitamaduni.

Ili kuikabili kazi hii kubwa, ambayo ilifanywa kuwa yenye utata na ngumu zaidi na wingi wa kumbukumbu za aina nyingi na ukweli kwamba nyaraka zilikuwa zimesambaa sana, imebidi UNESCO iende hatua kwa hatua. Hatua ya kwanza, kuanzia 1963 hadi 1969, ilikuwa ni ya kukusanya nyaraka na kutayarisha mpango wa kazi. Migawanyo ya kazi ilifanyika uwandani na ilijunuiisha kampeni za kukusanya mapokeo simulizi, uundaji wa vituo vya nyaraka vya kikanda kwa ajili ya mapokeo simulizi, ukusanyaji wa miswada isiyochapishwa ya Kiarabu na Kiajemi (lugha za Kiafrika zilizoandikwa kwa hati za Kiarabu), utengenezaji wa orodha ya kumbukumbu za kale na urayarishaji wa

Kiongozi cha Kumbukumbu za Historia ya Afrika (*A guide to the sources of the History of Africa*) kutokana na hifadhi za nyaraka na maktaba ya nchi za Ulaya na baadaye kuchapishwa katika majuzuu kumi na moja. Zaidi ya hayo, mikutano iliandaliwa kuwawezesha wataalamu kutoka Afrika na mabara mengine kujadili masuala ya mbinu, na kuweka misingi wazi ya utekelezaji wa mradi huu baada ya uchunguzi makini wa kumbukumbu zilizokuwepo.

Hatua ya pili, ambayo ilianza 1969 hadi 1971, ilihusika na uwekaji sawa wa *Historia* na kuunganisha sehemu zake tofauti. Madhumuni ya mikutano ya kimataifa ya wataalamu iliyofanyika huko Paris mwaka 1969 na Addis Abbaba mwaka 1970, yalikuwa ni kuchunguza na kufafanua matatizo yaliyopo kwenye kusawidi na kuchapisha *Historia*; kuitoa historia hiyo katika majuzuu manane, kuwa na chapa kuu katika Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu, kuitafsiri katika lugha za Kiafrika kama vile Kiswahili, Kihausa, Kifulfulde, Kiyoruba au Kilingala, matarajio ya chapa za baadaye kwa Kijerumani, Kirusi, Kireno, Kihispania na Kichina na vilevile chapa zilizofupishwa kwa ajili ya umma mpana wa Kiafrika na Kimataifa.

Hatua ya tatu imehusu usawidi wenyewe na uchapishaji. Hatua hii ilianza kwa kuteuliwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi yenye wajumbe 39, theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja wasio Waafrika, ambayo ndiyo Kamati inayochukua jukumu la kitaaluma kwa *Historia* hii.

Mbinu iliyotumika ni ya taaluma fungamano na imekitwa kwenye mkabala wenye jiha za namna tofauti na kumbukumbu za aina nyingi. Ya kwanza miongoni mwa hizi ni akiolojia, ambayo ndiyo taaluma yenye ufumbuzi kwa mambo mengi ya historia ya tamaduni na staarabu za Afrika. Kutokana na akiolojia, inakubalika sasa kuwa Afrika huenda ndio ilikuwa chanzo cha wanadamu na eneo - katika kipindi cha Neolithi — la moja ya mapinduzi ya kitekuolojia ya kwanza katika historia. Akiolojia pia imeonyesha kwamba Misri ilikuwa mahali ambapo kulikuwa na mojawapo ya tamaduni za kale maarufu mno duniani. Lakini kumbukumbu nyingine muhimu sana ni mapokeo simulizi ambayo baada ya kudharauliwa kwa muda mrefu, sasa yameibuka kama chombo muhimu cha kuvumbulia historia ya Afrika, kwa kufanya iwezekane kufuatilia mijongeo ya watu wake mbalimbali katika kitambo cha nafasi na wakati, kuelewa maono ya Kiafrika kuhusu dunia kutokea ndani mwake na kuzingatia sifa za asili za amali ambamo ndimo zilipokitwa tamaduni na asasi za bara hili.

Tunaishukuru Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi inayosimamia *Historia Kuu ya Afrika*, na kwa Waandishi, Wahariri na Watunzi wa majuzuu mbalimbali na sura zake, kwa kuipatia mwanga mpya ukale wa Afrika katika uasilia na muundo wake mzima na kwa kuepukana na inadi katika utafiti wa masuala inulumu. Miongoni mwa masuala haya tunaweza kutaja: biashara ya watumwa, "jeraha lisilopona", ambayo ilisababisha mojawapo ya uhamishaji wa kikatili wa watu wengi katika historia ya mwanadamu, ambao ulifyonza uhai wa bara la Afrika na papo hapo kuchangia sana katika upanuzi wa uchumi na biashara huko Ulaya. Masuala mengine ni ukoloni na athari zake zote kwa idadi ya watu, uchumi, saikolojia na utamaduni, mahusiano kati ya Afrika kusini mwa Sahara na ulimwengu wa Kiarabu; na mwisho, harakati za kutokomeza ukoloni na za

ujenzi wa taifa ambazo ziliamsha akili na hisia za watu ambao baadhi yao wangali hai na pengine wangali wakiendesha harakati. Masuala haya yote yametajwa kwa kuzingatia ukweli na umakini aambazo ni sifa kubwa za *Historia* hii. Kwa kuchunguza ujuzi wetu wote wa Afrika, kutoa mawazo ya namna mbalimbali juu ya tamaduni za Afrika na kwa kutoa mtazamo inpya wa historia, *Historia* hii ina faida ya pekee ya kubainisha mwanga na kivuli na ya kudhihirisha wazi tofauti za maoni ambazo yawezekana zikawepo kati ya wataalamu.

Kwa kuonyesha kasoro katika mikabala ya kimbinu iliyotunika kwa muda mrefu katika kufanya utafiti kuhusu Afrika, *Historia* hii inadai kufanyike utafiti mpya na wenye uangalifu kwa maeneo ya matatizo ya namna mbili ya uandikaji wa historia na mahusiano yaliyopo kati yake, namna ambazo zinaunganishwa na uhusiano wa kutegemeana. Kama vile ilivyo kazi yoyote ya kihistoria yenye thamani, *Historia* hii inaandaa njia kwa ajili ya utafiti mwingi zaidi kuhusu mada za aina mbalimbali.

Ni kwa sababu hiyo kwamba Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi, ikishirikiana kwa karibu na UNESCO, ilianua kuanzisha tafiti za ziada katika kujaribu kuyaingia kwa kina masuala kadhaa yatakayoweza kueleweka kwa vipengele fulani vya kale ya Afrika. Matokeo ya tafiti hizo yanayochapishwa katika mfululizo wa *Mitaala na Nyaraka za UNESCO- Historia Kuu ya Afrika*<sup>1</sup> yatakuwa kijalizo muhimu kwa *Historia* hii kama zitakavyokuwa pia kazi zilizopangwa kufanyika juu ya vipengele vya historia ya taifa au ya majimbo ya Afrika.

*Historia Kuu* inatoa mwanga kuhusu umoja wa kihistoria wa Afrika na pia mahusiano ya bara hili na mabara mengine, hasa Amerika na Caribbean. Kwa muda mrefu mambo ya kibunifu ya vizazi vya Waafrika katika Amerika yalilundikwa pamoja na baadhi ya wanahistoria kama mkusanyo wa mambo mchanganyiko wa *Uafrika*. Kwa hakika huu si mtazamo wa wandishi wa *Historia* hii ambamo upinzani wa watumwa waliosafirishwa kwenda Amerika, kushiriki mfululizo na kwa wingi kwa vizazi vya Waafrika katika mapambano kwa ajili ya uhuru wa mwanzo wa Amerika na katika harakati za ukombozi wa kitaifa, yanatazamwa vizuri kama yalivyokuwa: utetezi wa dhati wa kujitambua, uliosaidia kuunda dhana ya kilimwengu ya jamii ya watu. Ingawa jambo hili linaweza likatofautiana katika sehemu mbalimbali ni dhahiri sasa kuwa namna za kuhisi, kufikiri, kuota ndoto na kutenda katika mataifa fulani ya magharibi zimeathiriwa na urithi wa Kiafrika. Urithi wa kitamaduni wa Kiafrika unaonekana kila mahali kutoka kusini mwa Marekani hadi kaskazini mwa Brazil, katika Caribbean na kwenye pwani ya Bahari ya Pacific. Katika sehemu fulani urithi huo ni insingi wa ubainisho wa kitamaduni wa baadhi ya vipengele muhimu kabisa vya watu.

*Historia* hii pia huonyesha dhahiri mahusiano ya Afrika na kusini mwa bara la Asia

<sup>1</sup> Majuzuu kumi na mbili yafuatayo yamekwishachapishwa katika mfululizo huu:

*Kukaliwa kwa Misri ya Kale na ufasiri wa hati za Kimeroi; Biashara ya Utumwa Afrika tangu karne ya kumi na tano hadi karne ya kumi na tisa; Mahusiano ya kihistoria kuuwa Bahari ya Hindi. Uandikaji wa historia wa Kusini mwa Afrika; Kuondoka kutoka ukoloni Afrika Kusini mwa Afrika na Pembe ya Afrika; Majina ya mbari na ya sura ya nchi ya Afrika; Mahusiano ya kihistoria kijamii na kitamaduni baina ya Waafrika weusi na Waarabu tangu 1935 hadi leo; Mbinu za historia ya saso ya Afrika; Afrika na vita vya Pili vya Dunia; Uelimishaji na uandikaji historia Afrika Kale ya Libya; Dhina ya Vyana vya Wanafuzi wa Kiafrika kwenye mabadiliko ya kisiasa na kijamii ya Afrika kuanzia 1900 hadi 1975.*

kupitia Bahari ya Hindi na michango ya Kiafrika katika staarabu nyinginezo kutokana na mabadilishano baina yake na maeneo hayo.

Nina hakika kuwa juhudi za watu wa Afrika za kutwaa kwa nguvu au kuimarisha uhuru wao, za kupata maendeleo yao na kutetea maumbile yao ya kitamaduni lazima zitokane na utambuzi wa kihistoria uliohuishwa, wenye kushabikiwa na wa kuzingatiwa na kila kizazi.

Kwa kuangalia historia ya maisha yangu, uzoefu nilioupata kama mwalimu na kama mwenyekiti, toka siku za awali za uhuru, wa tume za mwanzo zilizoundwa kurekebisha mitala ya historia na jiografia katika baadhi ya nchi za Afrika Magharibi na Kati, ulinifundisha jinsi ilivyokuwa muhimu kwa elimu ya vijana na kwa taarifa kwa watu wote kwa jumla, kuwa na vitabu vilivyochapishwa na wataalamu wenye ujuzi wa ndani kuhusu matatizo na matumaini ya Afrika na wenye uwezo wa kuyaelewa mambo yote ya bara zima.

Kutokana na sababu zote hizi, shabaha ya UNESCO itakuwa ni kuhakikisha kwamba hii *Historia Kuu ya Afrika* inasambazwa katika lugha nyingi na kutumiwa kama insingi wa kuandaa vitabu vya watoto, vitabu vya kiada na vipindi vya radio na televisheni. Hivyo vijana wakiwa watoto wa shule au wanafunzi, na watu wazima katika Afrika na penginele vinavyoelezea picha hiyo na vilevile kuelewa vizuri urithi wake wa kitamaduni na mchango wake katika maendeleo ya jamii ya watu. Kwa hivyo, *Historia* hii itaweza kuchangia katika ushirikiano bora wa kimataifa na mshikamano imara miongoni mwa watu katika matumaini yao ya kupata haki, maendeleo na amani. Hii, walau, ndio tumaini langu kubwa.

Kinachobakia ni kwa inimi kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi, mwandishi, wahariri wa majuzuu mbalimbali, waandishi na wale wote walioshiriki katika kazi hii kubwa. Kazi waliyoikamilisha na mchango walioutoa unadhihirisha jinsi watu wenye usuli tofauti lakini wenye moyo mmoja wa ridhaa na hamasa wa kuhudumia ukweli wa kilimwengu wanavyoweza, ndani ya kiuuzi cha kimataifa kilichotolewa na UNESCO, kufanikisha mradi wenye umuhimu mkubwa kisayansi na kitamaduni. Natoa shukrani pia kwa mashirika na serikali ambazo ukarimu wake umeiwezesha UNESCO kuchapisha *Historia* hii katika lugha tofauti na hivyo kuhakikisha kwamba itapata uzito inaostahiki duniani kote, na kwa jinsi hiyo kuhudumia jumuiya nzima ya kimataifa.



---

## Wasifu wa Mradi

B.A. OGOT<sup>1</sup>

Rais wa Zamani, Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi  
kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (1978-1983)

---

Mkutano Mkuu wa UNESCO katika Kikao chake cha 16 ulinwagiza Mkurugenzi Mkuu kushughulikia usawidi wa *Historia Kuu ya Afrika*. Kazi hii kubwa ya kutekeleza mradi ilikabidhiwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi ambayo ilianzishwa na Bodi ya Utendaji mnamo 1970. Kamati hii kwa mujibu wa Sheria iliyopitishwa na Bodi ya Utendaji ya UNESCO mnamo mwaka 1971, ina wajumbe thelathini na tisa (theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja ni watu wengine wasio Waafrika) wanaoishiriki kwa nafasi zao binafsi na kuteuliwa na Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO kwa kipindi ambacho Kamati itadumu.

Kazi ya kwanza ya Kamati ilikuwa ni kufafanua sifa kuu za kazi hii. Hizi zilifafanuliwa katika kikao cha kwanza cha Kamati kama ifuatavyo:

- (a) Ingawa lengo lake ni kiwango cha juu kabisa cha kisayansi, Historia hii hainuii kuwa timilifu na ni kazi ya usawidi inayoepukana na inadi. Katika hali zake nyingi, historia hii ni tamko juu ya matatizo yanayoonyesha hali ya sasa ya maarifa na mikondo mikuu ya utafiti, na haisiti kuonyesha hitilafu za mtazamo pale ambapo zipo. Kwa namna hii inaweka msingi kwa kazi za siku zijazo.
- (b) Katika kazi hii Afrika inatazamwa katika ujumla wake. Nia ni kuonyesha mahusiano ya kihistoria kati ya seheni zote za bara ambazo mara nyingi liutengwa katika kazi ambazo zimechapishwa hadi sasa. Mahusiano ya kihistoria ya Afrika na mabara mengine yanashughulikiwa ipasavyo kwa kuchanganuliwa kuzingatia mabadilishano baina yake na athari kutoka pande zote na kudhihirisha, katika mwanga halisi, mchango wa Afrika kwa historia ya mwanadamu.
- (c) Kwa mahususi, *Historia Kuu ya Afrika* ni historia ya mawazo na staarabu, jamii na asasi. Imetegemezwa kwenye vyanzo vingi vya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na mapokeo simulizi na namna za sanaa.
- (d) Kimsingi, *Historia* inatazamwa kutokea ndani. Ingawa ni kazi ya kitaalamu, pia kwa kadri kubwa, inaakisi kwa uaminifu jinsi waandishi wa Kiafrika

<sup>1</sup> Wakati wa Mikutano Mkuu wa Sita wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kwa ajili ya Kusawidi historia Kuu ya Afrika (uliiofanyika Brazaville Agosti 1983), uchunguzi wa wajumbe wanya ulifanyika na nafasi ya Profesa Ogot ilichukuliwa na Profesa Albert Adu Boahen.

wanavyotazama ustaarabu wao wenyewe. Pamoja na kuandaliwa kwa mtazamo wa kimataifa, na ikichota maarifa yote ya kisayansi yaliyopo wakati huu, yapaswa pia iwe kipengele muhimu kabisa katika utambuzi wa urithi wa Kiafrika na yapaswa kudhihirisha vipengele vinavojenga umoja barami. Juhudi hii ya kutazama mambo kutokea ndani ni sifa mpya ya mradi huu na pamoja na thamani yake ya kisayansi, inapaswa kuipatia mradi umuhimu wa kujadiliwa vipana. Kwa kuonyesha sura halisi ya Afrika, *Historia* inaweza, katika enzi iliyozama kwenye mapambano ya kiuchumi na kiufundi, kutoa dhana mahsusi ya amali za mwanadamu.

Kamati imeamua kuwasilisha kazi ya miaka milioni tatu ya historia ya Afrika katika majuzuu manane, kila moja likiwa na karibu kurasa mia nane za matini na mifano, picha, ramani na michoro.

Mhariri Mkuu akisaidiwa, pale inapolazimu, na wahariri wasaidizi wawili, ana jukumu la kuandaa kila juzuu. Wahariri wanachaguliwa na Kamati ama kutokana na wajumbe wake au kutoka nje kwa wingi wa theluthi mbili. Hawa wana jukumu la kuandaa majuzuu kulingana na maamuzi na mipango iliyokubaliwa na Kamati. Kuhusu mambo ya kisayansi wanaiwajibikia Kamati, au kati ya mikutano miwili ya Kamati watawajibikia Idara kuhusiana na maudhui ya majuzuu, miswada ya mwisho ya matini, mifano na kwa jumla, vipengele vote vya kisayansi na kiufundi vya *Historia*. Idara mwishowe luthibitisha muswada wa mwisho. Inapoonna kwamba inuswada uko tayari kuchapishwa inaukabidhi kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO. Hivyo, katika kipindi kati ya Vikao Viwili, Kamati au Idara huendelea kusimamia mradi.

Kila juzuu lina kama sura thelathini. Kila sura ni kazi ya mwandishi mkuu, akisaidiwa, inapolazimu, na mshiriki mmoja au wawili. Waandishi wanachaguliwa na Kamati kutokana na sifa na uzoefu wa kitaaluma. Waandishi wa Kiafrika hupewa upendeleo alimradi wawe na sifa zinazohitajika. Juhudi maalumu pia hufanywa kuhakikisha kwamba kila inapowezekana kanda zote za bara na vile vile kanda nyingine zenye historia au utamaduni unaohusiana na Afrika zinapata uwakilishi sawa miongoni mwa waandishi.

Pale nihariri wa juzuu anapothibitisha matini za sura, zinapelekwa kwa wajumbe wote wa Kamati kwa uhakiki. Zaidi ya hayo, matini ya nihariri wa juzuu inawasilishwa kwa uchunguzi, kwa Kamati ya Wasomaji, iliyoundwa ndani ya Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kulingana na uwezo wa wajumbe wake katika uwanja wa kitaaluma. Kamati ya Wasomaji inachanganua sura kimaudhui na kimuundo. Kisha Idara hutoa uthibitisho wa mwisho kwa miswada.

Utaratibu kama huu unaonekana mrefu na mgumu, unaonekana kuwa wa lazima kwani unatoa uthibitisho bora kabisa wa uhakika wa kisayansi wa *Historia Kuu ya Afrika*. Kwa hakika, kumewahi kuwepo matukio ambapo Idara imekataa miswada au kusisitiza ifanyiwe marekebisho makubwa au hata mwandishi mwingine kuombwa asawidi sura. Hutokea pia wataalamu wenye ujuzi wa kipindi fulani cha historia au wa swali fulani mahsusi kuombwa ushauri ili kukamilisla juzuu fulani.

Kazi hii itachapishwa kwa inara ya kwanza katika matoleo ya jalada gumu kwa lugha

za Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu na baadaye katika matoleo ya jalada laini kwa lugha hizo. Matoleo yaliyofupishwa kwa lugha za Kiingereza na Kifaransa ndiyo yataatafsiriwa kwa lugha za Kiafrika. Kamati imechagua lugha za Kiswahili na Kihausa kama lugha za kwanza za Kiafrika za kufanyia tafsiri za kazi hii.


Aidha, kila juhudi itafanywa kuhakikisha *Historia Kuu ya Afrika* inachapishwa katika lugha nyingine kubwa kimataifa kama vile Kichina, Kireno, Kirusi, Kijerumani, Kiitaliano, Kihispania, Kijapani, n.k.

Hivyo, ni dhahiri kwamba hii ni kazi nzito inayotoa changamoto kubwa kwa wanahistoria wa Kiafrika na kwa wasomi kwa jumla, na vilevile kwa UNESCO ambayo kazi hii inafanywa chini yake. Hii ni kwa kuwa ni jukumu kubwa mno kuandika historia ya bara la Afrika ya miaka milioni tatu iliyopita kwa kutumia kanuni makini kabisa za kitaaluma na kulazimika kuwahusisha wataalamu kutoka nchi, tamaduni, itikadi na mahusiano ya kihistoria tofauti. Mradi huu unabeba peo kubwa za mambo ya bara, ya kimataifa na ya taaluuna mbalimbali.

Kwa kuhitimisha, ningependa kusesitiza umuhimu wa kazi hii kwa Afrika na dunia. Katika kipindi ambamo watu wa bara la Afrika wanajitahidi kuunda umoja na ushirikiano mkubwa ili kutoa mwelekeo kwa mwenendo wa maisha yao, uelewa muafaka wa kale ya Afrika na utambuzi wa uhusiano iniongoni mwa Waafrika na baina ya Afrika na mabara mengine, usingekuwa tu mchango mkubwa kwa maelewano miongoni mwa watu duniani bali pia chanzo cha maarifa ya urithi wa kitamaduni ambacho ni cha wataalamu wote.

---

*Maelezo kuhusu Wendo*



Imekubaliwa kufuata utaratibu ufuatao wa kuandika tarehe. Ama kuhusu kipindi kabla ya liistoria, tarehe zinaweza kuandikwa kwa njia mbili.

Njia ya kwanza ni kwa kurejea enzi ya sasa yaani tarehe KS (Kabla ya Sasa), mwaka unaorejewa ukiwa ni + 1950; tarehe zote zinakuwa hasi kuhusiana na + 1950.

Njia nyingine ni kwa kurejea mwanzo wa enzi ya Ukristo. Kuhusiana na enzi hii, tarehe huwakilishwa kwa kutumia alama + au - kabla ya tarehe. Zinaporejewa karne, vifungu KK na WK nafasi yake huchukuliwa na 'kabla ya enzi ya Ukristo' na '-a enzi ya Ukristo'.

Baadhi ya mifano ni kama hii Ifuatayo:

(i)  $230 \text{ KS} = - 350$

(ii)  $2900 \text{ KK} = - 2900$


$1800 \text{ WK} = + 1800$

(iii)  $\text{Karne ya tano KK} = \text{Karne ya tano kabla ya enzi ya Ukristo}$

$\text{Karne ya tatu WK} = \text{Karne ya tatu ya enzi ya Ukristo.}$

---

---



*Wanakamati wa Kamati ya  
Kimataifa ya Kisayansi ya  
Kusawidi Historia Kuu ya Afrika*

---

*Tarehe zilizotajwa zinawakilisha tarehe za Uanachama*

Profesa J.F.A. Ajayi  
(Nigeria), 1971  
Mhariri Juzuu VI

Dkt. Aklilu Habte  
(Ethiopia), tangu 1971

Profesa F.A. Albuquerque Mourao  
(Brazil), tangu 1975

Profesa D. Birmingham  
(Uingereza), tangu 1985

Profesa A. A. Boahen  
(Ghana), tangu 1971  
Mhariri Juzuu VII

Hayati H.E. Baubou Hama  
(Niger), 1971 - 8 (alijiuzulu 1978);  
alifariki 1982

Dakta (Bibi) Mutumba M. Bull  
(Zambia), tangu 1971

Profesa P. Chanaiwa  
(Zimbabwe) tangu 1975

Profesa P.D. Curtin  
(Marekani), tangu 1975

Profesa J. Devisse  
(Ufaransa), tangu 1971

Prof. M. Difaila  
(Angola), tangu 1978

Hayati Profesa Cheikh Anta Diop  
(Senegal), 1971- 86; alifariki 1986

Profesa H. Djait  
(Tunisia), tangu 1975

Profesa J.D. Fage  
(Uingereza), 1971 - 81 (alijiuzulu)

H.E.M. El Fasi  
(Moroko), tangu 1971; alifariki 1991  
Mhariri Juzuu III

Hayati Profesa J.L. Franco  
(Cuba), tangu 1971; alifariki 1989

Hayati Bw. M.I.I. Galaal  
(Somalia), 1971 - 81; alifariki 1981

Profesa Dakta V.L. Grottanelli  
(Italia), tangu 1971

Profesa E. Haberland  
(Ujerumani Magharibi),  
tangu 1971

H.E.A. Hampaté Bâ  
(Mali), 1971 - 8; (alijiuzulu; alifariki  
1991)

Dakta I.S. El-Hareir  
(Libya), tangu 1978

Dakta I. Hrbek  
(Chekoslovakia), tangu 1971  
Mhariri Msaidizi Juzuu III

Dakta (Bibi) A. Jones  
(Liberia); tangu 1971

Hayati Abbe Alexis Kagame  
(Rwanda), 1971 - 81; alifariki 1981

Profesa I.N. Kimambo  
(Tanzania), tangu 1971

Profesa J. Ki-Zerbo  
(Burkina Faso), tangu 1971  
Mhariri Juzuu I

Bw. D. Laya  
(Niger), tangu 1979

Dakta A. Letnev  
(Urusi), tangu 1971

Dakta G. Mokhtar  
(Misri), tangu 1971  
Mhariri Juzuu II

Profesa P. Mutibwa  
(Uganda), tangu 1975

Profesa L.D Ngcongco  
(Botswana), tangu 1971

Profesa D.T. Niane  
(Senegal), tangu 1971  
Mhariri Juzuu IV

Profesa T. Obenga  
(Jamhuri ya Watu wa Congo),  
tangu 1975

Profesa B.A. Ogot  
(Kenya), tangu 1971  
Mhariri Juzuu V

Profesa C. Ravoajanahary  
(Madagascar), tangu 1971

Hayati Profesa W. Rodney  
(Guyana), 1979 - 80; alifariki 1980

Hayati Profesa M. Shibeika  
(Sudan), 1971 - 80; alifariki 1980

Profesa Y.A. Talib  
(Singapore), tangu 1975

Hayati Profesa A. Teixeira da Mota  
(Ureno), 1978 - 82; alifariki 1982

Mgr T. Tshibangu  
(Zaire), tangu 1971


Profesa J. Vansina  
(Ubelgiji), tangu 1971

Hayati Mheshimiwa Dakta E. Williams  
(Trinidad na Tobago), 1976-8  
alijiuzulu 1978; alifariki 1980

Profesa A.A. Mazrui  
(Kenya  
Mhariri Juzuu VIII,  
Siyo mwanakamati

Profesa C. Wondji  
(Côte d'Ivoire)  
Mhariri Msaidizi wa Juzuu VIII  
Siyo mwanakamati

*Katibu wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi*  
A. Gatera  
Sehemu ya Utambuzi wa Tamaduni na  
Mahusianokati ya Tamaduni  
1, rue Miollis, 75015 Paris




## Wasifu wa waandishi waliochangia makala katika nakala kuu

Toleo lilihofupishwa lilitayarishwa kutokana na matini za  
toleo kuu lililoandikwa na waandishi wafuatao:

- SURA 1 I. Hrbek (Chekoslovakia), mtaalam wa historia ya Oriental Institute, Prague, na mshauri wa kisayansi wa Czechoslovak Academy of Sciences.
- SURA 2 M. El Fasi (Moroko), mwandishi wa vitabu kadhaa (katika Kiarabu na Kifaransa) vinavyolusika na historia ya isimu na tahakiki za fasihi, Makamu wa Mkuu wa Chuo wa Chuo Kikuu cha Karawiyin huko Fez.
- SURA 3 I. Hrbek/M. El Fasi
- SURA 4 Z. Dramani-Issifou (Benin), mtaalam katika mahusiano kati ya Afrika ya watu weusi na Maghrib, mwandishi wa nyaraka nyūngi na kitabu kimoja muhimu juu ya mada hiyo.
- SURA 5 F. de Medeiros (Benin), mtaalam katika uandishi wa historia; mwandishi wa vitabu vinavyohusu mahusiano katika ulimwengu wa Afrika ya watu weusi na watu wengineo.
- SURA 6 S. Lwango - Lunyigo (Uganda); mtaalam katika historia ya awali ya Afrika, hususani Enzi ya Chuma ya Afrika; mwandishi wa vitabu vingi kuhusu mada hiyo  
J. Vansina (Ubelgiji), mtaalam wa historia ya Afrika, mwandishi wa vitabu vingi na makala mengi kuhusu Afrika kabla ya majilio ya wakoloni, Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Wisconsin, Madison (Marekani).
- SURA 7 T. Bianquis (Ufaransa), mtaalam wa historia ya karne ya kumi na karne ya kumi na moja ya Arabuni Mashariki, mwandishi wa kitabu kitiwacho *Histoire de Damas et de la Syrie sous la domination fatimide*, Mkurugenzi wa zamani wa Institut française d'etudes arabes, Damaskas; hivi sasa ni mhadhiri wa historia na ustaarabu wa Kiislamu katika Chuo Kikuu cha Lumiere -Lyon II.
- SURA 8 S. Jakobielski (Poland), mtaalam wa akiolojia ya Kikristo; amechapisha vitabu kuhusu hati za Kikopti; mhadhiri wa akiolojia ya Nubia katika Catholic Academy of Theology, Warsaw; mwanachama wa Polish Centre of Mediterranean Archaeology iliyoko Kairo.
- SURA 9 H. Mones (Misri), mtaalam wa historia kuu ya Uislamu; amechapisha vitabu kuhusu mada hii; Profesa wa Historia, Kitivo cha Sanaa, Chuo Kikuu cha Kairo; mwanachama wa Arabic Language Academy, Kairo.
- SURA 10 M. Talbi (Tunisia), Mwana Uislamu; amechapisha vitabu vingi na makala mengi kuhusu jiha mbalimbali za dini na utamaduni wa Kiislamu; mwalimu wa zamani katika Kitivo cha Sanaa, Tunis.
- SURA 11 T. Lewicki (Poland) mtaalam katika historia ya Maghrib na katika historia ya Sudani katika Enzi za Kati; mwandishi wa vitabu vingi kuhusu mada hii; Profesa katika Chuo Kikuu cha Jagellonne, Krakow.
- SURA 12 I. Hrbek

- SURA 13 J. Devisse (Ufaransa), mtaalam wa historia ya Afrika Magharibi- Kaskazini tangu karne ya nne hadi karne ya kumi na sita; mwanaakiolojia; amechapisha makala mengi na vitabu kuhusu historia ya Afrika; Profesa wa Historia ya Afrika katika Chuo Kikuu cha Paris I, Panthéon - Sorbonne.  
I. Hrbek
- SURA 14 J. Devisse
- SURA 15 D. Lange (Ujerumani Magharibi), mtaalam katika historia ya kabla ya majilio ya ukoloni katika Sudan ya kati; amechapisha vitabu vingi kuhusu kipindi hiki; mwalimu wa zamani katika Chuo Kikuu cha Niamey.  
B. Barkindo (Nigeria), mtaalamu wa mahusiano baina ya nchi kabla na mapema wakati wa ukoloni kwenye bonde la Chad; mwandishi wa makala mengi na mhadhiri, Chuo Kikuu cha Bayero, Kano.
- SURA 16 Thurstan Shaw (Uingereza), mwandishi wa vitabu vingi kuhusu kipindi cha kabla ya historia ya Afrika Magharibi; Profesa wa akiolojia; Makamu wa Rais wa Pan -African Congress on Prehistory; Rais wa Prehistoric Society.
- SURA 17 B.W. Andah (Nigeria), mtaalam katika historia, akiolojia na anthropolojia ya Afrika; mwandishi wa vitabu vingi kuhusu mada hii; Profesa wa akiolojia na katika Chuo Kikuu cha Ibadan.  
J. R. Anquandah (Ghana), mtaalam katika historia na akiolojia ya Afrika toka Enzi ya Awali ya Chuana hadi takribani 1700; amechapisha vitabu vingi kuhusu mada hiyo; mhadhiri katika Akiolojia, Chuo Kikuu cha Ghana, Legon.
- SURA 18 B.W. Andah
- SURA 19 Tekle - Tsadik Mekouria (Ethiopia), mwanahistoria; mwandishi, mtaalamu wa historia ya siasa, uchumi na jamii ya Ethiopia tangu mwanzo wake hadi karne ya ishirini; amestaafu.
- SURA 20 E. Cerulli (Italia), mwanaethnolojia; mwandishi wa vitabu kuhusu mada hiyo.
- SURA 21 F.T. Masao (Tanzania), mwanaakiolojia; mtaalam wa sanaa-mawe ya Enzi ya Nyuma ya Mawe na ya kipindi kabla ya historia; mwandishi wa vitabu vingi kuhusu mada hiyo.  
M.W. Mutoro (Kenya), mtaalam katika akiolojia ya Afrika, mwandishi wa vitabu vingi kuhusu mada hiyo.
- SURA 22 C. Elret (Marekani), mtaalamu wa lugha na historia ya Afrika Mashariki; amechapisha vitabu vingi na makala kuhusu historia ya kabla ya majilio ya ukoloni na ya zama za ukoloni ya Afrika Mashariki; anafundisha katika Chuo Kikuu cha California, Los Angeles.
- SURA 23 D.W. Phillipson (Uingereza), mwangalizi wa makumbusho na mwanaakiolojia, mtaalamu wa historia ya awali ya kusini mwa Sahara ya Afrika na msisitizo vingi kuhusu mada hiyo na mhariri wa African *Archaeology Review*; mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Cambridge.
- SURA 24 T.N. Huffman (Marekani), mtaalam katika akiolojia na kipindi kabla ya historia cha akiolojia ya kitamaduni na kiantropolojia cha Afrika kusini mwa Sahara; mwandishi wa vitabu kuhusu mada hiyo.
- SURA 25 (Bibi) B. Domenichini-Ramiamanana (Madagascar), mtaalam katika lugha na fasilhi ya Kimalagasi; mwandishi wa vitabu vingi kuhusu ustaarabu wa Madagascar; Makamu wa Rais wa Sehemu ya Lugha, Fasilhi na Sanaa katika Malagasi Academy; anafundisha fasilhi simulizi na historia ya utamaduni katika Chuo Kikuu cha Madagascar; Mchunguzi Mwandamizi katika sayansi za lugha katika Centre national de recherche scientifique (CNRS), Paris.
- SURA 26 Y.A. Talib (Singapore), mtaalam katika Uislamu, ulimwengu wa Kimalay na Mashariki ya Kati, hususani Kusini-Magharibi mwa Uarabuni; mwandishi wa vitabu kuhusu mada hiyo; Profesa Mshiriki, Mkuu, Idara ya Taaluma ya Malay Chuo Kikuu cha Kitaifa cha Singapore.
- SURA 27 A. Bathily (Senegal), mtaalam katika historia ya Sudan ya Magharibi tangu karne ya nane hadi karne ya tisa; amechapisha vitabu vingi kuhusu mada hiyo.  
C. Meillasoux (Ufaransa), mtaalam wa historia ya uchumi na jamii ya Afrika Magharibi; mwandishi wa vitabu vingi kuhusu mada hiyo; Mchunguzi Mwandamizi katika CNRS; Paris.
- SURA 28 J. Devisse/J. Vansina





## *Afrika katika muktadha wa historia ya dunia*

### *Kuinukia kwa Ulimwengu wa Kiislamu*

Mgeni yeyote angeitazama Dunia ya Kale mwanzoni mwa karne ya saba ya enzi ya Ukristo na baadaye kuizuru tena baada ya karne tano katika mwaka wa 1100, angeweza kufikiria kuwa dunia nzima ilikuwa inaelekea kwenye Uislamu.

Katika ziara yake ya kwanza, angeona kuwa jamii iliyoishi karibu na Nabii Muhammad, ambaye alihubiri Uislamu katika Maka mji mdogo wa Arabuni, ilikuwa ya watu wasiozidi mia moja waliokuwa wanatafuta nusura dhidi ya uhasama shadidi wa wananchi wenzo. Karne tano baada ya hapo, wafuasi wa dini hiyo walikuwa wametapakaa kuanzia kingo za mito Ebro Senegal na Niger katika magharibi, hadi Syr-Darya na Indus katika mashariki, na kuanzia Mto Volga hadi pwani ya Afrika Mashariki. Ingawa wakati huo ulimwengu wa Kiislamu ulikuwa umekwishapoteza umoja wake wa awali wa kisiasa, lakini bado ulikuwa ukiwakilisha utamaduni na ustaarabu wa namna moja wenye uweza mkubwa wa kupanuka.

Wakati huo, Uislamu haukuwa tena dini ya Waarabu tu. Ikiwa imezaliwa katika Musoma (Peninsula) wa Arabuni uliopiwa na jua kali, iliweza kujinasibisha na mazingira ya kanda mbalimbali za dunia na miongoni mwa watu wa aina mbalimbali ambao nao waligetika kuwa watetezi wakubwa wa dini hiyo wakaieneza katika sehemu mpya.

Lisingekuwa jambo la kustaajibisha kwa mafanikio hayo makubwa kumvutia mgeni huyo, kama yalivyowavutia wanahistoria wengi ambao hawakusita kukiita kipindi baina ya karne ya saba na karne ya kumi – na moja na hata baada ya hapo – ‘enzi ya Uislamu’. Lakabu hii haina maana kwamba Waislamu walitawala dunia nzima, au kuwa walileta athari thabiti za kisiasa, kidini au kitamaduni nje ya maeneo yao; bali inapaswa kueleweka kwa kuulinganisha ukanda huu na kanda nyinginezo za kitamaduni na pia kwa kuzingatia kuwa katika kipindi hicho ulimwengu wa Kiislamu ulikuwa ukivuvumka na kuendelea kuliko tamaduni nyingine zote katika maeneo kadhaa ya amali za wanadamu.

Utamalaki wa Waarabu katika karne ya saba na karne ya nane ulileta athari mbili kuu na za kudumu. Athari ya kwanza na iliyokuwa ya kuvutia zaidi ilikuwa ile ya uanzishaji wa taifa jipya duniani katika Bonde la Mediterania na Mashariki ya Karibu<sup>1</sup>. Athari ya pili, ambayo haikutokea kwa vurumai kubwa kama ilivyokuwa ya kwanza, ilikuwa ukuzaji wa utamaduni mpya wa dunia katika taifa hilo jipya.

1 Kuhusu kuinukia kwa Ukalifa taz. Sura 2 ya juzuu hili.

Ilipofikia mwishoni mwa karne ya kumi na moja, dola ya awali ya Waarabu ilikuwa imekwishatoweka na badala yake kukawa na ulimwengu wa Kiislamu wa Enzi ya Kati. Kwa hakika huo ulikuwa zaidi ulimwengu kuliko dola - utaratibu wa kisiasa ulijumuisha mataifa mbalimbali lakini wenye kujitambua kuwa na msingi mmoja ulio tofauti na kanda nyingine za dunia; utaratibu ambao ulijengeka kwenye msingi wa dini moja badala ya mshikamano wa kimbari au kikabila.

Natija ya pili ya kudumu ya utamalaki wa awali wa Waarabu ilikuwa ujenzi wa utamaduni mpya wa dunia. Watamalaki wa Kiarabu walitumia mambo mawili yote, yaani dini yao mpya, Uislamu, na nguvu zao za kijeshi katika kuanzisha dola. Lakini utamaduni waliouleta kutoka kwao jangwani ulikuwa sahili. Mbali na kuleta dini yao, Waarabu pia waliitumia lugha yao kama chombo kikuu cha utawala, fasihi na sayansi.

Ustaarabu huo tajiri na uliokuwa bayana wa kiada ambao uliupambanua ulimwengu wa Kiislamu katika kilele cha ustawi wake ulitokana na muungano wa mapokeo mbalimbali ya watu wote walioukubali Uislamu au walioishi katika utawala wake. Mbali na kurithi mafanikio yakinifu na ya kitaalamu ya staarabu za Mashariki ya Karibu na ya Mediterania, ustaarabu huo pia ulitumia na kuhazimu vipengee vyenye asili ya Kichina na Kihindi na ulichukua nafasi kubwa katika uenezaji zaidi wa vipengee hivyo.

Dola ya Kiislamu ilijengwa katika ukanda wenye ustaarabu wa kale kuliko staarabu zote duniani; mahali ambako Waarabu watamalaki walikuta mapokeo ya siku nyingi ya maisha na uchumi wa mijini. Hawakufanya ajizi katika kutumia fursa hiyo. Aidha, mbali na kutamakani katika miji ya kale wahanzisha miji mipya pia. Muundo huo wa maisha ya kimji ndio ulioutofautisha sana ulimwengu na ustaarabu wa Kiislamu na ulimwengu na ustaarabu wa Magharibi ya Kikristo katika miaka ya awali ya Enzi ya Kati. Vituo muhimu kuliko vyote vya maisha ya kiuchumi na kitamaduni vilikuwa katika nchi kiini za Kiislamu ambapo Ulaya Magharibi wakati huo ilidhihirisha picha tofauti ya jamii za vijijini zilizotawanyika zenye amali chache tu za kibiashara na kitaaluma. Mikondo iliyokuwa inaongezeka ya kibiashara kati ya schemu mbalimbali za ulimwengu wa Kiislamu na nje ya mipaka yake ilichochea uzalishaji wa bidhaa katika kila schemu kwa ajili ya masoko yaliyoko kwingineko. Vilevile, mikondo hiyo ilichochea maendeleo katika mbinu za kimatumizi na za kinadharia, kama vile mbinu za ubaharia na nyanja zilizohusika za uundaji wa meli; falaki na jiografia; na pia katika shughuli za kibiashara na kibenki.

Kwa kiasi kikubwa usitawi wa kiuchumi ulioauza katika karne ya nane ulitokana na mmiminiko wa madini yenye thamani katika nchi za kati za Mashariki ya Karibu. Ongezeko katika upatikanaji wa dhahabu katika karne ya tisa lilisababisha mabadiliko katika mfumo wa fedha: nchi ambazo hadi hapo zilikuwa zikitumia sarafu za fedha tu zikaanza kutumia metali mbili. Aidha viwanda vyote vya kutengeneza fedha katika sehemu ya mashariki ya Ukhulafa vilianza kutengeneza dinari za dhahabu. Katika sehemu ya magharibi ya dunia ya Kiislamu, hali ilikuwa tofauti; kwa muda mrefu Maghribi na Hispania ya Kiislamu zilibaki katika eneo la sarafu za fedha, hasa kwa sababu hazikuwa na migodi ya dhahabu. Hali hii ilianza kubadilika tu katika karne ya kumi wakati uagizaji wa dhahabu kutoka Sudan ya Magharibi ulipoongezeka na kufikia kilele chake wakati dinari ya Kimoravi ilipoanza kupatikana na kuwa sarafu iliyotambuliwa kimataifa.<sup>2</sup>

Dola ya Kiislamu pia ilifaidika na kuwa kwake katikati ya kiini cha Ulimwengu wa Kale. Ukubwa wa ulimwengu wa Kiislamu pekee yake uliunda hali ya pekee kwa vile ilikuwa ni himaya pekee yake kati ya maeneo makuu ya kitamaduni iliyokuwa na ulusiano wa moja kwa moja na maeneo mengine kama vile Ubizenti, Ulaya Magharibi, Bara Hindi na Uchina. Nafasi hii ya

kijiografia pia iliawezesha Waislamu kuwasiliana na maeneo makuu ya mipakani na pia watu wapya katika tambarare za Ulasia, katika Asia ya Kati, kwenye jangwa la Sahara katika Sudan, na katika Asia ya Kusini-mashariki.

Kuwa kwake katikati ya kiini hicho kuliufanya ulimwengu wa Kiislamu kuwa na dhima ya wasta - au kiungo - kati ya kanda zote nyingine za Ulimwengu wa Kale. Pamoja na bidhaa za kibiashara zilizosafirishwa baharini na nchi kavu kulikuwa na mawazo, na dhana mpya, na mavumbuzi katika teknolojia na sayansi. Karatasi ni mfano wa bidhaa muhimu ya awali iliyosafiri mbali kutoka Uchina kupitia nchi za Kiislamu hadi Ulaya. Zao hili ambalo liligunduliwa na Wachina lililetwa katika dola ya Kiislamu na mateka wa vita wa Kichina walioletwa huko Samarkand mnamo mwaka 751, ambako waliwafunza Waislamu teknolojia ya utengenezaji karatasi. Ama kwa hakika, Samarkand ikawa mahali pa kwanza kuwa na tasnia ya karatasi katika ulimwengu wa Kiislamu. Kutoka hapo tasnia hiyo ilienea upande wa magharibi na kufika katika Hispania ya Kiislamu katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi. Katika karne ya kumi na mbili, karatasi ilifika Katalonia ambayo ilikuwa nchi ya kwanza ya Ulaya kuzalisha karatasi. Hapana haja ya kusisitiza natija kuu za uenezaji wa mojawapo ya mavumbuzi makuu kwa utamaduni na ustaarabu kwa jumla.

Kadhalika uvumbuzi wa Kihindi wa alama za kinafasi katika hisabati, ambazo zajulikana kama tarakimu za Kiarabu, zilikwishatumiwa na Waislamu (ambao waliziita tarakimu za Kihindi) kwenye karne ya nane, na mfumo huo ulikwishaingia katika ulimwengu wa Kimagharibi katika karne ya kumi. Upokezi huo wa Waislamu wa alama za kinafasi ulifungua njia ya kuchipuka kwa aljebra, ambayo ndiyo ilikuwa msingi ambao pasi na kuwepo kwake matawi ya kisasa ya hisabati na sayansi asilia yasingetokea.

### Ulimwengu wa Kiislamu na Afrika

Historia ya Misri ya Kiislamu kati ya karne ya saba na mwishoni mwa karne ya kumi na moja matoa picha ya kuvutia ya sulubu ambamo jimbo muhimu, lakini la pambazoni mwa Ukhalifa, lilikuwa nchi kiini ya dola mpya na yenye nguvu ya Kifatimi. Mwanzoni jimbo hilo lilikuwa ghala ya nafaka lakini likakua hadi kuwa ndiyo lango muhimu la biashara kati ya Mediterania na Bahari Kuu ya Hindi; kutoka kuwa nchi nyonge katika uwanja wa amali za taaluma za Kiislamu hadi kuwa kituo kimojawapo kikuu cha maisha ya kitamaduni ya Waarabu<sup>3</sup>. Katika mahusiano yake na sehemu nyinginezo za Afrika, Misri ilikuwa na dhima anuwai: ilikuwa ndiyo mahala pa kuanzia utamalaki wa Waarabu katika Magharib katika karne ya saba na uvamizi wa Kihilali katika karne ya kumi na moja. Kutoka Misri Mbedui wa Kiarabu polepole walipenya katika Nubia na huo tukawa ndiyo mwanzo wa kuanguka kwa falme za Kiukristo na kuarabishwa kwa Sudan ya Kiniloti. Ingawa Misri ilipoteza sura yake ya Kiukristo katika kipindi hiki, makao yake makuu ya Alexandria bado yaliendelea kudhibiti makanisa ya Kimonofisita ya Nubia na Ethiopia. Aidha inafaa kukumbuka kuwa Misri ilikuwa pia ndio kituo cha mwisho cha idadi kubwa ya watumwa weusi wa Kiafrika waliosafirishwa kutoka Nubia, Ethiopia na Sudan ya Magharibi na Kati.

Afrika ya Kaskazini ilichukua nafasi muhimu ya kisiasa na kiuchumi katika ulimwengu wa Kiislamu. Ni kutoka Magharib ambapo utamalaki wa Hispania na Sisilia ulianzia; nako ndiko chanzo cha matokeo yote yaliyoathiri historia ya Mediterania ya Magharib na Ulaya. Utawala wa Waislamu

3 Taz. Sura 7 ya juzuu hili

ulirejeshwa Maghrib kwenye eneo la uchumi mkuu uliotanda dunia nzima, ambamo ulichukua dhima muhimu; katika kipindi hicho, Maghrib ilikuwa zaidi kidemografia na kimiji na kusitawi upya kiuchumi na kibiashara.

Ama kwa upande wa dini, nafasi ya Waberiberi ilikuwa ya namna mbili: mosi, mila zao za kidemokrasia na za usawa zikawafanya tangu mwanzo kabisa washike mafunzo ya yale madhehebu ya Kiislamu ambayo yalihubiri mwelekeo huo<sup>4</sup>. Ingawa baada ya kusitawi kwa karne kadhaa, Ukhariji wa Kiberiberi ulivunjiwa na tikabakia tu katika jumuiya chache ndogo ndogo, moyo wa mageuzi na mwelekeo wa unasi ulibaki kuwa sehemu muhimu ya Uislamu katika Maghrib. Moyo huo ukajidhihirisha katika harakati kuu za Wamoravi na Wamoha; na vilevile katika kutokezea kwa wingi kwa tarika za Kisufii.

Panikio la pili la Waberiberi - kama inavyoonekana katika mtazamo wa Kiislamu na wa Kiafrika - lilikuwa la kuleta Uislamu katika sehemu ya Afrika kuvuka Sahara. Misafara ya wafanyabiashara wa Kiberiberi haikubeba tu bidhaa bali pia ilisafirisha mawazo mapya ya kidini na kitamaduni, ambayo mwanzoni yalipokelewa na tabaka la wafanyabiashara na baadaye katika majumba ya wafalme wa Kiafrika<sup>5</sup>. Luja ya pili ya kusilimishwa kwa ukanda wa Sudan ilitokea katika karne ya kumi na moja wakati wa usitawi wa Wamoravi, ambao ulikuwa harakati halisi za kidini za Kiberiberi.

Kufunguka milango kwa Sahara na Sudan ndiko kulikofanya Afrika ya Kaskazini ipate umuhimu wake mahsus katika uchumi wa ulimwengu wa Kiislamu. Dhahabu iliyokuja kutoka Sudan ilileta ustawi mkubwa wa kiuchumi ambao ulisaidia nasaba-tawala nyingi za Kiislamu katika Maghrib kuacha matumizi ya sarafu za fedha na kuanza kutumia sarafu za dhahabu. Uchimbaji wa migodi ya chumvi katika Sahara uliongezeka kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya madini hayo muhimu katika Afrika kusini mwa Sahara. Kwa muda wa karne nyingi biashara na Afrika kusini mwa Sahara yumkini ilileta faida kubwa kuliko matawi mengine yote ya biashara ya Waislamu ya nje. Ingawa Sudan haikutamalakiwa na Waarabu au Waislamu wengine wala kamwe haikuwa sehemu ya Ukhalifa, lakini ilizidi kuathirika na ulimwengu wa Kiislamu kutokana na mawasiliano ya kibiashara na kitamaduni.

Upanuzi wa haraka wa dola ya Kiislamu kwa kiasi kikubwa uliharibu maisha ya kiuchumi ya Ethiopia kwa kuikata njia yake ya kufikia Bahari ya Sham. Tokeo jingine la nguvu ya Kiislamu katika kanda za mwambao lilikuwa la kuhamishia kusini kituo kikuu cha Taifa la Ethiopia na kuendeleza kwa nguvu upanuzi wa dini hiyo katika uelekeo huo. Hivyo, kanda hizo za kusini zikawa kiini cha uhuishaji wa taifa la Kikristo la Ethiopia katika karne ya tisa.

Nafasi ya dola ya Kiislamu katika Afrika katika karne hizi tano inaweza kuelezwa kwa ufupi kama hivi ifuatavyo:

- (1) Sehemu ya Mediterania ya bara la Afrika iliingizwa kikamilifu katika ulimwengu wa Kiislamu. Mediterania haikuwa tena sehemu ya Ukristo na badala yake ikawa ndiyo mahala pa kuanzia kuendeleza upanuzi wa Kiislamu katika Hispania na Sisilia, kwa upande mmoja, na katika Sahara na Sudan kwa upande mwingine.
- (2) Katika Afrika ya kaskazini mashariki, mataifa ya Kikristo ya Nubia na Ethiopia yalidhoofika, ingawa hata moja kati yao halikutamalakiwa. Wakati Nubia hatimaye ilipoteza sifa yake ya Ukristo, Ethiopia ilinusurika na kuendelea kuwa kitengo huru cha kisiasa na kitamaduni Hata hivyo, ilibidi irekebishe mahusiano yake ya nje ili yawiane na athari

4 Taz. Sura 9 na 20 ya juzuu hili

5 Taz. Sura 3 ya juzuu hili kwa maelezo zaidi juu ya kuenea kwa Uislamu

iliyokuwa inaongezeka ya Waislamu waliopakana na nchi hiyo.

- (3) Sahara na sehemu kubwa ya Sudani zilihusiana kwa njia ya biashara na eneo la Kiuchumi la Kiislamu ambamo bidhaa nje zao kuu, dhahabu na watumwa, zilikuwa na nafasi muhimu. Dini na utamaduni wa Kiislamu vilipenya katika njia za biashara na asteaste vikapenya katika maisha ya Waafrika.
- (4) Katika Afrika Mashariki nafasi ya biashara ya kimataifa ilikuwa sawa na ile iliyotangulia, isipokuwa athari za Kiislamu hazikupenya bara. Lakini katika nchi za Kiislamu na Bara Hindi, haja zilizokuwa zinaongezeka, za dhahabu kutoka Zimbabwe, inaelekea zilisababisha mabadiliko kadhaa hata katika eneo la Zambezi pia. Baadhi ya sehemu za Bukini na Visiwa vya Komoro vilevile vilifanywa viwe sehemu ya Mfumo Mkuu wa kibiashara wa Bahari kuu ya Hindi.

### *Ulaya ya Enzi za Kati na Afrika*

Katika karne ya saba, Ulaya ilikuwa imegawanyika katika maeneo matatu ambayo yalihitalifiana sana katika hatua yaliyokuwa yamefikia katika maendeleo yao ya jumla. Maeneo hayo yalikuwa dola ya Wabizenti, majimbo ya zamani ya Kirumi ya Ulaya Magharibi ambayo wakati huo yalikuwa chini ya utawala wa mbari mbalimbali za Kijerumani, na mwishowe sehemu iliyoko mashariki ya Mto Rhine na kaskazini mwa mto Danube zilizokaliwa na watu wenye asili za Kijerumani na za Kislavu

### *Dola ya Wabizenti*

Ni dola ya Wabizenti tu iliyoweza kudai kuendeleza mapokeo ya Kiyunani-Kirumi na kuwa na mfumo halisi uliopevuka wa taifa wenye uendeshaji bora, uchumi tajiri wa kifedha na kiwango kikubwa cha amali za kitamaduni katika nyanja nyingi. Kutoka majimbo yao ya Asia na Misri Wabizenti walijaribu kufungua tena njia zote mbili za kibiashara za kwenda Mashariki, za nchi kavu (Njia Kuu ya Hariri ya kwenda Uchina) na ya baharini (kupitia Bahari ya Sham hadi Bara Hindi). Lakini jitihada hizo zilitafirishwa na dola kuu nyingine katika kanda hiyo, yaani dola ya Wasasani wa Kiajemi. Mapambano kati ya dola hizo yahendelea kuanzia katikati ya karne ya sita hadi thuluthi ya kwanza ya karne ya saba na yakaathiri vibaya pande zote mbili kijeshi na kifedha, kiasi kwamba walishindwa kuzuia mashambulizi ya Waarabu Waislamu.

Amma kuhusu Afrika, dola ya Wabizenti haikuwa na nafasi muhimu tena katika karne ya saba. Walikwishaipoteza tangu mwanzo kabisa na juhudi za hapa na pale za kuiteka tena kutokea baharini hazikufanikiwa. Baadhi ya maeneo ya pwani yalibakia mikononi mwa Wabizenti hadi mwisho wa karne hiyo. Kanisa Rasmi la Taifa lilikuwa halijawahi kuwa na nguvu katika maeneo ya Kiafrika kwa sababu Wamisri walishikilia imani yao ya Monofisita na wakazi wa mijini katika Afrika Kaskazini walishikilia imani katika Kanisa la Roma. Athari yoyote iliyokuwa imeletwa na Kanisa Rasmi katika karne zilizopita ilipotea kabisa kutokana na utamalaki wa Waislamu. Ingawa Nubia ilikuwa haijawahi kuwa sehemu ya dola ya Wabizenti lakini athari za kitamaduni na za kidini za Wabizenti ziliendelea kuwa na nguvu hata baada ya utamalaki wa Kiarabu wa Misri, hususa katika Makuria, taifa la kati la mataifa matatu ya Kiukristo ya Kinubia, ambalo lilikubali, kinyume na mataifa mengine, imani Rasmi (Melkiti). Utawala ulifuata mfano wa urasimu wa Kibizenti, na matabaka ya juu yalivaa nguo za Kibizenti na kusema Kigiriki. Lakini asteaste mahusiano na dini na utamaduni wa Kibizenti yalidhoofika na mwishoni mwa karne ya saba mfalme wa Makuria

alianzisha Umonofisita katika taifa lake ambalo wakati huo lilikuwa limekwishaungana na Nobadia kaskazini<sup>6</sup>.

Wakati ilipokuwa ikipambana na Uajemi, Ubizenti ilikuwa na hamu ya kuungana na Ethiopia ya Kiukristo, ingawa ilikuwa inafuata Umonofista. Upanuzi wa Waarabu uliikatia Ubizenti njia yake kutoka Bahari ya Sham hadi Bara Hindi. Hivyo mwungano huo haukuyamkinika. Jinsi Ukristo wa Kimonofisita ulivyozidi kuwa alama ya taifa la Ethiopia ambalo lilikuwa na uadui na Uislamu na imani nyinginezo za Ukristo, ukawa unajenga utambulisho wake wenyewe pasi kuhushwa na sfulubu za Kibizenti, ama katika teolojia au kauka sanaa au fasihi yake.

## Ulaya ya Magharibi

Kati ya karne ya nne na karne ya saba, nchi zote zilizokuwa magharibi ya into Rhine na kusini mwa Alps, pamoja na sehemu za Kisiwa cha Uingereza, zikawa nchi zenye kuguriwa na watu wa Kijerumani.

Uguraji huo uliipunguzia Ulaya Magharibi watu wengi sana: ikawa haina ustaarabu wa kimiji tena na badala yake kukawa na ustaarabu wa vitongoji vidogo vya wakulima vilivyobakiza sehemu ndogo tu ya mfumo wa mahusiano uliokuwapo hapo awali.

Lakini katika karne ya saba, Ulaya Magharibi ikaweza kujigawa upya katika nchi kadhaa ambazo kwa kiasi kikubwa zilikuwa imara. Kwa upande wa Magharibi, Wavisigothi walitawala musoma mzima na Iberia, ambapo katika Gaul na katika nchi za karibu nayo, Wamerovingi wa Kifranki walisitawisha utawala wao na Waanglo-Saxon kuanzisha falme zao huko Uingereza. Mwishoni mwa karne hiyo, Italia iligawika kati ya Wabizenti upande wa kusini na Walongobardi wa Kijerumani waliokuwa wamefika kitambo tu upande wa kaskazini.

Utamalaki wa Kiarabu-Kiberiberi wa Hispania ya Wavisigothi wa mwanzoni mwa karne ya nane ulimega sehemu ya kutosha ya Magharibi ya Kilatini. Wafranki waliweza kuzuia upenyaji zaidi wa Waislamu katika Gaul, lakini mashambulizi ya Waarabu kwenye mwambao wa Kusini mwa Ufaransa na huko Italia yaliendelea kwa muda wa zaidi ya karne mbili na yalichangia katika kuleta hali ya ukosefu wa utulivu huko Mediterania. Hata hivyo mwishoni mwa karne hiyohiyo ilifanyika juhudi ya kwanza - ambayo kwa muda mrefu ilikuwa ndiyo juhudi pekee iliyofanikiwa - ya kuleta umoja wa kisiasa katika Ulaya Magharibi. Kazi hii ilifanywa na Wakarolingi na Charlemagne (768-814). Lakini, sehemu nyingi za Ulaya Magharibi zilibakia nje ya dola hiyo, kikiwemo Kisiwa cha Uingereza, sehemu kubwa ya Hispania iliyotawaliwa na Waislamu, na Italia ya kusini, ambayo bado ilikuwa mikononi mwa Wabizenti na Walongobardi.

Jina la Charlemagne linahusiana na fikra maarufu za mwanahistoria wa Kibelgiji, Henri Pirenne, ambazo zimesababisha midahalo kuhusu ulusiano kati ya kuibuka kwa himaya ya Uislamu na jaala ya Ulaya ya Magharibi. Kwa mujibu wa Pirenne si mashambulizi ya makabila ya kishenzi ya Kijerumani bali uundaji wa himaya ya Waislamu ndio uliokomesha udhibiti wa Kirumi wa biashara katika Mediterania. Mafanikio ya Waarabu ya kuinyakua Afrika Kaskazini na majimbo ya Mashariki kutoka kwa Wabizenti ndiyo yaliyosababisha mgawanyiko wa mwisho wa Magharibi na Mashariki. Hiyo ililazimisha Ulaya Magharibi kujitegemea yenyewe na kutumia rasilimali zake; na pia kutafuta kibadala cha uchumi wa kibahari wa Wamerovingi katika uchumi wa bara iliyozingirwa. Matokeo yake yakawa kwamba Ulaya ya Magharibi ikawa maskini na ya kishenzi. Udororaji huo uliondolewa tu baada ya karne ya kumi, wakati uanzishaji miji upya wa Kiulaya ulipojitokeza.

Ingawa fikra hizo zimekataliwa na wanahistoria wengi lakini zimewadhishisha matatizo muhimu ya mabadiliko katika uchumi wa zama za kati na ya chanzo cha ukabaila wa Kiulaya. Vilevile zimewagutusha wanahistoria wazingatie athari za Waarabu na utawala wao wa Afrika Kaskazini juu ya maendeleo huko Ulaya, kadhia ambayo hapo mwanzo ilikuwa imepuuzwa.

Kasoro kubwa katika fikra za Pirenne ilikuwa ya kuhusisha matokeo makubwa kama hayo na usitishaji wa biashara ya masafa marefu. Biashara kama hiyo ya masafa marefu hata iwe yenye faida kubwa kiasi gani, haikuwa na nafasi kubwa kiasi hicho katika maisha ya kijamii na kiuchumi ya Ulaya Magharibi.


Athari za kudumu za Kiarabu na Kiislamu huko Ulaya hazikutokana na makabiliano ya kijeshi au usitishaji wa mawasiliano ya kibiashara kupitia Mediterania, bali zilitokana na muda mrefu wa utawala wa Kiislamu katika Hispania na Sisilia. Kutokana na uvumbuzi mpya kuingizwa katika kanda hizo kwa njia ya mazao mapya, usindikaji bidhaa za kilimo na hususani katika sayansi na falsafa, dhana mpya ziliingizwa Ulaya ambayo haikuwa imeendelea katika nyanja hizo kama ilivyokuwa katika ulimwengu wa Kiislamu. Ingawa kuzindukana kwa Ulaya kulianza hapo baadaye - kuanzia karne ya kumi na tatu na kuendelea - kwa hakika misingi iliyokusababisha iliwekwa katika kipindi cha usitawi wa ustaarabu wa Kiislamu, yaani, kati ya karne ya nane na karne ya kumi na mbili.

### Ulaya ya Mashariki na ya Kaskazini

Katika sehemu iliyobaki ya Ulaya, uhamiaji wa makabila za Kijerumani kuelekea magharibi ulifungua njia ya upanuzi wa Kislavu ambao ulielekea pande mbili kuu: kusini kupitia mto Danube hadi Balkans na magharibi katika nehi ambayo siku hizi hujulikana kama Poland, Chekoslovakia, Hungaria na Ujerumani (Mashariki).

Ama kuhusu ulimwengu wa Kiislamu, watu wa Kislavu kwa muda wa karne kadha, walikuwa kama walivyokuwa Waafrika Weusi, yaani walisafirishwa kama watumwa. Ni muhimu kuelewa kuwa katika lugha zote za Ulaya Magharibi neno la "mtumwa" ("slave" "Sklave" "esclave" "esclavo" "escravo" n.k.) linatokana na jinambari "Slav", ambalo ni jina linalotumiwa na watu mbalimbali wa Kislavu Hii inaashiria uhakika wa kuwa katika kipindi cha ukauji wa lugha za kitaifa za Ulaya, ambacho ni kipindi kinachosadifiana na kipindi kinachozungumziwa hivi sasa, mateka kutokana na vita vya Kislavu bila shaka walikuwa ndio idadi kubwa ya watumwa huko Ulaya Magharibi. Wakiwa mateka waliotokana na vita na mashambulizi ya mara kwa mara, hawakutumiwa tu kama nguvu kazi huko Ulaya, bali pia walisafirishwa kwenda nchi za Kiislamu kama watumwa. Wale waliotekwa huko Ulaya ya Kati walipitia nchi za Wafranki kwenda Hispania ya Kiislamu, ambapo wale waliotoka nchi za Balkania aghalabu waliuzwa na Wavenisi huko Afrika Kaskazini. Waarabu waliwaita watu hao "al-Sakaliba" (umoja "al-Saklabi") na waliwatumia zaidi kama askari; wale ambao walihasiwa walitumiwa kama walini na nyumba za wake na masuria. Wakati katika al-Andalus neno "AlSakaliba" lilitumiwa kwa maana ya watumwa wote wa Ulaya, bila ya kujali utafu wao, huko Magharibi na Misri ya Kifatimi lilibaki na maana yake ya asili. Na hapo ndipo hasa Waslavu wa asili ya Balkan walipokuwa na dhima muhimu ya kushiriki kama maaskari na waendeshaji katika uimarishaji na upanuzi wa mamlaka ya Kifatimi<sup>7</sup>. Mwanajeshi mashuhuri kuliko wote miongoni mwao alikuwa Jawhar, aliyetamalaki Misri na mwanzilishi wa jiji la Kairo na Chuo Kikuu cha al-Azhar. Ingawa punde tu Waslavu walimezwa kimbari na kitamaduni na jamii ya Kiislamu ya Kiarabu katika Maghrib na Misri, lakini bado walichangia katika kuunda

7 Taz. Sura 12 ya juzuu hili.



1.1 Dunia ya Zamani, k. 230-845. (I. Hrbek)



takadiri ya sehemu hizo za Afrika Kaskazini katika karne ya kumi na ya kumi na moja.

Kati ya karne ya nane na karne ya kumi, kikundi kingine cha watu kilitokea sehemu za mataifa ya Mediterania huko Ulaya. Hawa walikuwa washambulizi wa Kiviking'i (au Wanomani), watekaji na wafanyabiashara wajasiri waliosafiri katika meli zao kutoka Skandinavia na kuvamia kanda za mwambao na hata sehemu kadha za mrima. Baadhi ya Wanomani (walioitwa na Waarabu al-Madjus) walifika hadi Hispania ya Kiislamu na hata Moroko.

Hadi karne ya kumi na moja Wanomani hawakuwasiliana moja kwa moja na Afrika, isipokuwa waliposhambulia mwambao wa Moroko katika mwaka 858 au 859, jambo ambalo lilikuwa tukio la kupita. Kikundi kimoja cha Wanomani kililowea Ufaransa kaskazini (Normandy) na kuanzisha serikali imara huko. Mbali na kuitaka Uingereza, katika 1066, Wanomani haohao vilevile walianzisha serikali yao katika Italia kusini, ambako kutoka hapo walianza kushambulia Sisilia ya Kiislamu, na kuifanya kuwa kambi yao ya upanuzi ambao kwa kiasi fulani ulielekezwa Afrika Kaskazini. Katika muda wa karne moja, Wanomani wa Sisilia wakawa sehemu muhimu ya historia ya kisiasa ya Afrika Kaskazini ya Kiislamu.

Katika kurasa zilizotangulia, tumeonyesha vidokezo vya athari mbalimbali juu ya Ulaya Magharibi za kuwapo kwa Waislamu pwani ya kusini ya Mediterania, yaani Afrika kaskazini. Ingawa hatukubaliani na fikra za Pirenne, lakini bado ni hakika ya kihistoria kuwa kutokana na utamalaki wa Kiarabu wa Afrika Kaskazini, bonde la Mediteraniaa halikuwa tena sehemu ya eneo moja kubwa la kitamaduni kama ilivyokuwa katika milenia iliyotangulia bali liligawika kati ya kanda ya Ulaya (au Kiukristo) na ya Kiarabu-Kiberiberi (au Kiislamu); kila moja ikiwa na utamaduni na uelekeo wake yenyewe.

Katika mtazamo wa Ulaya, Afrika ikanasibishwa na ulimwengu wa Kiislamu, kwa sababu hapo ndipo mashambulio makuu na athari na mawazo mbalimbali vilipokuwa vikitokea. Mawasiliano ya kibiashara kati ya pwani za kaskazini na kusini za Mediterania yalipotokea hapo baadaye, Afrika, ambayo sasa Wazungu walifahamu, ilikuwa bado Afrika ya Kiislamu. Kwa hiyo si jambo la kustajabisha kuwa Afrika ilijumuishwa pamoja na adui mkubwa wa Ukristo na wakazi wake, bila ya kujali rangi zao, walihesabika na kutendewa vivyo hivyo. Kutokuwapo mawasiliano ya moja kwa moja kati ya Ulaya na Afrika iliyo nje ya eneo la Waislamu kuliifanya Ulaya iwe na picha potofu kabisa ya bara la Afrika, na hususani ya watu wake weusi. Uchunguzi uliofanyika hivi karibuni umewadhhihisha jinsi kutojua kwao huko na fikra ya kuwa Waafrika weusi walikuwa Waislamu vilifanya Wazungu wawe na taswira ya Waafrika kuwa ni watu wenye kutenda dhambi, maovu na duni. Ni katika kipindi hicho cha ya enzi kati ambapo mielekeo hasi, kashfa na uhasama wa Wazungu kwa watu weusi vilikuwa ilianza kutokea na baadaye kushadidi kwa sababu ya biashara ya watumwa na unumwa kwa jumla.

### *Afrika, Asia na Bahari ya Hindi*

Kwa kuwa vipengele vya jumla vya suala la Bahari ya Hindi katika historia ya Afrika vimekwishajadiliwa katika Juzuu la II<sup>8</sup>, hapa tutazingatia yale matukio muhimu tu yaliyotokea katika kipindi cha kati ya karne ya saba na karne ya kumi na moja.

Nafasi muhimu iliyochukuliwa na Dola ya Kiislamu katika mahusiano kati ya bara moja na nyingine ilidhihirishwa katika sehemu za awali za sura hii. Punde tu Bahari Kuu ya Hindi ikawa sehemu ya mfumo wa biashara wa Kiislamu uliokuwa unapanuka na ambao uliunganisha Uchina,

Indonesia, Bara Hindi na mwambao wa Afrika Mashariki na nchi kiini za Kiislamu.

Kinyume na Mediterania, Bahari ya Hindi kwa jumla inaweza kuonekana kuwa ilikuwa bahari ya amani. Ingawa mahusiano ya kibiashara tangu zama za zama hayakuwa yakiwafaidia sawasawa wote walioshiriki katika biashara hizo, lakini hapakuwa na vita vya kufuja mahusiano hayo. Katika Mediterania ya enzi ya kati, mataifa ya Kiislamu na Kiukristo yalikuwa yakipambana na ingawa mawasiliano ya kibiashara hayakukoma kabisa, lakini hali hii ya uhasama haikuwa muafaka kwa biashara. Upanuzi wa Uislamu katika Bahari ya Hindi haukuathiri vibaya shughuli za kibiashara za Kiarabu-Kiajemi, kwa sababu wafanyabiashara hawakutaka kuharibu mahusiano yaliyokwishasitawi ya kibiashara kwa kushikilia kuwa mageuzo ya watu yafanyike kwa nguvu.

Hii haina maana kuwa hali ya biashara katika Bahari ya Hindi ilikuwa nzuri sana. Pamoja na biashara ya watumwa, ambayo aghalabu iliambatana na uhasama na mapigano, uharamia wa kiwango kikubwa uliendelea kuwepo katika kipindi chote hiki. Lakini, uharamia huo haukufikia kiwango kilichojulikana katika Mediterania, ambako ulichochea na hata kurazinishwa kwa tofauti za kidini.

Katika nusu ya pili ya karne ya tisa, matukio mawili yalikuwaza sana biashara ya Waislamu katika Bahari ya Hindi. La kwanza lilikuwa maasi makuu ya Kizanzi katika kanda ya Iraki ya chini na Ghuba ya Arabuni/Ajemi katika miaka ya 866 - 31<sup>o</sup>. Baadhi ya bandari muhimu - Basra, Ubulla, Abadan ziliatitika na Baghdad haikuwa na njia ya kufikia pwani. Kwa muda wa miaka zaidi ya 15, biashara ya bahari katika kanda hii iliselelea nyuma kutokana na ukosefu wa mitaji, bidhaa na meli.

Pigo la pili kwa biashara ya Waislamu lilitokea takriban sawia na tukio la kwanza katika mwaka 878, wakati majeshi ya mwasi wa Kichina Huang Ch'ao yalipovamia Kanton na kuwaua wafanyabiashara wa kigeni kwa wingi, wengi wao wakiwa wa kutoka nchi za Kiislamu. Lakini inaelekea baadhi ya wafanyabiashara waliachiliwa kwa sababu mwandishi wa maelezo ya maafa hayo aliandika kuwa waasi waliwadhulumu marubani wa Kiarabu, wakawatoza wafanyabiashara kodi zisizo halali na kutwaa mali zao.

Katika karne ya kumi na moja, kulitokea badiliko kubwa katika biashara ya Waislamu, kutokana na kufikia kwa Ukhalifa wa Waabbasi katika Mashariki ya Kati na papohapo kusitawi kwa Wafatimi katika Afrika Kaskazini. Ushindani wa zama za zama kati ya njia zilizoishia katika Ghuba ya Arabu/Ajemi na njia iliyopitia Bahari ya Sham ulimalizika kwa faida ya njia ya bahari ya Sham.

Mpaka sasa tumezungumzia nafasi ya Waislamu wa Kiarabu na Kiajemi katika mahusiano ya Bahari ya Hindi. Je, hali ilikuwa vipi kwa wengine, kama Wachina, Wahindi na Waindonesia? Ni kwa kiwango gani watu hao walishiriki katika mahusiano haya na walileta athari gani Afrika? Waafrika walikuwa na nafasi gani katika Bahari ya Hindi?

## Uchina

Katika zama za zama na za kati mawasiliano ya Wachina na maeneo makuu mengine ya Ulimwengu wa Kale - Bara Hindi, Asia ya Magharibi na nchi karibu na Mediterania - yalianzishwa kwa sababu ya biashara ya bidhaanje ambamo bidhaa muhimu ilikuwa hariri na, baadaye, vyombo vya kauri.

Ingawa Uchina ilikwisha kuwa na ujuzi wa kifundi na nyenzo za kufanya safari za mbali baharini kwenye Bahari ya Hindi chini ya ufalme wa T'ang (618-906), lakini haikutumia meli zake kwenda mbali ya musoma wa Malay. Wachina walipata habari za safari ya Bahari ya Hindi kutoka kwa Wahindi na Waajemi, na baadaye kwa Waarabu. Maelezo nusunusu kuhusu Waafrika na Afrika katika maandishi ya Kichina inaelekea yalitokana na simulizi za Waislamu. Kwa hivyo, Wachina

wakaanza kufikiria kuwa Waafrika walikuwa raia wa watawala wa Kiislamuna nchi zao zilikuwa sehemu ya himaya ya Kiarabu.

Miongoni mwa bidhaa muhimu za Kiafrika zilizofika Uchina, zilikuwa pembe za ndovu, ambari, buhuri, manemane na vilevile watumwa wa Kizani.

Kwa muda fulani, ilidhaniwa kuwa historia ya Afrika Mashariki iliandikwa katika kauri za Kichina. Ama kwa hakika, idadi kubwa ya kauri za Kichina imegunduliwa katika miji ya mwambao ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, vyombo hivyo vinaelekea vilikuwa sehemu muhimu ya bidhaanjanje za Kichina kwenda Afrika. Hata hivyo, tukiacha mifano michache, kauri nyingine za Kichina ni za kipindi cha baada ya karne ya kumi na moja. Hali hadhalika, sarafuza Kichina zilizopatikana mwambao wa Afrika Mashariki.

Kwa hiyo, ushahidi huo unahitimisha kuwa wakati bidhaa za Kiafrika zilikuwa sehemu ya kudumu ya bidhaandani katika Uchina tangu zama za awali, bidhaa za Kichina zilikuja kwa wingi katika kipindi cha haada ya karne ya kumi na moja. Kama ilivyokwishaelezwa, mabadilishano kati ya Uchina na Afrika hayakuwa ya moja kwa moja bali yalipita kwenye mfumo wa kibiashara wa Waislamu katika Bahari ya Hindi.

## Bara Hindi

Suala zima la nafasi ya Bara Hindi katika Bahari ya Hindi, hususani katika milenia ya kwanza ya enzi ya Ukristo, hado halijafumbuliwa. Suala hilo kimsingi linahusiana na kushiriki kwa Wahindi katika biashara ya kimataifa na athari ya Bara Hindi kwenye sehemu mbalimbali za kanda hiyo. Kazi ya kutatua utata huo inakuwa ngumu zaidi kwa sababu ya ukosefu wa ushahidi kutoka vyanzo vya Bara Hindi katika kipindi kinachojadiliwa.

Katika kipindi kati ya karne za saba na kumi na moja, mahusiano kati ya Afrika na Bara Hindi yanaelekea yalikuwa madogo mno. Bila shaka mawasiliano yalikuwapo, nayo aghalabu yalikusiana na mabadilishano ya bidhaa. Bidhaa mojawapo muhimu ya bidhaanjanje kutoka Afrika kwenda Bara Hindi ilikuwa pembe za ndovu. Biashara ya pembe ilikwishashitadi tangu zama za kale na karibu huhusu vyanzo vyote vya Kiarabu vinataja jambo hili katika maelezo yao mwambao wa Afrika Mashariki. Al-Masudi aliandika kuwa pembe kutoka Afrika Mashariki zilisafirishwa nje kwenda Bara Hindi na Uchina na kuongezea kuwa kituo chake kikuu kilikuwa Oman. Hakuna ushahidi mwingine unaopatikana kuhusu bidhaa nyinginezo za bidhaa nje kutoka karne hizo, lakini inafaa ieleweke kuwa taarifa mashuhuri ya Al-Idrisi (t.1154) kuhusu usafirishaji nje wa chuma kutoka Afrika kuelekea Bara Hindi inazungumzia zama za awali. Hivyo, taarifa hiyo inaingia katika kipindi kinachozungumiwa. Bidhaa hiyo ya Kiafrika ilikuwa na nafasi muhimu katika kuendeleza tawi moja la ya Bara Hindi, uzalishaji wa nyembe za chuma. Huu unaelekea kuwa mfano mmoja adimu wa usafirishaji nje wa bidhaanjanje za Kiafrika ambazo hazikuingizwa katika kundi la bidhaa za msingi. Katika jambo hilo, inafaa kusisitizwa kuwa Afrika haikuchimba mtapochuma wa kiasi kikubwa, kwani meli za wakati huo hazikuweza kubeba kiasi kikubwa cha bidhaa hiyo ambayo ilikuwa tayari imekwishasindikwa na kuwa chuma kigumu.

Kwa hakika, baadhi ya watumwa wa Kiafrika walisafirishwa nje kwenda Bara Hindi kupitia Bara Arabu au Ajemi, lakini hakuna vyanzo vya kimaandishi vinavyoeleza jambo hilo au ushahidi mwingine uliodhihirika. Wala hakuna maelezo ya kutosha kuhusu miguro ya watu katika pande mkabala, yaani ya Wahindi kwenda Afrika. Katika baadhi ya mapokeo simulizi kutoka mwambao na visiwa vya karibu, kuna marejeo mengi kuhusu watu waitwao Wadabili. Jina lao linaelekea limetokana na bandari kuuya al-Daybul (Dabhol) kwenye lango la Mto Indus. Tarehe ya kufika

kwao Pwani ya Afrika Mashariki ni ya utatanishi; baadhi ya mapokeo yanaeleza kuwa wau hao walifika kabla ya usilimishwaji wa mwambao, wakati mengine yanahusisha ufikaji huo na uingizaji wa silaha za baruti na hivyo kuwa wa tarehe ya baadaye.

Hii yote haiondoi uwezekano kwamba baadhi ya watu wa asili ya Uhindi - zaidi wafanyabiashara- walikwishatamakani pwani hii mapema zaidi. Kwa vyovyote vile hawakuwa wengi, kwani ingekuwa hivyo mabaki ya kimaandishi au vitu vya utamaduni vingekuwa vimepatikana au kuhifadhiwa kwa namna fulani. Ama kwa hakika Kiswahili kina maneno mengi yenye asili ya Kihindi lakini mpaka wakati huu haikuwa rahisi kusema ni lini maneno hayo yalingizwa katika Kiswahili.

## Indonesia

Wakati mawasiliano kati ya Afrika, kwa upande mmoja, na Uchina na Bara Hindi, kwa upande mwingine, kama ilivyokwishaeleza, yalikuwa ya mzunguko kuliko ya moja kwa moja, kulikuwako kanda moja katika upande wa pili wa Bahari ya Hindi ambayo iliacha athari dhahiri walau katika sehemu fulani za Afrika. Mchango wa Indonesia wa kuwoko kwa watu wake katika Bukuni umetambulika siku nyingi. Lakini, kwa vile jambo hilo limejadiliwa katika sura nyinginezo za Juzuu hili<sup>10</sup>, hapa yanatajwa mambo yale tu yanayohusiana na bara la Afrika moja kwa moja.

Athari za Waindonesia kwenye bara la Afrika inaelekea zimepigwiwa chuku. Hakuna ushahidi wa kuonesha upenyaji wa moja kwa moja wa Waindonesia katika Afrika Mashariki kama ilivyo kwa upande wa Bukuni. Hadi hii leo, hakuna data za kiakiolojia, za lugha au za kiwiliwili zilizogundulika ambazo zinaonesha kuwa Waindonesia walikuwapo kwa kipindi kirefu. Nadharia iliyoeleza na Deschamps kuwa Wamame-Malagasi walitamakani kwa muda kwenye mwambao wa Afrika Mashariki kabla hawajastakimu huko Bukuni haina ithibati. Raymond Kent amepanua nadhariatete hiyo kwa kuchukulia kuwa kulikuwapo mguro kutoka Indonesia hadi Afrika Mashariki kabla ya majilio ya vikundi vya Wabantu, na kuwa Waindonesia na Wabantu hatimaye walikutana na kuchanganyika mrimani. Inachukuliwa kuwa mchanganyiko wa makundi hayo mawili ndio uliozaa watu wa Afro-Malagasi. Baada ya hapo, uenezaji wa Wabantu hadi maeneo ya pwani uliwalazimisha watu hao wahamie Bukini.

Mengi yamesemwa hususani na Murdock, juu ya "mchangamano wa kibotania wa Kimalaysia", unaohusu mazao kama mpunga, ndizi, majimbi, viazi vikuu, mashelisheli na mengineyo ambayo baadaye ndiyo yaliyokuwa chakula kikuu cha Waafrika wengi. Murdock na wengine wanaamini kuwa mchangamano huo uliletwa Bukuni katika milenia ya kwanza kabla ya enzi ya Ukristo na wahamiaji kutoka Indonesia, ambao walisafiri kwenye Pwani ya Asia kusini kabla hawajafika mwambao wa Afrika Mashariki. Lakini, inafaa idokezwe kuwa uenezaji wa mazao yanayopandwa hautegemei uhamaji wa watu ambao walianza kuyalima mwanzo au ambao walikuwa wa awali kuyatumia, kama inavyodhihirika vizuri katika mifano ya uenezaji wa baadhi ya mazao ya Kimarekani kupitia Afrika ya Magharibi na ya Kati baada ya karne ya kumi na sita. Kwa hakika, hii haiondoi uwezekano kuwa baadhi ya mazao ya Asia ya Kusini-Mashariki yaliletwa barani Afrika hapo baadaye kutoka Bukuni.

Lakini, hapana shaka kuwa Waindonesia walikuwa mabaharia stadi na kuwa walisafiri safari nyingi, wakitambaa pande zote kutoka kwenye visiwa vyao. Katika nusu ya pili ya milenia ya kwanza, mataifa yenye nguvu za baharini yalitokeza huko Sumatra na Java, kama vile dola ya Sumafra ya Srivijaya (karne ya saba hadi kumi na tatu) na ya dola ya Java ya nasaba ya Sailendra

(karne ya nane), ambayo hapo baadaye pia ilishika madaraka huko Srivijaya.

Hapa tunahusika tu na zile jiba za historia za mataifa yale ambazo zinahusiana na hali ya jumla ya ukanda wa Bahari ya Hindi na mawasiliano yake na Afrika. Watawala wa Srivijaya walidhibiti bandari kuu za bidhaanje ya kanda hiyo na kwa kufanya hivyo walikuwa na ukiritimba mpana juu ya biashara ya viungo vya chakula. Udhibiti wa Milangobahari ya Malaka uliwafaidia sana, kwa sababu meli zote zilipaswa zipitie huko na kutia nanga bandarini mwao.

Papohapo, meli za Srivijaya zilishiriki katika biashara ya Bahari ya Hindi. Ingawa kuna vyanzo vichache vya kimaandishi vya Waarabu kuhusu safari hizo, lakini vyanzo hivyo ni vya muhimu sana, na chanzo kikuu kati yake ni maelezo mashuhuri ya uvamizi wa watu wa Wak-wak huko Kanbalu (Pemba) (katika 945-6).

Ukweli kwamba kulihitajika mwaka mmoja mzima kwa watu hao kusafiri kutoka maskani yao kwenda Afrika Mashariki ulikwishamfanya msimulizi kuhitimisha ya kuwa visiwa vya Wak-Wak vilikuwa katika eneo lililokabiliana na Uchina. Waandishi wa Kiislamu walidhani kuwa neno Wak-Wak liliashiria kanda mbili au watu wa aina mbili - moja katika sehemu ya kusini magharibi ya Bahari ya Hindi, ikiwa ni pamoja na Bukuni, na mwambao wa Afrika kusini mwa Sofala, na ya pili katika Asia ya Kusini-Mashariki, katika Indonesia ya leo.

Kwa hiyo baadhi ya tondoti za masimulizi ya Ibn Laki zinaashiria pasi kukosea kuwa Asia ya Kusini-Mashariki ndiyo maskani ya watu wa Wak-Wak. Aidha, kwa vile Himaya ya Srivijaya katika kipindi hiki ilijulikana kuwa ilikuwa taifa lenye nguvu za baharini katika mashariki ya Bahari ya Hindi, halitakuwa jambo la kushangaza kuhesabu safari hizo za masafa marefu kama ni jitihada za kupanua biashara ya Srivijaya ili kupata njia ya moja kwa moja ya kufikia vyanzo vya bidhaa zitokazo Afrika na kwa hiyo kuepuka ukiritimba wa Waislamu. Ni kiasi gani safari hizi (na al-Idrisi anathibitisha kuwa meli za Indonesia pia ziliendelea kufika pwani ya Afrika ya Bukuni katika karne za baadaye) zilihusiana na luja mpya za Waindonesia kuhamia Bukuni kati ya karne ya kumi na kumi na mbili na mbili ni suala ambalo bado halijafumbuliwa. Kwa upande wa pili, inawezekana kuwa uhamiaji huo wa baadaye ulikuwa unahusika na mashambulizi ya Wachola wa Kusini mwa Bara Hindi kwenye Srivijaya katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na moja; mashambulizi ambayo yalikuwa na athari ya kudhoofisha dola hiyo, na pengine ndiyo yaliyosababisha uhamaji na miguro mingine ya watu.

## *Hitimisho*

Tukilinganisha na kipindi kilichotangulia, kadri na aina ya mawasiliano kati ya bara la Afrika na sehemu nyinginezo za kanda ya Bahari ya Hindi ilipata mabadiliko kadha ya kikiasi na kisifa.

Mosi, tunaona kuwa watu kutoka Mashariki ya Kati wanaongezeka katika sehemu zote za eneo hilo, hususani kwenye mwambao wa Afrika Mashariki. Jambo hili lilihusiana na usitawi wa Ukhalifa kama ndio dola kuu ya kisiasa, kitamaduni na kiuchumi. Waislamu waliweza kuhodhi biashara ya Afrika Mashariki na walikuwa na mamlaka juu ya mahusiano na nchi za kigeni katika kanda hizo. Wakati mawasiliano hayo bila shaka yalichangia katika usitawi wa miji kadha ya pwani kama vituo vya biashara za kimataifa na kusababisha utokezaji wa tabaka la Waafrika waendesha biashara, lakini inafaa kukumbukwa kuwa idadi kubwa ya watumwa wa Kiafrika walikuwa wakisafirishwa kwenda nje ya bara hili na walichangia katika uchumi wa nchi kadha za Kiasia, hasa katika Mashariki ya Kati.

Pili, mawasiliano ya moja kwa moja na Bara Hindi yalififia sana. Kabla ya karne ya saba, meli za Kiethiopia zilifanya biashara na bandari za Bara Hindi na mahusiano hayo yanathibitishwa wazi na dafina za sarafu za Kihindi (Kikushi) zilizopatikana Ethiopia, pamoja na mabaki mengi ya athari za Kihindi katika utamaduni yakiniifu na wa kisomi. Kati ya karne ya saba na karne ya kumi na moja, hakuna kitu chochote kinacholingana na hayo: hii ni kwa sababu safari kati ya Bara Hindi na Ethiopia zilikuwa zimeingia mikononi mwa Waislamu.

Tatu, WaIndonesia waliendelea kudumisha mawasiliano yao na Bukuni na hata na sehemu kadha za pwani ya Afrika. Lakini, inaelekea athari zao katika mrima hazikuwa kubwa; madai ya baadhi ya wanazuoni kuhusu mchango mkubwa wa Indonesia katika utamaduni wa Kiafrika yanapaswa kufikiriwa kuwa ni nadhariatete zisizo na ithibati ya kutosha.

Sasa tuangalie nafasi ya watu wenye asili ya Kiafrika katika muktadha wa Bahari ya Hindi. Katika kutathmini kipengee hicho tunapaswa kukumbuka kuwa katika kipindi hicho sehemu ndogo tu ya bara la Afrika, yaani ukanda mwembamba wa mwambao, ilikuwa na mawasiliano na dunia iliyoko nje yake. Idadi ya Waafrika ambao walikuwa na athari yoyote au walioathiriwa kutoka nje bila shaka ilikuwa ndogo. Hata hivyo, nafasi yao haiwezi ikapuuzwa. Kinyume na hayo, Waafrika walichangia vikubwa katika mabadiliko makuu yaliyotokea katika takadiri ya himaya kubwa. Maasi ya Wazanji yalikuwa na athari kubwa katika nyanja za siasa, jamii na uchumi: yalivunja umoja wa dola ya Waislamu na kusababisha kuanguka kwa utawala wa zamani wa Kiabbasi. Mzozo wa kisiasa uliotokana na maasi ya Wazanji uliongeza mtafaruku kati ya matabaka ya kijamii. Tabaka la wakwasi, katika kuogopa kupoteza maslahi yao, likaanza kuamini kuwa majeshi ya maaskari wa kukodishwa wa Kituruki na mamluki wengine ndiyo peke yao wangeweza kudumisha amani. Hii ikaanzisha enzi mpya katika historia ya Mashariki ya Kati ya Kiislamu. Maasi hayo pia yakawa fundisho kwa matabaka tawala ya Kiislamu: baada ya hapo kamwe hapakutokea mfano wowote katika Mashariki ya Kiislamu ya shughuli yoyote kubwa yenye kutumia nguvukazi ya watumwa, na yaelekea watumwa hawakutumiwa tena katika kilimo na umwagiliaji. Hayo yalisababisha kukua kwa ukabaila katika karne iliyofuata kama mfumo mkuu wa uzalishaji katika nchi za Kiislamu za Mashariki, na kutoweka kwa utumiaji wa watumwa kukaletea mfumo wa ukabaila. Inaelekea kuwa wakati huo tokeo jingine la maasi ya Wazanji lilikuwa kushadidisha hisia za kijamia na kuwadunisha Waafrika, ingawa Uislamu unakataza hayo, na maudhui mengi ambayo hayakujulikana kabla ya hapo yenye mielekeo hasi kwa watu weusi yalianza kujitokeza katika maandishi ya Waislamu.

Jiha nyingine za historia ya Afrika katika kipindi hicho zilitokana na maingiliano kati ya kanda mbalimbali za Bahari ya Hindi. Miongoni mwa jiha zinazofaa kutajwa ni kuongezeka kwa ushiriki wa miji ya Pwani ya Afrika Mashariki katika biashara ya kimataifa ya baharini. Ingawa meli zilikuwa zinamilikiwa na wafanyabiashara wageni, wazalishaji na wasafirishaji nje walikuwa Waafrika wa mwambao. Ingawa maisha ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni ya Kiswahili yalisitawi katika karne zilizofuata, lakini msingi wake uliwekwa katika kipindi hiki kinachozungumziwa.

# 2

## Majilio ya uislamu na ustawi wa himaya ya waislamu

### Utangulizi

Madhumuni ya sura hii ni kueleza majilio ya Uislamu, ueneaji wa siasa yake na ukuzi wa itikadi zake. Maelezo hayo yatakidhi haja ya kuwa na usuli ambao utasaidia katika kuelewa vizuri zaidi masuala ya kihistoria na kiitikadi ambayo yatajadiliwa au kutajwa katika juzuu hili na katika majuzuu yaliyobaki ya *Historia Kuu ya Afrika*

Katika mtazamo wa Kiislamu si sahihi kusema kwamba Nabii Muhammad ndiye aliyekuwa mwasisi wa Uislamu au kwamba alikuwa akihubiri imani mpya. Uislamu sio jina la imani ya kipekee iliyoletwa kwa mara ya kwanza na Muhammad kwa sababu yeye alikuwa nabii wa mwisho kati ya manabii ambao kila mmoja wao alikariri imani ya nabii aliyemtangulia. Baada ya kuleta mitume katika vipindi mbalimbali kuwaongoza wanadamu, Mwenyezi Mungu aliamua kuwa wanadamu walikwishafikia daraja lile la ukamilifu la kuwawezesha kupokea ufunuo wake wa mwisho. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu akamteua Mwarabu kutoka mji wa Maka aitwaye Muhammad ibn Abd Allah wa kabila la Wakuresthi kuwa nabii wa mwisho.

Watangulizi wa Muhammad katika unabii walikuwa Ibrahim, Musa na Yesu Ukristo ambao wote walihubiri imani katika Mungu mmoja kutokana na misahafu waliyoteremshiwa na kufunuliwa kutoka Mbinguni. Watu waliowaamini manabii hao na misahafu yao, Wayahudi na Waukristo, waliitwa *Ahl-al-Kitab*, yaani watu wa Msahafu. Kwa vile watu hawa ni watu wenye sehemu ya likweli uliofunuliwa basi wanastahiki kuchukuliwa na Waislamu kuwa ni watu mahsusi.

Kwa hiyo, Muhammad siyo mwasisi wa Uislamu, dini ambayo ilikwishakuwepo, ila tu ni wa mwisho katika silisila ya manabii, akiwa ndiye "Mwisho wa Manabii" (*Khatimu l-nabiya*). Uislamu

unawatukuza manabii wote waliotangulia kuwa ni wajumbe wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu. Kwa mujibu wa itikadi ya Kiislamu, Yesu Ukristo alikuwa mahuluki kama wengine, ingawa ilikuwa kudra ya Mungu kuwa kuzawa kwake kuwe kwa kimuujiza; lakini hiyo haina maana kuwa alikuwa Mungu. Mama yake, Siti wetu Mariamu *mawlatuna Miryam*, kama wanavyomwita Waislamu anaheshimika sana 3katika ulimwengu wa Waislamu. Yesu Ukristo hakuuliwa na Mayahudi bali aliitwa na Mungu arudi Mbinguni.

Muhammad mwenyewe alisisitiza kuwa yeye alikuwa binadamu tu na alipambanua waziwazi kati ya ubinadamu wake na dhima yake ya Utume. Lakini kwa vile ni muhali kwa Nabii Muhammad kuwa mjumbe wa Mungu na kutenda kinyume na mapenzi ya Mungu,

imani katika uongozi wake katika mashauri ya kidunia ikashikiliwa sana katika dini ya Uislamu Tutarejea dhima ya mapokeo ya Kitume (sunna) hapo baadaye.

### *Maisha ya Muhammad*

Mwanzoni mwa karne ya saba ya enzi ya Ukristo Bara Arabu ilikuwa imekaliwa na idadi kubwa ya makabila yaliyokuwa huru kisiasa na ambayo kwa pamoja yaliunda kaumu moja yenye lugha moja na utamaduni mmoja. Wengi wao walikuwa Wanomadi (Mabedui), lakini kusini mwa Arabuni na katika oasisi nyingi watu wenye makazi ya kudumu waliendesha kilimo. Kwenye njia za kale za biashara zilizotokea pwani ya Bahari ya Hindi hadi kufikia Mediterania, ilikuwapo miji kadha ambamo watu wake walifanya biashara. Mji wa Maka ulikuwa kituo kikuu cha biashara na dini huko Arabuni. Aghalabu Waarabu wa enzi ya kabla ya Uislamu walifuata dini za mizimu na waliabudu miungu au mizimu waliyoamini kuwa iliishi majabalini, mitini au visimani. Baadhi ya miungu walikuwa na asili ya kinyota (Jua, sayari Venasi). Kulikuwapo pia dhana ya 'Mungu' aitwaye Allahlakini hakuabudiwa. Sanamu za baadhi ya miungu hiyo ziliwekwa katika hekalu ya kale iliyojulikana kwa jina la Ka'aba huko Maka.

Vilevile huko Arabuni kulikuwapo makao makubwa ya watu waliofuata dini ya Warumi; wengi wao walikuwa Waarabu waliogeuzwa dini na aghalabu waliokuwa wakiishi katika oasisi. Ukristo ulilingia Arabuni mapema sana. Vituo vyake vikuu vilikuwa kusini mwa Bara Arabu (Nad'ran) na pambazoni mwa jangwa katika Mesopotamia na Transjordan. Waukristo wachache walisambaa katika miji yote, na watawa wapweke waliishi majangwani.

Lakini kwanza Muhammad aliletwa kwa ajili ya Waarabu wapagani kuwahubiria ujumbe wa Mungu. Alizaliwa Maka mara tu baada ya kifo cha baba yake na kuwa yatima udogoni; alikuwa akiishi kama mfanyabiashara hadi alipofikia umri wa miaka arubaini. Mnamo mwaka 610 wa enzi ya Ukristo, Mtume Muhammad alipata ufunuo wa kwanza kutoka kwa Mwenyezi Mungu ulioletwa na Malaika Jibrili (Gabriel), ambao ulimwamrisha kuhubiri Uislamu kwa wanaadamu wenzie. Ufunuo huo wa mwanzo ulihusika na upeke wa Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na kuwasih watu wasipuuze dini kwa kutamani dunia. Ufunuo huo pia uliweka misingi ya usawa wa wanadamu wote pasi kuzingatia hadhi zao za kijamii au utajiri wao.

Muhammad alipoanza mahubiri yake na kukusanya jumuiya ndogo ya waumini, watawala wachache wa Maka ambao walikuwa wafanyabiashara na wamiliki-benki walitambua mapinduzi yaliyokuwemo katika ujumbe huo na kuyaona kuwa ni tishio kwa maslahi yao. vilevile kulikuwa na hofu kwamba jiji la Maka ambalo lilikuwa kituo cha upagani wa Kiarabu pamoja na hekalu lake la Ka'ba, lingepoteza umuhimu wake kwa sababu ya dini hiyo mpya. Sifa za kimaadili na kiakili za Muhammad, zilizoimarishwa na ujumbe wake wa kitume, zikamfanya aonekane mpinzani hatari wa watawala hao. Kwa hiyo, historia ya Muhammad na jumuiya yake hadi mwaka 622 ni kisa cha mateso na hata majaribio ya kumwua. Katika hali kama hiyo, Mtume aliwaamuru baadhi ya waongolewa wake kuhamia Ethiopia ya Kiukristo, ambako walipokelewa kirafiki na mfalme Negus.

Mateso yaliposhtadi Muhammad na wafuasi wake walihamia mji wa oasisi wa Yathrib, ambao baadaye uliitwa *Madinat al Nabii* (Jiji la Mtume) na punde tu baada ya hapo kuitwa Madina. Hilo lilijiri mnamo mwaka 622 wa enzi ya Ukristo, ambao ndio ukawa mwaka wa



kwanza wa kalenda ya Waislamu. Uhamaji huo toka Maka kwenda Madina unajulikana kama hijra.

Muhammad alikaribishwa Madina na wakazi wake ambao baadaye waliitwa *Ansar* (Wasaidizi) na wale wahamiaji kutoka Maka waliitwa *Muhajirun* (wale waliofanya safari ya hijra au Wahamiaji). Makundi haya mawili kwa pamoja hufanya kundi la *Ashab* - Sahiba (wa Mtume). Katika miaka iliyofuata hadi kifo chake katika mwaka 63, Mtume aliimarisha na kutawala jamii ya Kiislamu (Kiarabu: *umma*) akiondosha mashambulizi ya maadui zake wa Maka na akapata mamlaka makubwa kwa njia ya diplomasia na vita katika maeneo makubwa ya makabila ya Kiarabu. Alipopata nguvu na uwezo wa kutosha alirudi Maka kama mshindi na kiongozi wa siasa na dini ambaye mamlaka yake yalikuwa ya mwisho. Wakati Mungu alipomchukua duniani Muhammad alikuwa takriban ndiye mtawala wa Bara Arabu yote.

### Mafundisho ya Kurani

Akiwa Maka na Madina Mtume aliendelea kupata ufunuo mfululizo katika umbo la aya za Kurani zilizopangiliwa katika sura. Sura 114 kwa pamoja, zisizolingana kwa urefu, hukamilisha Kurani.

Kurani si 'kitabu kitakatifu' kitichoandikwa na Muhammad. Neno hilo lina maana ya kukariri na kwa hakika, alichokifanya Muhammad ni kusoma neno la Mungu aliloambiwa na malaika Jibrili (Gabriel).

Mafundisho ya Kurani yanajumuisha kila kitu na yamekusudiwa kumpa mwanadamu welekea katika dini na katika mahusiano yake na watu wengine. Mafundisho na kanuni za Kiislamu ndiyo msingi wa imani ya Kiislamu.

Kanuni ya kwanza ya Kurani ni ukamilifu wa kipekee kama ulivyoielezwa katika shahada: 'Hapana mungu ila Mwenyezi Mungu' na Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu." Imani katika utume wa Muhammad ni sehemu muhimu ya shahada hiyo, kwa sababu pasi kuwako ujumbe wake wa kiutumbe Uislamu haukaniliki.

Kwa hiyo shahada ni nguzo mojawapo ya 'Nguzo Tano za Uislamu' (*arkan al islamu*). Nguzo ya pili ni faradhi ya kila Mwislamu ya kuswali (*salat*) mara tano kwa siku na kuswali swala hizo akiwa ameelekea Maka. Sehemu muhimu kabisa ya swala hizo ni unawaji na kujitia udhu kabla ya kuzitekeleza. Nguzo ya tatu ni mfungo (*saum*), ambao unahitajia kuaacha anasa zote za kimwili (kula, kunywa, ngono, n.k.) tangu alfajiri hadi magharibi katika mwezi wa Ramadhani, ambao ni mwezi wa kumi wa mwaka wa mzunguko wa mwezi. Wagonjwa na wasafiri katika mwezi wa Ramadhani, wanawake katika uchungu wa uzazi, wafanyakazi wa shughuli za sulubu na wapiganaji vitani wanasamehewa wasifunge, ilimuradi walipize saumu hizo siku za baadaye. Nguzo ya nne ni zaka (zakat), ambayo ni kutoa sehemu ya inali kuwapa maskini na baadhi ya wahitaji. Sehemu hiyo huwa kati ya 2.5% hadi 10%. Zaka (*Zakat*) husisitiza umuhimu wa moyo wa kutoa. Zaka ilikusanywa na jumua ya Uislamu (*umma*) na kugawanywa iniongoni mwa watu waliotajwa katika Kurani. Zaka hiyo hufanana na huduma za ustawi wa jamii wa kisasa zierendeshwazq na serikali. Nguzo ya tano ni kwenda kuhiji Maka (hajji). Katika nguzo hiyo ndimo ujumbe wa dini ya Kiislamu kwa watu wote unajitokeza dhahiri. Waislamu kutoka kila upande wa dunia hujumuika huko Maka katika mwezi wa *Dhul-Hijja* kutekeleza ada mbalimbali. Kuhiji ni faradhi kwa kila Mwislamu, lakini analazimika tu kutekeleza faradhi hiyo iwapo ana uwezo wa kufanya hivyo. Kwa sababu hiyo idadi ya watu wanaoweza kutekeleza faradhi hiyo ni ndogo kulingana na jumla ya idadi ya

Waislamu duniani. Hata hivyo, hija bado ndio mjumuiko mkubwa kuliko mijumuiko yote ya wanaadamu wa kimataifa duniani hii leo; nayo humfanya hujaji atambue vema maadili ya Kiislamu na humfanya aheshimike arudipo nyumbani baada ya kuhiji.

Siku ya Kiyama ni kiini kimojawapo cha imani ya Kiislamu; historia nzima ya mwanadamu itamalizika siku ya kufufuka na siku ya Kiyama. Watu wote watasimama mbele ya Mwenye Enzi Mungu kwenye hukumu ya mwisho, kila mmoja atahukumiwa kwa mujibu wa vitendo vyake na kumgizwa Peponi (*Janna*; yaani Bustani) au Motoni.

Vilevile ndani ya Kurani mna makatazo na maamrishi ya maisha ya kidunia. Kurani inakataza ulaji wa nguruwe na wanyama wengine kadha na unywaji wa mvinyo na ulevi. Katika sura ya 17, aya 23 -40, kuna mwongozo kuhusu mwenendo wa kila siku; ubadhirifu wa mali, kujiona na kuwa na kiburi kunalaaniwa na waumini wanaamrisha wawe waadilifu katika vipimo na uzami.

Ingawa utumwa unatambulikana, lakini watumwa wanatakiwa waonewe huruma, waruhusiwe kuoana na wahamasishwe kununua uhuru wao. Mabwana wanashauriwa wawaachilie huru watumwa waumini.<sup>1</sup>

Uislamu unatangaza usawa wa wanawake na wanaume, ila mila zinazokengeuka itikadi rasmi zimeficha jiha hiyo ya Uislamu Hata hivyo, katika sharia, wanawake wa Kiislamu wamekuwa na hadhi ya kisharia ambayo hadi hivi karibuni wanawake wa dini nyingine wamekuwa wakiihusudu. Wanawake wa Kiislamu siku zote wamekuwa na haki ya kwenda mahakamani pasi kuwauliza waume zao na kuendesha miliki yao bila ya kuwategemea waume zao.

Kurani humruhusu mwanamume kuoza wake wanne. Kanuni hii ilikuwa ni ya kimaendeleo kwani iliwekea masharti uoaji wa wake wengi ambao ulikuwepo kabla ya majilio ya Uislamu; na hivyo kuondoa kabisa uoaji wa aina hiyo au walau kupunguza kaida hii ya kijamii.

## Sharia na Fikhi

Uislamu sio dini tu bali pia ni njia kamilifu ya maisha ambayo inashughulikia nyanja zote za maisha ya mwanadamu. Uislamu huongoza kila mwenendo wa maisha - wa kibinafsi na wa kijamii, wa kimali na kimaadili, wa kiuchumi na kisiasa, wa kisharia na kiutamaduni, wa kitaifa na kimataifa.

*Sharia* ina maana ya kanuni timilifu ya mwenendo au mkusanyo wa kaida zinazotawala aina na njia za ibada, vigezo vya maadili na maisha, na sharia zinazoruhusu na kuamrisha, na zinazo hukumu kati ya haki na batili. Vyanzo vya *sharia* ni Kurani na *hadithi* (misemo ya Mtume), yaani vitendo vya Mtume Muhammad vilivyohifadhiwa na kupokewa na masahaba zake. Maelfu ya *hadithi* yalichujwa na kukusanywa na wanazuoni katika mikusanyo ya mapokeo, mashuhuri miongoni mwa hiyo ni makusanyo ya al-Bukhari (t.k. 870) na Abu Muslim (t.k. 875). Mambo yaliyomo katika mapokeo ya Mtume yanaitwa *sunna*, yaani tabia na mwenendo wa Muhammad.

Elimu inayosimba kanuni na kueleza maamrishi ya *Sharia* huitwa *fikh* na wanazuoni wenye elimu hiyo ni *fakihi* (wingi katika Kiarabu: *fukaha*) au wanasharia; kwa vile *fikh* ni elimu hasa ya Kiislamu, *fakih* wanahesabiwa kuwa ni wanazuoni au *ulama* (umoja: alim).

Madhali Kurani haizungumzii kadhia maalum na huweka misingi ya jumla ya kuelekeza

<sup>1</sup> Kwa mjadala wa mwelekeo wa Kiislamu kuhusu utumwa angalia sura ya 26 ya Juzuu hili.



2.1 Uwakilishi wa Maka: mapambo haya ya ukutani yametengenezwa Iznik, yanaonyesha kwa juu mchoro wa Msikiti Mkuu wa Maka na minara yake saba. Katikati ya uga mtu anaweza kuona Kaaba - ambayo inasemekana kuwa ilijengwa na Ibrahim - katika pembe liko Jiwe Jeusi ambapo Waislamu hawana budi, kama ikiwezekana, waabudie angalau mara moja katika maisha yao. Kila jengo dogo - na kila mlango - umepewa jina katika hati za Naskhi. Juu ya mchoro sura ya Korani iliyoandikwa kwa mikogo (Sura 3:90-2) inaelezea wajibu wa hija. (Hatimiliki ya picha: Maonyesho ya taifa, Paris).

maisha ya Waislamu, ilionekana kuwa majibu ya masuala fulani yaliyoikabili jamii ya Waislamu hayakupatikana katika kitabu kitakatifu wala katika hadithi za Mtume. Kwa hiyo, yanzo viwili viliongezwa kwenye sharia ya Kiislamu; mosi, kufikiria mambo kwa kutumia analogia (kiyas), ambayo ina maana ya kulinganisha kadhia inayotafutiwa ufafanuzi na kadhia ya aina hiyo iliyokwishaamuliwa kwa mujibu wa Kurani au hadithi fulani, na, pili, usuluhishi wa tauizo kwa kufuata kongamano la maulama mashuhuri (ijma).

Kati ya karne ya nane na karne ya tisa, wanazuoni kadha mashuhuri walisimba kanuni zote za Kiislamu na kuzifanya ziwe mfumo mmoja thabiti. Mielekeo ya kila mmoja wao kwenye kazi hii kubwa ilitofautiana na matokeo yake yakawa madhehebu manne ya sharia (*madhhab*, w. *madhahib*) yaliyochukua majina ya waasisi wake, ambao wamepewa lakabu ya heshima ya *Imam*.

Madhehebu hayo manne ni Hanafi Maliki, Shafi na Hambali. Madhehebu hayo yote manne ni ya sunni na huhitilafiana tu katika mambo ya tafsili. Hivyo, haisadifu kuyaita madhehebu hayo dini tofauti.

Ingawa katika historia kulikuwepo mabadiliko mbalimbali, lakini kila moja ya madhehebu hayo yanafuatwa katika maeneo maalum ya kijiografia; madhehebu ya Kihanafi yanatawala katika kanda ambazo zilitawaliwa na wafalme wa Kituruki, yaani Uturuki, Sham, Iraki, Asia ya Kati na Kaskazini mwa Bara Hindi/Pakistani; madhehebu ya Kishafi'i hupatikana Pwani ya Bahari ya Hindi, toka kusini mwa Arabuni na Afrika Mashariki hadi Indonesia; ambapo madhehebu ya Kimaliki yalianza zanam sana luko Afrika Kaskazini, Hispania ya Waislamu na Sudan ya magharibi na kati. Madhehebu ya Hambali ambayo yalikuwa yakifuatwa na watu wengi katika Sham na Iraki, sasa yanafuatwa katika Saudi Arabia tu.

Mojawapo ya sifa kuu za sharia ya Kiislamu ni utathmini wa vitendo vyote na mahusiano yote ya binadamu kufuatana na dhana zifuatazo: faradhi (*Wajib*); iliyopendekezwa (*mandub*); isiyokuwa na upande maalum; (*mubah*); isiyofaa au makruhi (*makruh*) na iliyokatazwa (*mazhur*).

Sifa moja ambayo inatofautisha *fiqh* kutoka mifumo mingine ya kisharia ni kuwa *fiqh* iliundwa na kukuzwa na wataalamu binafsi wa sharia. Taifa halikupitisha maamrisho; hivyo, halikutunga sharia wala vyombo vya taifa havikuamrisha kanuni rasmi. Badala yake, sharia ziliingizwa katika mwongozo wa kitaaluma ambao ulikuwa na mamlaka ya kisharia na ulitumiwa kama marejeo katika maamuzi halisi ya kisheria.

Muundo wa Uislamu ni wa namna ambayo haikuzaa aina yoyote ya muundo mwingine nje ya ule wa Kiislamu au utawala msonge. Hakuna ukuhari wala kanisa katika Uislamu Kila mmoja huhijubiri mwenyewe na hakuna mtu wa wasta kati ya muumimi na Mungu. Ingawa Uislamu ulitambua *idjma*, komangano la maulama, kuwa ni chanzo sahihi cha sharia ya Kiislamu, hapakuwa na baraza wala mahakama ya kutangaza maamuzi yake.

Lakini kilichojiri ni kuwa maulama katika hamu yao ya kuweka maamrisho ya Uislamu kwa kila jambo la ibada na maisha ya kila siku waliishughulisha sana na ada zinazohusiana na sharia za ibada na hawakujiachia nafasi kwa ibada ya binafsi. Jambo hilo lilisababisha kutokoa kwa usufii<sup>2</sup> wenye kupinga usomi na urasimi. Kabla ya karne ya kumi na mbili Masufii wengi maarufu walichangia katika uimarishaji wa imani za Kiislamu. Kwa upande wa pili, baadhi ya

2 Kutokana na neno la Kiarabu suf (sufi) kuashiria ada ya kuvaa joho la suf. Katika Kiarabu usufi unaitwa tasawwuf

wafuasi wa usufii walikuwa wakipuuzwa faradhi anazopaswa kutekeleza kila Mwislamu. Katika karne ya kumi na moja, mwanazuoni mashuhuri Al-Ghazabi (t. 1111) aliingiza usufii katika urasimi kwa kusisitiza kuwepo kwa uhusiano kati ya mtu binafsi na Mungu na wajibu wa kila mtu katika kufuata maamrishi ya *sharia* kuwa sehemu zisizotenganika za maisha ya kidini ya Mwislamu. Punde baada ya hapo, masufii walianza kujiandaa katika jumuiya za kisiri au tarika wakiongozwa na viongozi wa kidini waitwao mashekhe (Shaykhs). Wakati ulivyoziidi kupita tarika zikaongezeka. Kwa hiyo takribani kila Mwislamu akawa mwanatarika moja au nyingine.

Tarika hizi zinazoheshimika na kutambulika hazina budi kutofautishwa na madhehebu ya watakatifu, ambayo yanajulikana kama *marabout* huko Maghrib. Wengi wa hao *marabout* waliwadanganya Waislamu wenyeji kwa kudai kuonyesha miujiza, kwa kutengeneza hirizi na kago na kudai kuwa na uwezo wa kumfikia Mungu moja kwa moja na hivyo kuweza kuwapatia shufa wengine. Kwa mujibu wa Uislamu sahihi, ukupe ndio uliosababisha madhehebu haya ya "Watakatifu".

### *Faraka za Kiislamu*

Chanzo cha mgawanyiko mkuu hadi kuzua faraka kilikuwa siasa. Ni baadaye tu ambapo mgawanyiko huo uligeuka kuwa wa kitiikadi.

Tatizo kuu lililowashughulisha Waislamu wa mwanzoni lilikuwa nani awe mrithi wa Muhammad, si kwamba awe Mtume bali awe kiongozi wa jumuiya ya Kiislamu. Katika uhai wake, Mtume mara kwa mara alisema kuwa mfumo unaofaa wa kutawala jumuiya ulikuwa ule uliojulikana kama *shura* au kushauriana, ambao hivi leo unatambulikana kwa jina la demokrasia. Baada ya kufa kwa Mtume warithi wake walichaguliwa na wakaanza kuwa Makhalfi. Makhalfi wanne wa kwanza, waliojulikana kama *al-khulafa'al-rashidun* (Makhulafa waongofu) walikuwa Abu Bakr, Umar, Uthman na Ali; wote walikuwa wa kabila la Kureshi na walikuwa na mnasaba na Mtume kwa ndoa. Ali alikuwa binamu yake Mtume. Khalifa wa tatu Uthman alipouliwa na kikundi cha Waislamu waasi waliochukizwa na baadhi ya sera zake, na Ali bin Talib kuteuliwa huko Madina kushika nafasi yake, uteuzi huo ukawa haukukubaliwa na baadhi ya masahaba, hususani Muawiya, Gavana wa Shanu. Matokeo yakawa vita vya wenyewe kwa wenyewe kati ya wafuasi wa Ali na wafuasi wa Muawiya. Khalifa Ali alipokubali kuundwa kwa tume ya uamuzi wenye wajumbe wawili, mmoja akimwakilisha yeye na mwingine akimwakilisha Muawiya, wafuasi wake wengi walisusia ufumbuzi huo na wakaonyesha kutoridhika kwao kwa kujitenga naye; hivyo wakapewa jina la Wakhariji (kutokana na neno la Kiarabu: *kharaja* - kutoka nje). Katika karne ya saba na ya nane, Wakhariji waliwaasi Makhalfi na Serikali Kuu mara kwa mara, aghalabu nchini Iraki, Arabuni, Iran na nehi za jirani. Tangu mwanzo, Wakhariji waligawanyika katika faraka nyingi zilizotofautiana katika nadharia na amali. Walisisitiza umuhimu wa vitendo, siyo imani peke yake, na walidai kuwa yeyote aliyetenda dhambi kubwa hakuwa muumini. Kinyume na Waislamu wengine ambao waliuchukulia Uimamu (au Ukhalifa) kuwa ni haki ya baadhi tu ya nasaba ya Mtume (ama ya Wakuresh kwa jumla, au hususani familia ya Ali), Wakhariji walishikilia kuwa mtu yeyote angeweza kuchaguliwa kuwa kiongozi wa jumuiya ya Waislamu: iwapo alikuwa na sifa zilizohitajika za takua, uadilifu na ujuzi wa kidini. Mwelekeo huo wa kidemokrasia uliwanntia wale waliokuwa hawakuridhika na serikali. Huko Maghrib, baadhi ya faraka za Wakhariji- Waibadi, Wanukkari na Wasufri zilipata fursa nzuri ya kuenza

itikadi zao miongoni mwa Waberiberi waliokuwa hawaridhiki na utawala dhalimu wa Waumaya.<sup>3</sup>

Wale waliobaki na Ali waliitwa *Shi'atu Ali*, yaani wafuasi wa Ali, na ndipo jina lao la Shia lilipotokea katika lugha za Ulaya. Tofauti na Wakhariji, ambao walihitilafiana na Waislamu warasimi katika masuala ya kisiasa na kimaadili tu, Shia walikwenda mbali zaidi na kuongeza itikadi nyingi mpya ambazo zilikuwa za kidini. Waliikataa dhana ya makubaliano ya kijumuiya na badala yake waliani kuwa katika kila zama kuna *Imamu* intakatifu ambaye Mungu amemteua kuwa kiongozi wa wanadamu. *Imamu* wa kwanza alikuwa Ali na maimamue waliomfuata walitokana na dhuria yake. *Maimamu* hao walihesabiwa kuwa waliteuliwa na Mungu na kuwa ni walimu wa waumini na hivyo walikuwa na haki kamili ya kuongoza jumuiya ya Waislamu. Shia wanaamini kuwa hata baada ya Imamu wa mwisho kutoweka duniani anaendelea na uongozi wake kama "*Imamu asiyeonekana*." Atarudi siku moja kurejesha amani na haki duniani kama Mahdi (aliyeongozwa na Mungu).

Shia pia waligawika katika faraka kadha; tofauti kubwa kati yao ilikuwa ni nani hasa awe "*Imamu asiyeonekana*". Kikundi muhimu, kadri historia ilivyosonga mbele, kikawa cha Wathenashara (*Ithna'ashariyya*) ambacho kinamkubali mrithi wa kumi na mbili wa Ali, Muhammad al-Mahdi ambaye alitoweka katika mwaka 880. Shia ithnaashari wengi leo hupatikana Iran, ambako aina hii ya Ushia imekuwa dini ya kitaifa tangu karne ya kumi na sita. Vikundi vikuu vya Shia pia hupatikana Iraki, Shamu, Lebanon na Bara Hindi.

Shia waliomtambua *Imam* wa saba, Isma'ili, walijitenga na kikundi hicho kikuu na wakajulikana kama Waismailiya au Wasaba (*Sab'iyyuna*). Kwa muda mrefu Waismailiya walikuwa wakiendesha mambo yao kwa siri, lakini walijitokeza hadharani wakati Wafatimi walipotawala. Wafatimi walifanikiwa zaidi kuliko matawi yote mengine ya Shia na waliasisi himaya iliyotanda tangu Atlantiki hadi Shamu na Hijaz.<sup>4</sup>

Kutokana na mafarakano kati ya Waislamu, urasimi ukashinda katika umbo la Usuni, wafuasi wa *Sunna*, yaani njia ya Mtume. Hao ni zaidi ya asilimia 90 ya Waislamu wote duniani. Hitilafu za kutikadi kati ya Sunni na Shia ni kama zifuatazo: vyanzo vya kanuni za Kisunni ni Kurani, *hadithi* za Mtume, makubaliano ya jumuiya na analojia, ilihali misingi minne ya kanuni za Kishia ni Kurani, *hadithi* za Mtume na *Maimamu*, makubaliano ya Maimamu na urazini.

Hata hivyo, mojawapo ya dhana asilia ya Kishia, yaani imani katika majilio ya *Mahdi*, iliingia katika Uislamu wa Kisunni, siyo kama amrisha rasmi kama ilivyo katika Ushia bali katika kiwango cha dini ya watu, ambapo *Mahdi* ni Masihi (Mwokozi) atakayerudi duniani, atamwua 'Mpinga-Ukristo' na kueneza haki, kwa sababu kabla ya hapo dunia itakuwa imejaa dhuluma na mateso. Katika karne zote zilizopita, *Mamahdi* walijitokeza katika nchi mbalimbali za Waislamu; mifano mashuhuri ni ya *Mahdi* wa Sudan Muhammad ibn Abdallah na wa Somalia Muhammad ibn Abdille.

## Mielekeo ya Waislamu kwa wasio Waislamu

Uislamu unatofautisha kati ya wale wasio-Waislamu lakini wanaofuata dini zenye Misahafu iliyoteremshwa, yaani *ahl-al-Kitab* (Watu wenye Kitabu), na wasio Waislamu wanaohesabiwa

3 Taz. sura 2, 9-12 ya juzuu hili

4 Taz. sura ya 12 ya Juzuu hili

kuwa ni waabudu miungu mingi, waabudu sanamu au wapagani. Wayahudi na Waukristo kama jumuiya yenye vitabu vitakatifu hawalazimiki kuwa Waislamu na ustahimilivu huo pia ulitumiwa kwa Majusi na baadaye hata kwa Wahindu (tukiachilia mbali miungu yao mingi) na Wabudha.

Kwa vile Mtume Muhammad alibaathiwa kuhubiri Uislamu hasa kwa wale ambao walikuwa bado hawajapata uongozi ulioteremshwa, yeye na warithi wake walikuwa na wajibu wa kupambana na upagani na kuwaongoa "inakafiri." Watu hao walipewa hiari ya ama kusilimu au kupigana; kama wangeshindwa vitani wangeishia kuwa mahabusi au watumwa.

Kuna dhana potofu nyingi kuhusu *jihadi*. Mara nyingi neno hili limetafsiriwa kwa makosa kwa maana ya "vita vitakatifu"; lakini hakuna kitu kama hicho katika istilahi hiyo, ambayo kwa hakika ina maana ya "kujitahidi kwa mtu kwa uwezo wake wote" na hivyo, kwa kunyambua maana hiyo, kupambana ili kutakasa nafsi ya mwanadamu.

*Jihadi* kwa maana ya vita ilichukuliwa na wanazuoni wa sharia (isipokuwa Wahambaliti) kuwa ni faradhi iwapo masharti fulani yametimia, kama vile sharti la kuwa wasioamini ndio waanze uhasama na kwamba kunakuwapo matumaini ya kutosha na kufanikiwa. Katika hali fulani mahsusi, *jihadi* hupata ikawa faradhi ya mtu binafsi hata kwa watumwa, wanawake na watoto kama wakati ambapo adui anashambulia nchi ya Kiislamu.

Vita vya utamalaki vilivyopiganwa na dola ya Kiislamu baada ya kutawafu Mtume havikunua kuwageza watu waliotamalakiwa maana wengi wao walikuwa wafuasi wa dini zenye misahafu iliyoteremshwa, kama vile Wakristo, Majusi na Wayahudi. Hawa waliwajibika kulipa kodi ya kichwa (*jizya*) na walilindwa (dhimmi), bila kulazimika kuacha dini yao. Nia kubwa ilikuwa upanuzi wa dola ya Kiislamu kama eneo ambamo *sharia* (kanuni za Kiislamu) zitatawala. Kusudio hili lilipambanua baina ya *Dar - al-Islam* na *Dar al- harb*, yaani eneo la Uislamu na eneo la vita. *Dar al Islam*, au eneo la Uislamu la *oekumene*, haina maana kuwa wakazi wake wote shurti wawe Waislamu, bali kwamba ni sehemu ya dunia ambamo utaratibu wa Kiislamu kijamii na kisiasa ulitawala na ibada ya Kiislamu kufanyika. Kinyume cha *Dar al Islam* ni *Dar al harb* kwa vile inaainisha eneo la dunia ambalo bado halijaingia chini ya miliki ya Kiislamu. Nadharia inayotawala fikra hiyo ni kuwa siku moja eneo hilo *Da al harb* litatoweka na kuunganika na eneo la *oekumene* ya Kiislamu.

Hata hivyo, tokea karne ya tisa na kuendelea, wakati Ukhalifa wa kilimwengu ulipotawanyika katika madola madogo madogo, ulusiano wa kuvuniliana uliwekwa kati ya ulimwengu wa Waislamu na *Dar al harb*. Mahusiano ya kisiasa na kibiashara na madola ya Ulaya, Asia na Afrika yalitawaliwa na nadharia ya kuwa baadhi yake zilikuwa katika *Dar - al - Sulh*, eneo la suluhu. Hapo pakajengeka msingi wa kisharia wa kuwa na mawasiliano ya kiamani kati ya Waislamu na madola ya wasio Waislamu.

### *Upanuzi wa Kiislamu, kuinukia na kuanguka kwa Ukhalifa*

Chini ya uongozi wa Makhaliifa wanne wa kwanza, Abu Bakr, Umar, Uthman na Ali,<sup>5</sup> Waarabu Waislamu walianza upanuzi wao wa nje ya mipaka ya Arabuni. Katika wakaa wa miaka michache, makabila ya kinomadi ya Waarabu, yakiongozwa na mfuatano wa majenerali hodari wenye asili ya Maka, yaliyashinda majeshi ya mataifa makubwa mawili, yale ya Himaya ya Ubizenti na ya Ajemi

5 Abu Bakar. 632-634; Umar, 634-644; Uthman, 644-656, 656-661

ya Wasasani. Kampeni dhidi ya Wabizenti katika Shamu ilichukua miaka miwili tu kumfanya mfalme na majeshi yake waondoke kwenye majimbo hayo katika mwaka 636. Utamalaki wa Ajemi ulichukua muda mrefu zaidi na baada ya vipingamizi vya mwanzo mwanzo Waarabu wakaendelea kupata ushindi. Vita vya Kadisiyya na utamalaki wa mji mkuu, Ktesiphon, katika mwaka 637, vilivaingiza Waarabu kwenye tambarare zenye rutuba za Iraki, magharibi mwa Mto Tigris. Hapo majeshi ya Waislamu yakaingia nyanda za juu za Iran yakifuatilia majeshi ya Waajemi yaliyokuwa yanarudi nyuma. Mapigano makubwa ya mwisho huko Nihawend (642) yalikuwa hatima ya Dola ya Kisasani. Baada ya kukalia sehemu nyinginezo za Iran, Waarabu walisonga mbele upande wa Mashariki; ilipofika mwaka 650 walikuwa wamekwishafikia mipaka ya Bara Hindi, Iraki ya Kaskazini, Armenia na *Amu-Darja* (Oxus).

Kutoka Shamu, majeshi ya Waarabu yalielekea Misri, ambayo ilitekwa kwa urahisi. Kati ya 639 na 642, Misri ya Chini pamoja na mji wake mkuu, Alexandria ilitekwa na majeshi ya uvamizi na Ubizenti ilipoteza jimbo jingine tajiri. Baadaye Waarabu walitumia jimbo hilo kama mahali pa kuanzia mashambulizi zaidi katika Aftika ya Kaskazini.<sup>6</sup>

Mojawapo ya sababu kuu za ushindi mwepesi wa Waislamu ulikuwa kuishiwa kwa fedha na majeshi katika himaya hizo mbili baada ya milolongo mirefu ya vita vyao. Vilevile, Wabizenti walikuwa wanachukiwa na raja wao wa Kisemiti na Kikhufu kwa sababu ya kodi zao za uonevu na dhuluma kwa makanisa ya "kijadi" ya Monofisita. Kadhalika hali ya aina hiyohiyo ilikuwapo katika himaya ya Sassanidi, kwa vile jimbo lenye rutuba nyingi kuliko yote katika Iraki lilikuwa likikaliwa na Waukristo wasemao Kiarami, ambao waliwapinga watawala wa Kimajusi. Kwa jumla, katika nchi nyingi zilizotamalikiwa, wenyeji hawakuonyesha upinzani dhidi ya Waarabu wavamizi kwa sababu hakuna walichopoteza au kufaidika nacho kutokana na mabadiliko hayo. Katika baadhi ya nchi hizo watu walidiriki hata kuwakaribisha Waislamu.

Vita vya wenyewe kwa wenyewe kati ya Alina Muawiya baada ya kifo cha Uthman, ambavyo vilimalizika baada ya ukoo tawala wa Kimaya kuahika madaraka katika mwaka 661, vilizuia upanuzi wa nje wa dola ya Waarabu kwa muda wa miaka kadha. Lakini, katika enzi ya Muawiya mipaka katika Afrika Kaskazini ilipanuliwa na Ukba ibn Nafi, ambapo katika Mashariki jimbo lote la Khurasan (Kaskazini mashariki ya Iran na Afghanistan) lilitamalikiwa na Mto Oxus kuvukwa (kati ya mwaka 673 na 674).

Wimbi la pili la kutamalaki kwenye mipaka yote lilianzishwa na Makhalifa Abd al-Malik (685-705) na al-Walid (705-715); katika magharibi, Maghrib nzima ilitamalikiwa na Hispania ikavamiwa ambapo katika Mashariki Transoksania ilitamalikiwa na papo hapo majeshi ya Waarabu yakasonga mbele hadi Mto Indus na kwa kufanya hivyo yakaongeza jimbo jipya la Sind katika Ukhalifa Mashambulizi zaidi pande za magharibi yalizuiwa na Wafranki, wakati juhudi za kushambulia kaskazini mwa Kaukasus zilitafirishwa na Wakhazari wa Kituruki. Kwa hiyo, kwa muda mrefu, majabali ya Pyrenees na Kaukasus yakawa ndiyo vikomo vya dola ya Waarabu.

Hivyo, miaka mia moja baada ya kifo cha Mtume, dola ya Waarabu ilikwishachukua eneo kubwa ambalo hapo baadaye likawa ndilo kiini cha ulimwengu wa Kiislamu. Waarabu wakawa ndio wamiliki halali wa dola hiyo na wakawa ndio watawala peke yao. Sera ya Waumaya ilikuwa kuendeleza hali hii, ambayo kwayo kila asiye Mwislamu alipaswa kulipa kodi, wakati Waarabu Waislamu walisamehewa na hata kulipwa pensheni kutokana na mapato ya kodi. Kwa hiyo, tabaka tawala la Waarabu halikupendelea uongoaji wa watu katika nchi walizotamalaki, na Waislamu

6 Taz. Sura za 7, 8 na 9 katika juzuu hili



wapya, ambao walipaswa kujihusisha na mojawapo ya mbari za Waarabu kama wateja (mawalii), bado walilazimika kulipa kodi. Kinyume na hayo, watu waliotamalakiwa (huko Sham na Iraki walizidi kuajiriwa katika utawala changamano wa dola bila kujali kama walikuwa Waajemi, Wakhufu au Waaramenia. Mikinzano iliyotokana na wachache kuclukua madaraka yote ya kisiasa na kufaidika na maslahi yote ya kiuchumi, na walio wengi japokuwa walikwishasilimu - kutokufaidika nayo, vilikuwa ndiyo sababu kuu za mzozo ambao uliishia kwa kuangushwa kwa utawala wa Kiumaya na kuinukia kwa ukoo tawala mpya, wa Waabbasi. Waabbasi waliweza kupata ushindi kwa sababu waliungwa mkono na sehemu zote zisizoridhika, hususani sehemu zile za Waislamu wasio Waarabu, ambao walidai hisa yao kamili katika jumuiya iliyoanzishwa kwenye msingi wa usawa miongoni mwa waumini wote. Mapinduzi ya Waabbasi yakakomesha "ufalme wa Waarabu" - kama ambavyo kipindi cha Waumaya huitwa wakati mwingine - na yakaanzisha dola ya Kiislamu, ambamo tofauti zilitazamwa kwa misingi ya kidini, badala ya misingi ya kitaifa. Ingawa Waarabu walipoteza hadhi yao ya kipekee, Kiarabu bado kiliendelea kuwa lugha ya dola, na ya fasihi na sayansi na kilitumiwa sana na watu wasio na asili ya Kiarabu.

Katika enzi ya Waumaya, makao makuu ya dola yalikuwa Shamu na mji wake mkuu ukiwa Damasko. Ingawa majimbo ya mashariki hayakupuzwa, lakini mkazo zaidi ulitiliwa kwenye ulimwengu wa KiMedutrania wa Misri, Afrika Kaskazini na Hispania.

Kuhamishwa kwa makao makuu kutoka Shamu kwenda Irak, ambako Waabbasiwalijenga Baghdad (katika 762), hakukusogeza tu kitovu cha himaya kijiografia bali pia kuliashiria mwanzo wa enzi mpya. Kinyume na mkazo wa Waumaya juu ya Uarabu, warithi wao walisisitiza Uislamu kuwa msingi wa utawala wao na ukuzaji wa Uislamu wa Urasimi tkawa ndio shughuli mojawapo kuu ya utawala wao wa kikhalifa.


Katika karne ya kwanza ya utawala wa Kiabbasi, eneo la Ukhulifa lilikuwa bado limepantika kwa ufahari kama ilivyokuwa katika utawala uliotangulia: majimbo ya Kaspian yalitekwa na, katika mwaka 827, unasabatawala tegemezi wa Waaghlabi ulianza kutamalaki Sisilia. Kwa upande mwingine, ufalme wa Waabbasi ulikuwa mdogo kuliko wa Waumaya tangu mwanzo, kwa sababu Hispania ya Waislamu ambayo ilikuwa zao la Waumaya kamwe haikuwa sehemu ya ufalme huo, kwani yenyewe ilikwishakuwa na ufalme huru ambao ulianzishwa mnamo mwaka 756 na ambao uliendelea kutawala kwa karne mbili na nusu. Katika miaka hamsini ya mwanzo ya utawala huo Waabbasi walipoteza majimbo yote ya Afrika, magharibi mwa Misri, yakachukuliwa ama na Wakhariji au Waidris; katika mwaka 800, gavana wa Ifrikiya, al-Aghlab, akajitenga kabisa na kuanzisha utawala wake mwenyewe<sup>7</sup>.

Sababu za kuchanguka pole pole kwa himaya kubwa katika zama za zamani zinajulikana. Sababu hizo zinahusiana na ugumu uliokuwepo, kutokana na hali ya mawasiliano yaliyokuwepo wakati huo, wa kudhibiti vizuri kutoka makao makuu, eneo kubwa la ufalme lenye nchi zenye watu wa aina mbalimbali; zinatokana pia na mielekeo ya magavana wa majimbo kutaka kujitenga na serikali kuu.

Hata hivyo, hadi kufikia nusu ya pili ya karne ya tisa mlolongo wa makhalifa shupavu uliweza kudhibiti na kutawala kwa ufanisi. Lakini baada ya uasi wa Kizanji<sup>8</sup> uchangukaji wa dola ambao tayari ulikwishaonyesha dalili ulipata msukumo kadri falme za kienyeji zilivyojitokeza huko Iran, Asia ya Kati, Bara Arabuni na Shamu. Katika karne ya kumi, hata kiini cha ufalme wa Waabbasi,

7 Taz. Sura 10 ya juzuu hili

8 Taz. Sura ya 1 na ya 26



2.2 The expansion of the Islamic state. (I. Hrbek)

Irak kilitwaliwa na unasabatawala wa Kishia wa Wabuwayhi, ambao waliwafanya makhalifa wa Kiabbasi vibaraka wao. Huko magharibi, Wafatimi walianzisha ukhalifa pinzani na wakaanza kutekeleza mipango yao mikuu ya kutamalaki nchi zote za Kiislamu Wafatimi hawakufanikiwa kikamilifu lakini waliweza kuzitenga Misri Shamu na Arabuni kutoka kwenye nchi ya Kiabbasi. Aidha, kwa vile katika mwaka 929 Muumaya wa Kihispania 'Abd al-Rahman III' alijivika lakabu ya 'Kiongozi wa Waumini' (*amir al-muminin*), basi kwa kipindi kadha kulikuwa na makhalifu watatu katika Uislamu. Enzi mpya ilianza katika miaka ya kati ya karne ya kumi na moja wakati Wasaljuki wa Kituruki, ambao walikuwa wafuasi wa Uislamu wa Kisunni, walipowakomboa Waabbasi kutoka katika nira ya Wabuwayhi.

Waturuki wa Asia ya Kati walikuwa wakitawala katika nchi za Waislamu za Mashariki ya Karibu tangu karne ya tisa; majeshi ya nchi za Waislamu yalikuwa na askari wa Kituruki; majenerali (*maamiri*) wa Kituruki wakawa ndio wenye kutawaza na kuangusha wafalme. La ajabu katika uvamizi wa Wasaljuki lilikuwa ile azma ya Waturuki wote kutaka kutamalaki sehemu kubwa ya Asia ya magharibi. Harakati hii ilikuwa mwanzo wa enzi ya uluwa wa Kituruki katika historia ya kisiasa na kijeshi ya sehemu kubwa ya nchi za Kiislamu. Waturuki wakaendelea kuenea Uislamu kila upande. Waghaznavi wa Afghanistan wakaanzisha mashambulizi ya kutamalaki Bara Hindi kisha nasabatawala nyingine nazo zikafuata nyayo zao. Hivyo, ukoo uliokuwa na nguvu kuliko zote kati yao, Wamughali wakuu, ambao ulianza kuwa na enzi katika karne ya kumi na sita, uliweza kudai kuwa sehemu kubwa ya bara Hindi ulikuwa chini ya *Dar al-Islam*.

Wasljuki wenyewe waliuongozea ulimwengu wa Kiislamu nchi nyingi katika mashariki na Asia Ndogo ambayo ilikuwa ngome kuu ya himaya ya Kiukristo ya Ubizenti. Kilele cha mashambulizi ya Waislamu wa Kituruki kilikuwa utamalaki wa Constantinople katika mwaka 1433 uliofanywa na Sultani wa Kiottomani Mehmed II Fatih.

Katika masuala ya makuzi ya fikra za kidini za Kiislamu, kipindi cha Waabbasi kinawakilisha kipindi cha ukuaji wa matawi mbalimbali ya sayansi za dini, hususani maamrishi (*fikhi*) na teolojia dhalianifu (*kalam*).

Nafasi ya mwingi katika uanzilishi na uendelezaji wa fikra za Waislam ni ile ya *Wamu'tazila*. Hao ni wanazuoni Waislamu wa mwanzo ambao, kutokana na athari za falsafa ya Kiyunani, walitaka kutumia urazini katika Uislamu. Katika fasihi ya Ulaya, *Wamu'tazila* wakati mwingine huitwa 'wanatafakuri huru' au 'mahuria' lakini lakabu hizo zinapotosha. *Wamu'tazila* hawakuwa madhehebu tofauti; na kwa hakika miongoni mwa wafuasi wake walikuwemo Masunni na Mashia, na nia yao ilikuwa kuonyesha kuwa itikadi za Kiislamu zilikubalika si katika misingi ya imani tu bali pia katika mantiki na urazini. *Wamu'tazila* walisisitiza upeke na Umoja wa Mwenyezi Mungu na hata kuzikataa sifa halisi za Mwenyezi Mungu na aina zote za sanamu. Wa'mutazila waliamini kuwa Kurani haikuwepo tangu mwanzo bali iliumbwa baadaye. Maudhui yao ya mwisho makubwa yalitokana na imani ya Kiislamu kuhusu Adili ya Mwenyezi Mungu. *Wamu'tazila* waliona vigumu kulioanisha imani ya kadari na wema wa Mwenyezi Mungu. Walikirihika kufikiri kuwa binadamu atapata adhabu ya vitendo ambavyo Mwenyezi Mungu amenwamrisha atende. Kwa muda fulani katika nusu ya kwanza ya karne ya tisa, imani ya Kimu'tazila ilipata hadhi ya kuwa dini ya kitaifa ya Waabbasi, wakati ambapo *Wamu'tazila* walilazimisha kwa nguvu fikra zao zikubalike. Lakini, baada ya kipindi kifupi cha utawala huo, wao wenyewe waliandamwa na kukomesha. Hata hivyo, pamoja na imani zao kuu kukataliwa, kwa namna fulani imani ya *Wamu'tazila* ndiyo iliyosababisha kuundwa kwa imani za 'wale walioshikamana na Sunna ya Mtume' (*ahl al-Sunna*) na wanazuoni maarufu kama al-Ash'ari (k. 935) na al-Bakillani (k. 1013).

Wanateolojia hao wa Kisunni waliishi na kufanya kazi katika wakati ambapo matumaini ya Uislamu wa Kisunni na ya Ukhalifa wa Kiabbasi yalikuwa madogo mno. Wafatimi wenye kupenda kufarakana walitawala juu ya nusu moja ya ulimwengu wa Kiislamu na walikuwa

tishio la kiitikadi na kisiasa juu ya nusu iliyobaki. Mashia walisitawi hata katika mamlaka ya Waabasi ambako Wabuwayhi walikuwa wamewafanya Makhalifa vibaraka wao. Nasabatwala ndogondogo za Kishia zilitawala katika sehemu za Arabuni na katika Shamu na kaskazini mwa Iran.

Majilio ya Wasaljuki yalisaidia sana kurejesha umoja wa nchi za Kiislamu. Majilio hayo yalifuatana na uhuishaji wa kidini wa urasimi wa Kisunni. Inafaa kuelewa kuwa uhuishaji huo wa urasimi na upinzani wake dhidi ya imani za kuhitilafiana vilianza sawia huko Mashariki (Wasaljuki) na Magharibi (Wamoravi). Katika sehemu zote mbili waumini wa urasimi walikuwa wanomadi kutoka pambazoni mwa ulimwengu wa Kiislamu waliokuwa wamesilimishwa punde tu. Hamasa ya kidini na nguvu za kijeshi za Waturuki na Waberiberi pia zilionekana katika uanzishaji upya wa mapambano na Waukristo huko mipakani katika Antolia na Hispania.

### Hitimisho

Hivyo, mwisho wa karne ya kumi na moja katika ulimwengu wa Kiislamu ulishuhudia mabadiliko mengi katika viwango mbalimbali. Katika siasa, uliashiria utamalaki rasmi wa Waturuki katika sehemu za mashariki na wa Waberiberi katika magharibi. Mashambulizi ya Wasaljuki dhidi ya Wabizenti katika Asia Ndogo yalichokoza utendano katika Ulaya Magharibi katika umbo la Harubu ya Kwanza. Ingawa Wafranki, ambalo ni jina walilopewa Waharubu wa vita vya msalaba katika nchi za Kiislamu, hawakuweza kukalia nchi nyingi, lakini uingaji wa Waukristo wa vita vya msalaba katika Ardhi Takatifu na kwenye pwani za Mediterania za Asia uliingiza kipengele kipya cha kisiasa katika mandhari ya Mashariki ya Karibu.

Katika Hispania ya Kiislamu, utamalaki wa Toledo katika mwaka 1085 na mashambulizi yaliyofuata ya Waukristo dhidi ya *muluk al-tawa'if* ya Waislamu kwa mara ya kwanza yalitishia usitawi wa Uislamu katika musoma wa Iberia. Hatari hiyo iliambazwa kwa kuingilia kati kwa Wamoravi wa Kiberiberi, lakini katika Mediteani ya kati, Waislamu walipoteza Sisilia moja kwa moja. Kadhalika, mabadiliko katika uchumi na biashara pia hayakuwa madogo. Kutokana na majilio ya Wasaljuki, asasi ya *ikta* - aina ya umiliki wa kikabaila wa kijeshi - ikawa sehemu muhimu ya maisha ya kiuchumi na ya muundo wa kijamii-kisiasa katika sehemu kubwa za ulimwengu wa Kiislamu. Ingawa desturi hii imepewa tafsiri mbalimbali, lakini ni dhahiri kuwa iliwakilisha mfumo wa uzalishaji ambao ulikuwa wa aina ya ukabaila wa Kiulaya.

Kipindi cha karne ya kumi na moja vilevile kilishuhudia uhamaji taratibu wa manzili ya biashara ya Bahari ya Hindi kutoka Ghuba ya Arabuni/Ajemi kwenda Bahari ya Shamu na kwa hivyo kuingia katika eneo la Wafatimi. Misri ilifaidika sana na badiiko hili kuliko wote na kwa muda mrefu ilikuwa ndiyo kituo kikuu cha biashara ya mpito kati ya Mediterania na Bahari ya Hindi.

Hatua mbili zilichangia vya kutosha katika ushindi wa Waislamu wa Sunni wakati huo: kwanza ilikuwa uanzilishaji wa *madrasa* au asasi za juu za kidini za kuwafundishia *ulama*. *Madrasa* yalianzishwa ili kushindana na asasi kama hizo katika Misri ya Kifatimi na kama njia bora zaidi ya kupambana na uenezaji wa propaganda ya Kiismailia. Ama kwa hakika, ilikuwa sahihi kuyaita 'ngome ya urasimi'. Hatua changizi ya pili ilikuwa utambuzi na uingizaji wa Usufi katika mkondo rasmi wa Uislamu na kutokea kwa udugu wa Kisufii. *Maulama* wakawa wanachama na kwa hivyo wakaweza kuwaelekeza viongozi na wafuasi kwenye urasimi kuwatenganisha na imani za kuhitilafiana. Usufi wa kirasimi, kama ulivyokuwa ukifuatwa na tarika zinazojulikana, pia ulisisitiza ukamilifu wa kimaadili; ulihubiri juhudi za binafsi (Jihad kuu) kuwa ni msingi imara wa maadili ya kijamii ya Kiislamu, na ulitilia takazo vitendo vya utoaji sadaka na vya kujihini.

# 3

## Maendeleo ya Uislamu na kuenea kwake Barani Afrika

### Utangulizi

Uislamu - pamoja na Ubudha na Ukristo - ni miongoni mwa kundi la dini za kimisheni, yaani zile ambazo utangazaji wa ukweli na uongofu wa wasioamini vilichukuliwa kama jukumu la muasisi na pia la jumuiya nzima.

Wakati wa maisha ya Muhammad, Uislamu ulikuwa dini ya Waarabu; ikawa kazi ya Makhaliifa wa mwanzo kuipeleka nje ya mipaka ya musoma wa Arabuni. Huko Waislamu walikumbana na hali tofauti: wakati ambapo Waarabu wengi walikuwa wapagani (kwa Kiarabu *Mushrikun*, yaani imani katika miungu wengi), kabla ya uongofu wao, nchi jirani zilikalifiwa na Waukristo, Wayahudi na wafuasi wa Mtume Zoroaster wa Uajemi, ambao, kulingana na maoni ya Kiislamu, walikuwa watu wa Kitabu (*ahl al-kitab*) yaani wale wenye kitabu (Maandiko Matakatifu), na kwa hivyo wazingatifu wa ufundo katika mfumo wa dini wa imani katika Mungu mmoja, hata kama si kamili. Haikuwa lazima kwa Waislamu kuwaongoa au kuwaulia mbali watu hawa, kwa sababu Uislamu huzuia uongofu wa kulazimisha. Wakati wa utamalaki mkuu wa Kiarabu kwa hakika hapakuwa na majaribio yoyote ya kuwaongoa watu wa Kitabu kwa nguvu.

Ingawa vizazi vya wanazuoni vimekwisha- onyesha wazi kwamba taswira ya mpiganaji wa Kiarabu Muislamu, mwenye jambia katika mkono mmoja na Kurani katika mkono mwingine, ni kisa cha kuzua, taswira hii imedumu katika maandishi maarufu juu ya Uislamu, na kwa jumla huaminika katika nchi zisizo za Kiislamu. Hata hivyo, utamalaki, hasa katika karne ya kwanza ya *hijra*, ulifanywa si kwa nia ya kuongoa tu bali hasa kwa kupanua maeneo chini ya Uislamu (dar al-Islam), kwa kuwa Waislamu walipendelea kuwajumuisha wasioamini katika dola la Kiislamu, kitu ambacho kwa mtazamo wao, kiliwakilisha utekelezaji halisi wa mpango makini wa kiroho kwa binadamu, kuliko uongofu wao wa mara moja.

Watu wa Kitabu (Ahl al-kitab) walipewa kiasi kikubwa cha uhuru katika mambo yote ya kidini kwa sharti la ulipaji wa *jizya*, yaani kodi ya kichwa. Waislamu walikuwa wamesamehewa kodi hii, na Waarabu wapiganaji Waislamu na familia zao walilipwa kiinua-mgongo kutoka hazina kuu ya dola (diwan), na pia walikuwa na nafasi ya upendeleo katika jamii. Manufaa ya wazi ya kuwa muumini wa imani za washindi yalidhihiri kwa washinde na wengi wao walijiunga na Uislamu.

Ni hadi mnamo karne ya pili na ya tatu baada ya *hijra* ndipo wengi miongoni mwa watu wa Mashariki ya Karibu walipoanza kuukiri Uislamu. Sababu zilizofanya waongoke zilikuwa za namna nyingi: baadhi walivutiwa na mafunzo sabili na ya wazi ya Uislamu ilhali wengine walitaka kukwepa ushuru na kodi, na wengine zaidi walitafuta kujifaninisha na tabaka tawala na kushiriki kikamilifu katika utamaduni wa Kiislamu uliokuwa ukiinukia.

Hata hivyo, ni kweli kwamba utamalaki wa Kiarabu ulisababisha - si papo hapo bali katika kipindi-kirefu-usilimishwaji wa wengi wa watu wa Mashariki ya karibu na Afrika ya Kaskazini. Utawala wa Waarabu Waislamu uliunda hali za kisiasa, kidini, kijamii na kitamaduni zilizopendelea uongofu katika dini ya kundi lililotamalaki kisiasa bila kuwepo haja ya kutumia nguvu.

### *Usilimishwaji wa Afrika Kaskazini*

#### **Misri**

Misri ilikuwa nchi ya kwanza ya Kiafrika kuvamiwa na Waarabu. Wakhufu hawakutoa upinzani wowote, lakini kinyume cha matarajio. waliwakaribisha Waarabu kama wakombozi wao kutoka katika nira ya Wabizenti. Walikuwa wameumia si tu kutokana na mzigo mkubwa wa kodi na namna nyingine za unyonyaji bali pia kutokana na mateso ya kidini waliyokabiliwa nayo kama waumini wa Mungu mmoja na kanisa rasmi la imani halisi ya Kibizenti.<sup>1</sup>

Mapambano haya kati ya makanisa mawili ya Kiukristo huko Misri kwa kiwango fulani yalisahilisha uongofu wa awali wa Wamisri katika Uislamu. Ushindani usiokwisha wa kidini uliokuwa wa kificho na kidhahania, ni wazi haukueleweka kwa Waukristo wengi na hivyo wengi miongoni mwao walikaribisha imani iliyowapa ukweli sahili na wa wazi kuhusu Mungu na Mtume wake. Hii inasaidia kueleza kuenea kwa haraka kwa Uislamu katika siku za awali za utamalaki wa Kiarabu. Ingawa katika vipindi vya baadaye, Wakhufu waliteswa mara kwa mara na watawala ambao hawakuweza kuwavumilia na hivyo wengi wao kulazimishwa kuacha imani yao, matukio ya namna hii hayakuwa ya kawaida. Kinyume cha mambo, ilikuwa ni chini ya utawala wa Wafatimi na Waayubi, wote wakiwa koo tawala ambazo zilichukuliwa kuwa tetezi za Uislamu, raia wasiokuwa Waislamu walipofurahia uhuru wa kuabudu ambao ulikuwa nadra katika vipindi vya awali na vile vya baadaye. Kwa kuwaleta pamoja Waislamu na Waukristo, kuvumiliana huku polepole kukaondoa matumizi ya kila siku ya lugha ya Kikhufu na badala yake ikatumiwa lugha ya Kiarabu. Wakhufu walipewa nafasi nyingi za kazi za dola za kukusanya kodi na kutekeleza majukumu ya kifedha na ya kitawala. Waukristo wengine wengi (Waarmenia) na Wayahudi nao walijiriwa kwa namna hiyo hiyo.

Usilimishwaji na uarabishwaji wa Misri pia vilielezwa na uingiaji polepole kwa wingi wa mabedui wa Kiarabu ambao walikaa kama wakulima na kuchanganyika na Wakhufu na hivyo kuongeza idadi ya wasema Kiarabu na Waislamu. Kipengee kingine kilichosababisha uongofu kilikuwa ni kuongezeka kwa ulaji rushwa na uharibifu wa tabia miongoni mwa viongozi wa dini ya Kikhufu kuanzia karne ya kumi na moja na kuendelea, mambo ambayo yalileta kupuuzwa kwa mahitaji ya watu ya kiroho na kiadilifu.

Hivyo, usilimishwaji wa Misri ulikuwa mchakato changamano, ambamo vipengee vingi - kama vile, unyoofu katika imani ya dini, manufaa ya kifedha na kijamii, mateso, uozo wa kanisa la Kikhufu, majilio ya Waarabu kutoka nje - vilichangia. Matokco ya yote haya yalimaanisha kwamba Misri katika kipindi cha Mamluki tayari ilikuwa nchi iliyokuwa na Waislamu wengi na Wakhufu na Wayahudi wachache.

#### **Maghrib**

Hali ya kidini katika Afrika Kaskazini ilikuwa changamano zaidi kuliko ile iliyokuwepo Misri. Watu

1 Taz. Sura 7 ya juzuu hili.



3.1 The Islamized areas of Africa by c. 1100. (I. Hrbek)

walioathiriwa na Warumi mijini na katika tambarare za mwambao walishikilia Ukristo ilhali Waberiberi wa bara walibakia mapagani, na baadhi ya wakazi wa milimani walikuwa wamepokea imani ya Kiyahudi.

Taarifa tuliyonayo ya kuenea kwa awali kwa Uislamu huko Maghribi ni ndogo. Zaidi ya hayo, mwanzo wa usilimishaji unatiliwa shaka na vyanzo vya baadaye vya Kiarabu katika ngano ya Ukba ambapo mpiganaji hodari alibadilishwa kuwa mhubiri wa amani. Hata hivyo, ni kweli kwamba kutokana na kuanzisha kwa Kayrawan mnamo mwaka 670, Ukba aliunda si tu kituo cha kijeshi bali pia kituo muhimu cha kuhubiria Uislamu na kupanua athari yake<sup>2</sup>.

Ingawa utawala wa Kiarabu huko Ifrikiya ulikuwa imara zaidi kuliko ilivyokuwa katika sehemu nyingine za Maghrib zilizobaki, lakini hata hapa usilimishaji ulifanyika pole pole sana. Katika maeneo mengi Waafrika waliofuata dini za Kirumi na Kiukristo waliendelea kuwa sehemu kubwa ya watu katika karne mbili za mwanzo baada ya utamalaki. Katika sehemu za ndani zaidi na katika baadhi ya miji kama vile Karthage na Tunis bado kulikuwa na makundi madogo madogo ya Waukristo katika karne za baadaye kama ilivyokuwa katika Mzab (katika karne ya kumi na moja), Kafa (katika karne ya kumi na mbili) na katika baadhi ya vijiji vya Nafzawa (katika karne ya kumi na nne). Katika mji wa Tozeur wakazi Waukristo waliendelea kuwepo hadi karne ya kumi na nane. Kuendelea kuwepo huko kwa muda mrefu kwa wenyeji Waukristo kunapingana na fikra kwamba watu waliilazimishwa kusilimu: ama kwa hakika maisha na hali ya kijamii kwa ujumla vilikuwa na umuhimu mkubwa katika kuwafanya watu polepole wageuze dini. Kama ilivyokuwa katika sehemu nyingine za ulimwengu wa Kiislamu kuenea kwa Uislamu kulikuwa na kasi kubwa zaidi mijini kuliko vijijini.

Ingawa haiwezekani kusema kwa yakini ni kwa nini na kwa namna gani makundi mbalimbali ya Waberiberi yaliama kusilimu, tunaweza kubainisha mielekeo kadhaa ya jumla inayoonyesha hatua mbalimbali zilizofuatana katika mchakato huu. Katika hatua ya kwanza makundi mengi ya Waberiberi baada ya kupigana vikali na majeshi ya Waarabu yalishindwa na kulazimika kubadili dini. Katika mazingira haya kubadili dini zaidi kulikuwa kwa kijuujuu tu na pengine kulihusu zaidi machifu na wakuu wa koo mbalimbali ambao walifanya hivyo katika kuutambua utawala wa watawala wao wavya. Mara majeshi ya Kiarabu yalipoondoka au yalipofukuzwa – na hii ilitokea mara nyingi sana katika karne ya saba – Waberiberi walirudia imani zao za jadi. Hali hii ilimfanya Ibn Khaldun aseme kwamba Waberiberi waliasi dini mara nyingi katika miaka sabini ya kwanza ya kukutana kwao na Uislamu.

Kisha Waarabu wakabadili sera zao; wakaanza kuchagua vijana wa kiume, wenye asili ya koo bora, kati ya wafungwa na kuwaachia huru kwa sharti kwamba wangeukumbatia Uislam, kisha wakawapa vyeo vikubwa jeshini. Sera hii ikaanza kuzaa matunda punde si punde; vijana shujaa wa Kiberiberi, kwa kushawishiwa na mfano wa machifu wao, wakajiunga na majeshi ya Waarabu. Aidha kufanikiwa kwa uvamizi wa Uhispania kukaleta makundi makubwa ya Waberiberi upande wa Waislamu, ambao walikuwa na hamu ya kushiriki katika kutamalaki na kufaidi mali iliyotekwa nyara.

Hivyo muda mfupi baada ya kuzivunja vurumai za upinzani mkubwa wa mwisho dhidi ya Waarabu na Uislamu, maelfu ya Waberiberi walijiunga na majeshi na kupokea imani ya maadui wao wa hapo mwanzoni. Hata hivyo uongofu huo uliathiri sehemu tu ya jamii, na ilichukua muda mrefu kabla ya Uislamu kupenya katika maeneo ya milima.





3.2 Mimbari iliyonakshiwa (katika msonobari uliochongwa) kutoka makifi wa Kairawan (Haitilimilki ya picha: Bernard Nautet, Paris)

Mnamo nusu ya kwanza ya karne ya nane, Uislamu ulipata maendeleo makubwa miongoni mwa wakazi wa mijini na vijijini, na hata miongoni mwa baadhi ya Wanomadi katika tambarare na pwani. Ni katika wakati huu hasa ambapo mwelekeo bainifu wa kifikira wa Waberiberi kuhusu Waarabu na Uislamu ulipoanza kudhihirika: Waberiberi walikuwa tayari kupokea Uislamu kama dini au hata utamaduni wa Kiarabu - na walifanya hivyo kwa kiwango kikubwa - lakini wakati huo huo walikataa kutawaliwa na umangimeza wa kigeni, unaowakilisha utawala wa mbali uliowabagua waongofo wapya.

Hivyo uwanja ukawa umeandaliwa kwa awamu nyingine; Waberiberi walibadilisha mapambano yao dhidi ya utawala wa kigeni na kuyaingiza katika kiwango cha kitikadi katika muktadha wa Kiislamu. Katika kupinga unyanyasaji wa Waarahu halisi, walianza kushikilia imani za Kikhariji. Mafundisho ya kidini na ya kisiasa ya Kikhariji yalikuwa ya kidemokrasia, manyofu na ya msingi, na katika hali zote hizi, yalikuwa yakipingana na yale ya kirasmi na kiimla ya Makhalfi<sup>11</sup>. Mafundisho haya yaliingia kwenye udongo wa rutuba miongoni mwa Waberiberi, ambao wengi wao waliyapokea kama itikadi ya mapambano yao dhidi ya utawala wa Waarabu. Msimamo wa usawa wa waumini wote ulilingana na muundo wa jamii yao na mawazo yao. Kingine kilichowavutia kwa kiwango hicho ni mafundisho kwamba, kwa kuwa Waislamu wote ni sawa, maisha ya anasa na ufahari kwa baadhi tu ni dhambi na kwamba waumini wa kweli wanapaswa kuishi maisha ya kiasi. Hii hali ya usafi au unyoofu lazima ilikuwa na athari kubwa kwa Waberiberi wakulima na nusu Wanomadi waliozozwa na anasa na upungufu wa uadilifu katika matabaka tawala ya Kiarabu.

Imani za Kikhariji zilienea sana miongoni mwa Waberiberi wa eneo la mapululu lililoenea toka Tripolitania kwa upande wa mashariki kupitia Ifrikiya kusini hadi kusini mwa Moroko kwa upande wa magharibi, na ziliwaathiri mno Waberiberi wa mbari kuu ya Zanata.

Ni dhahiri kwamba kupokelewa kwa imani za Kikhariji na Waberiberi wengi kuna mizizi yake katika upinzani wao wa kijamii na kitaifa dhidi ya matabaka tawala ya Kiarabu. Ukhariji wa Kiberiberi haukukinzana kwa namna yoyote na harakati za Kiislamu bali ulikuwa namna Waberiberi walivyoonyesha kupokea kwao Uislamu kama dini.

Vivyo hivyo, upinzani wa Waberiberi haukuwa dhidi ya Waarabu Waislamu, ila dhidi ya tabaka tawala. Walipinga kwa nguvu utawala wa kulazimishwa wa kigeni na watawala wageni, lakini walikuwa tayari kuwapokea Waislamu wasio Waberiberi kama machifu wao kwa uchaguzi wao wenyewe. Hii ilitokea kuhusiana na Mwajemi Ibin Rustum huko Tahet, Mualidi Idris huko Moroko na Mfatimi Ubaydullah miongoni mwa Waberiberi wa Kutama. Katika matukio haya yote, watu hawa walikubaliwa si tu kama viongozi wa upinzani dhidi ya serikali, bali pia kwa mivuto yao mahsusni ya Kiislamu.

Kulikuwapo pia na majaribio ya kuanzisha dini ya Waberiberi peke yao kama dini sawa na Uislamu. Mojawapo maarufu na iliyodumu kwa muda mrefu ikiwa dini ya Wabarghawata; sehemu ya Wamasmuda walioishi katika tambarare ya Atlantiki ya Moroko kati ya Sale na Safi<sup>3</sup>.

Katika sehemu nyingine za Moroko, miongoni mwa Waawraba, Wamiknasa, Waghomara na wengineo, Uislamu ulikuwa umekwishapata maendeleo fulani mnamo karne ya nane, lakini ushindi halisi na kukubalika kwake kiundani yaelekea vilifanyika wakati wa nasaba tawala ya Waidrisi. Mwasisi wake, Idris I, baada ya kutangazwa Khalifa (mnamo mwaka 788), alianza kazi ya

<sup>3</sup> Taz. Sura 2 na ya 10 ya juzuu hili.

kuwaingiza Waberiberi ambao walikuwa hawajaongoka katika Uislamu. Sera hii iliendelezwa na mwanaye Idris II, na kufanya, katika karne iliyofuata, kaskazini yote ya Moroko, isilimishwe kwa kiasi kikubwa, isipokuwa "Wazushi" wa Barghawata.

Kusilimishwa kwa Maghribi nzima, kwa jumla, kulikuwa kumekamilika kufikia karne ya kumi; na ni katika maeneo na miji fulani tu ambako kulikuwa kumebakia jumuiya ndogondogo za Kiukristo na Kiyahudi, ilhali makundi machache ya Kiberiberi katika maeneo ya mbali ya milimani yaliendelea kushikilia imani zao za kale na "wazushi" wa Barghawata nao walikuwa hawajashindwa. Hata hivyo katika wakati huu hali za kisiasa na kijamii zilipata mabadiliko mengi, zikaathiri hali yote ya dini.

Kwa kuziondolea mbali dola za Kikharji za Tahert na Sijilmasa na kukandamiza maasi kadhaa ya Kikharji, Wafatimi walibomoa kabisa Ukhariji wa Kiberiberi. Hata hivyo, walishindwa kuuvutia umma wa Kiberiberi kwenye aina yao ya Uislamu wa Kishia; badala yake umma huu ulijiunga na madhehebu ya Kiislamu ya Sunni na hasa *madhhab* (chuo cha dini na sharia) ya Kimaliki. Wakharji waliobakia ama walihamia maeneo ya mbali kama Mzab na Djabal Nafusa, au polepole walijiunga na Umaliki. Ukhariji ukakoma kuwa namna mahsusi ya Uislamu wa Waberiberi kwa sababu ni katika wakati huo ambapo ulipoteza sababu ya kuwepo kwake kama alama ya upinzani wa Waberiberi dhidi ya utawala wa kigeni. Hapakuwa na utawala wa kigeni katika Maghrib baada ya Wafatimi kuhamishia kituo cha himaya yao Misri na kuacha Maghrib chini ya utawala wa Waberiberi wa Ziridi. Baadaye kidogo, sehemu ya magharibi ya Maghrib nayo ikaingia chini ya Waberiberi wa Wamoravi ambao walifutulia mbali mabaki ya mwisho ya Ukhariji, Ushia na uzushi wa Wabarghawata katika eneo hili na kuanzisha utawala wa kudumu wa tapo la Umaliki la Uislamu wa Kisunni.

### *Kuenea kwa Uislamu Kusini Mwa Sahara*

Kwa kuwa usilimishaji wa sehemu ya kaskazini ya Afrika ulitokana na utamalaki wa Waarabu, mara nyingi imefikiriwa kwamba kuenea kwa dini hii katika Afrika ya Tropiki nako kulifuata ruwaza hii hii; yaani kushindwa kwanza kwa wenyeji na Waarabu (au Waberiberi) na kisha kulazimishwa kuupokea Uislamu. Hata hivyo, utamalaki wa nje wa wavamizi wa Kiislamu ulikuwa na dhima ndogo sana isipokuwa Mashariki mwa Sudan ambapo tukahaji wa Waarabu wengi katika eneo hilo ulikuwa na umuhimu katika kusambaza Uislamu. Lakini hata hapa, uongofu wa wenyeji ulifanyika baadaye sana. Kutamalakiwa kwa jamii za Kiafrika na dola zilizosilimishwa kulikuwa na umuhimu katika eneo la Chad na kusini mwa Ethiopia, lakini katika sehemu mbalimbali za Afrika kusini mwa Sahara ruwaza ya kawaida ya ueneaji wa Uislamu ilikuwa tofauti kabisa, kama itakavyoonyesha hapa chini.

### Sahara

Waberiberi wa Magharibi mwa Sahara huenda walikutana na Uislamu ama kwa kupitia kwa wapiganaji wa Kiarabu waliokuwa wamejipenyeza katika nchi yao kutoka al-Sus al-Aksa au kwa kupitia wafanyabiashara wa Kiislamu ambao misafara yao ilikuwa imejitokeza katika njia za biashara za magharibi mwa Sahara kabla tu ya utamalaki wa Waarabu katika Maghrib. Hapana shaka makutano haya yalileta kuongoka kwa baadhi ya Waberiberi waliokuwa viongozi na wasi-ndikizaji wa misafara. Katika vituo vichache vya kibishara na kisiasa kwenye njia za misafara, kulikokuwa na makazi ya kudumu ya wafanyabiashara Waislamu, athari ya utamaduni wa Kiislamu juu ya wenyeji lazima ilikuwa kubwa na iliyopenya ndani zaidi.

Waberiberi wa kwanza wa Sahara ambao uongofu wao unathibitishwa ni Walamtuna, ambao yasemekana waliupokea Uislamu katika mwongo wa pili wa karne ya nane, wakifuatiwa baadaye kidogo na Wamassufa na Wajuddala. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba Uislamu wao ulikuwa mchirizi mdogo tu kwa karne nyingi zilizofuata; historia nzima ya mwanzo wa harakati za Wamoravi hutoa ushahidi dhahiri wa usilimishaji wa juujuu tu wa makundi haya matatu ya Waberiberi<sup>5</sup>.

### Sudani magharibi na kati

Uislamu ulikuwa umekwishavushwa jangwani hadi magharibi mwa Sudan hta kabla ya Maghrib na Sahara zenyewe kuongolewa kikamilifu. Waberiberi wa mji wa Tadmekka walisilimishwa miaka saba baada ya watu wa Ghana, wakiwa wamelazimishwa kufanya hivyo na waongofu wapya wa Ghana. Katika hali hii 'uongofu' yawezekana ulikuwa na maana ya kulazimishwa kupokea Uislamu wa kdesturi wa Wamoravi ambao tayari walikuwa wakitangaza imani ya Kikhariji. Tadmekka ilikuwa imetembelewa na wafanyabiashara wa Kiibadi kutoka Afrika Kaskazini tangu karne ya tisa na ilikuwa kituo cha shughuli zao za kimisheni miongoni mwa watu wa Sudan.

Ni dhahiri kabisa sasa hivi kwamba wafanyabiashara wa Kiibadi walipenya Sudan mapema zaidi kuliko Wasunni warasmi na yaelekea kwamba baadhi ya waumini wa kwanza miongoni mwa Wasudan walisilimishwa kutokana hasa na juludi za uenezaji dini za Waibadi. Tokea karne ya nane wafanyabiashara wa Kiibadi walitoka Tahert, Wargla, kusini mwa Tunisia na Jabal Nafusa, walikuwa wamekaha miji mbalimbali ya Sudan kama vile Ghana, Gao, Awdaghust, Tadmekka, Ghayaru, Zafunu na Kugha. Ingawa taarifa za shughuli za kimisheni za wafanyabiashara hawa si nyingi sana, yaweza kufikiriwa kwamba kuwepo kwao kwa muda mrefu katika vituo vingi muhimu vya Sudan kuliwaathiri kidini wenyeji. Kwa hali yoyote ile, waongofu wao wa kwanza wangukuwa Wasudani wenzi wao katika biashara. Kwa upande mwingine, hakuna alama zozote za imani ya Kiibadi zilizobakia katika tikanda wa Sudan. Yaelekea athari thabiti za Kiibadi huweza tu kuonekana katika usanifu-majengo wa kidini: aina za minara ya misikiti iliyopo katika sehemu nyingi za Sudan ni za asili ya kusini mwa Tunisia, ambapo *minbar* za mstatili zinafanana na zile za Mzab, ambacho kilikuwa kituo kikuu cha Kiibadi tangu karne ya kumi na kuendelea.

Athari ya awali ya Kiibadi kusini mwa Sahara na magharibi mwa Sudan ilifutiliwa mbali kutokana na athari ya Wamoravi waliohubiri imani ya mwanzo ya Uislamu na kuhakikisha kwamba Waislamu wa Kisudan wanazingatia Umiliki baada ya hapo.

Ni vigumu kutathmini uzito wa wimbi hili la mwanzo la usilimishaji lilivyokuwa. Kwa kutazama hali ya Uislamu ya siku za karibuni, yawezekana kufikiri kwa jumla kwamba Uislamu huu wa awali ulikuwa na vipengee vingi vya imani mbalimbali za kabla ya Uislamu zilizojulikana Maghribtangu mwisho wa kipindi cha Warumi (Warumi, Ukristo) na pia mabaki ya dini za Kiberiberi na za Kiafrika.

Hata hivyo, Waibadi walikuwa na sifa dhahiri ya kuwa wa kwanza kuingiza Uislamu katika Sudan, na kuweka misingi ambayo juu yake watangazaji wa baadaye wa Uislamu waliweza kujenga muundo wenye kustahimili zaidi.

Uhusiano wa Uislamu na biashara katika Afrika kusini mwa Sahara, ni ukweli unaojulikana sana. Wafanyabiashara hodari, Wadyula, Wahausa na Wadyakhanke walikuwa miongoni mwa makundi ya mwanzo kuongoka wakati Waislamu walipofika nchini kwao. Tukio hili lilitokana na sababu za kijamii na kiuchumi. Uislamu kama dini iliyoibuka katika jamii ya kibiashara ya Maka na

5 Taz. Sura 13 ya juujuu hili.

kutangazwa na Mtume ambaye yeye mwenyewe kwa muda mrefu alikuwa mfanyabiashara, hutoa maagizo ya adili na ya matendo yenye uhusiano wa karibu na shughuli za biashara. Maadili haya yalisaidia katika kukanya na kudhibiti mahusiano ya kibiashara na kutoa itikadi unganifu miongoni mwa watu wa makundi tofauti, na hivyo kuleta usalama na sifa, masharti mawili makuu ya biashara ya mbali.

Waislamu wa siku hizo za awali walipendelea kuunda jumuiya ndogondogo zilizotapakaa kwenye njia kuu za biashara katika Sahel na Sudan yote. Katika baadhi ya miji mikuu kama Ghana au Gao, wafanyabiashara na Waislamu - makundi mawili ambayo mara nyingi yalikuwa hayatenganishiki - waliishi katika makazi yao peke yao na mara nyingine walikuwa na kiwango fulani cha uhuru wa kisiasa na kisharia. Makazi haya katika njia za biashara na katika vituo vikuu, yaliunda sehemu zilizotumiwa kutangazia Uislamu.

Kufuatia wafanyabiashara, kukua kwa jumuiya za Kiislamu kuliwaleta wahubiri wa Kiislamu ambao kwao shughuli za kidini kwa jumla zilikuwa muhimu kuliko zile za kibiashara. Mwanzoni hawa walifanya shughuli mbalimbali za kidini katika jumuiya za Kiislamu zilizokwishaanzishwa; shughuli ambazo baadaye zilijumuisha uponyaji na uaguzi, maengenezo na uuzaji wa hirizi. Shughuli hizi nyingine zilifanya Uislamu kuwa na mvuto zaidi machoni mwa wasio Waislamu katika nchi za Sudani. Ufasiri wa ndoto, kuponya kwa imani, ubashiri wa mambo ya jayo, na imani katika nguvu za sala hasa kuombea mvua, yote yalikuwa ya umuhimu mkubwa.

Kundi la pili la kijamii - baada ya wafanyabiashara - kuongoka katika Uislamu lilikuwa la watawala na wajumbe wa mabaraza. Inasadikiwa kwa jumla kwamba mtawala wa kwanza magharibi mwa Sudan kuongoka katika Uislamu alikuwa War Dyabi wa Takrur katika Senegal ya chini ambaye alipokea Uislamu hata kabla ya kuinukia kwa Wamoravi katika miaka ya 1030. Aliamua kueneza dini hii mpya katika nchi jirani ya Silla; na mnamo mwaka 1056, mwanaye Labi aliungana na Yahya ibn Umar katika vita dhidi ya waasi wa Juddala. Katika karne za baadaye huko Afrika Kaskazini na Misri, jina la Takrur lilichukuliwa kuwa sawa na nchi zote za Kiislamu za Sudani Magharibi na Kati. Haija-thibitishwa bado kama matumizi ya jina hili yametokana na ukweli kwamba Takrur ilikuwa nchi ya kwanza ya Kiislamu Afrika Magharibi, au kwa vile kufikia karne ya kumi na nne, watu wa Takrur walikuwa wameanza kutoa wahubiri wao wenyewe wa dini (Waterodbe), ambao walichukua dhima muhimu katika usilimishaji wa Sudan Magharibi yote.

Uongofu mwingine wa awali zaidi wa mtawala wa wenyeji, nao wa kabla ya Wamoravi, ulitokea Gao (Kawkaw). Huko, kati ya mwaka 1009 na 1010, mtawala Dya (Za) wa kumi na tano, aliyelitwa Kurani kama alama rasmi, vitu ambavyo yasemekana vilitoka kwa Khalifa.

Uongofu wa Mfalme wa Mallal, mojawapo ya tawala za kichifu za Malinke, nao ni wa kipindi hicho hicho. Mfalme alishawishiwa kukubali Uislamu na mkazi Muislamu ambaye sala zake zilileta mvua zilizokuwa zimengojewa kwa muda mrefu nchini. Ingawa mfalme na nyumba yake na wajumbe wa baraza walikuwa Waislamu waadilifu watu wengine wote waliendelea kuzingatia dini yao ya jadi.

Uanzishaji wa Uislamu kwa mara ya kwanza Sudan ya kati ulifanyika katika karne ya kumi na moja kwa uongofu wa *Maïs* wa Kanem, Hummay Jilmi (1080-1097)<sup>6</sup>. Wakati huo chini ya baadhi ya watawala waliomtangulia Hummay tayari kulikwishakuwa na wahubiri wa Kiislamu katika baraza ambao waliwafundisha watawala amri za Kiislamu na kusoma nao aya fulani za Kurani; hata hivyo, hapana *Maïs* yeyote aliyetangaza Uislamu hadharani. Lakini mwana na mrithi wa Hummay, Dunama (1097-1150) alikwenda hija mara mbili Maka na akafa maji katika safari yake ya pili.

6 Taz. Sura 15 ya juzuu hili.

Karne ya kumi na moja yaelekea kuwakilisha kipindi ambapo Uislamu ulifaulu kwa mara ya kwanza katika Sudan Magharibi na Kati: kutoka Senegal ya chini hadi kwenye fuko za Ziwa Chad, Uislamu ulipokelewa na watawala na machifu mbalimbali na hivyo kutambuliwa rasmi katika kiunzi cha jamii za Kiafrika. Katika karne hiyo Ghana pia, dola ya Kisudan iliyokuwa maarufu na yenye nguvu kuliko zote wakati huo, iliongolewa.

Ilikuwa ikifikiriwa kwamba uongofu huu ulikuwa matokeo ya utamalaki wa Wamoravi katika Ghana mnamo 1076. Hata hivyo, utafiti wa karibuni umetilia shaka maoni haya na inazidi kukubalika kwamba utamalaki huo haukutokea na kwamba mamlaka haya mawili kwa hakika yalikuwa na mahusiano ya kirafiki wakati wote. Yaelekea zaidi kwamba Wasoninke wa Ghana walielewana vizuri na Wamoravi wa jangwani hata kuwa marafiki badala ya maadui na kwamba walisha-wishiwa kwa amani kukubali Uislamu wa Kisunni kama dini rasmi ya dola ya Ghana. Kwa muda mrefu watawala wa Ghana waliathiriwa na Uislamu; yaelekea pia kwamba Uislamu uliingia kwanza Ghana katika imani za Kikhariji. Kwa hiyo kuongolewa kwa watu wa Ghana na Wamoravi mnamo 1076, pengine kuna maana kwamba kulikuwa na ulazimishaji wa Uislamu wa Kimaliki juu ya jumuiya iliyokuwa ya Kiibadi kama ilivyotokea awali huko Awdaghust. Mafanikio muhimu ya maingilio ya Wamoravi bila shaka yalikuwa ni kusilimishwa kwa mfalme na baraza lake.


Wazo kwamba utamalaki na usilimishaji wa lazima katika Ghana vilizusha kuhama kwa Wasoninke walioupinga Uislamu na wakaona ni kheri kuiacha nchi ya mababu zao kuliko kuacha imani za dini yao ya jadi linakataliwa pia. Kwa kuwa hapakutokea utamalaki au usilimishaji wa lazima wa namna hiyo, uhamaji uliofanyika hauwezi kuhusishwa na mambo haya.

Kwa vyovyote vile, itakuwa makosa kushindwa kuona athari kubwa ya Wamoravi na mabadiliko ambayo uingilaji wao ulileta Sudan. Hata hivyo mabadiliko haya yalikuwa ya namna tofauti kuliko yale yanayofikiwa na wale washikiliao nadharia ya uhamiaji. Wafanyabiashara Wasoninke waliosilimishwa polepole walianzisha taratibu za kibiashara katika Sahel na kusini, kuelekea pambazoni mwa msitu wa tropiki. Kinyume na inavyofikiwa badala ya kuehukia Uislamu wao ndio waliosaidia kwa kiasi kikubwa kuenea kwa dini hii katika sehemu za watu wasio Waislamu huko Sudan; sehemu ambazo zilikuwa hazijapenywa na Waarabu wala Waberiberi.

Yaonekana katika karne ya kumi na moja, misukumo ya maendeleo ya awali katika dola nyingi za Sudan ilifikia hatua ambapo mapokezi ya Uislamu yalikuwa na faida kadhaa kwa matabaka tawala na kwa kundi lililokuwa likipanuka la wafanyabiashara wenyeji.

Katika himaya ya Mali usilimishaji wa yiongozi wake ulitokea mwishoni mwa karne ya kumi na tatu chini ya wazawa wa Sundiata. Ingawa Ibn Battuta na Ibn Khaldun wanashikilia kwamba huyu shujaa muasisi naye aliongolewa katika Uislamu, mapokeo simulizi ya Wamalinke husisitiza sana sifa zake kama mchawi mpagani na hukana uongofu wowote. Hata hivyo, mwana na mrithi wa Sundiata, Mansa Uli, alikuwa amekwisha kwenda hija wakati wa utawala wa Mamluk Sultan Baybars (1260-77). Tokea siku zake na kuendelea, hija za Kifalme zikawa ni desturi ya kuduunu miongoni mwa *Mamansa*. Mtazamo wa Kiislamu wa himaya ulidhihirika katika karne ya kumi na nne chini ya Mansa Musa (t. 1312-37) na ndugu yake Mansa Sulayman (t.1341-1360), ambao walihimiza ujenzi wa misikiti na maendeleo ya mafunzo ya Kiislamu.

Hali ya jumla ya usalama wakati wa upeo wa ustawi wa himaya ya Mali ilichochea upanuzi wa biashara magharibi mwa Sudan. Wafanyabiashara Waislamu waliendesha shughuli zao katika himaya yote na wakadiriki hata kuvuka mipaka yake. Wamalinke wengi zaidi waliongolewa na pia watu wa mbari nyingine kama vile Wafulbe katika bonde la Senegal na Masina. Tukio moja muhimu la maendeleo lilikuwa juhudi na ukuaji wa wahubiri wenyeji uliojitokeza katika miji mikubwa ya kisiasa na kibiashara, kama Nyani na Gao, lakini zaidi katika Jenne na Timbuktu. Kuna ushahidi wa



3.3 Maeneo ya Waislamu katika Afrika ilipofika k. 1500 (I. Hrbek)

kutosha kuonyesha kwamba, hadi karne ya kumi na sita, wengi wa wanazuoni wa Kiislamu katika Timbuktu walikuwa Wasudan, wengi wao wakiwa wamejifunza Fez na kufaulu vizuri mno sayansi ya Kiislamu na utawa katika kiwango cha kuwavutia watu kutoka ugenini. Kuanzishwa kwa kundi la wanazuoni na wahubiri wa Kiislamu walioelimika wenye asili ya Kisudan, lilikuwa tukio muhimu katika historia ya Uislamu katika eneo la Afrika kusini mwa Sahara. Baada ya hapo Uislamu ulitangazwa na kuenezwa na wenyeji wenye ujuzi wa mila, imani na lugha za mahali hapo. Ujuzi huu ulisaidia kazi zao za kimisheni na uliwahakikishia ushindi mkubwa kuliko ule walioupata wenzi wao wa kidini wa Afrika Kaskazini hapo awali. Machoni mwa Waafrika, Uislamu ulikoma kuwa dini ya wataalamu weupe, na kwa kuwa ujumbe ulibebwa na Waafrika wenyewe, Uislamu ukawa dini ya Kiafrika.

Athari ya kundi hili jipya la wahubiri wa Kiafrika ilifika hadi Sudan ya Kati. Hadi karne ya kumi na nne enco kati ya Ziwa Chad na sehemu za kati ya Niger lilikuwa halijafikiwa na Uislamu, na hasa nchi ya Wahausa ilikuwa haijaguswa na shughuli za kimisheni.

*Tarihi za Kano* huandika juu ya kufika, mnamo karne ya kumi na nne na ya kumi na tano, kwa makundi mawili ya wanazuoni wa Kiislamu kutoka magharibi mwa Sudan ambao walichangia katika ueeneaji wa Uislamu na kufikia kwake kiwango cha juu cha imani. Mbali na Kano, Uislamu pia ulianzishwa, mnamo nusu ya pili ya karne ya kumi na tano, huko Zaria na Katsina, ambako watawala na wajumbe wa baraza walisilimu. Kulikuwapo pia maelezo ya kufika kwa *Masharifu* (Wazawa wa Mtume) Kano wakati huo; na kuwepo kwao kuliimarisha imani na kufutilia mbali mabaki ya upagani.

Hata baada ya majaribio hayo kuimarisha nguvu zake, Uislamu haukuwa umekubalika kwa jumla. Ilikuwa dini ya jamii ndogondogo za wafanyabiashara na wahubiri. Mabaraza yalikuwa yameathiriwa juujuu tu, ambapo umma wa watu ulishikilia imani zao za jadi. Sababu moja nyingine ya kuenea zaidi kwa Uislamu katika sehemu za Sudani ilikuwa ni kupokelewa kwake na wafanyabiashara wa Kihausa ambao walikuwa mojawapo ya makundi ya wafanyabiashara Waislamu waliokuwa hodari sana. Kutokana na kufunguliwa kwa njia za kibiashara hadi kwenye nchi zilimozalishwa kola, ndani ya Gold Coast, wakaweza kuencia Uislamu hadi pambizoni mwa misitu.

Bila shaka, kulikuwepo pia kadha vikwazo katika maendeleo ya Uislamu. Warnossi katika kuruba ya Niger walipinga kuenea kwa Uislamu kwa muda mrefu, ingawa ni kweli kwamba walikuwa wamekwishakutana nao katika karne ya kumi na nne, waliposhambulia na kuharibu Timbuktu na Walata pia. Katika miaka ya mwisho ya karne iliyofuata *Askiya* Muhammad alianzisha *jihadi* dhidi yao kwa kukataa wito wake wa kuwataka waukubali Uislamu. Lakini hata kushindwa kwa jeshi lake hakukumfanya mtawala wa Warnossi kuacha dini yake ya jadi, na watu wake wengi walifuata mfano wake. Falme za Warnossi zilianza tu kupenywa na wafanyabiashara wa Kiislamu baada ya karne ya kumi na saba.

Kisiwa kingine cha dini ya jadi kiliundwa na Wabambara katika nchi ya himaya ya kale ya Mali. Kwa hakika, utamaduni wa Kiislamu wa Mali nao ulirudi nyuma kutokana na kudidimia kwa himaya. Baada ya kupoteza miliki zao za nje na wakiwa wametengwa kwenye biashara ya Sahara, Wamalinke waliishi katika *kafu* (tawala ndogo-ndogo za machifu), bila utawala mkuu wa kuwaunganisha wala makazi ya miji. Uislamu baada ya kuachwa na tabakatawala, uliwakilishwa ama na kundi la wafanyabiashara (Juula) au na wahubiri tu.

Hata hivyo, kwa jumla, kufikia karne ya kumi na sita Uislamu ulikuwa umeanzishwa katika ukanda wote wa Sudan kutoka Atlantiki hadi kuvuka Ziwa Chad. Matabakatawala ya dola zote kuu, na nyingi katika zile ndogo, yalikuwa ya Kiislamu, walau kwa jina. Kauka miji yote na katika vijiji



vingi kuliishi jumuiya za Waafrika Waislamu wa asili ya mbari mbali mbali, ambao mara nyingine walikuwa Waislamu kwa majina tu, lakini mara nyingi wakiwa watawa na wanazuoni wenye mtazamo mpana na mawasiliano na dunia pana kaskazini mwa Sahara. Ingawa wengi wa wenyeji wa vijijini waliathiriwa kidogo tu na dini hii ya ulimwengu, baada ya kuwepo kwake kwa miaka mingi, Uislamu ulikuwa kitu cha kawaida na sehemu ya maumbile ya kitamaduni ya Afrika Magharibi.

### Nubia na Sudan ya Kiniloti

Usilimishaji wa eneo hili umekuwa - na kwa hakika bado ungali - unaendelea. Ingawa Nubia imekuwa na mawasiliano na Uislamu tangu wakati wa utamalaki wa Waarabu huko Misri mnamo mapema katika karne ya saba, kuenea kwake kulizuliwa kutokana na kuwepo kwa dola za Kiukristo za Nubia na kuendelea kwa Wanubia kushikilia imani yao ya Kiukristo.

Baada ya majaribio kadhaa yaliyoshindwa kuteka Nubia, Waarabu wakaamua kufanya makubaliano na watawala wa Wanubia. *Bakt* hii, kama ilivyojulikana, ilihakikisha kuwepo kwa uhuru wa dola ya Kinubia wa Kinubia kwa karne nyingi zilizofuata<sup>7</sup>. Ingawa kulikuwa na majaribio ya mara moja moja kuwaongoa watawala (kwa mfano, mwanzoni mwa utawala wa Wafatimi katika Misri), sera ya jumla ya serikali za Kiislamu za Misri ilikuwa ya kutosumbua Ufalme wa Kiukristo.

Mahusiano ya kirafiki baina ya watawala wa Misri na wafalme wa Kinubia yaliruhusu wafanyabiashara wa Kiislamu kupenya dola hiyo. Ingawa wafanyabiashara hawa hawaonekani kujishughulisha na uenezaji wa dini ya Kiislamu, hata hivyo, waliingiza vipengee fulani vya imani mpya katika maenco ambayo hadi wakati huo yalikuwa ya Kiukristo tu.

Usilimishwaji (na "uarabishwaji") wa Nubia ulitokana na mambo tofauti kabisa. Mapema mnamo karne ya nane, baadhi ya makundi ya Waarabu, Wanomadi yalianza kwenda Misri ya juu, kuelekea Nubia, wakichagua hasa eneo kati ya Bonde la Nili na Upwa wa Bahari ya Shamu. Katika karne ya kumi walikuwa wamekwishakalia kaskazini zaidi ya Nubia ha wakati huohuo Wanubia wa kaskazini mwa Maporomoko ya Pili walikuwa wamesilimishwa. Makundi mengine ya Waarabu wahamaji yaliamia katika nchi ya Wabeja ambako baadhi yao walioana na familia zilizotawala Beja. Kuoana kwa namna hiyo kulifanyika pia Nubia na kuanzisha koo za Kiislamu zenye nguvu. Makundi ya Wabeja wa kaskazini zaidi, Wahadariba na Waababda, polepole "Wakaarabishwa" na hata kujipachika koo bandia za Kiarabu, lakini imani zao za kale ziligeuzwa kidogo tu na Uislamu. Kufikia karne ya kumi na nne, Wabeja wengi walikuwa wamekwisha kusilimishwa rasmi, kwani walijiona kuwa ni Waislamu na walitambuliwa hivyo na wenzi wao kidini, ingawa waliendelea kujishughulisha na imani na matendo yao ya jadi.

Hadi mwishoni mwa karne ya kumi na mbili, na hasa kutokana na kuendelea kubakia huru kwa Ufalme wa al-Makurra, kumininika kwa wahamiaji wa Kiarabu kulikuwa kwa kujipenyeza kama makundi madogo madogo ya mabedui. Kuingilia kati kwa Mamluki kwenye migogoro ya ndani ya ukoo wa kifalme, kuliwafanya wafalme wa Nubia kuwa watumwa au vikaragosi. Mnamo mwaka 1315, Mamluki walimchagua mwana wa mfalme wa Kinubia aliyekwishasilimishwa kuwa mfalmena tukio hili liliashiria mwanzo wa kudidimia kwa Ukristo katika Nubia.

Kuvunjika kwa ufalme wa Nubia kaskazini kulikotokana na kujipenyeza, hapo awali, kwa mbari za Kiarabu, kuliwawezesha Waarabu kuvuka jangwa la Nubia na kuingia katika malisho mazuri. Ingawa hawa mabedui wa Kiarabu walikuwa Waislamu kwa kiwango kidogo tu, hakuna sababu ya Kufikiri kwamba Uislamu wao ulikuwa wajuujuu kuliko ule wa Wanomadi wengine. Hawa

7 Taz. Sura ya 8.

hawawezi kuchukuliwa kuwa waenezaji wakareketwa wa imani yao. Kwa upande mwingine, mwisho wa Ukristo kama dini ya dola lazima ulifanya iwe rahisi kwa Uislamu kupokelewa na wakazi katika bonde la Nili. Katika dola ya kusini zaidi ya Alwa, Ukristo ulibakia hai hadi mwanzoni mwa karne ya kumi na sita ulipoondolewa kwa nguvu za pamoja za mbari za Kiarabu na Wafunji.

Kufuatia Waarabu Wanomadi, walikuja wahubiri wa Kiislamu na watawa. Ama walitoka au walikuwa wamesoma dini katika nchi za Kiislamu za siku nyingi; na ndio waliokuwa wa kwanza kuingiza, katika nchi hii, maarifa ya Sharia Takatifu (*sharia*). Katika karne zilizofuata, wamisheni wa Kisufi walianza kukalia Sudani na kuchangia katika kuhubiri Uislamu. Walifaulu kuwaongoa Wafundji, watu wa ngozi nyeusi ambao ni wa asili ya Blue Nili ya juu. Chini ya utawala wa wafalme wa Funji, Uislamu ulihimizwa na wanazuoni na watawa wengi walihamia katika Ufalme wao. Tangu karne ya kumi na sita na kuendelea, mpaka wa kusini wa Uislamu ulitulia katika mstari sambamba wa 13.

### Pembe ya Afrika

Upenyezaji wa Uislamu katika Ethiopia ulifuata njia mbili kuu za biashara zilizoingia ndani kutoka Visiwa vya Dahlak na Zayla.

Visiwa vya Dahlak vilikwishakuwa vya Kiislamu mwanzoni mwa karne ya nane, na wakati huo huo sehemu nyingine za pwani katika fuko za Bahari ya Shamu zilianza kukaliwa na Waislamu, wengi wakiwa Waarabu au watu wasio wa asili ya Kiafrika. Uislamu ulitangazwa kutoka vituo hivi miongoni mwa wenyeji ambao wengi walikuwa Wanomadi wa pwani, lakini athari za usilimishaji hazikuwa na nguvu hadi baada ya karne ya kumi.

Kikwazo kikubwa dhidi ya ueneaji wa Uislamu katika nyanda za juu kilikuwa uimara wa kanisa la Kiukristo miongoni mwa Watigre na watu wasemao Kiamhara wa kaskazini mwa Ethiopia. Hapana shaka watawala waliwakaribisha wafanyabiashara wa Kiislamu kutoka katika makazi ya pwani, lakini waliwazulia kutangaza imani yao. Mnamo karne ya tisa, jumuiya za Kiislamu zilikuwa zimekwisha kujitokeza katika vituo vikubwa na katika njia kuu za biashara.

Kusini lango kuu walimopenyezewa Waislamu lilikuwa bandari muhimu ya Zayla na ilikuwa ni katika sehemu hizi za kusini mwa eneo la Ethiopia ambako Uislamu uliehukua dhima kuu.

Hali katika nchi nyuma ya Zayla ilikuwa tofauti na ile iliyokuwapo kaskazini; lilikuwa eneo la mpakani kwa Waukristo na Waislamu ambao walianza kupambana, kila upande ukjaribu kuwaongoa wenyeji wengi waliokuwa na imani za dini za jadi. Hali zilizoruhusu kukua kwa athari ya Kiislamu tokea karne ya kumi na kuendelea, kwa kiasi zilikuwa za ndani - k.v. kudidimia kwa ufalme wa Kiukristo - na kwa kiasi za nje, k.v. kutwaa mamlaka kwa Wafatimi katika Bahari ya Shamu kulikofuatiwa na kufufuka kwa biashara.

Miji na vituo vya awali vya biashara vya Kiislamu katika fukwe za Ghuba ya Aden vilianza kupanuka kufuata nyanda za Harar mwishoni mwa karne ya kumi. Kufikia mwanzoni mwa karne iliyofuata, upanuzi wa Uislamu ulifanya zianzishwe tawala za Kisultani za Kiislamu miongoni mwa Wasemiti na Wakushi wa eneo hilo.

Mojawapo ya falme muhimu za Kiislamu ulikuwa ule wa Ifat ambao watawala wake walidai pia kuwa wa ukoo wa jamaa ya Mtume Mohammad kwa kupitia Abu Talib. Sultani wake mkuu Umar Walasma alitwaa Usultani wa Shoa na kuunganisha na ule wa Ifat mnamo mwaka 1285.

Vyanzo vya Kiarabu na Kiethiopia huonyesha kuwepo kwa walau falme tatu za Kiislamu mbali na Ifat: yaani Dawaro (magharibi mwa eneo la Harar), Sharka huko Arusi, na Bali kusini mwa Dawaro. Katika nyakati za baadaye hutajwa dola nyingine kama Hadya, Arabuni na Darah. Hasa

Hadya ilikuwa maarufu kama kituo cha biashara ya watumwa kutoka karne ya kumi na tatu na kuendelea<sup>8</sup>.

Ni vigumu kusema ni kwa kiasi na kina gani usilimishaji wa wenyeji, ukiacha kando wafanyabiashara na wajumbe wa mabaraza, ulienea katika karne hizi za awali. Tarihi ya Usultani wa Shoa huelezea uongofu mkubwa ndani ya nchi hizi kufikia tu mwanzo wa karne ya kumi na mbili, hasa kwenye vilima vya mashariki mwa nyanda za juu za Shoa. Katika eneo la Harar, maandishi-picha ya Kiarabu ya karne ya kumi na tatu hushuhudia kuwepo kwa jamii za Kiislamu zilizoendelea sana na hivyo kuthibitisha umuhimu wa Harar kama kituo cha uenezaji wa Uislamu katika eneo hili. Wakati wa mashambulizi ya Waukristo kusini, hapana shaka Uislamu ulipata hasara kubwa katika athari na idadi ya watumini wake. Wakati Ahmad Gran alipoanzisha *jihadi* yake dhidi ya Ethiopia ya Kiukristo, katika karne ya kumi na sita, alifanikiwa kuwaingiza katika jeshi lake Waafar na Wasomali wengi kutoka sehemu za tambarare, na pia watu mbalimbali wasemaji wa lugha za Kisemiti na Kikushi wa nyanda za juu, ambao walikuwa wamekwishaathiriwa na Uislamu kwa muda mrefu. Hata kama jaribio hili la kuanzisha himaya ya Kiislamu ya Ethiopia lilishindwa hatimaye, kingo za mashariki na kusini mwa Ethiopia zilibakia kikamilifu chini ya athari za Kiislamu.

Kuanza kwa usilimishwaji wa Wasomali nako hakueleweki vizuri. Hapana shaka kwamba vikundi vya Kisomali vilivyoishi katika pwani ya Ghuba ya Aden vilikutana na Waislamu mapema sana. Wafanyabiashara wa Kiarabu na Kiajemi, yaelekea ndio walikuwa wa kwanza kukalia miji ya pwani, ambako walioana na wenyeji na baadaye kuungana na wenyeji wa Kisomali. Walileta Uislamu kama dini na kuwaathiri Wasomali walioishi katika makazi haya na pia ndani ya nehi, ambao nao polepole wakawa Waislamu. Mapokeo ya Kisomali huelezea kwamba Shayk Dard Ismail alifika Bara Arabuni, akakalia miongoni mwa Wadir na kuwa babu wa ukoo mkubwa ulioitwa kwa jina lake, yaani Darod. Inakubalika kwa jumla kwamba tukio hili lilitokea mnamo karne ya kumi au ya kumi na moja. Kuna mapokeo yanayofanana na haya kuhusu kufika, karne mbili baadaye, kwa Mwarabu mwingine, Shayk Ishak, muasisi wa Wasomali wa Isaq, waliokaa magharibi mwa Darod. Mapokeo haya yanaelekea kutupa picha ya kipindi cha harakati kubwa za usilimishaji miongoni mwa Wasomali wa kaskazini na pia kukua na kupantuka kwa koo za Darod na Isaq karibu katika kipindi hicho hicho. Kuundwa kwa koo kubwa zilizounganishwa na Uislamu kulitoa nguvu na kuanzisha uhamiaji wa jumla wa vikundi hivi ndani ya pembe ya Afrika, mwelekeo wao ukiwa kusini ambako walieneza athari zao kwa makundi ya Wasomali wa Isaq, waliokaa magharibi mwa Darod ambao, hadi hapo, walikuwa hawajafikiwa na wageni.

Wasomali waliokuwa wakiishi katika pwani ya Bahari ya Hindi waliujua Uislamu kutoka miji ya pwani ya Mogadishu, Brava na Marka, ambako Waarabu na Waislamu wengine wafanyabiashara walikuwa wamekaa kwa wingi tangu karne ya kumi. Kuungana kwao baadaye na wenyeji kuliubua jamii na utamaduni wa mchanganyiko wa Kisomali- Kiarabu; jamii ambayo sifa yake muhimu ilikuwa Uislamu. Miji ya pwani, ikiwa mno ni vituo vya biashara, lazima ilikuwa na mawasiliano ya mara kwa mara na wakazi wa bara. Haijulikani kwa yakini kama miji hiyo nayo ilichangia katika uenezaji wa Uislamu kwa kiwango sawa na vikundi vya Kiislamu vya kaskazini.

### Pwani ya Afrika Mashariki na Visiwani

Kufika na kukaa kwa Waarabu na Waajemi Waislamu pwani ya Afrika Mashariki, Visiwa vya

8 Taz. Historia ya nchi hizi, Sura 20 ya juzuu hili

Ngazija na Bukini, kutajadiliwa kwa undani katika sura zinazohusika, katika Juzuu hili<sup>9</sup>. Hapa tutajihusisha tu na kuenea kwa Uislamu; na kuhusu swala hili, katika kipindi kina-chojadiliwa, eneo hili hutoa picha tofauti sana na ile ya sehemu iliyokwishajadiliwa ya Afrika ya tropiki. Ni kweli kwamba Uislamu ulishamiri hapa, lakini ulishamiri tu kama dini ya wahamiaji kutoka ng'ambo walioishi kama jumuiya zilizojitenga katika makazi pwani na visiwani. Ingawa vyanzo vya kiakiolojia na vya Kiarabu hutoa ushahidi wa kutosha wa tabia za Kiislamu za miji ya pwani toka Lamu hadi Msumbiji, wakati huohuo vinathibitisha kwamba Uislamu haukupenya ndani na kwamba hakuna Wabantu wala makundi mengine walioguswa na dini hii hadi karne ya kumi na tisa. Uislamu ulifaulu tu miongoni mwa watu wa pwani waliokuwa karibu na Waarabu na/au Waajemi kutoka ng'ambo, katika miji.

Hapana shaka kuwa katika miji ya pwani ilikuwa ya Kiislamu, lakini haikuwa ya Kiarabu. Wahamiaji ambao hawakuwa wengi sana walioa wanawake wa Kiafrika na kuungana na wenyeji. Kwa muda mrefu baadaye, Waislamu Afrika Mashariki walikuwa wachache sana wakiwa na mwelekeo wa baharini kuliko wa barani Afrika kwenyewe.

Kupenya kwa Waislamu katika sehemu za bara za nchi za sasa za Msumbiji na Zimbabwe, wengi wao wakiwa wafanyabiashara wa Kiswahili, kulikuwa kinyume na hali hii ya jumla. Vyanzo vya Kireno vya karne ya kumi na sita vina maelezo mengi kuhusu wafanyabiashara wa Kimoori (*Moor*) katika himaya ya Mutapa ambao ushindani wao uliwatia uchungu Wareno. Wengi wa wafanya-biashara hawa walikuwa Waafrika weusi, ama wahamiaji wa Kiswahili kutoka vituo vya zamani vya pwani kaskazini au wenyeji waliokwishapokea utamaduni wa kibiashara wa kimataifa wa jamii za Kiislamu za mijini. Kupenya kwa Waislamu wa pwani kuingia ndani ya bara la Afrika kusini-mashariki hakukuacha urithi wowote wa kuonekana miongoni mwa watu wa eneo hilo. Kwa nia na madhumuni yake yote, Uislamu haukupokelewa kama dini na Waafrika wa bara ingawa walikuwa na mawasiliano na Waislamu kwa karne nyingi.

Waislamu wa pwani walifanya juhudi za kutangaza dini katika visiwa vya Ngazija. "Washirazi" ambao *Tarhi ya Kilwa* hueleza kuwa ndio wasilimishaji wa Kilwa, yasemekana nao walikikaha Kisiwa cha Anzuan. Yaelekea kwamba, Waislamu wa kwanza walifika mnamo karne ya kumi na tatu, wakachanganyika na wenyeji wa Kimalagasi na wa Kiafrika visiwani humo na kuibua watu wanaojulikana kama Antaloatra ('Watu wa baharini'). Kulingana na utafiti wa karibuni, usilimishaji wa mwisho wa Visiwa vya Ngazija ulitokea mnamo karne ya kumi na tano.

Japokuwa katika muongo uliopita maendeleo makubwa ya kuafiti Uislamu Bukini yalipatikana, bado kuna maswali mengi zaidi kuliko majibu yaliyotolewa. Kwa mujibu wa maelezo ya kiakiolojia, mapokeo simulizi, na maelezo ya awali ya Kireno hapana shaka kwamba watu waliosilimishwa, wakiwa wa asili ya Kiarabu au zaidi wa asili ya Kiswahili, walianza kukalia upwa wa kaskazini magharibi na visiwa vidogovidogo jirani kuanzia karne ya kumi na kuendelea. Kutoka kaskazini watu waliosilimishwa hulienea upwa wote wa mashariki hadi Port Daughin.

Mapokeo ya baadhi ya makundi ya Wamalagasi hudai babu zao walikuwa wa asili ya Kiarabu, si kaskazini tu, lakini hasa kusini-mashariki; makundi muhimu miongoni mwao yakiwa Zafiraminia, Onjatsy na Antemoro. Wahamiaji wa 'Kiarabu' polepole walimezwa na wenyeji wa Malagasi, na kitu tu cha ustaarabu wao wa Kiislamu kilichobakia ni hati za Kiarabu (*sorabe*), kumbukumbu hafifu zisizo wazi za Kurani na tabia za kijamii na kidini (hasa katika nyanja za *geomancy* (jiomansia na ujusi); lakini hakuna mabaki ya asasi za Kiislamu wala misikiti. Hivyo makundi haya hayawezi kuchukuliwa kama ya Waislamu.

Lakini kinyume na hali hiyo, kwa kuwa Waislamu wa kaskazini waliendelea kuwasiliana na Waislamu wa nje na kuimarishwa na luja za wahamiaji wapya, walibakia na dini yao na hata kuweza kueneza kwa majirani wao wa Kimalagasi. Tabia halisi ya Kiislamu ya makazi haya huthibitishwa na wageni wa awali wa Kireno katika karne ya kumi na sita, waliozungumzia misikiti mingi na *mashehe* na *makadhi* kama wawakilishi wa mamlaka ya kisiasa na kidini. Kama ilivyokuwa katika visiwa vya Ngazija wakazi wa dola-miji hizi nao walijulikana kama Antalaotra, neno ambalo hutumiwa hadi leo hii kuonyesha kundi la wakazi wa Bukini waliosilimishwa.

Mwisho, yafaa isisitizwe kwamba Uislamu haukuwa na dhima sawa huko Bukini kama ilivyokuwa katika sehemu nyingine za Afrika ya tropiki ambako, katika muda fulani, ulikuwa dini ya mbari nzima na kuathiri jamii za Kiafrika. Haukupata kulazimisha utamaduni wake juu ya Malagasi, na kwa hakika, katika sehemu za mbali kisiwani humo, mambo yalikuwa kinyume, yaani kumezwa kwa Waislamu na wenyeji.

### Hitimisho

Kati ya karne ya saba na ya kumi na sita, Uislamu ulikuwa umeanzishwa katika sehemu kubwa za Afrika. Usambazaji wake haukuwa sawa au wa namna moja katika sehemu zote, kwani mbinu, njia na vichochezi tofauti vilitumika katika kila sehemu ya Afrika. Kwa jumla ruwaza zifuatazo za Usilimishaji zinaweza kupambanuliwa.

- (1) Utamalaki wa Waarabu Misri na Afrika Kaskazini. Hii ingawa haikuandamana na uongofu wa lazima wa wenyeji wa Kikhufu na wa Kiberiberi, iliunda hali ya kijamii na kiuchumi ilizofanya Uislamu ukubalike kwa wenyeji wengi.
- (2) Shughuli za kibiashara za Waislamu, kwanza biashara ya mbali au ya ng'ambo na baadaye biashara ya kikanda, zilichochea usili-mishaji katika sehemu kubwa ya Afrika ya tropiki. Mawakala wa mwanzo walikuwa wafanyabiashara wa asili ya Kiarabu (kutoka Bara Arabu kwenyewe kwa upande wa Mashariki), Kiajemi (mashariki) na Kiberiberi (magharibi). Tangu karne ya kumi na moja na kuendelea, uenezaji Uislamu uliendelezwa kupitia shughuli za Waafrika Waislamu - Wasoninke, Wamalinke, Wafulbe, Wakanembu, Wahausa, n.k.
- (3) Wahubiri au watawa walikuwa wa kwanza kuingiza Uislamu kwa Wasomali ambapo katika maeneo mengine walichangia katika uimarishaji wa imani miongoni mwa watu waliosilimishwa rasmi (Afrika Magharibi na mashariki mwa Sudan) na kueneza kufuatia wafanyabiashara.
- (4) Katika Sudan ya Kiniloti usilimishaji ulifuata kupenya kwa Waarabu Wanomadi, ambapo katika nchi ya Wasomali uhamiaji wa baadhi ya koo kuelekea kusini ulikuwa kipengee muhimu kilichosababisha kuenea kwa imani mpya katika makundi mengi.

Kaskazini mwa Afrika, Nubia na Ethiopia, Waislamu waliokuwa wakiingia walikumbana na upinzani wa dini za Kiukristo za *imani ya Mungu* mmoja. Upinzani wa Wawakristo wenyeji dhidi ya usilimishaji ulitofautishwa kulingana na hali za kisiasa na kijamii za mahali hapo. Katika Maghrib, ambako Wakristo walikuwa wachache tu (mara nyingi watu mchanganyiko au wageni), usilimishaji ulikamilika na kufikia karne ya kumi na moja Ukristo ukakoma. Huko Misri, usilimishaji ulichukua muda mrefu na uliongezeka kasi tu chini ya Wafatimi; usilimishaji haukukamilika kabisa, kwani asilimia 10 ya Wamisri wote bado ni waumini wa Kanisa la Khufu.

Katika Nubia ya Ukristo, Uislamu, hadi mwishoni mwa karne ya kumi na tatu, haukuwa na

uzito, lakini katika karne mbili zilizofuata, Ukristo ulitoweka polepole na nafasi yake kuchukuliwa na Uislamu. Ni katika Nyanda za juu za Ethiopia tu ndipo Ukristo ulipostahimili. Si upenyezaji wa amani wa wafanyabiashara wa Kiislamu wala mashambulizi ya kijeshi ya dola za Kiislamu kusini mwake vilivyoweza kutikisa imani ya Waethiopia ya toka kale. Ingawa katika Ethiopia Ukristo ulishinda mapambano haya ya karne nyingi, ulibakia kuwa eneo dogo lililozungukwa na Uislamu.

# 4

## *Uisilamu Kama Mfumo wa Kijamii katika Afrka Kuanzia Karne ya Saba*

Uisilamu kama dini, na hivyo kama sehemu mojawapo ya utamaduni wa kiroho na kijamii, ni kipengee kimojawapo kati ya vipengee muhimu vya ustaarabu wa kileo wa Kiafrika, kiasi kwamba wakazi wengi wa bara hili mara nyingi huuchukulia Uisilamu na Afrika kama kitu kimoja.

Ujumbe wa Uisilamu ulielezwa kwa lugha ambayo Mungu "aliteremshia neno lake," lakini, hata hivyo, Kiarabu kikawa ndicho chombo cha utamaduni maalumu ambao kwanza ulikuwa wa Kiarabu na baadaye ukawa wa Kiislamu. Kwa hivyo Uisilamu ungeweza kuwa chombo kilichobeba utamalaki wa kitamaduni ambao ulikuwa chanzo cha migongano na tamaduni nyingine zilizokuwa zimeota mizizi katika jamii za aina nyingine. Tamaduni na jamii za kabla ya Uisilamu huko Mashariki ya Karibu zilihitaji kutiliwa maanani, hasa kwa sababu urithi wa maandishi yao na utamaduni wa Kiislamu, kwa kiasi fulani, vilikuwa ni mwendelezo wake. Swala la tamaduni na jamii za Kiafrika lilikuwa gumu zaidi kushughulikia. Ama kwa hakika, tofauti na wakazi wa Mashariki ya Karibu na Waethiopia, kwa kuwa Waafrika hawakuwa na Msahafu ambao ndio ufunuo wa masharti ya Mungu, tangu mwanzo Waafrika weusi na dini yao waliainishwa kuwa kati ya watu wasio na dini inayoheshimiwa, wasioweza kupata hadhi ya kulindwa na Uisilamu na hivyo kuwa na uwezekano mdogo wa kuwa na lugha na tamaduni za kuheshimika.

### *Uisilamu, Waafrika na tamaduni zao*

Uisilamu unaamini na kufundisha umoja ambao hauzuili tofauti za kitamaduni. Unasisitiza sana umoja wa binaadamu na kutambua kuwa watu wote wana asili moja, wameumbwa na Mungu. Wote wametokana na "jamia" moja ya Adam ambaye Mungu amempa, katika kipindi kisichokuwa na mwanzo wala mwisho, "masharti ya mwanzo." Katika kiwango hiki cha ujumla wa kinadharia, msingi huu wa umoja wa Uisilamu usingeleta matatizo yoyote kwa Waafrika.

Chini ya umoja huu, kitu ambacho ni rahisi kuelewa na kukubali, inaelekea kuna hatua ya pili ya mawasiliano na Uisilamu: desturi zinazoashiria kuwa mtu anakuwa katika jumuiya ya Kiislamu na hivyo, pia, kuzuiwa kujihusisha na maisba mengine ya kidini zaidi ya yale yanayotakiwa na Kurani. Umoja katika imani na shughuli za kidini, mshikamano wa kidugu baina ya waumini ambao wote ni "ndugu", ukarimu na haki ambavyo vinatokana na hisia hii ya udugu wa kijamii navyo pia havileti matatizo makubwa kinadharia. Fikra za kijamii za Muisilamu mwaminifu zinaonekana kama zilizoainishwa na nguvu za kibinaadamu katika kusaidiana, ukarimu, wema na kuwa na wajibu kwa jamii yako (umma) kwanza, lakini pia kujihusisha na jamii nyingine, na kupunguza tamaa. Haya ndiyo malezo ya msingi wa umoja ambayo yanauainisha Uisilamu na ambayo yanaupa Uisilamu

upekee wake. Moyo huu wa kijumuia unalingana sana na tamaduni zilizokomaa za Kiafrika za mfumo wa kijamii. Hata hivyo umoja huu unakwenda sambamba na majukumu ya kikweli ya maadili binafsi: mtu hawezi kuadhibiwa kwa kosa la mwingine; kila mtu awajibike kwa matendo yake. Kwa hiyo hisia hii ya udugu wa kijamii, imeungana, kama vile kwa mfumo wa mawazo, na hali ya kila mtu kujali hatima yake na majukumu yake.

Lazima toka mwanzo ielezwe kuwa kitendo cha kuukubali Uislamu ni cha kibinafsi; kama ni lazima kiwe kitendo cha kuaminika, lazima kichaguliwe kwa ridhaa ya mtu: kulazimisha maadili na kutumia nguvu kumekatazwa na Kurani. Lakini pia ni usilimishaji kijamii ambao unaashiria kitendo cha kuunganisha jumuiya ya aina mpya na kukata mahusiano na aina nyingine za jumuiya za kijamii na kitamaduni. Hii ni hoja muhimu ya kujadiliwa kwa ajili ya mahusiano baina ya ulimwengu wa Kiislamu na jamii na tamaduni za Afrika. Mwafrika wa dini tofauti asingeweza kulazimishwa kuukubali Uislamu; hata hivyo, hadhi yake kidini - bila ya s- iliifanya ategemea kabisa Uislamu na bila kulindwa dhidi ya jumuiya ya Waislamu.

Kwa hivyo tumekwishaelekea kwenye hatua ya tatu ya mawasiliano: ile ya sheria. Zilipita karibu karne tatu kabla kanuni za kisharia hazijaanzishwa katika ulimwengu wa Waislamu kulingana na Kurani na mafundisho ya Mtume yaani *Sunna*. Sharia tukufu - yaani *sharia*, inakusanya maelekezo ya Kurani yakiwa yamejalizwa na makatazo na ufafanuzi uliomo kwenye maarifa ya sharia (*fiqh*). Sharia zimefasiriwa na vyo vyote vya maarifa ya sharia kwa njia tofauti na katika hali zilizotofautiana kwa viwango vya usisizi na usahihi wake. Kitu kimoja cha kuzingatia ni kwamba vyo vya maarifa ya sharia ambavyo Waafrika walihusika navyo upande wa magharibi havikuwa sawa na vile vya upande wa mashariki wa bara hili. Upande wa magharibi, kuanzia Maghrib hadi Afrika Magharibi, kulikuwa na msisitizo mkubwa na maatum wa Umaliki. Chuo cha Maliki ambacho kilikuwa na urasimi zaidi kuliko vyo vingine vya maarifa ya sharia, hasa baada ya ushindi wake katika karne ya kumi na moja, kilifikishwa kwenye kiwango cha juu cha kutokubaliana. Upande wa mashariki, Ushafii, ambao ulikwishaota mizizi huko Misri na ulitoa uhuru zaidi, ulitawala zaidi katika Pembe ya Afrika na Pwani ya Mashariki.

Mwisho, ni muhimu kuongeza kwamba karne ya kumi na moja ilishuhudia mielekeo ya pande mbili ambazo zilipingana kijuujuu tu. Kwa upande mmoja, Usumni ambao ulikuwa umeshinda, ulielekea kulazimisha uwiano kwenye mamlaka ya nchi na elimu, na kanuni moja ya Kiislamu, kwa kutumia sharia; kwa upande mwingine, kulitokea tena nguvu mpya ya mafundisho ya Kiislamu (usufii), ambayo kwa muda mrefu yalikuwa yamepingwa na ambayo yalijaribu kuelezea hisia za kidini kwa kutumia hali ya utawa au kuukana ulimwengu. Maghrib ilikuwa ndiyo ya kwanza kuyapokea mafundisho hayo. Mnamo karne ya kumi na mbili kulitokea udugu mbalimbali, wa kwanza ukiwa ni Kadiriyya; huko Moroko, udugu wa Shadhiliyya ulikuzwa sana na al-Jazuli mnamo karne ya kumi na tano na ulikuwa na dhima ya kisiasa na kidini. Mienendo yote hii ya karne ya kumi na moja ilikuwa na athari za msingi kwenye majadiliano baina ya Uislamu na jamii za Kiafrika. Athari ya kwanza, ambayo ilitawaliwa na Umaliki, iliifanya jumuiya ya Waislamu isikubali kupatana katika shughuli zake na desturi za utamaduni wa Kiafrika. Nyingine ilisambaza kwa mafanikio makubwa madhehebu ya watu watakatifu waliokuwa na dhima ya kubariki watu (*baraka*) - ambao waliweza kuwa waaguzi na wabashiri na walikuwa tayari kusilimisha vipengele vya kale kadhaa vya maisha ya kila siku ya Waafrika. Katika macho ya watu wa kawaida, ambao wakati wote walikuwa tayari kuamini miujiza, mawalii na *masufii* walielekea kuwa karibu zaidi na watu kuliko Mungu Mtukufu wa Kiislamu aliye mbali. Madhehebu ya mitume wa kienyeji wakati mwingine yalilipinga jukumu la Maka kuwa ndio mahali pa hija na wakati mwingine kuchukua madhehebu ya awali. Kutokana na hali hiyo kulitokea, kwanza huko Maghrib na baadaye hasa



baada ya karne ya kumi na saba - huko Afrika maghari, mwakilishi wa jamii tawala ya Uislamu wa magharibi - *Sufii*.

Hivyo, maendeleo ya sharia za Kiislamu, udhamini wake wa wataalamu walioungwa mkono na taifa, uongezekaji wa mafundisho ya imani katika Mungu, ni vitu vinavyoyahusu maisha ya jamii za Kiafrika kwa karibu zaidi kuliko imani au kufuata ibada tu. Katika maswala haya makutano hayakuwa rahisi kama makutano ya awali yalivyokuwa. Hapa hatari ilikuwa ile ya mkanganyiko baina ya kaida za maisha ya kijamii ya Mashariki ya karibu na imani ya Kiislamu.

Kulikuwa na wasiwasi kuwa jambo jingine la nne lingechangia: lile la kujaribu kuiga utamaduni uliofanana na wa Kiarabu; ikiwa na maana ya kuyakana mapokeo ya utamaduni wa Kiafrika na kuyakubali kikamilifu maadili ya ulimwengu wa Kiarabu bila kujali kama maadili haya yalichukuliwa kama yenye kufaa au mazuri zaidi au kama yalilazimishwa kuwepo. Katika muktadha huu, kulikuwa na uwezekano wa kuchanganya uarabishwaji na usilimishwaji.

Hili ni jambo ambalo linaweza kupimwa hata kabla mtu hajaanza uchambuzi wa hatua zilizofanya Uislamu uanzishwe kama mfumo wa kijamii katika Afrika; ilikuwa ni makutano baina ya watu, utamaduni na jamii za desturi tofauti, makutano ambayo matokeo yake yalitegemea kiasi ambacho kila upande uliweza kubainisha kati ya kile ambacho kilikuwa cha kitamaduni tu na kile kilichokuwa cha muhimu kwa ujumla. Mwishowe hili lilikuwa ni swala la kupenyezeka kwa jamii na tamaduni za Kiafrika, ambazo kwa vyovyote hazikuziachia kupita vivi hivi tu athari mpya ambazo zilitokea mashariki. Hii pia ina maana kuwa mkabala wowote juu ya mfumo wa kijamii unahitajia uchambuzi wa usilimishaji na kutamalaki, na kukutana kwa watu. Kuishi pamoja kijiografia kulisababisha kutoepukika kwa majadiliano baina ya Waislamu wa asili tofauti na baina ya Waislamu na wasio Waislamu kwa kuelezea eno la Kiislamu ambamo tatizo lifuatalo lilijitokeza: je upo, au haupo, umoja kwa maana moja ya neno hilo au kuna umoja katika sura tofauti?

### *Kipindi cha kuishi pamoja kwa urahisi: Karne ya kumi na moja*

Mapambano ya kishupavu ya Waberiberi dhidi ya aina fulani za usilimishaji<sup>1</sup> mara nyingi, yamenukuliwa kama ushahidi wa kuunga mkono dai kuwa katika Afrika ya watu weusi utamalaki ulikuwa wa kutumia nguvu. Ama kwa hakika, mara nyingi Waarabu walizuiwa katika kuendelea kwao mbele kuelekea kusini wakati walipopambana na ukinzani ambao ulikuwa mgumu sana kuushinda katika muktadha wa kihistoria na kisiasa ambao ama ulikuwa haufahamiki, ulifahamika kidogo au ulikuwa mgumu kuumudu: na hivyo kusababisha mashambulio kidogo dhidi ya Nubia, Fezzan, Kavar na dhidi ya Sus na Sahara Magharibi<sup>2</sup>. Mashambulio haya hayakuwa na athari kubwa na matokeo yake mara nyingi yalikuwa makubaliano ambayo yalihakikisha kuwa watu walioishi kusini walikuwa na amani. Baadaye usilimishaji wa Misri na Maghrib ulichukua maumbo ambayo yanajadiliwa katika sura nyingine za juzuu hili<sup>3</sup>.

Upenyaji wa Uislamu ndani ya Afrika ya watu weusi ulikuwa na vipengee changamani sana na ambavyo kimsingi havikuwa vya kutumia nguvu katika kipindi hiki cha mwanzo: Waberiberi wa jangwani waliosilimishwa, wafanyabiashara wa Kikhariji au wawakilishi wa maslahi ya Wafatimi walichukua dhima ambazo zilikuwa tofauti sana lakini ambazo hazikuwa na sifa ya utumiaji nguvu wa dhahiri. Mawazo yanatofautiana hata kwenye mbinu zilizotumiwa na Wamoravi katika

1 Taz. Sura 3 ya juzuu hili.

2 Taz. Sura 8, 9 na 11 ya juzuu hili.

3 Taz. Sura 3, 7 na 9 katika juzuu hili.

mahusiano yao na watu weusi mwishoni mwa kipindi hiki cha mwanzo. Kumekuwa na tabia ya kuegemea sana maandishi ya kihistoria ambayo yameathiriwa sana na ushindi wa waumini dhidi ya wasio waumini pamoja na utukuzaji wa mashujaa kadhaa kama 'Ukba ibn Nafi'.

Ama kwa hakika katika karne za mwanzo, ulimwengu wa Kiislamu ulikuwa na majukumu ambayo yalikuwa tofauti sana kaskazini mwa Sahara, kwa upande mmoja, na kusini mwa Sahara na Afrika Mashariki, kwa upande mwingine. Kuhusu upande wa kwanza, fikra za kimkakati zilikuwa za muhimu sana kwani Afrika Kaskazini wakati huo huo ilikuwa chipukio la upanuzi zaidi kuelekea Hispania, visiwa vya Mediterania na Italia, pamoja na ngome dhidi ya kurudi kwa aina yoyote ya Waukristo wapiganaji ambao walikuwa ni tishio la kila wakati.

Waberiberi walikalika maeneo makubwa kuanzia Atlantiki hadi Nili, wakazaga kote na kumiliki maeneo hayo kwa kutumia ngamia. Walikuwa na maisha tofauti tofauti, kuanzia kwenye maisha ya makazi maalum hadi kwenye maisha ya kutangatanga<sup>4</sup> Kaskazini ya bara la Afrika, walilazimika pia kukubaliana na matakwa ya kisiasa ya Dar- al-Islam. Ingawa jitihada zilifanywa na waumini warasimi kuondoa dalili za hatari - na zilizodumu kwa kipindi kirefu za muungano wa kidini, Waberiberi walibakia na kiasi fulani cha uasili wao ndani ya Uislamu na kiasi fulani cha uhuru wa lugha. Kwa muda mrefu kuheshimu kwao mapokeo yao ambayo hayakuathiri vipengee muhimu vya maisha ya Kiislamu kulivumiliwa. Kwa mfano, sharia za kimila na mifumo ya sharia zisizokitwa kwenye Kurani ni vipengee vinavyojitokeza katika sharia za Waberiberi, kwa mfano kwenye viapo vya pamoja kama njia mojawapo ya ushahidi, shuruti na viwango vya adhabu zinazofahamika kwa jina la *Ikanun (kanuni)*, na haki zinazoendeshwa na majaji wasuluhishi au mabaraza ya vijiji. Desturi za aina hiyo hazikugongana na sharia za Kurani, lakini zinaweza kuwa zimechangia kwa kiasi fulani upinzani katika maendeleo ya kusanifisha Usunni - Umaliki katika kipindi cha Wamoravi. Kwa vyovyote vile tunakuta vipengee hivi vikijitokeza katika utaratibu wa dola ya Wamoha. Baada ya mapambano makubwa ya karne ya nane, mwingiliano wa kinchi na kisiasa wa Waberiberi wa kaskazini ulikuwa kwa kiasi fulani umekamilika, na ulikuwa ni muhimu kwa ulimwengu wa Waislamu.

Kusini mwa Sahara, Waislamu waliingia kwenye majimbo walimoishi watu waliojibainisha kitamaduni na kijamii na ambako kulikuwa na tawala za kale ambazo zilikuwa na nguvu kama zile za kaskazini mwa Afrika au Ulaya Magharibi katika nyakati hizohizo. Ulimwengu wa Wasoninke, upande wa Magharibi, ule wa Wazaghawa au Wakenembu sehemu ya kati, ule wa watu wanaozungumza Kibantu upande wa mashariki, uliwashangaza Waislamu ambao hawakuchelewa kutoa maelezo marefu kuhusu taratibu za tabia za mbari zao. Hawakutaka kuwabadili na pia hawakutaka kabisa kuwafanya waache shughuli zao za kidini, kitamaduni na kijamii. Kwa muda mrefu waliridhika kuishi pamoja nao wao wakiwa wafanyabiashara tu, hali ambayo ilikuwa ya manufaa kwao na walifurahia kwa kiasi kikubwa uhusiano mzuri uliokuwepo baina yao na wafalme weusi na wafanyabiashara. Tena basi sera hii, ilikuwa na manufaa pia kwa upande wa dini.

Kabla ya karne ya kumi na mbili, Uislamu uliendelea kukua barani Afrika bila vita, yaani bila ufundishaji dini kwa kutumia nguvu. Maendeleo haya hayakuwa na athari kubwa kwa *Da-al-Islam*, hayakuweza kugeuzwa, na yali-zingatia zaidi wafalme na wafanya biashara kuliko wakulima. Lakini hata hivyo, mafanikio kadhaa yalipatikana kabla ya jitihada kubwa za kuipanua *Da-a-Islam* ambayo ilianza kukua mnamo karne ya kumi na moja na kuendelea.

Mara nyingi kilichotokea hakikuwa zaidi ya kumsilimisha rasmi mfalme: ngano inayohusiana na

4 Taz. Sura 9 ya juzuu hili.

kusilimu kwa mfalme wa *Mallal* inaelezea kipengee hiki vizuri sana<sup>5</sup>. Baadaye, tutarejea kwenye ukweli unaoshangaza kwa kiasi fulani kuwa Mansa wa Mali alipokuwa Kairo wakati wa hija alionyesha ujuzi wa kijuujuu sana wa sharia za Kiislamu kuhusu maisha. Kama hii ilikuwa kweli kwa wana wa wafalme tutasemaje kuhusu wafanyabiashara 'waliosilimu', ambao walikuwa washiriki waaminifu kwa sababu za kibiashara lakini ambao labda walikuwa Waislamu wa kijuujuu? Kwa upande wa vijijini, kulikuwa hakuna swala la kushawishi imani na ibada zao; hiyo ingenaanisha kuiharibu jamii yote na njia zake za uzalishaji. Tena basi inawezekana kwamba watawala ambao walisilimu waliona kuwa kulikuwa na faida ya kufanya hivyo; na hivyo waliweza kuyakwepa majukumu mengi yaliyopo katika taratibu za utawala wa Kiafrika pamoja na mfumo wa miiko yake iliyotawala utendaji wake, bila kugawana faida za imani mpya na wafuasi wao. Kwa kiasi fulani, Uislamu uliweza kukuza utawala wa kale na hata mamlaka ya kifalme.

Kwenye nyaraka za Waarabu tunapata marejeo mengi kuhusu upoteaji wa dhahabu wakati wazalishaji waliposilimishwa. Uwezekano huu ulikuwa na uharibifu sawa kwa Waislamu wa kaskazini (kama wateja) na kwa watawala wa wenyeji ambao ndio waliokuwa watu wa kati. Hivyo wauza dhahabu hawakusilimishwa, na walikuwa wengi sana<sup>6</sup>. Al - Umari anaelezea kuwa Mansa wa Mali alivumilia "kuwepo" kwa wapagani katika dola yake, ambao aliwasamehe kodi iliyowekwa kwa wale wasioamini lakini ambao aliwatumia kwenye uchimbaji dhahabu. Sababu kubwa ni kuwa utafutaji na uchimbaji wa dhahabu uliandamana na shughuli nyingi za kisihiri na ulifungwa na mfumo wa imani ambazo mpaka sasa dalili zake zinaweza kuonekana.

Hali hiyohiyo ilijitokeza kuhusu chuma, bidhaa ambayo inatoa mfano unaoeleweka zaidi kuliko dhahabu. Katika sehemu nyingi kulikuwa na uhusiano wa karibu baina ya utawala wa kifalme na mabingwa wa uyeyushaji na ufutaji chuma. Nafsi ya "mhunzi" pia ilihusishwa na sihiri, na nguvu hatari za mafundi chuma. Baada ya muda kupita, 'aina' hii ya uganga inazidi kuwa kinyume cha ile ya *masufii*. *Sufii*, au kwa ufupi bingwa wa sharia za Kiislamu alikusudiwa kuondoa athari za mfuachuma; inaelekea usilimishaji ulifuatiwa na kuvunjika kwa makubaliano ya awali baina ya nguvu za kifalme na wafuachuma. Hawa wa pili bado walikuwa wakiogopwa kutokana na nguvu zao za kisihiri na kiuchumi na polepole wakaunda kundi lililojitenga. Kwa vile jukumu lao lilikuwa muhimu, hawakutengwa kutoka kwenye maisha ya kiuchumi. Polepole kukazuka miongoni mwa wazo la matabaka, na mazingira ambamo wazo hili lilitokea yaliashiria hofu iliyosababishwa na sihiri yao. Mfano huu unaonyesha ni aina gani ya hatua ndefu na za polepole zilizochukuliwa kwenye kuanzisha mfumo wa kijamii wa Kiislamu, na kulikuwa na hadhari kiasi gani wakati zilipoanza kuhusiana na tabia zilizokuwa na mizizi thabiti.

Makundi ya wafanyabiashara wa Kiislamu yaliyoanzishwa kusini mwa jangwa yaliishi hapo katika jumuiya ndogo na yalikuwa yakipewa na watawala wa kipagani hadhi inayoweza kulinganishwa na ile waliyopata Waukristo au Wayahudi wachache katika maeneo ya Kiislamu ingawa wao labda walisamehewa malipo ya kodi.

Waibadi walikuwa na jukumu kubwa la wazi wakati wa kipindi hiki. Uhusiano wao ambao haukuwa na ugumu wowote na *Wasudani* (Wanegro) unaweza kuangaliwa kwa mshangao wa kiasi fulani, hasa kwa vile walikuwa na uchungu mkubwa sana dhidi ya Waislamu wengine. Labda hii ni ishara moja ya uhusiano mzuri ambao ulikuwepo kwa karne nyingi baina ya Waberiberi wa Sahara na watu weusi.

Vyanzo vya Kiibadi vinatoa mifano ya uvumilivu wa dhati wa kidini, kiasi kikubwa cha

5 Taz. Sura 3 ya juzuu hili. J.M.Cuq. 1975 uk. 101 na 195-6.

6 Taz. Sura 14 ya juzuu hili.

kuelewana na tamaduni za Kiafrika za 'kipagani' na shughuli zao za kijamii.

Mambo yalibadilika baada ya ushindi wa waumini wa Sunni kwenye karne ya kumi na moja na kutokeza hali za kidini ambazo hazikuwa tayari kuonyesha uvumilivu, kama vile kikundi cha Wamoravi. Huu ulikuwa ni mwanzo wa kipindi cha pili ambapo jitihada za Kiislamu zilizidi kuelekezwa kwenye usanifishaji wa mifumo ya maisha katika nchi zilizokuwa chini ya dola yake.

### *Mikinzano ya kijamii na kitamaduni baada ya karne ya kumi na moja*

Katika upande wa kijamii mambo yote yalitegemeana na jamii za Kiafrika kukubali mabadiliko yoyote yaliyopendekezwa au kulazimishwa na Uislamu, hasa kwa vile kimsingi hakukuwa na vikwazo kwenye kuzikubali imani hizi chini ya Mungu mmoja. Jamii za Waafrika weusi ambazo ziliingwiwa na Uislamu zilikuwa za vijijini; zilikuwa zinajishughulisha na ardhi pamoja na vipengee vingine vya mazingira yao (madini, mbuga, hewa na maji). Familiakiini- mume, mke, watoto - haikuonekana kama kitu kimoja huru: familia pana, yenye kizazi cha ukoo mmoja uliokitwa kwenye udugu na ardhi, ilikuwa ndio kitu cha msingi, kilichounganishwa na kiwango kikubwa cha muungano wa kiuchumi. Jamii hizi, bila kujali ukubwa wao zilionelea kuwa mshikamano wao - hata kama ulikuwa wa kimawazo tu - ulikuwa wa kidini na kwamba walikuwa na mfungamano wa kidini na ardhi, vichaka na maji, vitu ambavyo vilivapatia chakula na vilivyokuwa vya kuabudiwa. Miundo hii ya kijamii-kidini haikuweza kutenganishwa bila kuharibu uwiano mzima wa maisha yao. Hata katika jamii changamani zaidi, ambapo mazao ya ziada yaliruhusu kuwepo kwa madaraja ya kijamii yaliyojikita kwenye shughuli maalum (majusi na waganga, uongozi wa kisiasa, wakijeshi n.k.), Mwafrika alibakia na maoni yake kuhusu dunia kuwa kama mgongano mkubwa wa nguvu ambazo zilitakiwa kutulizwa au kutumiwa. Mara nyinyi muungano wa mawazo ya kidini ya uhusiano wa kijamii ulijitokeza kwenye tofauti za mali, na mara nyingi, nafasi ya mama na mwanamke kwenye uhamishaji mali ilikuwa kubwa. Njia za kuishi zilibakia kuwa tofauti sana na zile familia za Kiarabu za ukoo wa baba ambazo zinakubaliana sana na sharia za Kiislamu.

Ilikuwa kauka uwanja huu ambapo mivutano na migongano ilitokea; shinikizo liliwekwa na wanasharia wa Kiislamu, ambao wangependelea kuwashawishi Waafrika kujiingiza kikamilifu zaidi kwenye 'mfumo wa jamii' uliofikiriwa kuwa wa Kiislamu. Mivutano hii ilikuwa ya aina zilizotofautiana sana kutoka jimbo moja hadi jingine na katika nyakati tofauti kutegemeana pia na mahusiano ya nguvu za kila aina kati ya Waislamu na wasio Waislamu. Kwa hiyo, tunapojaribu kufanya tathmini ya jinsi Uislamu ulivyobadili au ulivyoshindwa kubadili jamii za Afrika ya watu weusi, tunashughulikia historia kubwa na changamani.

Wakati sehemu ya matukio ilipogeuka kuwa mji iliwezekana mtu kubadili jina lake na kujiingiza kwenye jumuiya mpya ya Kiislamu ambayo ilikidhi mahitaji yake yote, na kuanzisha familia mpya kwenye jumuiya hiyo chini ya misingi mipya ya kütikadi. Katika mtazamo wa kijamii, kubadili jina kunaruhusu uhamaji mzuri na rahisi, kutoka kwenye jumuiya ya asili kwenda kwenye jumuiya ya Kiislamu. Katika Afrika ya Saheli, uhamaji huu unaclekea ulifanyika kwa urahisi, lakini, kwa sababu ambazo ni yakini, hauonyeshi kuwa ulikuwa kamili: jina la Kiislamu, ambalo limefanywa liwe la Kiafrika kabisa - Muhammad lilinakuwa Mamadu, Ali linakuwa Aliyu - linaongezwa kwenye majina ya Kiafrika yaliyopo: haya yanasilimishwa tu baadaye na kulingana na taratibu maalum sana. Hali hiyo haikuwa hivyo katika majimbo mengine ya bara hili, ambapo kusitishwa kwa majina kulitokea kwa wingi na kwa namna ya kushangaza.

Waislamu wenyewe walikuwa wamegawanyika kuhusu mwelekeo wa kufuatwa kuhusu desturi za kijamii na kitamaduni za Kiafrika. Wanasharia wa kaskazini walielekea kuona kutokana na

ushahidi wa vitendo vya jamii za watu weusi 'wasiofuata ada' kuwa walikuwa wanahusiana na ulimwengu ambao ulikuwa mgeni kwa Uislamu na ambao ilibidi upingwe. Waislamu weusi waliozaliwa katika jamii hizi walishawishika zaidi kuziona shughuli za dini za Kiafrika kuwa hazikuwa kipingamizi dhahiri katika kukubali Uislamu, uvumilivu wao pengine ulikuwa mkubwa zaidi na wanadini wenzao kutoka kaskazini mara moja waliwashutumua kwa ulegevu, uchanganyaji wa imani na hata uhaini dhidi ya Uislamu Hata hivyo, ilikuwa ni hawa wa pili na wala sio wale wa mwanzo ambao, kama tutakavyoona, walihakikisha kuwepo na mafanikio ya muda mrefu ya Kiislamu kuanzia karne ya kumi na mbili hadi karne ya kumi na sita.

Ukaidi wa kisharia ulikuwa ndiyo sababu ya mkinzano juu ya swali la kuzikiuka sharia za urithi za nasaba za kukeni na kupendelea zile desturi za urithi za nasaba za kuumeni. Bila shaka mgongano huu ulizuka mapema mnamo karne ya kumi na moja; tukio linalokumbukwa sana likiwa ni ushauri wa al-Maghili ambao tutaurejelea baadaye: mwandishi alieleza kuwa wale waliokataa kanuni za Kiislamu na wakafuata mkondo wa urithi wa nasaba ya kukeni hawakuwa Waislamu.

Yaelekea kwamba dhana ya kumiliki mali ndiyo iliyoleta zaidi ile hali ya kutopatana kati ya jamii moja na jamii nyingine. Al - Bakhri alipoyaita baadhi ya maamuzi ya Abdallah ibn Yasin kuwa 'ya ovyo na ya kuchekecha' alikuwa anaonyesha chuki ya miliki mali binafsi dhidi ya mifumo ya 'kijamii', usawa na ugawanyaji upya wa mali ambao maimamu wa Kimoravi walitaka kufanya. Ndiyo kusema basi sababu kubwa ni kwamba ardhi katika jamii ya Kiafrika ilikuwa dhana isiyoleweka kwa Waislamu ambao walikuwa wamezoea maisha ya mtu na familia yake tu na utajiri wa mijini.

Migomo mingine midogo iliyojitokeza dhidi ya 'utovu wa maadili ya Waafrika' pia haikuwa na athari: upotofu mkubwa kwenye tabia za wanawake, kushindwa kwao kuvaa shela na vijana kukaa uchi. Waandishi wa Kiarabu wasingeweza kufanya mengi zaidi ya kuweka kwenye maandishi au kushutumua 'kashfa' zilizoudhi mtazamo wao.

Katika ngazi zote hizi zenye aina ya mifumo ambayo haifanani, tofauti baina ya jamii za Waarabu Waislamu na Waafrika, wawe Waislamu au vinginevyo, zilibakia bila kupatanishwa kati ya karne ya kumi na mbili na karne ya kumi na sita.

### *Majukumu waliyokuwa nayo watawala wa kiafrika*

Watawala wa Kiafrika kwa ujumla walikubali kwa haraka mgawano wa nafasi na kazi ambao uliwahakikishia kuwa maofisa wa utawala waliowahitaji wangepatikana katika miji ambayo ama ilikuwa imesilimishwa kabisa au kwa kiasi fulani, wakati sehemu ya vijijini ilikuwa ni ehimbuko kubwa la watu wa kufanya kazi za kilimo ambao kusilimishwa kwao hakukuwa kunahitaji kuharakishwa. Wakiwa wameridhika na kusilimishwa kwa wanamfalme, ambao baada ya muda mrefu walikuwa ndio wadhamini wa kuusilimisha umma, Uislamu huenda ulichukua mtindo wa 'kichungaji' ambao pia ulipatikana katika Ulaya ya Ukristo katika nyakati hizo hizo.

Watawala wa Kiafrika, hata kama walikuwa Waislamu kweli kweli, haiwezi kusemwa kwa namna yoyote ile kuwa walikuwa watangaza dini. Hata hivyo, kulikuwa na jitihada za kupata muungano wa kisiasa na kijamii chini ya mfumo wa Kiislamu, kwa upande wao na pia kwa upande wa washauri wao wa Kiislamu kutoka kaskazini ya Afrika. Mfano mzuri hapa ni wa Mansa Kanku Musa anaporudi kutoka mashariki na msanifu-majengo al - Sahili, au Askiya Muhammad I au mtawala wa kinasaba wa Kano, Muhammad Rumfa: watawala hawa wawili wa mwisho walitumia huduma za imamu wa dini mcha-Mungu wa Tilimsan, al-Maghili, au zile za Mmisri al-Suyuti. Waandishi wengi wanaelekea kukubali uamuzi mkali uliotolewa na al-Idrisi kwamba 'hakuna

wasomi kati yao na wafalme wao wanapata kile wanachokijua kuhusu serikali na sharia kutokana tu na maelekezo ya wasomi wageni kutoka kaskazini zaidi." Kufikiri kama al -Idrisi anavyofanya ni kusahau kuwa jamii za Kiafrika, muda mrefu kabla ya uhusiano wao na Uislamu, zilikwisha vumbua miundo ya kisiasa ambayo hii leo tunaanza kuielewa zaidi lakini ambayo Waislamu na Waukristo hawakujua kabisa kwa karne nyingi. Namna ambavyo utawala uliendeshwa, ambao ulikuwa sehemu mojawapo ya dhana ya dini ya Kiafrika, haikuweza kuachiwa bila makubaliano ya jamii kwa ujumla na bila kuukubali Uislamu kikamilifu. Hivyo, tuna haki ya kujiuliza kama kweli watawala weusi hawakuchukua kutoka kwenye jamii ya Kiislamu, pamoja na imani yake ya Mungu mmoja, kile tu kilichowafaa na kukidhi utawala wa himaya yao na kama jitihada hizi za 'usasa' hazikuwa ni mfululizo wa jitihada za kuanzisha uwiano haina ya uzito wa utamaduni wa Kiafrika kabla ya Uislamu na mahitaji ya dini mpya.

Kwa kutumia mifano michache maalum, tunaweza kupima upeo wa kweli na sera ya kifalme ya kuingiliana na Uislamu.

Karne ya kumi na nne mara nyingi inachukuliwa katika historiografia ya Afrika kusini mwa Sahara kuwa kama enzi iliyoshuhudia kilele cha dola ya Mali; iliyoainishwa zaidi na maendeleo makubwa ya kiuchumi, athari za kisiasa katika medani ya kimataifa zilizohusisha mahusiano ya kidiplomasia baina yake na Moroko na Misri; na zaidi ya yote, maamuzi ya kuanzisha Uislamu.

Ingawa hakuna wasiwasi juu ya uchaji Mungu wa Kiislamu wa Mansa Musa, mfalme wa hija, na ingawa hatuwezi kukana kuwa Uislamu ulikuwa umeanzishwa kwa kiasi fulani, hasa mijini lakini umma wa wakulima arabao ndio waliokuwa idadi kubwa ya watu wa Mali, ulibakia na imani yao ya jadi na ambayo ilivuniliwa na *Mansa* kwa kubadilishana na utii wao na kodi zao.

Hebu tuangalie hali ilivyokuwa karne moja na nusu baadaye. Kipindi cha mwisho wa karne ya kumi na tano na karne ya kumi na sita kinatoa mifano mingine ya haja zilizoonyesha na viongozi fulani wa Kiislamu kuleta mabadiliko ya msingi ya tabia za Waafrika, na jinsi ambavyo watawala walikuwa wakisita kutekeleza haja hizo.

Askiya Muhammad alifanya jitihada kubwa ya kupata muungano wa kisiasa na kijamii kulingana na maadili ya Kurani. Ili kuhalalisha mapinduzi yake, aliamua kutumia kila njia iliyoweza kutumiwa katika dini ya Kiislamu. Alikwenda kuhiji Maka na cheo chake cha *Khalifa* kilimpatia madaraka ya kidini huko Sudan. Huko bara aliomba ushauri hasa hasa wa wasomi wa Kiislamu wa Timbuktu; aidha aliomba ushauri kutoka kwa wanasharia maarufu watatu: Abdulla Al-Amsammani wa Takedda, al -Suyuti na al -Maghili.

Askiya Muhammad, kwa kutaka kutimiza vigezo vya ukhalifa, alichukua alama za vyeo vya utawala wa kimashariki: mhuri, upanga na Kurani. Akaamua kuwa Ijumaa iwe ndiyo siku ya kuwaona watu kwa juma, akaingia kwenye vita vya kidini - ingawa bila mafanikio - dhidi ya 'makafiri'. Lakini hakuweza kuwa mbali na tamaduni za Kiafrika ambazo zilimfanya abakie na tabia za jadi alizorithi kutoka kwa wahenga katika kipindi cha ufalme uliotangulia: ngoma, moto mtakatifu, kanuni maahum zinazohusu mavazi, miundo ya nywele, mapambo ya kifalme, kutambika, kuwepo na utawala wa juu wa kiongozi mkuu wa dini kwenye ibada ya wahenga na majini.

Vivyo hivyo, hakutekeleza ushauri mkali aliopewa na al-Maghili dhidi ya "Waislamu bandia" waliomzunguka. Mafundisho ya al-Maghili yalibaki bila kutumika katika Afrika ya Maghribi hadi Uzman Dan Fodio alipoyatumia kama silaha dhidi ya wafalme wa jadi ambao wakati huu hawakuwa na faida tena katika upanuzi wa Uislamu.

Huko Bornu watawala (*mai*), ambao walikuwa miungu watu, hata hivyo walijaza vitala vyao na wasomi wa Kiislamu. Hawa wakati wa utawala wa Ali ibn Dunama (1422-1504) walijaribu kuyaingiza maadili ya watu mashuhuri katika uelekeo wa maagizo ya Kurani. Sultani alikubali lakini

watu mashuhuri walikataa kukubaliana naye. Vivyo hivyo, sharia zilizotekezwa na kadhi zilibakia mijini tu na hazikuchukua nafasi ya sharia za makundi ya Kiafrika. Katika eneo la Hausa, ambapo Uislamu uliingizwa mnamo karne ya kumi na nne, viongozi wa watawa wote wali-pambana na matatizo ya aina hiyo hiyo kwenye kuwashawishi watu wa vijijini, na hata wa mijini, kuingia kwenye dini ya Kiislamu. Huko Katsina, baada ya ziara ya al - Maghili, ambaye alijaribu kuwatakasisha Waislamu-nusu wa Kihausa, 'miti mitakatifu ya walioamini mizimu ilichomwa moto na misikiti ikajengwa mahali pake.'

Kutoshughulika kwa wafalme labda kulikuwa ni ishara ya kufahamu kwao kuwa misukumo ya kijamii ingeishia kwenye kuukataa Uislamu.

Ni katika maeneo yaliyokuwa nje ya uwezo wao, miongoni mwa watu wa kawaida, ambako maendeleo kamilifu ya Uislamu yalifikiwa wakati wa karne hizi. Wafanyabiashara wa Kiafrika, Wangare na baadaye Wajuula na Wamisheni wa Kiislamu wa aina zote waliufikisha ujumbe wa Uislamu vijijini na mijini hadi kwenye ukingo wa misitu. Upanuzi huu wa polepole haukubadili tabia za jamii ambamo makundi madogo ya Waislamu yalijitokeza.

### *Matokeo*

Katika hali ya sasa ya uchunguzi, matokeo ni magumu sana kufanyiwa tathmini na migongano iliyopo inaudhi.

Hapana shaka kwamba sana ya kuandika na mbinu za kupima uzito vilianzishwa kusini mwa Sahara na Waislamu mapema katika karne ya kumi. Ni kwa kiasi gani uvumbuzi wa vitu hivi viwili ulibadili tabia za mwanzoni? Je hapo awali ilikuwaje kuhusu utunzaji mambo ya zamani, kuhesabu na maarifa ya kimahesabu?

Yaweza kuwa sahihi kusema kuwa fasihi katika lugha ya Kiarabu kusini mwa Sahara inaelekea kuwa haikujali tamaduni za Kiafrika na lugha zake. Wale walokuwa wanaweza kusoma na kuandika 'Kiarabu' hawakujali tamaduni za kale za Kiafrika kwa vile kwanza zilikuwa ni za kipagani na pia kwa sababu hawakuwafahamu kuwepo kwake. Labda haitakuwa haki kuangalia kutoelewa huko kama kiashiria cha dharau toka mwanzo kwa jamii za Kiafrika na tamaduni zao.

Ilikuwa ni kawaida kwa watu walioelimika kama vile Wamalinke, Wafulani, Wasoninke, Waberiberi au Waberiberi Weusi, watu kama Mourimagha Konkoi wa Jenne, Baghayogho, Kati, Ibn Dansal al-Fulani, Ahmad Baba, ibn al - Mukhtar Gombele wa Timbuktu, na wengine ambao walikuwa wamefungamana zajdi na maandishi na imani za Kiislamu, kufikiria katika Kiarabu, kuandika kwa Kiarabu na kutoa maelezo kuhusu vitabu vinavyohusiana na tamaduni za Kiislamu. Fikra hizi za kuuona uislamu kuwa ndio kiini cha elimu zilivifanya vyo viko vya Timbuktu vionekane si vya kitaaluma sana kama ambavyo Waafrika weusi leo hii wangependelea kuviona, hasa kwa vile kwa kadri tujavayo hakuna alama zozote za utamaduni wao wa kale katika vyo hivyo. Wasomi wa Kiislamu walikuwa kwenye ulimwengu uliokuwa umejifunga kwa kiasi fulani na bado walikuwa kundi dogo dhidi ya umma wa 'wapagani' ambao walijiona wana wajibu wa kuwasilimisha na labda kuwaelekeza kwenye namna nyingine za maisha; hivyo hawakujiweka tayari kuwa wanahistoria wapevu wa Afrika ya kale au hata watazamaji walioyaonea imani maisha ya jamii za 'Kipagani'.

### *Usilimishaji-Uarabishaji*

Labda ni katika Kanem na Afrika Mashariki ambako mabadiliko ya mwisho ya jamii ya Kiafrika

yalianza kufanyika: 'kuarabishwa' kwa asili zao na maisha yao ya zamani. Afrika Magharibi nayo haikuchelewa kufuata mkondo huo.

Katika karne ya kumi na tatu, wakati wanashajara wa unasabatawala wa Kanembu walipojaribu kuunda upya ukoo wa watu bora waliokuwa wakitawala, walifanya uvumbuzi mmoja muhimu, nao ni ule wa kutafuta asili hizo upande wa Mashariki.

Huku kulikuwa kuingizwa kwa wazo ambalo lilitokea kuonyesha mafanikio makubwa na kuleta mabadiliko ya msingi katika uhusiano wa kitamaduni baina ya jamii za Kiafrika na ulimwengu wa Uislamu. Mwanamfalme wa hadhi yoyote ilikuwa lazima atokee Mashariki; asili yenye hadhi ya ustaarabu ilikuwa tu ile iliyotokea Mashariki na hakukuwa na uzamani mwingine ulioongelewa isipokuwa kama ulihusiana na Mtume, familia yake au marafiki zake.

Fasihi ya kishajara ilikuja kunawiri baada ya karne ya kumi na nne katika Afrika ya Mashariki, ambako ilitokea kuwa silaha mojawapo katika migongano ya kiitikadi baina ya vikundi vya upinzani vya Kiislamu na watawala hadi karne ya kumi na tisa. Katika Afrika ya Magharibi, mageuzi ya hadithi zinazohusu asili ya Wamandingo yalikuwa ya kuvutia sana, na yale ya asili za waanzilishi wa Wawagadu halikadhalika. Polepole kila kikundi kilichosilimishwa kikapata nasaba kutoka Arabuni. Hali hii kwa kiasi fulani ilikomaza nadharia ambayo inada kuwa watu wa Afrika walitokca Mashariki ya Kati, pamoja na matokeo ya kusambaa kwake ambayo yanaendana na nadharia hiyo. Jambo jingine lilikuwa ni ile shauku ya kuingiza asili ya 'weupe' - hapa neno 'weupe' ikimaanisha Waarabu na Waajemi - kwa kitu chochote chenye thamani Afrika, hata kama hiyo ilimaanisha kushusha kabisa thamani ya tamaduni za Kiafrika ambazo zilionekana ni za zamani sana. Hivyo ndivyo ilivyoanza kufiia historia ya Kiafrika ambayo baadaye ilififishwa zaidi na Wazungu.

Hakuna familia au kundi lolote ambalo mwishowe liliweza kuepuka mantiki hii ya 'Uarabishaji'. Hata Wabetsileo wa Bukini ya kati ambao walikuwa mbali na ambao hawakuwa na utamaduni wa Kiislamu, walivutiwa na 'mfano wa kustaarabika' wa Kiislamu wakatafuta asili za Kiarabu kwa wafalme wao; hawakuwa peke yao katika kufanya hivyo huko Bukini.

Hiki 'kiburi cha kishajara' kilikuwa ni uhibitisho wa umri na thamani ya shughuli za Kiislamu kwa wale waliofuatilia asili zao hadi kwenye vizazi vya Kiarabu; pia kilithibitisha 'haki za kihistoria' za umwinyi ambazo zilikuwa zinaanzishwa. Baadaye kiburi hiki kilikuwa na maana kubwa kiasi kwamba kilikuwa ni hatua za kawaida za kufanya makundi mengi yahusiane na Uarabu na kusilimishwa. Wamaba huko Waddai ni mfano mmoja mzuri; hadi karne ya kumi na sita walikuwa bado hawajaathiriwa na Uislamu. Majilio hasa hasa, au ya kisa cha kuzua, ya Mwarabu aliyedai kuwa na asili ya Kiabbasi, aliyetwa Jame mwishoni mwa karne ya kumi na sita, ndiyo yaliyobadili mkondo wa matukio. Jinsi dini mpya ilivyoziidi kupata mashiko ndivyo koo fulani za Kimaba zilivyodai kuwa na asili ya Uarabu Uislamu. Kabla ya muda mrefu kupita Waarabu walioa kwenye familia kubwa za Wamaba; wakawa nusu-wakazi na nusu wahamaji. Aidha kwa kiasi kikubwa wakajingiza kwenye tamaduni za Kiislamu za Wamaba. Athari zilikuwa kwa pande zote. Wamaba walijifunza lugha ya Waarabu na hivyo wakajiona kuwa hawakuwa na tatizo la kuelewa Kurani.

Kadri mafunzo ya Kiislamu yalivyoziidi kusambaa, Wamaba hawakuiga tu mfumo wa maisha ya Kiarabu uliotolewa na Uislamu bali pia walijinasibisha na Waarabu. Katika kila ukoo, mtawala yeyote aliyetawazwa alitafuta asili yake katika ulimwengu wa Uislamu Uarabu; shajara ya uzao ilifuatiliwa kwa kurudi nyuma mara nyingi hadi kwenye familia ya Mtume au kwa mmoja wa masahaba wake halisi wanne.

Usilimishaji, pamoja na Uarabishaji, vilikuwa na matokeo muhimu sana katika jamii yote ya Wamaba. Wamaba bila kujijua walijaribu kuandika upya historia, yao kwa kutunga historia ya uongo ya shajara zao iliyoandamana na kubadilisha kabisa jina.



Kiungo cha mwisho katika mfululizo wa mabadiliko yaliyoletwa na Uislamu katika maisha ya jamii za Kiafrika labda ndicho kilichokuwa kitu muhimu kati ya vyote. Kiungo hicho kinasababisha 'kubadilishwa kitamaduni' kwa jamii ambamo mfululizo wa mabadiliko hayo ulipata mashiko na kuunda 'Uarabu - Weusi' ambao unaelekea kuwa ukinzani wa kihistoria na ambao unadhoofisha kitamaduni jumuiya ya Kiislamu. Jamii nyingi za Kiafrika hazikufanya kama walivyofanya Wamaba. Zilitathmini madhara yaliyoelekea kuwepo katika njia hizo nyingine zilizoletwa au kulazimishwa. Wakati mwingine, jibu lao lilikuwa hata kuukataa Uislamu. Hatimaye wale waliohusika kwenye tatizo hili walikuwa ni wale ambao, baada ya kuwekwa pembeni nje ya mabadiliko yaliyoletwa na Uislamu, waliumia kutokana nayo kwa sababu ya kudharauliwa kwa imani zao na ule mtazamo ambao uliwachukulia wao kama chanzo tu cha kupatia watumwa. Hivyo, mara nyingi kulikuwa na kutoaminiana na idadi fulani ya jamii za Kiafrika ilishawishika kukataa waziwazi na hata kujikuta waziwazi, na hata kupambana na Uislamu.

### *Mjadala ulivyoingiliwa: mwishoni mwa karne ya kumi na sita hadi mapema karne ya kumi na saba*

Mwishoni mwa karne ya kumi na sita na mwanzoni mwa karne ya kumi na saba ni kipindi kinachonyesha hatua muhimu katika historia ya Afrika Magharibi. Kilikuwa ni kipindi cha mapumziko kati ya kumalizika kwa kipindi kirefu na cha utajiri mkubwa ambacho kilishuhudia kuanza na kukua kwa madola makuu ya watu weusi wa kusini mwa Sahara pamoja na migongano ya mitazamo miwili ya ulimwengu, ule wa dini ya asili ya bara la Afrika na ule wa Uislamu, na mwanzo wa kipindi kingine, ambacho kilikuwa kifupi cha ghasia kubwa na wasiwasi wakati ambapo dini ya Kiislamu ilisitisha kidogo upantikaji wake au hata kujitoa kwenye kanda nyingi.

Ilikuwa ni wakati wa himaya ya Songhay, chini ya uongozi wa Sonni Ali (1464 - 1492) ambapo chuki dhidi ya Waislamu ilipopamba moto, ilielekezwa sio dhidi ya watu bali dhidi ya athari za itikadi waliyotangaza, ambayo ilionekana kutolingana na amali na tamaduni za Kiafrika.

Wakati mamlaka kuu ya Mali ilipokuwa inapungua nguvu, kadhaa ya majimbo na maeneo vijijini na mijini yalipata uhuru. Watu matajiri wa mijini, ambao waliongozwa na kuratibiwa vizuri na Uislamu, walianza kufanya mambo yao katika uhuru na hata kukawa na jamhuri huru za wafanyabiashara. Kwa mfano, hali hiyo ilijidhihirisha huko Jenne, Walata na Timbuktu. Katika himaya mpya ya Songhay ambayo kutokana na ushindi iliweza kurithi majimbo ya mashariki ya Mali, mahusiano baina ya Sonni Ali na miji hii, hasa Timbuktu, yaliharibika haraka sana na kuwa migongano mikubwa. Kisa hasa kinaelekea kuwa serikali kukiwa kwenye misingi ya utawala wa kifalme. Sonni Ali, mfalme msihiri, aliyekuzwa chini ya maadili ya ufalme wa Kiafrika wenye nguvu hakuweza kuvumilia kuona nguvu zake za kisihiri, ambazo zilitambuliwa na idadi kubwa ya wafuasi wake wa imani ya dini ya jadi, zikipingwa na wasomi wa Kiislamu wa Timbuktu ambao, zaidi ya hayo, walikuwa wageni. Waberiberi, Waberiberi - Weusi na Wafulani, kwa kweli walikuwa ndio idadi kubwa ya watu wa mji huo. Utawala wa Sonni Ali ulitambulika kwa kudhibiti Timbuktu, kukua kwa himaya ya Gao na kwa namna nyingine, kutokeza kwa upinzani wa dini ya Kiafrika dhidi ya Uislamu. Mapinduzi ya 1493 yaliyoongozwa na Askiya Muhammad na haja ya kufanya "chaguo la Kiislamu" lisibatilishwe yanaweza kuelezwa tu katika muktadha huu.

Mwisho wa karne ya kumi na sita ulikumbukwa kwa utamalaki wa Moroko. Kuanguka kwa kiunzi cha kisiasa na uvurugaji wa mfumo wa kijamii vilisababisha kuanguka ghafla kwa miji ya Songhay. Ukinzani dhidi ya majeshi ya kivamizi ya Moroko kwa muda wa miaka kumi ulisababisha watu kwenda kusini, hasa kwenda Dendi. Watu hawa waliungana kama serikali ndogo huru zenye

miundo ya kijamii na kidini iliyotokana na jadi zao za kale na hawakubaki na kitu chochote cha Kiislamu isipokuwa majina yao.

Kilichokuwa muhimu zaidi ya kurudi nyuma huku ni ule uchafuzi wa kijamii na kidini katika ombwe la kisiasa lilotokana na kutoweka kwa dola ya Songhay na mvurugano wa uvamizi wa Moroko, kujitokeza kwa ufalme uliodai kufuata imani za mizimu na kuzingatia mila na amali za Kiafrika. Huu ulikuwa ni ufalme wa Kibammana (Bambara) ya Segu katika karne ya kumi na saba. Hii ilisababishwa na uvunjwaji wa 'nguvu za dola ya Kiislamu' na pia kuanguka kwa muundo wa mjini wa himaya hiyo.

Maingiliano ya Uislamu na Afrika yalijidhihirisha kuwa mojawapo ya juhudi za kibinadamu zilizofanikiwa sana katika historia ya ulimwengu. Uislamu ulitoa kile kinachoweza kuitwa 'chaguo la jamii'. Maana zake zilitafsiriwa kwa namna tofauti katika nyakati na sehemu tofauti kwenye bara la watu weusi. Masharti yalikuwa magumu: yalihusu kubadili mtazamo, kubadili namna ya kuona na kuiwakilisha dunia, kubadili tabia. Lilikuwa ni jambo la kubadilisha utamaduni wa mtu na ule wa mwingine - karibu na kuwa mtu mwingine kabisa. Licha ya upinzani wa mwanzo, Afrika ya Mediterania ilikubali chaguo la kuwa Waislamu. Ilisilimishwa na kuanza kuarabishwa.

Kwingineko Afrika Uislamu haukupata mazingira mema kihistoria kama yale yaliyoleta mafanikio yake kwa ujumla upande wa mashariki na kaskazini mwa bara hili na Uhispania. Ingawa Uislamu haukuwa umeshinda wala kushika hatamu kikamilifu, jambo ambalo ilibidi Uislamu uliache mikononi mwa wafalme ambao bado walikuwa wamejawa na utamaduni wa Kiafrika- ulipata kiasi kikubwa cha mafanikio ya kidini kusini mwa jangwa na katika Afrika Mashariki. Mnamo karne ya kumi na sita Uislamu ulikuwa bado haujapata jibu la jumla ambalo lingewezesha kujiingiza kwenye jamii za watu weusi na utamaduni zao bila kusababisha matatizo kwenye Nyumba ya Uislamu. Mapumziko yaliyofuata hayakuwa yenye kufaa tena katika kupata ufumbuzi wa aina hiyo. Mwisho, mara nyingi mshikamano wa kijamii ulitokea wakati wa matukio ya kimapinduzi mnamo karne ya kumi na nane na mapema kwenye karne ya kumi na tisa; matukio haya yenyewe, yaliufanya Uislamu uwe ni kielelezo kamili cha maisha ya watu kijamii na kitamaduni katika majimbo kadhaa.

---

# 5

## *Watu wa Sudan: miguro ya watu*

---

### *Tatizo na vyanzo*

Katika hatua ya sasa ya uandikaji wa historia ya Afrika mitaala ya miguro ambayo mwisho wake ulikuwa kuwepo kwa watu wa Sudan haiwezi kuepukika ingawa ni changamani sana.

Katika vitabu vingi vya historia ya Afrika, miguro ya makundi ya watu hupewa nafasi muhimu sana. Ukubwa wa eneo la Sudan ulifanya uwepo uwezekano mkubwa wa miguro ya watu, mawasiliano na mabadilishano, na kuwepo kwa uwezekano mkubwa wa kuingiza athari kutoka nje. Mara nyingi simulizi mapokeo hutumika katika kujaribu kuonyesha uhusiano ulioko kati ya tamaduni za watu wa Sudan na utamaduni wa watu maarufu wa kale.

Nadharia ya Kihami, ambayo ndiyo ilikuwa ikitumika kueleza maendeleo ya tamaduni za Kiafrika katika zama za kale, imetumika sana kama kiunzi cha kulifasiri suala hili. Kwa mujibu wa nadharia hii, Wahami walikuwa ni Waafrika waliotofautiana na watu wengine weusi, kijamia na kilugha. Katika kundi hili la Wahami walikuwamo wakazi wa Sahara, Waberiberi, Watubu na Wafulani. Nadharia ya Kihami huwatofautisha sana Wahamiti wafugaji na wakulima weusi, ikichukulia kwamba hivi ni vikundi viwili mbalimbali. Wahami wanachukuliwa kuwa ndio walioleta maendeleo na mambo yote mapya yaliyopatikana Afrika. Kwa hivyo shughuli za ufugaji wa ng'ombe zinapewa hadhi ya juu kitamaduni. Inasemekana kwamba wanomadi hawa weupe wameleta mambo ya ustaarabu kwa watu weusi waliotulia pahali pamoja.

Waandishi kama Delafosse, Palmer na Urvoy, ambao ndio waliotupatia sehemu kubwa ya maarifa juu ya watu wa Sudan, kwa makusudi kabisa walichukua msimamo huu wa mtawanyiko. Uandikaji wa historia ya Afrika wa kiloo unaanza kuitazama itikadi iliyomo kwenye dhana zinazoambatana na nadharia hii na hivi sasa misingi hiyo inahakikiwa kitaalamu, lakini tafsiri za namna hiyo bado zinatumika katika vitabu vya kiada na kwenye maandishi mengine, ingawa nadharia hizi na athari zake sasa vinasailiwa kwa dhati, bado ni vigumu kupata nadharia mpya ambazo zimekitwa kwenye matokeo ya utafiti.

Matatizo mengine yanatokana na ukweli kwamba hatuna ushahidi na hati za kutosha kutuwezesha kulishughulikia suala hili kwa kina. Kipindi kati ya karne ya saba hadi karne ya kumi na moja aghalabu huwekwa chini ya kichwa cha 'zama za giza'. Pamoja na kupatika hivi karibuni kwa mitaala ya historia ya Afrika, habari tulizonazo kuhusu vipindi vya awali bado si kamili.

Kuingia kwa Afrika Kaskazini katika utamaduni wa kutumia lugha ya Kiarabu kulileta pia ongezeko la habari za kuaminika zaidi kuhusu Afrika kusini mwa Sahara. Wakati tunawiwa vikubwa na wanajiografia na wanahistoria wa Kiarabu kwa mchango wao mkubwa juu ya habari za maeneo haya, hatuwezi kuyafumbia macho matatizo yanayotokana na maelezo yao. Hakuna hata mmoja wa

waandishi hao aliyewahi kutembelea Sudan kabla ya Ibn Battuta (katika karne ya kumi na nne), na wengi wao walikusanya habari zao kutokana na maelezo waliyosikia katika sehemu zilizokuwa mbali na maeneo waliyokuwa wakielezea. Kwa hiyo maelezo yao hayakuwa kamili. Aidha maelezo hayo yanaakisi upendeleo wa kitamaduni wa wasomi wa Kiislamu. Wakati mwingine waandishi waliunganisha habari za vipindi mbalimbali katika kipindi kimoja, na hivyo kuchanganya mfuatano wa kitaribia (kikronolojia). Wanahistoria hawana budi kumaizi matatizo hayo ili waweze kuvitazama vyanzo hivi kwa hadhari itakiwayo. Makusanyo ya vyanzo vya Kiarabu yaliyofanywa na J.M. Cuoq (1975) na N. Levtzion na J.F.P. Hopkins (1981) sasa yamekuwa kazi za kurejelewa na uchunguzi wa vyanzo vya Waarabu bado vinaweza kuwa miangaza muhimu juu ya historia ya Sudan.

Simulizi mapokeo ni uwanja mwingine muhimu wa kutalii. Visakale vya Wagadu, maelezo ya wanatarahi na wanamapokeo kutoka nchi za Mali na Mande, mapokeo ya Songhay, Zarma, Hausa, Fulani na Mossi, pamoja na kazi za akiolojia zinazofanywa kuanzia Mauritania hadi Chad, vinatuwezesha kulitazama somo hili kwa uhakiki na kupanua mawanda ya habari.

Sehemu iliyohusika ni kubwa mno. 'Nchi ya Watu Weusi', yaani Bilad-al-Sudan, inakusanya siyo tu mabonde ya Senegal, Niger na Chad bali pia sehemu za nyika na za msitu zilizo kusini zaidi. Nyaraka kuhusu sehemu hii ni chache mno. Kazi inaendelea huko Kong (Ivory Coast), Begho (Ghana) na Poure (Upper Volta), lakini ukiacha Taruga na Ife huko Nigeria, utaona kwamba kilichopatikana katika sehemu hizi ni kidogo sana ukilinganisha na taarifa zilizopatikana Tischit, Tegdaust na Kumbi Saleh, au katika nchi ya Dogon. Utafiti huu mkubwa katika Sahel kwa kweli unatoa habari muhimu kwa ajili ya kufanyia tathmini upya uhusiano kati ya Sudan na mipaka yake ya Sahara. Hii nayo inatuwezesha kuona ni katika hali zipi watu wa Sudani waliyakalia mazingira yao na vipi walijirekebisha nayo na kujipatia nyenzo za utamaduni.

### *Mpaka wa Kaskazini*

Kwa muda mrefu tumezoa kuyaangalia maeneo ya kusini mwa Sahara kwa kutumia 'miwani ya Uislamu', yaani kuitazama historia yake kwa jicho la jamii ya Kiislamu iliyofanya maskani yake Afrika ya Kaskazini, ambayo ndicho chanzo chetu kikubwa cha nyaraka.

Mwelekeo wa kuchukulia kwamba dhana ya 'Nchi ya Watu Weusi' chanzo chake ni Afrika Kaskazini umeanza zamani sana. Ulianza zama za kale wakati "sehemu ya dunia iliyojulikana", ambayo ilikuwa kando ya bonde la Mediterania, ilionekana kuwa ndiyo sehemu muhimu kijiografia. Hali hii haikubadilika kimsingi wakati wa Uislamu. Matokeo yake ni kuweco hali ya kutolingana kati ya pande mbili, upande mmoja kukiweko maandishi mengi sana kuhusu misafara iliyokuwa ikivuka jangwa la Sahara katika zama za kale na za kati, na upande wa pili kukiweko taarifa zizizokamilika kuhusu watu weusi katika kipindi hichohicho.

Watu wa Sahara na Waberiberi walikuwa muhimu katika miguro ya watu huko Afrika Magharibi. Tangu zama za kabla ya historia andishi watu hawa walijishughulisha na harakati mbalimbali katika eneo la Sahara mpaka kwenye kingo za kusini za jangwa hilo. Mababu zao kutoka Fazzan, yaani Wagaramante, walikuwa ndio kiungo imara kati ya *Jimbo la Afrika* na Nchi ya Watu Weusi katika enzi ya Warumi.

Kwa jumla, maisha yao yalikuwa ya kinomadi, hali ambayo iliwapa uwezo mkubwa wa kwenda hapa na pale na ikawapatia nafasi nzuri zaidi ya kuhusiana na sehemu za kusini, wakisaidiwa sana na ngamia wao. Ndiyo maana Waberiberi hawakujali mfululizo wa tawala za Afrika Kaskazini kuanzia utawala wa Wakariteji mpaka kufikia kutamalaki kwa Waislamu. Upinzani wa Waberiberi

dhidi ya utawala mpya wa Waarabu ulijidhihirisha katika vuguvugu mbalimbali za upinzani lakini zaidi katika namna walivyozishangilia kufuru za Wakhariji<sup>1</sup>.

Miongoni mwa vikundi vya Kiberiberi vya Sahara, Watuaregi, ikiwa ndio jina waliloitwa baadaye, walikuwa na umuhimu maalumu. Eneo la Watuaregi, ikilinganishwa na maeneo mengine ya Waberiberi, lilikuwa karibu zaidi na Nchi ya Watu Weusi. Watuaregi walianzisha miungano mingi na waliikalia sehemu iliyoanzia eneo la Ghadames mpaka kufikilia Niger na mbele zaidi, makazi yao makuu yakiwa katika miinuko ya Hoggar, Aïr na Adrar des Ifoghas. Ingawa waliamini Uislamu, waliahifadhi pia mambo ya kimsingi ya utamaduni wao, kama vile lugha yao, (*tamashegh*), maandishi yao (*tifnagh*) na muundo wao wa kijamii uliokuwa na matabaka ya wapiganaji, ya kidini, ya kitumwa na ya kiufundi na sanaa. Katika maelezo kuhusu asili yao, wanadai walitokana na kizazi kilichofungamana sana na utamaduni wake. Kwa mujibu wa masimulizi yao, Watuaregi wanatokana na Tin Hinan, mwanamke kutoka Tafilatet. Machimbuo yaliyofanyika mwaka 1929 na mwaka 1933 katika jengo la kaburi huko Abalessa, magharibi ya Hoggar, yanathibitisha masimulizi haya. Vifaa vingi vya kuanzia karne ya nne ya enzi ya Ukristo viligunduliwa vilivyoashiria, vilevile, kuwepo kwa njia ya kale baina ya Moroko kusini na Hoggar, ngamia walipotumika. Kianthropolojia, Watuaregi, kwa kweli, ni kama nyumba ya kati baina ya Sahara na Sudani. Watu hawa wanagawika katika makundi mawili: wale wanaoishi Tassili-n-Ajjer na Hoggar kwa upande wa kaskazini na wale walioko kusini, Waawelimidi na Wakelwi wa Aïr ambao wameoana na Wahausa ambao ni watu weusi. Katika hali hii watu weusi wameweza kuathiri utamaduni wa Watuaregi kiasi. Watuaregi hufanya utabiri ujulikanao kama *tachchel'* (yaani chatu), ambapo mtambaachi huyo huulizwa maswali kwa kurogonya. Nyoka pia hujitokeza katika mambo mengi mengine, lakini maana yake ina utata: ana dhima ya kulinda watu, lakini hujitokeza pia katika ndoto kama mbashiri wa mikosi. Habari hizi zikilinganishwa na ngano za Al Bakri na kunasibishwa na Wazafkawa wa Sudan, inaonekana kuwa kuna uhusiano wa kitamaduni baina ya Watuaregi na Ghana.

Kuna watu weusi sehemu ya kati ya Sahara, hasa upande wa magharibi. Watu hao wa magharibi, yaani Waharatini, aghalabu ni miongoni mwa wakazi wa sehemu za chemchem zilizoko kusini mwa Moroko na Mauritania. Suala la asili ya watu hawa bado linatatanisha: wameitwa Waberiberi weusi.

Mitazamo mipya juu ya suala la kutamakani kwa watu katika Sahara zama za kale inatoa picha tofauti. Kuna dalili kwamba wao ni mifano hai ya watu weusi ambao walihama kuelekea kusini tangu zamani sana.

### *Miguro ya watu katika Sahel*

Kwanza tutajaribu kulibainisha eneo ambamo jamii za Kiafrika zilijijenga na kujiunda katika makundi katika kipindi tukizungumziacho. Iko haja ya kutumia habari zilizopatikana kwa kutumia mbinu za kisasa za utafiti kama vile palakiojia, palinolojia na akiolojia kwa madhumuni hayo. Kwa kuchanganya mchango uliopatikana hapa pamoja na habari zipatikanazo kwa urahisi kutoka masimulizi na kutokana na nyaraka za Kiarabu, inawezekana kufikilia nadharia kadha zinazokubalika. Kazi iliyoanyika Mauritania kuhusiana na kipindi cha kabla ya historia andishi na baadaye katika Sahara itatumiwa kama mfano. Maeneo yanayojitokeza zaidi ni Adrar, Tagant na Awkar. Maeneo haya yanahusika moja kwa moja na sehemu ya magharibi ya Nchi ya Watu Weusi

1 Taz. Sura 3 na 10 ya juzuu hili.



na yanatoa matumaini ya kuweza kuyaelewa makundi wakilishi kama yale ya Wafulani na ya wakazi wa Ghana. Imekwisha hakikishwa hivi sasa kwamba ramani ya wakazi wa Sahara ya Kiniolithi ilikuwa tofauti na hali ilivyokuwa kufuatia mabadiliko ya hali ya tabia ya nchi na kuna dalili za kuaminika zinazoonyesha kuweco kwa wakazi wengi weusi waliotamakani. Katika kikwi cha mwanzo cha kipindi cha Ukristo huenda kulikuwa na jamii za wakulima weusi walioishi na pia kuhusiana sana na Walibyko-Waberiberi na baadaye Waberiberi wanomadi. Waberiberi wanomadi waliwafanya watu waanze polepole kuhama kuelekea kusini, yaani kuelekea kwenye makazi ambayo kwa jumla watu weusi wamebaki nayo.

Wafulani wanalikalia eneo kubwa la nyika za Afrika Magharibi, na kuweco kwao katika majimbo kadhaa baina ya Senegal na Kameruni kunalipa umuhimu suala la asili yao na hatua mbalimbali za safari zao. Ikilinganishwa na vikundi vingine, umuhimu wa Wafulani huffilishwa na jinsi wanavyoishi na kuwafanya wafikiriwe kuwa ni jamii isiyo na utulivu ambayo siku zote imo katika 'kuhama'. Hii inaeleza kwa nini wananadharia wa utawanyikaji wa watu waliwaona 'Wafulani kuwa msingi mzuri wa nadharia kadhaa za Kihami. Pahala pa asili ya Wafulani pametafutwa sehemu mbalimbali ndani na nje ya Afrika: wahenga wao labda walikuwa Waberiberi, au Wanubi, au, kwa mujibu wa Delafossa, Wayahudi-Washamu.

Nadharia hizi zote zinaamini kwamba kuanzishwa kwa madola makubwa ya Sudan kumesababishwa hasa na athari kutoka nje zilizochangiwa na jamii za wachungaji kama vile Wafulani. Mitaala iliyopo hivi sasa inaelekea kukubali kwamba Ufulani unatangamana na Afrika Magharibi na ni sehemu muhimu ya jiografia inayohusu binaadamu, maendeleo yake ya kihistoria na utamaduni wake. Kwa upande wa isimu, Kifulfulde, bila ya shaka yoyote kina kijitabaka cha Kiafrika kinachoshabihiana na Kiwolof na Kisereri. Ama kuhusu asili yao, ushahidi unatuelekeza upande wa Mauritania kusini ambapo ndipo Wafulani walipokuwepo katika mwanzo wa enzi ya Ukristo. Mshabaha mkubwa pamoja na athari za lugha ya Kifulfulde umedhihirika katika toponimia (majina ya sehemu) za maeneo ya Brakna na Tagant huko Mauritania. Haya yote yanaonyesha kwamba Wafulani wamezalika kutokana na jamii ya wachunga ng'ombe wa Mauritania katika kikwi cha tatu na cha pili kabla ya enzi ya Ukristo. Katika kipindi tukizungumziacho, walihamia upande wa Bonde la Senegal na wakashiriki katika kuundwa kwa baadhi ya dola kama vile Takrur. Kuweco kwa Wafulani Afrika Magharibi kunajidhihirisha huko Futa Toro katika karne ya kumi na moja, ingawa kuweco kwao hakuelezwi waziwazi kwenye nyaraka za Kiarabu kabla ya al Makrizi na *Tarihi ya Kano* (karne ya kumi na nne mpaka karne ya kumi na tano).

Inafaa sasa kutoa maelezo kuhusu majina ya kimbari yanayoitwa watu walewale, ya *Fulani* na *Tukuloor* (Toucouleur). Wafulani wanajiita kwa jina la Pullo (ikiwa ni mtu mmoja) na Fulbe (ikiwa ni wengi). Kila anayosema lugha yao, iitwayo *Pular* au *Fulfulde*, huitwa *Hal-pularen*. Jina hili la mwisho hutumiwa pia na wakazi wa Futa Toro ambao huitwa *Tukuloor* kwenye nyaraka. Wanazuoni wa wakati wa ukoloni walianza kuwaita wachungaji Wafulbe (Wafulani) halisi na wale wanaokaa kwenye maskani na kutumia lugha ileile walipendekeza waitwe *Tukuloor* na kuwahesabu kama ni watu tofauti. Ingawa vikundi viwili hivi vina mila tofauti, tofauti hizo zinatokana na sababu za kijamii na kiuchumi na hazihusiani na mambo ya kimbari, kiisimu au kitamaduni. Imekuwa kama kudra imewadhiki, kwani Wafulbe walipohamia Mashariki kutoka kwenye eneo lao la asili la bonde la Senegal(Futa Toro) waliitwa jina lililokuwa geni kwao.

Sasa inakubalika karibu na watu wote katika zama za historiaandishi kwamba, *Wafulani* walitokea sehemu za Senegal Futa na kwamba kikundi hiki cha Wasenegal, ambacho kilikuwa *jirani* na jamaa zao wa karibu, yaani Wasereri na Wawolof, kichukuliwe kuwa ndicho kiini cha vikundi

vingine, ambavyo lugha yao ilikuwa *Pular* au *Fulfulde*, vilivyosambaa na kuhamia mashariki na kusini.

Suala la asili ya Wafulani na miguro yao ni muhimu katika historia ya watu wa Afrika Magharibi, kwani linaathiri vikundi vyote vya Sudani ya magharibi na kati. Lakini vipengee vingine vya mahusiano kati ya Wafulani na vikundi hivi, hasa vikundi vya Wawolof, Wasereri, Wasoninke na Wamand na pia ufalme wa kale wa Ghana vinahitaji kuchunguzwa zaidi. Kuanzishwa kwa Ghana, kama ilivyo asili ya Wafulani, kumetafsiriwa katika mtazamo wa kutawanyika kwa watu kwa kutumia misingi ya maelezo ya waandishi wa tarihi; Delafosse anasema kwamba Ghana ilianzishwa na Wapalestina wa Shamu waliokuja kwa Wasoninke wa Awkar kutokea Sirenaika. Wageni hawa wanafikiwa kuwa ndio waliowazaa Wafulani pia, na wanasemekana kuwa walianzisha dola yenye nguvu ya Ghana katika karne ya tatu ya enzi ya Ukristo. Karibu na mwisho wa karne ya nane Wasoninke weusi, wakiwa chini ya mfalme wao wa kwanza (*tunka*), Kaya Maghan Cisse, wanasemekana waliwarejesha nyuma watu weupe kuelekea sehemu za Tagant, Gorgol na Futa.

Sasa inaelekea imekwishahitishwa kwamba wengi katika wakazi wa kiniolithi wa Sahara walikuwa watu weusi ambao dalili za kuwepo kwao zinaweza kuonekana mpaka sehemu za Adrar. Kutokana na kubadilika kwa tabia ya nchi na kuwa kavu zaidi, wakazi weupe (*Walibyko-Waberiberi*), Waberiberi wa Libya, walihamia kusini, lakini wakapambana na jamii za wakulima weusi waliojizatiti kama vile Wadhar-Tishit, ambao ndio wazazi wa Wasoninke wa Ghana. Sehemu za

kujihami za Wadhar-Tishit zinaonyesha kwamba watu weusi, kwa kweli, walikwishajitayarisha dhidi ya kuingiliwa na vikundi vya wanomadi. Tukizingatia haya yote inawezekana kuwa kuanzishwa kwa dola madhubuti kama la Ghana kulitokea katika kikwi cha kwanza kabla ya enzi ya Ukristo na inawezekana kwamba ile nadharia tete kwamba kulikuwa na awamu ya Chebka baina ya mwaka 1000 na mwaka 900 kabla ya enzi ya Ukristo ni nadharia inayoweza kuaminika.

Nadharia tete kuhusu watu weusi wa Ghana na makazi yao ya mwanzo katika Sahara ya kiniolithi kwenye eneo lilioko kaskazini zaidi kuliko Ghana ya leo si nadharia tete za ovyo hasa kwa vile kuendelea kuonekana kwa 'masalia' yanayoanzia tangu wakati wa Waarabu mpaka enzi zetu kunachangia katika kuzifanya ziaminike. Maandishi ya Kiarabu na masimulizi vinaonyesha kwamba katika zama za historia watu weusi walilikalia eneo lilioko kaskazini zaidi kuliko eneo wanalolikalia hivi sasa. Waliyadhibiti maeneo ya Tagant, Awkar, Hodh (Hawd), Tiris na Adrar. Uchambuzi wa maandishi na masimulizi haya unatuwezesha kufikiria kwamba makazi ya Wasoninke yalikuwa Tagant na Hodh na ya wazazi wa Wasereri na Wafulani yalikuwa katika sehemu nyingine za Mauritania ya leo. Vikundi hivi viwili vya mwisho hapo awali vilishi pamoja Mauritania kusini na baadaye huko Futa Toro. Wakati Wafulani walibakia kwenye bonde la Senegal, Wasereri walihamia kusini zaidi kuelekea eneo wanalolikalia hivi sasa huko Sine na Salum.

Mfarakano na mapigano makali na ya kikatili yaliyokuwepo baina ya wanomadi wa Kiberiberi na watu weusi waliokaa maskanini yalipewa msisitizo usiostahili. Ingawa hatuwezi kukataa kwamba vikundi viwili hivi vilipambana, tusisahau kwamba mahitaji muhimu ya kiuchumi na kisiasa yaliwafanya waishi pamoja na kushirikiana. Ndiyo maana si sahihi tena kuyatazama mahusiano baina ya watu weupe na watu weusi wa Sahel kwa kufikiria mapambano ya kijamia na ya kidini tu.

Haitoshi kusema kwamba kutawanyika kwa Wasoninke kumesababishwa na shinikizo la Waberiberi, na hasa Wamoravi; kulikuwa na sababu nyingi nyingine: hasa mabadiliko ya tabia ya nchi. Makazi ya asili ya Wagadu, yanayotajwa katika hadithi ya kale ya Soninke, yalikuwa katika jimbo lenye mabadilikobadiliko ya tabia ya nchi ingawa yalikuwa katika sehemu inayofaa



kibiashara. Hadithi ya Wagadu inatueleza kwamba Wagadu walikimbilia upande wa kusini baada ya kutokea ukame ulioendelea kwa muda wa miaka saba. Maafa haya yaliyotokana na mabadiliko ya tabia ya nchi ambayo yanatukumbusha ukame wa miaka ya 1970, yanaonekana kuwa ndiyo sababu kubwa ya kutawanyika kwa Wasoninke. Kuhama kwao kuliwapeleka kila mahala kauka Sudan ya magharibi, kuanzia Gambia na kufikia sehemu za mbali za Songhay lakini kikundi kimoja kikubwa kilibakia katika makazi yao ya asili huko Awkar na Hodh, ambapo walianzisha dola yao ya mwanzo, yaani Ghana ya kale. Kuhama huko kwa Wasonike kulichukua karne kadhaa.

### *Kuibuka kwa Tawala za Kisudan: mfano wa Ghana*

Katika kikwi cha kwanza cha enzi ya Ukristo mfululizo wa jamii zilizostaarabika ulijitokeza huko Sudan ya kati na ya magharibi, na jamii hizi ziliendelea mpaka zikawa dola halisi. Baadhi yake, kama vile Kanem au Ghana, zilikuwa na nguvu sana; nyingine ndogondogo kama zile za Hausa, Songhay na Takrur, zilikuwa katika hali ya kuundwa. Waislamu walipofika Sudan katika karne za kwanza za Uislamu walijikuta miongoni mwa makundi haya na ilibidi wafanye makubahiano nao.

Ingawa kuna mapengo katika maarifa tuliyonayo kuhusu hatua zilizopitiwa hadi kufikia kuundwa kwa madola haya, bado tunaweza kuzifuata hatua hizo kijumla kwa kuangalia vikundi vilivyoanzisha Ghana na Kanem<sup>2</sup>.

Milki ya Ghana iliundwa na makabila mbalimbali: watu wa jamii kubwa ya Mande walijitawanya kutoka nchi za kusini zenye misitu mpaka kufikia Sahel inayoungana na Sahara. Ufalme wa Ghana ulikuwa katika sehemu ya kaskazini ukikaliwa na Wasoninke amhao walikuwa na mawasiliano na wanomadi weupe wa Sahara. Mapokeo simulizi yaliyokusanywa Timbuktu kiasi cha miaka elfu baada ya kuanzishwa kwa Ghana yanaeleza kwamba ukoo wa mwanzo ulioitawala nchi ile ulikuwa wa watu weupe.

Mtindo wa mara kwa mara wa masimulizi yanayotokana na jamii za Kisudan kujinasibisha na wahenga weupe ni jambo la kushangaza na husababisha kuwepo maswali kuhusu asili ya madola ya huko Sudan. Lakini tarehe za maelezo haya ambazo ni za wakati wa baadaye kabisa na hali ya jamii za watu weusi zilizotoa maelezo haya zinatoa jawabu kidogo ya swali hili: maelezo haya yanarudisha nyuma kiwakati taarifa ambazo kwa kweli ni za wakati ule ule ambapo jamii hizi za baadaye ziliishi.

Kuna mtindo uliozagaa miongoni mwa Waislamu wa kuzinasibisha tabaka au familia tawala na Mturne au masahaba wake na kwa hivyo, kuyapa madaraka yao nguvu za kisharia. Lakini waandishi wa Kiarabu wa kabla ya kati ya karne ya kumi na mbili hawazungunzii nasabatawala zenye asili ya watu weupe zilizotawala Sudan, iwe Ghana, Takrur au Songhay. Al-Bakri, ambaye ndiye anayetupa taarifa nyingi juu ya Ghana ya karne ya kumi na moja, anaondoa wasiwasi wote juu ya suala hili: Ghana ilitawaliwa na mfalme mweusi aliyekuwa haamini mojawapo kati ya dini kubwa za dunia. Haikuwa mpaka wakati wa al-Idrisi ndipo ile dhana kuhusu asili ya watu weupe ilipoendelezwa; kwa hivyo dhana hii inatangamana na kuenea kwa Uislamu katika Sudan.

Dola za Sudan ziliundwa na watu weusi wenyewe. Watu hawa walikuwa na uhusiano changamano na majirani zao wenye asili ya Kiberiberi. Bila ya shaka wakulima weusi kwanza walirudi nyuma kutokana na kusukumwa na wachungaji wanomadi na kufanya maskani yao kauka maeneo ya Sahel yasiyokuwa na shida sana lakini baadaye walijiunda upya ili waweze kuzipinga nguvu kama hizo. Wasudan walijipatia miongoni mwao nyenzo za kisiasa na kijamii zilizohitajika kuyakabili matishio kutoka kaskazini. Ingawa dola lenye nguvu la Ghana katika kilele cha nguvu

2 Kuhusu kuanzishwa kwa Kanem taz. Sura 15 ya juzuu hili.

zake liliishi bega kwa bega na dola ya Kiberiberi la Awdaghust, baadaye lilishambuliwa mara kwa mara na Wamoravi. Hata kama hali ya mvutano ilikuwepo baina ya Waberiberi na watu weusi, hali hiyo haikusababisha Waberiberi kuyateka madola za Kisudani kwa vile madola haya yalikuwa yameundwa kwa misingi madhubuti.

Kuzaliwa na kuendelea kwa madola ya Sudan katika wakati tunaouzingatia kulitokana na utumiaji wa vifaa na mbinu maalum ambazo ziliwawezesha walioyamiliki kuvitawala vikundi vidogo vidogo vya wakulima na wachungaji wa Sahel. Mambo mawili yanaonyesha yalikuwa muhimu katika suala hili: kumiliki chuma na utumiaji wa farasi na ngamia.

Baadhi ya uchunguzi uliofanywa kuhusu madini katika Afrika ya watu weusi umeonyesha uhusiano kati ya kuwepo kwa chuma na kuundwa kwa madola makubwa ya Kisudan. Mbali ya umuhimu wake kwa ajili ya kuwinda na kulima, chuma ni muhimu katika kuleta nguvu za kijeshi, humpatia anayekimiliki uwezo mkubwa wa kifundi juu ya wengine. Kwa upande wa Sudan, jeshi lilikuwa muhimu katika kuundwa kwa madola kama yale ya Kanem na Ghana. Wataalamu wanazidi kuvutiwa na masimulizi yanayohusu chuma na wahunzi, ambao huwa ni kikundi cha watu wenye madaraka kwa namna mbalimbali.

Kama ilivyokwisha semwa mara nyingi, kuna uhusiano wa karibu kati ya kuwepo kwa chuma na utumiaji wa farasi, kwa sababu vyote viwili hivi vimehusishwa na kuundwa kwa dola kubwa za Sudan. Inajulikana kwamba kulikuwa na farasi huko Sahara katika nusu ya pili ya kikwi cha pili na katika kikwi cha karne za kwanza za mwisho kabla ya enzi ya Ukristo. Hata hivyo farasi walifuata miguro ya makundi ya watu; farasi wa Kiberiberi walipatikana sehemu za magharibi na sehemu za Dongola huko kusini magharibi. Farasi wa Kiberiberi walitumika Afrika Magharibi sehemu za Hodh na Sahel mpaka Jerma. Lakini tangu mwanzo wa enzi ya Ukristo, nafasi ya farasi ilichukuliwa na ngamia, mnyama anayeweza kuvumilia zaidi hali ngumu za jangwani, kwa ajili ya misafara ya kuvuka jangwa. Ngamia alichukua nafasi kubwa katika kuanzishwa kwa utawala wa Sudan kutoka Takrur mpaka Kanem<sup>3</sup>.

Utafiti mwingi umefanyika juu ya biashara baina ya watu wa Sudan na wenzao wa kaskazini, kwa kiwango cha kuathiri vibaya suala la biashara ya ndani miongoni mwa jamii za watu weusi wenyewe. Kasoro hii inadhihirika zaidi katika suala la uhusiano baina ya dola za Sahel na nchi zilioko savana na zilizoko sehemu za msitu. Hata hivyo, tunaweza kuchambua na kuona nafasi ya watu weusi katika uwiano wa mamlaka ulioletwa na mawasiliano baina ya Waberiberi na watu wa Maghrib na watu weusi wa Sudan kwa kuangalia mahusiano yalisababishwa na safari za kuvuka jangwa la Sahara. Fikra inayojitokeza sasa ni kwamba hali hii ilizifanya nchi zilizokuwa kusini mwa Sahara zinyonywe sana na madola ya kaskazini zilizokuwa na zana bora zaidi.

Suala linalojitokeza ni kwamba madola ya Sudan yalifanya nini katika hali hii, tukikumbuka kuwa mambo mengi yaliwasaidia watu wa kaskazini kuendeleza maslahi yao na kwa vile hali ilizidi kuwapendelea wao. Shughuli za madola ya watu weusi zinaweza kusngaliwa katika daraja tatu: kuongezeka kwa madaraka yao, udhibiti kamili wa sehemu iliyokuwa chini ya mamlaka yao na kuzingatia sera zinazoendana na maslahi ya watu wao.

Maelezo ya al-Bakri kuhusu wafalme wa Ghana na Kaw-Kaw (Gao) yanatoa mfululizo wa habari unaonyesha vipi ufalme katika tawala zote mbili hizi ulitukuzwa ili kuwafanya watu waushimu. Mfalme wa Ghana alitofautishwa na watu wengine kwa vazi maalum: yeye tu na mrithi wa ufalme ndio waliovaa nguo zilizoshonwa, pia alivaa kofia na kilemba vilivyonakishiwa, vidani na vikuku. Mfalme alifanya baraza maslumu kwa ajili ya kuhukumu kesi kwa kufuata taratibu

3 Taz. Sura 14 ya juzuu hili.

maalumu zilizoonyesha mbwembwe, zilizoelezwa kwa urefu na uwazi na Al-Bakri. Al-Bakri alieleza jambo muhimu sana kuhusu dini: raia wa mfalme walijilaza kifudufudi alipotokea mfalme pamoja na kujirushia udongo vichwani mwao. Mwishowe, sherehe za fahari kubwa zilizofanywa kwa ajili ya mazishi ya mfalme zinaelezwa: ile mila ya Kiafrika halisi ya kuwazika watumishi pamoja na mfalme, mihanga na pombe anazopewa, miti mitakatifu inayotoa vivuli kwa ajili ya makaburi ya wafalme, na utukufu wake — haya yote yalichangia katika kuufanya ufalme uwe chombo kitakatifu kinachostahiki kuenziwa.

Kuhusu mfalme wa Kaw-Kaw (Gao), al-Bakri anaeleza kwamba kula kwake chakula kuliambatana na tambiko maalum: wanawake huचेza kufuatia mdundo wa ngoma, shughuli zote mjini husitishwa na kulikuwa na tangazo la hadhara la kumalizika kwa kula mfalme kwa kelele na chereko.

Ufalme wenye sifa ya utakatifu ulikuwa kama ndio alama maalumu ya utamaduni wa madola makubwa ya watu weusi ya Sudan hasa katika enzi ya Kiislamu<sup>4</sup>. Asasi hii inajitokeza kama ni kitu cha kienyeji; ni jambo lenye uzito kwamba wanajiografia wa Kiarabu, kwa mfano, hawaelezei mambo yalikuwaje kwa mtawala aliyesilimishwa kama vile mtawala wa Takrur. Asasi kama hiyo inaweza pia kuchukuliwa katika jamii hizi kama ni chombo madhubuti cha kutawalia nchi zao, hasa kwa upande wa falme zinazotawala eneo kubwa sana kama vile Gao na Ghana.

Ingawa wafalme wa Sudan walikuwa na mamlaka na madaraka ndani ya madola yao ambazo waliyatawala kwa njia madhubuti kwa kutumia asasi zinazofaa, walihusika pia na mambo ya nchi nyingine. Mahusiano ya Ghana na Waberiberi walioitawala Awdaghust tangu ilipoanzishwa na Walamtuna katika karne ya tisa yanaweza kufasiriwa kwa msingi huu. Watawala wa Ghana walitanua mipaka yao pande zote kuanzia mwisho wa karne ya nane na kuendelea. Kuweko kwa kituo cha biashara cha Kiberiberi sehemu ya mwisho ya ukingo wa kusini wa jangwa kungeweza kusababisha kuweko kwa biashara na sehemu za kaskazini, na tukitazama hivi tutaona sababu ya kuweko kwa mji wa Awdaghust. Kwa vyo vyote vile shughuli hizi za biashara zilibidi zitendeke katika mipaka inayolingana na utawala wa Ghana. Ilitosha wao kuwa madalali wa kiungo cha kati katika misafara ambayo kituo chake hasa cha kusini lazima kilikuwa Ghana. Kuongezeka kwa madai yao na kuzidi kwa nguvu za Waberiberi huko Awdaghust kulikuwa tishio kwa Ghana, ambayo ilifikia kilele cha madaraka yake katika karne ya kumi na ya kumi na moja. Hii inatuonyesha kwa nini Awdaghust ilitakwa mwishoni mwa karne ya kumi na kuwekwa kwa gavana wa Kisoninke. Utawala wa Kisoninke unaonekana ulitekeleza makusudio ya utawala huo ukamilifu, kwani watu weusi waliyadhibiti mambo huko Awdaghust mpaka ilipoangushwa na Wamoravi katika mwaka 1055.

Kudhibiti hali ya kisiasa kwa Wasoninke hakukuweza kutengwa na kudhibiti kwao kikweli kweli kwa sekta ya uchumi kwenye eneo lote lililokuwa chini ya mamlaka yao. Moja kati ya shuruti muhimu kwa mamlaka haya ni kule kuweza kupatikana taarifa kuhusu msingi wa neema yao. Watawala wa Ghana walidhibiti sawa sawa jambo hili, hasa kuhusu pahala ilipopatikana dhahabu na jinsi ya kuipata dhahabu hiyo.

Mtawala wa Ghana, katika juhudi zake za kuzidhibiti sehemu zinazoanzia biashara huko Sahara kusini alitumia sera madhubuti: alitoza ushuru maalumu wakati bidhaa zilipoingia au kutoka nchini mwake. Wafanyabiashara ilibidi kuilipia chumvi mara mbili: dinari moja wanapoleta na dinari mbili wanapoitoe nje. Kwa hivyo Ghana ilikuwa ndicho kitovu cha usambazaji wa chumvi, ambayo ilikuwa ni zao muhimu sana katika Afrika kusini mwa Sahara. Kwa mujibu wa al Bakri, mfalme wa

4 Kuhusu ufalme 'mtakatifu' taz. Sura 28 ya juzuu hili.

Ghana alijiwekea mwenyewe madonge yote ya dhahabu yaliyochimbwa ili kukwepa kuanguka kwa bei ya dhahabu. Kutokana na kuzielewa kwake vyema harakati za uchumi ambazo kituo chake kilikuwa Ghana, aliazimia kudhibiti mikononi mwake pekee bidhaa muhimu kama dhahabu. Kwa hivyo ulimwengu wa watu weusi uliupanga uchumi wao wa kibiashara ili uweze kupambana na nguvu za wale waliotoa chumvi, kwa vile chumvi ikitumika kubadilishwa na dhahabu.

Kwa hali hiyo, haiyumkini kuwa biashara pamoja na mfumo mzima wa mahadilishano ya kiuchumi unaotokana nayo umeletwa kwa Waghana weusi na Waberiberi, kama inavyosemekana wakati mwingine. Inasemekana kwamba Waberiberi siyo tu ndio waliioleta fikra za biashara hii bali pia walibuni mbinu za biashara hii (pamoja na biashara ya watumwa) na ndio waliosababisha kuundwa kwa dola la Ghana. Udhhibiti wa sekta za biashara uliofanywa na wawakilishi wa Sultani unaonyesha kwamba dhana hii si ya kweli. Wafalme wa Kisudani walionyesha maarifa makubwa ya kisiasa katika uhusiano wao na ulimwengu wa Kiislamu pamoja na utamaduni wa wenzao waliokuwa kaskazini ambao walikutana nao kwa shughuli mbalimbali. Wafalme hawa waliutumia kwa maslahi yao wenyewe ule ujuzi wa Waislamu waliokuwa wakizizuru nchi zao mara kwa mara. Kwa mujibu wa al-Bakri, mfalme wa Ghana alichagua wakalimani, mhazini na mawaziri wake miongoni mwa Waislamu. Kwa hivyo, alitarajia kuwepo ufanisi katika utekelezaji kwa kuwakabidhi Waislamu wenye elimu baadhi ya sekta za utawala wake. Kwa upande wake, alijaribu kuanzisha hali ya kuwawezesha Waislamu kutekeleza ibada zao. Ghana, kama Gao, ilikuwa na mji ambapo Waislamu waliishi jirani na mji wa mfalme wenye misikiti kumi na miwili, yote ikiwa na maimamu, waadhini na mashekhe wake. Wanasharia na wataalamu pia waliishi hapa. Waislamu hawakulazimika kufuata mila zisizolingana na imani zao za kidini.

Kwa kawaida mtawala wa Gao alitakiwa awe Mwislamu. Vile vile kati ya zana za madaraka ya ufalme alizokabidhiwa wakati wa kutawazwa, mbali ya lakiri, upanga, na Kuran, alipewa pia, kwa mujibu wa al-Bakri, 'hidaya kutoka kwa Amiri wa waumini'. Lakini ukweli kwamba wafalme wote wawili waliwatawala watu ambao waliendelea na dini zao za jadi bila ya pingamizi unaleta tatizo kuhusu uhusiano kati ya Sudani na ulimwengu wa Kiislamu mwanzoni mwa kipindi cha kuenea kwa Uislam.<sup>5</sup>


## *Hitimisho*

Awali ya yote, mitalaa ya miguro ya watu inahitaji kuzifanyia tathmini upya dhana zilizozagaa kuhusu 'kuhamahama' kwa watu weusi kwa masafa marefu sana. Kuhama kwa watu wa Sudani kabla ya karne ya kumi na moja hakuonyeshi vurugu ya watu wanaohamahama katika maeneo makubwa.

Watu weusi, ambao ndio waliokuwa wakazi wengi wa Sahara, ilibidi wahamie upande wa kusini kuelekea Sahel kutafuta mazingira yanayofaa kwa kilimo. Waliviachia ardhi zao vikundi vya wachungaji wanomadi ambao walikuwa na uwezo wa kujirekebisha na hali mpya. Wahamiaji hawa walivikuta vikundi vingine vya watu weusi ambavyo walishirikiana navyo ili waweze kupambana na matishio kutoka kaskazini. Jambo hili lilitoa nguvu katika kukua kwa vikundi vya kijamii na kisiasa vya ukubwa mbalimbali vilivyojitawanya tangu Kanem huko mashariki mpaka Takrur upande wa magharibi katika kipindi kilichotangulia kufika kwa Uislam huko Sudan.

Waislamu walipofika Sudan walijikuta wamekabiliwa na mfululizo wa madola, baadhi yake yakiwa yameshajizatiti, mengine yakiwa bado yanaundwa. Ufalme wenye nguvu wa Kisoninke wa


5 Taz. Sura 3 na 4 ya juzuu hili.



5.2 Msikiti wa Tegdaoust/Awdahust, baada ya uchimbuzi na kazi ya kuhifadhi kuta zake. Ukuta wa kiba unaelekes kusini-kusini magharibi. (Taasisi ya Uchunguzi wa Kisayansi ya Mauritania, Nouakchott)

Ghana ulikitawala kikundi kikubwa cha Wamande katika eneo lililokuwa baina ya Senegal na Niger, wakati kitovu cha ufalme uliojulikana baadaye kama ufalme wa Songhay kilikuwa ndio kinaanza kutokeza katika sehemu ya mashariki ya ghuba ya Niger. Ufalme huo ulidhibiti misafara katika mto huo na njia iliyoiunga Niger na Afrika Kaskazini kupitia Adrar des Ifoghas na Hoggar.

Kipindi kuanzia karne ya nane mpaka ya kumi na moja kilikuwa muhimu kwa watu wa Sudan. Kutokana na taratibu madhubuti za utawala ulioongozwa na Serikali kuu ya kifalme, waliweza kutambua umuhimu wa kufanya biashara na maeneo ya Afrika yaliyoko Mediterania na Sahara. Lakini jambo lililowashughulisha wakati wote ni kuweza kubakisha mikononi mwao shughuli za biashara ili waweze kuwazuia watu wa kati kutoka Sahara kudhibiti biashara na chanzo cha ustawi wao. Walipohisi kutakuwa na manufaa ya kitamaduni na kiuchumi kwa kuwepo wenzao kutoka kaskazini, waliyaruhusu vya kutosha madai yao ya kidini mpaka wakafikia kusilimu na wakati ulcule kubaki katika misingi ya dini zao za jadi. Kwa kufanya hivyo, viongozi wa Kisudan, na zaidi wale wa Kighana, waliweza kuhimili mashindano ya majirani zao, Waasanhaja, ambao walikuwa sehemu ya mguro wa Wamoravi katika karne ya kumi na moja. Jambo hilo lilizuia kuanguka kwao ingawa walivamiwa na Wameravi na kudhoofika kwa muda fulani. Kwa hivyo madola ya watu weusi yalifauhi kulinda utu wao na kuweka misingi ya ustaarabu wa kudumu ambao maendeleo yake ya baadaye yalijitokeza huko Mali, na katika dola la Songhay na madola ya miji ya Wahausa.



## Wabantu na kuenea kwao

### Familia ya Lugha za Kibantu

Karibu watu wote wanaoishi katika theluthi moja ya kusini ya Bara la Afrika, kutoka pwani ya Kameruni na Nigeria, upande wa magharibi, hadi ukanda wa pwani ya Somalia na Kenya, upande wa mashariki, na kuelekea upande wa kusini hadi Port Elizabeth, wanazungunza kundi la lugha zinazohusiana sana ambazo zinajulikana kama lugha za Kibantu.

Familia ya lugha za Kibantu ina zaidi ya lugha mia nne, zote zikitokana na lugha ya nasaba moja inayojulikana kama 'Kibantu mama'. Huu ni ukweli uliothibitishwa dhahiri katika misingi ya mifanano ya kiliksika na kisarufi ambayo haiwezi kuelezewa kwa kubahatisha tu au kukopa. Lazima kuwe na asilimia kubalifu ya mfanano. Kwa mfano chukua neno lenye maana ya 'watu' katika lugha zifuatazo:

|         |                |           |                |             |                 |
|---------|----------------|-----------|----------------|-------------|-----------------|
| Kiduala | : <i>bato</i>  | Kimongo   | : <i>banto</i> | Kinyarwanda | : <i>abantu</i> |
| Kifang  | : <i>bot</i>   | Kibusbong | : <i>baat</i>  | Kishona     | : <i>vanhu</i>  |
| Kitio   | : <i>baaru</i> | Kiluba    | : <i>bantu</i> | Kiherero    | : <i>abandu</i> |
| Kikongo | : <i>bantu</i> |           |                |             |                 |

Inawezeka kuonekana kuwa maneno haya yote yanatokana na umbo lililojengwa na mzizi \**-ntu* na kiambishi awali \**ba-*, kinachonyesha wingi. Zaidi ya hayo, tofauti baina ya lugha ni za kawaida kama inavyoweza kuonekana kutoka kwenye milinganisho mingine. Ulinganifu pia unaweza kupatikana katika mfumo mzima wa kisarufi wa lugha za Kibantu. Katika mfano uliotolewa hapo juu, kiambishi awali kinatawala upatanisho wa kisarufi na cheneyewe (kiambishi) huwa katika ngeli maalum ya viambishi awali. Kiambishi awali cha umoja kinachofanana nacho ni \**mu-*, ambacho kikiunganishwa na mzizi, kinaunda neno lenye maana ya 'mtu'. Mfumo wa vipatanisho, uundaji wa vivumishi, aina zote za viwakilishi, viambishi awali na viambishi kati na namna vipashio hivi vinavyofanya kazi, vyote viunefanana katika lugha za Kibantu kama ilivyo katika muundo wa kisarufi wa lugha za Kirumi zinazotokana na Kilatini. Ushahidi wote huo unaonyesha ukweli kwamba zaidi ya lugha mia nne zilizosambaa kwenye zaidi ya theluthi moja ya eneo la Bara la Afrika zina chimbuko lake katika lugha ya nasaba moja. Matokeo ya kihistoria ya tukio hili kuu yapo wazi.

## *Chanzo na Mgawanyiko wa vikundi mbalimbali vya lugha za Kibantu*

Kadhia iliyotajwa hapo juu ni dhahiri haikuacha kuonekana na, kusema kweli, mabaharia wa kwanza wa Kireno tayari walikwishashangazwa na uhusiano wa kiisimu uliowaunganisha wakazi wa ufalme wa Kongo na wale wa pwani ya Afrika Mashariki.

Tokea wakati ambapo Wilhelm Bleek alipowainisha kwa mara ya kwanza watu waliokuwa wanazungumza lugha ya Kibantu kama kundi moja mnamo mwaka 1862, na kuwapa jina la 'Wabantu', kutokana na muundo wa neno lenye maana ya 'watu', wanazuoni wamevutiwa sana na suala hili la Wabantu na wamejaribu kutoa maelezo kuhusu chanzo na kuenea kwa watu wanaozungumza lugha za Kibantu. Utafiti wa H.H. Johnston uliochapishwa kati ya mwaka 1919 na 1922, ulikuwa ndio jaribio la kwanza la kuonyesha chanzo cha Wabantu na kuonyesha hatua za kuenea kwao. Aliliweka chimbuko la wahenga wa Wabantu huko Bahr-al-Ghazal, karibu na Bahr al-Jebel, mashariki ya Kordofan, upande wa kaskazini, au katika mabonde ya Benue na Chad upande wa magharibi, nyendo zao za mwanzo zikielekea mashariki kwenye mlima Elgon na kutoka pale kuelekea kandokando ya Nyanza (ziwa Viktoria), Tanzania, na msitu wa Kongo (Zaire); na uhamiaji mkubwa wa kwanza kuelekea Afrika ya Kati na Kusini ukiwa unaanzia mnamo miaka 300 kabla ya enzi ya Ukristo.

Nadharia kuu mbili zimetolewa na wanaisimu hivi karibuni kuelezea chanzo cha watu wanaozungumza lugha za Kibantu. Joseph Greenberg alikuwa na mawazo kuwa lazima chanzo chao kilikuwa katika eneo la mtawanyiko mkubwa zaidi wa wazungumzaji wa lugha za Kibantu; na kwa kufuata nadharia hii, alifuatilia chanzo chao hadi katikati ya jimbo la Benue nchini Nigeria.

Hitimisho hili lilikataliwa na mtaalam maarufu wa lugha za Kibantu, Malcom Guthrie, lakini hivi sasa linakubaliwa na wanaisimu wote kuwa ni sahihi. Kwa maoni ya Guthrie, mahali hasa pa chanzo cha 'Kibantu mama' kilikuwa kwenye eneo la mkusanyiko mkubwa wa watu waliokuwa wanazungumza lugha ya Kibantu, kandokando ya makutano ya mto Kongo na Zambezi, chanzo kikuu kikiwa katika jimbo la Shaba la Kongo.

Kuanzia mwaka 1973, makundi matatu ya wanaisimu yaliyokuwa yakifanya kazi kila moja peke yake yamethibitisha kuwa Guthrie hakuwa sahihi. Makundi yote matatu yanatumia mkabala unaofanana (uliojikita kauka uchunguzi wa msamiati) lakini hayatumii data hizo hizo.

Kwa hivyo, ukweli kuwa lugha za Kibantu zilianzia huko magharibi umthibitishwa. Katika mkabala linganishi kuhusu isimu ya kihistoria, jukumu kubwa lililopo ni kujenga 'mti' wa nasabu ambapo mhenga wa familia ndiyo chanzo cha moja kwa moja cha wahenga wa makundi madogomadogo ambayo yenyewe ndiyo yaliyovyaa makundi madogomadogo ya lugha n.k. Hadi sasa, hakuna mtu aliyetoa mapendekezo ya mgawanyo wa kifamilia wa kundi la lugha za Kibantu uliojikita katika ushahidi thabiti wa kutosha kuweza kukubaliwa. Sababu ni kile kinachojulikana kwa baadhi ya wanaisimu kama 'dhana ya ukaribiano', ikiwa na maana ya uazimanaji mkubwa baina ya lugha za Kibantu kuanzia kipindi cha nasaba yao moja hadi leo. Hali hii yenyewe ina umuhimu mkubwa kwa wanahistoria, hasa kwa vile inathibitisha kwamba makundi mbalimbali yanayozungumza lugha za Kibantu muda wote yamebaki kuwa na uhusiano wa karibu na jirani zao na hayajawahi kupata kutengana hasahasa.

Kwa ujumla hivi sasa inakubalika baina ya wanaisimu kwamba kuna makundi makuu mawili ya lugha za Kibantu: kundi la magharibi, ambalo hasa lipo katika majimbo ya misitu ya ikweta, na kundi la mashariki linaloanzia Uganda hadi Afrika Kusini. Lugha za kundi la mashariki zinafanana sana kuliko zile za kundi la magharibi. Hii inamaanisha kuwa kupanuka kwa kundi la mashariki kulianza baadaye na kulifanyika haraka zaidi kuliko kule kwa kundi la magharibi. Kwa upande





6.1 Ueneaji wa Wabantu (J. Vansina)

mwingine wa kipimo cha wakati, inakubalika kwa ujumla kuwa idadi ndogo ya makundi yenye asili moja ya yana mizizi yake katika kipindi cha kiisimu kilichopita hivi karibuni, kwa mfano, kundi la asili ya Kongo na kundi la lugha lenye asili moja lililopo kwenye ukanda wa Maziwa Makuu.

Mapema kabisa mnamo mwaka 1948 Guthric alianza kutumia mfumo "tendaji" wa uainisho, akiyapanga makundi ya lugha zinazokaribiana kijiografia katika kanda za ufano uliojikita kwenye ulinganisho wa data zilizopo. Kategoria hizi zilikuwa za muda tu na zilikusudiwa kutumika kwa majaribio. Lakini zilionekana kuwa zinafaa sana kiasi kwamba bado zinatumika mara kwa mara hivi leo. Kila kanda imepewa herufi kati ya A na T, ikifuatiwa na tarakimu kwa kila kundi dogo na tarakimu ya pili ikisimama badala ya lugha yenyewe. Hivyo, A70 ina maana ya lile kundi la lugha linaloitwa 'KiPahouin' na A74 ina maana ya lugha ya Kifang.

Kwa kuangalia haraka, mfumo huu wa uainishaji unaonekana kuwa hauna thamani kihistoria; na hili linadhihirishwa na jitihada nyingi zaidi zinazofanywa ili kubuni mfumo wa kuaminika wa uainisho wa kihistoria. Hata vikundi vidogovidogo vilivyopewa tarakimu haviwezi kila mara kulinganishwa, na kategoria hizo hazina thamani ya ushahidi wa kihistoria.

Kasoro za kutumia mfumo usio na ushahidi wa kihistoria ni nyingi sana na wanaisimu wanasita kutumia mfumo wa alama au istilahi uliojikita katika data ya asili moja hadi hapo ambapo mgawanyiko wa vikundi vya familia ya Wabantu utakapokuwa umethibitika kikamilifu.

Data iliyopo hivi sasa inahusu nusu tu ya lugha zote za Kibantu, wakati ambapo ili kupata hitimisho lisilopingika, kinachohitajika tu ni alama sahihi za kiisimu, msamiati mpana zaidi na maelezo mafupi kuhusu muundo wa kisarufi wa kila lugha. Kama masharti haya yangetekelezwa ingeliwezekana kuendelea bila wasiwasi. Hivyo mahitaji ya msingi ya kazi ambayo hasa ni kamili ni seti kamilifu za kamusi na sarufi, lakini sehemu kubwa ya urithi wa kiisimu wa watu wanaozungumza lugha za Kibantu bado haujaandikwa.

## *Isimu na Historia*

Ni ukweli usioweza kukataliwa kuwa data za kiisimu zina athari za kihistoria. Dhana ya familia moja ya lugha zilizotapakaa katika eneo kubwa kiasi hicho ni lazima ina umuhimu wa aina fulani kuliko inavyoonekana. Waandishi wote wamechukulia kuwa lugha hiyo ilienea kutokana na uhamaji wa wazungumzaji wake. Pia kuna mwelekeo wa kuweka pamoja au hata kuchanganya lugha, utamaduni na jamia.

Ingawa hapo awali kulikuwa na jumua ya Wabantu wenye kuzungumza lugha ya Kibantu-Mama ambao walikuwa wa jamia maalum iliyokuwa na tabia maalum za maisha, jambo hili bado halijawa wazi sana kwa sababu data zinaonyesha kuwa wakati ambapo kazi kuu ya jumuiya hiyo ilikuwa uvuvi, baadhi ya vikundi vyake huenda badala yake viliishi kwa kilimo. Zaidi ya hayo lugha ndizo tu chanzo chetu pekee cha habari zinazohusu utamaduni wa Wabantu-Mama.

Wazo jingine, ambalo linahusiana na kuenea kwa familia za lugha kwa njia ya uhamaji si kamili sana kama inavyoonekana. Kwa mfano, lugha za Kirumi hazikuenea kwa uhamaji wa watu wengi wa nchi za Kilatini. Vipo vipengee vingi vya kiisimujamii ambavyo vinaweza kusababisha mabadiliko katika maeneo ya lugha kijiografia, kipengee kimojawapo muhimu kikiwa ni kile cha badiliko la lugha. Watu wanaweza kujifunza lugha ya kigeni, wakawa wanafahamu vizuri lugha mbili na kisha wakaiacha lugha yao na kuishikilia lugha ya kigeni. Hivi ndivyo ilivyotokea kwa Wasekyani wa Gabon, ambao wote wanafahamu lugha mbili za Mpongwe na wanaanza kupoteza lugha yao ya asili. Ni vivyohivyo wakazi wa Rasi ya magharibi na Namibia ya kusini ambao wamepoteza lugha za Kikhoi na Kisani na hivi sasa wanazungumza Kiafrikaansi tu. Mabadiliko haya

yanaletwa na nguvu za mahusiano ya kiutamaduni-jamii. Mitendano ya kidemografia pia inachangia katika hali hiyo. Wanorman waliotamalaki Uingereza waliacha kuitumia lugha ya Kifaransa baada ya kusimilishwa kitamaduni na raia wao waliokuwa wengi zaidi. Nguvu za shughuli za kibiashara na za kitamaduni zinaweza pia kuathiri maendeleo. Wasekyani waliichukuwa lugha ya Kimpongwe kwa sababu ilikuwa ni lugha ya kibiashara. Kwa kuhitimisha, inaweza kuonekana kwamba mara nyingi uhusiano wa kibiashara, kisiasa-jamii na hata kidini unaweza kuaababisha kuzalishwa lugha mpya kwa wote, zilizotokana na lugha iliyokuwa na heshima, kama vile Kikoines, Kikrioli na Kisabirs. Kwa kuzingatia kiwango kikubwa cha dhana ya kukutanika kwa lugha za Kibantu, hali kama hii lazima ilitokea zaidi ya mara moja. Katika wakati uliopita wa hivi karibuni lugha za Kilingala, Kiswahili au Kimonokituba zinaweza kutajwa kama lugha za biashara na ambazo zimo katika kundi la lugha za Krioli.

Ili kupata maelezo sahihi zaidi kuhusu kupanuka kwa lugha za Kibantu, wanahistoria lazima waendelee kuzilinganisha lugha hizo kwa kutumia analogia na wakati huo wakizingatia vipengee vyote vya mbinu zinazohusika za kiisimu-jamii. Hawawezi kuchukulia kwamba kila kitu kimetokana na uhamaji. Kwa vyovyote vile, kulingana na wingi wa idadi ya watu kabla ya kipindi chetu, ni kupotosha kuzungumza misingi ya miguro mikubwa ya idadi ya watu. Ubova wa mahali kidemografia au kijamii, kiuchumi, kiutamaduni au nafasi nzuri kisiasa ni mambo ambayo yana uwezekano mkubwa wa kutoa mwanga kuhusu dhana hii. Historia ya kuenea kwa lugha za Kibantu ni ndefu sana na eneo lililoathiriwa ni kubwa mno kiasi kwamba ni lazima ichukuliwe kuwa katika muda fulani au mwingine, vipengee vingi kama siyo vyote tunavyovifahamu kwa kutumia analogia, vingeweza kuwa vinechangia.

Data za kiisimu zina matumizi ya moja kwa moja katika kipengee kimoja tu, nacho ni kile cha kujaribu kuiunda upya jumuiya ya Wabantu-Mama kwa misingi ya kile msamiati wake unachoonyesha. Msamiati wa Kibantu unaoweza kutumika hivi leo unaelezea lile kundi la Kibantu kama lilivyoelezwa kwa ufinyu, yaani 'Wabantu wa jumla' walio karibu nasi kihistoria. Ingawa ni rahisi kuunda upya msamiati huo kwa umbo, si rahisi kufanya hivyo kwa upande wa maana, hasa kwa vile maana hubadilika kadri wakati upitavyo na huenda sasa ikawa imebadilika sana kutoka lugha moja hadi nyingine. Kwa mfano, shina 'kumu' lina maana ya 'tabibu' au hata 'mtabiri' katika sehemu za mashariki na likawa 'chifu' sehemu za magharibi na katika kundi moja la lugha upande wa magharibi (A70's) lina maana ya 'yule aliye tajiri'. Bila ya shaka, maana hizi zinaweza kunasibishwa na tunaweza kufikiria kwamba chifu wa 'Wabantu-Mama' alikuwa tajiri, tabibu na mtabiri. Lakini matokeo yanaweza kudhihirisha kuwa ya bandia kwa namna fulani. Kwa hali hii inabidi tuchague ile maana ya 'kiongozi,' ambayo ni sahihi lakini si ya wazi sana.

Hata hivyo, inaweza kueleweka kutokana na msamiati wa kale kwamba ile jamii iliyokuwa ikitumia lugha ya Kibantu ya jadi ilikuwa ikiotesha viazi vikuu, aina nyingine za vyakula vya mizizi na hata nafaka. Mbuzi alikuwa ndiye mnyama pekee wa kufuga aliyejulikana. Jamii hii iliwinda (hasa ngiri), lakini fani yao maalum ilikuwa uvuvi. Mahusiano ya damu yalikuwa ni msingi muhimu katika muundo wa kijamii, na jamii ilikuwa na mabingwa wake wa fani mbali mbali, viongozi wake na wataalamu wa kidini. Dhana ya wahenga na imani za uchawi zilikuwa zimeshamiri. Hisia fulani zinaweza kujengwa kuhusu tabia za makundi ya watoa wake kwa wapokea wake.<sup>6</sup>

Msamiati huo, ukinasibishwa na taarifa za akiolojia pamoja na ujuzi wa asili ya kijiografia ya jamii hiyo, unaweza kutupatia tarehe ya kuanza kwa upanuzi wa Kibantu. Hapa tunashughulika na jamii ya Enzi ya Mawe ambayo ilijishughulisha na kilimo (kama vile kilimo cha nafaka) lakini iliyokuwa haifahamu teknolojia ya kutumia metali. Dalili hizi zinatowezesha kupunguza kipindi cha Kibantu-Mama kuwa baina ya mwaka 1000 (au hata mapema zaidi) na mwaka 400.

Upanukaji wenyewe ulikuwa ni hatua ndefu sana, hasa kwa vile hata kwenye karne ya kumi na tisa ulikuwa bado haujamalizika kabisa katika Afrika Mashariki. Licha ya hayo, wasafiri wa kwanza wa Kiarabu walirudisha maneno ya Kibantu kutoka mwambao wa Afrika Mashariki. Kwa hivyo mnamo karne ya nane, jamii zinazozungumza Kibantu tayari zilikwishafanya maskani yao kandoni mwa Bahari ya Hindi. Inaonyesha kwamba upanuzi wa Kibantu ulitapaka siyo tu kwenye theluthi moja ya bara la Afrika bali pia ulichukua muda wa miaka elfu mbili mpaka tatu.

### *Isimu na Akiolojia*

Mkondo unaofuatwa na wanazuoni unaeleweka na unaonekana katika namna ambavyo vyanzo vya kupanuka kwa Wabantu vilifikwiwa. Msamiati lazima uchambuliwe kwa kupata taarifa ambazo zinaweza kuthibitishwa kwa kufanyiwa utafiti katika maeneo ya akiolojia. Aidha, japo si kwa ukamilifu sana ushahidi wa kiakiolojia wa uhamaji wa kiasi kikubwa cha watu unaweza kulinganishwa na kile kinachojulikana kuhusu ueneaji wa lugha za Kibantu.

Kinadharia, ushahidi huu ungeweza kutoa jibu, lakini kazi ya kuanzisha upya michakato hiyo si rahisi na wala haiwezi kufanywa kwa haraka. Baadhi ya matatizo yanayoonekana wazi yanaweza kutajwa. Eneo la zamani la Enzi ya Chuma linaweza kuwa na tarehe ya kuanzia miguro ya kwanza ya kupanuka kwa lugha za Kibantu, lakini jambo hilo halimaanishi kuwa, baada ya hapo ni watu waliokuwa wanazungumza lugha za Kibantu tu waliofahamu kuyeyusha chuma. Kuna ushahidi katika Afrika ya Mashariki wa kuenea kwa haraka sana kwa aina ya ufinyanzi vyungu ulioanzia katika kipindi cha awali cha Enzi ya Chuma, na kwa vile sehemu hizo zote zipo katika eneo la kupanuka kwa lugha za Kibantu za Mashariki, matokeo haya nasibu (na ni matokeo nasibu kweli) yamechukuliwa kama ushahidi kuwa haya yalikuwa masalia ya kiakiolojia ya kuenea kwa Wabantu. Kwanza, ugunduzi mdogo sana umepatikana kauka machimbo kwenye sehemu nyingine za Afrika zinazozungumza lugha za Kibantu. Pili, inawezekana pia kusema kuwa kuenea huku kwa kasi kwa matumizi ya chuma kumetokana na wahunzi na wafinyanzi vyungu ambao pengine waliwakilisha sehemu ndogo tu ya idadi ya watu walimokuwa wakiishi.

Lakini kila mara tuzingatie ukweli kwamba akiolojia haiwezi kuthibitisha ni lugha ipi iliyokuwa inazungumzwa na watu waliotengeneza au kutumia vyungu, waliokuwa wanalima vyakula vya nafaka au waliotengeneza zana za chuma, mawe au mifupa iliyogunduliwa katika maeneo hayo. Kwa upande mwingine, data za kisimu na za kiakiolojia zinaweza kulinganishwa, na kama kuna ulinganifu mkubwa basi ushahidi wake pia utakuwa na thamani kubwa.

Yatosha kuzingatia kwamba maeneo ya awali kabisa ya watu waliokuwa wanazungumza lugha za Kibantu bila shaka yanahusishwa na zana zilizoainishwa kama za kineolithi na kwamba maeneo ya Enzi ya Chuma yaliyoko kusini, kati na mashariki mwa Afrika yanaweza kuhusishwa na mabaki yaliyoachwa na wazungumzaji wa lugha za Kibantu.

### *Kuenea kwa Wabantu*

Nadharia mbili zimetolewa kuelezea ueneaji wa Wabantu kutoka kwenye makazi yao ya asili. Mwanaakiolojia Merrick Posnansky, akiandika mnamo mwaka 1962, alipendekeza kuwa uhamaji wa Wabantu kutoka Afrika Magharibi hadi Afrika ya Kati ulihusisha jumua ya wakulima na kuwa uhamaji huo ulipata nguvu baada ya mbinu za kilimo (ulimaji wa migomba na viazi vikuu) zilizoletwa na Waindonesia kati ya miaka - 400 na +200 kuenea kwa watu waliokuwa wanaishi misituni huko Afrika ya Kati. Nadharia nyingine, iliyojikita katika wazo la utamalaki inaonyesha

uhusiano baina ya kuenea kwa Wabantu na kuanza kwa ya Enzi ya Chuma. Utengenezaji wa chuma uliweza kuongeza uzalishaji wa mazao yanayotokana na kilimo kwa kuzifanya zana ziwe bora zaidi na kuwawezesha Wabantu kuwatawala watu katika maeneo waliyoyakalia. C.C. Wrigley anadai kuwa 'Wabantu walikuwa wakazi wachache waliokuwa wakiwinda kwa mikuki, kila mara wakiwawutia wafuasi wapya ... kwa umaarufu wao wa ugavi wa nyama, kila mara wakiyaacha makundi mapya ya wahamaji mpaka nusu ya bara lote la Afrika lilipoweza kutumia chuma na kuzungunza lugha za Kibantu'. Kwa kuzingatia ruwaza ya uhamaji katika sehemu ya pili ya miaka elfu ya sasa, pengine sababu nyingine kubwa zaidi zinaweza kutajwa: njaa, kutafuta hali bora zaidi za maisha katika hali ya kilimo bora na ardhi nzuri ya ufugaji, magonjwa yanayoambukiza haraka, vita na ari ya kutaka kugundua maeneo mengine pia vilitia motisha miguro ya awali ya Wabantu; lakini vipengee hivi vimetiliwa maanani kwa kiasi kidogo sana.

Tukurudi katika upande wa nadharia za wingi wa watu na utamalaki, lazima izingatiwe kuwa uanzishwaji wa kilimo ulikuwa ni mchakato wa polepole na haukubadilisha mara moja shughuli za awali za uwindaji, uchumi wa uokotezaji chakula pembezoni mwa ikweta ya Afrika. Ni dhahiri kuwa, aina hizi mbili za uchumi zilitegemeana, kama ambavyo bado zinategemeana mpaka leo katika sehemu nyingine za Afrika. Hivyo, kuanzishwa kwa shughuli za kilimo kwaichukuliwe kama mgeuko wa ghafla. Ulikuwa ni mchakato wa mabadiliko ambao usingeweza mara moja kusababisha mapinduzi ya kidemografia ya hioyoteleza uhamaji mkubwa wa Wabantu kwa ajili ya kutafuta mahali pa kuishi. Ufuaji chuma ulikibadilisha kilimo hatua kwa hatua kwa sababu ni kiasi kidogo tu cha chuma ambacho mwanzoni kiliweza kupatikana katika Afrika ya Wabantu. Kwa vyovyote vile, teknolojia ya chuma haikukibadilisha kilimo kuwa cha kisasa wakati wa zama za awali za Enzi ya Chuma. Hadi mwanzoni mwa karne ya sasa usafishaji wa mapori na misitu ulifanywa kwa uchomaji moto, na jembe la mti liliweza kutumika hadi karne ya ishirini katika Afrika. Bila shaka, teknolojia ya chuma iliweza kuongeza ubora wa zana za Wabantu katika kipindi hicho, hasa mikuki na mishale yenye ncha za chuma ikiwa ni zana zilizojitokeza zaidi. Lakini zana hizo hazikuonekana kama ni za kufaa zaidi kama zile za mawe au mifupa yenye ncha na mikuki ya miti na marungu, na wala hazikuwawezesha wenye silaha hizo kuonekana kama wana nguvu zaidi.

Kuenea kwa Wabantu hakukuwa ni uhamaji mkubwa wa watu kutoka kwenye eneo moja hadi jingine bali miguro ya idadi ndogo ya watu kutoka kijiji kimoja hadi kingine na wakati mwingine kurudi katika kijiji hichohicho tena; hatua ambayo ilirudiwarudiwa hadi vizazi vilivyofuata vilipofika katika sehemu zote za eneo lililo pembezoni mwa ikweta ya Afrika. Miguro hiyo ilikuwa ikitokea katika pande zote kwa zaidi ya maelfu ya miaka.

Je, leo hii tunaweza kuaema nini kuhusu kuenea kwa Wabantu? Kibantu-Mama kilizungumzwa karibu na mstari-ainishi wa kiekolojia katika mazingira yaliyokuwa na rutuba. Uhamaji wa watu waliozidi, angalau kwa kiwango kidogo sana, pengine ulitokea hapa. Kupenya kwao kwenye msitu labda kulikuwa ni mchakato wa polepole. Mgawanyiko wa lugha za kaskazini-magharibi unaonyesha kuwa walitawanyika katika pande kuu tatu: kwanza kupitia ukingoni mwa bahari kuelekea kusini na kuvuka bahari kuelekea kwenye kisiwa cha Malabo. Katika mguro huu wa kwanza, inawezekana kuwa walifika kwenye lango la mto Gabon. Mguro wa pili ulipita kwa msukumo wa kuambaa pembeni mwa msitu kuelekea mashariki hadi Sangha. Mguro wa tatu ulipitia msituni kutoka vituo mbalimbali ukingoni mwa msitu huo, ama kwa maendeleo ya kawaida ya kuendeleza kilimo au pengine kwa sababu za shughuli za wavuvi katika Sangha.

Mafanikio ya kwanza ya Wabantu yalikuwa ni ya kuyaelewa vyema mazingira ya msitu wa Kongo. Mchakato wa upenyaji ulitokea katika awamu mbili:

- (1) kutoka kaskazini hadi kusini, Wabantu wakiifuata tu mito na tukanda mwembamba wenye udongo wa kitope, na

(2) kuendelea kuharibu msitu kulikofanywa na wakulima wa Kibantu waliokuwa wakisonga mbele kwa mapana.

Hakuna mambo mengi yanayojulikana kuhusu historia ya kilimo au ya utaalumu wa chuma katika eneo la magharibi la Ubuntu-Mama. Impendekezwa kuwa Kongo ya ikweta ilikuwa kituo huru cha maendeleo ya kilimo, maendeleo yaliyotokana na umuhimu mkubwa uliowekwa kwenye viazi vikuu na mafuta ya mawese. Katika kisiwa cha Malabo, maendeleo ya kilimo yaliyojikita katika utengenezaji wa mafuta ya mawese yalianza mnamo karne ya sita na shughuli za kilimo katika eneo pana zaidi la ikweta pengine zilianza katika wakati huohuo. Inasadikiwa kuwa Wabantu walilima viazi vikuu na michikichi lakini hakuna ushahidi wa wazi wa jambo hilo kwani shughuli hizi huacha ushahidi mdogo sana kwa mwanaakiolojia.


Nchini Kongo, kuna mapokeo makuu mawili ya Enzi za Chuma za mwanzo, mapokeo ya Kasai/Stanley Pool na yale ya Shaba/mashariki ya Kivu. Katika eneo la magharibi la Ubuntu-Mama (lile la mapokeo ya Kasai/Stanley Pool) hakuna maeneo yaliyokuwa na matabaka ambayo yamekwisha chunguzwa. Lakini ni mantiki kudhani kuwa ufuaji chuma haukufanyika sehemu hiyo mapema zaidi kuliko katika ukanda wa Shaba/mashariki ya Kivu ambako kulipatikana ukadiriaji umri wa rediokaboni wa karne ya nne kwa upande wa Shaba na wa kikwi cha kwanza cha Enzi ya Ukristo kwa Kivu. Wakati maeneo yenye matabaka ya Shaba yanaonyesha wazi tarehe ya kuanza kwa Enzi ya Chuma, yale ya Kivu hayaonyeshi hivyo, kwani maeneo kama hayo yaliyoko Rwanda na Buhaya (Tanzania) yamepewa tarehe ya zamani kabisa, kati ya miaka 300 hadi 500 kabla ya Enzi ya Ukristo.

Mabadiliko ya kilimo katika eneo la magharibi la ubuntu-mama yalianzia ndani ya eneo hilo lenyewe na hivyo kuhimiza miguro ya watu, ingawaje mazingira ya kiikweta hayaruhusu hali hiyo. Hivyo, hadi kufikia mwishoni mwa kikwi cha kwanza cha Enzi ya Ukristo, kundi la Wabantu wa magharibi labda ndilo lilikuwa imara zaidi kati ya makundi makuu mawili ya Wabantu. Kwa hali yoyote ile Wabantu walikuwa wakitumia chuma katika kikwi chakwanza ya Enzi ya Ukristo. Lakini haielekei kuwa waliweza kuwa wameendeleza matumizi yake kwa kiwango cha kilimarisia kilimo cha mashamba kufikia kiwango cha kusababisha kuongezeka sana kwa watu ambako nako kungesababisha kupanuka kwa eneo lao, au pale ambapo kulikuwa na mbinu mpya za kupigana kwa kiasi cha kuwatia tamaa Wabantu wa magharibi kuanzisha kampeni za kijeshi nje ya eneo lao.


Kutokana na mtawanyiko wa jumla wa makundi ya lugha za Kibantu, lazima kulikuwa na uhamaji mkubwa kuelekea mashariki ukingoni mwa msitu, ukiwachukua watangulizi wa wazungumzaji wa lugha za Kibantu zilizo mashariki hadi kwenye Maziwa Makubwa. Nadharia hii haikutokana wala kuthibitishwa na data nyingine. Kitu ambacho kinawezekana ni kuwepo kwa kundi la lugha za mashariki. Katika hatua hii ya kwanza ueneaji ulichukua nafasi ya wahenga wa lugha zingine zilizokuwa zinazungumzwa na Wabantu wa magharibi, hasa wahenga wa kundi la lugha la misitu ya kati kuelekea kwenye nchi nyingine zilizokuwa mbele ya Ubangi na Kongo. Tukichukulia kuwa uhamaji wa moja kwa moja ulizuiwa kwa kuwepo na kinamasi kikubwa tunaweza kusema njia iliyofuatwa ilikuwa ama ile ya kaskazini, kuelekea kaskazini mwa Dongo, au ya kusini, kuelekea kusini mwa sehemu mto Sangha unapoingilia. Mtawanyiko wa kijiografia wa lugha zilizo katika sehemu hii unaonyesha kuwa njia ya kuelekea kusini ndiyo iliyochaguliwa, na lugha ya awali inawezekana ilizungumzwa kati ya mto Alima na msitu, upande wa kulia wa ukingo wa mto Kongo. Hatimaye, lugha hizi zilienzwa katika sehemu zote za msitu na wavuvi waliojenga kando ya mito, pamoja na wanomadi waliokuwa wakihama kutoka kijiji kimoja hadi kingine.

Eneo hili lililopo kati ya Alima na msitu, lilikuwa ni mchanganyiko wa msitu na mbuga za

6.2 Ufinyanzi wa Enzi ya Awali (Urewe) uliogunduliwa katika eneo la Kabuye, Rwanda. (F. Van Noten, 1983; mchoro na Y. Baele)



6.3 Ujenzi upya wa tanuu la enzi za awali za Chuma katika Rwanda: Nyaruhengeri I. (C. van Grunderbeek, E. Roche, II. Doutreleponi na P. Craddock. Maonyesho ya Kifalme ya Afrika ya Kati, Tervuren, Ubelgiji)



savana, sawa kabisa na eneo lililokuwa limekaliwa na jamii ya Wabantu-Mama. Lakini lugha zilicndelea kukua katika mazingira yenye tofauti kubwa, jambo ambalo lisingewezekana kutokea bila kuingiliwa au angalau kuzuiwa katika miguro ya uhamiaji. Kwa mfano, polepole baadhi ya makundi yaliweza kuyazoea maisha ya mbuga za savana ambazo hazikuwa na maji kama ulivyo uwanda wa Bateke. Kwa upande mwingine, katika upande wa mashariki kulikuwa na maji mengi zaidi na baadhi ya jumuisia zilijizoeza kuishi kwenye sehemu za vinamasi. Lakini lugha nyingi zilizungumzwa na watu ambao walipenda maisha ya msituni, kama wakulima au wavuvi. Baadhi ya lugha nyingine zilizuka katika hatua hii ya pili upande wa kusini na kusini magharibi ukingoni mwa msitu na hatimaye katika mkondo wa chini wa mto Kongo katika sehemu mpya za msitu na mbuga za savana.

Hakuna alama za lugha za wenyeji wa sehemu hii ya ukanda wa magharibi wa lugha za Kibantu. Kwa kuwa Wabantu waliishi vijijini, walikuwa na nafasi kubwa ya kunufaika dhidi ya wenyeji wao ambao walikuwa wawindaji na waokotezaji chakula. Kijiji kilikuwa ni kituo cha eneo zima

lililokizunguka na athari ya lugha yake ilienea kadri eneo hilo lilivyozidi kupanuka katika mipaka yake. Ukweli huu unakubaliana vizuri na nadharia ya ueneaji wa haraka wa lugha uliofanywa na wavuvi katika mito mikuu na pwani ya bahari. Watu hawa walikuwa wakihamahama na inawezekana kuwa waliweza kuyaathiri maisha ya wakulima waliokuwa wakiishi pamoja nao, ama moja kwa moja au kwa biashara ya samaki, vyombo vya ufynyanzi, na chumvi ya bahari kwa kubadilishana na bidhaa zilizotokana na uwindaji au uokotezaji chakula. Kwa kutazama ramani, tunaweza kusema kwa uhakika kuwa jumua za wavuvi ndizo zilizohusika sana na kiwango kikubwa cha lugha ya aina moja katika bonde la kati kwa sababu ya kukutana kwao na wakulima. Kukutana huku kulidhibiti hali ya mtawanyiko wa kilugha na kuelekea katika mkaribiano.

Miguro mingi ya kilugha iliyotokea baadaye ilikuwa katika eneo hilo. Upane wa kaskazini, hasa kati ya mto Ubangi na Kongo, kutoka Bangui hadi mto Uele, kulikuwa na miguro kauka pande mbalimbali. Wakati mwingine lugha za Kibantu ziliweza kuondosha makundi mengine ya kiisimu (kwa mfano kundi la Mba-Mondunga kutoka Lisala hadi Kisangani) na kuchukua nafasi yao; lakini wakati mwingine lugha za Kibantu zilifunika na lugha za Sudan ya Kati, hasa kauka Ituri, ambapo kundi kubwa la lugha za Kibantu liliathiriwa na muundo wa kisarufi wa lugha hizo.

Mwanaisimu Christopher Ehret aliubuni nadharia ya kuwa lugha za Kisudan zilienea hadi Kusini mwa Afrika lakini zilimezwa na ueneaji wa Wabantu. Katika maoni yake, Kundi la Kibantu-Mama cha mashariki kuzunguka ukingo wa magharibi wa Ziwa Tanganyika lilitoa jumua tatu zilizofuatana kati ya miaka -600 na -400 ambazo ni za Kilega-Guha, ambao waliikalia Kongo ya mashariki hadi magharibi ya upande wa magharibi wa Bonde la Ufa; kundi la Wabantu kuzunguka ziwa Nyanza (Viktoria) ambalo liliyakalia maeneo ya nchi za Rwanda, Burundi, Uganda kusini na magharibi; kundi la Kituli ambalo baadaye liligawanyika katika makundi mawili ya Wapela na Wapembele; kundi la kwanza likijumuisha wazungumzaji wote wa labaja za Kibantu nchini Kenya na sehemu za Tanzania na lile la pili likijumuisha watu wanaozungumza lugha za Kibantu katika sehemu kubwa ya Malawi, Msumbiji, mashariki mwa Zambia na eneo lote la kusini-mashariki mwa Afrika. Hadi kufikia mwisho wa kikwi cha kwanza kabla ya Enzi ya Ukristo jumua hizi za Wapela na Wapembele zilikwisha jitokeza kama vikundi vilivyotofauti na vizazi vya Wabantu-Mama vya mashariki upande wa magharibi mwa Ziwa Tanganyika, na wakaenea haraka katika karne mbili au tatu za kwanza za kikwi cha kwanza cha Enzi ya Ukristo, hadi mashariki na kusini mwa Afrika. Wazungumzaji wa lugha za Kibantu wa hivi sasa wa maeneo haya wametokana na makundi hayo.

Hakuna mwanaisimu aliyefuatilia nadharia ya Ehret kwa sababu ushahidi ambamo nadharia hiyo imejikita ni mdogo sana. Baadhi ya data za kiakiolojia zilizopo zinaonyesha vipengee fulani vya nadharia ya Ehret, lakini hakuna utafiti wa kiakiolojia uliofanywa katika kipindi cha Enzi ya Mwanzo ya Chuma kauka eneo lililo magharibi mwa Ziwa Tanganyika ambalo, kwa maoni yake, ndilo eneo ambapo kundi la Wabantu-Mama wa mashariki liligawanyika katika makundi mbalimbali. Kwa hivyo basi, bado hatufahamu namna ambavyo lugha za Kibantu ziliweza kushamiri katika eneo la mashariki mwa Afrika. Yalikuwa ni mazingira mapya kabisa, wenyewe walikuwa wamepiga hatua zaidi kuliko makundi yaliyokuwa yanazungumza lugha za Kibantu na bila shaka baadhi yao walikuwa wanazungumza lugha cha Kisudan cha kati, angalau katika sehemu ya eneo lililo kaskazini magharibi.

Taaluma ya akiolojia inatambua kuwa ufundi wa kutumia chuma ulikuwa tayari umekwishapiga hatua katika eneo hilo katika karne za mwisho kabla ya Enzi ya Ukristo na kwamba ufundi huo ulienea kutoka kwenye Maziwa Makuu hadi Transvaal na Natal katika karne chache za mwanzo za kipindi hicho. Kutokana na hayo, mtu anashawishika kuhitimisha kuwa uwezo mkubwa wa kiufundi ndio ulioziwezesha lugha za Kibantu kupata umaarufu katika eneo lote. Kuelekea kusini, faida ya



uwezo mkubwa wa kiufundi ingeweza pia kujumuisha kilimo na ufugaji. Lakini hapa kuna tahadhari. Katika Afrika Mashariki yenyewe, lugha nyingi zinafanana sana kiasi kwamba hakuna mfumo ulio wazi wa kuzigawanya lugha hizo katika makundi madogomadogo isipokuwa tu kwa lugha zilizoko kusini mwa mto Zambezi. Licha ya hayo, ni muhimu kuzingatia kuwa lugha za Kibantu za mashariki zinazungumzwa pia magharibi zaidi, kusini mashariki mwa Kongo na Zambia. Aidha, bado kuna mashaka kuhusu nafasi ya lugha mbalimbali kutoka kusini mwa mto Kongo hadi Namibia. Lugha hizi ziliathiriwa kwa kiasi kikubwa na lugha za Kibantu za mashariki, na katika maeneo ambamo lugha hizo zinazungumzwa, katika sehemu chache sana ambako kumefanyiwa utafiti wa kiakiolojia, hazioani na migawanyiko halisi ya tamaduni katika Enzi ya Mwanzo ya Chuma.

Hivyo bado ingali inawezekana kuliunga mkono wazo la Profesa Ehret kuwa chanzo cha lugha hizi kilikuwa magharibi mwa Ziwa Tanganyika na kisha kuenea upande wa kaskazini na kusini. Inawezekana pia kukielezea chanzo chao kuwa ni sehemu ya kaskazini zaidi au katika sehemu yoyote ya maeneo mengi kandokando ya mto Kasai wa juu au mto Zambezi wa juu.

Katika eneo hilo, mabaki ya lugha zisizo za Kibantu yanaonekana katika lugha za Kibantu zilizo kusini kabisa ambazo zimeazima baadhi ya msamiati na fonolojia zao kutoka katika lugha za Kikhoi na Kisani. Katika Afrika Mashariki, mgawanyo wa lugha kijiografia unaonyesha kuwa ueneaji wao ulijaa matukio. Lugha za Kibantu na nyinginezo zimeingiliana sana, hata hivi karibuni lugha zisizo za Kibantu zimeathiri lugha za Kibantu na kinyume chake. Ueneaji wa Wabantu haukufanyika bila matatizo. Kinyume chake, ni wazi kuwa matatizo yalitokea na kuwa vikwazo vilidumu kwa karne nyingi, vikiathiri sehemu kubwa ya eneo la watu waliokuwa wanazungunza lugha za Kibantu. Iwapo

hivyo ndivyo, ni rahisi kupata mabaki ya lugha hizi nyingine kama ilivyo katika athari ya Kisudan mashariki mwa Kongo.

Mtaala wctu unaishia katika mwaka +1100 wakati Wabantu tayari walikwisha kuikafia sehemu kubwa ya eneo lililo kando ya misitu ya ikweta (eneo ambalo bado wanalikafia hadi leo) na muhimu zaidi wakati ambapo tamaduni zao zimeanza kuchukua tabia maalumu za kikanda.

Katika hatua hii ya utafiti, si rahisi kutoa kauli thabiti kuhusu chanzo cha Wabantu au kwa nini walienea katika mapana na marefu yote ya eneo lililo kando ya misitu ya ikweta.

Kama chanzo chao ni Afrika Magharibi au eneo la Bahr-al-Ghazal la Jamhuri ya Sudan au kwenye eneo linalozunguka mito ya Kongo na Zambezi au katika eneo linalozunguka Maziwa Makuu ya Afrika Mashariki, kuna kipengee kimoja muhimu kilichokwisha dhihirika: Iwe ni chanzo chochote kile kiwacho cha wazungumzaji wa lugha, za Kibantu ni lazima walihama kutoka katika eneo lao la asili na mwishowe waliwaondoa na kuwajumuisha Wakhoisani na pengine makabila ya Kisudan katika maeneo mapana ya pembezoni mwa misitu ya ikweta katika Afrika, zoezi walilolikamilisha ilipofika mwishoni mwa Enzi ya Mwanzo ya Chuma na mwanzoni mwa kikwi cha pili cha Enzi ya Ukristo.

---



## *Misri kuanzia utamalaki wa Waarabu hadi mwisho wa dola ya Wafatimi (1171)*

---

### *Utamalaki*

Waarabu walipoingia Misri walikwishatamalaki eneo kubwa la ardhi katika Shamu na Mesopotamia, wakiwa wamevutiwa na utajiri mkubwa wa vitongoji vyake na idadi kubwa ya watu wenye juhudi. Kutoka nchi hii, Uislamu, ambao ulikuwa na muundo mzuri na uliokuwa umeshinda, ukafika Afrika. Hadi sasa, Misri imekuwa ikiendelea kuwa na nafasi hii muhimu ya kuwa mpatanishi kati ya Mashariki ya Kiarabu na Afrika ya watu weusi.

Amr ibn al-As, jenerali mmojawapo katika kikundi mashuhuri cha majenerali wa Kiarabu wenye kushiriki katika utamalaki wa awali, aliingia Misri akiongoza jeshi la wastani. Baada ya kuteka al-Arish na al-Farama kwa urahisi, alisonga mbele hadi Bilbays na Heliopolis pasi kupata upinzani mkali kutoka Jeshi la Wabizenti. Wabizenti walijikita kauka mji wa ngome wa Babylon, ulioko kwenye sehemu ambapo Mto Nili hutawanyika na kuwa Delta. Baada ya kuzingirwa kwa miezi kadhaa mji wa Babylon ulitekwa kunako Aprili 641; papo hapo majeshi ya Waarabu yakashambulia Fayyum na Delta na kutamalaki vitongoji.

Miezi miwili baada ya Babylon kutekwa, Amr alianza kushambulia mji wa Aleksandria, mji mkuu wa Misri ya Kibizenti ambao ulikuwa mji mkubwa wenye ngome kuu na wenye idadi ya watu laki sita, na mmojawapo kati ya miji mikuu ya Mediterania. Mnamo Septemba 642, Aleksandria ilitekwa na jeshi la Waarabu, na baada ya kusnguka kwa mji huo, utawala wa Wabizenti huko Misri ukamalizika. Mitafaruku ya kichama ambayo iliwigawanya Wagiriki na chuki ya Wakhufu dhidi ya watawala wao kwa sababu za kidini na nyinginezo, ilirahisisha kazi ya wavamizi. Utamalaki wa Waarabu ulikuja wakati ambapo Wamisri walichukia sana mamlaka ya Wabizenti ya Konstantinople na wawakiishi wake katika Aleksandria. Wakhufu hawakutaka kujinasibisha na dola ya Kibizenti ama katika masuala ya dini, ya siasa au ya lugha.

Akiachana na desturi ya kuweka makao makuu ya mamlaka ya kisiasa kauka bandari ya Aleksandria, 'Amr alichagua Babylon, ambayo ilikuwa kati kati ya Delta na Misri ya Kati, kuwa ndio mji mkuu wa jimbo hilo. Msikiti ambao ulikuwa kituo kikuu cha mkusanyiko wa shughuli za kidini na kisiasa, ulithibitisha umoja wa mji mpya, ambao ulijulikana kama Fustat, ya Fustat-Misir.

Mpaka kufikia kipindi cha Wafatimi, Aleksandria ilibaki kuwa mji wenye umuhimu mdogo ambao ulikuwa chini ya utawala na uangalizi wa jimbo, kwa sababu kulikuwa na hatari ya Wabizenti kutua bandarini mwake, na hivyo kuwawezesha kusnzisha kantara (kituo cha kufanyia uvamizi). Ama kwa hakika, katika mwaka 645 kwa muda mfupi manowari za Kibizenti zilitamalaki mji huo na Waislamu waliupata tena kwa taabu.


Muundo wa kifedha uliowekwa huko Misri na Waarabu wakati wa utamalaki haukueleweka vizuri, kwa sababu haikujulikana wazi kama Misri ilikuwa nchi iliyotekwa kwa sababu ya watu wake kusalimu amri pasi kumwaga damu au ilikuwa nchi iliyonyakuliwa kwa nguvu za kijeshi. Katika hali ya kwanza ardhi hiyo ilikuwa mikononi mwa watu waliolima, ambao walitozwa kodi ya vitu, iliyojulikana pia kama *kharaj*, mbali na kodi ya kichwa, ambayo pia ilijulikana kama *jizya*. Katika hali ya utamalaki wa kijeshi, ardhi ilimilikiwa na Waislamu ambao walikuwa na uhuru wa kuwaajiri wakulima waliotamalikiwa na ambao walisamehewa kuuliwa ili wafanye kazi za utumishi au za wakulima wapangaji.

Utata wa hali hii ulitumiwa kwa njia mbalimbali. Makubaliano ya kusalimu amri yalikuwaza madai ya kumiliki ardhi ya machifu wa Kiarabu, ambapo Wakhufu ambao walisita kukidhi matakwa ya watalamaki walikumbushwa kuwa wangeweza kunyang'anywa ardhi iliyotekwa kwa nguvu ya majeshi. Kodi ya kichwa iliyolipwa na Waukristo na Wayahudi ilikuwa kati ya dinari moja na nne kwa kila mwanamume mwenye umri uliopindukia miaka kumi na minne. Kodi ya vitu, kutokana na eneo la ardhi lililolimwa, ilikuwa ya nafaka, mafuta, siki, na pengine nguo au wanyama. Chakula kiliweza kusafirishwa Bara Arabu kupitia Mto Nili na Bahari ya Shamu; vilevile, sehemu kubwa ya dhahabu iliyokusanywa ilipelekwa kwa Khalifa. Mwanzoni, watawala walipanga kiwango maalum cha jumla ya mapato ya kodi iliyoipaswa kutolewa na kila eneo la kitawala, na kazi ya kuamua kiasi cha kuwatoza watu binafsi na makonde iliachwa mikononi mwa wakusanyaji kodi na Kanisa. Khalifa Uthman, kwa kuhisi hatari ya nguvu ya gavana wa jirabo aliyekuwa na jeshi pamoja na dhahabu ambayo ndiyo iliyokidhi mahitaji ya kiuchumi ya Ukhalifa na ngano kwa chakula katika mji mkuu, alipendekeza kuwa Amr anwachie madaraka ya uendeshaji wa fedha gavana wa Misri ya Juu, `Abd Allah b. Sa'd, lakini ashike madaraka ya kisiasa na kijeshi. Amr alipokataa `kushikilia pembe za ng'ombe na kumwachia mtu mwingine akame maziwa' Uthman alimrejesha nyumbani na badala yake akamteua `Abd Allah kuwa gavana pekee wa Misri katika mwaka 644.

Mwaka 652 `Abd Allah alifunga safari ya kuvamia Nubia na kufanikiwa kufika hadi Dongola. Watu wa hapo ambao walikuwa Waukristo, wakiwa na mahusiano ya karibu na kanisa la Monofisitia la Misri, walipigana vikali dhidi ya wavamizi ambao nao waliamua kufanya makubaliano nao. *Bakt* (Mkataba) iliyotiwa saini na Wanubia ilisema kuwa Wanubia wangetoa watumwa na badala yake kupata vyakula na nguo. *Bakt* hiyo, ambayo wanasharia wa Kiislamu waliichukulia kama makubaliano ya kibiashara na wala siyo chombo cha kisiasa kilichokubaliwa kwa pamoja, ilikuwa bado inaendelea kutumika mwishoni mwa kipindi cha Wafatimi. Wakati mwingine kulitokea mifarakano - mavamizi na mashambulizi ya Kinubia katika Misri ya Juu, mapambano ya kumiliki migodi ya dhahabu au zumaridi lakini nchi iliyoko upande wa juu wa Aswan ilibaki huru.

Utawazaji wa Ukhalifa wa Kiurumaya huko Damasko katika mwaka 661 ulimaanisha uhamiaji kaskazini wa makao makuu ya ulimwengu wa Kiislamu. Vita vya baharini kati ya Waarabu na Wabizenti ambavyo vilianza kwa ushindi wa Masti (Dhat al-Sawari) wa mabaharia wa Kimisri katika 665, viliathiri vibaya sana biashara katika Mediterania. Kuanzia wakati huo na kuendelea, Bahari ya Shamu iliachwa na badala yake kutumiwa njia za nchi kavu za Ghuba, ambazo huko Misri zilielekea mashariki-magharibi na siyo kaskazini-kusini tena.

Ingawa uasi, ambao ulisababisha kuuliwa kwa Khalifa Uthman, kiongozi wa chama cha Waumaya, ulianza miongoni mwa maaskari wa Kiarabu huko Misri, lakini jumbo hilo pia lilichangia sana, kupitia vitendo vya gavana wake, `Amr ibn al-'As, katika kushindwa kwa mwisho wa madai ya Khalifa `Ali huko Siffin na Adhrub, na katika ushindi wa nasabatawala ya Waumaya. Kwa hiyo, chama cha `Ali - Mshia - kamwe hakikupata wafuasi wengi huko Misri, pamoja na upendo ambao



7.1 Misri ya Kiarabu (G. Duby, 1978)

siku zote unekuwaga ukionyesha juu ya vizazi vya Mtume baada ya kufa kwaga.

Waarabu walipoingia Misri kwa mara ya kwanza walichukua taratibu za utawala wa dola ya Wabizenti. Lugha ya Kigiriki, maofisa wadogo wa kodi, maeneo ya kitawala na sarafu, zote zilibakishwa zilivyo. Kanisa la Monofisitia liliendelea na dhima yake ya kuwa mpatanishi kati ya dola na raia. Asteaste alama za Kiukristo zilizokuwa zinatunika kwenye sarafu na nyaraka za mafunjo za dola ya Kibizenti zilibadilishwa na badala yake yakawekwa matini kutoka katika Kurani. Kuanzia mwaka 706 na kuendelea, Kiarabu kikatunika katika hati zote rasmi katika Ukhalfifa wote. Huko Misri mafunjo yaliyoandikwa kwa lugha thaniya, Kiarabu/Kigiriki, yalitokea punde tu baada ya kuanza utamalaki huo na desturi hiyo haikuachwa hadi takriban mwaka 720. Katika robo ya mwanzo wa karne ya nane, Misri ikatunika Kiarabu moja kwa moja. Ukhufu tikaendelea kuwega vijijini kwa karne mbili na kwa muda zaidi ya huo katika ibada ya Kanisa la Kikhufu la Monofisitia. Lakini, mwishoni mwa karne ya kumi, hata wanahistoria wa Kiukristo walikwishaanza kuandika tarihi zao kwa Kiarabu. Tofauti na Waajemi na Waturuki, ambao waliukubali Uislamu lakini wakabakiza lugha zao za kitaifa na hivyo kudumisha utamaduni wao, Wamisri waliungana na dunia ya wasema Kiarabu iliyotanda tangu Atlantiki hadi Mesopotamia. Dunia ya wasema Kiarabu iliyozaliwa katika Enzi za Kati, na ambayo mipaka yake ilikuwa tofauti na himaya yoyote ya huko nyuma au yenye umoja wa asili, imeendelea kuwega hadi hii leo, ikiunganisha ustaarabu wa Misri katika kiunzi kipana zaidi kuliko kile cha bonde la Nili.

Wakati wa Ukhalfifa wa Kiumaya, Waarabu wachache walikuwa wakiishi katika vijiji vya Misri na kuwaga kwa maaskari wa Kiislamu mijini miongoni mwa Wamisri hakukuleta tatizo. Tamaduni zikaathiriana na Waarabu na Wakhufu wote wakafaidi maisha ya mijini amhaya hapo awali yalitengwa kwa ajili ya matabaka ya Kigiriki. Idadi ya watu ambao hawakushiriki katika uzalishaji wa kilimo iliongezeka, kama vile maaskari, watawala, mafundi na makarani. Maisha ya mijini yalihatija gharama kubwa na utamalaki ulipopungua, hazina haikuweza tena kutegemea ngawira. Matatizo ya fedha yakaongezeka na kodi zikatozwa katika hali ya kuathiri vibaya vijiji.

Mwanzoni upinzani wa kodi mpya ya fedha ulikuwa wa kimyakimya. Wakulima wakavikimbia vijiji walimoandikishwa, wakitoweka au kuwa watawa ili kucpukana na kodi ya kichwa. 'Abd al-Aziz' (b. Marwan 685-704) alipowaingiza watawa katika mkumbo wa kodi ya kichwa, Wakhufu wakakwepa tatizo hilo kwa kusilimu. Watawala wa Kiislamu walipaswa kuchagua kati ya mambo mawili, ama kuhimiza uongoaji, ambao ungepunguza mapato au kurekebisha sharia, ili msamaha usitolewe kwa Waislamu wanya. Kurra b. Sharik, ambaye alikuwa gavana tangu mwaka 709 hadi mwaka 714, alikataa kutangua kodi ya kichwa kwa ajili ya Wakopti waliosilimu na akawachukua hatua watoro; aliongeza uzalishaji kwa kulimisha ardhi iliyo kuwa hailimwi na kupanda miwa. Khalifa 'Umar b. 'Abd al-Aziz (717-720) alitunika mbinu ya kisharia kutatua tatizo hilo la uongoaji - ambao, yeye akiwa ni muumini wa Uislamu alitaka kuongeza - kwa kuwatenganisha watu waliosilimu, ambao walisamehewa kodi ya kichwa na ardhi zao, ambazo zilibakia kuwa ardhi za kiharaj.

Katika mwaka 750 Waumaya walipinduliwa na Khalifa wao wa mwisho aliuliwa huko Misri mnamo mwezi Agosti wa mwaka huohuo. Makao makuu ya Ukhalfifa mpya wa Waabasi yaliamia Baghdad katika Mesopotamia, nje ya mipaka ya kihistoria ya dunia za Kigiriki na Kirumi na mbali zaidi na Misri. Hivyo, kazi ya kanda ya *Fustat*, ambayo ilikuwa ya kuwa kiungo cha utawala ulioko mbali ambao ulitenganishwa na Misri na mbuga pana, iliongezeka na kupanuka. Tangu mwaka 767 hadi mwaka 868, maasi yaliendelea kutokea huko Misri pasi kukoma. Maasi ya Wakhufu yalitokea kwa sababu ya kubadilishwa maofisa wa Kiukristo na kuwega Waislamu hususani katika miji midogo ya Delta. Katika mwaka 832, kwa mara ya mwisho huko Misri, Waukristo walipigana

peke yao dhidi ya Waislamu; katika maasi yote yaliyofuata, Waukristo waliungana na Waislamu katika harakati zilizoongozwa na Waislamu.

Kuanzia karne ya tisa na kuendelea Waarabu wa makabila mbalimbali na maaskari walikuwa chanzo cha fujo hizo kubwa. Ngawira polepole ilikuwa inakwisha lakini maaskari walihitaji kulipwa katika nyakati za amani na gharama ziliongezeka wakati walipokuwa vitani. Utiifu wao ulitegemea kulipwa kwao (katika wakati uliotakiwa). Yalipotokea maasi, majeshi ya nchini yaliungana na ya maadui na kwa hivyo hayakuaminika na ilibidi maaskari waletwe kutoka Mesopotamia kwa gharama kubwa.

Baadhi ya Waarabu baada ya kustakimu kwenye kingo za Delta, bado waliendelea kudumisha mtindo wao wa maisha ya wafugaji wa kuhamahama, kinyume cha hayo Waarabu wengine wakawa wakulima na wakachukua mtindo wa maisha na desturi za Wakhufu. Ikawa vigumu kuwatofautisha na Wakhufu kwa sababu Wakhufu pia walikuwa wakiingia katika Uarabu na Uislamu. Wote hao kwa pamoja waliwapiga vita wakusanya kodi.

Taarifa za Waarabu kushiriki katika maasi zinaanza kupatikana tangu mwaka 785 na kuendelea. Kati ya mwaka 814 na mwaka 832 utaratibu ulitenguka kabisa huko Misri, na madaraka ya Fustat hayakuheshimiwa tena isipokuwa katika Misri ya Kati na Juu. Bila ya kutoa maelezo marefu, inafaa kusema hapa kuwa maaskari elfu nne wa Kituruki pamoja na kuwepo kwa Khalifa al Ma'mun wa Waabasi katika Misri vyote vilikuwa muhimu katika kurudisha amani nchini katika mwaka 832. Kuanzia mwaka uliofuata na kuendelea, Waarabu waliondolewa katika kundi la *madiwan*. Kwa hiyo walipoacha kazi za kijeshi hawakustahili tena pensheni ya taifa.

Ama kuhusu vizazi vya Waarabu waliotamalaki, walikuwa na hiari tatu. Mamwinyi au familia za wafanyabiashara wakubwa wa Arabuni na wale wa *kabila* walistakimu mijini na wakawa wanamiji. Wakiwa maofisa, mawakili, na wafanyabiashara, watu hao walifaidika na maendeleo ya kiuchumi ya majiji. Kama tulivyokwishaona, vikundi vingine vilisimilishwa katika wenyeji vijijini navyo pia vikachukua mzigo wa ulipaji kodi. Aidha Waarabu wengi walibakia kuwa Mabedui, ama waliokuwa nusu wanomadi waliotamakani kandoni mwa maeneo yaliyolimwa, kama vile huko Misri, au wanomadi halisi walioishi kwa kutangatanga katika sehemu za mapululu. Walipofukuzwa jeshini, Waarabu hao wakarudia hali ya kutopenda sana utawa uliokuwepo na wakaonyesha hisia za kuchukua maisha ya mijini ambako walipigwa marufuku kuingia. Kwa hiyo, wakaungana na vikundi vilivyopinga serikali. Kwa kuteka nyara misafara mahali patakatifu au miji isiyolindwa vizuri, Waarabu hao waliweza kumiliki tena mali iliyokusanywa vitani na mababu zao hapo zamani. Kwa hiyo, utamalaki wa Waarabu ulisababisha hali ambamo, baada ya karne mbili, vizazi vya washindi vitani vilikuwa miongoni mwa wale waliofaidika na utawala uliokuwepo na miongoni mwa wale walionyonywa na kupuuzwa.

### *Misri yenye kujitawala*


Katika utawala wa Khalifa wa Waabasi, al-Mu'tasim (833-842), watumwa wa Kituruki waliletwa kwa wingi kiasi ambacho kilifanya wawe na madaraka jeshini na punde si punde wakaanza kuathiri utawala wa raia, fedha na majimbo. Makhaliifa wakawa wa jina tu, na utawala wa majimbo ukawekwa mikononi mwa machifu wa Kituruki, ambao waliendelea kuishi Baghdad au Samarra, wakawapa jamaa zao madaraka ya uendeshaji serikali. Ahmad b. Tulun, ambaye aliwasili huko Misri katika mwaka 868, akifuatana na Bakbak, mwanzoni alipewa madaraka ya kisiasa na kijeshi tu ya jimbo hilo; mamlaka ya kifedha yalikuwa mikononi mwa mtawala wa Kiarabu. Baada ya miaka minne, Ibn Tulun aliweza kumpindua Mwarabu huyo na kuwa mtawala pekee.

Ibn Tulun, ambaye alikuwa na umri wa miaka thelathini na tatu, alikuwa mwanajeshi thabiti kama Waturuki wenzie, lakini alitofautiana nao katika utamaduni wa kidini na kielimu. Alitumia akili yake kufanikisha lengo lake na hakupendelea sana kutunika mabavu. Kwanza alilazimika kuingilia kati huko Misri ya Juu, ambako yalitokea maasi katika mwaka 869 na 870. Eneo hili lilikuwa muhimu sana kwa sababu lilikuwa kiungo kati ya Misri na Nubia ambako kulikuwa na migodi ya dhahabu huko Wadi al-'Allaki na ambako watumwa walipatikana mara kwa mara kutokana na mapatano ya *bakt*. Baada ya mifulizo ya kampeni, Ibn Tulun alirejesha amani. Mahusiano mapya ya kibiashara yakaanzishwa katika Misri na Bahari ya Shamu, Arabuni na Maghrib kwenye njia za misafara zilizoanzia oasisi za magharibi.

Ibn Tulun akamiliki ngano ya Misri na dhahabu na watumwa wa Nubia: Ukhalifa ulihitaji malipo yaliyokuwa yakipelekwa Iraki kulipa majeshi yake, lakini ambako hakukutarajiwa kupatikana chochote kama fidia. Gavana wa Misri, aliyekuwa mwenye nguvu na mpenda makuu alikuwa na njia mbili: ama kujitenga na Khalifa na kuwa huru kama alivyokuwa amefanya mwanamfalme wa Afrika Kaskazini na kuitumia hongo yeye mwenyewe, au kinyume chake, kuingilia kati mashauri ya ndani ya Iraki. Katika mwaka 870, Khalifa mpya, al-Mu'tamid, alitawazwa na alimkabidhi nduguye al-Muwaffak sehemu ya mashariki ya himaya. Ibn Tulun akaweza kupata kwa Khalifa jukumu la kutoza *kharaaj* huko Shamu na Silisia. Katika mabadilishano alimpelekea Khalifa moja kwa moja hongo kutoka Misri kwa matumizi yake binafsi. Kutokana na mapato ya dinari 4,300,000 Ibn Tulun alimpelekea Khalifa dinari 2,200,200 kwa mwaka na katika mwaka 876 nyongeza ya dinari 1,200,000 ikapelekwa kwa al-Muwaffak. Lakini huyu al-Muwaffakh, ambaye alikabiliwa na maasi mawili ya hatari - Wasaffarid wa huko Uajemi na watumwa weusi wa Zanji huko Irak kusini, hata hivyo, aliona kiasi hicho kutoka Misri hakikutosheleza. Hivyo, alipeleka jeshi kumtoa Misri Ibn Tulun, lakini kwa vile maaskari wake walikuwa hawajalipwa kitambo kirefu walitawanyika zao huko Rakka.


Ibn Tulun katika kulipiza kisasi akaivamia Shamu mnamo mwaka 878 ambako hakupata upinzani wowote isipokuwa katika Antiokia. Kwa vile sasa alikuwa na madaraka thabiti juu ya Misri na Shamu, akamwaliika Khalifa kwa siri aje aishi Fustat. Lakini, Khalifa baada ya majaribio ya kutaka kukimbia, alikamatwa na kurejeshwa mji mkuu wake na kushurutishwa na al-Muwaffak kutia saini hati za kumwondoa Ibn Tulun madarakani. Ibn Tulun akaitisha mkutano wa makadhi, wanasharia, na masharifu kutoka Misri, Shamu na Silisia huko Damasko na akapata kura za kuhalalisha *jihad* dhidi ya al-Muwaffak. Lakini kabla vita vyenye havijaanza, Ibn Tulun alifariki huko Fustat mnamo Machi 884.

Ibn Tulun alirithiwa na mwanawe Khumarawayh, ambaye aliongeza Tarsus na Jazira kwenye ukanda wake, na kumfanya Khalifa akubali utawala wa nasabatawala ya Kituluni juu ya Shamu na Misri kwa kipindi cha miaka thelathini. Baada ya miaka kumi na miwili ya utawala, mnamo mwaka 896, Khumarawayh alifiliwa huko Damasko na kuiacha hazina ikiwa tupu. Utawala wa mwanae Jaysh na baada yake wa mwanawe Harun, uliangamiza kabisa utawala huo ambao ulishindwa kulinda Shamu dhidi ya Wakarmati. Paraka hii ya Kiismaili yenye asili ya kumtambua 'Ali kuwa Khalifa wa kwanza wa Mturne', ambayo ilijitokeza katika Mesopotamia katika karne ya nane, iliutumia uchungu wa Waarabu walioondolewa katika majeshi ya Khalifa, ambayo sasa yalikuwa ya Waturuki au ya watu Weusi. Kuanzia mwaka 902 na kuendelea, Mbedui walivamia Shamu na kulitaka kwa urahisi jeshi la Kituluni la Damasko. Ushindi huo ulifwatisha Waabbasi; jenerali wao Muhammad b. Sulayman, aliingia Shamu na kuwashinda vibaya Wakarmati katika mwaka 903. Kisha akaendelea hadi Fustat, ambako aliingia mnamo Januari 905, kitambo tu baada ya kuuawa kwa Harun b. Khumarawayh.



7.2 Msikiti wa Bin Tulun wa Kairo: sehemu ya mandhari ya uga, mnara na hodhi la kutawadhia. (Unesco/A. Khalil)

7.3 Msikiti wa Fatimi: nakshi ya usoni ya kame ya kumi na moja. (J. Devisse)





Baada ya kifo cha Ibn Tulun, mamlaka ya kisiasa yalikuwa dhaifu: yalitishiwa na huruma ya Mwanamfalme, jamaa zake au majenerali wake, ambao walifahamu kuwa msingi wa uhalali wa mamlaka hayo ulitokana na nguvu za jeshi. Wakati mwanamfalme alipoondolewa kwa mavavu, kikundi hicho kiliweza kufanya mamlaka ya misikiti kukubali walichokifanya, nao wakakubali hivyo bila pingamizi. Hao waliamini kuwa kitendo chochote kilichoimarisha mamlaka ya kisiasa yaliyokuwa na uwezo wa kutenda kazi kilistahiki sifa kimaadili na kisharia. Ridhaa hiyo iliyotolewa bila pingamizi inaonyesha kuwa mamlaka ya kidini hayakuwa na ragha na misingi ya kisharia ya mamlaka ya kijimbo mradi tu *khuba* iliitolewa kwa niaba ya Khalifa. Mfarakano kati ya jamii ya kiraia na jeshi ulianza kudhihiri. Fustat na Damasko, miji ya majimbo yenye mafundi na wafanyabiashara, ambao walikuwa na mwelekeo wa kushindana bei na wenye mawazo finyu, hawakuwaamini wanamfalme wa Kituluni, ambao maadili ya utamaduni wao yalikuwa yameathiriwa na Waajemi. Tabaka hii ya kati ilijinasibisha na tabaka ya watu wa dini, *ahl al-masjid*, na iliwachunga sana watu wa matabaka ya chini, *as fal al-nas*, wana wa wakulima na maaskari, ambao hawakumudu maisha ya jijini.

Tangu kuanguka kwa Watuluni katika mwaka 905 hadi kutawazwa kwa Muhammad b. *Tughj* kama gavana mnamo mwaka 935, Misri ilipata mfululizo wa machafuko ambayo si ya muhimu kuzungumzia. Magavana, ambao kazi zao zilikuwa za mashauri ya kisiasa na kijeshi tu, walirithiana. Jeshi, ambalo halikuwa likilipwa kama inavyotakikana, likianza kuteka nyara. Kuepukana na hayo, wakazi wa Fustat waliomba majeshi yahamishiwe Giza. Hilo lilikuwa ombi la kimantiki kwa sababu mji huo ulitishiwa na Waberiberi. Wakitamakani kwenye ukingo wa kushoto wa Mto Nili na katika Delta na Fayyu, Waberiberi hao waliwakilisha nasabatawala ya Kifatimi iliokuwa imekwishajikita huko Ifrikiya. Majeshi ya Kiberiberi yalikuwa yameunganishwa na jeshi la Kimisri, pamoja na majeshi mengine yaliyoundwa katika kipindi cha Kituluni. Mchanganyiko huu wa vikundi vya mbari tofauti ulisababisha matatizo ya kinidhamu. Mapambano yaliyozuka baina ya 'wamagharibi' na 'wamashariki' yalikuwa chanzo cha mapambano makubwa ya kipindi cha Wafatimi.

Desturi mbili za Enzi ya Kati ya Waislamu, *ikta* na *wakf*, zilitokea huko Misri mwishoni mwa kipindi cha Kituluni na katika nyakati za fujo zilizofuata. Huko nyuma dhima ya kulipa malipo ya fedha taslimu na marupurupu kwa majeshi ilikuwa ya majimbo ambamo majeshi yaliajiriwa. Sasa, ili kugawana madaraka ya uongozi wa fedha, afisa kiongozi alipewa ruhusa ya kukusanya kodi moja kwa moja kutoka vijijini na alikuwa na dhima ya kuwakimu watu waliokuwa chini ya uongozi wake. Hivyo *ikta* ilimlazimisha afisa kiongozi abaki katika eneo lake alilokabidhiwa alinde, wakati huo huo akiupunguzia mzigo utawala wa kijimbo.

*Ika*'za kiraia bila sbaka zilifanyika kwa ajili ya manufaa ya wasimamizi wa fedha, kama vile Madharai, ili kuhakikisha kuwa wanayafikisha mapato hayo katika hazina. Vyeo vyao bila shaka viliwawezesha kukusanya mali nyingi ya miliki ya ardhi na majengo, kitu ambacho kiliwafanya wale wenye madaraka kuwahusudu sana. Watawala hao wakaamua kutoa mali yao kauka *wakf* ili kuhakikisha kuwa ni vizazi vyao tu ambavyo vingefaidika nayo.

Kutokana na desturi hizi mbili, miji ilielemea kwa nguvu zaidi juu ya vijiji, ikiongeza kodi juu ya mazao ya kilimo, na kuachia wakulima kiasi kidogo tu cha kukimu familia zao. Papohapo wakulima hawakuweza tena kutumia mavavu - angalau kwa kufanya maasi makubwa. Hilo lilitokana na jinsi vijiji vilivyosimamiwa kutokana na mfumo huo wa *ikta* na ujuzi wa pekee wa wanajeshi weledi dhidi ya raia wenye silaha.

Mnamo Julai 935, Muhammad b. *Tughj* aliteuliwa kuwa gavana wa Misri. Ibn *Tughj* ambaye alikuwa mjukuu wa askari mmoja wa Kituruki miongoni mwa walinzi wa Khalifa na mwana wa

gavana wa zamani wa Damasko, aliwahi kuongoza jeshi nyakati mbalimbali. Akiwa na lengo kuu la kulinda upande wa magharibi wa Ukhalifa dhidi ya uvamizi uliokuwa unakaribia kufanywa na Wafatimi, alipewa haki ya kuunda jimbo lake huru. Mnamo mwaka 939 alijivisha lakabu ya al-Ikhshid, Mtumishi, ambayo ni lakabu ya kimila ya wanamfalme wa Ferghana. Katika mwaka 935 aliwashinda na kuwafukuzwa Waberiberi waliokuwa wametamalaki Kisiwa cha Roda mkabala na Fustat. Baada ya mwaka mmoja walirejea na jeshi la Wafatimi kushambulia Misri, lakini walishindwa tena. Utajiri wa Ifrikiya ambao ulikuwa dhahabu iliyopatikana kupitia Sahara na mahusiano yake na Andalusia na Sisilia, ni mambo yaliyowavutia sana watu wa misafara kutoka Bahari ya Shamu. Kwa hivyo, njia za misafara zilizokwenda sambamba na mwambao wa Mediterania na kuunganisha Afrika Kaskazini na Delta, oasisi na Misri ya Juu ziliongezeka. Lakini, ililwiwa vigumu jeshi kudhibiti njia hizo za biashara.

Kufuatana na mila ya Kituluni, Ibn *Tughj* alichukulia Shamu kuwa ni sehemu unganifu ya jimbo lake. Ilibidi azozane na viongozi kadhaa wa kijeshi waliofukuzwa kutoka Mesopotamia, ambao walilichukulia jimbo hilo kama fidia yao. Aliingia katika uhusiano wa kindoa na kiongozi mmoja kati yao, Ibn Ra'ik, kisha wakaigawanya Shamu; kusini ikawa mali ya *Ikhshid*, kaskazini pamoja na Damasko ikiwa ya Ibn Ra'ik. Miaka ya mwisho ya maisha ya Ibn *Tughj* ilishughulishwa na mapambano baina yake na nasabatawala yenye nguvu mpya ya Hamdani kutoka Mosul, ambayo baada ya kumwua Ibn Ra'ik, ilitamalaki Aleppo na kudai Shamu ya kaskazini. Baada ya kifo cha Al-Ikhshid (katika mwaka 945), mtoto wake Unujur aliendelea na mapambano ambayo yalimalizika katika mwaka 947 kwa makubaliano ya amani ambayo yaliwapa Waikhshidi udhibiti wa Ramla-Palestina, Tiberias-Jordan na Damasko. Isipokuwa mipaka iliyowekwa iliendelea kudumishwa takriban kwa karne moja na nusu.

Ibn *Tughj* alimfanya Kafur, towashi mmoja mweusi ambaye alikuwa mwenye haiba ya kuvutia, na ambaye alichanganya uwezo mkubwa wa kijeshi, kiutawala na kidiplomasia pamoja na imani yake kubwa katika Usunni, kuwa kiongozi wa jeshi. Baada ya kifo cha Ibn *Tughj*, Kafur aliongoza dola ya Kiikhshidi chini ya tawala za wana wawili wa Ibn *Tughj*, Unujur (946-961) na Ali (961-966). Kuanzia 966 hadi kufa kwake katika 968, Kafur alishika madaraka huko Misri na Shamu kusini akiwa na cheo cha *al-Ustadh*, na mamlaka yake yalitambuliwa na Khalifa wa Kiabbasi.

Kipindi cha utawala wa Kafur kilijaa wasiwasi huko Misri na Shamu. Mbali na kitisho cha Wafatimidi kutoka upande wa magharibi, kulikuwa na ushambulizi mpya wa Wanubia huko kusini, ambao walizivamia oasisi katika mwaka 950 na Aswan katika mwaka 956. Mabedui wa Bara - Arabu na Shamu walivamia misafara ya mahujaji. Matukio hayo yanaweza kuhusishwa na upungufu wa chakula uliotokea mara kwa mara huko Misri katika kipindi hicho kwa sababu ya kuadimika kwa mafuriko ya mto Nili. Mabedui na Wanubia walinunua nafaka. Bei zilipopanda huko Misri biashara ikawa ngumu kwao; kwa hiyo wakaamua kutumia nguvu za silaha kupata chakula rahisi.

Kwa hiyo, Kafur akaimarisha jeshi kwa kuwaingiza watumwa weusi walionunuliwa katika masoko ya Misri ya Juu. *Wakafuriyya* hao kamwe hawakuwa wameingizwa kikamilifu katika *Ikhshidiyya* - ambayo iliundwa na *Waghulam* weupe, Waturuki au Wadayilami - na kwa hakika vikundi hivyo viwili vilikuwa maadui. Baada ya kifo cha Kafur, maafisa waandamizi hawakuweza kukubaliana nani awe mriithi wake miongoni mwao na mfumo wa asili ulioanzishwa na Kafur haukudumu baada yake. Iwapo angetokea mtu mwenye sifa kama zake miongoni mwa wakuu wa kijeshi, utawala ulioashiria utawala wa Wamamluki ungetokeza karne tatu kabla, kwenye kingo za Mto Nili.

## Misri ya Kifalme

Mwanzoni mwa kiangazi cha mwaka 969, jenerali wa Kifatimi mwenye asili ya Kidalimati, Jawhar, alipata ushindi kwenye kingo zote mbili za Mto Nili katika mkondochini wa Fustat. Ushindi huo ulimfungulia njia ya kuingia mji huo na kuwalazimisha machifu wa Kiikhshidi na Kikafuri kukimbilia Shamu. Ushindi wa Kifatimi ulikuwa umetayarishwa na wanapropaganda waliotumia fedha nyingi, na ambao walitumia athari zao za kisaikolojia kusaidia katika kutoa maoni ya umma ambao ulikwishachoshwa na ombwe la kisiasa lililotokea baada ya kifo cha Kafur na athari mbaya za tikame mgumu. Matumizi ya silaha yakawa yameleta matokeo mazuri katika Misri ambayo ilikuwa imeyumba kwa muda mrefu.

Jawhar aliteka Misri kwa ajili ya Bwana wake, *Inam* al-Muizz wa Kifatimi, ambaye alibakia huko *Ifrikiya*. Kabla ya kumwomba *Inamu* huyo aje kwake, Jawhar alikuwa na mambo mawili ya kutenda: kutengeneza mji mkuu ambao ulistahili kukaliwa na Khalifa na kuhakikisha usalama wa nchi. Alianzisha Kairo, kaskazini mwa Fustat, akajenga maskani ya *Inam* huko, msikiti mkuu, ambao unajulikana kwa jina la Al-Azhar, na makambi kwa ajili ya vikosi mbalimbali vya jeshi. Hakupoteza muda katika kufanya hayo, kwani ilipofikia mwaka 971 majengo ya mwanzo yalikwishakuwa tayari, na Jawhar akampelekea bwana wake ujumbe kumwarifu kuwa alikuwa anasubiriwa katika mji mkuu wake mpya.

Wafatimi walidai kuwa walikuwa warithi wa al-Husayn, mwana wa Fatima, binti ya Mtume Muhammad, na wa Ali, mrithi wa kidini wa Mtume. Kinyume na Ushia wa Kiimami, ambao uliwatambua warithi kumi na wawili wa `Ali, Wafatimi walikuwa wafuasi wa tawi la Kiismaili la Mashia ambalo linatambua warithi saba tu na ambalo lilikuwa na madai makali ya kidini na kijamii ya harakati za wafuasi wa Ali. Ukaramati, ambao pia ulichiptuka kutoka Uismaili, ulipigana na teokrasia ya Kiabbasi mwishoni mwa karne ya tisa na wakati huohuo kukataa ada za kidini za Kiislamu na maadili ya Kiislamu ya kifamilia na kijamii. Huo ulikuwa mmitikio wa hamu za siri za wale ambao hawakusimilishwa katika miji mipya.

Kadhhalika asili ya vuguvugu la Kifatimi ilikuwa ya aina liyohiyo, lakini vuguvugu hilo lilitengana na ile la Wakaramati wa mwanzoni mwa karne ya kumi, wakati Wakaramati walipoezea athari zao huko Shamu. Ubayd Allah al-Mahdi, *Imamu* wa Kifatimi, alitoka Shamu kwenda *Ifrikiya* ambako ahasisi Ukhalifa. Warithi wake waliweza kumiliki sehemu kubwa ya Afrika Kaskazini na Sisilia kutokana na kujiegemeza kwao kwenye ujasiri wa vikundi vichache vya Waberiberi, hasa Wakutama, na jeshi teule la Waslavu, Kisha walijitayarisha kuiteka Misri, ambayo ilikuwa hatua ya mwisho kabla ya kuiteka Baghdad. Uislamu waliouhubiri watu bao haukuwashtua watu wa Misri - tofauti ndogo chache katika ada, haki sawa ya mirathi kwa wanawake, lakini maadili makali zaidi kwa wanawake haohao - si mambo ambayo yangewaogofya Masunni wa Fustat, ambao walivutiwa na Uislamu kutokana na nama walivyokuwa watii kwa familia ya Mtume. *Jawhar* hakupata upinzani wowote wa kidini na aliwabakisha *makadhi* walewale wa zamani ambao waliendelea kuhukumu katika msikiti wa `Amr. Ni kweli kwamba pamoja na imani dhahiri, ambayo ilikuwa inafanana na ile ya uimamu, imani timilifu ya siri ilikuwa imebakia kwa ajili ya waumini wao.

Wakaramati, ambao walizipinga ada hizo kadarnasi, hususani hija, sasa wakawa maadui wakali wa Wafatimi, marafiki wao wa zamani. Kisingizio cha kupigana vita kilikuwa uvamizi wa Shamu na jeshi la Waberiberi la *Jawhar*, ambalo liliteka eneo la zamani la Kiikhshidi la Ramla, Tiberias na Damasko. Jeshi moja lilipelekwa kupigana na Antiokia, ambayo Wabizenti walikuwa wameitika karibuni, lakini jeshi hilo lilibidi lirejeshwe kutokana na mashambulizi ya Damasko yaliofanywa na

Wakaramati; mashambulizi ambayo yalichocheva na Khalifa wa Kiabbasi wa Baghdad, ambaye alitaka kuimiliki tena Shamu. Katika mwaka 971 Wafatimi waliondoka Shamu na Jawhar aliharudisha nyuma kwa shida Wakaramati waliokuwa wamezingira Kairo.

Mnamo Juni 973 *Imam* al-'Muizz aliuchukua mji mkuu wake mpya na kasri yake. Mashambulizi mengine ya Kairo yaliyofanywa na Wakaramati yalirudishwa nyuma hadi Shamu ambayo pia ilibidi waiache. Usalama ulirejeshwa mashariki; kaskazini, meli za biashara katika Mediterania ziliongezeka kufuatana na mapatano na Ubizeni, kusini, *bakt* pamoja na mfalme wa Kiukristo wa Nubia ilianzishwa tena. Ama kwa hakika shughuli kubwa hasa ya himaya ya Kifatimi ilikuwa biashara. Athari ya mshauri wa al-Mu'izz, Yakub ibn Killis, Myahudi wa Kiiraki, ilikuwa ya muhimu katika jambo hili. Akiwa Waziri katika sehemu kubwa ya utawala wa al-Aziz, Yakub ibn Killis aliendesha vizuri sera ya nchi za nje. Akipendelea zaidi kusaidia vijihimaya huko Shamu badala ya kuingia gharama za kupeleka majeshi, alijishughulisha sana kuona kuwa mahusiano ya kiuchumi yalikuwenda vizuri. Alitia shime biashara ya masafa marefu ya bidhaa zenye bei za juu sana na kuunganisha Ulaya kusini na Afrika Kaskazini pamoja na Bahari ya Hindi na Pembe ya Afrika. Iliyokuwa Wakaramati walikwishashindwa, na njaa kuwa jambo lililopitwa na wakati katika Misri, hija zikaanza tena katika mwaka 974 na *khuba* katika jina la mfalme wa Kifatimi zilitolewa Maka na Madina, na kisha ngano ikapatikana kutoka mto Nili. Mahujaji kutoka kila nchi ya Kiislamu walishiriki katika kutukuzua ufalme wa Kairo.

Chini ya utawala wa al-Aziz (975-996), Misri ikawa na utulivu na ustawi. Athari zake zikaenea kusini mwa Mediterania, Afrika Kaskazini, Peninsula ya Bara Arabu na Shamu ya Kusini na Kati. Katika majimbo haya ya mwisho sera ya kuwa na hadhari ilifuatwa mpaka alipokufa Ibn Killis katika mwaka 991. Kuanzia mwaka 992 al-'Aziz alichukua hatua za ujasiri zaidi. Akitegemea jeshi ambalo lilikuwa limepata mageuzi makubwa kutokana na kuingizwa maaskari wa Kituruki wapanda farasi wenye silaha na kwa kutumia mbinu bora zaidi za utekaji miji alimshambulia mtawala wa Kihamdani wa Aleppo na walinzi wake wa Kibizeni wenye nguvu. Wakati buohuo alimweka gavana wa Kifatimi huko Damasko na kuwafukuza Mabedui kutoka Palestina.

Al-'Aziz alimwachia mwanawe al-Hakim (996-1021) hali dhaifu zaidi kuliko ilivyotegemewa. Idadi ya watu katika Kairo na Fustat, ambayo ilikuwa miji mikuu-pacha ya himaya tajiri kuliko zote za kipindi hicho, ilikuwa imeongezeka sana, kwani maaskari wa Kiberiberi, Kislavu, Kituruki na Weusi na wafanyabiashara na mafundi wa Kiiraki na Kishamu, walikuwa wamejazana katika miji hiyo ambamo ilisemekana dhababu ilipatikana kwa urahisi. Hongo kutoka majimbo na kodi zilizotozwa misafara iliyokuwa inapita Misri ilisababisha bidhaa hiyo ya madini yenye thamani kukusanika. Vyanzo vikuu vya mapato ya kodi, ya metali na mengine, vilikuwa vijiji vya Kimisri na mafundi wa miji ya majimbo, ingawa wakusanayaji kodi na maafisa wa fedha walijitengea wenyewe sehemu kubwa. Aghalabu hao walikuwa Wayahudi au Wakristo, na waliamsha hisia za chuki dhidi yao katika vikundi vya watu wa hali za chiri miongoni mwa Wasunni wa Fustat.

Kuongezeka kwa haraka kwa Waturuki jeshimi pamoja na faida za kifedha walizopata ziliwafanya maaskari wa Kiberiberi ambao walichukua madaraka alipokufa Al-'Aziz, kwa vile al-Hakim alikuwa bado mtoto, waone wivu. Maaskari hao madhalimu wa kimashariki waliungana na matowashi wa Kislavu (as-Sakaliba) na maafisa wa Kiukristo na Kiiraki kuwafyeka Waberiberi.

Al-Hakim alikuwa mfalme wa mwisho wa Kiarabu katika historia mwenye kuwa na madaraka kamili juu ya himaya kubwa. Hakuteua waziri wala mkuu wa majeshi, bali alimteua jenerali katika nyakati za vita. Alipokuwa kijana, al-Hakim alishuhudia tabia ya utegemezi uliofanywa na al-'Aziz na maisha yake yote aliwachukia na kuwadharau wapambe hao wa ikuu. Alipendelea kuzuru

Fustat, na alipenda masoko yake na nyumba zake za hali ya unyonge. Aidha alikuwa na mawasiliano ya moja kwa moja na mafundi na wafanyabiashara wa Kisunni. Alielewa mzigo ambao nchi ilikuwa imetwishwa kwa sababu za anasa na vikwazo vilivyowekwa na watu wenye vyeo baina ya mfalme na raia wake. Alijaribu kuondoa kikundi hiki cha kati kwa kuwaua wale wote aliowashuku kuwa ni wadanganyifu na wenye kupenda makuu. Akiwa amelemewa na mavune ya shughuli nyingi za mamlaka kamili, alijaribu kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo bila mafanikio; urazini wake ulifunikwa na ujuha na vitendo vya kikatili vya kiwendawazimu.

Sera yake ya kidini haikuwa thabiti. Alijaribu kufanya ada za Kifatimi zikubalike huko Fustat, na baadaye, ili kuwavutia Masunni, aliwalazimisha Wayahudi na Waukristo wasilimu na akajenga misikiti kwenye mahakalu yao. Katika 1009 alibomoa hata Kaburi Takatifu katika Yerusalem. Wakati huohuo, tangu 1006 hadi 1013, alivumilia ada za Kisunni na hata kuwateua walimu wa Kisunni wafundishe katika Taasisi ya Elimu *Dar al ilim*, ambayo alianza. Baadaye alirejea kupiga marufuku ada za Kisunni na katika 1017 aliwaruhusu baadhi ya Waajemi kuhubiri utukufu wake. Hilo halikufanikiwa: Wahubiri hao waliuliwa. Katika mwaka uliofuata al-Hakim aliona maeneo ya kaskazini ya Fustat yakibomolewa na maaskari weusi. Akihisi kuwa jaribio lake la kuasisi ufaalme wa moja kwa moja kwa ikibali ya matabaka ya kati ya Kisunni ya mjini limeshindwa, akawa hana hamu tena na Fustat na akawaruhusu Wayahudi na Waukristo kukana Uislamu alioulazimisha waufuate miaka kumi iliyopita. Kuuawa kwake ambako kulifichwa na kufanywa kana kwamba kapotea, kulichochea na wapambe wake wa karibu, ambao walihofia kufukuzwa. Baadhi ya wafuasi wa utukufu wake walianzisha faraka ya Kidruzi huko Shamu.

Makabila ya Waarabu yalizichochea fujo nyingi katika kipindi cha utawala wa al-Hakim. Abu Rakwa, Muumaya, alichocha maasi ya Waberiberi wa Kizanata na ya Waarabu wa Banu Kurra huko Tripolitania. Baada ya kuteka majeshi kadhaa ya Kifatimi, Abu Rakwa alitishia Fustat katika 1066. Raia wakaonyesha utii wao kwa al-Hakim, ingawa vitendo vya uhaini viliripotiwa katika ikulu ya mfalme na miongoni mwa wanajeshi wa Kiberiberi. Abu Rakwa alikamatwa kwa msaada wa Wanubia, na kuuliwa karibu na Kairo. Ilihahirika kuwa jeshi la Kifatimi halikuwa na nguvu na iligharimu hazina dinari milioni moja kuyazima maasi hayo.

### *Mtataruku Mkuu wa Karne ya Kumi na Moja*

Katika utawala wa al-Zahir mwaka (1021-1036) na wa mwanawe, al-Mustansir (mwaka 1036-1094), sera iliyofuatwa haikuwa tena kama alivyotaka *Imam*, bali ilitokana na mwingiliano changamani wa vikundi pinzani. Hadi kufikia mwaka 1062 hali katika himaya polepole iliharibika kutokana na taathira za udhaifu uliokwishatajwa. Katika hali ya amani, jeshi, ambalo liliundwa na vikundi anuwai vya kimbari vyenye kuhasimiana, liligharimu sehemu kubwa ya mapato ya taifa. Nyakati za vita ilibidi pia majeshi yapatiwe rikabu na silaha na kupewa malipo ya ziada. Fedha zilizokuwamo katika hazina hazikuongezeka lakini idadi ya watu waliostahiki malipo ya uzeeni kama vile jamaa ya *Imamu*, *masharifu*, watumishi wa serikali na majeshi iliongezeka, na siku zote kulitokea mikinzano ya kimaslahi. Maaskari hawakulipwa vya kutosha na hivyo wakawa wanashambulia vijiji na vitongoji. Jeshi halikuwa tena chombo cha kutunza amani bali likawa ndio kiini cha wasiwasi.

Miji ilisongamana watu; maziko ya Karafa yalikalifiwa na watu waliokimbia uvamizi wa Mabedui, ambapo waali walivihama vitongoji kutafuta usalama mijini Fustat au Kairo. Wafanyabiashara walingojea karamu kuu za Waislamu kwa hofu kubwa kwani wakati huo watu walivamia masoko yaliyofungwa. Uhaba wa chakula ukazidi na ukawa wa mara kwa mara. Kila

palipotarajiwa mafuriko machache, bei ya ngano ilipandishwa. Al-Jarjara'i, ambaye alikuwa waziri tangu 1027 hadi 1045, aliweza kusimamisha upandaji wa bei kwa kuweka soko moja la ngano na kwa kuhimiza ushindani wa kupunguza bei miongoni mwa waoka mikate. Lakini, viongozi wote wakuu, pamoja na *Imam*, walilimbikiza bidhaa na kuendeleza uuzaji bidhaa uliocgemezwa kwenye kukisia hali ya mambo ya baadaye.

Vilevile kulidhahirika hali ya kuwayumbisha kwa jumla watu walioishi ukingoni mwa jangwa: makabila makuu ya Waarabu wa Shamu yalitaka kuingia katika makonde yaliyolimwa kulisha mifugo yao na kushambulia miji pia. Mabadiliko ya hali ya hewa ikiwa ni pamoja na vipupwe vikavu zaidi, huenda yalisababisha mambo hayo. Mpaka 1041 jenerali wa Kifatimi al-Dizbiri aliweza kuyazuia makabila hayo huko Shamu. Katika Misri ya Juu uhaini wa Zirid Ibn Badis ulitumiwa kuwahamisha Banu Hilal na Sulaym Banu waliokuwa wakiharibu nchi (mwaka 1050) na kuwapeleka Tripolitania na Ifrikiya.

Mwaka 1059 Wafatimi walipata ushindi wao wa mwisho mkubwa wa kidiplomasia: jenerali wao wa Kituruki, al-Basasiri, alimfunga jela Khalifa wa Kiabbasi al-Kaim na kufanya msikiti wa Baghdad umwombee dua al-Mustansir. Lakini, baada ya miezi kadhaa, Tughril Bek, mfalme wa Kiseljuki, maliki wapya wa Kisunni wa mashariki, aliitaka tena Baghdad na kumrejesha al-Kaim madarakani. Hali hii iligeuka wakati, katika mwaka 1070, jenerali wa Kifatimi Nasir al-Dawla, katika maasi ya Aleksandria alipomtambua Khalifa wa Kiabbasi na kisha, katika 1072, akamtia al-Mustansir kizuizini Kairo na kuwomba Waseljuki wamsaidie. Dola ya Kifatimi ingeweza kumalizika wakati huo.


Njaa kubwa ambayo ilianza katika mwaka 1062 na ambayo ilishadidi tangu 1065 na kuendelea, ilia idadi kubwa ya Wamisri. Muundo mzima, ambao wao wenyewe waliuunda nchini humo, ulikuwa unaanguka. Katika mwaka 1703 *Imam* alimwita Muarmenia Badr al-Jamali, gavana wa Palestina, kuja kumsaidia. Mpiganaji huyo katili alikuja Kairo katika Januari 1074 na akawaua maofisa wakuu, akayatawanya majeshi ya waasi na akaunda upya jeshi dogo lakini lenye ufanisi kwa kutumia askari wake wa Kiarmenia na kulitumia kuyateketeza majeshi ya Weusi waliokuwa wakivamia Misri ya Juu. Alirudi mnamo mwaka 1076 kulinda Kairo, ambayo ilikuwa inashambuliwa na Mturuki Atsiz, rafiki na msaidizi wa Waseljuki. Katika 1077 aliwafurusha Waberiberi wa Kilawata kutoka kwenye Delta, na kuwauza wanawake 20,000 wa kabila hilo sokoni. Ingawa hakuweza kuitaka tena Damasko, hata hivyo aliimarisha utawala wa Kifatimi katika bandari za Palestina. Ili kuwasaidia wakulima warudie kulima makonde yao yaliyoharibiwa, Badr aliwasamehe kodi kwa miaka mitatu. Aliunda upya wilaya za kitawala, dola na jeshi; na kwa kufanya hivyo akawa ameongeza maisha ya enzi ya Kifatimi kwa karne moja zaidi.

### *Kutapatapa kwa enzi ya kifatimi*

Baada ya mzozo wa mwaka 1062-1076, ndoto ya Kifatimi ya kuunda himaya ilikufa. Dua kwa jina la al-Mustansir hazikuombwa tena ama huko Ifrikiya, Maka, Aleppo au Damasko. Lakini Misri, ambayo iliundwa upya kwenye Bonde la Nili, polepole ilikuwa inarejea katika hali yake ya zamani na Aleksandria ilikuwa inarudia tena maendeleo yake kutokana na biashara yake na Italia. Hali kadhalika, Kus, jimbo la Misri ya Juu, ilikuwa inauza watumwa weusi kutoka Nubia na viungo kutoka Bara Hindi. Lakini, wote wawili, Badr na al-Mustansir walipokufa, katika mwaka 1094, mgogoro mpya uliukumba ukoo tawala wa Kifatimi na itikadi yake. Al-Afdal, mwanawe Badr, alimtawazisha kuwa Khalifa al-Hasan mwana mdogo wa al-Mustansir, na kumzika hai kaka yake Nizar. Kiongozi wa ujumbe (*da'wa*) wa Kiismaili katika nchi ya Kiseljuki, Hasan b.al-Sabbah,



7.4 Kauri ya Kimisri (Kifatimi) yenye picha za mng'aro. Jagi la karne ya kumi; bakuli la karne ya kumi na moja (Hlatimiliki ya picha: Nyumba ya sanaa ya Freer, Washington)



alimtambua Nizar kuwa ni *Imam* na madhehebu yake ya *Waasasini*, ambayo kama yalivyokuwa madhehebu ya Wadruci, yalianzishwa nje kabisa ya Misri, yalikomesha shughuli za kimapokeo za shughuli za kipropaganda na kimisionari za Wafatimi.

Al-Mustansir alitawala takribani robo-tatu ya karne. Katika kipindi kifupi kilichopita kabla ya kutoweka kwa unbasabatawala huo Makhalfi sita walirithiana. Hakuna hata mmoja kati yao aliyekuwa na madaraka kamili wala aliyemteua mrithi wake. Madaraka yalikuwa mikononi mwa mawaziri wa kijeshi, ambao baadhi yao walinyakua madaraka kwa kutumia upanga, na wengine kwa kuyarithi. Baadhi ya mawaziri hao walikuwa shupavu, kama vile Talai b. Ruzzik, lakini wengine walikuwa viongozi wa ovyo tu. Katika Misri ambamo itikadi ya Kifatimi ilikuwa imetoweka, mawaziri hao walishika itikadi mbalimbali. Al-Afdal Kutayfat, mjukuu wa Badr, aliasisi imani ya Uimamu wa 'maimamu kumi na wawili', na Ridwan alikuwa Sunni na alianzisha *madrasa* ya Kishafii huko Aleksandria. Watu hawakujali aina gani ya Uislamu ilitawala; utii kwa watawala hao ulitokana tu na fahari ya kuwa na mamlaka ya Kiislamu yenye makao makuu huko Misri.


Miaka mitatu baada ya kifo cha Badr wapiganaji wa Vita vya Msalaba waliingia katika nchi za Waislamu, wakawapindua Waseljuki, na katika 1099 waliitaka Yerusalem. Waliwashinda Wafatimi huko Askalon. Hapo mambo yakatulia kwa miaka mingi, ingawa palitokea migongano hapa na pale. Hapakuwa na ushirikiano mzuri kati ya Wafranki na Wafatimi, ambao hawakujali kutopatana kwao kwa sababu zinazoeleweka fika. Tangu karne ya kumi, mapato ya dola ya Kifatimi yalitokana na kodi zilizotoweka katika biashara ya nafaka, lakini katika karne ya kumi na mbili bei ya nafaka ilianguka baada ya maafa yaliyowafika watu katika karne ya kumi na moja, na pia bila shaka kutokana na

kupanuliwa kwa makonde yaliyolimwa kufuatia mabadiliko ya kitabianchi huko Shamu. Dhahabu, ambayo ilikuwa adimu zaidi huko Shamu, aghalabu ilizunguka kati ya Bara Hindi na nchi za Magharibi. Kwa hiyo, Wafatimi walihitaji kudhibiti Bonde la Nili tu na vituo vya biashara kwenye pwani ya Palestina, ambavyo kama ilivyokuwa Aleksandria, vilifikiwa na wafanyabiashara wa Kiitalia mara kwa mara. Kwa Wafatimi, kuwepo kwa wapiganaji wa vita vya Msalaba huko Shamu, ambao walikuwa kizuizi kati ya Waseljuki na Misri, na kugeuza mkondo wa biashara toka Bahari ya Shamu kwenda Bonde la Nili, kulikuwa na manufaa. Mpaka mwaka 1154, ambapo Nur al-Din alitawazwa huko Damasko, hapakuwa na dalili ya mshikamano wa Waislamu kwa lengo la kuwafurusha Wafranki kutoka Sbamu.

Nur al-Din, ambaye alikuwa kibaraka huru wa Waseljuki, akitegemea jeshi lenye nguvu, aliitaka tena Shamu. Dola iliyodhoofika ya Kifatimi, yenye jeshi lililogawanyika katika vikundi vilivyoshindana vya kimbari, ilikuwa na hiari kuchagua kati ya siasa ya kuwaunga mkono wapinzani wa sera wapiganaji Vita vya Msalaba, - ambayo ilikuwa siasa ingemtia hatarini kushambuliwa na Wafranki - na kuwaomba Wafranki wamsaidie dhidi ya Nur al-Din, ambaye alitaka kuurejesha Usunni. Wagombea madaraka huko Misri walichagua mojawapo ya hiari hizo mbili na pengine kutumia zote mbili wakati mmoja, kwa matumaini ya kudhibiti hali ya mambo. Hilo liliharakisha kudhoofika kwa dola.

Kutawazwa kwa Nur al-Din huko Shamu ya kati kuliwafanya Wapiganaji wa Vita vya Msalaba watafute fidia huko Misri na wakaikamata Askalon katika mwaka 1153. Jambo la kwanza walilofanya mawaziri wa Kifatimi lilikuwa ni kulinda njia kuu ya kusini kutoka Bahari ya Shamu hadi Aleksandria kupitia Misri ya Juu, na hawakujali sana mpaka wa kaskazini-mashariki. Lakini, Tala'i b. Ruzzik alifanya safari mbili za mashambulizi dhidi ya Palestina ya Wafranki. Ingawa alishinda, hakupata matokeo ya kudumu, kwa sababu Nur al-Din hakuendelea kujishughulisha na sehemu hiyo. Katika 1161 Wafranki walifanya mashambulizi ya kwanza ya moja kwa moja dhidi ya





7.5 Bab al-Nasr: mojawapo la lango kwenye ukuta wa nji wa Fatimi. (Misikiti ya Kairo, na G. Wiet, uk. 8. Picha: Albert Shoucair; Hatimiliki: Hachette, Paris)

Misri, na baadaye walifanya mashambulizi manne zaidi, baadhi yakiwa ni kutokana na aridha za mawaziri wa Kairo, katika kipindi hadi 1169. Ni katika mwaka 1153 tu ndipo Wafranki hao walipokumbana na majeshi yaliyopelekwa na Nur al-Din chini ya uongozi wa Shirkuh na mpwa wake, Salah al-Din (Saladin wa tarihi za Ulaya). Kutokana na ahadi zilizovunjwa, mabadiliko ya ghafla ya urafiki na hadaa aliyofanya waziri Ibn Sallar na Khalifa al-'Adid, mashambulizi hayo ya Waislamu hayakuumbua lolote. Kwa hiyo, katika mwaka 1169 Shirkuh alishika mwenyewe wadhifa wa waziri wa Kifatimi. Punde tu baada ya hapo akafariki na kurithiwa na Salah al-Din.


Hivyo waziri wa mwisho wa Kifatimi alikuwa jenerali wa Kissuni Mkurdi, kibaraka wa mwanamfalme wa Damasko, Mturuki wa Kisunni, Nur al-Din, ambaye jina lake lilitajwa katika dua baada ya lile la *Imam* al-Adid. *Imam* huyo hakuweza kuvumilia hali hiyo, naye akamwagiza Jawhar, towashii mweusi, kumwua Salah al-Din. Aliposikia hayo Salah al-Din aliamrisha Jawhar auliwe. Walinzi weusi wa Kairo wakagoma. Kukatokea mapambano makali na al-Adid akawakana maaskari weusi ambao walikuwa wamejitolca maisha yao kwa ajili yake. Mlinzi huyo akauawa. Salah al-Din ambaye alitumia ngano ya Ukhalifa wa Kifatimi katika mapambano yake ya mamlaka, alikataa kuubatilisha Ufatimi, ijapokuwa Nur al-Din alimshawishi hivyo. Lakini, katika 1171, *kuuba* kwa niaba ya Khalifa wa Kiabbasi ilitolewa hadharani huko Kairo. Kwa hiyo, Uimamu wa Kifatimi huko Misri ukamalizika bila ya kuwa na haja ya kumwondoa al-'Adid. Naye Al-'Adid alikufa kifo cha kawaida. Utawala uliodumu karne mbili hatimaye ulitoweka pasi Wamisri kuonyesha jaziba ya aina yoyote.

### Hitimisho

Katika 1171, zaidi ya karne tano baada ya kutekwa na Waarabu, Misri ilikuwa nchi tajiri kuliko zote katika Mashariki. Vifinyange, vifaa vya kioo, nguo na vitu vya metali na mbao vilivyotoka katika karakana zao vilikuwa kamili pasi na mfano. Kilimo pia kiliendelea kuwa kama kilivyokuwa miaka na miaka, papo hapo mazao mapya yaliyotoka Asia yakaingizwa katika kilimo hicho. Usanifu majenzi wa kidini na kijeshi ulidhihirisha sanamu za kupendeza; na karne zilizofuata zilionyesha mafanikio mengi katika kazi hizo. Fasihi katika Kiarabu asteaste ilikuwa inaendelea na papohapo

kujitokeza kuwa ya kitaifa zaidi kuliko ya kijimbo. Wairaki na Washamu walioishi katika mji mkuu walikuwa na dhima muhimu, lakini ni ubora wa kazi za kihistoria na maelezo ya maumbo ya nchi ya Misri vilivyoleta sifa ya uasili katika fasihi hiyo.

Lakini utamadunishaji haukwenda haraka wala kuwa kamili. Sehemu kubwa ya watu, ama wakulima wa Misri ya Juu au mafundi wa miji ya majimbo, walibaki kuwa Waukristo. Wasunni wa Fustat hawakujali mapambano ya madaraka yaliyopambanisha viongozi wa kijeshi, ambao aghalabu waliinukia kutoka utumwani na kuwa viongozi wa majeshi yenye mchanganyiko wa mbari mbalimbali. Haiba ya Kimisri, ambapo kuna matini machache tu yanayocleza juu yake, ilikuwa inakua polepole, ukilinganisha na maendeleo ya haraka ya Fustat na Kairo.



## *Nubia ya Kikristo katika kilele cha ustaarabu wake*

### *Mahusiano ya awali na Misri ya Kiislam*

Kutokea kwa ufalme wa Kiukristo wenye nguvu kusini mwa Maporomoko ya Kwanza ya Nili kulileta matarajio mazuri ya maendeleo kwa raia wa Nubia. Mambo mawili yaliwasaidia kufikia ustawi wa kiuchumi. Jambo la kwanza lilikuwa kuungana kwa ufalme wa Kaskazini wa Nobadia ('Nuba' kwa Kiarabu), ukiwa na makao makuu yake huko Faras, na ufalme wa kati wa Makuria ('Makurra' kwa Kiarabu), makao makuu yake yakiwa huko Dongola ya Kale (Dunkula al-Adjuz kwa Kiarabu), na kuanzishwa kwa serikali kuu imara. Jambo la pili ni mahusiano mazuri na nchi jirani yake, Misri, kwa kutia saini mkataba uliojulikana kwa jina la *bakt*, kufuatia uvamizi wa Dongola uliofanywa na Waarabu wakiongozwa na Abdallah ibn Abi Sarh katika miaka ya 651-2.

Huenda wakati wa uvamizi, Nubia ya Kaskazini na ya kati zilikuwa zimeungana chini ya Mfalme Kalidurut wa Dongola. Kwa hiyo, Abdallah ibn Abi Sarh alitia saini mkataba mmoja tu - ule wa Dongola - na kutojihusisha na Nobadia ambayo mahusiano mazuri nayo yalikuwa muhimu kwani nchi hiyo ilipakana moja kwa moja na Misri. *Bakt* ilikuwa ni aina ya mkataba wa kipekee katika ulimwengu wa Kiislam, na kwa hakika ulikuwa mkataba wa kusitisha mapigano au wa kutoshambuliana.

Matini ya *bakt* yalikuwa na maafikiano yaliyohusu mambo kama vile Waarabu kutoshambulia Nubia, kwamba raia wa nchi hizo mbili wawe na haki ya kupita katika nchi nyingine kama wasafiri lakini si kama watamakani, na kwamba mamlaka ya nchi iliyohusika yahakikishe kuwepo kwa usalama wa raia wa nchi nyingine. Mkataba ulikuwa pia na sehemu inayohusu kubadilishana wahalifu. Wanubia wangesimamia msikiti uliojengwa Dongola ya Kale wa kuwahudumia wageni Waislamu.

Nubia pia ililazimishwa kutoa kodi ya watumwa 360 kila mwaka ambao wangewasilishwa kwa Gavana wa Aswan. Waarabu nao walitakiwa watoe *ardeb* 1300 za ngano, *kanir* 1300 za mvinyo na viwango maalum vya kitani na nguo, n.k. ikiwa ni mabadilishano kwa hao watumwa. Kwa hiyo, mkataba huu ulikuwa na vipengee vya makubaliano ya kibiashara. Mkataba ulitumika katika karne tano zilizofuata za ustaarabu wa Kiukristo katika Nubia na katika awamu yake ya mwanzo ulikuwa muhimu kwa ajili ya kudumisha amani na uwezekano wa maendeleo ya kitaifa.

Falme mbili za Kinubia ziliungana chini ya Mfalme Merkurios, ambaye alitawazwa katika mwaka wa 697. Baada ya muungano wa ufalme wake alijihusisha zaidi na swala la umoja wa kidini katika Nubia yote na mwanzoni mwa karne ya nane akashughulikia kuliweka kanisa la Nubia chini ya jimbo la Askofu Mkuu wa madhehebu ya Kimonofisita katika Aleksandria.

Muungano wa nchi na baadaye wa dini, yaani kuanzishwa kwa dini moja chini ya Kanisa la Kimonofisita la Misri, muungano wa ufalme wa Nubia na ufalme wa kusini wa Alodia (tunajua mambo machache sana kuhusu ufalme huu katika kipindi hiki) pamoja na Ethiopia, bila shaka ulileta hali nzuri kwa maendeleo ya Nubia. Kutokuwepo na tishio lolote kwa upande wa Waarabu na uwezekano wa kufanya biashara na Misri pamoja na kudumisha mawasiliano na Ubizenti kulileta utamaduni mpya na bayana katika Nubia katika kipindi kilichofuata. Mapokeo ya utamaduni wa Kibizenti yafiathiri muundo wa utawala wa kitaifa na mfumo wa mahakama; halikadhalika na ujenzi, sanaa na ufundi wa kazi za mikonu.

Hivyo, mwisho wa karne ya nane ulipeleka Nubia katika kipindi cha ustawi ambao uliendelea hadi kufikia zaidi ya nusu ya karne ya kumi na mbili, wakati ambao pia kulikuwa na hali nzuri ya uchumi.

Mipaka ya muungano wa ufalme wa Nubia ilianza al-Kasr Kaskazini (kilometa chache kusini mwa Aswan) hadi kati ya Maporomoko ya Tano na ya Sita (al-Abwab), ambapo ilikutana na mpaka wa Kaskazini wa Alodia ('Alwa' kwa Kiarabu) ikiwa na makao makuu yake huko Soba, jirani na Khartaoum ya leo.

Hatujui lolote kuhusu Alodia. Masimulizi ya Ibn Salimal-Aswani yanatueleza kwamba Soba ilikuwa na majengo makubwa na mazuri, bustani maarufu, pamoja na makanisa yaliyojaa dhahabu. Inasemekana pia kwamba Mfalme wa Alwa alikuwa na nguvu zaidi kuliko mtawala wa Makuria, kwamba alikuwa na jeshi shupavu na kwamba alitawala nchi iliyokuwa ya rutuba zaidi. Lakini, haya hayajawahi kuthibitishwa katika machimbo ya kiakiolojia yaliyofanywa hivi karibuni katika Soba. Eneo la Soba halionyeshi dalili za kuwepo kwa nyumba za mijini za hali ya juu, isipokuwa kiasi kidogo cha majengo ya matofali yaliyochomwa iliyotawanyika hapa na pale.


Hakuna taarifa za moja kwa moja kuhusu muungano wa Alodia na Makuria, ingawa katikati ya karne ya kumi falme mbili hizi ziliunganishwa na mahusiano ya damu. Katikati ya karne ya nane Mfalme Kyriakos ahelezwa kuwa mtawala wa ufalme wa Nubia "hadi kufikia mwisho wa dunia kusini" Lakini inaelekea kwamba Alodia ilikuwa sehemu ya muungano wa ufalme wa Nubia kwa muda mfupi tu, lakini ilikuwa nchi iliyojitenga kwa karibu muda wote wa Ukristo katika Nubia.

## *Mashariki na Maghribi ya Mto Nili*

Mpaka wa mashariki ya ufalme wa Nubia ulipakana na nchi iliyokaliwa na makabila ya Wabeja. Kuanzia karne ya nane hadi karne ya kumi, hawa walikuwa watu muhimu katika kuunda mahusiano ya kisiasa katika sehemu hii ya dunia.

Hadi kufikia mwanzoni mwa karne ya tisa karibu makabila mengi ya Wabeja waliokuwa wakiishi katika eneo la Milima ya Bahari ya Shamu walikuwa bado ni wapagani. Katika mwaka wa 831, kutokana na ugomvi wa mara kwa mara juu ya mpaka, Khalifa al-Mutasim alituma jeshi la kuiadhibu Beja. Baada ya kushindwa, kiongozi wao Kanun ibn Abdal-Aziz alilazimishwa kuutambua utawala wa Khalifa. Ndipo basi ukaundwa mkataba wa makubaliano. Ingawa mkataba huo ulikuwa na vifungu fulani fulani vilivyofanana na vile vya mkataba wa *bakt*, mkataba huu ulikuwa na dhima tofauti, na Wabeja walilazimika kulipa kodi kila mwaka bila ya kuhakikishiwa kupata chochote kutoka kwa Waarabu. Tena basi Waarabu wakawa na haki ya kutamakani kwenye ardhi ya Wabeja na kiongozi wa Wabeja akabakia kama mnyapara tu.

Ardhi iliyokaliwa na makabila haya ya kuhamahama ilikuwa katika maeneo ya machimbo ya dhahabu (hasa katika eneo la Wadi al-Allaki), na kwa hali hiyo kuingia kwa Waarabu katika maeneo haya kukaongezeka kwa nguvu. Vita vya waziwazi vilianza tena katikati ya karne ya tisa, wakati



8.1 Unubi ya Kikristo (S. Jakobielski)

kiongozi wa Wabeja wakati huo akiwa Ali Baba, alipolazimika kusalimu amri mbele ya majeshi ya Kiarabu. Kufuatana na vyanzo fulani vya Kiarabu, wakati huo kodi ilikuwa imefikia gramu 2,400 za dhahabu kila mwaka.

Kwa kuwa Wabeja walitishiwa usalama wao mara kwa mara, halikuwa jambo la kushangaza kwamba walitafuta ulinzi kutoka kwa Wanubia na inaelekea majeshi ya Nubia yalihusika kwa namna fulani katika vita vilivyotajwa hapo juu. Ibn Hawkal aliarifu kwamba Ali Baba na Mfalme wa Nubia, Yurki (Georgios) walichukuliwa mateka, na kwamba walipeleka Baghdad mbele ya Khalifa, al-Mutawakkil. Kwa vyovyote vile, hata katika kipindi cha ustawi wake mkubwa, ufalme wa Nubia ulipata misukosuko ya maadui kwa upande wa Bahari ya Shamu kuvuka mipaka ya mashariki ya Nubia.

Mahusiano na makabila yaliyoishi Maghribi mwa bonde la Nili yalifuata mfumo mwingine. Ingawa hatuna habari za kutosha kuhusu jambo hili, inaelekea kuwa, katika nchi ya mwendo wa siku nyingi kutoka bonde la mto Nili hadi jangwa lenye mchanga, paliishi makundi ya wachungaji walioitwa Wajibaliyyun (watu wa sehemu za miinuko) na Waliadiyyun walioishi kusini (milima ya Nubia) na Kaskazini mwa Kordofan. Yasemekana kuwa hawa wa mwisho walifuata Ukristo. Imekwishathibitishwa kwamba kulikuwa na uhusiano wa kilugha baina ya baadhi ya makabila katika milima ya Nubia (Wadair, Wadilling) na Darfur (Wabirgid, Wamidob, Watunjur), na wale waliotumia lahaja za Kinubia katika bonde la Nili. Mawasiliano kati ya ufalme wa Nubia na hiyo sehemu ya Sudani kwa kiasi fulani yamethibitishwa kiakiolojia, kwa mfano ugunduzi wa vyombo vya ufinyanzi vinavyohusu mambo ya Ukristo vya wakati wa urasimi wa Kinubia huko Ayn Farah (Kaskazini mwa Darfur) na vyombo vya aina hiyo vya baadaye kidogo huko Koro Toro katika Chad. Haiwezekani kutupilia mbali wazo kwamba Kordofan na Darfur vilikuwa ndivyo hasa vyanzo vya kupata watumwa ambao Nubia lililazimika kuwapeleka Misri kwa mujibu wa *bakt*. Hatujui ni kwa kiwango gani biashara ya watumwa ilikuwa shughuli ya kiserikali au msingi wa uchumi; wala hatujui ni kwa kiwango gani maeneo ya Maghribi mwa Sudan yalitawaliwa na Wanubia.

### *Dongola, Faras na miji mingine*

Mji wa Dongola, makao makuu ya Nubia, uliojengwa mapema mnamo karne ya kumi na moja, ulielezwa na Abu Salih kama ifuatavyo: 'Hapa ndipo makao ya Ufalme. Ni jiji kubwa kandoni mwa Nili, mto uliobarikiwa, na kuna makanisa mengi, majumba makubwa na barabara pana. Nyumba ya Mfalme ni kubwa na ndefu na yenye kuta nyingi zilizojengwa kwa matofali mekundu na inafanana na majengo ya Iraki'. Matokeo ya machimbo yanaelekea kuthibitisha haya yanayosemwa. Hii leo kuna masalia ya mji wa majengo ya hali ya juu ambayo yanaonekana kwenye eneo la zaidi ya hekta 35, ambamo mabaki ya majengo ya mwanzoni yamefunikwa na majengo ya kipindi cha Kiislamu (karne ya kumi na tano hadi karne ya kumi na tisa). Kaskazini kuna jiji la Waukristo ambako kuna makanisa ya hali ya juu yaliyogunduliwa na wanaakiolojia wa Poland. Kuelekea zaidi Kaskazini kuna majumba ya hali ya juu ya karne ya nane na karne ya tisa. Nyumba zililogunduliwa hapa zinatofautiana katika mpangilio wake wa nafasi na vilevile katika vitu vinavyorahisisha maisha (mabomba ya maji, vyumba vya kuogea vyenye mfumo wa maji moto) na kuta za ndani zilipambwa kwa michoro; mambo ambayo hapo nyuma yalikuwa hayajulikani.

Mwanzo wa karne ya nane unachukuliwa kama kipindi cha ujenzi wa jumba maarufu la kifalme lenye ghorofa mbili, ambalo lilikuwa kwenye vilima vyenye mawe mashariki ya katikati ya mji. Jengo hili lilikuwa na bwalo la mfalme kwenye ghorofa ya mfalme, ambalo lilikuwa na kuta zilizopambwa kwa michoro. Katika mwaka wa 1317 jengo hili lilifanywa msikiti, na Sayf al-Din

Abdallah, na ambao ulitumika kwa shughuli za kidini hadi 1969. Ndiyo bwalo peke yake la mfalme lililobaki salama katika eneo hilo lote ambalo hapo awali liliathiriwa na utamaduni wa Kibizenti. Yawezekana kwamba jumba hilo la mfalme lilifuata muundo wa ujenzi wa Kibizenti ambao ulikuwa umetumika katika kujenga ikulu kuu katika Konstantinople ambayo inafahamika katika maelezo tu.

Lakini, tunazo taarifa dhahiri zaidi kutoka Kaskazini mwa ufalme huo (uliokuwa Nobadia) zilizopatikana katika kampeni kabambe ya UNESCO (Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni) ya kuhifadhi minara ya makumbusho ya Nubia isifunikizwe na mafuriko ya Ziwa Nubia katika kipindi cha kuanzia 1961 hadi 1966. Faras, pamoja na kanisa lake kuu zuri, makanisa madogo, ikulu zake na nyumba za watawa, iliendelea kuwa na dhima yake kama makao makuu ya mambo ya kidini. Kutokana na Mnubia Kyros (866-902), ambaye picha yake kubwa imepamba kuta za kanisa kuu la Faras, kuchukua cheo cha uaskofu, Faras ikapanda na kuwa jimbo kuu la kiaskofu.

Huenda Faras pia ilibakia kuwa makao makuu ya utawala, makao ya mkuu wa jimbo (Gavana), ambaye alihusika pia na mawasiliano kati ya ufalme huo na Misri, pamoja na kuwa mkuu wa hazina. Makao ya mkuu wa jimbo (*Eparch*) baadaye yaliamishiwa kwenye ngome ya Kasr Ibrim.

Pamoja na kanisa kuu na majengo mengine ya mji, Kasr Ibrim imetoa mambo mengi muhimu ya ugunduzi na mamia ya vipande vya miswada yenye maandiko, yakiwemo maandiko ya kidini na ya kifasihi, barua na nyaraka.


Hali kadhalika mji mkubwa wa Gebel Adda, Kaskazini mwa Faras kwa upande wa mashariki ya Nili nao ulikuwa na umuhimu mkubwa. Miji hii miwili ilikuwa na maelfu ya wakazi, ambapo miji mingine midogo kama Kurta, Kalabsha, Sabagura, Ikhrindi au Shaykh Dawud ilikuwa imeimarishwa katika kipindi kilichotangulia na kulikuwa na mamia ya watu katika kila mji.

### *Hali ya kiuchumi na kijamii*

Pamoja na wingi wa mabaki ya kiakiolojia yaliyopo tuna taarifa kidogo sana kuhusu vipengee vingi vya ustaarabu wa Nubia. Makazi yaliyochunguzwa yanaonyesha sura ya ustawi na wakati huohuo jamii huru na yenye usawa ambamo tofauti za kitabaka hazikujitokeza katika mambo ya utamaduni. Ukulima kwa kiwango kidogo uliendelea kuwa msingi wa maisha. Tofauti na Misri, wakulima walikuwa wanalima mazao kadhaa kwa mwaka, mazao makuu yakiwa shayiri na mawele. Huenda tendele pia zilikuwa na umuhimu mkubwa katika uchumi. Mwanzoni wakulima walifuga ng'ombe, kondoo, punda na kuku; na baadaye nguruwe pia walifugwa.

Sehemu kubwa ya ardhi ilikuwa imegawanywa katika mashamba madogo madogo, lakini ukweli ni kwamba Wanubia walikuwa wakulima-wapangaji kwa sababu kisharia, ardhi yote ilikuwa ya mfalme. Kodi ya msingi ilitoka kwenye ardhi (pengine kulikuwa na kodi nyingine pia), na bila shaka wafanyakazi wa kanisa walitumika kama wakusanya kodi. Nyumba za watawa wa Nubia zilikuwa na mashamba ya kuwasaidia kwa chakula.

Sehemu za vijiji na miji midogo midogo zilikuwa zinajitosheleza kabisa na ufundi wa mikono wa Wanubia ulitosheleza karibu mahitaji yote ya kila siku. Kati ya vitu vilivyokuwa vinatengenezwa kwa wingi katika kipindi hiki cha kwanza kabisa ni vyombo vinavyotokana na ufynyanzi, vilivyokuwa vimerembwa vizuri sana na ambavyo vilikuwa bora zaidi ukivilinganisha na vyombo vya Kimisri vya wakati huo, na wala havikuwa vya kuiga tu. Mwisho wa karne ya nane ulishuhudia maendeleo ya aina mpya ya ufynyanzi wa vyombo vya kauri ambao ulitumia rangi nzuri katika kuremba na kuchora maua mazuri na picha za wanyama. Kanuni ya sanaa ya kiurasimi ya Kiukristo inaonyesha kufanana sana na ile ya wakati wa Kimeroe kuliko jambo lingine lolote wakati wa karne



8.2 Jengo la kifalme la Dongola ya Zamani, lilibadilishwa kuwa msikiti mnamo 1317 (Haitimiliki ya picha: Kituo cha Utafiti wa Uchimbuzi cha Mediterania, Akademia ya sayansi ya Pologne, Warsaw)





8.3 Picha ya Kyros, Askofu wa Faras (866-902): picha ya ukutani ya Kanisa Kuu la Faras (Haimiliki ya picha: Kituo cha Utafiti wa Uchimbuzi cha Mediterania, Akademia ya sayansi ya Pologne, Warsaw)

tano za katikati. Wakati fulani katika karne ya nane na mwanzoni mwa karne ya tisa, vifaa vya ufinyanzi vilivyoagizwa kutoka Misri vilipungua sana, hasa *amphorae* (chombo kilichokuwa kinatumika kuhifadha mvinyo au mafuta) zilizokuwa zinatengenezwa katika majumba ya watawa wa Kikhufu wa Misri ya Juu. Kushika madaraka kwa mfululizo kwa nasabatawala ya Waabbsi huko Baghdad kulizidisha mauaji ya Wakhufu na pia kulisababisha kuongezeka kwa vikwazo vilivyowekwa katika majumba ya watawa ya Misri.

Vijiji vingi vilikuwa vinatengeneza vifaa vya udongo kama vile magudulia ya kuhifadha vitu na vyungu vya kupikia au *kadus* - kifaa maalum kilichotumika kwenye *sakiya* (au gurudumu la maji). Ufinyanzi wa Kikristo wa kirasimi katika karne ya tisa na karne ya kumi ulitoshesha mahitaji yote nchini. Ilikuwa tu katika karne ya kumi na moja wakati, pamoja na vifaa vilivyotengenezwa, vingine vilianza kuagizwa kutoka Misri (vilipachikwa jina la bidhaa za Aswan), pamoja na vyungu vya Kiarabu vilivyorembwa ambavyo vilikuwa havijawahi kuigwa huko Nubia.

Ufundi mwingine muhimu katika kipindi hiki ulikuwa ni ufumaji. Bidhaa kuu zilizotengenezwa zilitokana hasa na manyoya ya kondoo au manyoya ya ngamia. Kanzu za manyoya ya kondoo za huko Nubia zilikuwa zimepambwa kwa mistari inayopishana yenye rangi zinazong'aa au wakati mwingine kwa rangi za mirabamiraba. Kufuatana na vitu vilivyogunduliwa, moja kati ya schemu maarufu zilizojiishughulisha na kazi hiyo, bila shaka, ni Kasr Ibrim.

Mafundi wa kazi za mikono wa Nubia walitengeneza pia vyombo vya chuma (majeinbe, visu, n.k.) pamoja na vifaa vya ngozi na vya aina zote za ususi. Vitu vya ususi vilitokana na nyuzi za minazi, utamaduni ulioendelezwa hadi hii leo.

Mbali na vitu hivi vilivyokuwa vinatengenezwa nchini, vitu vingine vya utamaduni vinadhahirisha utumiaji wa vitu vingi vya kigeni. Mbali na bidhaa zilizotajwa katika mkataba wa *bakt* (ngano, shayiri, mvinyo, kitani, majora ya nguo na nguo zilizoshonwa), Nubia ilikuwa inaagiza vyombo vya kioo vya aina mbalimbali kutoka Misri.

Biashara katika Nubia iliendeshwa kwa mfumo wa kubadilishana bidhaa. Hakukuwa na mfumo wa fedha, isipokuwa sehemu za Kaskazini ambako sarafu za Kimisri zilitumika katika kufanya biashara na Waarabu. Ndiyo kusema, katika biashara ya nje; Nubia ililazimika kulipa kwa fedha lakini shughuli za kifedha ndani ya nchi zilikuwa marufuku kama inavyoonyeshwa kwa kutumia mpaka mkali (kituo cha forodha mpakani), uliowekwa katika Maks ya Juu (Akasba), katika eneo la Batn al-Hajar lililokuwa linatenganisha eneo la biashara ya nje na eneo la biashara ya ndani ambako biashara ya nje ilikuwa chini ya udhibiti mkali wa mfalme. Bidhaanje ya Nubia ilikuwa hasa watumwa, lakini bidhaa za asili kama dhahabu, pembe, na ngozi bila shaka nazo zilikuwa muhimu katika biashara ya nje. Sehemu ya Dongola bila shaka nayo ilikuwa na mawasiliano, kupitia Kordafan na Darfur, na wafanyabiashara waliodhibiti njia za biashara katika nchi za Sudani ya Maghribi.

### *Historia ya siasa kuanzia karne ya tisa*

Katika mwongo wa tatu wa karne ya tisa, Nubia ilitumia vizuri mzozo wa nasabatawala uliokuwa katika Ukhalfa kwa kusimamisha malipo ya *bakt*. Lakini, mara tu al-Mutasim alipokuwa Khalifa alimwagiza mfalme wa Dongola, Zakaria, si tu kuendelea kulipa kodi ya kila mwaka, bali pia kulipa malimbikizo yote ya kodi. Mfalme, kwa kushindwa kutimiza matakwa hayo alituma mtoto wake mrithi wa ufalme, Georgios, huko Baghdad kushauriana na Khalifa (katika mwaka 835). Mkutano kati ya mwanamfalme wa Nubia na Khalifa ulikuwa jambo la pekee na ulimaanisha ushindi mkubwa

wa kiasia kwa upande wa ufalme wa Nubia ya Kiukristo. Mashauriano hayo yaliishia kwenye mkataba kati ya nchi hizo mbili ambao uliyatazama upya masharti ya *bakt*; na kuanzia wakati huo kodi hiyo ikawa inatolewa mara moja tu katika kila miaka mitatu.

Wakati wa ufalme mrefu wa huyu Georgios I (t. 856-915), machafuko makubwa yalitokea kufuatia shambulio la Abd al-Rahman al-Umari, Mwarabu aliyekuwa anatafuta dhahabu, ambaye pamoja na jeshi lake binafsi aliyateka kwa muda fulani machimbo ya dhahabu yaliyokuwa karibu na Abu Hamad. Baada ya kampeni ya muda mrefu iliyochochewa na hila za washiriki wa jamii ya kifalme ya Nubia ambao waliliongoza jeshi la Nubia, al-Umar alilazimika kuondoka na kuelekea katika nchi ya Beja ambako hatimaye aliuawa.

Shambulio la al-Umari halikuwa tamko rasmi la siasa ya Misri kwa Nubia, lakini hata hivyo, linaonyesha kuwa Waarabu walikuwa wakijaribu kuingia ndani zaidi katika Nubia kama ilivyokuwa katika mzozo na Beja, kwa kusudi la kuhakikisha kuwa upatikanaji wa dhahabu kutoka kusini hadi Misri haukuwa na kizuizi.

Yaelekea karne ya kumi ilikuwa kipindi cha ustawi katika nchi ya Nubia, kama ilivyokuwa katika nusu ya pili ya karne iliyotangulia. Ustawi huu yaelekea uliingiliwa kati tu na mafuriko makubwa ya Nili ambayo yalisababisha raia kuhamia katika baadhi ya sehemu za Nobadia. Lakini taifa la Nubia, likiwa na misingi yake madhubuti ya uchumi, liliweza kujitoa katika matatizo haya.

Katika mwaka 956 Nubia ilikuwa tena katika vita dhidi ya Misri. Lakini wakati huu si Waarabu waliokuwa wagomvi, bali Wanubia ambao waliishambulia na kuiteka Aswan. Jibu la Wamisri la shambulio hilo liliwapeleka Waarabu hadi Kasr Ibrim, lakini hawakufanikiwa sana.

Katika mwaka 962 Wanubia waliteka sehemu kubwa ya Misri ya Juu hadi Akhmim. Uvamizi huu bila shaka ulisababishwa na hali iliyokuwepo Misri katika kipindi cha Waikhshidi cha mwisho (936-968), na pengine hali hiyo ilikusudiwa kuwapa Wafatimi ushindi katika nchi hiyo; watu ambao baadaye Nubia iliendelea kuwa na mahusiano mazuri nao.

Kukaliwa kwa Misri na Nubia hakukumalizwa na kushika madamka kwa Ukhalifa wa Wafitimi katika mwaka 969, na huenda mipaka ya eneo hilo ilipangwa upya tu, hivyo Edfu ikaendelea kubakia Nubia. Hadi kufikia katikati ya karne ya kumi na moja, mji huu ulikuwa kituo muhimu cha utamaduni wa Kinubia. Habari nyingi tulizonazo kuhusu kipindi hiki zinatokana na maandishi ya Ibn Salim al-Aswani, ambaye, katika takriban mwaka wa 969, alipewa ujumbe kupeleka kwa mtawala wa Nubia, Georgios II. Mfalme aliupokea kwa shangwe ujumbe wa Kiarabu. Lakini, kwa kuwa Nubia wakati huo ilikuwa nchi yenye nguvu, mfalme alikataa kulipa kodi kama ilivyo katika *bakt* na hali kadhalika agizo la kutakiwa kusilimu.

Katika karne ya kumi, kanisa katika Nubia lilikuwa na jukumu kubwa sana katika mambo ya nchi; jambo hili linadhahirishwa na ukweli kwamba tume ya Waarabu ilipoletwa Dongola wakati wa utawala wa Georgios II, mfalme ahitisha baraza la maaskofu ili kujadili jibu la kuwapa Waarabu. Baadaye mfalme akawa mtu wa kati tu katika mambo yaliyohusu dini kama alivyoingilia kati katika ombi la viongozi wa Ethiopia, na Askofu Mkuu Philotheas (979-1003), kuhusu kuteuliwa kwa askofu wa jimbo Kuu la Ethiopia.

Kati ya majimbo saba ya kiaskofu ya Nubia yaliyotambuliwa na Waarabu, matano - Kurta, Kasr Ibrim, Faras, Sai na Dongola - yamethibitishwa na uchunguzi wa kiakiolojia. Taarifa zilizokamilika hasa kuhusu historia ya jimbo la kiaskofu ni zile za jimbo la Faras, ambapo, kutokana na orodha ya maaskofu walioandikwa kwenye ukuta mmoja wa kanisa kuu, mawe ya makaburi na maandishi mengine ya michoro, iliwezekana kuonyesha mfuatano usiotenganika wa wakubwa wa kanisa katika jimbo hili tangu mwanzo wake katika karne ya saba hadi mwaka 1175.

Sifa za Kimonofisita za kanisa la Nubia zinathibitishwa na taarifa nyingi kuhusu Faras na

majimbo mengine ya kidini. Kwa upande mwingine, ithibati iliyopatikana inaashiria kuwepo kwa mabadiliko fulani katika utii kwa uongozi mwishoni mwa karne ya kumi ambapo tunakuta kuwepo kwa maaskofu wa Pachoras wawili katika kipindi kimoja : Petros I (974-999) na Ioannes III (997-1005). Ufafanuzi wa kimantiki wa jambo hili unaweza kuwa kwamba Yoannes aliwakilisha imani tofauti na ile ya Monofisita Petros, Askofu Mkuu wa Faras, yaani imani ya Wagiriki ( ya Kimelki).

Yaelekea Wamelki walinufaika sana na kupendelewa katika Misri na Khalifa wa Kifatimi Al-Aziz na walifaulu kupata tena baadhi ya majimbo katika Nubia. Warithi wawili wa Yoannes wa kiti cha uaskofu katika Faras: Marionos (1005-1036) na Mercurios (1037-1056), waliitwa katika maandishi ya kutani "wanawe" - usemi unaozwa kufafanuliwa kwamba walikuwa na imani moja.

Mambo machache yanajulikana kuhusu hali ya litujia katika Nubia. Huenda Kigiriki kiliendelea kuwa lugha muhimu katika Kanisa na kuwa lugha ya mawasiliano katika ulimwengu wote wa Kiukristo wakati huo. Pamoja na Kigiriki, lugha ya Kikhufu ilikuwa inatumiwa sana katika maandishi ya kidini, katika maandishi rasmi na kwenye mawe ya makaburi.

Kuanzia katikati ya karne ya kumi na kuendelea Nubia ilionyesha kuongezeka kwa idadi ya matini katika lugha ya kienyeji ya Kinubia cha Kale (ambayo pia ilijulikana kama Kinubia cha kipindi cha Kati (Medieval Nubian), ambayo ni lugha-mama ya lahaja ya Mahas kando ya mto Nubia na iko katika kundi la lugha za Sudan ya mashariki. Kinubia cha Kale kimeandikwa katika alfabeti ya Kikhufu (ambayo nayo inatokana na ile ya Kigiriki), pamoja na kuongeza alama nne kwa ajili ya sauti mahususi za Kinubia.

Matini ya zamani kabisa yaliyothibitishwa katika Kinubia cha Kale ni maandikomchoro yaliyoandikwa katika mwaka wa 795 katika kanisa la al-Sebua na Petro, padre kutoka Faras. Yaliyoandikwa kwenye matini kwa lugha ya Kinubia cha Kale yanahusu hasa dini, lakini pia yana mambo muhimu sana kama nyaraka za kisharia na barua zilizopatikana hivi karibuni katika Kasr Ibrim. Haya yote yana umuhimu wa hali ya juu sana siyo tu kuhusu historia na dini, lakini pia kuhusu isimu, leksikografia maana ya Kinubia cha Kale na sarufi yake bado havijaelezwa vizuri na matini yaliyogunduliwa hivi karibuni bado hayajachapishwa.

Hakuna mambo mengi ya kihistoria yaliyopo kuhusu karne ya kumi na moja. Nubia iliingilia tena mambo ya Misri, wakati mwanzoni mwa karne hiyo, mwasi aliyeshindwa dhidi ya Wafatimi, Abu Rakwa, alipokimbilia Nubia na akafuatwa na jeshi la Khalifa. Lakini, kwa ujumla katika kipindi kirefu cha utawala wa Wafatimi katika Misri (969-1169), nchi mbili hizo zilikuwa na amani na zilidumisha mahusiano ya kirafiki. Hata Wanubia walikuwa wanaandikishwa katika jeshi la Wafatimi, ambamo idadi yao iliongezeka hadi kufikia 50,000 mwishoni mwa karne hiyo.

Baadhi ya wafalme wa Nubia walifaulu kuingilia kati katika kumsaidia Askofu Mkuu wa Kimonofisita katika Aleksandria, jimbo ambalo lilisumbuliwa mara kwa mara na mawaziri wa Kifatimi; jambo hili lilisababisha uimarishaji wa kanisa la Kimonofisita katika Nubia, ambako lilikuwa kwa wakati fulani katika wasiwasi wa kupoteza nafasi yake kama dini ya nchi.

Kutokana na kuanguka kwa Wafatimi (1169), mahusiano kati ya Nubia na Misri yakavurugika kwa haraka na enzi maarufu ya Nubia ikafikia mwisho wake karibu wakati huo huo. Wapiganaji wa kijeshi na vikosi vya Sultani wa Kiayyubi, Salah al-Din (Saladin), walifungua sehemu inayofuata ya historia ya Nubia ambayo inajulikana kwa jina la Kipindi cha baadaye cha Ukristo.

### *Sanaa na ujenzi*

Karne ya kumi na karne ya kumi na moja katika Nubia zilikuwa vipindi vya mafanikio katika maendeleo ya sanaa na ujenzi.

Mambo tuliyonayo ni mengi sana. Kulikuwa na zaidi ya makanisa 120 yaliyojulikana katika Nobadia na karibu 40 katika Makuria. Kwa muda mrefu ilichukuliwa kuwa ujenzi wa majengo matakatifu wa Kinubia ulitokana na aina ya kanisa la basilika *basilican* pekee, aina ambayo ilikuwa imeshamiri Kaskazini. Sasa inaelekea kwamba kulikuwa na mielekeo miwili iliyolingana katika ujenzi wa majengo matakatifu: mtindo wa kati na mtindo wa urefushaji wa kibasilika. Mtindo hiyo yote miwili iliathiri miundo ya kanisa. Mielekeo mikubwa katika ujenzi inaonekana kwanza katika majengo makubwa yaliyojengwa katika vituo vya utamaduni na utawala kama Dongola ya Kale, Faras au Kasr Ibrim. Ujenzi katika majimbo umefuata mitindo hiyo kwa kiwango fulani, lakini, kwa sababu ya uwezekano mdogo wa utendaji na vifaa, mitindo hiyo iliunda kilichoitwa 'aina ya ramani ya Kinubia' ya kanisa iliyoapatikana sana Kaskazini mwa Nubia katika Nyakati za Kiukristo za Urasimi na za Nyuma. Katika aina hii ya ujenzi viwakilisho vya ndani vya kienyeji vinaonekana.


Tunaweza kupamhanua vipindi vingi katika maendeleo ya ujenzi wa nyumba za ibada za Kinubia. Mwanzoni mwa kipindi cha kwanza, athari ya kigeni, hasa ya Kikhufu, ilijidhihirisha, na makarisa yalifuata plani ya makanisa marefu, yenye njia tatu, yanayofuata mstari mmoja, na kujengwa kwa matofali ya udongo na kufunikwa kwa dari za mti. Katika awamu ya baadaye, makanisa makuu maarufu yalijengwa kwa mawe yaliyochongwa au yaliyochomwa na yalifuata ramani ile ile. Utamaduni wa matofali ya udongo ya kujengea uukuwa unaendelezwa katika majengo madogo madogo na ni katika awamu hii ambapo aina ya kanisa la Kinubia, ambalo limekwishaelezwa hapo juu, lilipotokea.

Katika kipindi cha pili, maendeleo ya aina za makanisa zikiingiliana na athari za ujenzi wa Kiarmenia na Kibizenti, yalibadilisha kabisa maumbo ya maeneo katika ujenzi. Wakati huu mielekeo miwili ilitokea: wakati mtindo wa kiasili ulikuwa unaendelezwa katika majimbo, namna mpya na rasmi yenye kufuata plani ya kati katika ujenzi ilijitokeza katika mji mkuu. Matofali ya kuchoma yalikuwa yakitumiwa sana. Ujenzi wa Kinubia ulifikia kilele chake cha uwezo wa ubunifu. Moja kati ya mifano mizuri ya ubunifu katika ujenzi wa Kinubia ni Mausoleum (kanisa lenye umbo la msalaba) katika Dongola ya Kale, ubunifu ulitokana na plani ya msalaba wa Kigiriki. Katika kipindi hiki Dongola ikawa makao makuu ya shughuli za ujenzi.


Katika kipindi cha tatu, si rahisi kubainisha mtindo maalum ulioendelezwa katika uelekeo wa maendeleo. Shughuli za ujenzi zilisambazwa katika sehemu nyingi na zilichukuwa athari mbalimbali, hasa muundo ulitokea Ubizenti. Kipengee kilichojitokeza kote wakati huo kilikuwa kuanzishwa kwa paa za kuba kuelekea mwishoni mwa karne ya kumi. Ramani zote mbili za makanisa, yaliyorefushwa na yaliyofuata plani ya kati zilibadilishwa kwa kuongeza kuba katika sehemu ya katikati na kubadilisha nguzo za mawe kuwa nguzo za matofali. Matofali ya udongo yalitumiwa sana tena. Pamoja na kujenga upya makanisa ya zamani sana, mengine yalijengwa, kwa umbo lililotokana na urahisishaji mbalimbali pamoja na mabadiliko ya ubunifu wa Kinubia.

Mwishoni mwa karne ya nane, mapambo ya kawaida ya ndani ya majengo matakatifu yalikuwa picha zilizochorwa kwenye kuta. Michoro ya Faras ina - pamoja na picha nyingine za Ukristo na Bikira Maria - watakatifu na malaika wakuu, picha kutoka Agano Jipya na Agano la Kale, pamoja na sanamu za watukufu wa kienyeji ambao wanahudwa na watakatifu.

Mambo yaliyoapatikana Faras yamewezesha kubainisha na kuweka katika mfuatano orodha ya mitindo ya makundi mbalimbali ya uchoraji wa zamani. Uchoraji katika kuta wa kipindi hiki cha awali uliitua kizazi kipya cha wasanii wenyeji wa Nubia, ambao katika karne ya kumi wahanzisha shule yao ya upakaji rangi ambayo sifa zake kuu zilikuwa aina za urembaji ambapo vipengee vya kigeni vilivyogeuzwa kiufundi, vilitoa aina ya urembaji uliokuwa wa Kinubia pekee na uchaguzi wa rangi ambao ulibainisha kila kipindi. Kutokana na hali hiyo, mwanzoni mwa karne ya kumi, baada



8.4 Awamu ya pili ya maendeleo ya usanifu majengo wa makanisa ya Unubi. Juu: jengo la jadi la mkoa; kanisa la watawa la Ghazali na kanisa kwenye mteremko wa Kom, Faras. Katikati: mvendeleo wa mindo wa awamu ya kwanza, mfano wa mpango wa nafasi na sehemu ya kati (kanisa la minara ya matale la Dongola ya Zamani) au mchoro wa wima (kanisa kuu, Kasr Ibrim). Chini: mfano wa mindo mkuu, awamu ya pili, kaburi kuu la Dongola ya Zamani, kanisa la kimsalaba (P.M. Garkiewicz, 1982a)



8.5 Kipindi cha tatu cha maendeleo ya usanifu majengo ya kanisa ya Unubi. Mifano kutoka makanisa yaliyojua mitindo mbalimbali. Juu: athari ya makuba ya basilika (basilika ya Tamit). Mstari wa pili: athari ya mtindo wa kombe maradufu (kanisa la Nag'el Okba) au ruwaza ya msalaba katika mraba (kanisa la Sonki Tino). Mstari wa tatu: athari ya ruwaza ya kuba na msalaba (kanisa kuu la Faras, lililolengwa upya mwishoni mwa karne ya kumi, na Kanisa la Malaika la Tamit). Chini: athari ya ukumbi wenye mihimili mingi (Kanisa la Mt. Raphael la Kaw). (P.M. Gankiewicz, 1982a)

ya kupaka rangi upya tena ndani ya kanisa kuu mtindo mpya ulioitwa njano-nyekundu ulikuwa umechipuka. Baada ya ukarabati mkubwa wa kanisa kuu la Faras ambao ulifanywa mwishoni mwa karne ya kumi, mtindo wa rangi nyingi tofauti ulianzishwa. Huu ni mtindo mmojawapo kati ya mitindo iliyojulikana sana katika Nubia ya Kaskazini na ulidhihirika katika makanisa mengi, kama yale ya Abdallah Nirki, Sonki Tino na Tamit. Mfano mmoja maarufu wa sanaa hii mpya ni picha ya Askofu Marianos ambayo ilichorwa katika miaka ya mwanzo ya karne ya kumi na moja. Kazi maarufu ya sanaa inayoonyesha kuzaliwa kwa Yesu Ukristo, ambayo sasa iko katika Jumba la Makumbusho ya Taifa la Sudani huko Khartoum, inatokana na kipindi hicho. Huu rdio uchoraji katika kuta ulio mkubwa kuliko yote katika Nubia na unaonyesha vizuri jinsi wasanii wa Kinubia walivyo mahiri katika kuchora matukio ya sura nyingi kwenye picha moja. Mtindo wa rangi nyingi uliendelezwa hadi mwishoni mwa kipindi cha Ukristo kauka Nubia.


Kwa ujumla, katika uchoraji wa kupaka rangi wa Kinubia wa kipindi cha kirasimi cha Kiukristo, athari ya sanaa ya Ubizenti inaonekana (hasa kauka uenezi wa urembaji), ingawa haikuchukua nafasi yote ya vipengee vya Kikhufu vilivyokuwa vimeenea katika vipindi vilivyotangulia. Kitambulisho kikubwa cha sanaa hii kinaonyesha vipengee vya kienyeji vya usanii wa kuchora wa Kinubia peke yake.

Tawi hili la sanaa katika Nubia linadhihirisha ujuzi ulioboea wa mila za zamani za mawazo ya Kiukristo na Maandiko Matakaufu. Katika kilele chake, Nubia ilibakia kuwa mkondo muhimu wa Ulimwengu wa Kiukristo wa wakati huo (Christian *oikumene*). Kupitia mahusiano na mawasiliano yake (kama inavyoonekana walau katika sanaa ya kienyeji na ujenzi) siyo tu na Wakhufu wa Misri, na bila shaka Ethiopia, bali pia ulimwengu mzima wa utamaduni wa Kibizenti kuanzia Armenia hadi Shamu na Palestina, Nubia ilichota mawazo kutoka vyanzo hivi vyote na kujiundia utamaduni wenye haiba yake tofauti.





8.6 Mandhari ya kaskazini ya upande wa kanisa kuu la Faras na picha kubwa ya ukutani ya kuzaliwa kwa Kristo yenye rangi nyingi, iliyochorwa k. 1000. (Hatimiliki ya picha: Kituo cha utafiti wa uchimbuzi wa Mediterania, Akademia ya sayansi ya Pologne, Warsaw)



## *Kutamalakiwa kwa Afrika ya Kaskazini na ukinzani wa Waberiberi*

### *Waberiberi mwanzoni mwa utamalaki wa Waarabu*

Katika Juzuu la pili msomaji atakuwa amekwishapata mwanga kidogo kuhusu Waberiberi, chanzo chao, muundo wao wa kimbari na baadhi ya mila na desturi zao. Lakini, kwa kuwa hii ni sura ya kwanza kuhusu Maghrib (Afrika ya Kiislamu ya Kaskazini ukitoa Misri), itakuwa vizuri hapa kufahamisha msomaji jinsi Waberiberi walivyokuwa wakati Waarabu walipoingia kwa mara ya kwanza na kutamalaki Maghrib kuanzia mwaka wa 642 na kuendelea. Wakati huu, Waberiberi walikuwa na mfumo wao wa maisha, kama ule wa Waarabu wenyewe, uliojulikana kama  *kabila*. *Kabila* hizi zilikuwa zimegawanywa katika makundi mawili: Butr na Baranis.

Mwanahistoria wa Waberiberi, Ibn Khaldun, aliandika kwamba Waberiberi walikuwa wamegawanyika katika makundi mawili tangu enzi za wahenga, na kwamba kutoelewana na kushambuliana mara kwa mara ilikuwa kama desturi katika historia yao kabla na baada ya kuingia Uislamu.

Pengine kuainishwa katika makundi mawili kunaaweza kuwa kunaakisi hisia za Waberiberi wa Maghrib wenyewe kuhusu wahenga wao. Inaelekea wanasabu wa Kiberiberi na Kiarabu waliunda mgawanyo huu baadaye, lakini kwa kuzingatia mambo yanayotokana na uzoefu wa kihistoria.

Wakati wa utamalaki wa Waarabu, mashirikisho muhimu ya kimbari ya Wabutri yalikuwa yale ya Wazanata, Wamatghara na Wanafzawa. Inaelekea Wazanata walikuwa na mamlaka juu ya wengine, kwani inasemekana kwamba walizipa jina lao mbari zote za kinomadi za Butr.

Kuhusu Wabaranis, mashirikisho yao makubwa ya mbari wakati wa utamalaki huo yalikuwa yale ya Waawraba, Wahawwara na Wasanhaja.

Lakini tunapoanza kuchunguza utamalaki wa Waarabu na historia ya Afrika Kaskazini chini ya utawala wa Kiislamu, tunapata habari za kuzuka mbari mpya na vikundi vidogo vidogo vya kimbari ambavyo vilikuwa na umuhimu kuliko mashirikisho yaliyotajwa hapo juu.

Ili kueptuka kutokuwa sahihi, tutajuhusisha na muhtasari mpana wa mgawanyo wa kimbari wa Waberiberi wakati wa utamalaki wa Waarabu na baadaye, hadi kufikia karne ya kumi na mbili.

Wakati wa utamalaki wa Waarabu, Wabaranis walikuwa wamegawanyika katika makundi makubwa makubwa kadhaa kama vile Wasanhaja, Wakutama, Watakata, Waawraba na Wamasuda. Wazanata waliishi Sirenaika na Tripolitania, wakisambaa kuelekea kusini hadi Fezzan. Hapa mashirikisho muhimu ya kimbari yakiwa yale ya Wahawwara, Waluwata, Wanafusa na Wazaghawa.

Makundi haya pia yalitawala sehemu ya mashariki ambayo leo hii ndio nchi ya Algeria, eneolililokuwa linajulikana kama jimbo la al-Mzab wakati wa enzi za Waarabu. Yalichukua enco la

malisho katika miteremko ya Kaskazini ya milima ya Atlas ya Kati hadi Mto Muluya. Haya yalikuwa makazi ya kundi kubwa la kimbari lililojulikana kwa jina la Wamiknasa, ambalo lilisambaa kuelekea kusini hadi sehemu yenye rutuba ya oasisi za Tafilalet.

Wakutama na Wasanhaja waliishi katika Maghrib ya kati ikiwa ni pamoja na kundi la milima la Awras na nchi ya Kaba'il (Kabylic Kubwa), wakiwa na makazi yao karibu na sehemu za Tahert na Tilmsan. Hiki ndicho kilikuwa kitovu cha idadi ya makundi makubwa; Wakutama ambao walihusika katika kuunda Ukhaliifa wa Kifatimi; Wataalkata, waanzilishi wa falme mbili za Kiziri; na Waawraba, ambao walichangia sana katika kuanzisha falme za Kiidrisi Kaskazini mwa Moroko. Ibn Khaldun anaziita hizi *cabila* za Wasanhaja wa Moroko ya kati 'kizazi cha Kwanza cha Wasanhaja'. Kulikuwa na vikundi vingine vidogo vya Wasanhaja Maghribi mwa Maghrib, kikundi kikubwa kikiwa kile cha Wahaskura, walioishi katika Atlas ya Juu, katika nchi ya Masmuda: baadaye Wasanhaja walijiunga kijeshi na Wamasmda, muungano uliokuwa chanzo cha ufalme wa Wamohadi.

Kundi jingine la Wasanhaja liliishi katika sehemu inayoanzia kusini mwa jangwa la Wadi Dara (*Oued Dra*) hadi kwenye ukanda wa Sahara uliosambamba na pwani ya Atlantiki kuendelea hadi mto Senegal. Mbari zao kubwa zilikuwa Walamtuna, Wamassufa, Wajuddala, Wagazula (Jazula), Wabanu Warith, Walamta na Watarka. Kwa hakika hii ya mwisho ilikuwa kwa kweli ya Watuareg (al-Tawarik), watu maarufu sana, ambao wameendelea kuwa watawala wa Sahara kuu hadi wakati wetu. Makundi haya yote yalikuwa ya wanomadi wafuga ngamia. Ibn Khaldun analiita kundi hili la Wasanhaja 'kizazi cha pili cha Wasanhaja'.

Aidha, kundi muhimu la Wabaranis ni liie la Wamasmda au Wamasamida. Walitawala takribani Maghribi ya Maghrib nzima isipokuwa vikundi vichache vya Wasanhaja na Wazanata. Matawi makubwa ya kundi hili yalikuwa Waghumara (katika sehemu ya Tangier kupitia Rif), na Wabarghwata, ambao pamoja na Waawraba walitawala bonde la Sebu. Wamasamida waliishi katika sehemu za milima ya Atlas ya Juu na mlolongo wa milima ya Anti-Atlas pamoja na uwanda wenye rutuba, wa Sus, ambao uko katikati ya mlolongo miwili ya Atlas kusini mwa kundi la milima ya Sirwa. Hawa ndio walikuwa waanzilishi wa chama cha kidini na ufalme wa Wamohadi mambo ambayo yaliunganisha Maghrib na Hispania. Miongoni mwa mbari kubwa katika kundi hili ni pamoja na Wahintata, Wahaylana (au Waaylana, Waurika, Wahazarja, Wamasfiwa, Wadughgha, Wahargha, Waahl-Tin mallal, Wasawda, Waganfisa, Wabanu, Wawawazgit, Wafatwaka na Wamastana.

Bila shaka, yaliyoelezwa hapo juu ni muhtasari wa kijuujuu tu wa Waberiberi na mbari zao wakati Waarabu walipofika Kaskazini mwa Afrika. Baadhi yao walipingana na Waarabu, ambapo wengine waliwakaribisha na kushirikiana nao na kusilimu katika kipindi kirefu cha utamalaki.

Aidha hakuna haja ya kumkumbusha msomaji kwamba karibu mbari zote hizi zilikuwa na dini ya kimapokeo (ya jadi). Wanahistoria wa Kiarabu wanawaita *Majus*, yaani 'Waabudu moto', lakini kwa kawaida neno hili lina maana ya wapagani kwa jumla.

Ukristo ulikuwa haujaenea miongoni mwa Waberiberi; ni wakazi wa pwani tu waliopewa jina la *al-Afarika* na Waarabu ndio walikuwa Waukristo. *Waafarika* walikuwa watu wa pembezoni, mchanganyiko wa Waberiberi waliochukua utamaduni wa Warumi na Wakariteji, Warumi na Wagriki. Miongoni mwa Waberiberi halisi, Ukristo ulienea kidogo. Isitoshe, Waukristo wa Afrika ya Kibizenti walitenganishwa na mifarakano ya kidini; kwa Waberiberi hawa Ukristo ulikuwa kiini cha umoja dhidi ya utawala wa Kirumi, na waliyapokea mafundisho yanayopingana na ya Kirumi kwa mikonno miwili kama yale ya Uariani (Arianism) na Udonati (Donatism) ambayo yalipinga itikadi ya kanisa la Ruma.

Dini ya Kiyahudi pia haikuwa na umuhimu ambao baadhi ya waandishi wameipa; hata hivyo ilikuwa imeenea Afrika ya Kaskazini. Wazawa wengi wa Kiyahudi wa Afrika ya Kaskazini kote wanatokana na hao wafuasi wa dini ya Kiyahudi kabla ya Uislamu.

### *Kutamalakiwa kwa Sirenaika na Tripolitania*

Katika mwaka wa 641, mkataba wa Aleksandria ulisainiwa kati ya Amr ibn al-As na Kiongozi Mkuu Cyrus, Gavana wa Kibizanti wa mwisho huko Misri na kuthibitisha kwamba nchi yake ilikuwa imetekwa na Waarabu. Baadaye kidogo, tarehe 17 Septemba 642, askari wa mwisho wa Kibizanti waliondoka Aleksandria.

Lakini Amr ibn al-As, aliyeitamalaki Misri, alifikiri kwamba ililazimu achukue Sirenaika (Barka) pia. Tangu kuundwa upya kwa himaya hiyo kulikofanywa na mfalme Maurice (582-602), Sirenaika ilikuwa sehemu ya jimbo la Misri, kama ilivyokuwa Tripolitania. Amr alifikia Sirenaika mwanzoni mwa mwaka 643, na kuiteka karibu bila kipingamizi chochote.

Hakukuta Wagriki wala Wabinzenti wa kumpinga isipokuwa makundi ya Waberiberi ya Waluwata na Wahawwara. Hawa, baada ya kusalimu amri walikubali kulipa kodi ya dinari 13,000 kila mwaka, ambayo tokea hapo ilikuwa sehemu ya kodi iliyokuwa ikilipwa na Misri.

Wakati huo huo, Amr alituma naibu wake Nafi ibn Abd al-Kays kuiteka Zawila, oasisi ndogo kati ya Sirenaika na Fezzan, lakini muhimu sana, yenye maji, katika njia ya kuelekea kusini.

Mwaka mmoja baadaye, wapiganaji wa Kiarabu wakiongozwa na Amr ibn al-As walirudi kuendeleza utamalaki wa Afrika ya Kaskazini. Lengo lao lilikuwa Tripoli ambayo ilikuwa sehemu ya Misri ya Kibizanti. Amr aliteka Tripoli katika mzingiro mfupi na baadaye jeshi lake likashambulia Sabra au Sabrata, na kuteka Waddan, oasisi kubwa sana katika bara ya Tripoli. Kutekwa kwa Waddan kulimaanisha kuchukuliwa kwa sehemu yote ya milima ya Nafusa, ngome ya shirikisho la kimbari la Nafusa.

Amr ibn al-As alikuwa amemaliza kazi ya kutamalaki Misri. Mipaka ya Maghribi ya eneo lake ilikuwa imepatikana. Mbele ya mipaka hiyo kulikuwa na jimbo la Kibizanti la Bizasena, ambalo lilikuwa karibu sawa na Tunisia ya leo.

### *Uvamizi wa kwanza katika Ifrikiya*

Katika mwaka wa 647, Abd Allah Ibn Sa'd, gavana mpya wa Misri, aliongoza shambulio katika Byzasena na jeshi la wapiganaji wapanda farasi mashuhuri 20,000. Gavana wa Afrika ya Kibizanti alikuwa Gavana wa kijeshi Gregory, ambaye miaka michache iliyopita alikuwa amekwisha jitangazia uhuru; gavana huyo aliondoka Kariteji na kwenda ndani ya nchi katika ngome ya Suffetula. Vikosi vya Waarabu vilipofika Tripoli, alitayarisha wapiganaji wengi. Mapigano makali yalitokea mahali si mbali sana na Suffetula, sehemu iliyoitwa na Waarabu Sbeitla (Subaytula); ambapo Waarabu walipata ushindi. Gavana wa kijeshi Gregory aliuawa, binti yake alikamatwa pamoja na jamaa wake wengine wengi alikuwa akiishi nao, na hatimaye Sbeitla ilichukuliwa. Wabinzenti waliobaki walikimbilia Kariteji, Sus (Hadrumetum) na bandari nyinginezo, na wengi walihama Afrika bila matarajio ya kurudi.

Baada ya ushindi, vikosi vya Kiarabu vilishambulia sehemu zote za nchi. Waliteka maelfu ya watu kiasi kwamba raia walimsihi Abd Allah ibn Sa'd apokee fidia kubwa ili aondoke. Alikubali na kuondoka. Kampeni hiyo ilimalizika mwanzoni mwa mwaka wa 649.

### *Awamu ya Pili ya Utamalaki*

Kampeni hizi zilizofanywa na Amr ibn al-As pamoja na Abd Allah ibn Sa'd zinaweza kuchukuliwa



9.1 Kutamalaki kwa Waarabu Magharib. (I. Hrbek)

kama utangulizi au sehemu za matayarisho ya utamalaki wa Afrika Kaskazini.

Wakati huu, Waarabu walikwishapata undani wa sehemu hiyo pamoja na wakazi wake; kikosi cha kudumu kiliwekwa Barka na kikosi kidogo kilikuwa huko Waddan.

Lakini mipango ya Waislam ya kutamalaki ilifizwa karibu kwa kipindi cha miaka kumi na miwili kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyokuwepo baina ya Waarabu wenyewe kuanzia katikati ya kipindi cha ukhalifa wa Uthman (644-656) hadi kushika madaraka ya Ukhalfi kwa Muawiya ibn Abi Sufyan mwaka 661.

Mara tu amani iliporejea katika Ufalme wa Waarabu, Muawiya, mwanzilishi wa utawala ya Umayya, aliamua kwamba utamalaki uendelezwe katika pembe zote. Katika mwaka 663, alimteua Ukba ibn Amir al-Juhani kuwa Gavana wa Misri, na Muawiya ibn Hudayj al-Sakuni kuwa Kamanda Mkuu wa Majeshi ya Kiarabu ambayo yalipewa jukumu la kuendelea tena na utamalaki wa Maghrib.

Wakati huu hali ya mambo ilielekea kuwafaidia zaidi Waarabu barani Afrika. Kwa kutumia vizuri kutokuwepo kwa Waarabu, Wabizanti walikuwa wamejaribu kuimarisha tena utawala wao hapo. Gavana wa Kijeshi mpya, kutoka ukoo wa Watawala wa Kirumi, Nicephorus, alitaka watu wa jimbo hilo walipe kodi iliyokuwa sawa na fidia iliyokuwa inalipwa kwa Waarabu. Kwa vile raia walikataa, kwa sababu hawakuwa na uwezo wa kupata kiwango hicho, kukatokea mvutano ambao ulisababisha mapambano ya silaha. Wakati huo katika mwaka wa 655, jeshi la Muawiya ibn Hudayj lilitokea na kupambana nao. Alimshinda Nicephorus kwa urahisi na kumlazimisha kutafuta hifadhi huko Hadrumetum (Sus). Lakini katika muda mfupi Waarabu waliitaka Sus na kumlazimisha Nicephorus kukimbia haraka na kwa mfululizo, ndipo Waislamu walipochukua maeneo ya jalula (Cululis), Bizerta, na kisiwa cha Jerba. Katika mwaka wa 666 walithubutu hata kujaribu kwa mara ya kwanza kushambulia pwani ya Sisilia.

Katika mwaka wa 670, Khalifa Muawiya alimvua madaraka Ibn Hudayj na kumteua Ukba ibn Nafi kuwa Kamanda Mkuu wa Majeshi ya Kiarabu Kaskazini mwa Afrika. Uteuzi huu utilenga kuimarisha utamalaki.

Akitokea Waddan, Ukba aliendesha mashambulio mapana, kwa kupitia Fazzan na kusini mwa Kavar hadi mpakani mwa nchi ijulikanayo hii leo kama Jamhuri ya Chad. Alikuwa makini katika kuanzisha utawala wa Kiislamu, kwa kujenga misikiti na kuacha kambi za jeshi na wamisionari. Kisha akaenda Kaskazini tena hadi Ghadames. Alianza kwa kushambulia ngome za mwisho za Kibizanti zilizokuwepo katikati ya Gabes (Kabis) na sehemu ambayo alikusudia kuifanya kituo cha majeshi na makao makuu ya kisiasa (*misr*) ya jimbo lake. Bila kuehelewa, alianzisha ujenzi wa makao yake makuu aliyoitia Kayrawan, inayomaanisha 'Kambi' au 'Ghala kubwa la kuwekea silaha na zana za vita.'

Kuanzishwa kwa Kayrawan, moja ya miji ya zamani sana na inayoheshimiwa ya Kiislamu, jimbo la kwanza la Kiislamu la Afrika Kaskazini lilizaliwa. Lilipewa jina la Afrika (*Ifrikiya*). Wakati huo, lilichukua eneo lililokuwa karibu sawa na eneo la sasa la Tunisia.

Ukba alianza kutayarisha kampeni mpya, lakini mwaka 675 aliachishwa ukamanda. Mrithi wa cheo chake, Dinar ibn Abu al-Muhajir ambaye alichukua nafasi hiyo kuanzia 675 hadi 682, alijidhirisha kuwa mmoja miongoni mwa watu mashuhuri na wenye akili waliowahi kuongoza utamalaki wa Kiarabu katika Maghrib. Wakati huo huo hali ilikuwa inagotika kuwa mbaya kidogo kwa upande wa Waarabu. Mfalme wa Ubizanti Konstantini IV (Pogonatus) alikuwa amekwishapata ushindi dhidi ya shambulio kubwa la kwanza la Waarabu na mzingiro wa Konstantinople iliyokuwa imechukuliwa wakati wa utawala wa Khalifa wa kwanza wa Kiumaya, Muawiya. Konstantini alidhamiria kutumia ushindi huo kurudisha sehemu za nchi yake zilizokuwa zimechukuliwa.

Alirudisha Kupros na baadhi ya visiwa vya Aegean, na kutuma wajumbe wa kuimarisha tena uhusiano na Wabizanti waliobaki huko Kariteji na sehemu nyingine za jimbo la zamani. Kwa hiyo wajumbe walilakiwa na kukubaliwa na kiongozi mashuhuri wa Kiberiberi, Kusayla, chifu wa Waawraba na wa shirikisho la mbari za Wasanhaja lililokuwa likitawala Maghrib ya kati yote.

Abu al-Muhajir alifanikiwa kumshawishi Kusayla kwa kumwambia kwamba kama angefuata imani yake na kumuunga mkono katika kuitetea, yeye na mbari yake wangukuwa wafuasi wa jamii ya Kiislamu.

Kusayla na watu wote wa mbari yake walipokea imani ya Kiislamu. Tukio hili lilitokea mwaka wa 678, tarehe isiyosahaulika katika historia ya kusimilisha. Mwaka uliofuata, Abu al-Muhajir, akisaidiwa na mshiriki wake shupavu alivamia na kutamalaki musoma unaojulikana leo kwa jina la Iklibiyya, akashambulia Kariteji, na akaiteka Mila, msingi wa ngome ya Wabizanti iliyokuwepo umbali mdogo Kaskazini mwa Sirta (Konstantini ya leo).

Baadaye kidogo, Abu Al-Muhajir alirejeshwa nyumbani na Ukba akateuliwa tena kuwa Gavana wa Ifrikiya. Uteuzi huu kwa mara ya pili wa Ukba ibn Nafi lilikuwa jambo muhimu la kwanza kabisa katika kutamalaki kwa Waarabu Afrika Kaskazini. Mara tu baada ya kushika wadhifa wake huo Ukba alitangaza nia yake ya kuingiza Uislamu katika eneo lote la Maghrib na moja kwa moja akaendesha mashambulizi kuanzia Kayrawan na wapanda farasi 15,000 na maelfu ya Waberiberi wa Kusayla.

Katika muda mfupi wapiganaji wa Kiislamu waliokuwa wakiingia katika Milima ya Awras, walipata ushindi mkubwa sana kwa kuteka miji mingi kama vile Baghaya na Masila, na kwa kuzishinda mbari za hapo za Waberiberi. Na hata muungano mkubwa ulioundwa na Walawata, Wahawwara, Wamatmata, Wazanata na Wamiknasa kutoka Maghrib ya kati haukuweza kuyakabili majeshi ya ushindi ya Ukba hadi wakashindwa vibaya sana katika eneo karibu na Tiaret (Tahert).

Ushindi huu ulimpa Ukba sifa ya kuwa ni mtu ambaye hawezi kushindwa kamwe. Kwa kudanganywa na vitendo hivi, maelfu ya Waberiberi walipokea Uislamu na kujiunga na jeshi lake kwa wingi. Lakini Ukba alifanya kosa kubwa la kisiasa: kinyume na ushauri wa Abu al-Muhajir, alivamia na kupora sehemu ya karibu na Tilimsan, makao ya Kusayla na watu wake wa Awraba, ingawa walikwisha kuwa Waislamu na mtawala alikwishaingia urafiki wa shirika naye. Bila shaka *Kusayla* alighadhikika, lakini aliahirisha kulipiza kisasi hadi wakati unaofaa.

Katika hatua iliyofuata ya kampeni yake, Ukba alivuka Moroko ya sasa na kujiimarisha katika mbari nyingi za Waberiberi na kuingia kusini hadi Wadi Dara na Tafilalet na kuanzisha misikiti katika maeneo mengi. Alifika pwani ya Atlantiki huko Safi, Kaskazini mwa Mogador, karibu na kijiji cha Ighiran-Yatuf (Cap Guir). Pale, kwa mujibu wa hekaya za maeneo hayo, alipanda farasi hadi baharini na kusema kwamba alikuwa amefikia mwisho wa dunia kwa kumpigania Mungu na kama hakuendelea mbele ilikuwa kwa sababu hakukuwa na ardhi nyingine zaidi ya kushika na kuingiza katika himaya ya Uislamu.

Lakini safari ya kurejea kwake ilikuwa mkasa. Askari wake walikuwa wamechoka, na baada ya mapigano marefu walikuwa na haraka ya kurudi kuona familia zao tena; Ukba aliwaruhusu waliotaka kutangulia; mwishoni alibakia na askari 5,000 tu. Huu ulikuwa wakati ambao Kusayla alikuwa anausubiri kulipiza kisasi. Walipofikia sehemu ya Tilimsan, makao yake, alianza kambi ya Ukba na kukimbilia katika sehemu ya kati kabisa ya milima ya Atlas ambako aliwasiliana na Waukristo waliokuwa wamekimbilia huko na alifanya nao mkataba wa kumsubiri Ukba katika uwanda wa nchi karibu na Tahudha, kuelekea kusini mwa Biskra. Ukba alijikuta amezingirwa na askari takriban 50,000. Akadhahirisha ushujaa wa hali ya juu uliulingana na hadhi yake: akaweka silaha chini pamoja na Abu al - Muhajir na wenzake, akatoa sauti ya kuisha kwa adui wake na

kuwafuata, na ndipo alipouawa. Karibu watu wake wote waliuawa (Agosti 683). Mwisho huo wa tanzia wa jemedari wa Kiarabu ulimfanya awe mtakatifu na shahidi wa dini (*mujahid*). Kaburi la Sidi Ukba likawa sehemu takatifu inayoheshimiwa katika Afrika ya Kaskazini nzima.

Habari za tanzia hii ziliishitua Maghrib nzima. Katika Kayrawan, Waislamu walijawa na woga. vikosi vya jeshi vilikimbia kuelekea mashariki. Kusayla alikwenda Kayrawan na kuiteka. Hakuiacha imani ya Kiislamu lakini alijitangaza kuwa gavana.

Kwa mara ya kwanza katika historia, Ifrikiya ikatawaliwa na Mberiberi halisi: Kusayla, chifu wa Waawraba.

### *Mwanzo wa ukinzani wa Waberiberi*

Kampeni ya Ukba ilikuwa na athari mbaya moja muhimu: Waberiberi waligundua kwamba mashambulizi ya Waarabu yaliwalenga wao na wala hayakuwalenga tu Wabizenti. Sasa ilidhihirika kwamba lengo la Waarabu lilikuwa kuwameza Waberiberi na nchi yao na kuwaingiza katika Uislamu. Ingawa Waberiberi wengi hawakupinga kuupokea Uislamu, lakini watawala wao hawakutaka kumezwa na dola ya nje. Ushindi wa Kusayla ni mfano dhahiri wa kwanza wa hisia hiyo: alikuwa rafiki na mshiriki wa gavana wa Kiarabu Abu al-Muhajir, lakini alikataa kuwa mtumwa wa nguvu za nje. Kwa upande mwingine Waumaya hawakuwa tayari kuacha mamlaka ya jimbo jipya katika utawala wa chifu asiyekuwa Mwarabu hata kama alikuwa Mwislamu.

Katika mwaka wa 688 Khalifa Abd al-Malik (685-705) alimteua Zuhayr ibn Kays kuongoza vikosi vya kuendeleza utawala wa Kiarabu katika Maghrib.

Kusayla, aliyekuwa ameunda ufalme wa Kiberiberi uliotanda hadi Awras, eneo la kusini mwa Konstantini, na sehemu kubwa ya Ifrikiya (687-90), alijisikia kuwa katika hali isiyo na usalama alipojua kuwa jeshi jipya la Kiarabu lilikuwa linamjia. Aliamua kumsubiri adui huko Mamma, kijiji kidogo kinachokaliwa na Wahwwara, kilichoko kati ya Kayrawan na Laribus.

Mapigano ya Mamma yalikuwa makali na ya uhakika. Waarabu waliwashinda Waberiberi (690), Kusayla aliuawa na watu wake waliumizwa vibaya. Waawraba ambao wakati huo walikuwa moja kati ya mbari za Kiberiberi yenye nguvu sana waliangamizwa. Waliihama eneo karibu na Tilimsan na kukaa Kaskazini mwa Sebu, karibu na mji wa Wulili (Volubilis).

Zuhayr hakufurahia ushindi wake kwa muda mrefu; kundi la Wabizanti likitumia mwanya mzuri wa mapigano ya Waarabu na Kusayla, lilifika huko Barka na kuiteka. Zuhayr na kikosi chake cha mstari wa mbele aliwafuata, akifuatiwa nyuma na jeshi lake lote, lakini aliuawa katika mapigano. Ilipita miaka minne kabla ya Khalifa kutuma vikosi vipya katika Ifrikiya chini ya Gavana mpya Hassan ibn al-Numan, aliyeunda jeshi kubwa na kuchukua kodi za mapato za Misri zote ili kuharamia vita vyake; lengo lake lilikuwa kutamalaki kabisa Maghrib bila kuacha eneo lolote.

Lengo la kwanza la Hassan lilikuwa kuwashinda Wabizenti ili kuzuia muungano wao na Waberiberi. Baada ya kufika Kayrawan alikwenda Kariteji na kubomoa bandari yake ili isituniwe na meli za Kibizenti. Wengi wa Wabizenti walikimbilia visiwani katika Mediterania. Kulikuwa na mapigano makali karibu na Istafura (au Satfura) na kwenye musoma (mkono wa nchi) ambako kulikuwa na Hippo Diarhytus (Bizerta), Hippo Regius (Bone, sasa Annaba), na Tabarka; makoloni haya yote ya Wabinzenti na ngome vilichukuliwa na Waarabu.

Alipokwishatimiza lengo hili, Hassan alifikiri kwamba jukumu lake la kijeshi lilikuwa limekwisha, na akaanza kushughulikia ujenzi wa nchi; lakini kabla ya yote mkasa mpya ulijitokeza. Mwanamke wa Kiberiberi ambaye Waarabu walimwita *al-Kahia*, 'padre wa kike' au 'nabii', jumbe wa mbari ya Jarawa katika milima ya Awras, alikuwa amekwishakusanya watu wote wa sehemu ya



Zanata na kutangaza kwamba angewaondoa Waarabu katika Ifrikiya. Mwanamke aliyegopwa, nusu malkia, nusu mchawi, al-Kahina - kwa kuwa ni kwa jina hili la Kiarabu ameweza kuingia katika historia - ni moja kati ya watu ambao hekaya zinawasisimulia.

Kama chifu wa kabila la Wazanata, hakupendezwa kabisa na ushindi usiotarajiwa wa Kusayla, chifu wa Wasanhaja ambaye alikuwa ameimarisha utawala wake katika sehemu inayopakana na ya kwake. Sasa kwa kuwa Waarabu waliokuwa wamekuja walikuwa wamewashinda Wasanhaja na walikuwa wanatishia kupanua utawala wao katika Maghrib nzima, wasiwasi ulizidi na alinua kuwapinga vikali wavamizi wa Kiarabu.

Mara Hassan alimshambulia adui yake mpya. Al-Kahina alitegemea kwamba Waarabu watajaribu kuchukua Baghaya, ambapo pangukuwa mahali pazuri pa kuanzia kumshambulia katika Awras; kwa hiyo alichukua mji huo na kuzuia njia yoyote ya kuingilia ndani.

Katika mwaka wa 696 Hassan akawashambulia na Wajarawa wakapigana vikali kiasi cha kuwarudisha nyuma Waarabu wakiwa wameacha nyuma mamia ya maiti na mateka karibu themanini. Hassan alikwenda kujenga upya jeshi lake huko Barka. Al-Kahina, akiwa ameridhika na ushindi wake alisimama na kuweka kambi yake milimani hadala ya kuelekea Kayrawan.

Akiwa na mawazo kwamba Waarabu walikuwa wanataka kuteka nyara vitu tu, aliamua kutumia 'siasa ya kuangamiza mazao ya shambani' na mazaotote yaliyokuwepo kati ya Awras na Ifrikiya yaliangamizwa. Tendo hili lilifanywa wakazi wa kudumu wamegukie Al-Kahina, na Hassan alionbwa aje kuwaokoa. Mwaka uliofuata, (697) mambo yaliharibika; mfalme wa Ubizenti Leon (695-698) aliwatuma watu wakaja kucepeka Kariteji na kuwaua Waislamu wengi huko.

Khalifa Abd al-Malik, kwa kuchoshwa na mapambano ya kutamalaki Afrika yasiyomalizika akaamua kufanya mapambano ya mwaka. Jeshi ambalo Hassan alipigana nalo dhidi ya Al-Kahina lilikuwa kubwa kabisa kuzidi jeshi lolote lililowahi kupatikana katika sehemu hii; vikosi vya Kiarabu vilisaidiwa na maelfu ya Waberiberi.

Pambano la mwisho kati ya Hassan na al-Kahina lilifanyika katika mwaka wa 701. Malkia aliuawa na wafuasi wake walitawanywa. Waberiberi wa Awras waliomba kulindwa katika himaya ya Kiarabu. Walikubaliwa kwa msingi kwamba wangetoa wapiganaji katika majeshi ya Kiarabu. Watu elfu kumi na mbili walilipelekwa kwa Hassan ambaye aliwaweka chini ya ukamanda wa watoto wawili wa malkia aliyeshindwa. Hawa wapiganaji wote pamoja na hao watoto wawili wa malkia waliingia katika dini ya Kiislamu.

Kwa kuhakikisha kwamba Wabizenti hawataweza kamwe kurudi, Hassan alitoa amri ya kuharibu kabisa Kariteji. Jambo hili lilifanywa katika mwaka wa 702; hadithi ya jiji hili lilokuwa maarufu wakati wake iliishia hapa.

Badala yake, Hassan alianzisha bandari nyingine mahali pa Tarshish ya zamani, ambayo ndiyo Tunis ya sasa. Katika miaka ya baadaye bandari hii ikawa kituo muhimu cha bahari na biashara cha jimbo la Ifrikiya.

Jimbo hili lilijumuisha pia sehemu ya Tripolitania (Tarabulus), Ifrikiya yenyewe, kuanzia Gabes hadi Annaba, na sehemu ya Mzab kuanzia Annaba hadi matawi ya juu ya mto Shelif, kusini mwa Algiers. Maghribi ya mto Shelif kulikuwa na Maghrib ya kati na mbele yake kulikuwa na Maghrib ya Maghribi. Kinadharia, maeneo haya yalikuwa chini ya ufalme wa Kiislamu, lakini hakukuwa na utawala wa Kiarabu katika sehemu hizi wakati huu.

Hassan alilitawala jimbo lake la Ifrikiya kwa misingi ya mfumo wa kiutawala uliokuwepo katika ufalme wa Kiislamu. Katika ngazi ya juu ya kila jimbo kulikuwepo na gavana (*amil*), ambaye alijichagulia makamu wa gavana (*wali*) kwa kila wilaya. Kodi zilikuwa zinatozwa kwa kiwango cha karibu ya asilimia kumi ya mapato ya mtu. Katika Ifrikiya, ambako karibu hakukuwa na Wayahudi

au Waukristo wa kutozwa kodi ya kichwa (*jizya*), chanzo hiki muhimu cha aina yake cha mapato katika sehemu nyingine, kilikuwa kama hakikuwepo.

Ifrikiya ilikuwa kama Arabia, kwa vile katika sehemu zote mbili kulikuwepo uongozi wa kijamii wa aina ya kimbari. Serikali ililazimisha kodi ya asilimia mbili ya uchumi wa kila kabila kwa kuhesabu ngamia au kondoo. Hii ilikuwa *sadaka*, na mkusanyaji alijulikana kama *Musaddik*. Lakini, kwa kuwa serikali ilikuwa inamteua hakimu (*kadhi*) kwa kila kundi la kimbari na kuwatuma wamisionari au walirnu wa kuwaclimisha raia katika misingi ya Kiislamu na kuongoza wanaoswali, kwa wastani hakukuwa na mapato yaliyokuwa yanatoka katika mbari, kwa kuwa hawa wafanyakazi mbalimbali wa serikali walikuwa wanalipwa kutokana na michango ya wenyeji hao (*sadakat*).

Kwa hali yoyote ile, Hassan aliweka mfumo thabiti wa utawala katika jimbo lake kiasi cha kulifanya liwe msingi wa ujenzi wa himaya na utukufu wa Kiarabu katika Afrika Kaskazini nzima. Kayrawan, makao makuu yake pamoja na msikiti wake maarufu, ziligetka kuwa moja ya vituo muhimu vya Kiislamu vya kufundishia dini na utamaduni.

Inaweza kusemekana kwamba wakati huu Ifrikiya nzima ilikuwa ya Kiislamu; raia wake polepole wakaanza kutumia lugha ya Kiarabu kutokana na idadi kubwa ya Waarabu waliokuwa wakiishi huko.

### *Kutamalaki magharibi ya Maghrib*

Hassan ibn al-Numan hakukaa katika madaraka kwa muda mrefu ili kumaliza kazi yake. Mnamo mwaka wa 704 nafasi yake ilichukuliwa na Musa ibn Nusayr, ambaye alikuja katika Ifrikiya na vishindo vya nguvu ingawa alikuwa mzee; alitaka kuivamia Maghrib ya kati na ya Maghribi, na alikusudia kuteka vitu vingi kutoka huko. Kwa bahati mbaya, Maghrib haikuwa na kitu chochote ukilinganisha na ghala za dhahabu na madini ya thamani kubwa zilizotekwa katika Iran na Iraki zilipotamalakiwa. Hapa hapakuwa na kitu isipokuwa watu, familia zao na makundi yao ya mifugo.

Lengo la kampeni yake kwanza lilikuwa ni (kutiisha) maeneo ya baadhi ya vijikundi vya Wahwwara na Wadjarawa ambao walikuwa hawajaonyesha utii. Alifanya shambulio kali na kuchukua mateka wengi. Pigo hilo lilileta woga miongoni mwa mbari kutoka mwisho wa upande mmoja wa Atlas ya Kati badi mwisho wa upande mwingine. Walipoanza kukimbia kuelekea Maghribi ya Maghrib, Musa aliwafuata. Baada ya kuteka idadi ya vijiji na kulazimisha utii kutoka mbari mbalimbali za Rif, Musa alichukua Ceuta Tanja na kukubali kuhifadhi Sabta na gavana wake, Julian. Kuanzia hapo, Musa alituma vikosi vilivyoongozwa na watoto wake wanne na maofisa wengine kwenda Maghribi mwa Maghrib na kuishambulia kutoka pande zote.

Wengi wa Waberiberi wa maghribi ya Maghrib walisalimu amri na kusilimu. Musa aliunda majimbo matatu mapya: Maghrib ya kati, Tilimsan ikiwa makao yake makuu, Maghrib ya Maghribi ya mbali (al-maghrib al-Aksa), Tanja ikiwa makao yake makuu, na al-Sus al-Aksa. Ili kuthibitisha utii wa mbari zilizotekwa, alichukua idadi kubwa ya wapiganaji kama mateka na kuwaingiza katika jeshi lake la Kiislamu. Huko Tanja, Musa alimteua mtoto wake Marwan kuwa gavana na kumpa askari wa Kimasmuda 17,000; baadaye, nafasi ya Marwan ilichukuliwa na Tarik ibn Ziyad.

Musa ibn Nusayr alikuwa amemaliza kujinyakulia Maghrib nzima. Ilikuwa kazi kubwa, lakini alikuwa ametumia mbinu za kikatili ambazo Waislamu walikuwa hawana budi kulipia kwa gharama kubwa.

### *Utamalaki wa peninsula ya Iberia (Al-Andalus)*

Hakuna uchunguzi wa utamalaki wa Kiarabu Kaskazini mwa Afrika na mabadiiliko ya Waberiberi kuwa Waislamu ambao unaweza kutupilia mbali mchango mkubwa wa Waberiberi katika

kutumalaki musoma wa Iberia, au mchango wao katika historia ya Hispania ya Kiislamu na kutokea hapo utawala wa Kiislamu katika Mediterania.

Kiongozi wa kijeshi Muislamu wa kwanza kuendesha (katika mwaka wa 710) uchunguzi wa awali wa kijeshi kusini mwa Iberia ili kuona uwezekano wa utamalaki alikuwa Mberiberi Tarif, aliyekuwa mtoto wa Zara ibn Abi Mudrik. Alifaulu katika uchunguzi wake huo na kutokana na kufaulu huko, bandari ndogo kusini mwa Hispania, Tarifa, ilipewa jina hilo kwa heshima yake. Jemadari Mwislamu aliyeamua kwa mara ya kwanza kuishambulia Hispania alikuwa pia Mberiberi, Tarik ibn Ziyad ibn Abd Allah ibn Walghu. Kama tulivyoona, Musa alikuwa amemteua Tarik ibn Ziyad kuwa gavana wa mkoa wa Tanja, au al-Maghrib al-Aksa, 'Maghrib ya Maghribi ya mbali.' Alikuwa kamanda wa jeshi la watu 17,000, wengi wao wakiwa Wasanhaja.

Pamoja na jeshi hili la kutoka nje na nyongeza ya baadhi ya vikosi vya Kiarabu, Tarik alivuka mlngobahari na kushukia karibu na musoma wenye mawe ambao kuanzia siku hiyo hadi leo ulichukua jina lake: Jabal Tarik ('Miima wa Tarik'), au, kama tunavyoutamka sasa, Jibralta. Katika Agosti 711, alipata ushindi mkubwa dhidi ya jeshi la Visigoth, ambamo mfalme wa mwisho wa Wavisigoth, Roderick au Rodrigo (Rudrik katika Kiarabu) aliuawa. Tarik alisonga mbele na kikosi cha jeshi la wapanda farasi hadi Toledo (*Tulaynula* katika Kiarabu); baada ya mwendo wa nguvu wa zaidi ya kilometa 500, aliteka makao makuu ya Wagothiki, kwa kutumia ushindi wake wa kwanza vizuri. Katika mwezi mmoja, kuanzia Septemba 711, Tarik, jemadari wa kwanza wa majemadari wa Kiberiberi mashuhuri wa Maghrib ya Kiislamu, alikuwa amekomesha utawala wa Wavisigothi katika musoma na kuingiza enzi ya Hispania ya Kiislamu.

Musa ibn Nusayr alivuka kuelekea Hispania na kumaliza kazi ya utamalaki kwa kutumia jeshi la watu 18,000, wengi wao wakiwa Waarabu. Tarik na Waberiberi wake walipewa kazi ya kutamalaki Kaskazini-Maghribi mwa Hispania; katika miezi mitatu. Katika mwaka wa 712, waliteka eneo lote la nchi Kaskazini mwa Ebro hadi Pyrenees. Kabla ya muda wake wa ukamanda katika Hispania kumalizika, Tarik pamoja na vikosi vyake vya Kiberiberi aliteka sehemu yote iliyojulikana baadaye kwa jila la Kastile ya zamani (Old Castile), akatamalaki Amaya, Astorga na hatimaye Leon.

Baada ya mfululizo wa ushindi nchini Hispania Waberiberi kwa maelfu walijaa katika musoma wa Iberia. Kwa kadri walivyofika, ndivyo walichangia katika utamalaki wa sehemu iliyokuwa imebaki ya musoma na katika kampeni za Kiislamu kusini mwa Ufaransa. Inakadiriwa kwamba Waberiberi 80,000 walipigana katika vita vya Poitiers peke yake. Pambano hili, ambalo lilikomesha kushinda kwa Waislamu katika sehemu ya Gaul, lilifanyika katika majira ya majani kupukutika (autumn) mwaka wa 732. Maelfu ya Waberiberi walibaki kusini mwa Ufaransa kwa kipindi cha miaka arobaini iliyofuata. Wengine waliweka makao yao katika Hispania (al-Andalus), jina la Kiarabu la Hispania ya Kiislamu), walioa wanawake wa Kiarabu au wa Kirumi waliokuwepo katika Iberia, na kuwa Waislamu wa Andalusia. Kulikuwa na makoloni ya Kiberiberi yaliyokuwa yamesambaa katika musoma wote. Watoto wao walijulikana kwa jina la *Muwalladun*, yaani, waliozaliwa kati ya Waandalusia na Waarabu au Waberiberi wa kiume na wanawake wa Iberia; hawa walikuwa asilimia sabini ya raia wa Hispania ya Kiislamu. Hawa Waandalusia wenye asili ya Kiberiberi ambao walipatikana katika tabaka zote za jamii wametuachia orodha ndefu ya majina maarufu: majemadari, mabalozzi (kadhi), wataalamu wa dini, wavumbuzi, washairi na mafundi.

### *Waberiberi baada ya utamalaki wa Kiarabu*

Utamalaki wa Afrika Kaskazini uliofanywa na Waarabu ulipomalizika (642-711) kulikuwa na nchi mpya ambayo raia wake walikuwa wanabadilika kijamii na hata kimbari, kimuundo, kimaisha, jinsi

wanavyofikiri na hata namna wanavyoielewa dunia. Kuanzia pwani ya Atlantiki hadi Sirenaika, raia waligeukia upande wa mashariki ya Arabia ya Kiislamu; kadri walivyoendelea kuwa Waislamu na kuchukua tabia za Kiarabu ndivyo walivyoizidi kujifikiria kuwa watu wa ulimwengu huo. Baadhi ya makundi muhimu kijamii yalianza kujitapa kuwa mababu zao wa kabla ya Uislamu walikuwa Waarabu.

Wakati wa utamalaki Waberiberi walishika imani ya Kiislamu kwa wingi japokuwa mwanzoni kukubali huku Uislamu kulibakia kuwa kwa kijuujuu tu, hakukuwa kwa dhati. Waliendelea kushikilia Uislamu kwa sababu mafundisho na itikadi yake rahisi viliwavutia. Wakati wote wa kipindi cha utamalaki, waharniaji wa Kiarabu walikaa katika sehemu zote za Afrika Kaskazini. Maeneo makubwa yaliyokaliwa na Waarabu yalikuwa katika sehemu nyingi za Sirenaika na jimbo la Ifrikiya.

Kulikuwa pia na vikundi vidogo vya Waarabu, wakati mwingine hata mtu mmoja mmoja, ambao walikaa katika mbari za Kiberiberi ambako walionekana kama waalimu; walifanya kazi kama *imam* au viongozi wa kidini. Huu uongozi wa kiroho mara nyingi ulizaa uongozi wa kisiasa pia, *imam* wa Kiarabu alitokea kuwa mkuu wa kisiasa wa mbari. Kwa upande mwingine maendeleo haya yaliwafanya wakoloni wa Kiarabu waonekane kama Waberiberi.

Mara nyingine wengi wa hawa wakoloni wa Kiarabu walikuwa wafuasi wa madhehebu moja au mengine kati wa madhehebu ya waasi wa Kiislamu yanayojulikana kwa jina la Wakhariji (*Khawarij*) ambayo yalipinga utawala wa Umayya na kutoa mafundisho ya usawa ambayo yalipokelewa vizuri miongoni mwa Waberiberi.

Utamalaki maarufu uliowafanya Waarabu kutawanyika hadi kuvuka mipaka ya musoma wao, ulifanywa kwa jina la dini mpya ya Kiislamu. Katika kipindi hiki cha mwanzo, maeneo 'Mwarabu' na 'Mwislamu' yalikuwa na maana moja. Ufalme wa Umayya ulikuwa ufalme ulioongozwa na utawala wa Wakurayshi wa Maka ambao waliwahi kuwa wapinzani wa Nabii na walikuwa waumini mwishoni tu. Kundi hili la utawala lilitawala nchi ya Kiislamu kwa manufaa yao hasa na kutupilia mbali misingi ya kidemokrasia ambayo ndiyo kaida ya Kiislamu. Waumini wapya wasiokuwa Waarabu waliendelea kuchukuliwa kama raia wa tabaka la pili na hawakuwa na haki sawa na Waarabu, hasa kwa upande wa kodi ambazo walilazimika kutoa. Kwa kutaka kuendelea faida zao na mapato yao makhalifa wa Kiumaya – isipokuwa mcha Mungu Umar ibn Abd al-Aziz (717-720) – hawakutaka kuwapa haki zao waumini wapya kama washiriki wa jumua ya Waislamu (*umma*) au kuwaona sawa na Waarabu.

Kama ilivyotokea mara nyingi kihistoria, mivutano ya kimbari na kijamii ilijidhihirisha katika vyama vya waasi wa kidini. Kwa upande wa Waberiberi, hali zote za kusababisha jambo kama hili zilikuwepo. Magavana wa Kiumaya wa mwisho walileta utawala wa kimabavu ambao ulisababisha machafuko: Waberiberi walichukuliwa kama watu duni, walikuwa watu wa kutawaliwa kwa mabavu, ingawa wote walikuwa waumini wa Kiislamu, walikuwa wamepigania Uislamu na kujiona wenyewe kama sehemu ya ufalme wa Kiislamu kama walivyokuwa Waarabu. Waberiberi walilalamika kwamba hawakuzawadiwa ilivyopasa kwa kazi yao (kama ilivyoonekana sana kwa upande wa Hispania ambako walipewa sehemu zisizo na rutuba kama ardhi ya kuazima). Kwa hiyo Maghrib ilitupilia mbali imani halisi ya Wasunni ambayo iliwakilishwa na siasa ya Kiumaya na kujiunga na mafundisho ya Wakhariji badala yake. Wakhariji walifaulu kuunda jumua za madhehebu yao katika sehemu zote. Vituo hivi vya uasi viliundwa pia na Waberiberi wenyewe pamoja na Waarabu. Wote pamoja walipinga utawala wa Kiumaya. Misukosuko mikubwa dhidi ya Waumaya iliyoanzia maghribi ya Maghrib katika mwaka wa 741 haikuwa ya Waberiberi dhidi ya Waarabu ili kuwaondoa katika Maghrib bali uasi wa Kiislamu dhidi ya utawala wa Kiumaya.

### Maghrib chini ya Waumaya

Baada ya vita vya Poitiers (732) kanikitovu ambayo ilikuwa imcivuta idadi kubwa ya majimbo yaliyozunguka Damasko ilikwisha. Miaka minane baadaye, mnamo mwaka 740, kinyume chake kilianza: kulikuwa na hali ya kanipewa ambayo ilisababisha kuanzishwa kwa majimbo huru kadhaa. Kati ya mwaka 697 na 740 kulikuwa na mfululizo wa magavana wanane wa Kiumaya huko Kayrawan, mji mkuu wa eneo hili ambapo ndipo nchi zote za Waislamu wa Maghribi zilitawaliwa, kuanzia Lebda, mashariki ya Tripoli hadi Narbonne, kupita Pyrenees. Hivyo utawala wa moja kwa moja kutoka Damasko ulidumu kwa zaidi kidogo tu ya miaka arubaini. Kipindi kifupi kiasi hicho kinaweza kuonekana chenye athari ndogo wakati kinapolinganishwa na muda wa Warumi, utawala wa Wavandal au Wabizenti. Hata hivyo, matokeo yake yalikuwa muhimu na ya kudumu zaidi. Kwa nini iwe hivyo? Inawezekana kabisa kuwa ni kwa sababu wenyeji, wakati walipokuwa wanakataa kutawaliwa na wageni, waliunga mkono kwa dhati maadili yalioanzishwa na Waarabu. Kama tutakavyoona, mapenzi ya maadili hayo yalikuwa ya msingi sana kwa sababu yalichangia kwa kiasi kikubwa kwenye kuanzisha na kutia moyo nguvu zilizokuwa zinawasukumama watu kupigania uhuru.

Ili kuelewa jinsi mwanzo wa Maghrib mpya, ulivyokuwa mgumu pamoja na uhuru wake uliokuja baada ya utamalaki, tofauti bayana lazima iainishwe baina ya ujumbe wa Kurani na tafsili yake kihistoria. Karibu kila mara tafsili hupotosha maana. Matarajio ya kidugu, ambayo yalitarajiwa kumiliki mahusiano baina ya Waislamu bila kubagua kwa kufuata taifa, rangi au mahali, hayakutekelezwa ipasavyo kimatendo. Hata hivyo hakukuwa na ubaguzi uliokitwa kwenye kanuni au msingi maalumu, wala hakukuwa na kutengana. Lakini, Waarabu walielekea kuwaona, Waberiberi kama "washenzi wa dunia". Hata hivyo, ili tusitoe picha mbaya, lazima isemwe kuwa, kiasi fulani cha Waarabu waliokuwa wakarimu sana walijaribu kuwatukuza kidogo kwa kuwaandia koo fulani za Kiarabu, hasa za Kiyemeni. Lengo hapa lilikuwa kutumia hadithi ya kubuni ya kishajara ili kuwapata Waberiberi, kuwasilimisha na kuwafanya wawe ndugu. Hii iliakisi kusitasita na utata ambao Waarabu waliuonyesha kwa Waberiberi.

Mkabila huu wa kusitasita unajitokeza kwenye siasa. Hassan b. al-Numan aliwaingiza Waberiberi katika jeshi lake na kuwahusisha katika utumiaji pamoja wa ardhi (*fiay*). Mrithi wake, Músa b. ibn Nusayr (698 - 714), akiwa amejijazia Waberiberi wengi na waaminifu ikiwa ni pamoja na Tarik, mshindi mashuhuri wa Hispania, alianzisha kwa nguvu sana kampeni ya kuleta amani. Khalifa Sulimayn (715 - 717), alimweka Muhammad b. Yazid badala yake na akampa maagizo kuhusu usawa wa kifedha. Hali hii iliwekewa msisitizo na mcha Mungu mkubwa Umar b. 'Abd al-'Aziz (717 - 720) ambaye gavana wake, aliyekuwa mawla na mtawa, alitumia nguvu zake zote

kueneza Uislamu na kuupa sura nzuri kadri ilivyowezekana. Umar b. Abd al- Aziz alipokufa, gavana mpya, Yazid b. Abi Muslim, ili kumudu kiasi cha kodi ambacho kilikuwa kinazidi kushuka kutokana na watu wengi kufanywa kuwa Waislamu, aliamua, kinyume na maandiko na fikra za Kurani, kuwa wale ambao walikuwa wamesilimishwa muda si mrefu lazima waendelee kulipa *jizya* au kodi ya kichwa; akaendelea hadi kufikia kiwango cha kuwaaitisha walenzi wake wa Kiberiberi kwa kuwapiga mhuri kwenye mikono yao. Walenzi hao hatimaye walimuua (720 - 1).

Kuanzia wakati huo na kuendelea, hali ikazidi kuwa mbaya. Katika taarifa ya ukumbusho aliyoachiwa Khalifa Hisham (724 743) na ujumbe ulioongozwa na Maysara, ambaye baadaye alikuja kuanzisha maasi yaliyokuwa chanzo cha uhuru wa Wamaghrib, dukuduku kubwa la Waberiberi lilielezwa kwa muhtasari kama ifuatavyo: kuwaondoa askari wa Kiberiberi Waislamu katika kugawana mateka na Waarabu; kuajiriwa kwao kama askari wa mbele katika vita vikali wakati majeshi ya Kiarabu yaliwekwa nyuma; kushika na kuuwa mifugo yao na pia kuteka nyara wasichana na wanawake wa Kiberiberi; na kwa ujumla, matendo yasiyo ya haki na yasiyo sawa mikononi mwa Waarabu na makamanda wao.

### *Ukhariji: itikadi ya kimapinduzi*

Maysara, ambaye alifahamika kama Mdhaliishwaji (al-hakir), hapo nyuma alikuwa Mberiberi mtekamaji ambaye alisilimishwa na kuwa Msufri wa Kikhariji. Chini ya Waumaya, Ukhariji ulikuwa ndiyo nguvu imara zaidi ya kimapinduzi. Ulitokea wakati wa fitna au vurugu kubwa ambayo ilitingisha jumua ya Kiislamu baada ya kuuawa kwa Uthman (656) na ukawa umeingizwa kwanza kabisa katika teolojia ya kisiasa. Teolojia hii, kama msingi wa jumla, ilikuwemo kaika aina zote za Ukhariji na ilikuwa na kanuni ya Imam aliyechaguliwa na watu, kiongozi mkuu wa jamii, bila kujali utafai, rangi au nchi, madaraka yakiwa yamepewa mtu hodari zaidi, 'hata kama ni mtumwa wa Kihabeshi mwenye pua nyembamba'.

Kulikuwa na mikondo minne kwenye Ukhariji ambayo inaweza kuorodheshwa kwa kufuata ukali wake wa kimapinduzi: Waazarika, Wanajadat, Wasufri na Waibadi. Kati ya hawa waliokuwa wakali zaidi ya wote ni Waazarika. Mkondo lhu uliondolewa kabisa mashariki kwenye miaka ya 700 ambapo mkondo wa Wanajadat takriban ulikuwa umekwishaondoka kabisa kwenye medani ya kisiasa miaka michache iliyotangulia, mnamo mwaka 693, kabla Maghrib hajjatamalakiwa kabisa, kiasi kwamba ni mikondo ya Wasufri na Waibadi tu iliyobakia. Inaweza kusemwa kwa kiasi fulani cha uhakika kuwa wafuasi wao walianza kuenea Maghribi mnamo mwaka 714.

Walichokileta Maghrib kilikuwa ni mkakati wa kimapinduzi ambao waliufahamu na kuutumia huko Mashariki, pamoja na kanuni iliyotumika katika mkakati huo. Mkakati huo ulijumuisha *kuud*, kitendo cha siri cha uasi kwa kutumia kisingizio cha *takiyya* au mbinu ya unafiki, na *khruji*, uasi wa dhahiri ulioanzishwa wakati unaofaa. Kanuni hiyo ilisisitiza usawa kamili baina ya Waislamu wote, na kuharamishwa kwa mamlaka ya utawala wa Waumaya ambao waliingia madarakani kwa nguvu. Ililaani hali ya ukandamizaji ya utawala huu, ambao mara nyingi ulivunja kanuni za maandishi na imani ya Kurani, hasa kwenye mambo ya kifedha. Dhamira zote muhimu za kiitikadi ziliungwa mkono na *hadith* au misemo ya Mturne. Uasi dhidi ya udhalimu wa Kiumaya ulihubiriwa si tu kama mapambano bali pia kama jukumu la kidini.

Ukhariji ulikuwa na mvuto fulani kutokana na tikali na umakinifu wake. Ni wazi kuwa kulikuwa na ukamilishano safi kati ya kanuni hiyo, kwa upande mmoja, na mazingira ya kisaikolojia, kijamii-kiuchumi na hali yakinifu kwa upande mwingine. Kama Dozy alivyoandika katika mistari michache ambayo imebakia na uzito wake licha ya miaka karibu mia kupita, huk

Maghrib, 'Ukalvin wa Kiislamu hatimaye ulipata mahala pake'. Hata hivyo, licha ya ukamilishano huu ambao ni kama wa kibiojolojia, kiini cha ushindi wa Ukhariji kimo katika ukweli kuwa Waberiberi walijikuta katikati ya dhoroaba. Walijihisi kuvunjwa moyo, kudhalilishwa na kunyanyaswa, na malalamiko yao hayakutiliwa maanani huko Damasko.

Hivyo Maysara aliongoza maasi chini ya bendera ya Usufri (740) na alipewa cheo cha Khalifa. Hata hivyo, utawala wa Khalifa wa kwanza wa Kiberiberi ulikuwa mfupi sana. Baada ya kurudi nyuma hadi Tanja wakati wa kukabiliwa na maadui, alinyang'anywa madaraka na kuuawa. Mrithi wake, Khalid b. Humayd al - Zanat, ndiye aliyepata ushindi katika mapigano ya watu wa nasaba bora (741) ambayo yalikuwa pigo lililouaibisha umwinyi wa Kiarabu. Karibu na mwisho wa mwaka huo huo, ushindi huu ulifuatiwa na ushindi mwingine kwenye kingo za mto Sebu.

Lakini jinsi ushindi ulivyokaribia kulitokea kutokuelewana miongoni mwa washindi. Mwaka uliofuata, kwenye kuta za mji uliozingirwa na Kayrawan, kulikuwa na majeshi mawili yaliyopigana ambayo yalishindwa bila kutarajia, moja baada ya jingine, na jeshi la Kiarabu lililoongozwa na Hanzala b. Safwan (743).

### *Falme za Kisufri*

Baada ya ghasia hizo ramani ya Maghrib ilibadilishwa kabisa. Kayrawn ilisimama tisti, lakini Maghrib ya Maghribi na kati sasa zilikuwa nje ya mamlaka ya Mashariki.

Moyo wa kidemokrasia wa Wakhariji, ikiwa ni pamoja na kuhusika kwao sana na kujitawala wenyewe kulikokitwa kwenye mfarakano wa kimbari, ulisababisha dola nyingi kuanza kutokeza, na kuanguka kwa utawala uliokuwa umekitwa kwenye kiini cha mji mmoja wa mamlaka ya Waarabu. Dola zilizokuwa ndogo sana kati ya hizi, pamoja na mipaka yake ambayo ilikuwa ikibadilika badilika na kudumu kwa muda usio na uhakika, hazijulikani sana. Falme kubwa zaidi tu zilizoongoza katika matukio, ndizo zilizoacha alama katika historia.

Dola ya kwanza kuanzishwa kati ya dola hizi ni Tamasna, katika pwani ya Atlantiki ya Moroko, baina ya Sale na Azemmour, na lilifahamika vizuri zaidi kwa jina la Ufalme wa Barghawata. Lilianzishwa na Tarif ambaye alishiriki katika mashambulizi ya Wasufri katika eneo la Kayrawan. Utaifa wa Waberiberi ulipita kiwango wakati mfalme wa nne wa nasaba ya Banu Tarif, Yunus b. Ilyas (842 - 884) alipoamua kuwatunukia watu wake dini ya kitaifa iliyokitwa kwenye Uislamu ili kuwaacha huru zaidi. Alimtangaza babu yake, Salih b. Tarif, kuwa alikuwa nabii na akamhusisha na Kurani ya lugha ya Kiberiberi na mfululizo wa kanuni zilizoainishwa na miiko ya chakula. Jambo hili, kwa ufupi, lilifikia kwenye aina fulani ya uhuru wa kitamaduni uliolengwa kwenye kukamilisha uhuru wa kisiasa ambao tayari ulikwishapatikana. Hali hii, licha ya tofauti ndogo ndogo, haitofautiani na baadhi ya matukio ya kisasa ya kujikomboa kutoka kwenye ukoloni. Wabanu Tarif walifanikiwa kuulinda uhuru wao wa asili yao kwa karne nyingi; hata maadui wao Waislamu wa Kisunni hawakuweza kuacha kusifu ushujaa wao na maadili yao.

Wakati ufalme wa Tamasna ulipokuwa unaoundwa, ufalme wa Tilimsan (742-789) ulianzishwa katikati ya Maghrib na Abu Kurra, ambaye pia alishiriki katika shambulio la mji wa Kayrawan ambalo halikufanikiwa. Hata hivyo, ufalme wake haukudumu kwa muda mrefu, kwani mnamo mwaka 789 ufalme wa Tilimsan uliwekwa chini ya utawala wa Waidrisi bila kipingamizi chochote.

Ufalme wa tatu wa Kisufri, yaani ule wa Banu Wasul, ambao ulifahamika zaidi kama Banu Midrar, ulianzishwa huko Sijilmasa (757-976) na Waberiberi wa Miknasa. Ufalme huu ulidumu kwa amani hadi mwaka 909 wakati Wafatimi waliposhika madaraka. Imamu al Yasa b. Midrar aluawa na badala yake akawepo gavana wa Kifatimi ambaye hakuweza kukaa madarakani zaidi ya miezi

miwili. Wabanu Wasul walishika tena madaraka ya mji huo na waliweza kuutawala licha ya vipingamizi vyote, wakatupilia mbali Usufri na kuchukua Uibadi na hatimaye Usunni, hadi walipoondolewa madarakani moja kwa moja na Wabanu Khazrun wa Kizanat, waliosaidiwa na Waumaya wa Hispania. Kwanza kabisa, Sijilmasa ulikuwa mji mkuu wa kibiashara huko Sahara, kituo cha mapumziko kwenye njia ya dhahabu na sehemu muhimu ya biashara baina ya nchi za kusini mwa Sahara, Maghrib na Mashariki.

## Falme za Kiibadi

Kama ilivyoelezwa hapo juu, uasi kwanza ulitokea kutokea Maghribi; ulikuwa wa Kisufri kiitikadi na uliongozwa na Waberiberi wa Zanata. Waibadi, ambao hawakuwa na fujo sana, iliwabidi kuwa waangalifu zaidi; walianza kuvuta subira na kuona litakalotokea. Kwanza walijitayarisha, kulingana na teolojia ya dini yao, ambayo iliwakubali *Wakuud* na *Wakitman*, wakiwa wanajitayarisha na kusubiri wakati unaofaa.

Haya yalitokea mwaka 745. 'Abd al-Rahman b. Habib, gavana wa Kayrawan ambaye kwa kiasi fulani alikuwa huru, alifanya kosa la kusababisha kuuawa kiongozi wa Kiibadi wa jimbo la Tripoli, 'Abd Allah b. Masud al-Tudjibi. Mauaji hayo yalikuwa ni ishara ya maasi ya wazi dhidi ya serikali. Viongozi wawili wa Kiibadi, wote Waarabu, walipata mfululizo wa ushindi na hatimaye wakalichukua jimbo lote la Tripoli. Kama kaka zao wa Kisufri, wao pia waliangukia kwenye upinzani mkali na baadaye walikutwa wamekufa, kila mmoja wao akiwa amechomwa na upanga wa mwenzake. Mberiberi, Ismail b. Ziyad al-Nafusi, akawa kiongozi na akauzingira mji wa Gabes lakini Abd al-Rahman b. Habib alifanikiwa kumshinda mnamo mwaka 748-9 na kuupata tena mji wa Tripoli, ambapo aliwaua Waibadi kwa kiasi kikubwa ili kuondoa majungu katika jimbo hilo.

Hata hivyo, Uibadi uliendelea kuwepo na ukarudia tu kwenye unjama au *kuud*, na miundo inayostahili ya *kitman* au usiri na *takiyya* au mkakati wa usilimishaji ambao ulihakikisha kuwa ungeendelea kuwepo hadi muda wa kuzinduka tena ufike. Uibadi ulijitokeza tena kwa fujo katika nyakati mbili. Baada ya kuuawa Abd al-Rahman b. Habib, uliishika Tripoli mnamo mwaka 754. Halafu Abdu al-Khattab aliendelea kuelekea Kayrawan, mji ambao wakati huo ulikuwa umekaliwa na kuteswa na Warfajuma wa Kisufri kutoka kusini mwa Tunisia. Aliingia katika mji huo mwaka 758 na kumchagua Abd al-Rahaman b. Rustum, mwanzilishi wa baadaye wa Tiaret, kuwa gavana. Mwaka 761 Ibn al-Ashath alipandisha tena kiwango cha weusi cha Waabasi huko Kayrawani, lakini miaka kumi baadaye kulikuwa na uasi, tena wa fujo kubwa zaidi. Abu Hatim, Muibadi ambaye alitokea Tripoli aliushikilia mji mkuu wa Ifrikiyad na kuwashusha wakazi wake hadi kwenye kiwango cha kula paka wao na mwa. Mnamo mwanzo wa mwaka 772, mji uliokuwa unakufa kwa njaa uliangukia tena katika mikono ya Waibadi, lakini napo kwa miezi miehache tu. Mwezi Mei mwaka 772 Yazid b. Hatim al-Muhailabi alizimaliza kabisa jitihada za Waibadi za kuteka sehemu ya mashariki ya Maghrib.

Tiaret lilikuwa ndilo taifa pekee la Kiibadi ambalo lilikuwa limefanikiwa kusnzishwa na kudumu kwa kipindi kirefu (761-910). Lilianzishwa na Mwajemi, Abd al-Rahmani b. Rustum, ambaye alifanikiwa kutoroka kutoka Kayrawan wakati ilipovamiwa na Ibn al-Ashath. Mnamo mwaka 778, alipandishwa hadhi kuwa Imam na umashuhuri wake ulisikika hadi Mashariki, ambako waumini wa Kiibadi walimtumia fedha nyingi. Nasabatawala aliouanzisha, licha ya mgawanyiko, haukuweza kupingika. Taifa la Warustumili lipanuka kuanzia Maghrib ya kati hadi Jabel Nefusa. Lakini kwa sababu lilikuwa na mipaka ambayo haikuainishwa vyema, taifa hili halikuweza kuwa na muundo mkubwa. Aidha nje ya mipaka ya mji mkuu wa Tiaret wenyewe, mamlaka ya Imam yalikuwa ya



kidini zaidi kuliko ya kimaisha halisi. Licha ya kanuni zilizopingana, Warustumi walianzisha uhusiano mkubwa wa kirafiki na Waumaya wa Hispania.

### *Kudidimia kwa Ukhariji na kuanzishwa kwa ufalme wa Kiidrisi*

Ukhariji haukuingia Maghrib peke yake. Karibu na wakati huohuo, Wamutazali pia walipata idadi kubwa ya wafuasi, na Waibadi walilazimika kuwatafuta wasomi wao mashuhuri kupambana dhidi ya Wamutazali katika mashindano ya hadharani ya ulumbi ambayo yalivutia sana na kukumbukwa kwa muda mrefu. Ufalme wa Wamutazali, uliotawaliwa na Mberiberi, Ibrahim b. Muhammad al-Mutazal, uliweza hata kufanikiwa kuanzishwa huko Ayyaraj, Maghribi ya Tiaret.

Kuanzia katikati ya karne ya nane, Waislamu wa Kishia walianza kuwa washindani wakubwa wa Wakhariji, ambao walipata viziwi vingi. Baada ya maasi ambayo hayakufaulu yaliyoongozwa na Muhammad al-Nafs al-Zakiyya huko Maka mwaka 762, na maafa yaliyotokana na maasi hayo, Washia wengi walilazimika kuwa wakimbizi mahali pengine. Wengine walikwenda kuishi Maghrib, ambapo walijishughulisha na ufundishaji wa dini na siasa, wakisaidiwa zaidi na hadhi ya kuhusiana kwao na Mtume mwenyewe. Abu Sufyan na Al-Hulwani walikwenda kuishi Maghribi ya Ifrikiya mnamo mwaka 762, ambapo walianzisha misingi ya mwanzo ya kufika kwa Wafatimi. Hivyo Ukhariji, pamoja na mawazo yake ya kidemokrasia, ulisnza kuruhusu kanuni zinazopingana na serikali ya Kishia.

Mabadiliko haya ya kikanuni yalikuwa kwenye msingi wa mafanikio ya Waidrisi. Idris I, mmoja wa kaka zake al-Nafs al-Zakiyya, hatimaye alikuja Wulili (*Volubilis*), mji mkuu wa zamani wa ustaarabu wa Kiukristo, ambapo alikaribishwa mwezi Agosti 788 na kiongozi wa Waberiberi wa Awraba, Mmutazali Abd al-Hamid. Miezi sita baadaye, aliapa kiapo cha kutawazwa, *bay'a*. Mara moja alianza na kujishughulisha na kampeni kubwa ya kuupanua utawala na usilimishaji. Haukupita muda mrefu Tilimsan ilifungua milango kumruhusu. Vitendo vyake vilisababisha Khalifa wa Waabbasi kuwa na wasiwasi kiasi kwamba alimfanyia njama akauawa (795). Hakuna kilichotatuliwa na kuuawa kwake. Idris I alimwacha kimada wake wa Kiberiberi, Kanza, ambaye alikuwa mja mzito. Mtoto alipewa jina la baba yake na serikali yake ikaendeshwa na mtu mwingine kwa njaba yake hadi alipoweza kula kiapo cha kutawazwa. Hata hivyo Baghdad ilikuwa kwenye hadhari muda wote. Mshia hata kama alikuwa na damu ya Kiberiberi kidogo tu alichukuliwa kuwa tishio, hata kwenye sehemu za mbali za mipaka ya dunia 'iliyostaarabika'. Kwa hivyo Ukhalifa ulijaribu, kwa hila za siri au hongo, kuharibu mipango yoyote ile ikiwa bado katika hatua zake za mwanzo. Kutawazwa kwa Idris II kulifanyika mapema mnamo mwaka 803; lakini hajulikani alikuwa na cheo gani, japokuwa inawezekana kilikuwa kile cha Imam, kwa mujibu wa kanuni za Kizaydi. Hata hivyo, hii haikuondoa njama za sirisiri. Mwaka 808 Idris II aliamuru kuuawa kwa Ishak b. Muhammad b. Abd al-Hamidi - kiongozi wa Waawraba ambaye ndiye hasa aliyekuwa chanzo cha mafanikio ya baba yake kwa kuwa na uhusiano na maadui wa Kiaghlabi. Je ilikuwa labda ni kutokana na kutaka kueptuka kukandamizwa na wapinzani wake wa Kiberiberi kwamba mfalme huyu kijana alianzisha makao yake makuu mwaka uliofuata kwenye kingo ya kushoto ya Wadi Feas na kuwa katikati ya Waarabu? Hata hivyo, baada ya muda, uadui baina ya Waaghlabi na Waidrisi polepole ulififia baada ya kueleweka kuwa Waidrisi lawakuwa hatari kwa majirani zao, na hasa hawakuwa hatari kabisa kwa Ukhalifa.

Imani zao asilia za Kishia ziliachwa haraka sana na badala yake zikachukuliwa za Kisunni. Hivyo, kwa makusudi na kwa kila hali Maghrib ilikuja kugawanywa katika maeneo matatu ambayo mbari hizo zilikuwa na ushawishi nayo; Waaghlabi upande wa mashariki, Wakhariji katika sehemu ya kati na Waidrisi upande wa Maghribi.

Idris II aliendeza sera zilizoanzishwa na baba yake ambazo zilihusu usilimibaji na uingizaji Uarabu na kupanua mipaka ya ufalme huo. Idris II alihakikisha kuwa madaraka yake yanatambuliwa na Wamasmuda wa Atlas ya Juu, akaibakisha Tilimsan chini yake, na akaichukua Nefis upande wa kusini. Hata hivyo, alishindwa upande wa Maghribi ambapo alikuta upinzani kutoka kwa Wabarghawata ambao walikuwa wakikaa katika nyanda za Tamasna kando ya pwani ya Atlantiki.

Alipokufa, mnamo Septemba 828, alikuwa ni mtawala wa ufalme mkubwa na ulioneemeka na aliugawa kwa watoto saba kati ya watoto wake wa kiume. Mgawanyo huu wa himaya hiyo ulikuja kuwa na athari mbaya sana. Muhammad (828-836), mwana mkubwa wa kiume wa Idris II alipewa Fez na hivyo kupata haki ya heshima kubwa ya kuwa mfalme mkuu. Kaka zake wakiwa na kila kitu, walitakiwa wawe watumishi wake na chini ya mamlaka yake. Kwa hakika, mpango huo haukufanya kazi vizuri. Mafanikio ya Idris I na Idris II kwa upande wa muungano na upanuzi wa kisiasa yalifuatiwa na kugawanyika polepole wa himaya hiyo. Matokeo yake ni kuwa, baada ya kifo cha Yahya II (859), tawi kuu la familia hiyo lilipoteza mamlaka yake ya kifalme, ambayo yaliangukia kwenye mikono ya tawi dogo la Banu Umar. Kuanzia hapo, historia ya ukoo tawala huu ilikuwa si zaidi ya mfululizo wa magomvi wa ndani kwa ndani, vurugu na umwagaji damu; mambo ambayo yalikuwisha tu baada ya ufalme huo kuanguka mnamo 985. Baada ya kutoweka huko Moroko, ukoo tawala huu ulijitokeza tena mnamo mwaka 1016 huko Kordoba chini ya Ali b. Hammud, mzawa wa Bamu Umar, Khalifa aliyeishi kwa muda mfupi sana.

Mwisho mbaya lakini ambao haukuzuilika wa ufalme wa Idrisi usitufanye tukaufumbia macho umuhimu mkubwa wa nafasi yake katika maisha ya baadaye ya Moroko. Waidrisi walihusika na kuanzishwa kwa kujitambua kitaifa kwa Wamoroko ambako kunaweza kufuatiliwa hadi hivi leo na waliipa nchi hiyo mji mkuu wake wa kwanza, Fez. Kwa upande wa Maghrib ya Maghribi, Fez ilichukua jukumu lililopewa Kayrawan huko Ifrikiya na Kordoba huko Hispania. Kwa msaada wa Levi-Provencal, tumeweza kufahamu kuwa Fez ilianzishwa kwanza na Idris I ambaye mnamo 789 alijenga mji huo kwenye ukingo wa kulia wa mto Wadi Fas, uliokuwa ukikaliwa na Waberiberi na baadaye tikakaliwa na Idris II ambaye, mnamo mwaka 809, alijenga mji mpya mkabala na mji wa kwanza, uliopangwa vizuri kwenye ukingo wa kushoto. Kwa vile mji huo ulinufaika sana kutokana na kuwepo kwake mahali pazuri sana kwenye mhimili mkuu wa mashariki-Maghribi kando kando ya bonde la Taza na ulikuwa na maji ya kutosha, miti, mawe ya kujengea na udongo kwa ajili ya ufynyanzi, mji wa Fez uliendelea haraka sana na ulikuwa kitu cha kujivunia cha Waidrisi. Kikiwa kituo cha kidini cha taifa jipya, ulikuwa kituo cha kitaaluma cha daraja la juu, na umeendelea kuwa hivyo tokea wakati huo.

Tokea mwanzo, Ufalme wa Waidrisi, ulioanzishwa katika mazingira ya Kiberiberi, haukuwa wa Kiarabu zaidi kuliko namna Ufalme wa Warustumi ulivyokuwa wa Kiajemi. Hata hivyo kwa kuwakubali wakimbizi kutoka Kayrawan na Kordoba, Fez kwa haraka ukaanza kuwa kituo kikuu cha kuupokea Uarabu. Msikiti ambao bado ni mashuhuri na Chuo Kikuu cha al-Karawiyyin vilianzishwa na mwanamke kutoka Kayrawan mnamo mwaka 859. Jambo hili lilikuwa na jukumu kubwa katika historia ya kidini na kitamaduni ya Moroko. Hivyo Fez ukawa mji mkuu ambao ulikuwa na Uarabu, kisiasa na kitaaluma, ndani ya mazingira ya Kiberiberi. Ingawa Waidrisi kiasili walikuwa Washia wa Kizaydi, hawaelekei kuwa walifanya jitihada yoyote kuwalazimisha watu kufuata kanuni zao wenyewe. Walishabikia kusambazwa kwa mafunzo ya Malik, mwanazuoni mashuhuri wa Madina, labda kwa sababu alikuwa hajafanya maajabu yoyote kuhusu huruma zake kwa Waali, hasa wakati wa maasi yalioongozwa na al-Nafs al-Zakiyya, kaka yake Idris I. Kufuatana na hayo Umiliki ukawa ndio mtazamo uliyotawala katika Moroko wakati wa enzi ya Waidrisi.

Mafanikio ya Waidrisi yalikuwa na athari kubwa ya kuambukiza, kwani wazawa wengine wa

Ali baadaye waliitoka Maghrib ya kati kutoka kwenye Ukhariji kwa mafanikio ya kiasi fulani. Al-Yakubi, ambaye alilitembea jimbo hilo kati ya mwaka 876 na 889, aliorodhesha sio chini ya tawala tisa za Ali.

### *Jaribio la kwanza la uhuru huko Ifrikiya*

Waarabu wenyeji wa Ifrikiya, hasa katika majeshi, walianza kupata taabu chini ya Waarabu wenzao kutoka Mashariki, ambao walikuwa wameletwa kuwasaidia baada ya vita vya Wafalme (740), dharau kwa Waberiberi ikiwa imekithiri. Katika baadhi ya nyakati, mapigano ya wazi baina ya makundi haya mawili yaliweza kuepukwa kidogo, lakini uhasama ulizidi kuendelea. Hii inaelezea kukua kwa mwamko wa dhali wa kitaifa katika fikra za Waarabu wa Maghrib, hasa baina ya wale wa kizazi cha pili au cha tatu ambao, kwa kuwa walizaliwa nchini humo, walikuwa hawajawahi kufika Mashariki. Hali hii ndiyo hasa itakayotupatia msingi thabiti wa mfululizo mzima wa matukio ambayo labda yangebakia kutoeleweka.

Hivyo ni rahisi zaidi kuelewa jinsi Abd al-Rahman b. Habib alivyofanikiwa kuwafukuza kutoka Kayrawan Hanzala b. Safwan (aliyesifika kutokana na ushindi wake dhidi ya Waberiberi, licha ya kuwa 'mgeni' na kuanzisha taifa huru la kwanza mashariki ya Maghrib (744-754). Kwa kupata uhuru, jeshi la Ifrikiya lilizinduka kutoka kwenye kuaibishwa na kushindwa kwao na likajipatia tena ushupavu wao wa awali. Mnamo mwaka 752-3 lilifanikiwa kuzishambulia Sisilia, Sardinia na Tilimsan.

Abd al-Rahman b. Habib alikuwa kiongozi wa taifa ambalo lilikuwa na uongozi wa Kiarabu na aliishi kwa kufuata maongozi na kanuni za Kisunni. Hivyo alikuwa na ari kungojea kupata Ukhaliifa, kwa kuanza na Damasko ambayo mwisho wake ulikuwa karibu, na baadaye Baghdad. Alikula kiapo cha uaminifu bila kusita kwa Khalifa wa Waabbasi. Hii ilimaanisha kuwa aliitambua rasmi serikali mpya, akitarajia kutambuliwa kisharia ambako kungehititisha na kuthabitisha uhuru ambao ulikuwepo. Khalifa wa mwanzo wa Waabbasi, Khalifa al-Saffah (750-754) alionyesha kama aliyekubaliana na maendeleo ya aina hiyo katika mahusiano baina ya Baghdad na Kayrawan, lakini mrithi wake al-Mansur (754-775) alionyesha wazi hamu yake ya kurudi kwenye hali kama ilivyokuwa mwanzo, hasa kuhusiana na taratibu za kifedha na mapokeo ya kuuza watumwa.

Abd al-Rahmani b. Habib alikataa kwa kusema kuwa Ifrikiya ilikuwa sasa nchi ya Kiislamu kabisa na kuwa isingewezekana tena kuwafanya watumwa au kutoza kodi kubwa. Aidha alikataa kutuma pesa zozote zile Baghdad. Muda mfupi baadaye aliuaa na hivyo ukawa ndio mwisho wa jitihada ya kwanza ya kuipatia Ifrikiya uhuru.

### *Waghlabi*

Al-Mansur alifanikiwa kuirudisha Ifrikiya katika himaya yake kwa muda wa miaka arubaini mingine au zaidi (761-800). Uehungu wa mapambano baina ya vikundi vya kiadui vya *jund* (jeshi la Kiarabu) katika jiihada yao ya kushika madaraka kwa nguvu ulifikia upeo wa juu kiasi kwamba Ifrikiya haikuweza kuongozeka kabisa. Jimbo hili sasa lilikuwa ni chanzo tu cha wasiwasi usiokwisha kwa Ukhaliifa, na liligharimu hazina kubwa. Licha ya hayo, Baghdad ilizidi kuwa katika hali ambayo isingeiwezesha kuingilia kati kivita. Hivyo, Harun al-Rashid aliamua kuipatia Ifrikiya uhuru ambao bila shaka ingeliuchukua kwa nguvu. Uchaguzi wake uliangukia kwenye mwakilishi aliyestahili, Ibrahim b. al-Aghlab, ambaye alikuwa mwanzilishi wa ufalme ya Waaghlabi (800-909).

Ibrahim b. al-Aghlab alikuwa makamu wa gavana wa zamani wa Wamzab na mara nyingi alikwishatoa ushahidi wa utii wake kwa Waabbasi, kwa kuchukua nafasi ya mtetezi wa haki kila

Ali baadaye waliitaka Maghrib ya kati kutoka kwenye Ukhariji kwa mafanikio ya kiasi fulani. Al-Yakubi, ambaye alilitembea jimbo hilo kati ya mwaka 876 na 889, aliorodhesha sio chini ya tawala tisa za Ali.

### *Jaribio la kwanza la uhuru huko Ifrikiya*

Waarabu wenyeji wa Ifrikiya, hasa katika majeshi, walianza kupata taabu chini ya Waarabu wenzao kutoka Mashariki, ambao walikuwa wameletwa kuwasaidia baada ya vita vya Wafalme (740), dharau kwa Waberiberi ikiwa imekithiri. Katika baadhi ya nyakati, mapigano ya wazi baina ya makundi haya mawili yaliweza kuepukwa kidogo, lakini uhasama ulizidi kuendelea. Hii inaelezea kukua kwa mwamko wa dhati wa kitaifa katika fikra za Waarabu wa Maghrib, hasa baina ya wale wa kizazi cha pili au cha tatu ambao, kwa kuwa walizaliwa nchini humo, walikuwa hawajawahi kufika Mashariki. Hali hii ndiyo hasa itakayotupatia msingi thabiti wa mfululizo mzima wa matukio ambayo labda yangebakia kutoeleweka.

Hivyo ni rahisi zaidi kuelewa jinsi Abd al-Rahman b. Habib alivyofanikiwa kuwafukuza kutoka Kayrawan Hanzala b. Safwan (aliyesifika kutokana na ushindi wake dhidi ya Waberiberi, licha ya kuwa 'mgeni' na kuanzisha taifa huru la kwanza mashariki ya Maghrib (744-754). Kwa kupata uhuru, jeshi la Ifrikiya lilizinduka kutoka kwenye kuaibishwa na kushindwa kwao na likajipatia tena ushupavu wao wa awali. Mnamo mwaka 752-3 lilifanikiwa kuzishambulia Sisilia, Sardinia na Tilimsan.

Abd al-Rahman b. Habib alikuwa kiongozi wa taifa ambalo lilikuwa na uongozi wa Kiarabu na aliishi kwa kufuata maongozi na kanuni za Kisunni. Hivyo alikuwa na ari kungojea kupata Ukhalifa, kwa kuanza na Damasko ambayo mwisho wake ulikuwa karibu, na baadaye Baghdad. Alikula kiapo cha uaminifu bila kusita kwa Khalifa wa Waabbasi. Hii ilimaanisha kuwa aliitambua rasmi serikali mpya, akitarajia kutambuliwa kisharia ambako kungethibitisha na kuthabitisha uhuru ambao ulikuwepo. Khalifa wa mwanzo wa Waabbasi, Khalifa al-Saffali (750-754) alionyesha kama aliyekubahana na maendeleo ya aina liyo katika mahusiano baina ya Baghdad na Kayrawan, lakini mrithi wake al-Mansur (754-775) alionyesha wazi hamu yake ya kurudi kwenye hali kama ilivyokuwa mwanzo, hasa kuhusiana na taratibu za kifedha na mapokeo ya kuuza watumwa.


Abd al-Rahmani b. Habib alikataa kwa kusema kuwa Ifrikiya ilikuwa sasa nchi ya Kiislamu kabisa na kuwa isingewezekana tena kuwafanya watumwa au kutoza kodi kubwa. Aidha alikataa kutuma pesa zozote zile Baghdad. Muda mfupi baadaye aliuawa na hivyo ukawa ndio mwisho wa jitihada ya kwanza ya kuipatia Ifrikiya uhuru.

### *Waghlabi*

Al-Mansur alifanikiwa kuirudisha Ifrikiya katika himaya yake kwa muda wa miaka arubaini mingine au zaidi (761-800). Uchungu wa mapambano baina ya vikundi vya kiadui vya *jund* (jeshi la Kiarabu) katika jitihada yao ya kushika madaraka kwa nguvu ulifikia upeo wa juu kiasi kwamba Ifrikiya haikuweza kuongozeka kabisa. Jimbo hili sasa lilikuwa ni chanzo tu cha wasiwasi usiokwisha kwa Ukhalifa, na liligharimu hazina kubwa. Licha ya hayo, Baghdad ilizidi kuwa katika hali ambayo isingeiwezesha kuingilia kati kivita. Hivyo, Harun al-Rashid aliamua kuipatia Ifrikiya uhuru ambao bila shaka ingeliuchukua kwa nguvu. Uchaguzi wake uliangukia kwenye mwakilishi aliyestahili, Ibrahim b. al-Aghlab, ambaye alikuwa mwanzilishi wa ufalme ya Waaghlabi (800-909).

Ibrahim b. al-Aghlab alikuwa makamu wa gavana wa zamani wa Wamzab na mara nyingi alikwishatoa ushahidi wa utii wake kwa Waabbasi, kwa kuehukua nafasi ya mtetezi wa haki kila

**10.1** Mandhari ya jumla ya Fez kukiwa na ukuta wa nje wa mji ambao ulijengwa upya mara kadha na falme zilizofuatana. (M. el-Fasi)



**10.2** Mnara wa msikiti wa Karawiyyi wa Fez. (Wizara ya Utamaduni ya Moroko, Rabat)

wakati. Alikubali kuteuliwa kwenye ugavana kwa masharti kuwa asingeweza kuondolewa kitini na kuwa cheo hicho kingeweza kurithiwa. Badala yake alijitolea kukubali kutopata ruzuku ya dinari 100,000 zilizotengwa kwa Ifrikiya kutoka kwa *kharaj* huko Misri na yeye, kwa upande wake, kuchangia kwenye hazina ya Baghdad malipo ya mwaka ya dinari 40,000. Al-Rashid alikubali pendekezo hili na hivyo uhuru wa Ifrikiya ulipatikana kwa mapatano, bila mfarakano au kuachana na Baghdad.

Watawala wa mwanzo watatu wa nasabatawala hiyo mpya waliweka jitihada zao kwenye

kuimairisha serikali yao. Walizindua kipindi cha amani na ukomavu wa kisiasa ambapo Ifrikiya ilipata utajiri mkubwa. Abu Ibrahim Ahmad (856-863) aliacha kumbukumbu ya mfalme bora, ambaye alijihusisha kikamilifu na maslahi ya watu wake. Alijenga ngome (*ribat*) nyingi kwa ajili ya ulinzi wa pwani na alijaza Kayrawan na mahodhi ambayo yanavutia hata hii leo. Kipindi hicho cha ustawi mkubwa, kilichofuatiwa na kufifia kwa ustawi, kilitokea chini ya utawala wa Ibrahim II (875-902) ambao ulianza kwa neema sana. Watu wake walifurahia mfumo wa haki sawa na serikali ya busara. Hata hivyo, kwa bahati mbaya, mfalme aliugua ugonjwa wa mfadhaiko wa moyo na akili zake polepole zilianza kupungua. Alizidi kuwa mkali na alifanya makosa mengi zaidi ya kisiasa, na hivyo kuwapatia wafundishaji dini ya Kishia nafasi nzuri sana ya kufanikisha mahubiri yao.

Propaganda ya Washia, wakiwa na Abu Abd Allah al-Dai kama msemaji mkuu, aliyewafikia Waberiberi wa Kutama wa Kabyilia, ilitangaza majilio ya Mahdi, au Mwokozi, ambaye angeanzisha paradiso ya haki duniani. Mafundishi ya dini ya aina hii yalifanikiwa na utawala wa Kiaghlabi, ukiwa na mali nyingi lakini bila kuungwa mkono na watu, ulifurahia vilivyo makundi ya watu wanaofanya ghasia ambao waliteremka kutoka kwenye sehemu zisizokuwa na kitu za milimani na uja kunyakua mabonde yenye rutuba. Pigo la mwisho liliangukia katika jimbo la el-Kef, huko al-Urbus (18 Machi 909). Ziyadat Allah III, akiwa amechukua utajiri uliohodhiwa na wahenga wake, alitoroka usiku kutoka kwenye mji mkuu wa Rakkada ambao ulikuwa umeanzishwa na babu yake. Siku iliyofuatia, mji huo ulitekwa na kuporwa na kuharibiwa sana.


Harakati za uhuru hazikuishia Maghrib tu. Uhispania, kwa mfano, ilipitia maendeleo ya aina hiyo lakini haikuathiriwa sana na Ukhariji. Hapa mapambano yalifanyika hasa baina ya makundi mawili makubwa ya mbari za Kiarabu, ambayo yalikuwa maadui wa jadi, Wakay na Wakalbi.

Mwishowe madaraka yalishikwa na mfalme wa Waumaya, Abd al-Rahman b. Muawiya, ambaye mama yake, Rah, alikuwa Mberiberi aliyetekwa kutoka kwenye *kabila* la Nafza. Alitoroka kutoka Maghrib, na baada ya safari ya mikasa mingi aliweza kuingia tena Uhispania na kuanzisha utawala huru. Mnamo mwaka 929, mtawala wa nane wa nasabatawala huo wa kifalme, Abd al-Rahman III, aliabadili utawala huo na kuufanya kuwa Ukhalifa, na hivyo kufuata mfano ulioanzishwa na Wafatimi. Huu ulikuwa wakati mzuri kwa Waislamu wa Hispania.


Maghrib ya Enzi ya Kati, pamoja na upanuzi wake kwenye mkono wa nchi ya Iberia, ilikuwa na mapendeleo yaliyofuata mielekeo miwili: Kaskazini, kwenye ulimwengu wa Kiukristo, nchi ya biashara na *jihadi* na kusini, yaani Afrika kusini mwa Sahara, ambako kulipatikana dhahabu.

Wimbi la upanuzi nje ya Pyrenees lilisimamishwa mara moja mnamo mwaka 732. Maamiri wa Kordoba walilazimishwa kuingia kwenye *jihadi* ya kujihami dhidi ya msukumo wa Kiukristo katika mpaka wao wa Kaskazini. Kuipoteza kabisa Barcelona mapema mwaka 801 kunaonyesha mafanikio kidogo ya *jihadi* hiyo, ambayo ilikuwa imeanza na nguvu mpya kutoka Maghrib kuelekea Ulaya kuanzia Kayrawan mnamo karne ya tatu na nne. Ziyadat Allah I (817-838) alichukua nafasi aliyopewa na Euphemius, bwanyenye mkuu wa Sisilia, kwa kukiingilia kisiwa hicho. Shambulio hili liliongozwa na *kadi* Asad b. al-Furat. Utamalaki huo ambao kwao Kayrawan ilipingwa na Byzantium, baada ya muda mfupi ukawa tatizo na kazi ngumu. Ulianzia mwaka 827 na haukwisha hadi baada ya miaka hamsini hivi, kwa kutekwa mji wa Sirakusi (878). Waaghlabidi pia waliukalia mji wa Salabria, ambako walikuwa wakitokea kuisumbua miji kadhaa ya pwani. Shambulio lililowauma sana Waukristo wote lilikuwa dhidi ya Roma (846), ambapo hata sehemu takatifu hazikusalimika, lakini wakati wa kurudi nyumbani jeshi la Waaghlabidi liliangamia katika dhoruba.

Ishara ya hatari iliyoikumba Italia ya kusini iliongezwa wakati Ibrahim II alipofika kwenye ardhi ya Italia mwaka 902, akiiongozwa na wazo la kijinga la kufika. Maka kupitia Roma na Byzantium. Ujasiri huo ulifikia kikomo miezi kadhaa baadaye wakati amiri akiwa anaumwa ugonjwa wa kuhara,



10.3 Kuba la Baradiyi la Marakesh: urembo wa kina chini ya kuba. (J. Devisse)



10.4 uga wa ndani wa ribat ya Sus, ukionyesha jengo la ghorofa mbili: kuba dogo likiremba mlango wenye mnara (Taasisi ya taifa ya uchimbuzi na sanaa, Tunis)

alipokufa chini ya kuta za Kosenza (tarehe 23 Oktoba 902). Ieleweke kwamba matukio haya yaliwezesha uamiri mdogo wa Kiislamu, ulioanzishwa na mamluki ambao mwanzoni walikuwa wakilipwa na wafalme wa Italia, kuwa na mizizi yake huko Bari kuanzia 847 hadi 871.

Migongano hii yenye ghasia isitufanye tufikiri kuwa hapakuwepo na mahusiano ya amani wakati wa chuki hizo. Miaka hamsini ya migongano, ikiwemo na safari za mashambulizi ya baharini kama ishirini hivi zilizoanzishwa kati ya mwaka 703 na 752, hasa dhidi ya Sisilia na Sardinia, ilifuatiwa na miaka hamsini ya amani kamili Maghribi ya Mediterania (725-807), wakati ambapo mapatano ya

kuacha kupigana yalifanyika na kukawa na kubadilishana mabalozi. Mojawapo ya shughuli hizi ambayo inafahamika sana ni ile iliyoanzishwa kutokea Baghdad kupitia Kayrawan kwenda Karolingian Gaul wakati wa vuli ya mwaka 801. Kinyume na H. Pirenne alivyofikiri, hakukuwa na kuvunjika kwa mahusiano baina ya ufalme wa Muhammad na ule wa Charlemagne. Biashara iliendelezwa na hata kujumuisha bidhaa nyeti kama vile kupri (shaba nyekundu), chuma au silaha, ambazo Ifrikiya ilizipatia Sisilia. Katika kilele cha vita, miji ya Naples, Amalfi, Gacta, Venise na Genoa iliendeleza biashara zake huko Maghrib na haikusita kufanya nayo makubaliano ya kirafiki.

Uhusiano wa Afrika ya kusini mwa Sahara ulikuwa wa amani wakati wa kipindi kinachozungunziwa. Ni kweli kwamba Afrika ilitoa watumwa, lakini ndani ya muktadha wa kipindi hiki kitendo hiki si lazima kwamba kilikuwa cha ghasia, au kwamba kilihusu Afrika tu. Naples, kwa mfano, iliua watumwa weupe, *Sakaliba* huko Maghrib, na nafasi ya Verdun katika biashara ya kuwauza matowashi inafahamika vizuri. Iwe ni Kayrawan au Kordoba, Waafrika walionunuliwa katika jimbo la kusini mwa Sahara walifanya kazi kwenye jeshi. Hivyo hapo walichangia kikamilifu katika kuipantua Ifrikiya huko Sisilia na Italia ya kusini, na ndani ya nchi waliyaimarisha mamlaka ya maamiri wa Kiaghlabi na Kiunmaya.

Ndani wa mfumo huu wa nyendo nyingi mchanganyiko za watu na bidhaa, wafanyabiashara matajiri wakati mwingine pia walitokea kuwa mabalozi au wanasiasa mashuhuri. Hiki ndicho kilichotokea hasa kwa Muhammad b. Arafa, ambaye alitumwa na Aflah b. Abd al. Wahhab (823-871), Imamu wa Tiaret, kupeleka zawadi ya thamani kwa mfalme wa Sudan. Ubalozi aliokabidhiwa ulikuwa ndio wa mwanzo kabisa tunaoufahamu, kulingana na nyaraka za kidiplomasia, ambao ulikuwepo baina ya Maghrib na Afrika ya kusini mwa Sahara.

### *Jamii na Utamaduni*

Maghrib ya Enzi za Kati haikuwa na watu wengi kama ilivyokuwa katika karne ya tisa. Hali ilivyokuwa wakati huo, tofauti kabisa na ile ya vipindi vya baadaye, ilikuwa ya kuelekea kwenye kuwapatia makazi wanomadi ambao waliishi Maghrib ya kati kwenye sehemu zinazopakana na Sahara, na kuelekea kwenye ukuzaji wa miji. Miji mikuu minne ya kisiasa na kitamaduni ya jimbo hili, yaani Kayrawan, Tiaret, Sijilmasa na Fez - ilikuwa ndiyo matunda ya utamaduni wa Kislamu-Kiarabu. Mnamo karne ya tisa, Kayrawan ilikuwa kwa hakika na wakazi zaidi ya mamia ya maelfu na Sijilmasa nayo ilikuwa na watu wengi na utajiri mkubwa. Mkusanyiko wa watu mijini haukuwa sawa sehemu zote katika eneo hili la dunia. Maghrib ya mashariki, Sisilia na Uhispania, kwa mfano, zilikuwa ndizo sehemu zilizokuwa na hali ya kimji zaidi.

Kitu hasa kilichokuwa kikitofautisha jamii hii na jamii nyinginezo ni ile hali yake ya kuwa na mchanganyiko wa watu tofauti. Watu wa Maghrib walikuwa na msingi wao wa Waberiberi, nao wenyewe walikuwa wametofautiana sana. Hispania ilikuwa na watu ambao zaidi walikuwa Waiberia na Wagothi. Hadi katikati ya karne ya kumi na moja idadi ya Waarabu ilikuwa ndogo. Huko Ifrikiya kulikuwa na makumi kadhaa ya maelfu ya watu, labda laki moja au sana sana laki moja na hamsini elfu. Waarabu walikuwa wachache zaidi huko Hispania, na takriban kulikuwa hakuna hata mmoja huko Maghrib, ambako dalili za kuwepo kwao zinaweza kuonekana tu huko Tiaret, Sijilmasa na Fez. Waberiberi, kwa upande wao walikuwa wamejitawanya hadi kwenye musoma wa Iberia ambapo waliwazidi Waarabu. Pamoja na haya, kulikuwa na makundi ya makabila mawili ambayo idadi yao na nafasi yao maalum ni vigumu zaidi kuitathmini. Kwa upande mmoja, kulikuwa na Wazungu - watu wa asili ya Kirumi, Kijerumani au Kislav - ambao walichukuliwa kwa jumla kuwa *sakaliba*. Kwa upande mwingine, kulikuwa na watu weusi, ambao maisha yao yalifungamanishwa



na maisha ya familia tajiri au zinazojiweza au ambao walifanya kazi kama wapambe wa maamiri, kama ambavyo imekwishaeleza.

Aidha jamii ya kale kwenye nchi za Maghribi za Uislamu ilikuwa na aina tatu za wanaume: watumwa, waliokuwa watumwa zamani, ambao kwa jumla waliitwa *mawali*, na watu huru kwa kuzaliwa.

Watumwa walikuwa wengi sana katika sehemu za miji mikubwa, lakini takriban hapakuwa na watumwa kwenye sehemu zilizokuwa na idadi kubwa ya wanomadi na zenye mifumo thabiti ya kikabila. Inakadiriwa kuwa watumwa walikuwa ni moja ya tano ya idadi ya watu wa miji mikuu ya Ifrikiya na Hispania. Kama ilivyokuwa kwenye tabaka nyingine za kijamii, kulikuwa na wale waliokuwa na bahati na wale ambao hawakuwa na bahati. Watumwa walikuwa wanapatikana kwenye nyumba za masuria - kama vipenzi weupe au weusi na matowashi - kama vile kwenye kila sekta ya maisha ya kiuchumi na ngazi zote. Hadhi ya mtumwa ilikuwa sio ya kuonea wivu, licha ya ulinzi uliotolewa na sharia ya Kiislamu na mafanikio yasiyo ya kawaida ya watumwa kadhaa. Hata hivyo, jukumu lao la kiuchumi lilikuwa kubwa, kwani wao ndio waliokuwa 'mashini' za kuzalisha mali. Katika sehemu ya mashariki ya Maghrib na Hispania, sehemu kubwa ya wafanyakazi wa nyumbani, mafundi-stadi na wafanyakazi wa mashambani walikuwa watumwa au nusu-watumwa, hasa kwenye mashamba makubwa ambayo wakati mwingine yalizunguka vijiji kadhaa.

Hata hivyo, hadhi ya mtumwa haikudumu milele. Ilikuwa ni ukweli unaofahamika kuwa Kurani iliweka msisitizo wa kuridhisha kuhusu ustahiki wa uhuru. Kulingana na hayo, daraja za watumwa, kwa kutumia muungano wa athari ya uhuru na ununujaji wa haki, zilipunguzwa polepole kadri watumwa walivyozidi kutaka kupanda juu kwenye ngazi nyingine kijamii, ile ya *mawali*. Nyendo za kijamii, ambazo kwa kweli zilikuwepo, zilichangia sana katika kuleta uhuru.

Ingawa kisharia *mawali* walikuwa huru kutokana na kuondoshwa kwa utumwa, waliendelea kuishi wakiawa karibu sana na mabwana wao wa zamani na hivyo wakawa katika jumla ya watu waliowategemea mabwana zao hao. Kulikuwa na watu wa aina kadhaa wanyenyekevu ambao walikuwa katika kundi la *mawali*. Wale wasiokuwa Waarabu, kwa hiari yao wenyewe wakajiweka chini ya ulinzi wa mtu mashuhuri, Mwarabu, na kuchukua *nisba* au kizazi cha mbari yake. Mabwana na watwana wote wakawa wamefaidika na muungano huu wa *wala*. Wadaminiwa walifaidika kutokana na ulinzi wa bwana zao, wakati mdhamini alijipatia sifa na madaraka kulingana na idadi ya watu wanaomtegemea.

Watu huru kwa jumla waligawanywa katika madaraja mawili, jamii ndogo ya watu walio bora, mashuhuri na mara nyingi matajiri, *wakhassa*; na watu hohehahe ambao ndio waliokuwa wengi, *waamma*. *Wakhassa* ndio waliokuwa watawala. Kundi hili lilijumuisha waali wa kuzaliwa, au kwa waliotokana na jadi ya uaskari, wasomi na, kwa jumla, watu wote wenye mali. Utajiri wa baadhi ya *wakhassa* mara kadhaa ulifikia kiasi kikubwa. Wakilinganishwa na *wakhassa*, *waamma* walikuwa ni makundi anuwai ya wakulima wadogowadogo, wakulima wa kati, mafundi, wauza maduka na kundi kubwa la vibarua ambao walifanya kazi katika mashamba na mijini. *Waamma* hawakunyimwa nafasi ya kujiunga na *wakhassa*, kwani hapakuwa na muundo thabiti wa kisharia ambao ulizuia jambo hilo.

Pamoja na vipingamizi vya kimbari na kijamii kulikuwa na vipingamizi vingine vya kidini. Wakati wa kutamalakiwa kwa Maghrib dini ya jadi, Uyuda na Ukristo, ziliendelea kuwepo kwa pamoja. Uislamu tikawavutia watu wengi kutoka katika tabaka zote za kijamii. Hadi kufikia karne ya tisa Uislamu ulikwishakuwa ndiyo dini ya walio wengi. Wakati takribani hakuna chochote kilichokuwa kimebakia kwa upande wa dini ya jadi, Uyuda na Ukristo ziliendelea kuwa na kiasi fulani cha wafuasi wenyeji wa sehemu hiyo. Wafuasi hawa walikuwa *wadhimmi* wa jadi au watu

walioruhusiwa na Waislamu kuendelea na dini yao ya jadi ambao mbali na kuwa na uhuru wa kuabudu dini yao walikuwa na nafasi nzuri maalumu kifedha na kihadhi. Nchini Hispania, *comes* ndiye aliyekuwa kiongozi wao, wakati mwingine akiitwa *mlinzi*. Vyanzo vingi vinaeleza kwamba *wadhimi* na Waislamu waliishi maisha ya namna moja na walielewana. Kiwango cha kuelewana kilikuwa kikubwa kiasi kwamba katika nyakati fulani fulani baadhi ya Waukristo, hasa wale wa matabaka ya chini, waliwaheshimu kwa dhati na kuwasifia Waislamu maarufu katika jamii yao walioishi maisha ya kujinyima anasa na kumwabudu Mungu. *Majariya*, au wanawake watumwa walioolewa na Waislamu na ambao waliendelea kuwa na imani zao za Kiyahudi na Kiukristo, walikuwa si haba. Watoto waliozaliwa katika ndoa mchanganyiko kama hizo aghalabu walichukua dini za baba zao.

Aidha ubaguzi wa rangi haukuwepo katika nchi za Maghribi za Kiislam katika Enzi ya Kati. Bila shaka, kama ambavyo imekwishasisitizwa, Waarabu walijiona kuwa bora kuliko wengine lakini walichanganyika na watu wengine bila matatizo yoyote. *Majariya* weusi walithaminiwa kama wengine na *machotara*, ambao hawakuwa na hisia zozote mbaya, waliingia katika tabaka lolote la kijamii bila matatizo. Kadri mwingiliano wa kidini na kuoana baina ya mbari mbalimbali ulivyozidi kuongezeka, ndivyo ilivyokuwa vigumu kufuatilia nyuma nasaba za koo mbalimbali, japokuwa jadi ya Kiarabu ilielekeza nasaba kwa upande wa baba. Kwa ufupi, jamii ya Kihispania-Kimaghrib, enzi hizo za kati ilikuwa na tabia ya kuvumiliana, changamani sana, yenye mtandao wa jamii ndogo zenye upekee lakini zenye kuhusiana kwa karibu sana kwa njia maridhawa.

Lugha kadhaa zilizungumzwa kwenye nchi za Maghribi za Kiislam katika kipindi hiki kinachozungumziwa. Kwanza kabisa kulikuwa na lahaja za Kiberiberi, zilizotofautiana na zilizosambaa Maghrib kote, hasa kwenye sehemu za vijijini na milimani, ambako Kiarabu kisingeweza kupenyeza kwa urahisi. Lahaja hizi hata hivyo, hazikufuata majeshi kwenda pwani ya Kaskazini ya Mediterani. Kwa kweli, hakuna alama ya aina yoyote ya lahaja za Kiberiberi iliyoonekana Hispania au Sisilia ambako lugha za kienyeji zilishindana sana na Kiarabu. Huko Hispania, lugha ya Kihispania-Kirumi haikuendelea, na ilitumika zaidi mashambani na mijini. Lugha ya Kiifrika-Kirumi lazima ilitumika miongoni mwa wakazi wa mjini wa Kiukristo. Lugha zote hizi zilikuwa hasa za mazungumzo. Lugha pekee ambayo ilikuwa ya kitamaduni na iliyoandikwa ilikuwa ni Kiarabu, ambacho kilitumiwa na Waislamu na *Wadhimmi*.

Kulikuwa na idadi kubwa ya vituo vya kitamaduni. Kila mji mkuu wa jimbo na miji mikuu mingine yote ilikuwa na washairi wake, *waadib* wake (wasomi), na viongozi wao wa dini au *Fakih*. Vituo vilivyokuwa maarufu zaidi vilikuwa Kayrawan, Kordoba na Fez. Katika vituo hivi, fasihi ilipata msukumo zaidi kutoka Mashariki. Katika mapana yote ya Uislamu, ilikuwa ni washairi wale wale na *waadib* wale wale ambao walihamasisha mapenzi hayo na njia zile zile za kifasihi zilifuatwa. *Rihla* au safari iliyojumisha maadili ya kisomo na yale ya hija, ilihakikisha kuwepo kwa mahusiano ya karibu na yasiyo katizwa baina ya miji mikuu ya Maghribi na ile ya Mashariki. Watu na mawazo yalihama kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine kwa kasi ambayo ilishangaza sana, kwani mawasiliano yalikuwa ya polepole mno, magumu na ya hatari. Ifrikiya, kama ilivyokuwa katika sehemu zingine za ulimwengu wa Kiislamu, kulikuwa na upendeleo wa tenzi baina ya watu wa daraja la wasomi, na kila mtu alikuwa ni mshairi wa aina fulani. Hata kulikuwa na wafalme kadhaa ambao walikuwa weledi wa kuandika tenzi, kama vile Muhammad b. Ziyadat Allah II (d. 896), ambaye alikusanya diwani mbili, ambazo, zote kwa bahati mbaya, zimepotezwa. Mji mkuu wa Waaghlabi nao ulikuwa na wanafilolojia ambao walikuwa maarufu sana kiasi cha kuainishwa peke yao na al-Zubaydi kwenye kitabu cha *Tabakat al Nahawiyin*. Hata hivyo, inaonekana kuwa falsafa, ambayo ilikuwa tayari inaanza kutambulika kwa kiasi fulani Mashariki na al-Kindi (d. 870), ilikuwa

bado na isingeweza kukubalika Ifrikiya. Mji ambao Sidi Ukba aliutabaruku kwa ajili ya ulinzi wa Uislamu haukukubaliana na uhuru wa mawazo ambao ulikuwa na mashaka kama huu. Taaluma hii ilikuwa bado ipo katika uchanga wake, hata huko Hispania ambako ilichambuliwa vyema na mabingwa waliotambulika kidunia, hasa Ibn Massarra (d. 931).

Katika ulimwengu wote wa Kiislamu wakati wa Enzi ya Kati, watu hawakufurahia tu kujihusisha kwenye kuandika tenzi na majadiliano ya kifalsafa, bali pia walifurahia kunywa, kuimba na kucheza, hasa kwenye majumba ya kifalme. *Wajariya*, waliofundishwa kwenye shule za kuimba na kucheza huko Madina na Baghdad, walitafutwa sana na bei zao wakati mwingine zilihitaji fedha nyingi sana. Watunzi mashuhuri pia walitafutwa sana. Mmoja wao kati ya hawa alikuwa Ziryab (789-852), *mawla* mweusi wa *Kiabbasi*. Baada ya kukaa kwa muda fulani huko Kayrawan, alikwenda Kordoba kwa mwaliko wa al-Hakam I (796-822). Ziryab alileta mabadiliko makubwa kwenye tabia za kifalme na tabaka tawala katika jamii na akawa ndiye msuluhishi mashuhuri sana. Muziki wake, ukisaidiwa na namna fulani ya uboreshaji ambao aliubuni mwenyewe, baada ya kipindi kifupi tu ulichukua nafasi ya nyimbo za zamani na umeendelea kuwepo karne zote hadi leo. *Maluf* mtindo ambao bado unatumika hadi hii leo huko Maghrib, na *flamenko* ya Kihispania zinahusiana kwa mbali na mapinduzi yaliyoletwa kwenye muziki na Ziryab.

Wakati huu, sayansi ilikuwa haijafika popote zaidi ya hatua zake za mwanzo huko Hispania. Huko Kayrawan, hata hivyo, shule ya tiba ikiwa na mabingwa kama vile Ishak b. Imrani na Ziyad b. Kalfun (d. 920-1) ilikuwa imekwisha pata sifa ya aina fulani. Karne ya tisa lazima ikumbukwe hasa kwa sababu ya majengo yake mawili ya ukumbusho wa Uislamu, msikiti wa Kayrawan, ambao ulijengwa hasa na Waaghlabi, na msikiti wa Kordoba ambao, ingawa ulianzishwa na Abd al-Rahman I mwaka 785, haukumalizika hadi zilipopita karne mbili chini ya utawala wa 'Bwana wa Kasri' Ibn Abi Amir (988). Lazima pia ifahamike kuwa chuo kikuu mashuhuri na msikiti wa al-Karawiyin huko Fez, vilianzishwa mwaka 859 na mwanamke kutoka Kayrawan.

Katika kipindi chote cha Enzi ya Kati, masuala ya kitamaduni yalibakia hasa kwenye mikono ya makasisi, yaani 'fakih' katika ulimwengu wa Kiislamu. Katika karne ya tisa, hakuna mtazamo wa kitaaluma ambao ulikuwa unepata kuongoza na hivyo kulikurwa na uhuru wa mawazo kwa kiasi fulani na fujo za imani zilizoshikwa na hasira. Jambo la kuabangaza ni kwamba mji mkuu ambapo uhuru wa mawazo ulizuiwa sana ulikuwa Kordoba. Kulikuwa na uvumilivu mkubwa huko Tiaret; mji huo ulitawaliwa na Waibadi ambao walifahamika sana kwa uasi wao. Ni ukweli unaokubalika kuwa kwa upande wa Kayrawan, kuanzia katikati ya karne ya tisa na kuendelea, Msikiti Mkuu ulikuwa wazi kwa vikundi tofauti vya Waibadi, Wasufri, na Wamutazili, ambao walidiriki kuomba na kufundisha waziwazi mawazo yao yasiyokubaliana na ya dini iliyokuwepo mbele ya macho na masikio ya Wasunni. Majadiliano hayo yalikuwa ya kuvutia, ya makelele na wakati mwingine yalisababisha magomvi yaliyofuatiwa na kupigana ngumi.

Karne hii ilikuwa ni kipindi cha shauku ya sharia na dini. Kwa upande mwingine Wamutazili wakiwa kwenye madaraka huko Kayrawan walijihusisha na kujihami kiupembuzi, wakati kwa upande mwingine, Wasunni, ambao ndio waliokuwa idadi kubwa ya watu na ambao mara nyingi walichukua nafasi ya upinzani, walichota ushauri wao kutoka kwenye mapokeo. Washikilia ukale na washikilia usasa walikuwa katika hali ya mgongano.


Hatimaye, kuanzia katikati ya karne ya tisa na kuendelea, wakati Sahnun (777-854) alipowafukuza 'wasambazaji wa uzushi' kutoka kwenye Msikiti Mkuu wa Kayrawan, kipindi ambamo imani 'sahihi' ilikuwa ikianza kupata mashiko, magomvi yaliendelea bila kupungua. Migogoro ilijitokeza na kuendelea kati ya waumini wa Usunni na maadui wao walikuwa wakijitokeza kwenye ngazi za Waibadi au Wasufri. Sahnun alitekeleza majukumu muhimu sana



10.5 Mlango na matao yaliyozibwa ya sura ya magharibi ya msikiti wa Kardoba. (Hatimiliki ya picha: Hifadhi za Nyaraka za Werner Forman, London)

katika maendeleo ya vurugu hizi, na kitabu chake cha adhimu cha sharia kiitwacho *Mudawwana* kilisababisha hatimaye kuzidi kwa umaarufu wa mafundisho ya Malik. Sahnun alipata heshima ya bingwa na alikuwa na idadi kubwa ya wafuasi ambao walisambaza neno lake, sio tu katika Ifrikiya, bali pia huko Hispania.

Kipindi hiki ambacho tumemaliza kukiangalia kilikuwa muhimu katika historia ya Maghrib. Ni wakati huu ambapo sehemu hii ya Afrika ilipata uhuru wake, ilifanikiwa kuainisha mipaka yake ambayo imebakia vilevile bila mabadiliko hadi hivi leo, na kuvipa mwelekeo vipengee muhimu vya utambulisho wa utamaduni na imani yake.



## *Dhima ya jangwa la Sahara na wana Sahara katika mahusiano kati ya Kaskazini na Kusini*

Japokuwa ni mahali penye mazingira magumu, Sahara, jangwa kubwa kuliko yote duniani, halikuwa kizuizi tu bali pia kiungo kati ya nchi za Kaskazini mwa Afrika na Sudan na lilikuwa na dhima muhimu sana katika mahusiano hasa ya kibiashara kati ya Kaskazini na kusini. Njia chache na ngumu kupitika za misafara zilizokatisha jangwa hili, zilitumiwa mara nyingi, katika kipindi cha Uislamu, na wafanyabiashara kutoka Maghrib, Ifrikiya, Misri na vituo mbalimbali vya biashara vya Kaskazini mwa Sahara.

Watu wa Sahara walikuwa wamechanganyika. Sahara Maghribi na kati ilikaliwa na Waberiberi ambao mara nyingine walikuwa na damu ya Kinegro. Mashariki mwa Sahara, likiwemo jangwa la Libya pia ilikaliwa na Waberiberi, kwa upande wa Kaskazini, ambapo sehemu za kusini zilikalikwa na Wanegro wa jamii mbalimbali za Watubu kama vile Wazaghawa Wateda na Wadaza. Watu hawa walisambaa Kaskazini hadi kufikia maoasisi ya Kufra na Taizerbo yapata digrii za latitudo 26 Kaskazini.

Waberiberi wa Sahara walikuwa wa makundi mawili, yaani Wasanhaja na Wazanata. Wasanhaja zaidi walikuwa wanomadi, wafuga ngamia, kondoo na mbuzi, ilhali Wazanata na makundi mengine ya Kiberiberi yenye udugu na kundi hili kama vile Wamazata na Walawata walikuwa nusu wanomadi na nusu wakazi wa kudumu. Oasisi nyingi za kuvutia za Sahara ya Algeria zilianzishwa na baadhi ya makundi haya pengine baada ya kipindi cha utawala wa Warumi. Watu hawa walikuwa wachimba visima wenye uzoefu ambao walichimba visima vya ardhini na kutumia mfumo wa mifereji iliyojulikana kama *kanat* au *foqqara*. Walitoboa pia visima vya kububujika. Mambo haya mawili yana historia ndefu na yaelekea Wazanata walijifunza ufundi wa kuchimba *mafogqara* na visima vya kububujika kutoka kwa Waberiberi-*Walibyco* wa kale wa Sahara ya Mashariki.

Katika kipindi hiki, Watubu peke yao waishio kusini mwa Sahara Mashariki, ndio waliendelea kuzingatia dini yao ya asili. Wasahara wengine wote, isipokuwa pengine baadhi ya Wazanata waishio Kaskazini mwa Sahara, polepole walisilimishwa.

Kusilimu kwa Waberiberi wa Sahara kulianza mapema mnamo nusu ya kwanza ya karne ya nane. Yaelekea kwamba Wasanhaja na Wazanata wa Sahara, kama Waberiberi wa Afrika Kaskazini, mwanzoni walikuwa waumini wa imani halisi ya Kiislamu. Lakini baadaye, wakati Waberiberi wa Afrika Kaskazini walipoikataa imani ya Sunni kutokana na unyanyasaji wa kisiasa na kifedha wa Makhaliifa wa Kiurnaya, na kunako katikati ya karne ya nane, walijiunga - hasa na vikundi vile vyenye asili ya Wazanata - na madhehebu mawili ya Kikhariji yaliyopingana na Sunni, yaani madhehebu ya Sufri (wa itikadi ya mrengo wa kushoto) na madhehebu ya Ibadi (wa itikadi ya

mrongo wa kati). Wazanata wa Sahara, au baadhi yao, pia walifuata madhehebu haya mawili. Wasahara wenye asili ya Kisanhaja, ambao mnamo karne ya nane walikuwa Waislamu wa mashakamashaka, hawakuzingatia imani halisi hadi katikati ya karne ya kumi na moja kutokana na propaganda za Wamoravi. Wazanata walioishi katika vijiji vya Sahara ya Tripoli walishika mapema imani ya Kiibadi iliyokuwa imepokelewa na ndugu zao wa maeneo ya mashariki na katikati ya mkoa wa Waberiberi ambao walianzisha huko tawala za kiimamu au madola kadhaa, wakianza na Uimamu mdogo ulioanzishwa sehemu ya Kaskazini-Maghribi mwa Tripolitania na kuishia Uimamu wa Kirustumi huko Tahert ambao umaarufu wake ulitambuliwa na Waberiberi wote wa Kiibadi wa Afrika Kaskazini.

Wamiknasa ambao walipokea imani za Kisufri, waliishi Tafilalet ambapo walianzisha, mnamo mwaka 757, dola ndogo ya Kisufri, ambayo mji wake mkuu ulikuwa Sijilmasa. Mji huu, uliotawaliwa na ukoo wa Banu Midrar, haraka ukawa kituo kikubwa cha biashara na Sudani kama mojawapo ya vituo vya mwisho vya misafara iliyounganisha Afrika Kaskazini na ufalme wa kale wa Ghana, uliojulikana kwa wanajioografia wa Kiarabu wa zama za kati kama 'nchi ya dhahabu'. Ndani yake mlipita njia ya biashara hadi mji wa Tahert (ujulikanao hivi leo kama Tiaret), mji mkuu wa Uimamu wa Kiibadi wa Warustumi ambao ulikuwa kituo muhimu cha kisiasa na kiuchumi. Mji huu wa soko maarufu haukuivutia tu idadi kubwa ya wafanyabiashara wa Afrika Kaskazini, Waibadi na wasio Waibadi tu, bali pia ulivutia mabepari wa Kiarabu kutoka Kayrawan, Basra na Kufa.

Wafanyabiashara wa Kiberiberi waliojiingiza katika mahusiano haya kwa jumla walikuwa wa makundi mbalimbali ya Wazanata, wakati ambapo Wasahara wa kuzidi la Wasanhaja mara nyingi walitumika kama waongoza misafara waliopewa nyenzo na wafanyabiashara wa Afrika Kaskazini, na pia walisindikiza misafara hii chini ya ulinzi wa machifu wa Wasanhaja wa Awdaghust, Tadmekka na sehemu nyingine.

### *Jangwa la Libya*

Wakati Waarabu walipoteka Misri, oasisi nne katika jangwa la Libya, yaani, Kharja, Dakhla, Farafra na Bahriyya (Bahnasat al-Wah), ziliunda dola ndogo iliyotawaliwa na ukoo wa al-Abdun, wa asili ya Waberiberi wa Lawata. Dola hii ilitajwa kwa mara ya kwanza katika nusu ya pili ya karne ya nane kama Amal Wah au 'Nchi ya Oasisi'. Katika karne ya kumi, mwana wa mfalme wa Kiberiberi, Abd al-Malik ibn Marwan, alitawala hapo akiamrisha maelfu kadhaa ya askari wapandafarasi. Mbali na Waberiberi wa Lawata, katika sehemu hii paliishi pia jumua kubwa ya Kiukristo yenye asili ya Kikhufu, na Waarabu wanomadi wa mbari ya Banu Hilal. Njia kadhaa ziliunganisha nchi ya Oasisi na miji mbalimbali ya Misri, kwa upande mmoja, na Oasisi ya Santariya (Siwa), kwa upande mwingine. Oasisi zilikuwa na idadi kubwa ya mitende na miti mingine ya matunda na pia migodi ya alumi.

Njia yenye kuchukua mwendo wa siku kumi kwa mguu iliunganisha oasisi ya Bahnasat al-Wah (Bahriyya) na Oasisi ya Santariya au Siwa (iliyojulikana awali kama Ammonium), ambapo ndipo palikuwa makutano ya njia zote za Maghribi. Njia muhimu zaidi kati ya hizi zote iliunganisha Santariya na Misri kwa upande mmoja na Maghrib na Kawar kwa upande mwingine. Yaelekea Santariya kwa muda mrefu haikutegemea Misri na iliunganishwa kwenye jimbo la Aleksandria mnamo karne ya kumi na tatu.

Katika sehemu za mbali za Nchi ya Oasisi kulikuwa na mkoa wenye ufanisi mkubwa, uliojulikana kama Wah Sebru au Shebru, ambao haukufikika kwa urahisi na ambako, katika karne ya kumi na moja, 'hakuna aliyewahi kufika huko ila wasafiri wachache waliopotea njia





jangwani'. Mkoa huu ulikuwa na mitende mingi, nafaka na aina zote za mtunda na pia migodi ya dhahabu; kutajwa kwa migodi ya dhahabu hapa kumekusudiwa kukumbusha tu juu ya biashara ya dhahabu na Maghribi ya Sudan ambako dhahabu ilikuwa ikisafirishwa hadi Misri. Kaskazini-Mashariki mwa mji huu kulikuwa na ziwa ambalo katika kingo zake kulikuwa na kambi za watu wajulikanao kama wanomadi wa Kawar (Watubu?).

Sebru au Shebru hii (jina lililotokana na neno la Kikhufu *tchobro* lenye maana ya kijiji) ni kundi la Kufra, ambako kuna maji mengi na mitende na milimao inalimwa, pamoja na nafaka. Wakazi wa sasa wa sehemu hii ni Wazawiya, Waberiberi walioathiriwa na Waarabu waliotoka Kaskazini mnamo katikati ya karne ya nane na kuwakuta wakazi wasio Waislamu (Kufra - kufara = 'makafiri') wa jamii ya Watubu ambao walikimbilia kwenye milima ya Tibesti au baadhi yao kunawa na wageni. Hivi leo katika Oasisi ya Kufra kuna mamia ya watu wachache wenye asili ya Watubu na wote wamesilimu na kuwa chini ya utawala wa Waarabu.

Njia ya kale ya msafara ambayo kabla ya karne ya kumi iliunganisha Misri na Ghana na iliyorejelewa na Ibn Hawkal, pengine ilipitia Oasisi ya Kufra. Njia hii ilitumiwa zamani, wakati wa Ahmad ibn Tulun (868-884), na baada ya kufika Kufra ilielekea Wadi al-Namus na Wadi al-Kabir, kupitia Fezzan na kutoka hapo, Kawar, Gao na mwisho Ghana. Hii ndiyo njia ambayo Ibn al-Fakih (903) alielezea ifuatavyo: 'Njia kutoka Ghana hadi Misri hupitia katika nchi ya watu wajulikanao kama Wakawa - kaw, (Wagao), kisha katika nchi ya Wamaranda, kisha katika nchi ya Wamurrawat, na kutokea hapo kwenda hadi oasisi za Misri huko Malsana.' Maranda ndiyo Marandet, sehemu muhimu ya kupatia maji kusini mwa Agades, na Malsana pengine ni nyanda za Gilf Kabir zilizoko Maghribi ya Dakhla.

Maghribi mwa Siwa kulikuwa na kundi la oasisi za Awjila zilizokuwa maarufu kwa mitende yake. Kundi hili pia lilijumuisha mji na oasisi ya Jalu (Jalo). Mji mkuu wake ulikuwa Arzakiya na eneo lote lilikuwa na vijiji na mitende na miti ya matunda. Watu wa Awjila kwa hakika walikuwa wa asili ya Waberiberi na pengine walikuwapo pia watu wa makundi ya Lawata kama Wasantariya na Wabarka. Awjila ilikuwa katika njia panda ya njia kadhaa za biashara na ilikuwa kituo muhimu katika njia ya kwenda Sndan. Kwa kupitia katika oasisi hii iliwezekana kuifikia 'sehemu kubwa ya nchi ya Weusi kama vile, Kawar na Kaw-Kaw (Gao)'

Maghribi mwa oasisi ya Awjila kulikuwa na jimbo la Surt au Sirt, lililochukua sehemu yote ya Mashariki ya Tripolitania. Hili ni eneo la Sahara, ambapo jangwa liljulikanalo kwa jina la jangwa la Syrte huenea hadi Syrtis Kuu. Wakazi wake ambao walikuwa wafanyabiashara walizungunza 'lahaja ambayo haikuwa Kiarabu wala Kiajemi wala Kiberiberi wala Khufu'. Pengine ilikuwa lugha ya Kipuni cha Kale.

Jimbo la Surt lilikaliwa na Waberiberi wa Mazata ambao majirani zao walikuwa Walawata wa Barka na Wahawwara ambao walikuwa wanaka Tripolitania ya kati. Mpaka wa Maghrib wa nchi ya Wamazata ulipitia karibu na Tawargha, ambapo huko kusini, eneo walilolikalia lilienea kuvuka Jabal al-Sawda. Mji wa jangwani, Tajrift, ulikaliwa na mchanganyiko wa Wamazata na Waarabu. Katika kipindi hicho oasisi ya Zalha (au Zella) pia ilikuwa ni sehemu ya nchi ya Mazata.

Wamazata wa mashariki mwa Tripolitania walitawaliwa mapema zaidi na Uibadi; wilaya ya Surt ikiwa moja ya majimbo ya dola ya Waibadi iliyodumu kwa mnda mfupi na iliyoanzishwa Tripolitania na Imamu Abul-Khattab Abd Allah ibn as-Samh al Maaffir (757-761).

Imani ya Waibadi ilidumu kwa mnda mrefu huko Tripolitania, na Wamazata waliendelea kuitangaza hadi mwishoni mwa karne ya tisa. Mji wa Waddan, kusini mwa Surt, uliunganishwa kwa njia na mji wa Maghmadas (uliojulikana kama Masemades) ulioko katika pwani ya Mediterania na pia na jiji la Jarma (liliojulikana awali kama Garama). Pengine hii ndiyo njia iliyotumiwa kupitisha

watumwa waliotolewa kama ushuru kwa Waarabu na watu wa Waddan. Watumwa wlikuwa wafungwa weusi kutoka maeneo ya Kawar, Tibesti na Kanem. Njia nyingine iliyounganisha Waddan na Awjila ilipitia mji kwa Zalha (Zella) ambako tende zilikuwa nyingi sana.

Nyaraka za Kiarabu hazitaji sana Hammada al-Hamra na milima iliyozunguka, tukiacha al-Bakri ambaye anatoa maelezo ya njia iliyotoka mji wa biashara wa Jadu, mji mkuu wa sehemu ya mashariki mwa Jabal Nafusa, hadi jiji la Zawila, kituo muhimu cha misafara kilichokuwa kwenye njia ya kuelekea eneo la Kawar na nchi nyingine za watu weusi. Hata hivyo, ilikuwa lazima kutembea jangwani kwa miguu kwa siku tatu kabla ya kufika Tiri au Tira, sehemu iliyokuwa kando ya mlima na iliyokuwa na mitende mingi sana.

Katika mipaka ya Maghribi ya Hammada al-Hamra, kati ya nyanda za juu na Mbuga Kuu ya Mchanga ya Mashariki kuna oasisi ya Sahara na mji wa Ghadames. Eneo hili ambalo hata hapo kale lilikuwa kituo muhimu jangwani (kilichojulikana kama *Cydamus* au Kidame) lilikuwa lango kuu walimopitia wafanyabiashara watokao Tripolitania kwenda katika Nchi ya watu Weusi. Njia iliyounganisha mji wa Sharus katika Jabal Nafusa na eneo la Takrur ilipitia Ghadames. Hadi leo hii, karibu na Sharus, bado inaonekana njia inayokwenda Ghadames inayojulikana kama *trik el Sudan* (njia ya Sudan). Njia hii ndiyo iliyoelekea katika eneo liljulikanalo kama Zafunu (Diafunu) katika Senegal ya juu. Yaelekea kwamba, baada ya Ghadames, njia hii ilipita katika nchi ya Waberiberi wa Kiaskar (Tassili-n-Ajjer ya leo), ikiwa mwendo wa siku kumi na nane kwa miguu kutoka Ghadames.

Wakazi wa Ghadames, tangu kale, walikuwa wakijishughulisha kidogo na kilimo, wakilima mitende na pia kufanya biashara ya Sahara. Wakazi wa mji walikuwa wa makundi kadhaa ya Waberiberi na lugha ya Kiberiberi bado ingali inazungumzwa Ghadames.

Watu wa Ghadames walizikubali, toka mapema, imani za Kiibadi kama majirani zao wa upande wa Kaskazini, Wanafusa, ambao waliishi katika eneo liljulikanalo leo kama Jabal Nafusa na ambao walikuwa na udugu wa karibu nao.

Mwanzoni mwa karne ya tisa, watu wa Ghadames walichukua imani potofu za madhehebu ya Kiibadi ya Khallafiya na Nukkar, na ni kutokana na utumiaji wa nguvu za kijeshi uliofanywa na Wanafusa ndipo imani safi za Uibadi-Uwahbi zilianzishwa tena.

Umbali mdogo mashariki mwa Ghadames kuna oasisi na mji wa Daraj ambao ulikuwa kituo muhimu cha Waberiberi wa Kiibadi. Haiyunkiniki kwamba jina Daraj hutokana na tawi la Wanata la Wabamu Idradj. Njia iliyopitia Sinawan na Daraj iliunganisha Ghadames na mji wa Nalut (au Lalut), ulioko katika sehemu ya Maghribi ya Jabal Nafusa.

### *Kati ya Fezzan na Ziwa Chad*

Katika sehemu ya kusini mwa Tripolitania kuna Fezzan, ambalo ni kundi la oasisi lililoko kati ya Hammada al-Hamra, kwa upande wa Kaskazini, Tassili-n-Ajjer, kwa upande wa Maghribi, miinuko ya Tibesti, kwa upande wa kusini, na Jangwa la Libya, kwa upande wa mashariki.

Ustaarabu wa kale wa Wagaramante haukwisha hadi baada ya utamalaki wa Waarabu huko Maghrib, na hivi sasa kuna sababu za kufikiri (kutokana na misingi ya tikadiriaji tarehe kwa kutumia njia ya kaboni-14 ya vitu vilivyochimbuliwa) kwamba ustaarabu huu haukuharibiwa hadi kati ya karne ya nane na karne ya kumi. Sababu kubwa ya kusnguka kwa ustaarabu wa Wagaramante yaelekea ilitokana na mashambulizi yaliyoongozwa na amiri jeshi wa Kiarabu Ibn al-Ashath ambaye mnamo mwaka 762 hadi 763 aliteka ufalme wa Zawila mashariki mwa Fezzan na kuwaua wakazi wa mji mkuu. Yafaa ikumbukwe, hata hivyo, kwamba ufalme wa Zawila ulinusurika na pigo hili na tikaendelea kuwepo kama dola huru hadi mwishoni mwa karne ya tisa.

Ufalme wa Zawila ulichukua tu sehemu ya mashariki ya Fezzan ya leo. Ulianzishwa ama mwishoni mwa karne ya saba au mapema katika karne ya nane. Sehemu inayobaki ya Fezzan ilikuwa chini ya ufalme mwingine uliochepuka kutoka ufalme wa Wagaramante, unaorejewa na waandishi wa Kiarabu wa enzi za kati kwa jina la Fezzan.

Dola hii hutajwa katika vyanzo vya Kiarabu tokea mwaka 666, wakati Ukba ibn Nafi, ambaye baada ya kuteka Waddan, alielekea mji wa Jarma, mji mkuu wa Fezzan Kuu, ambao mfalme wake alijisalimisha na wakazi wake kusilimu. Nafi akajipenyeza hadi kwenye 'ngome' nyingine za Fezzan, mpaka ukazifikia zile za Kaskazini kabisa.

Kuanzia mwishoni mwa karne ya nane, wakazi wa Fezzan wakawa Waibadi na toka mwanzo walitambua mamlaka ya Maimamu wa Kirustumi wa Tahert. Hata hivyo, kwa muda fulani walikuwa wafuasi wa muasi wa Kiibadi Khalaf ibn al-Samh. Mwishoni mwa karne ya tisa, Fezzan iliunda dola kubwa iliyotawaliwa na chifu huru (*rais*).

Jarma, mji mkuu wa Fezzan, ulisitawi kwa miaka kadhaa hadi karne ya kumi na mbili. Wakati huo pamoja na Jarma, kulikuwepo pia katika Fezzan mji mwingine mkubwa, Tassawa (Tessaoua) ambao 'Weusi' (Wafezzan?) waliuita 'Jarma Ndogo'. Vyanzo vya Kiarabu pia hutaja miji mingine katika Fezzan kama vile Tamarma, uliyopo katika njia ya kwenda Jadul katika Jabal Nafusa. Mji huu haujulikani kabisa kwetu na jina lake yafaa lisahihishwe ili lisomeke kama 'Tamzawa', yaani Tamzau (Tamseua) ya leo. Mji mwingine mkubwa ulikuwa Sabha ambao ni sawa na mji mkuu wa sasa wa Fezzan na ambao ulikuwa na msikiti mkubwa na masoko kadhaa.

Watu wa Fezzan wa enzi za kati walikuwa wa vikundi mbalimbali vya kimbari ambao wote kwa pamoja walijulikana kama Wafezzan. Pamoja na Wafezzan, kulikuwepo pia makundi mengine ya Kiberiberi katika eneo hili. Al-Bakri amewataja Wabanu Kaldin (au Kildin) ambao waliishi katika mji wa Tamarma (Tamzawa) pamoja na Wafezzan na ambao walikuwa na udugu na Wahawwara.

Wakazi wa Jarma (na wale wote wa 'ngome' nyingine za Fezzan) ambao, mapema mwaka 569 walikuwa Waukristo, walisilimu kufuatia mashambulizi ya Waraabu mnamo 666-7. Baadaye walishiriki katika harakati za Kiibadi huko Tripolitania na kupata hasara kama iliyowapata Waibadi wa Waddan na wale wa Zawila baada ya mashambulizi yaliyoongozwa na amiri jeshi wa Kiabbasi Ibn al-Ashath manamo 762-3. Wakati wa Imamu wa Kirustumi Abd al-Wahhah ibn Abd al-Rahman (d. 823) Wafezzan walikwisha kuwa Waibadi.

Yaelekea kuwa mapema katika karne ya tisa Waibadi wa Fezzan walikuwa wamejiunga na muasi wa Kiibadi Khalaf Ibn al-Samh, ambaye baada ya kuwaasi Maimamu wa Kirustumi wa Tahert, alifaulu kuifanya karibu Tripolitania yote kukubaliana naye, isipokuwa Jabal Nafusa ambayo wakazi wake waliokuwa waumini wa dini ya Kiibadi-Kiwahbi walibakia waaminifu kwa Warustumi. Hata hivyo, mnamo nusu ya mwanzo ya karne ya tisa, Fezzan ilichukuliwa tena kama eneo lenye waumini wa dini ya Kiibadi-Kiwahbi.

Dola ya pili iliyokuwepo Fezzan kati ya karne ya nane na karne ya kumi na mbili, yaani Ufalme wa Zawila, imepata jina lake kutokana na jiji la Zawila, lililokuwa mji wake mkuu. Dola hii inajitokeza katika kumbukumbu za kwanza katika karne ya nane wakati wa vita kati ya Waarabu wa Kisunni na Waberiberi wa Kiibadi. Baada ya ushindi uliopatikana, mnamo mwaka 761 - 2, wa Ibn al - Ashath juu ya Abu I-Khattab, *Inamu* wa Kiibadi wa *Ifrikīya*, jeshi la Kiarabu liliteka jiji la Zawila na wakazi wake, Waberiberi wa Kiibadi, kuchinjwa. Pamoja na matokeo haya, Zawila, kwa muda mrefu, ilibakia kituo kikubwa cha Kiibadi.

Mnamo mwanzo wa karne ya kumi, jiji la Zawila lililhamwa, pengine baada ya vita kati ya wakazi wake na Wamazata wa mashariki mwa Tripolitania lakini lilijengwa tena mnamo mwaka 918 ili liwe makao ya nasabatawala wa Banu al Khattab ambao ulitokana na Wamazata.

Raslimali kuu ya Fezzan ilikuwa mazao, hasa mitende na ulezi na shayiri. Ufundi wa umwagiliaji wa *foggaras* (mfumo wa mifereji ya chini ya ardhi) ulienea Fezzan mwishoni mwa kipindi cha Warumi; mashamba huko Zawila yalimwagiliwa kwa maji ya visima kwa kutumia ngamia, njia ambayo bado inatumika Fezzan, au kwa kutumia mashine zijulikanazo kama *injafa* ambazo wakazi wa Maghrib walizijua kwa jina la *khattara*.

Pamoja na ulimaji mazao, shughuli nyingine kuu ya Fezzan ilikuwa biashara ya Sahara. Eneo hili baada ya Nili, kihistoria, ni sehemu muhimu sana kwa mawasiliano na nchi za kusini mwa Sahara. Wagaramante wa kale walikuwa wakipeleka katika bandari za Tripolitania bidhaa kama vile tende, pembe za ndovu na vito vya thamani vijulikanavyo kama *garamantiques* kutoka nchi za kwao na pia kutoka ndani ya Afrika. Biashara ilipitia katika njia ya kale sana iliyounganisha Tripoli na Kawar na Kanem huko Sudan ya kati. Njia hii ilipitia jiji la Zawila na Jabal Nafusa. Biashara ya kuvuka Sahara ndiyo iliyosababisha watu wa makundi yaliyotofautiana sana wenye asili ya Khurasan, Basra na Kufa kufanya makazi yao Zawila kandoni mwa Waberiberi wa Kiibadi. Wafanyabiashara wa Zawila pia walisafirisha watumwa weusi waliotekwa kutoka miongoni mwa watu wa Sudan wa Miri, Murru, Zaghawa na wengineo, ambao wengi wao walikuwa wa kundi la Wateda-Daza.

Njia tatu ziliunganisha mji wa Zawila na Tripolitania na Misri. Njia ya kwanza ilielekea Jadu na halafu Tripoli, hali ya pili iliunganisha Zawila na jiji la Ajadabiya katika ukingo wa mashariki mwa Tripolitania; na njia ya tatu ilitoka Zawila kwenda Fustat, mji mkuu wa Misri. Oasisi zilizojulikana sana katika njia ya kusini zilikuwa zile za Kawar. Mnamo mwaka 666-7 wakati Ukba ibn Nafi alipomiliki *ksurs* (ngome za Fezzan), ngome kubwa miongoni mwao ilikuwa ngome ya al-Kasaba (au al-Gasba); na ilikuwa kubwa sana. Kusini mwa al-Kasaba kulikuwa na Ankalas (Dirki ya leo), jiji kubwa kabisa katika Kawar na ambalo lilikuwa muhimu sana katika masuala ya kibiashara na wakati huo huo lilikuwa makazi ya chifu wa pale. Kusini kabisa mwa Kawar kulikuwa na jiji dogo la Tamalma (au Talamla) lililofanana na mji wa Bilma ya leo.

Mwishoni mwa karne ya tisa, eneo la Kawar lilikaliwa na watu mchanganyiko wakiwemo Waislamu wa kila namna ambao wengi wao walikuwa Waberiberi. Kandokando mwa Waberiberi na wafanyabiashara Waarabu, kuliishi wenyeji wa kundi la Watubu (Wateda-Daza). Mnamo karne ya tisa watu hawa walikuwa warnekwisha kusilimu na labda walikuwa wa madhehebu ya Kiibadi.

Mali ya wakazi wa Kawar ilitokana na mazao (tende), machimbo ya migodi ya alumi, na biashara, hasa ile ya watumwa. Ngamia pia walifugwa kwa matumizi ya wafanyabiashara wa hapo; samaki waliopatikana kwa wingi katika ziwa kubwa lililokuwa karibu na Abzar walivuliwa na kuhifadhiwa kwa kutiwa chumvi. Chanzo kikubwa cha mali ya wakazi wa *kawari* kilikuwa migodi ya madini mbalimbali ya alumi yaliyojulikana kwa jina la Kawar ambayo usafi wake ulisifiwa na wafanyabiashara Waarabu. Migodi hii ilikuwa kusini mwa Kawar katika Anklas na Abzar. Chanzo kingine cha mapato ya wakazi wa Kawar kilikuwa biashara ya watumwa. Idadi kubwa ya watumwa weusi walipitia Kawar kuelekea katika masoko ya Jarma, Zawila na Waddan ambako walisafirishwa kwenda Maghrib na Ifrikiya na pia Misri. Ni dhahiri biashara hii tayari ilishakuwepo tangu zama za kale na ilifanywa na Wagaramante.

Historia ya kale na ya enzi za kati ya Kawar haijulikani kwetu. Yaelekea kwamba mnamo karne ya tisa eneo hili lilikuwa huru, lakini baadaye usultani wa Kawar ulijumuishwa chini ya mamlaka ya ufalme wa Zaghawa au Kanem.

Pamoja na Watubu wa Kawar na Waberiberi wa Kiibadi, ambao pamoja na wafanyabiashara Waarabu waliishi katika oasisi za Kawar, bado paliishi pia katika eneo hili la Sahara Waberiberi wa

Lamita ambao wengi wao waliishi maisha ya kinomadi, Maghribi mwa Sahara, hasa kusini mwa Sus.

Watubu au Wateda-Daza-Zaghawa, ambao tangu zamani sana waliishi katika oasisi za Kufra katika jangwa la Libya na pia katika enco la Kawar, ndio pia walioishi katika ukingo wa kusini ya Fezzan, nyanda za Jado na milima ya Tibesti. Pia waliishi Borku, ambalo ni bonde la chini la jangwa kati ya Tibesti na Chad, na katika nyanda za Ennedi na maeneo ya Kaskazini-Maghribi mwa Darfur. Watubu ambao bado wanaishi katika maeneo yaliyotajwa mwisho hadi leo hii wanaendelea kuitwa Wazaghawa. Yaelekea jina hili, katika wakati huo, ndilo lililotumiwa na wanajiografia wa Kiarabu kuita makundi yote ya Watubu, isipokuwa Wagoran na wahamaji wa Kawar. Maeneo ya kusini mwa Kawar tayari yalikuwa sehemu ya ufalme wa Kanem ambao historia yake inajadiliwa katika Sura ya 15.

## Sahara ya Kaskazini

Oasisi za Sahara ya kaskazini zinaweza kugawanywa katika makundi matatu:


- (1) Oasisi za mashariki, zinazotumia mfumo wa umwagiliaji maji wa visima vya kububujika, zilizoko katika mzunguko wa chini ya milima ya Atlas;
- (2) Oasisi za Maghribi, zinazotumia mfumo wa umwagiliaji wa mifereji ya *foggara*, za tikanda wenye urefu wa kilomita 1,200 kati ya Figuig, kwa upande mmoja, na Tidikelt, kwa upande mwingine;
- (3) Katikati ya makundi haya mawili kuna kundi la tatu la oasisi muhimu litwalo Mzab.

Kundi la mashariki kabisa miongoni mwa makundi haya matatu ya oasisi ni Suf, lililozungukwa na mchanga, likiwa katika njia inayotoka Jarid kwenda Tuggurt na Wargla. Tokea mwanzo wa kipindi cha utamalaki wa Waarabu Afrika Kaskazini, oasisi hii ilikuwa muhimu kiasi, ikiwa kituo kimojawapo katika njia ya biashara iliyounganisha kusini mwa Tunisia iliyokaliwa na Waberiberi wa Kiibadi na vituo vingine vya Kiibadi vya Wadi Righ, Wargla na Sndan.

Wakazi wa Suf walikuwa wa makundi mbalimbali ya uzao wa Wazanata au wenye udugu na kundi hilo la Kiberiberi (kama Walawata). Kaskazini mwa Suf, kuelekea wilaya ya Nefzawa, kulishi wahamaji wa Banu Mulit, ambao pia walikuwa sehemu ya Wazanata.

Maghribi mwa oasisi ya Suf kuna oasisi kubwa za Wadi Righ zilizoko katika mto wenye upana wa kilomita ishirini. Katika kipindi kinachojadiliwa, Wadi Righ ilikuwa na miji kadhaa na vijiji vilivyozungushiwa ngome (*Kusur*). Righ au Arigh hutokana na Waberiberi wa Righa, kikundi cha Wamaghrawa wa kundi kuu la Wanata. Pamoja na kikundi cha Righa kulikuwepo makundi mengine ya Wazanata kama vile Wabanu Wartizalen, Wabanu Wilil, Wabanu Zalghin, Wabanu Itufa, Wamghrawa, Wabanu Yandsajen na Banu Lant. Miongoni mwa Waberiberi wengine waliokalia Wadi Righ au kuishi kama wanomadi karibu na sehemu hiyo ni Wabanu Waarmaz (Warzemar), na jamii tatu zilizoishi kama mabedui zikijulikana kama wabanu Warsifan, Wabanu Ghomara (au Wahomra) na Wabanu Sindjasen.

Historia ya Wadi Righ kabla ya karne ya kumi na mbili haijulikani sana. Katika nusu ya mwisho ya karne ya kumi, watu wa Wadi Righ walikuwa wa makundi mbalimbali ya Wamaghrawa wa Kiibadi. Katika karne ya kumi na ya kumi na moja, oasisi za Wadi Righ zilikuwa na dhima muhimu katika maisha ya Wabadi wa Afrika Kaskazini, lakini vita vya wenyewe kwa wenyewe mnamo mwaka 1078 na mwaka 1108 vilipunguza umuhimu wake.



11.2 Msikiti wa karne ya kumi katika jiji la Tazeur, Djarid. (M. Brett)

Oasisi muhimu kuliko oasisi zote za mashariki mwa Sahara ya Kaskazini ni ile ya Wargla, iliyojulikana kwa wanajiografia wa Kiarabu wa enzi za kati kama Wardjlan au Warklan. Hatujui chochote juu ya asili ya Wargla kutokana na kukosekana taarifa kuhusu oasisi hii kabla ya utamalaki wa Waarabu. Hata hivyo, si jambo lisilowezezana kwamba katika kipindi cha himaya ya baadaye ya Ubizenti tayari kulikuwa na kijiji katika eneo hili kilichotumiwa kama kituo katika njia ya msafara iliyounganisha Numidia na Hoggar na pengine pia kuruba ya mto Niger. Jina 'Wargla' linapatikana katika mbari ya Kimoori ya *Urceliani* ambayo ilijenga makazi fulani Wargla katika kipindi kabla ya uvamizi wa Waarabu. Katika oasisi ya Wargla kulikuwepo pia miji kadhaa wakati walipofika Waarabu wa kwanza, ambayo magofu yake bado yanaonekana.

Wakazi wa Wargla mapema kabisa walipokea imani za Kikhariji kupinga utawala dhalimu wa serikali iliyoifuata imani za mapokeo. Waliongoa kuwa Waibadi, wafuasi wa tawi la mrembo wa kati wa madhehebu hayo na baadaye kidogo wakawa na uhusiano wa karibu na Maimamu wa Kiibadi wa Tahert.

Yaelekea Sadrata au Sadrata ndio ulikuwa mji mkuu wa oasisi ya Wargla kati ya karne ya kumi na karne ya kumi na mbili. Jina la jiji hili linatokana na jina la Waberiberi wa Sadrata, kundi jingine lililokalia Mzab kandokando mwa Biskra. Magofu ya Sadrata yako kilomita kumi na nne kusini mwa jiji la Wargla. Katika magofu haya, kumepatikana mabaki ya msikiti na ya kaburi la Imamu Yakub ibn Aflah, Imamu wa mwisho wa Warustumi ambaye alikimbilia Wargla kufuatia kutekwa kwa Tahert na jeshi la Kifatimi mnamo mwaka 908. Mnamo mwaka 934, jiji la Sadrata lilizingirwa na jeshi la Kifatimi na wakazi wake wakatoroka na kukimbilia Karima (Gara Krime ya leo, kusini mwa Wargla).

Tuna taarifa kiasi juu ya makundi ya watu wa oasisi ya Wargla kati ya karne ya nane na karne ya kumi na mbili. Wawarjlan waliioanzisha, walikuwa tawi la Wazanata, lakini miongoni mwa wakazi wa mwanzo pia walikuwepo watu wa kundi la Wasadrata waliokuwa tawi la Walawata.

Miongoni mwa Waberiberi wengine waliotamakani katika oasisi ya Wargla ni Wabanu Yajrin (au Wayagrin), Watinawata wanaotoka Ghadames; Wabanu Warzemar, kundi lililoishi kama wanomadi kandokando mwa Wadi Righ; na mbari kuu ya Wabanu Wartizalen ambao pia walikalialia Wadi Righ mapema zaidi. Yaonekana kwamba Waberiberi waishio Righ na Wargla walikuwa wamekwisha changanyikana na weusi kabla ya karne ya kumi na mbili.

Miji yote ya oasisi ya Wargla ilikuwa sehemu ya wilaya iliyojulikana kama *iklim Warjlan* (wilaya ya Warjlan). Mwanzoni mwa karne ya kumi, oasisi ya Wargla ilitawaliwa na rais ("chifu") aliyeishi Taghyart; yaelekea *wulat Warjlan* ("Magavana wa Warjlan") walikuwa chini ya huyu rais. Katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na moja Wargla ilikuwa na *mamutawalli* ishirini na watatu. Hawa, pengine walikuwa watawala ambao madaraka yao hatuyajui. Pamoja na rais na magavana, vyanzo fulani hutaja kuwepo huko Wargla kwa wastahiki (ambao pengine walikuwa wafanyabiashara wakubwa) wakijulikana kama *ayan* na *akabir*. Mabaraza ambamo wakazi wa vijiji vyote katika oasisi hiyo waliwakilishwa pia yalikuwa na dhima katika mfumo huu wa uongozi. Mabaraza haya yalikutana katika kijiji cha Tamawat. Baada ya kuanguka kwa Uimamu wa Kirustumi ambao utamalaki wake ulitambuliwa na wakazi wa Wargla, oasisi hii ilikuwa huru kabisa hata pamoja na juhudi za Wafatimi ambao walijaribu kuteka mnamo nusu ya kwanza ya karne ya kumi hasa kutokana na umuhimu wake kiuchumi. Baadaye ilitawaliwa kwa muda fulani na ukoo wa Wabanu Hammad, ukiwakilishwa na gavana.

Tokea mapema katikati ya karne ya tisa, njia ya moja kwa moja iliunganisha Wargla na Tahert, hali njia nyingine ya biashara ilikuwepo kati ya Wargla na mji wa Sijilmasa ambao ulikuwa mmojawapo wa vituo muhimu vya Kaskazini vya njia za misafara kati ya Afrika Kaskazini na Maghribi mwa Sudan ambako dhahabu na watumwa kutoka Ghana na nchi ya Wankara (Mali) walifikia. Mwanzoni Wargla ilikuwa mojawapo tu ya vituo katika njia kuu kati ya Sudan na Misri; njia hii ilipitia Tripolitania na Jarid kuelekea kwanza Wargla na kislia Sijilmasa. Lakini wafanyabiashara wa Wargla punde tu walianza kujishirikislia zaidi katika biashara kati ya Sijilmasa na maeneo yenye dhahabu ya Maghribi mwa Sudan.

Njia ya kale kabisa na ambayo wakati huo huo ilikuwa ya moja kwa moja ikiunganisha Wargla - na hivyo Maghrib yote - na Sudan, ilikuwa ni ile iliyotoka Wargla hadi Tadmekka katika Adrar des Ifoghas na kutokea lipo kuelekea mji wa Gao. Njia hii ilianza Tadmekka na kuelekea Kayrawan ikipitia Wargla na Kastiliya (Tozeur). Biashara kati ya Wargla na Tadmekka ilifanyika tokea mapema mnamo nusu ya mwisho ya karne ya kumi. Mojawapo ya bidhaa muhimu ya biashara ilikuwa nguo zilizobadilishwa kwa dhahabu.

Pamoja na njia ya Wargla-Tadmekka-Gao, kulikuwa na njia nyingine kuu ya kupitia Sahara iliyounganisha Wargla na soko la Maghribi mwa Sudan. Hii ilikuwa njia ya Wargla-Ghana ambayo ilikuwa muhimu kuliko ile ya Wargla-Tadmekka kwa sababu mji wa Ghana ulikuwa ghala kubwa la dhahabu iliyotoka katika maeneo yenye dhahabu ya Bambuk na Bure. Njia ya Wargla-Ghana ilipita katika mji wa Sijilmasa ikiwa njia halisi ya kwenda Sudan. Watawala wa Sijilmasa (ambao walikuwa Wamiknasa na hivyo wenye udugu na Wazanata) walitangaza imani za madhehebu ya Kisufri zilizohusiana kwa karibu sana na zile za Kiubadi na walikuwa wakistahiwa na Maimamu wa Kirustumi wa Tahert. Baada ya kutoka Sijilmasa, njia ya Wargla-Ghana ilielekea mji wa Tamdult katika Sus al-Aksa. Njia hii twaijua kutokana na maelezo ya al-Bakri ambaye pia anatupatia majina ya vituo viwili vilivyofuata, yaani Izil (*Kediat d'Ildjil*) na jiji la Awdaghust, soko muhimu katika sehemu ya kuaini mwa Mauritania ya leo palipo na magofu ya Tegdausti sasa. Njia kutoka Sijilmasa kwenda Ghana pia ilipitia mji wa Azuki (Azugi) katika Adrar ya Mauritania. Kulikuwepo pia njia nyingine kutoka Wargla kwenda Ghana iliyopitia Tadmekka. Njia ya moja kwa moja

kabisa kati ya Wargla na Tahert ilipitia mkoa wa Mzab, kupitia Tilghment na Laghwat, yaani kupitia kundi la kati la oasisi za Kaskazini mwa Sahara, lililoko kati ya Wadi Righ na Wargla, kwa upande mmoja, na Tuwat-Gurara, kwa upande mwingine.

Jina la Mzab hutokana na kundi la Wazanata walioanzisha vijiji katika mkoa huu. Wabanu Mzab na mkoa wenyewe vilijulikana tokea mapema mnamo karne ya tisa kwa jina 'Mus ab' kwa Kiarabu. Mwanzoni walitangaza imani ya Kimutazili, lakini baadaye (katika karne ya kumi na moja) waliingia katika imani ya Kiibadi.

Miongoni mwa miji iliyoanzishwa Sahara ya Kaskazini na Wazanata yapasa kutaja ngome ya Talghment (Tilghment au Tilrhemt ya leo) na mji wa Laghwat (Laghout), ambao tayari ulikuwa ukijulikana mnamo karne ya kumi kwa jina la al-Aghwat. Mji mwingine muhimu katika eneo hili ulikuwa *Ksar El-Golea* ambako njia kutokea Wargla kwenda Tadmekka iligawanyika. El-Golea (au kwa usahihi al-Kala = 'ngome' ni mji uliokaliwa na watu wengi sana na ambao ulikuwa na msikiti na mabaki ya makumbusho kadhaa ya kale.

Kundi la Maghribi la oasisi za Sahara ya Kaskazini huundwa na Gurara, Tuwat na Tidikelt, ambazo huunganishwa na mipaka dhahiri ya kijiografia. Miongoni mwa oasisi hizi tatu, Gurara ndiyo yenye wakazi wengi zaidi na ina maji mengi zaidi na mitende pia. Tuwat ni 'mtaa wa mitende' wenye urefu wa zaidi ya kilomita 200 kati ya Buda na Taurirt; ina wakazi wachache kuliko Gurara, lakini idadi ya mitende iliyomo hupita ile ya Gurara kidogo. Oasisi za kundi la Maghribi hutumia mfumo wa umwagiliaji wa mifereji ya chini ya ardhi inayojulikana kama *foggara*.

Historia ya Gurara, Tuwat na Tidikelt hadi karne ya kumi na nne haijulikani. Huchukuliwa kwa jumla kwamba oasisi hizi zote zilianzishwa karibuni tu; katika karne ya sita ya Enzi ya Kikristo kwa Gurara, na karne ya kumi na saba kwa baadhi ya oasisi za Tidikelt. Katika Tamentit huko Tuwat sanamu ya jwe yenye kichwa cha kondoo dume imepatikana inayofanya ifikiriwe kwamba mahali hapa palikalwa kabla ya kipindi cha Uislamu na Walibyco- Waberiberi ambao pengine walitoka mashariki mwa Libya ambako walipokea, labda huko Siwa, imani ya Ammon iliyotumia pembe za kondoo dume. Wageni hawa pia walijifunza kutoka kwa watu wa mashariki mwa Libya sanaa ya uchimbaji *foggara*.

Kuhusu kupokelewa kwa imani za Kiyahudi na Waberiberi wa Sahara, hii pengine ilianza katika karne ya pili ya enzi ya Ukristo kutokana na mtawanyiko wa Wayahudi wa Sirenaika ambao walikimbilia Mauritania na Sahara baada ya tikandamizaji ulioamriwa na Mfalme wa Kirumi, Trajan.

Makundi ya Wazanata yalipenya zaidi kuelekea Gurara na Tuwat katikati ya karne ya kumi na moja, wakiwa wamesukumwa na uvamizi wa Wabanu Hilal na pia ule wa Wamoravi katika Moroko. Baada ya tukio hilo, baadhi ya Waberiberi, Wazanata na wengineo, wakiwa Waislamu au waliofuata imani ya Kiyahudi, walikimbilia Sahara.

## Sahara ya Kati

Katikati mwa Sahara na kusini mwa El-Golea na Wargla kuna eneo la nyanda za juu lijulikanalo kama Ahaggar au Hoggar, ambalo huenea Kaskazini-mashariki hadi Tassili-n-Ajjer na Maghribi hadi Muydir. Milima mingine miwili ijulikanayo kama Air na *Adrar des Ifoghas* huendeleza nyanda za juu za Ahaggar kuelekea kusini. Eneo hili la Sahara lilikalwa, kati ya karne ya nane na karne ya kumi na mbili, na makundi mbalimbali ya Waberiberi wazawa wa tawi lijulikanalo kama Wasanhaja, ambao ndio walikuwa mababu wa Watuareg wa leo. Katika kipindi hiki hapana mji mkubwa au mashamba ya mitende yaliyokuwepo Ahaggar na Tassili-n-Ajjer.



Katika *Adrar des Ifoghas na Air*, mambo yalikuwa kinyume. Hapa kulikuwa na miji mikubwa ambayo wakazi wake walishiriki katika biashara, lakini, ukiacha kando Tadmekka katika *Adrar des Ifoghas*, hakukuwepo kabisa mitende na bustani (aghren).

Jina Tassili-n-Ajjer hutokana na Waberiberi wa Ajjer au Azger ambao walikuwa waendesha ngamia na ambao kituo chao cha utawala huenda kilikuwa katika eneo la sasa la Ghat au Janet, mwendo wa siku kumi na nane kwa miguu kutoka Ghadames na siku kumi na mbili kutoka jijini hadi Tassawa huko Fezzan. Njia hii ya mwisho yaelekea ni sawa na ile njia ya kale ya 'waendesha farasi wa Kigaramante' ambayo mnamo kikwi cha kwanza kabla ya Enzi ya Ukristo iliunganisha Fezzan na Gao ikipitia eneo la Ajjer, Ahaggar na *Adrar des Ifoghas*. Kuwepo kwa njia hii ya kale huthibitishwa kutokana na ugunduzi wa Abalessa na idadi ya sarafu za kale zilizopatikana jirani yake.

Twajua kidogo sana kuhusu historia ya Ahaggar katika kipindi kinachojadiliwa. Kulingana na mapokeo ya mahali hapo, kuliishi katika Ahaggar, kabla ya nyakati za Uislamu, watu walioitwa Waisebeten, waabudu sanamu na wasema lugha ya Kituareg, ambao walitumia mfumo wa kilimo wa kabla ya ule wa Watuareg (mitini, mizabibu na mashamba ya mitende) na walikuwa na mifereji ya unwagiliaji maji. Mbari moja ya sasa ya Wadag-Ghali hudai ni wazawa wa Waisebeten hawa na kwamba ndio hasa wenye ardhi. Baadaye Ahaggar ilivamiwa na Walamta na kisha na Wahawwara ambao walipatia hilo jina (kwa kubadilisha fonimu *ww* ya Kiberiberi kuwa *gg* kama ilivyothibitishwa na Ibn Khaldun). Kulingana na mwandishi huyo, kundi la Wahawwara, lilivuka mchanga na kukaa kandokando ya Walamta, 'wavaa-buibui', walioisli karibu na mji wa Kaw-Kaw (Gao) katika "Nchi ya Weusi". Yaelekea kwamba kufika kwa Wahawwara wa Ahaggar katika nchi wanamoishi sasa, lazima kunahusiana na kushindwa kwa Wahawwara wa Awras na mwana wa mfalme wa Kifatimi al-Muizz mnamo mwaka 953 na kufukuzwa kwa waasi hawa ambao baadhi yao walikimbia 'hadi Nchi ya Weusi', ambapo hasa ni katika uelekeo wa Ahaggar ya leo.

Sehemu au maeneo kadhaa katika Air yalikuwa yamekwisha julikana katika karne ya tisa. Al-Yakubi anataja falme tatu miongoni mwa falme zilizokuwa chini ya dola ya Kisudan ya Kaw-kaw, ambazo kwa hali yoyote ile, zilikuwa Air. Hizi zilikuwa falme za Maranda, al-Hazban (katika mswada al-Harbar) na Tikarkarin (katika mswada Tidkarir). Jina la ufalme wa kwanza limetokana na mji mdogo na kisima cha maji (Marendet ya leo) ulioko kusini mwa Agades. Mabaki ya kijiji cha kale bado yanaonekana pale, pamoja na mabaki ya kiwanda cha kusubia shaba. Watu wajulikanao kama Wamaranda waliishi Kaskazini mwa Kaw-Kaw na "nchi" yao (au hasa makao yao makuu) yalikuwa kituo katika njia kuu ya Sahara kutoka Gao hadi oasisi za Misri katika nusu ya pili ya karne ya kumi. Sehemu hiyo ilikuwa kituo katika njia itokayo Ghana hadi Ajadabiya katika Sirenaika. Ilikuwa umbali wa mwendo wa mwezi mmoja kwa miguu kutoka mji wa Kaw-Kaw, ikiwa ni kituo kinachofuata (baada ya Gao) katika njia hii, ambayo baadaye ilipita katika mji wa Zawila huko Fezzan. Maranda ni jiji lililokalifiwa na watu wengi sana, kimbilio na mahali pa mapumziko kwa wote waliokuja na kwenda katika safari na misafara yao. Al-Hazban (al-Hazbin) ni sawa na Azben au Azbin, jina la awali la Air, lililotumiwa na watu weusi au machotara wa eneo hilo. Ufalme wa tatu huhjulikana kwa jina la Tikarkarin; neno hili katika Kiberiberi lina maana ya wingi wa Tararkart, katika jinsi ya kike; jina lijitokezalo katika ramani zetu kama *Tacarcart*. Ufalme huu uko katikati ya Tahua na Agades, katika eneo ambalo lina uthibitisho wa ustaarabu wa kale. Katika karne ya kumi na nne, Ibn Batuta alizungunzia Sultani wa Kiberiberi mwenye jina al-Takarkari ambaye alikuwa na mgogoro na Sultani wa Takedda (Azelik ya leo katika sehemu ya kusini-Maghribi ya Air).

Mlima wa *Adrar des Ifoghas* ulijulikana kwa wanajiografia wa Kiarabu wa awali hasa kutokana

na maelezo ya jiji la Tadmekka (ambalo leo hii ni magofu ya Es-Suk, kilomita 45 Kaskazini mwa kijiji cha Kidal) lililokuwa kituo chake cha utawala. Tadmekka pia ilikuwa kituo muhimu katika njia ya msafara kutoka Gao hadi Ghadames na Tripoli. Kulikuwa na urnbali wa kutembea siku arobaini kati ya Tadmakka na Ghadames, kwa kupitia eneo la Saghmara na majangwa manne.

Wasaghmara walikuwa Waberiberi walioishi katika eneo la Kaskazini au hasa Kaskazini-mashariki mwa Tadmekka. Hawa walikalia pia eneo lililotawaliwa na Watadmekka na lilikuwa kusini mwa jiji hili linalotazamana na Gao. Kundi hili linaweza kuhusishwa na Watuareg wa Isekkamaren (umoja Asekkamar), ambao baadhi yao bado ni wanomadi katika *Adrar des Ifoghas* hadi hii leo.

Tadmekka ilikuwapo katika karne ya tisa na ilikuwa kituo muhimu cha biashara, ikitembelewa zaidi na wafanyabiashara Waberiberi wa Kiibadi kutoka Wargla, Jarid na Jabal Nafusa, ambao walifika hapo mara kwa mara kupata dhahabu iliyoletwa kwa wingi kutoka migodi ya dhahabu karibu na Ghana. Ilikuwa pia ghala kwa bidhaa kutoka Maghrib, hasa nguo, zilizoletwa kupitia njia ya Wargla. Tadmekka ilijengwa vizuri kuliko Ghana na Gao, lakini haikuwa na mazao. Katika karne ya kumi, Tadmekka iliunda dola iliyotawaliwa na Wafalme kutoka Wabanu Tadmak (tawi la Wasanhaja). Hata hivyo wakazi wa mji huo hawakuwa Waberiberi wa tawi la Wasanhaja bali la Wazanata. Japokuwa Wazanata, wakazi wa mji mkuu, walikuwa Waislamu wa Kiibadi tokea karne ya tisa na kuendelea, Wasanhaja wa Tadmakka hawakuwa Waislamu hadi mwaka 1109.

Mwendo wa siku sita kwa miguu toka Tadmekka kulikuwa na eneo liljulikana kama Tutak au Tawtak lenye machimbo ya chumvi ya chini ya ardhi. Jimbo la Tuak lilipata jina lake kutokana na tawi la Wasanhaja. Haiwezekani kuthibitisha kwa hakika eneo hili lilipo, ingawa jina lake na pia la mbari ya Tutak, linawiana na lile la Taitok, kundi moja la wastahiki wa Kituareg linaloishi Ahnet leo hii, eneo lililoko Kaskazini mwa *Adrar des Ifoghas* na Kaskazini Maghribi mwa Tamnaraset.

## Sahara Maghribi

Hali ya kimbari na ya kisiasa katika sehemu hii ya Sahara iliyocnea Maghribi kutoka *Adrar des Iforas* na kusini kutoka Moroko, inajulikana vizuri zaidi, kutokana na vyanzo vya Kiarabu. Taarifa za awali kabisa zilihusu msafara ulioongozwa na jenerali 'Ukba ibri Nafi huko kusini mwa Moroko. Mwaka 682, jenerali huyo aliingia katika jimbo la as al-Aksa na alidiriki kuvuka mipaka yake ya kusini na kuingia Sahara ambako aliwashambulia Warnassufu na kisha baada ya kuwateka wengi wao, akarejea.

Madhumuni ya msafara huu wa kijeshi hayakuwa utamalaki wa kudumu wa Waarabu na usilimishaji wa kusini mwa Moroko na Sahara Maghribi, ingawa mwanahistoria wa Kiarabu wa enzi za kati huzungumzia usilimishaji wa lazima uliofanywa na amiri jeshi huyu, na Waberiberi wa kundi la Wajazula wa kusini mwa Moroko. Madhumuni yake yalikuwa ni kwenda kuyadadiji maeneo yenye migodi ya dhahabu ya Maghribi mwa Sudan; madhumuni hayo yakiwa sawa na yale ya msafara uliofanywa na huyu huyu amiri jeshi Ukba ibn Nafi mnamo 666-67 kuchunguza njia ya biashara toka pwani ya Tripolitania kupitia Fezzan na Kawar hadi Ziwa Chad.

Kati ya miaka ya 705-6 na 708-9, Musa ibn Nusayr alipenya hadi eneo la as-Sus al-Aksa, ambalo wakazi wake walipokea imani ya Kiislamu na kumkubali Marwan, mwana wa Musa ibn Nusayr, kuwa gavana wao.

Lakini ni hadi msafara ulioongozwa na amiri jeshi wa Kiarabu Habib b. Abi Ubayda (kati ya 734 na 740), ndipo jimbo hili hatimaye lilipotamalakiwa na kusilimishwa. Msafara huu wa kijeshi ulielekezwa dhidi ya kusini mwa Moroko na pia dhidi ya Maghribi mwa Sudan. Habib ibn Abi

Ubayda alirudi mshindi akiwa ameleta mateka wengi na kiasi kikubwa cha dhahabu.

Mwanawe Ismail aliendeleza misafara ya kijeshi dhidi ya Waberiberi wahamaji wa Sahara Maghribi. Kiongozi wake mmoja wa kijeshi alidai: 'Nilipanga misafara ishirini ya kijeshi dhidi ya nchi ya Anbiya, kuanzia as-Sus al-Aksa. Niliona Nili (yaani mto Senegal); kati ya mto huo na bahari ya chumvi (yaani Bahari ya Atlantiki) kulisimama mlima wa mchanga ambao chini yake ndipo mto huo ulipoanzia'.

Maelezo haya ndiyo yanayotaja kwa mara ya kwanza jina Anbiya (ambayo matamshi yake si ya hakika) kuita nchi zilizoko kati ya as-Sus al-Aksa na mto Senegal. Mwishoni mwa karne ya tisa, al-Yakubi anazungumzia Waanbiya kama Waberiberi wa kundi la Wasanhaja, ambao nchi yao ilienea toka Sijilmasa hadi jiji la Ufalme wa Waberiberi wa Ghist (unaorejelewa na waandishi wengine kama Awdaghust) lililoko pambazoni kusini mashariki mwa nchi tunazozijadili hapa. Jina hili la ajabu laelegea ni la shirikisho la kale kabisa la Waberiberi wa Sahara Maghribi lililojumuisa Wamassufa, Walamtuna na Wajuddala.

Hata hivyo, yaelekea kwamba misafara ya kijeshi ya Waarabu ilichukua muda mfupi tu na kwamba punde kidogo tu makubaliano yalifikiwa kati ya Waislamu wa Afrika Kaskazini na machifu wa shirikisho la Anbiya ambayo yalileta amani katika nchi za Maghribi mwa Sahara. Hii iliibua hali nzuri ya biashara kwa kupitia Sahara na kwa utangazaji wa dini ya Kiislamu, vyote vikiwa vimeletwa na Wafanyabiashara wa Afrika Kaskazini ambao wakati huo huo walikuwa wamisionari wakihubiri Imani ya Mtume. Kwa maoni yetu, maneno yafuatayo ya Ibn Khaldun hurejea hiki kipindi kifupi: 'Katika wakati wa kutamalaki Afrika Kaskazini (kwa Waarabu), wafanyabiashara wachache waliingia katika sehemu ya Maghribi ya Nchi ya Weusi ambako hawakukuta mfalme yeyote aliyekuwa na nguvu kuliko mfalme wa Ghana.'

Chifu wa kwanza wa Kisanhaja Maghribi mwa Sahara alikuwa Tihutan ibn Tiklan (au Itutan ibn Talakakin) wa Walamtuna, ambaye alitawala jangwa lote, na zaidi ya wafalme ishirini wa Sudan walilipa ushuru kwake. Nchi yake ilienea sehemu iliyokuwa na ukubwa wa mwendo wa 'miezi mitatu urefu na miezi mitatu upana.' Alifariki mnamo mwaka 837 akiwa na umri wa miaka themanini. Mjuku wake al-Athir ibn Batin alimrithi na kutawala hadi mwaka 900. Mfalme wa mwisho wa dola ya Sanhaja alikuwa mwana wa al-Athir, Tamim ambaye alitawala mbari hizi hadi mwaka 918. Aliuawa na Wasanhaja maarufu ambao walipigana naye. Matokeo yake mfarakano ulizuka kati ya mbari za Kisanhaja na hawakuungana hadi miaka 120 baadaye chini ya uongozi wa kadhi Abu Abd Allah Muhammad ibn Tifat (Tifawt) ajulikanaye kwa jina la Tarsina, mmojawapo wa machifu wa Walamtuna (1035), ambaye alitawala kwa miaka mitatu tu. Shemeji yake, Yahya ibn Ibrahim, Mdujuddali, akawa chifu wa shirikisho la Wasanhaja. Huyu ndiye aliyemrudisha Abd Allah ibn Yasin, mwasasi wa harakati za Kimoravi.

Kulingana na mapokeo, mamlaka ya juu kabisa miongoni mwa Wasanhaja yalikuwa chini ya Walamtuna, ambao walikuwa wamekwishaunda ufalme mkubwa mnamo nusu ya pili ya karne ya nane.

Mfalme maarufu kabisa miongoni mwa Wafalme wa Wasanhaja aliyetawala 'Sahara yote' katika karne ya kumi, alikuwa Tinazwa ibn Wanshik ibn Bizar, aliyejulikana pia kama Baruyan ibn Wanshik ibn Izar. Huyu mwana wa mfalme ndiye yule ajulikanaye katika maandishi ya al-Bakri kwa jina la Tin Yarutan ibn Wisnu ibn Nazar, aliyetawala kati ya mwaka 961 na 974. Ibn Hawkal hutaja Mfalme Tanbarutan ibn Isfishar, anayemwita 'mwana mfalme wa Wasanhaja wote' na ambaye pengine alikuwa mtu huyo huyo.

Kusini mwa nchi ya Anbiya kuna eneo lijulikanalo kama Ghist, ufalme wa kipagani ambao mfalme wake alifanya mashambulizi katika Nchi ya Watu Weusi. Baadhi ya wakazi wa eneo hili

waliishi katika makazi ya kudumu. Haya yalikuwa ni pamoja na mji wa Kiberiberi na ufalme uliojulikana kwa waandishi wa kale wa Kiarabu kwa jina la Awdaghust; ambao ulikuwa kituo muhimu cha biashara, mwendo wa siku kumi kwa miguu kutoka mji wa Ghana. Chanzo chetu cha taarifa hii ni msafiri na mwanajiografia wa Kiarabu, Ibn Hawkal aliyepitia Awdaghust mnamo miaka ya 951-2 na ambaye anaeleza zaidi kwamba kulikuwa na umbali wa mwendo wa miezi miwili kwa miguu kati ya Awdaghust na mji wa Sijilmasa. Awdaghust ulikuwa na masoko mazuri, na wasafiri waliingia humo kwa wingi toka pande zote; wakazi wake walikuwa Waislamu. Chifu wa eneo hili alikuwa wa mbari ya Wasanhaja.

Kuanzia mwaka 961 hadi 971, dola ya Awdaghust ilitawaliwa na Tin Yarutan aliyetajwa hapo juu na ambaye alikuwa wa mbari ya Wasanhaja. Hivyo kwa muda fulani ufalme wa Awdaghust ulikuwa wa shirikisho la mbari za Wasanhaja.

Baadaye (hadi mwaka 1054) mfalme wa Kiberiberi wa Awdaghust alitambua mamlaka ya mfalme mweusi wa Ghana (kinyume na Walamtuna, Wamassifa na Wajuddala ambao hawakuitgemea Ghana). Na wakati huo Awdaghust lilikuwa jiji kubwa na lenye watu wengi na matajiri ambao walikuwa Waarabu na Waberiberi (wakiwemo Wanafusa, Walawata, Wazanata, Wanafzawa na pia mbari za Waberakajana). Katika soko la Awdaghust dhahabu ndiyo iliyotumiwa kununulia vitu. Kuna uwiano kati ya Awdaghust na Tegdaust ambayo magofu yake yako kusini-Maghribi mwa Tichitt (umbali wa kilomita 200 hivi) na Maghribi-Kaskazini- Maghribi mwa Kumbi Saleh (au Ghana ya zamani) umbali wa kilomita 400 hivi.

Wengi wa wakazi wa Sahara Maghribi katika karne hizi walikuwa Waberiberi wa tawi la Wasanhaja (Walamtuna Waassufa na Wajuddala). Walamtuna na Wajuddala waliishi kusini kabisa mwa eneo la Kiislamu, jirani na watu weusi, na wakati fulani walikuwa sehemu ya dola kuu ya Wasanhaja ya Anbiya. Kulingana na maelezo ya al-Idrisi, eneo la Tazukkaght (Sakiyyat al-Hamra ya leo) lilikuwa la Walamtuna. Nchi za Walamtuna pia zilijumuisha eneo la Nul kusini mwa Moroko kwa upande wa Kaskazini. Kusini zaidi, nchi zao zilienea hadi Izal (au Ayzal) ambayo inawiana na *Rediat d'Idjil* ya leo. Kwenye mwaka 1054-55, Walamtuna pia walikalika Adrar Tmar ya Mauritania, iliyojulikana baadaye kama Jabal Lamtuna. Hili ni eneo lililokuwa na mashamba ya mitende yaliyopandwa na watu waliolikalia eneo hili kabla ya Wabafur, kama wanavyojulikana katika mapokeo na kwa waandishi fulani wa Kireno. Jiji kuu la Jabal Lamtuna lilikuwa Azuki, ambalo lilijengwa kuzunguka ngome ya Kimoravi yenye jina hilo. Jiji hili lilikuwa kituo muhimu katika njia kutoka Sijilmasa hadi Maghribi mwa Sudan. Weusi walilijua jiji hili kwa jina la Kukadam (al-Idrisi) au Kakadam. Mji huu huwiana na Azugui ya leo, makazi madogo yenye magofu ya kale ya Kimoravi na ya kabla ya Wamoravi Kaskazini mwa Mauritania; si mbali sana na mji ya Atar.

Wamassufa waliishi jangwani katika eneo lililokatisha njia inayounganisha jiji la Sijilmasa na jiji la Ghana. Mnamo katikati ya karne ya kumi na mbili, Wamassufa walikwenda kusini hadi jiji la Asuli. Kusini-mashariki kuna Taghaza, kupatikanapo chumvi, sehemu ambayo ilichukuliwa nao. Katika eneo hili ilipita njia ya misafara kwenda Iwalaten (au Walata), kituo muhimu cha biashara katika ukingo wa Sahara Maghribi.

Kusini-Maghribi mwa nchi iliyokaliwa na Walamtuna waliishi Wajuddala, ambao pengine walikuwa wazawa wa Wagetuli wa kale. Waliishi usawa wa Kaskazini ya Senegal chini karibu na bahari, ambapo hawakutengwa na kundi lolote. Hivyo Wajuddala walikalika kusini-Maghribi mwa Mauritania ya leo na pia eneo linalozunguka al-Jabal al-Lamna (*Cap-Blanc*).

Imedhihirika kutokana na machimbo ya kiakiolojia na piamapokeo simulizi kwamba katika maeneo fulani ya Sahara Maghribi, kando kando mwa wanomadi palikuwepo pia makundi ya

wakulima ambao wazawa wao wapo hadi leo. Kulingana na vyanzo vya Kireno, hawa walikuwa wa makundi mawili tofauti. Wakulima weupe waliojulikana kama *Baffor* au *Abofur* (*Bafur* katika mapokeo ya mahali hapo) na wakulima weusi waliojulikana kama *Barbar* (Barbara, Barabir, Barbaros) ambao walikuwa na udugu na Wasoninke.

Kundi la kale kabisa kati ya makundi haya liliacha idadi kubwa ya vijiji vilivyoharibiwa, na maeneo ya kiakiolojia katika Adrar ya Mauritania. Maeneo haya ya kale huelezwa katika mapokeo kuwa yalikuwa ya watu wa ajabu waliojulikana kama *Baffor*, *Abofur* au *Bafur* ambao walikalia Adrar ya Mauritania kabla tu ya kufika kwa *Walamtuna*. Kulingana na mapokeo fulani *Wabafur* walikuwa weupe (na mwandishi wa makala haya anafikiri kuna uwezekano huo) wa mbari ya *Waberiberi* wa *Zanata*. Kulingana na mapokeo ya *Kimauritania*, wenyeji wasio *Waislamu* wa Adrar *Tmar* walikuwa wakulima na ndio waliopanda mitende ya kwanza Adrar. Twafikiria, *Wabafur* pengine ni sawa na mbari (ya *Kimoori*) ya *Wabavare* wa *Libya*, ambao walijishughulisha katika selimu ya *Maghribi* ya Afrika Kaskazini katika karne ya tatu na ya nne ya enzi ya Ukristo. Hawa ndio baadaye walihamia Mauritania ya leo na kuacha utamaduni na jina lao kwa wakazi wa Adrar *Tmar* ambayo mapema katika karne ya kumi na sita ilikuwa ikijulikana bado kama 'mlima wa *Baffor*.'

Kulingana na vyanzo vya *Kiarabu* vya karne ya kumi na mbili, weusi wajulikanao kama *Barbar* au *Barbara* (wingi kwa *Kiarabu*: *Barabir*) ndio watu wa nchi ya *Sudan* ya *Zafunu* yenye uwiano na *Diafunu* ya leo. *Walihesabika* miongoni mwa *Wajanawa*, yaani weusi, na waliishi katikati ya jangwa (pengine katika majangwa na mbuga za kuaini mashariki mwa Mauritania), na katika maeneo karibu na *Ghana* na *Tadmekka* (Kaskazini mwa *Gao*), ambayo wakazi wake walivamia nchi zao kwa lengo la kuchukua watumwa. Walikuwa na wafalme wao na walivaa ngozi za wanyama kama ilivyokuwa kawaida kwa watu ambao baadhi yao ni wanomadi. *Wabarbar* waliamini ndio *Wasudani* wastahiki kuliko wenzao na walidai kwamba watawala wa *Ghana* walitokana na mbari yao. Kwa hali hii, yaonekana kwamba *Wabarbar* ni kundi la *Wasoninke*. Je, *Waal-Barabir* hawa si sawa na watu weusi wajulikanao kama *Wal-Barbar* ambao, katika mapokeo ya mahali hapo, awali walikalia mji wa *Tichit* kusini-mashariki mwa Mauritania? Wachunguzi wengine huwanasibisha watu hawa wasiojulikana vema na wakulima wenye ngozi nyeusi wanaorejelewa kama *Wabarbaros* katika tarihi za kale za Kireno na kujitokeza katika karne ya kumi na tano na kumi na sita za Enzi ya Ukristo kwenye Adrar ya Mauritania, kando kando mwa '*Azenegues*' au *Waberiberi* wa *Zenega* (*Sanhaja*).

---

## Kutokea kwa Wafatimi

12

---

### Kuanzishwa kwa nasabatawala wa Wafatimi

Mwishoni mwa karne ya tisa sehemu kubwa ya eneo la Maghribi lililokuwa chini ya Waislamu (Maghrib na Hispania) lilikwisha kuwa nje ya utawala imara wa kisiasa wa Ukhalifa wa Kiabbasi wa Baghdad<sup>1</sup>.

Kwa upande wa dini Maghrib iligawika baina ya imani halisi ya Sunna, Kayraman ikiwa mojawapo kati ya vitovu vya falsafa ya kisharia ya Kimaliki, na imani pinzani ya madhehebu ya Kikhariji. Ingawa Waidris walikuwemo katika ukoo wa Ali na kuanzishwa kwa mamlaka yao kulitanguliwa na uenezi wa mafunzo ya Kishia, inaonekana kwamba mafunzo ya madhehebu ya Kishia, kama yalivyofafanuliwa huko sehemu za Mashariki, hayakuenezwa sana na yalipata wafuasi wachache tu katika milki yao.

Yote haya yalibadilishwa na kufika, huko Afrika Kaskazini, kwa aina ya Kishia iliyokuwa na nguvu na hamasa kubwa, yaani madhehebu ya Kiismaili, mwishoni mwa karne ya tisa. Kiini cha imani ya Kishia ni lile fundisho kwamba *uimamu* wa jamii ya Kiislamu unapasa utokane na vizazi vya Mtume Muhammad vilivyopitia kwa mwanawe mwanamke Fatma na mumewe Ali, Khalifa wa nne<sup>2</sup>. Washia waligawika katika vikundi vingi juu ya suala la nani awe imamu wa mwisho aliyebayana na *imamu* wa mwisho aliyejificha (yaani *Mahdi*). Wale wanaoamini kwamba *imamu* wa kumi na mbili, Muhammad, aliyetoweka mwaka 878, ndiye *imamu* asiyefahamika wanajulikana kwa jina la Wa-kumi-na-mbili (Ithna-ashariyya) na hivi sasa wao ndio sehemu kubwa ya Washia.

Kikundi kingine kilijitenga wakati huu, kikionyesha imani yao kwa *uimamu* wa Ismail (tarehe 760) badala ya ndugu yake Musa ambaye ndiye aliyetambuliwa na walio wengi katika madhehebu ya Shia. Kwa hivyo kwao Ismail (baadaye mwanawe Muhammad) akawa ndiye imamu wa saba na aliyejificha. Madhehebu haya yakachukua jina la Ismaili na wafuasi wake pia kujulikana kwa jina la Wa-Saba (Sabiiyya).

Historia ya madhehebu haya kidogo haieleweki. Kama aghalabu inavyokuwa miongoni mwa madhehebu pinzani, kikundi cha Waismaili kiligawika katika matawi mengi, sababu kubwa yatokana na hitilafu zao ikihusika na ile hali ya *uimamu*. Lile kundi ambalo Wafatimi walitoka lilikubali mafunzo yanayodai kuwcko kwa *imamu* bayana kwenye uongozi wa jamii ya Kiislamu. Maelezorasmii ya Wafatimi yanadai kwamba ule mfululizo wa Makhalifa wa Kifatimi ulitanguliwa na

1 Taz. Sura 10 ya kitabu hiki.

2 Tafauti nyingine za imani ling. Sura 2 ya juzuu hili

msururu wa 'Maimamu wasiofahamika' waliotokana na Muhammad ibn Ismail.

Waismaili walibuni moja kati ya kampeni za propaganda ya kisiasa na kidini iliyokuwa ya kijanja na madhubuti kabisa. Wakuu wao walianza kupeleka wahubiri (*da'i* na wingi wake *du'ai*) kueneza mafunzo yao na kutangaza kurejea kwa haraka kwa imamu asiyefahamika ambaye ndiye huyo *Mahdi* anayetarajiwa. Uismaili ulisbawishi tabaka mbali mbali za jamii ambazo zilikuwa hazikiridhika na hali ya mambo ilivyokuwa kwa kuziahidi utawala mpya utakaoleta haki za kijamii zilizoelazewa kijujuu tu pamoja na mabadiliko ambayo yatapatikana kutokana na kudhihirika kwa *Mahdi*. Katika baadhi ya majimbo walifaulu kuanzisha tawala ndogo ndogo lakini hapana pahala ambapo propaganda zao zilifaulu zaidi kama huko Afrika Kaskazini, kwanza kabisa ikiwa ni miongoni mwa Waberiberi wa Kikutama. Miongoni mwa matawi yote ya Kiismaili Wafatimi tu ndio walioweza kuanzisha na kuendeleza utawala uliobakia kwa muda wa zaidi ya karne mbili na kukaribia kulifikilia lengo la kusambaza mafundisho yao kwa watu wote.

Tawi la Kikutama la Waberiberi lilikalika jimbo la Kabyilia ndogo. Ingawa hawakutekwa na Waaghlabi, Wakutama walikuwa na chuki kubwa dhidi ya Waarabu waliowateka na waliokuwa watawala wa Ifrikiya.


Mwishoni mwa karne ya tisa Waaghlabi walijaribu kuwaleta Wakutama chini ya utawala wao kwa kukalia baadhi ya sehemu zilizokuwa zimeimarishwa kwa ngome katika sehemu za kuingilia eneo huru la Wakutama. Tishio hili lilitumiwa kwa ubingwa katika propaganda ya Kiismaili.

Kilichokuwa na unuhimu mkubwa ni zile shughuli za mhubiri Abu Abd Allah al-Shii, mwananchi wa Yemen ambaye alipelekwa miongoni mwa Wakutama karibu na mwisho wa karne ya tisa.

Halecweki kabisa ni kitu gani hasa katika madhehebu ya Kishia ya Kiismaili, kama, yalivyohubiriwa na Abu Abd Allah, kiliehowavutia Wakutama. Ni taabu kugundua sifa za kijamii zilizo wazi katika tawi la Kifatimi la madhehebu ya Kiismaili. Huko Maghrib walichukulia ile hali ya kutoridhika ya wakazi wa sehemu hiyo na kwa kiwango fulani pia ile siasa ya kutaka kueneza utawala wao kwa mavu; lakini hata hao Waberiberi kamwe hawakuyakubali mafunzo yao. Baada ya kushika madaraka huko Maghrib na baadaye Misri, Wafatimi hawakuleta mabadiliko yoyote ya kijamii. Ilikuwa katika tawi jingine la madhehebu ya Kiismaili, yaani tawi la Karmatis la Bahrayn na Arabia ya Mashariki, ndipo zile fikra za kikale za kijamii za vuguvugu hili ambazo zilisitiza haki za kijamii na usawa zilipotia mizizi. Hapakuwa na cho chote cha kuotofautisha utawala wa Kifatimi, kwa upande wa kijamii, na tawala nyingine za Kiislamu. Wale walio wengi miongoni mwa Wakutama mara moja waliraghbika kutokana na propaganda ya Abu Abd Allah na kujiunga na vuguvugu la vizazi vya Ali na Fatma ambalo kwa wakati huu liliwakilishwa na Imam Ubayd Allah.

Mapambano muhimu dhidi ya Waaghlabi yalianza mwaka 903, wakati majeshi ya Wakutama yalipotoremka toka milimani mwao na kumiminikia kwenye nyanda za Ifrikiya. Majeshi ya Waaghlabi yalishindwa kwa urahisi, na kwa muda wa miaka michache, sehemu kubwa ya Ifrikiya ilikuwa mikononi mwa Abu Abd Allah. Kuungwa kwake mkono na watu kuliongezeka zaidi kutokana na sera yake ya fedha, kwani alipiga marufuku kutoza watu kodi zisizotambulika kisharia na kuwarudishia watu wa miji iliyotamalakiwa mali waliyokuwa wamenyang'anywa na Wakutama. Baada ya kampeni ya muda mrefu Kayrawan, mji mkuu wa Ifrikiya, ulitamalakiwa na Abu Abd Allah.

Ziyadat Allah akaacha makazi yake katika Rakkada na kukimbilia Misri, na hapo kipindi cha Waaghlabi, katika historia ya Afrika Kaskazini, kikawa kimefikia mwisho. Baada ya mafanikio ya kwanza ya wafuasi wake katika Ifrikiya, *Imam* Ubayd Allah, ambaye mpaka wakati huo alikuwa akiishi Salamiyya huko Syria, aliamua kuhamia Maghrib. Lakini badala ya kumuunga mkono Abu



12.1 Magribi katika nusu ya kwanza ya karne ya tano/kumi na moja. (I.. Hb bek)



Abd Allah huko Ifrikiya alikwenda Sijilmasa, mji mkuu wa dola ya Wakhariji, Midrarid, katika Moroko kusini. Hili ni tukio la kushangaza na mpaka sasa haijawezekana kupatikana jawabu thabiti la kufafanua suala hili. Nini yalikuwa madhumuni yake ya kwenda Maghribi ya mbali, miongoni mwa maadui wakubwa, Washia, wakati kulikuweco na eneo kubwa mikononi mwa wafuasi wake? Je madhumuni yake yalikuwa kuanzisha kituo cha pili huko Sijilmasa au kutia mikononi ule mtiririko wa dhahabu kutoka Sudan? Azma yake ya mwanzo na iwe itakavyokuwa, muda mdogo baada ya kuwasili kwake aliwekwa kizuizini nyumbani kwake na baadaye akatiwa jela na Yasaibn Midrar.

Katika mwaka 909, Abu Abd Allah aliliongoza jeshi la Wakutama mpaka Sijilmasa kumtoa kifungoni bwana wake; katika shughuli hiyo na kwa msaada wa wenyeji, aliwapingua Warustumi huko Tahert. Sijilmasa ilisalimu amri bila ya mapigano na Ubayd Allah aliachiwa huru. Katika mwaka uliofuatia aliingia Rakkada kwa ushindi na luko akatangazwa kama ni 'Amiri wa Waumini' (cheo cha Kikhalifa) na 'Mahdi.' Kwa mujibu wa imani ya Kiismaili hilo lilimaanisha kumalizika kwa utawala wa mabavu na kuanza kwa enzi mpya ya furaha.

Asili ya Ubayd Allah, na kwa hivyo ya Wafatimi, bado imefunikwa na kiza. Wanahistoria wa Kiislamu wamegawika katika makundi mawili juu ya suala la uhalali wa madai yao. Maadui wa Wafatimi walikana kuzaliwa kwao kutokana na Ali na Fatma na kuwaita wanafiki na uhalali wa madai yao haukuonekana kuungwa mkono hata miongoni mwa wanahistoria maarufu wa Kisunni kama vile Ibn al Athir, Ibn Khaldun na al Makrizi. Hili ni tatizo gumu na hata utaalamu wa kisasa haukulipatia ufumbuzi wa kutosha. Lakini jambo lililokuwa muhimu kabisa ni kwamba wafuasi wao wa mwanzo waliamini kabisa kwamba walitokana na nasaba ya Ali.

Ubayd Allah al-Mahdi (909-934) alifanya maskani yake kwanza Rakkada, lakini mara baada ya hapo aianza kujenga makao makuu mapya, al-Mahdiyya, upande wa mwambao wa mashariki ambako aliamia mwaka 920. Baadaye, kufuatia upinzani alioufanya Abu Yazid, Khalifa al-Mansur (946-953) kwa mara nyingine tena alianzisha makao makuu mapya kusini mwa Kayrawan huko Sabra-Mansuriyya ambako yalimalizika mwaka 969.

Kuanzishwa kwa dola ya Kishia Afrika Kaskazini kulithibitisha kugawanyika kwa ulimwengu wa Kiislamu katika tawala tatu zilizokuwa zikipingana: Ukhalifa wa Kiabbasi wa Baghdad, Ukhalifa wa Kifatimi katika Afrika Kaskazini na falme za Kiumaya huko Hispania. Muda mfupi baadaye, katika mwaka 929, mfalme wa Kiumaya wa Kordoba, Abd al-Rahman III alipojiona kakabiliwa na makhalifa wawili - mmoja mpotofu aliyekuwa Tunisia na wa pili muumini halisi aliyekuwa mahali si mbali sana, pale Baghdad - alijitangazia ukhalifa wake mwenyewe. Baada ya hapo kwa muda fulani kulikuwa na makhalifa watatu katika Uislamu.

### *Harakati za kupigania uongozi katika Afrika Kaskazini*

Wakati kupinduliwa kwa ukoo wa Waaghlabi na kukaliwa kwa Ifrikiya hasa ni mambo yaliyotendeka kwa muda mfupi, utamalaki zaidi wa Wafatimi katika sehemu za Maghrib ulionekana mgumu zaidi na wenye kuchukua muda mwingi.

Mafundisho mapya ya Ushia wa Kiismaili bila shaka yalileta matatizo kwenye jimbo lililokwishagawanyika kati ya madhehebu ya Sunni ya Kimaliki na madhehebu ya Kikhariji. Vikundi hivi vyote vilikubali utawala wa Wafatimi kwa shingo upande na mara nyingi vilidhihirisha upinzani wao. Nguzo kubwa ya upinzani wa Kisunni ilikuwa Kayrawan, kituo maarufu cha imani halisi ya Kimaliki ambacho athari yake kubwa kwa wakazi wa mjini na vijijini iliendelea bila ya kupungua. Ingawa vikundi hivi vya Kisunni havikupata kufanya uasi kwa bayana, lakini mgomo wao baridi na



12.2 *Mandhari kutoka angani ya rasi ya Mahdiyya (katika miaka ya 1970). (Picha imetolewa na Ofisi ya Ardhi na Ramani, Tunis)*

uwezekano wao kujiunga na Wakhariji ambao walikuwa na siasa kali, ni mambo yaliyozidi kuongeza matatizo katika nasaba tawala hii.

Tangu mwanzo, Wafatimi, walichukulia Afrika Kaskazini kama pahala pa kurukia kusonga mbele na utamalaki upande wa Mashariki ili kuwaondoa Waabbasi na kutekeleza ndoto zao za kueneza mafunzo yao kwa watu wote. Mipango hii mikubwa iliwalazimisha kuweka vikosi vikali na vya gharama kubwa baharini na nchi kavu.

Kuanzishwa kwa kituo cha kijeshi kwanza kulionyesha kuwa ni kitendo cha wasiwasi kwa vile waliounga mkono nasabatawala huu walikuwa Wakutama tu na baadhi ya matawi mengine ya Wasanhaja. Vikundi hivi vya mbari vilikuwa na mtindo wa kuasi. Ubayd Allah alipowasababisha Abu Abd Alla na ndugu yake wauwawe kwa sababu zisizoeleweka kabisa, Wakutama walifanya uasi na kumtangaza *Mahdi* mpya ambaye alikuwa mtoto mdogo; uasi huo ulikomeshwa mara moja na kulikuwa na umwagaji damu mwingi. Ingawa Wakutama walisaidia nasabatawala hii katika kuteka Maghrib na Misri na kutoa mchango ambao umuhimu wake haifai kuudunisha, kuna mifano mingi mingine ya uasi wao, uchache wao wa utifu na vurumai. Kwa hivyo muanzilishi wa nasaba tawala hii alipaswa kuangaza kwingine katika jnhudi zake za kutafuta askari wa kuaminika kwa ajili ya jeshi lake. Hao aliwapata miongoni mwa mataifa mbali mbali ya Kislavoni kutoka ghuba ya Baltiki: Wasakaliba (Saklabi katika umoja), kama walivyoitwa na Waarabu, mara moja wakawa ndiyo nguzo ya pili, na imara zaidi, ya jeshi la Kifatimi na hata ya mfumo wao wa utawala. Watu hawa wenye asili ya Uslavoni wa kusini, walikuja Ifrikiya kwa kupitia njia mbali mbali ama wakiwa watumwa walioagiziwa na kuuzwa na Wavenisi au wakiwa mateka kutokana na uvamizi wa Waarabu kwenye sehemu za mwambao wa Bahari ya Adriatiki. Katika dola ya Kifatimi walitekeleza shughuli kama zile za askari watumwa wa Kituruki katika sehemu za mashariki zaidi za ulimwengu wa Kiislamu, na walikuwa siyo tu kikundi bora cha kijeshi lakini pia walikuwa waendeshaji wa shughuli za utawala, magavana na marafiki wa mfalme; na walikuwa maarufu kwa uhodari wao wa kijeshi na utifu wao. Baadhi yao walishika nyadhifa za juu kabisa kama Jawhar, ambaye siku za baadaye ndiye aliyeiteka Misri na kuanzisha mji wa Kairo, msikiti wa al-Azhar na chuo kikuu.

Kwa upande mwingine, Waafrika weusi hawakutekeleza shughuli kama zile walizozitekeleza baadaye wakati wa awamu ya Wamisri. Lakini walifanya kazi za uaskari katika jeshi na walijulikana kwa jina la Wazawili kufuatana na jina la soko kuu la watumwa lililokuwa Fezzan, jambo linaloonyesha kwamba jimbo la Chad ndiyo nchi yao ya asili.

Ingawa Wafatimi wanachukuliwa kwamba ndio nasabatawala ya kwanza kuanzisha umoja wa kisiasa wa Afrika Kaskazini nzima (Ifrikiya na Maghrib), uzingatifu wa makini wa suala hili unadhihirisha udhaifu wa mamlaka yao katika sehemu ya Maghribi ya Ifrikiya hasa. Majimbo mengi au miji iliyodhibitiwa na majeshi ya Kifatimi ilitekwa tena na tena na wenyeji wa sehemu hiyo, machifu au maamiri siku zote walichukua nafasi ya kwanza kujikomboa kutoka utawala wa kigeni.

Baadhi ya majimbo katika Afrika Kaskazini hayakuwahi kuwa chini ya mamlaka ya Wafatimi. Baada ya Tahert kutekwa *Imamu* wa mwisho Wakirustumi alikimbia pamoja na watu wake na kuelekea Wargla ambapo Waibadi walibaki huru na hata kutawanyika hadi kufikia Mzab. Vile vile Jabal Nafusa, makao makuu ya kale ya Waibadi, hayakupata kutekwa.

Katika karne ya kumi, sehemu za kando kando ya Kaskazini ya Sahara, zilibakia mikononi mwa Wazanata, ambao walidhibiti vituo vya misafara ya biashara iliyokuwa ikiendea kwenye jimbo la Ziwa Chad na Gao. Makhalifa wa Kifatimi hawakuweza kuteka sehemu ile ya Maghrib katika utawala wao; ilikuwa katika kituo kilichokuwa sehemu ya mwisho ya Maghribi, yaani Sijilmasa, ndipo walipojaribu kuigema ile dhahabu iliyomiminika kutoka Sudan ambayo ilihitajika sana kwa ajili ya mipango yao mikubwa ya utamalaki. Kuweza kudhibiti njia ya upande wa Maghribi

iliyokuwa ikipitia dhahabu, na wala siyo kutaka kuitawala Maghrib yote, yaelekea ndiyo yaliyokuwa madhumuni makubwa ya sera yao ya Afrika Kaskazini.

Juhudi za Wafatimi za kutaka kuitekeleza sera hiyo zilivizwa mfululizo na wapinzani wenyeji na pia maadui kutoka nje. Uhasarna wa kijadi kutokana na tofauti zilizokuweko katika mwenendo wa kimaisha, maslahi ya kibiasara, na imani za kidini zilitumbukizwa katika mapigano makubwa yaliyotokea katika karne ya kumi baina ya Waumaya wa Hispania na Wafatimi wa Ifrikiya. Dola mbili hizi ziliingia katika mapigano ya kugombea utawala kwa kuwatumia wafuasi wao wa Kiberiberi: kwa jumla (wakati mwingine mtindo huu haukufuata) Wazanata na hasa Wamaghrawa, walisimamia maslahi ya Khalifa wa Kordoba; kikundi cha Wasanhaja, hasa Wabanu Ziri kilisimama imara upande wa Wafatimi. Maadamu msingi wa mamlaka ya Wafatimi ulibaki Ifrikiya (mpaka katika miaka ya sabini ya karne ya kumi), muungano wa Wasanhaja na Wafatimi ulichukua uongozi. Katika kipindi hicho majeshi yao yalifika sehemu ya Maghribi ya Maghrib si chini ya mara mbili, lakini hawakuweza kuanzisha utawala wa kudumu katika mikoa hii ya mbali. Na wakati Wafatimi walipokuwa wakikusanya majeshi yao kwa ajili ya kuivamia Misri, sehemu ya Maghribi ya Maghrib ilitoleza na kutumbukia katika upande wa Waumaya na kutoweka moja kwa moja mikononi mwa Wafatimi na vibaraka wao wa Kiziri.

Nyuma ya mapambano ya Wafatimi - Waumaya na Wasanhaja-Wazanata ilijitokeza tangu mwanzo taswira ya ile dhahabu ya Sudan na uwezo wa kudhibiti vituo vya misafara. Wataalamu ndio kwanza wanaanza kuolewa maana ya jambo hilo kuhusu historia ya Afrika Kaskazini na Magharibi, hasa katika kuitafsiri historia ya Wafatimi.

Kule tutoridhika kwa sehemu kubwa ya wananchi na madhala ya kidini na kiuchumi waliyofanyiwa na Wafatimi ingawa kuliendelea mfululizo, lakini hakukufikia kiwango cha hatari mpaka miaka ya mwisho ya utawala wa al-Kaim. Halafu katika mwaka 943 ulizuka ghafla uasi mkubwa unaoweza kuonekana kama ni mapinduzi halisi ambao ulikaribia kuiangamiza dola yote ya Kifatimi. Kiongozi wake alikuwa Abu Yazid Makhlad ibn Kaydad ambaye alijulikana kwa jina la Abu I-Himar (yaani aliyepanda punda) ambaye alizaliwa ama Tadmekka au Gao (Kaw-Kaw) huko Sudan, akiwa mtoto wa mfanyabiashara wa Kizanati kutoka Bilad al Jarid pamoja na msichana mweusi mtumwa wake. Abu Yazid alijitokeza sana kama ni mtaalamu na pia mwalimu wa iikadi ya Kiibadi na mara alikuwa miongoni mwa viongozi wa mstari wa mbele wa tawi la Nukkari ambalo lilikuwa ndilo lenye siasa kali kabisa miongoni mwa Waibadi. Ubayd Allah al-Mahdi alipoanzisha utawala wa Kishia, Abu Yazid alianza kutangaza jihadi dhidi ya Wafatimi miongoni mwa Waberiberi waliokuwa katika Milima ya Awras na wakulima waliokuwa katika nyanda za chini. Aliungwa mkono kidogo na Waumaya wa Hispania na alijiingiza katika muungano wa kuyumbayumba pamoja na mabwanyenye wa Kimaliki wenye imani hafifu waliokuwa huko Kayrawan. Miezi sita baada ya kuanza uasi wa dhahiri, jeshi lake lilizipondaponda nyanda za Ifrikiya, likaitoka Kayrawan (katika mwaka 944) na kuyashinda majeshi ya Wafatimi katika mapigano mengi makali. Baada ya hapo, kwa muda wa miezi kumi, Abu Yazid alizunguka al-Mahdiyya, makao makuu ya mwisho ya utawala wa Wafatimi ambayo yaliindwa na Khalifa al-Kaim. Utawala wa Kishia katika Afrika Kaskazini ulikuwa karibu na kuporomoka.

Halafu tena ukaja mpomoko: vikundi vya askari wa kienyeji vya Abu Yazid vilianza kutawanyika na kurejea nyumbani na hata kifo cha al-Kaim katika mwaka 946 hakikuweza kupunguza hali ya uasi ambayo iliendelea kuwa mbaya.

Khalifa mpya, al-Mansur, alichukua hatua madhubuti kukomesha uasi na katika mapigano yaliyoendelea kwa muda wa miezi sita alifishinda kabisa jeshi la Kikharji. Abu Yazid aliyaeleza mapigano kwenye Milima ya Hodna lakini katika mwaka 947 alifariki kutokana na mashambulio

makali aliyoyapata kwenye mojawapo ya mapigano na majeshi ya Wafatimi.

Uasi wa Abu Yazid ulikuwa ndio uasi mkubwa kabisa uliopata kufanywa dhidi ya Wafatimi na ulikaribia kuipindua utawala wao. Ushindi wa al Mansur uliashiria mwanzo wa kupungua kidogo kidogo kwa bahati ya Wakhariji huko Afrika Kaskazini. Baada ya uvamizi wa Banu Hilal katika karne ya kumi na moja, hali hiyo iliendelea kwa kasi; Waibadi waliokuwa wakali kabisa walirudi nyuma na kuelemea mikoa ya mbali wakati wengi wao kidogo kidogo walianza kugetuka na kufuata madhehebu halisi ya Kisunni.

### *Sera ya Kibeberu: Sisilia Mediterania, Misri*

Wafatimi walirithi kutoka kwa wale waliowatangulia, yaani Waaghlabi, raghba juu ya kisiwa cha Sisilia, lakini mwanzo wao huko haukuwa wakutia moyo, kwani magavana wawili mfululizo walifukuzwa na wenyeji. Sisilia ilirejea kwenye utawala wa Kifatimi katika mwaka 916, lakini katika kipindi cha miaka thelathini iliyofuata, kisiwa hiki kilikuwa pahala pa machafuko yaliyokuwa karibu kupindukia katika vita baina ya wenyewe kwa wenyewe. Ilikuwa mpaka Khalifa alipompeleka al-Hassan ibn Ali al-Kalbi (kf. 965) kuwa gavana katika mwaka 948 ndipo mambo yalipoanza kuwa mazuri na hali ya utulivu kurejca tena. Chini ya al-Hassan na waliochukua nafasi yake baadaye, yaani nasabatawala ya Kalbi, Sisilia ya Kiislamu ilikuwa jimbo lenye neema na wakati huo huo likiendelea kujipatia uhuru zaidi na zaidi.

Waislamu huko Sisilia walipunguza kidogo ule mzigo mzito wa kodi ya Kibizenti na walistawisha kilimo huko Sisilia kwa kuanzisha mbinu mpya na mazao mapya. Ilikuwa katika kipindi hiki ndipo ulimaji wa matunda ya sitrasi, miwa, nazi na forosadi ulipoanza. Kuhusu pamba, kilimo chake kiliendelea kwa muda mrefu na hakikutoweka mpaka karne ya kumi na nne.

Muhimu pia ilikuwa ile biashara ya bidhaa muhimu kati ya Sisilia na Ifrikiya ambayo ilipeleka mafuta kwa ajili ya kubadilishana na nafaka pamoja na mbao za Sisilia; mbao ambazo uadimu wake katika nchi nyingine za Kiislamu ulikuwa mkubwa sana, ziliwawezesha Waaghlabi na baadae Wafatimi kuunda jeshi imara la wanamaji na kujitokeza kama ni dola zinazoongoza katika Mediterania ya kati na Siciiy, na kuwa ndio chimbuko kubwa la mabaharia wakomavu waliohitajika kuviendesha vikosi vya manowari vya Wafatimi (na baadae vya Waziri).

Udhibiti wa Sisilia uliwapa Wafatimi uongozi katika mikakati ya kivitta katika eneo la Mediterania, na Palermo ilikuwa kituo muhimu cha jeshi la wanamaji. Karibu kila mwaka kikosi cha manowari cha Wafatimi kilizishambulia schemu za pwani za bahari ya Adriatiki, mwambao wa Tyrrhenia na kusini mwa Italia (hasa Taranto na Otranto); pia kilifanya fujo katika mwambao wa kusini wa Ufaransa kikaiteka Genoa na kusambaa na mwambao wa Kalabria huku kikijinyakulia watumwa na ngawira nyingine.

Uongozi wa Wafatimi katika bahari ya Mediterania ulikuwa mkubwa kiasi kwamba, karne fulani baadaye, Ibn Khaldun alieleza huku akikumbuka ya kale kwamba 'Waukristo hawakuwa na uwezo hata wa kukifanya kibao kielee baharini.'

Falsafa ya ubeberu ilikuwa sehemu ya iukadi ya Kiismaili ambayo Wafatimi walikuwa ndio viongozi wake wa mstari wa mbele; katika matawi yote ya Kiismaili ya Kishia wao tu ndio waliokaribia kulifikilia lile lengo la mafunzo yao la kuunganisha madhehebu yote. Waliuona ufalme wao wa Afrika Kaskazini kama ni kipindi cha matayarisho kwenye safari yenye lengo la kuunda dola ya Kiismaili ya watu wote. Utawala wa ile sehemu ambayo ilikuwa ndilo shina la Uislamu tu, yaani lile jimbo kuanzia Misri mpaka Iran pamoja na nchi zote mbili hizi, ndiyo ungeluweza kuufanya ule mpango wa kueneza utawala wa Kiismaili kwa watu wote ukaribie kufaulu, siyo

utawala wa nchani mwa Ifrikiya na Maghrib. Juu ya hivyo makhalifa waliielewa vya kutosha hali ilivyokuwa, kuweza kutambua kwamba, kwa wakati huo, jimbo hilo lilipaswa liwe ndicho kituo chao cha kiuchumi na kivita. Ama kwa hakika ni ile mali asilia ya Afrika Kaskazini ya watu na vifaa, iliyowezesha nasabatawala hiyo kufunga safari ya ushindi kuelekea mashariki.

Mara tu baada ya kuanzisha utawala wake Ifrikiya, Ubayd Allah al-Mahdi alifikiria, kidoqo kwa papara, kwamba wakati wa kuiteka Misri ulikuwa umewadia. Lakini misafara mitatu iliyofanywa katika kipindi cha robo ya kwanza ya karne ya kumi haikufaulu. Kushindwa huku kwa mara kwa mara kulisababishwa na nasabatawala kuwa na uchehecfu wa vifaa katika siku za mwanzo. Ilichukuwa takriban nusu karne kabla ya hali ya kiuchumi, kijeshi na kisiasa ya dola ya Kifatimi kuweza kufikilia kiwango cha kuyafanya majaribio mapya ya kuiteka Misri yafaulu. Na kwa wakati huu, Ifrikiya pamoja na zile nchi zilizokuwa katika himaya yake (Sisilia, sehemu ya Algeria na Libya) ilipitia kipindi cha fanaka ambacho kilikuwa hakijawahi kutokea kabla na ambacho kilisababishwa kwa kiasi fulani na Ifrikiya kuwa miongoni mwa bandari kuu za biashara katika Mediterania; na kwa upande mwingine kwa sababu ya kudhibiti kwake uagizaji wa dhahabu kutoka Sudan. Na la mwisho, lakini pia muhimu, ni kwamba Wafatimi waliweza kuanzisha utawala madhubuti uliodhibiti mambo yote na uliohakikisha kuendelezwa bila ya vikwazo kwa huduma zilizohitajika kwa ajili ya majeshi yao.

Kufaulu huku kulimwzesha Khalifa wa nne, al-Muizz, kutayarisha na kukamilisha uvamizi wa mwisho katika Misri. Uvamizi huu ambao ulitayarishwa kwa hadhari kubwa na kusaidiwa na propaganda kamambe ya kisiasa ulikamilishwa bila taabu kubwa na Jawhar ambaye aliingia al-Fustat mwezi Julai, 969. Muda mfupi baada ya kutekwa kwa al-Fustat Jawhar alianza kujenga mji mpya, Kairo, ambao kwa Kiarabu huitwa *al-Kahira*, na mwaka wa pili aliweka msingi wa msikiti wa al-Azhar. Miaka minne baada ya kutamalaki, katika mwaka 973, al-Muizz aliondoka Ifrikiya na kuhamia Kairo; na hivyo kuifanya Misri kuwa makao makuu ya utawala ambao ulinusuraika na kuendelea kwa muda wa karne tano<sup>3</sup>. Kuhamia huku kwa makao makuu ya Wafatimi kuelekea upande wa Mashariki kulisababisha matokco mengi na makubwa katika historia ya Afrika Kaskazini.

### *Kurejea kwa utawala wa Waberiberi: Waziri*

Katika mapigano makubwa dhidi ya uasi wa Abu Yazid, Watakata, ambao walikuwa tawi la Wasanhaja, wakiongozwa na Ziri ibn Manad, walithibitisha utiifu wao kwa Wafatimi. Kuonyesha kukitambua kitendo hiki, Khalifa alimpa Ziri, baada ya kushindwa kwa Abu Yazid, uongozi juu ya Wasanhaja wote pamoja na ardhi yao. Katika kipindi cha Wafatimi kilichobakia huko Maghrib, Ziri na mwanae Bulukkin waliongoza mapigano mengi yaliyofaulu dhidi ya Wazanata na Wamaghrawa katika Maghrib ya Kati na ya upande wa Maghribi.

Kwa hivyo halikuwa jambo la kushangaza kuona kwamba Khalifa huyo, kabla ya kuhamia Misri katika mwaka 972, alimchagua Bulukkin ibn Ziri kuwa ni mwakilishi wake katika sehemu yote ya Maghribi ya utawala wake. Toleo hili lilianzisha awamu mpya katika historia ya Afrika Kaskazini. Hadi majilio ya Waziri, nasabatawala zote kubwa, yaani Waidrisi, Warustumi, Waaghlabi na Wafatimi wote walikuwa wa asili ya Mashariki. Waziri walikuwa watawala wa kwanza wenye asili ya Kiberiberi: zaidi ya haya wao walianzisha kipindi katika historia ya Maghrib ambacho kwacho mamlaka ya kisiasa katika jimbo hilo yalikuwa mikononi mwa nasabatawala za

3 Kuhusu historia ya Wafatimi katika Misri ling. Sura 9 ya Juzuu hili na Sura 15 ya Juzuu la IV.

Kiberiberi peke yao (yaani Wamoravi, Wamoha, Wazayani, Wamarini na Wahafsi).

Chini ya Waziri watatu wa mwanzo, yaani Bulukkin (972-84), al-Mansur (984-996) na Badis (996-1016) mahusiano yao na Wafatimi kwa jumla yalikuwa ya kuridhisha. Malipo ya Kairo yalifanywa kideshuri na maamiri mara chache na walipeleka hidaya za thamani kwa Makhaliifa ambao juu ya hayo yote waliwafanya wawakilishi wao waandamane na maamiri hao ili kuwadhibiti. Wakati huo huo Waziri walijaribu kujipatia uhuru wa kweli bila ya kuutupilia mbali utawala wa kisharia wa Wafatimi. Inaonyesha kwamba Wafatimi walipoendelea kushughulikia sera zao za mashariki walianza kidogo kidogo kutokwa na hamu juu ya sehemu za Maghribi za utawala wao; ni vgumu kuamua kama jambo hili lilisababishwa na kuanguka kwa uchumi wa Ifrikiya, au kushindwa kuziingilia sehemu hizi kivita au lilisababishwa na mchanganyiko wa yote mawili.

Waziri wawili wa kwanza, yaani Bulukkin na al-Mansur, waliendelea na hujuma kali dhidi ya Wazanata na wahami wao wa Kiumaya huko Maghribi, lakini bila ya kupatikana athari ya kudumu. Al-Mansur, akitambua kwamba kuikalia kabisa Maghribi ya Maghrib pamoja na wakazi wake wenye fujo lilikuwa ni jambo asilokuwa na nguvu nalo, aliyasitisha mashambulizi na badala yake alijishughulisha zaidi na kuliimarisha jimbo la kati, yaani Ifrikiya.

Utawala wa Badis ulishuhudia mabadiliko makubwa ambayo yaliacha athari yake katika ramani ya siasa ya Maghrib. Badiliko la kwanza lilikuwa yale mashambulizi ya Wazanata (hasa Wamaghrawa) ambao waliivamia Maghrib ya kati katika mwaka 998-9 na wakafika mpaka Tripoli. Wakati huo huo, vikundi vya Kizanata vilivyokuwa vikiishi katika eneo la Waziri vilifanya uasi; manusura yalipatikana kutokana na ujasiri wa kivita wa Hammad ibn Bulukkin, mjomba wa Badis ambaye alituliza Maghrib ya kati na kuwatoa Wazanata mpaka kufikia Moroko. Badis alilazimika kumpa mjomba wake sehemu kubwa katika Maghrib ya kati ambako Hammad katika mwaka 1007-8 alianzisha makao makuu yake katika ngome ya Kala Banu Hammad, ambayo ni miongoni mwa majengo ya kuvutia kabisa katika Afrika Kaskazini. Katika muda mfupi Hammad alitangaza uhuru wake (mwaka 1015) huku akivunja uhusiano na Wafatimi na kujifanya mtiifu kwa Waabbsi. Kwa hivyo nasabatawala ya Kisanhaja iligawika sehemu mbili - Waziri walioizuia Ifrikiya hasa, na Wahammadi walioitawala Maghrib ya kati. Ingawa Badis, na baada ya kifo chake, mrithi wake al-Muizz (1016-62), alimshinda Hammad mwishoni, hata hivyo walilazimishwa kuutambua uhuru wa Wahammadi; suluhu ya mashaka ilifuatita kati ya matawi mawili haya.

Wengi kati ya wakazi wa Ifrikiya na Maghrib ya kati walikuwa wapinzani wa madhehebu ya Washia wa Kiismaili ambayo ndiyo iliyokuwa dini rasmi ya Wafatimi na Waziri. Lakini upinzani huu ulikuwa upinzani baridi. Katika mwaka wa mwisho wa utawala wa Badis mauaji ya kwanza ya Washia yalitokea. Harakati hizi ambazo zilionyesha hisia za wananchi wa shamba na mijini zilimbainishia al-Muizz kwa uwazi hatari ya serikali ya kimadhehebu iliyobambikizwa kwa watu ambao wengi wao walikuwa na imani halisi ya Kisunni. Hii haina maana kwamba suala la dini ndilo lililotoa mchango muhimu katika mfarakano kati ya Waziri na Wafatimi ulitokea kati ya karne ya kumi na moja, lakini lilichangia katika uamuzi wa al-Muizz kutupilia mbali utiifu wake kwa Wafatimi huko Kairo na kurejea kwenye imani halisi.

Umoja wa Maghrib, ambao Wafatimi waliutaka lakini hawakuupata kwa msingi wa kudumu, haukucendelea baada ya kuondoka kwa Wafatimi kuelekea mashariki. Kule kugawika kwa Waberiberi na kupinga kwao kwa utaratibu wa kudhibiti shughuli zote za kisiasa kulikuwa na nguvu zaidi kuliko juhudi dhafu za Waziri za kutaka kuendeleza sera za kuimarisha umoja uliokuwa ukifuatwa na watawala wao. Katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na moja, ramani ya kisiasa ya Maghrib ilitoa sura ifuatayo:

- (1) Upande wa mashariki, huko Ifrikiyya, milki ya Kiziri ilikuwa ndiyo dola iliyoendelea kabisa na yenye utulivu ikilinganishwa na nyingine.
- (2) Upande wa Maghribi wa ufalme wa Kiziridi, Wahammad walianzisha dola yao huru ambayo daima ilikuwa ikipigana na Wazanata na mara chache na Waziri pia.
- (3) Baada ya kuondoka kwa Wafatimi na kuanguka kwa ukhalifa wa Umayya huko Hispania, vikundi mbali mbali vya Wazanata vilichukua nafasi hii kuanzisha vijidola huru vidogo vidogo huko Tilimsan, Sijilmasaf Fes na kwengineko. Kabisa hawakuanzisha mpango wa kudhibiti shughuli zote za kisiasa bali vilikuwa vikundi vya Kilugha na Kimbari vilivyunganishwa na chuki yao dhidi ya Wasanhaja.
- (4) Katika mwambao wa Atlantiki, wakufuru wa Kibarghwata waliweza kuuhifadhi uhuru wao dhidi ya mashambulizi ya Waziri na baadaye Wazanata.
- (5) Waghomara walikuwa katika hali kama hiyo huko Moroko ya Kaskazini, na waliuimarisha uhuru wao zaidi baada ya kuanguka kwa Waumaya.
- (6) Vikundi vya Wamasmuda katika Moroko ya kusini, yaani Waanti Atlas na Wasus, waliendelea kuishi katika hali ya uhuru kama jamii ndogo ndogo zisizokuwa chini ya chombo cho chote kikubwa.

Kwa jumla, hali ya Waberiberi ilishabihi hali ilivyokuwa kabla ya uvamizi wa Waarabu: athari za Kiarabu zilijitokeza katika miji tu, na kasi zake zilipungua kidogo kidogo kuanzia mashariki kuelekea Maghribi. Sambamba na hali hii kulikuwepo muundo wa kisiasa: katika Ifrikiya muundo wa dola ulikuwa umeendelea sana, wakati katika selemu za Maghribi ya Maghrib jamii zilizokuwepo zilikuwa bado kufikia kiwango cha kuwa dola.

Hali ya kidini ilipata mabadiliko makubwa katika kipindi kilichofuatia utawala wa Wafatimi: ilivyofika kati ya karne ya kumi na moja sehemu yote ya Maqhrb iliweza kuonekana kama ni jimbo lenye imani halisi ya Kisunni lisilokuwa na alama za Ushia na lililokuwa na visehemu vichache tu vya Kikhariji. Mabadiliko haya yanaweza kuelezewa kuwa ni matokeo ya moja kwa moja ya kule kurejea tena kwa uongozi wa kisiasa wa Waberiberi. Katika hali hii madhehebu ya Kikhariji yalipoteza ule msingi wake wa itikadi wa upinzani wa Kiberiberi dhidi ya wavamizi na watawala wa Kiarabu wenye imani ya Kisunni. Pia ni miongoni mwa kejeli za kihistoria kwamba wale Wafatimi, ambao ni miongoni mwa nasabatawala za Kishia zilizofaulu na kuwa na nguvu kabisa, kwa kuyashinda na kuyahasiri kabisa madhehebu ya Kikhariji ya huko Afrika Kaskazini walifungua njia ya kupatikana ushindi sahihi wa madhehebu ya Kimaliki ya Kisunni katika sehemu za mashariki na kati ya Maghrib.

### *Uvamizi wa Banu Hilal na Banu Sulaym*

Wakati Mziri al-Muizz ibn Badis mwishoni kabisa alipovunja uhusiano na mtawala wake wa Kifatimi, al-Muntasir, na kuutambua Ukhalifa wa Waabasi wa Baghdad, na kwa hivyo kuyaacha madhehebu ya Kishia na kuyafuata yale ya Kisunni, kisasi cha Wafatimi kilikuwa cha aina ya pekee. Kutokana na kutowezekana kupeleka jeshi dhidi ya watawaliwa hawa waliovunja utiifu, waziri, al-Yazuri, alimshauri bwana wake kuwatia adabu Wasanhaja kwa kuikabidhi Ifrikiya mikononi mwa makundi ya Waarabu yasiyokuwa na maskani maalum ya Wabanu Hilal na Banu Sulaym ambayo wakati huu yaliishi sehemu za juu za Misri.

Kuwashawishi machifu wa mbari zote mbili hizi kuhamia upande wa Maghribi inaonekana hakukuwa jambo gumu sana, kwa vile kuhamia huko kulikuwa na tamaa ya kujipatia ngawira za



thamani na sehemu bora zaidi za malisho kuliko zile za Sehemu za Juu za Misri.

Waarabu walianza kuhama katika mwaka 1050-1, na katika kipindi cha mwanzo walilivurugavuruga jimbo la Barka; kikundi cha Banu Hilal tena kilielemea mbele zaidi sehemu za Maghrib, sehemu ya Barka wakiwaachia Wabanu Sulaym ambao walibakia huko kwa baadhi ya vipindi vya miaka kumi kabla ya kusonga mbele tena. Kikosi cha mwanzo cha Wabanu Hilal kilipochomoza Tunisia ya kusini, al-Muizz hakutambua mara moja kisirani gani kilikutambalia utawala wake. Alijaribu kuwaandikisha wavamizi katika jeshi lake kama ni wenzake wa siku za usoni: kufuatia mwaliko wake wengi kati ya watu wa Banu Hilal waliondoka Barka na mara tu makundi yao yalizitia mikononi sehemu za kusini za ufalme wa Kiziri. Ule unyakuaji wa ngawira ulipozidi kuendelea kwenye vijiji na miji ulivuruga tamaa za al-Muizz za kuwafanya wanomadi wawe ndiyo nguzo ya jeshi lake. Alijaribu kuzizuia hujuma zao lakini, katika mapigano mengi, miongoni mwao yale mapigano yaliyofanyika katika jimbo la Gabes (mwaka 1051-2) yakiwa ndiyo maarufu kabisa, jeshi lake lilishindwa moja kwa moja. Sehemu za mashamba pamoja na vijiji muhimu na hata baadhi ya miji ziliangukia mikononi mwa machifu wa kinomadi na hali ya machafuko na kutoweka kwa usalama ilizagaa zaidi. Katika mwaka 1057, al-Muizz alilazimika kuihama Kayrawan na kukimbilia al-Mahdiyya ambao sasa ukawa ndio mji mkuu wa milki yake ambayo ilikuwa imepungua sana. Mara baada ya hapo, Kayrawan ilivamiwa na Wabanu Hilal na kutokana na maafa haya haikuweza kuja juu tena.

Waarabu walipovamia Maghrib ya kati Wahammadi wa Kala walijaribu kujinyakulia fursa kutokana na machafuko ya jamaa zao wa Kiziri. Katika mwaka 1065, Mhammedi al-Nasir, akiongoza mkusanyiko mkubwa wa Waberiberi na Wabanu Hilal (Wasanhaja, Wazanata na sehemu za Wahilali wa Athbadj na Adi) alipigana dhidi ya sehemu nyingine za Kiarabu (Wariyadh, Wazughba na Wabanu Sulaym) na kushindwa vibaya huko Sabiba. Uwezo wa kudhibiti wa Wabanu Hilal uliendelea kuzidi kuimarika mpaka ikambidi al Nasir auhame mji mkuu wake, Kala, na kuelekea Bijaya (Bougie) na kuwaachia wanomadi sehemu za kusini za utawala wake. Bijaya ukawa ndio mji mkuu mpya wa nasabatawala ya Wahammadi. Wakati huu Waarabu wa kinomadi walikalika sehemu kubwa za Ifrikiya na Maghrib ya kati na kuanzisha tawala huru kadhaa ndogo ndogo ambazo ziliendelea mfululizo kupigana wenyewe kwa wenyewe na pia dhidi ya masalia ya dola za Kiziri na Kihammadi na kuongeza vurugu zilizokuwepo na kuzidi kuteremsha maisha ya kiuchumi. Haikuwa mpaka kati ya karne ya kumi na mbili ndipo utulivu uliporejeshwa kutokana na kuwasili kwa Wamoha.

Ibn Khaldun ndiye mwanahistoria wa mwanzo aliyesisitiza uharibifu uliofanywa na Mabedui ambao aliwalinganisha na 'wingu la nzige wenye njaa'. Wanahistoria wa leo kwa jumla wamekubaliana na maoni hayo na wameonyesha matokeo mbali mbali mabaya kwa historia ya Afrika Kaskazini yaliyosababishwa na 'maafa makubwa ya Wahilali.'

Katika miaka ya karibuni majaribio yamefanywa ya kusahihisha nadharia hii kuhusu 'maafa makubwa ya Wahilali'; hivi sasa inaelezwa kwamba wanomadi wa Kiarabu hawakuwa wengi kama ilivyodhaniwa na uharibifu wao pia haukuwa kama ilivyofikiriwa na kwamba kabla ya kuwasili kwao dalili za kuanguka kwa uchumi zilikwishajitokeza katika jamii ya Afrika Kaskazini. Mjadala huu umeweza kutoa mwangaza kuhusu masuala mengi na kwa kiasi fulani umeweza kusawazisha ule mtazamo wa upande mmoja uliowaona Wahilali kuwa ndio wakosa wakuu na pekee katika kuanguka kwa mwisho kwa jamii ya Afrika Kaskazini.

Haiwezi kukatalika kwamba kuwasili kwa kikundi kikubwa cha Wanomadi kiliashiria mabadiliko kauka historia ya Afrika Kaskazini kwa pande nyingi. Ingawa maendeleo ya kuleta Uarabu yalikwishafika mbali, mathalani huko Ifrikiya, sehemu kubwa za mashamba zilikuwa

zimekaliwa na kulimwa na watu waliokuwa wakisema lugha ya Kiberiberi. Wakati wavamizi wa Kiarabu wa kwanza walipokuja katika karne ya nane, walimezwa na wakazi wa Kiberiberi, vikundi vya Wabanu Hilali na Wabanu Sulaym vilianzisha mtindo kinyume ya huu. Baadhi ya vikundi vya Kizanata, hasa Wabanu Marin, vililazimika kurudi nyuma kuelekea Maghribi ili kuwapa nafasi Waarabu. Ingawa Waarabu hawakupenya katika majimbo ya mwambao wala katika sehemu za miima ambamo ndimo walinokimbilia Waberiberi waliozoea maisha ya utulivu, sehemu za tamarare nusu ya upande wa mashariki wa Maghrib kidogo kidogo zilianza kupata athari yao.

Kwa upande wa madhara yaliyopatikana kutokana na majilio yao, kwa jumla inakubalika kwamba yalikuwa makubwa ingawa pengine neno 'maafa' kidogo limezidi mpaka. Hapana wasiwasi kwamba kuweco kwa maelfu ya wanomadi na wanyama wao lazima kulileta matokeo makubwa katika maisha ya kiuchumi nchini. Ule ulinganifu uliokuwepo zamani baina ya wale wasiokuwa na maskani maalum na wale waliokuwa wametulia mahala pamoja huko Afrika Kaskazini uliparaganywa, na matokeo yake yakawa kwamba sehemu nyingi za ardhi iliyokuwa na rutuba ziliharwa na wakulima zikaachiwa Mabedui.

Ingawa ile hali ya machafuko ambayo ilikuwa ni matokeo ya kuanguka kwa dola ya Waziri na Wahammad huenda ikawa haikuzagaa kama ilivyoelezwa na Ibn Khaldun, hali ya usalama kwa jumla iliathirika vibaya kutokana na kuweco vikundi vingi vilivyokuwa huru na vyenye fujo. Kuanguka kwa miji katika sehemu za ndani kulitokea kwa haraka na wakati Kayrawan haikuwa na budi kupoteza umuhimu wake wa zamani, Kala ya Bani Hammad kidogo kidogo ilitoweka:

Majeruhi wakuu walioathirika walikuwa ni tawala za Waziri na Wahammadi ambazo zilibakia katika mwambao wa sehemu za al-Mahdiyya na Bijaya tu. Maendeleo ya wanomadi wa Kiarabu katika sehemu za ndani yalichangia katika kuwafanya Waberiberi Wasanhaja waeleeme upande wa pwani na hata yaliupa nguvu ule mgawanyiko baina ya majimbo yaliyokuwa sehemu za ndani ya yale yaliyokuwa sehemu za mwambao. Katika mabaki ya dola za Kiziri na Kihammadi uharamia ulishamiri. Bijaya, ambayo ilikuwa pahala pazuri zaidi kuliko al-Mahdiyya, ambayo haikuwa na mbao za kujengea meli, ilikuwa kituo muhimu cha bahari na iliingia katika biashara iliyokuwa imepamba moto iliyofanyika na sehemu nyingine za Mediterania hasa katika miji ya Kiitalia. Wahammadi waliweza, mwanzoni mwa karne ya kumi na mbili kukiteka na kukitawala kisiwa cha Jerba.

Uchumi wa Afrika Kaskazini kama ilivyokuwa zamani ulidhoofishwa sana. Ule uchumi wa Maghrib mashariki uliokuwa na msingi wa kilimo na urulivu kidogo kidogo ulibadilika na kuupisha uchumi mwingine uliotawaliwa na sifa za kinomadi na za kiuchungaji. Mabadiliko haya makubwa katika sehemu za mashariki pia yalitokea wakati ule ule ambapo majimbo ya Maghribi yalikuwa yanaathiriwa na kikundi kingine cha wanomadi, yaani Wamoravi. Matokeo yote haya mawili yalianzisha sura mpya katika historia ya Maghrib.

Karibu wakati ule ule ambao Wabanu Hilal na Wabanu Sulaym walipoanza kujipenyeza Afrika Kaskazini kutoka mashariki<sup>1</sup>, ulianza kutokea upande mwingine wa Maghrib mguro wa Waberiberi wa jangwani ambao, kwa muda mfupi, waliyavamia majimbo ya mashariki na ya kati. Harakati zote mbili hizi sambamba zilidhihirisha hamasa za kinomadi na zote zilisababisha kudhibitiwa na wanomadi kwa muda kwa jamii za watu waliotamakani, na pia vile vile vyombo vya nchi vilivyokuwa vimekwisha mizizi.

### *Usuli wa kisiasa, kiuchumi na kidini wa mguro wa Wamoravi*

Katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na moja, eno la Moroko pamoja na eno la kusini mwake hadi kufikia kwenye mto Senegal palikaliwa na Waberiberi ambao waligawika katika vikundi vingi vilivyopingana na kupigana wenyewe kwa wenyewe. Moroko yenyewe katika karne iliyotangulia ilikuwa ndicho kiini cha mapambano baina ya dola mbili kubwa za Maghribi, yaani Waumaya wa Kihispania na Wafatimi. Kwa jumla, Waumaya waliwakilishwa na kikundi cha Wazanata, wakati Wafatimi walikabidhi shughuli hii kwa Waziri wa Kisanhaja wakiwa ndio wapiganaji wao. Moja ya madhumuni makubwa ya mapambano haya yalikuwa ni kudhibiti njia za biashara kuelekea Sudan Maghribi na/au biashara ya dhahabu. Tawala mbalimbali za wana wa kifalme wa Kizanata huko Moroko ambazo zilikuwa zikipigana, si dhidi ya Waziri tu bali mara nyingi baina yao pia, zilieneza utawala wao taratibu kutoka Fez hadi Sijilmasa, Aghmat, Tamdult na selimu ya Wadi Dara, ambazo mpaka wakati huo, zilikuwa chini ya udhibiti wa Wasanhaja wa Sahara. Mfululizo wa mapigano na machafuko kwa jumla yalifanya maisha na shughuli za kawaida za kiuchumi chini ya utawala wa Kizanata kuwa magumu.

Hali kama hiyo ya machafuko ilikuwepo pia kusini mwa Moroko miongoni mwa Wasanhaja wa Sahara wavaa buibui (*mulathuhamun*). Wasanhaja hao wa kinomadi walikuwa katika matawi matatu: Wamassufa kwa upande wa Kaskazini na mashariki (huko Wadi Dara, Hawd na Taghaza), Walamtuna huko sehemu ya kati na kusini (huko Adrar na Tagant) na Wajuddala (au Waguddala) kwa upande wa Maghribi katika sehemu ya Sahara inayopakana na bahari ya Atlantiki. Hadi mwanzoni mwa karne ya kumi, Waberiberi wa Maghribi ya Sahara walijulikana kwa jina la Waanbiya na mpaka sasa si dhahiri kama hilo lilikuwa jina la ule muungano legelege wa matawi matatu haya au kama lilikuwa ni jina la tawi mojawapo<sup>2</sup>.

1 Taz. Sura ya 12 ya kitabu hiki.

2 Taz. Sura 11 ya juzuu hili.

Mnamo karne ya kumi kulikuwa na majaribio ya kuwaunganisha Wasanhaja, pengine ili kuhakikisha udhibiti bora wa njia za biashara au kwa madhumuni ya kuivamia Sudan. Lakini haya yalifuatiwa na kipindi kirefu cha mfarakano, mkanganyiko na machafuko. Hakuna hata kundi moja lililoweza kutamalaki huko jangwani na hivyo kufanya uongozi wa mahali hapo kubadilika mara kwa mara.

Hali hii iliyojitokeza miongoni mwa vikundi vya Kisanhaja haikuacha kudhuru ustawi wao wa kiuchumi. Ingawa uchungaji wa kinomadi ndio ulikuwa msingi wa maisha ya wengi miongoni mwa Wasanhaja wa jangwani, kushiriki kwao katika biashara za misafara baina ya Maghrib na Wasudan kupitia nchini kwao kulisaidia kurwaongezea pato.

Hadi kufikia robo ya tatu ya karne ya kumi, mtuungano wa Wasanhaja ulidhibiti migodi muhimu sana ya chumvi huko Awlil na kuhodhi biashara ya chumvi iliyopitia Awdaghust mpaka Ghana. Ingawa mji wa Awdaghust ulikuwa haujafikia upeo wa kukua kwake, bado ulikuwa kituo muhimu cha biashara kilichodhibitiwa na chifu wa Kisanhaja na kukaliwa na watu ambao wengi wao walikuwa Wasanhaja. Hata hivyo, baada ya mwaka 970, biashara ya Awdaghust ilianza kutawaliwa na wafanyabiashara Wazanata na Waarabu wa Ifrikiya, na Wasanhaja wakiwa karibu wameondolewa kabisa katika biashara hiyo.

Kudhoofika kwa Wasanhaja kuliwaruhusu pia Waberiberi wa Maghrawa wa huko Sijilmasa kudhibiti na kuikalia sehemu kubwa ya malisho huko Dara, Aghmat na Tamdult, na sehemu hizi zilikuwa muhimu kwa uchumi wa kinomadi wa makundi ya Kisanhaja ya upande wa Kaskazini.

Hivyo, katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na moja, Wasanhaja wa Sahara Maghribi walipoteza udhibiti wao wa zamani wa Kaskazini na kusini ambako maadui wao wa jadi, Waberiberi wa Zanata, walivinyakua si tu vituo vya njia za kuvukia Sahara (Sijilmasa na Awdaghust) bali pia sehemu za bora kabisa za malisho.

Sasa tukigeukia hali za kidini zilizokuwepo katika sehemu ya Maghribi kabisa ya ulimwengu wa Kiislamu kabla ya kuchomoza kwa Wamoravi, tunakuta si tu aina mbali mbali za madhehebu yaliyokengeuka, bali pia viwango mbalimbali vya usilimishaji toka ujuzi wa kijuujuu tu wa misingi ya dini, kama waliokuwa nao Waberiberi wa jangwani na wa milimani, hadi vyombo vya hali ya juu vya dini ya Kiislamu kwenye baadhi ya miji na majimbo.

Miongoni mwa madhehebu yaliyokengeuka yaliyokuwa yakivutia kuliko yote ni yale ya Wabarghawata, kundi la Waberiberi lililoishi kwenye sehemu tamarare za Atlantiki za huko Moroko kati ya Sale na Safi<sup>3</sup>. Katika sehemu za kusini za Moroko, kwenye jimbo la Sus, katika milima ya Atlas na bonde la Dara kuliishi makundi ya Kishia ya madhehebu mbali mbali. Lakini madhehebu yasiyokuwa na imani halisi yaliyokuwa muhimu kabisa miongoni mwa Waberiberi, yalikuwa yale ya Kikhariji, na hasa Waibadi<sup>4</sup>. Ingawa baada ya majilio ya Wafatimi na ule uasi ulioshindwa wa Abu Yazid huko Ifrikiya, umuhimu wa kisiasa wa Wakhariji huko Mediterania Maghribi ulipungua, bado walibakia na nyadhifa na athari muhimu huko Sahara na Sudan, hasa kama wafanyabiashara na wahubiri wa dini.

Nyaraka zote za Kiarabu za hapo mwanzoni kuhusu kuibuka kwa vuguvugu la Wamoravi zinakubaliana katika kusisitiza usilimishwaji wa juujuu wa watu wa Sahara na kutolewa na kupuuzwa kwao mambo ya kidini. Ni kweli kwamba miongoni mwa machifu na viongozi, walikuwepo watu waliokuwa na ujuzi mkubwa wa dini ya Kiislamu, ambao walikuwa wamekwisha kwenda kuhiji huko Maka na hata baadhi ya mafakihi waliojaribu kuendeleza

3 Taz. Sura 3 na 10 ya juzuu hili.

4 Taz. Sura ya 10, 11 na 12 ya juzuu hili.

hali ya kidini ya wananchi wenzao.

Nusu ya kwanza ya karne ya kumi na moja ilishuhudia kufufuka kwa madhehebu halisi ya Uislamu wa Kisunni katika ulimwengu wa Kiislamu kutoka Maghrib, kwa upande wa Maghribi, mpaka Iran, kwa upande wa mashariki. Hali hii ilizuka kama sehemu ya upinzani dhidi ya nasabatawala za Kishia kama vile Wafatimi na Wabuwayhi. Chini ya utamalaki wao ilikuwemo sehemu kubwa za nchi za Kiislamu. Waliojitokeza katika mapambano ya kiitikadi dhidi ya Washia na madhehebu mengine yaliyokengeuka walikuwa *mafakihi* wa Kimaliki wa Afrika Kaskazini, hasa wale waliotoka katika ngome ya kale ya Kimaliki huko Kayrawan.

### *Mwanzo wa shughuli za Ibn Yasin za kuleta mabadiliko*

Maelezo yanayokubalika kwa jumla kuhusu chanzo cha vuguvugu la wa Wamoravi yanasema kwamba Yahya ibn Ibrahim, mmoja wa viongozi wa Waberiberi wa Kijuddala kutoka Sahara Maghribi, ambaye, wakati akirejea kutoka kuhiji Maka, alimtaka Abu Imran al-Fasi (mwaka 1039), mwanasharia maarufu wa Kimaliki wa huko Kayrawan, kumpa mtu wa kwenda naye akawafunze watu wake dini halisi ya Kiislamu, kwani watu hao walikuwa hawajui vizuri. Kwa vile Abulmran hakuweza kumpata mtu yeyote huko Kayrawan aliyekuwa tayari kwenda kuishi miongoni mwa washenzi wa Kisanhaja huko jangwani, alimshauri Yahya aende kumtembelea mmoja wa wanafunzi wake wa zamani, Waggag ibn Zallu al-Lamti, huko Malkus karibu na Sijilmasa, ili akapate msaada kutoka kwake. Waggag alimpendekeza mwanafunzi wake Abdallah ibn Yasin kama mhubiri wa kutumainiwa.

Hatuna habari nyingi kuhusu maisha ya Abdalla ibn Yasin kabla ya kupelekwa kwake kwenye jangwa la Sanhaja. Tunachojua ni kwamba alitoka miongoni mwa Wajazula, kundi la Waberiberi kusini mwa Moroko, mama yake akiwa ametoka kijiji cha Tamamanawt kwenye kingo za jangwa zilizopakana na Ghana. Baadhi ya vyanzo vya baadaye vinaonyesha kwamba alisoma kwa muda wa miaka saba katika sehemu ya Uhispania iliyosilimu, lakini maandishi ya al-Bakri ya karibu wakati huohuo yanatilia mashaka makubwa kiwango cha ujuzi aliokuwa nao Yasin wa Korani na sharia ya Kiislamu.

Historia ya harakati za Ibn Yasin za kuleta mabadiliko miongoni mwa Wasanhaja inajulikana kwa jumla jumla tu, kwa vile kronolojia ni ya mashaka na yenye mikanganyiko. Katika shughuli zake jangwani tunaweza kubainisha awamu mbili: katika awamu ya kwanza alijaribu kuendeleza au kubadilisha imani ya dini miongoni mwa Wajuddala na alifaulu kujipatia wafuasi kadha. Awamu hii ilidumu kuanzia karibu mwaka 1039 mpaka mwaka 1053 na ilisitishwa na ugomvi baina ya mleta mabadiliko na viongozi wa Wajuddala uliofanya Ibn Yasin afukuzwe. Katika awamu ya pili ambayo ilidumu hadi kifo chake mnamo mwaka 1059, Walamtuna walikuwa ndiyo nguzo kubwa ya vuguvugu la Wamoravi. Kutoka kipindi cha kwanza kumbukumbu zimewekwa za matukio mawili tu: shambulio dhidi ya Walamtuna, ambao walishindwa kwenye milima yao (ya Adrar), na kuanzishwa kwa mji wa Arat-n-anna ambako, kulingana na fikra za Ibn Yasin kuhusu usawa, nyumba zote zilikuwa ziwe na urefu ule ule kwenda juu.

Baada ya kuishi miongoni mwa Wajuddala kwa zaidi ya miaka kumi, Ibn Yasin alihitilafiana na *fakihi* wa hapo na watukufu wawili wa Kijuddala. Chanzo cha mfarakano huu yaonekana kilikuwa mchanganyiko wa tofauti za kidini na kugombea madaraka baada ya kifo cha Yahya ibn Ibrahim al Juddali.

Matashi makali ya Ibn Yasin kuhusu nidhamu na uzingatifu wa majukumu yote ya kidini

na vile vile falsafa yake ya imani safi na ya usawa wa watu wote labda hazikupokelewa kama alivyotarajia; na kwa vile alikuwa mwalimu mkali, alipuuza maadili na miko ya jamii ya Wasanhaja. Tamko hili linaonyesha kwamba uwezo wa madaraka wa Ibn Yasin haukuwa mkubwa na haukumwezesha kulazimisha mambo yake.

Ilikuwa miongoni mwa Walamtuna wakiongozwa na Yahya ibn Umar ndipo Ibn Yasin alipoupata mwege wa kisiasa wa kutekeleza dhamira zake. Hiki ndicho kilichokuwa chanzo cha sababu kubwa ya kutamalaki kwa Walamtuna. Yote haya yalitokea kabla ya 1055 na kwa wakati huo yaonekana kulikuwepo mvutano mkubwa baina ya Wajuddala na Walamtuna ambao pengine ulisababishwa na sera tofauti kati yao kuhusu mwelekeo wa vuguvugu kwa siku za baadaye.

### *Kugeuzwa kwa vuguvugu la mabaliliko kuwa Jihadi*

Kutamalaki kwa Walamtuna katika mguro ndiko kumefanya mara nyingi wameonekana kuwa wao ndio Wamoravi halisi. Hata hivyo, kabla ya kuendelea na historia ya mguro huu, yafaa tujadili tatizo la asili ya hili jina la Moravi (Kiarabu, *al-Mrabitun*).

Mpaka hivi karibuni, ilikuwa ikichukuliwa kwamba neno hili linatokana na *ribat* (*al Murabitun* = watu wa *ribat* au *rabita*) ambalo maana yake inayokubalika ni 'mpaka ulioimarishwa au kituo cha mwambao' au 'kituo kinachoirimarishwa kwa ajili ya shughuli za kidini na za utawa'. Kulingana na Ibn Abi Zar (kipindi baada ya 1326), Ibn Yasin, baada ya kutokukubaliana na Wajuddala, alihamia katika kisiwa ambako alijenga '*rabita*' pamoja na wenzake saba; baadaye aliwafunza wafuasi wengi wengine na akawaita *al Marabitun* kwa sababu ya kushikamana kwao na *rabita* ile. Hata hivyo, hakuna hata moja ya vyanzo vya kale zaidi kinataja kuwepo kwa jengo kama hilo na kama ilivyoelezwa kwa usahihi na P. de Moraes Farias, 'inashangaza ni kwa nini maelezo yaliyotolewa na Ibn Abi Zar yamekubaliwa bila kusailiwa na wanahistoria wengi.'

Utaalamu wa hivi karibuni mwishowe umeachilia mbali dhana ya *al-Murabitun*, yaani watu wa *ribat*. Jina hili yaelekea limetokana na maana ya Kikurani ya mzizi *r-b-t* ambayo inakaribiana na maana ya kupigana *jihadi*; na hivyo *ribat* pia lingeweza kufafanua mkusanyiko wote wa mafunzo ya Kiislamu yaliyotayarishwa na Ibn Yasin kwa ajili ya Wasanhaja. Si jambo la kukataliwa kabisa kwamba jina *al-Murabitun* linahusiana kwa namna fulani na jina '*Dar-al Murabitin* la Waggag ambapo ndipo Ibn Yasin alipoishi kabla ya shughuli zake za kuhubiri.

Uthibitisho wa mwisho kwamba hakukuwepo *ribat* (kwa maana ya kituo chenye ngome) katika kisiwa ulipatikana kutokana na shughuli za uchimbaji za IFAN (Institut fondmental de l'Afrique noire) katika kisiwa cha Tidra karibu na mwambao wa Mauritania mnamo mwaka 1966, ambako hakukugunduliwa masalia yoyote ya *ribat*.

Ni vigumu kujua ni lini hasa Ibn Yasin alikimbilia katika kisiwa hiki, lakini pengine tukio hili lilitokea kabla ya mwaka 1052-3. Ibn Yasin alipotoka mafichoni na kuwakuta miongoni mwa Walamtuna, hasa katika familia yao ya kichifu, iliyowakilishwa na Yahya ibn Umar na ndugu yake Abu Bakr, wafuasi wake waaminifu kabisa, mguro ulilingia katika awamu muhimu: yaani kutoka mguro wa kuleta mabadiliko ukawa wa kipiganaji ambao wanachama wake walikuwa tayari kueneza mafunzo ya muasisi wao miongoni mwa Wasanhaja wengine na hata mbali zaidi ama kwa kuwashawishi au kwa *jihadi*. Ingawa Ibn Yusuf alitaka tangu mwanzo kufanya mguro wake kuwa na sifa zilizovuka ukabila, *Waal-Murabitun* walikuwa na

waliendelea kubakia wanachama wa makundi mahsusi ya Waberiberi. Uongozi ulikuwa mikononi mwa Walamtuna chini ya chifu wao Yahya ibn Umar, ambaye Ibn Yasin alimkabidhi uongozi wa kijeshi akiwa ndiye amir wakati ambapo matawi mengine yaliyoshiriki katika uanzilishi wake, yaani Wamassufa na Wajuddala ( walau hapo mwanzo) walifuata uongozi huu wa jumla.

Kuwaunganisha Wasanhaja hakukuwa kazi nyepesi; Wajuddala ambao walilazimishwa kujiunga tena na mguro waliendelea na upinzani na walijitenga pale walipopata nafasi. Wakati jeshi kubwa la Wamoravi lilipokuwa likipigana huko kusini mwa Moroko, Wajuddala waliasi na Yahya ibn Umar alipelekwa kupigana nao lakini akauawa mnamo mwaka 1056 katika mapigano ya Tabfarilla, ambapo jeshi lake, japokuwa lilikuwa limeimarishwa na majeshi ya Labi ibn War-Dyabi, chifu wa Takrur, lilishindwa. Kwa upande mwingine Wajuddala walishiriki baadaye katika mapigano ya Wamoravi huko Maghrib na wakachukuliwa kuwa Wamoravi halisi. Kitu ambacho hakikuwa wazi zaidi ni mahusiano yao na Wamassufa: kwa mujibu wa Ibn Khaldun, kulikuwa na mgogoro baina yao na Walamtuna, lakini yaelekea kwamba mgogoro huo ulisuluhishwa mara moja na Wamassufa na Walamtuna wakaunda muungano imara katika mapigano yaliyofuatia. Ama kuhusu Waberiberi wengine, Walamta walishindwa mapema na wakajiunga na Wamoravi kama walivyofanya hata baadhi ya Wazanata na Wamasmuda.

Pamoja na mfarakano wa ndani kwa ndani na mielekeo ya kutaka kujitenga, mfumo mpya wa kisiasa na kidini na maslahi yaliyofanana yaliwaletea umoja Waberiberi wa Kisanhaja. Wale walioishi katika njia za biashara walikuwa na haja ya kutaka kudhibiti tena njia hizo pamoja na biashara iliyohusika. Zile mbari za Kaskazini yaani Walamta na Wajazula, na vilevile baadhi ya Walamtuna zilitaka kukamata sehemu za malisho mazuri kati ya milima ya Atlas na jangwa la Sahara. Adui kwa makundi yote mawili walikuwa Wazanata. Ingawa si Wazanata wote walikuwa waumini wa madhehebu ya Kikhariji, lakini wengi wao waliyapokea na kukufuru kwao ndiko kuliwapa Wamoravi wa Kimaliki sababu nyingine ya kuwashambulia. Kilichochangia sana katika ushindi wao wa mwanzo ni ile hali ya kutoweka utawala thabiti huko Moroko chini ya koo tawala za Wamaghrawa, na watu wengi waliwakaribisha Wamoravi na kuwaona kuwa ni wakombozi kutokana na madhila ya Wamaghrawa. Katika kipindi cha zaidi ya miaka mitano kati ya mwaka 1054, Wamoravi walivunja hatamu ya uongozi wa Wazanata katika Afrika ya Kaskazini - Maghribi. Mapigano ya mwanzo yalikuwa dhidi ya miliki ya Wazanata katika bonde la Dara na baadaye dhidi ya Wasijilmasa. Baada ya kukikamata kituo cha mwisho cha biashara ya misafara kwa upande wa Kaskazini, jeshi la Wamoravi mara moja lilirejea kusini, dhidi ya Awdaghust. Baada ya kuteka Awdaghust wakazi wake wa Kizanata waliuawa kikatili. Hivyo kituo cha mwisho cha njia inayovuka Sahara kiliingia katika mamlaka yao na kwayo wakaweza pia kudhibiti biashara ya Maghribi.

Katika miaka michache iliyofuatia, Ibn Yasin alithibitisha si tu kwamba alikuwa mleta mabadiliko ya kidini na mpiganaji mkali, bali pia mwanasiasa aliyekamilika. Kwa kutumia diplomasia nzuri, aliweza kuwasalimisha amri Waberiberi wa Kimasmuda wa milima ya Atlas kwa njia ya amani na vivyo hivyo baada ya majadiliano ya muda mrefu, mji muhimu wa Aghmat, na eneo lote la Sus viliingia chini ya udhibiti wake (mnamo mwaka 1058). Kwa namna hii imani zote za uzushi na nyingine zinazotofautiana katika sehemu hii kama ya Moroko zilikomeshwa na imani ya Kimaliki kama ilivyochukuliwa na Wamoravi kuanzishwa kila mahali.

Lakini katika mapigano yao dhidi ya adui mkali kabisa wa imani halisi, Wabarghawata, Wamoravi walikumbana na pingamizi lao kubwa la mwanzo; mnamo mwaka 1059 walishindwa na Ibn Yasin aliuwawa katika hali isiyoeleweka sawa sawa katika mapigano karibu na Kurifalat. Mrithi wake katika uongozi wa jamii ya Kimoravi akawa Abu Bakr ibn Umar.


Ingawa kifo cha muasisi huyu kilisababisha mgogoro wa muda, bado ni ushahidi wa umadhubuti wa mafanikio yake kwamba mguro mzima haukuvurugika, ila baada ya muda mfupi lilijipatia nguvu mpya na kubwa zaidi zilizowawezesha Wamoravi kuendelea kufanikiwa katika kueneza mafunzo yao mapya na katika kuziteka sehemu nyingine.

Baada ya kifo cha Ibn Yasin, jamii ya kidini ilijigeuza na kujiunda kuwa ufalme. Hapo uongozi wa kidini ulipoanza kupoteza umuhimu wake wa awali, cheo cha *amir* kilipata utukufu na aliyechukua nafasi hiyo akawa mwanzilishi wa nasabatawala. Wakati huo huo, ngazi tofauti za nyadhifa zilianzishwa: wa juu kabisa katika utawala walikuwa Walamtuna, tawi la watawala, na hivyo Wamoravi kujulikana kwa cheo cha *al-Lamtuniyyun al-murabitun* au kwa kifupi wakiitwa *Walamtuna*. Cheo cha *al-murabit* kilitumika tu kwa wajumbe wa matawi matatu ya mwanzo.

'Waliojigubika' (yaani *al-mulaththamun*) ni jina jingine walilopewa Wamoravi, na jina hili linatokana na ile mila ya jadi ya Wasanhaja wa jangwani ya kuvaa kitu cha kufunika mdomo. Katika sehemu ya Hispania iliyosilimu buibui ilichukuliwa kuwa heshima ya pekee ya Wamoravi halisi, na watu wote isipokuwa Wasanhaja walizuiwa kuivaa. Buibui ilikuwa ndio kama sare iliyolitofautisha tabaka tawala.


Kuanzishwa kwa Marrakesh kama mji mkuu mpya upande wa Kaskazini wa milima ya Atlas mwaka 1070, kulifungua sura mpya katika historia ya Wamoravi. Wakati huo huo kulitokea mgawanyiko wa mguro wa Wamoravi katika sehemu mbili, sehemu ya kusini, ikiongozwa na Abu Bakr, na sehemu ya Kaskazini, ikiongoza na binamuye Abu Bakr, ajulikanaye kama Yusuf ibn Tashfin<sup>5</sup>. Abubakar alipoitwa arudi jangwani ambako

5 Nasaba ya maamiri wa mwanzo Wamoravi inaonyeshwa katika shajara ifuatayo (ambayo imerahisishwa):



migogoro mikubwa baina ya Walamtuna na Wamassufu iliyotishia umoja wa mguro, Yusuf ibn Tashfin akawa naibu wake sehemu ya Kaskazini akiwa amepewa jukumu la kuendeleza mapigano dhidi ya Wazanata. Baada ya kutuliza migogoro huko Sahara, Abu Bakr alirejea Kaskazini kuuchukua tena uongozi wa mguro mzima. Hata hivyo, wakati huo Yusuf ibn Tashfin aliimarisha nafasi yake na ilivyotarajiwa hakuwa tayari tena kumpisha jamaa yake,





13.1 Marakesh: uchiumbuzi wa kwanza wa Kasri ya Wamoravi. (J. Terrasse)

ingawa aliendelea kumtambua kama mkubwa wake. Kwa sababu mbali mbali, Abu Bakr hakutaka kuendelea kudai nafasi yake na kwa nia njema kabisa alimkabidhi madaraka Yusuf. Kisha alirejea Sahara kabisa. Hata hivyo, aliendelea kutambuliwa kama mkuu wa himaya nzima ya Wamoravi mpaka alipofariki mwaka 1087. Dinari za dhahabu za Kimoravi zilichapishwa mpaka wakati huo kwa jina lake, na hata Yusuf b. Tashfin aliendelea kuonyesha utii kwake japo kwa jina tu.

### *Utamalaki huko Kaskazini*

Katika miaka kati ya 1075 na 1083, jeshi la Wamoravi likiongozwa na Yusuf ibn Tashfin kidogo kidogo liliitaka Moroko na sehemu za Maghribi za Algeria. Kwa kuiteka Sabta, jeshi la Kimoravi liliudhibiti Mlangobahari wa Gibraltar na hii ikaiweka sehemu ya Hispania iliyosilimu machoni mwa mashujaa wa jangwani.

Huko Hispania kwenyewe si chini ya tawala uchwara ishirini zilichipuka kutokana na masalia ya utawala wa Makhalifa wa Kiumayya uliowahi kustawi.; Tawala hizi ndogo ndogo, ambazo kwa jumla zilitwa *muluk al tawaf* (wafalme wa chama), kwa Kihispania *reyes de taifas*, hazikuweza kuzipinga juhudi kali za tawala za Kiukristo za Kaskazini za kuzitaka kuzishinda nguvu. Baada ya Wakastiliana kuiteka Toledo (kwa Kiarabu, Tulaytula) katika mwaka 1085, hatari ya kumezwa kabisa dola zote za Kiislamu zilizokuwa katika peninsula ilianza kuonekana wazi, na ni msaada kutoka nje tu ndio ungeluweza kuwazuia Waukristo kusonga mbele. Nguvu pekee ambayo ingekamilisha kazi hii ilikuwa mikononi mwa Wamoravi. Kutokana na mwaliko wa mtawala wa Kiabbasid wa Seville, al-Mutamid, jeshi la

Wamoravi, likiongozwa na Yusuf b. Tashfin, lilivuka Mlango bahari wa Gibraltar mwaka 1086 na kujipatia ushindi mkubwa dhidi ya jeshi la Kikastiliana likiongozwa na Mfalme Alfonso VI huko huko al-Andalus; na kisha Yusuf akarejea Moroko kama alivyokuwa ameahidi kabla.

Lakini mara tu baada ya kuondoka kwake, mfarakano zaidi kati ya watawala uchwara uliwawezesha Waukristo kushambulia tena. Wamoravi waliitwa kuja kuingilia kati tena na katika mwaka 1088 walijipatia ushindi mwingine katika mapigano ya Aledo. Hata hivyo, *Wamuluk al tawaif* walionesha chuki za dhahiri kwa wakombozi wao ambao waliowaogopa kama vile walivyowaogopa maadui wao Waukristo, na Ibn Tashfin aliondoka al-Andalus kwa mara ya pili.

Ustahimilivu wake sasa ukawa umekwisha na katika mwaka 1090 alirejea tena lakini mara hii akiwa mvamizi, siyo rafiki msaidizi. Akiwa ametwaa *fatwa* (maoni ya kisharia) zilizotiwa sahihi na *mafukaha* wengi wa Moroko na wa Andalusi, aliongoza mapigano dhidi ya *Wamuluk - al - tawaif* ambao walituhumiwa kwa vitendo viovu dhidi ya Uislamu kama vile kushirikiana na Waukristo, ubadhirifu, utozaji haramu wa ushuru na kadhalika. Hadi kufikia mwaka 1094 sehemu yote ya Hispania iliyosilimu ilitwaliwa, isipokuwa Toledo, ambayo ilibaki mikononi mwa Waukristo, na Saragossa, ambako nasabatawala wa Banu Hud uliruhusiwa kuendelea kutawala na kuwa kama kinga. Watawala wote wa Kiislamu waliondolewa madarakani na umoja wa sehemu ya Hispania iliyosilimu - wakati huu ikiwa chini ya utawala wa Wamoravi - kuanzishwa tena.


Utamalaki wa Wamoravi kwa upande wa mashariki haukuvuka mji wa Algiers na maeneo yanayouzunguka. Kilichowafanya wasijipenyeze mashariki zaidi mpaka kufikia Ifrikiya, na kuamua kukomea hapo badala ya kukamilisha umoja wa Maghrib yote, mpaka sasa hakijulikani. Ni dhahiri hawakukutana na Waarabu wa Kihilal, ambao wakati ule walikuwa wakizurura katika majimbo ya kusini zaidi ya Ifrikiya na ya mashariki mwa Algeria. Yaelekea sababu ambayo ilifanya mambo yawe livyo, pengine ni hali iliyoendelea kuwa mbaya huko sehemu ya Hispania iliyosilimu ambayo iliendelea kumshughulisha zaidi na zaidi Yusuf ibn Tashfin; na kwa kuwa watu aliokuwa nao hawakutosha kupigana katika sehemu mbili, aliamua apigane dhidi ya Wakristo kwa kuzingatia umaarufu wa Wamoravi kama mashujaa wa Uislamu.

Kile kilichoanza tu kama mguro wa mabadiliko katika sehemu ndogo miongoni mwa Waberiberi wa jangwani kikageuka kuwa himaya iliyoanzia Ebro mpaka kwenye mito ya Senegal, ikiwa na ukubwa wa masafa ya karibu digrii 30 katika longitudi yenye mandhari za aina nyingi, kanda za shughuli za kiucrumi na mapokeo ya kitamaduni, zikitofautiana kuanzia tamarare zenye rutuba nyingi za Hispania na Moroko hadi majangwa ya Mauritania.

### *Masukumo wa Wamoravi kuelekea upande wa Kusini mwa Sahara*

Kwa bahati mbaya hali katika upande wa kusini haijulikani vizuri kama ile ya Kaskazini mwa himaya ya Wamoravi. Shida kubwa ni uchache wa vyanzo vya taarifa: vyanzo vya maandishi vinatoka katika fasihi ya Kiarabu ambayo waandishi wake waliishi sehemu za mbali, wakati ambapo mapokeo simulizi yamekumbwa na mabadiliko mengi, na ingawa hivi sasa yanaanza kuchunguzwa kitaalamu bado, ni vigumu kuyatumia.

Hatujui kwa hakika hali ilivyokuwa katika bonde la Senegal. Sasa hivi ni dhahiri kwamba sehemu muhimu ambamo makazi na masoko yaliendelezwa hazikuwa pwani bali katika cneo la ndani kabisa. Machimbo yaliyofanywa katika sehemu za Sintiu Bara yameonyesha kwamba



13.2 *Nakshi ya Walmoravi: kigongeo cha mlango cha shaba nyeusi (Fez). (UNESCO/Dominique Roger)*

hapo palikuwa pahala muhimu tangu karne za tano na sita. Katika makazi mengine makubwa, huko Ogo, chuma kilikwishaanza kuyeyushwa katika karne ya tisa.

Tunaelewa kutokana na Al-Bakri na al-Idrisi kwamba Silla na Takrur, maeneo ambayo yote hayajabainishwa vya kutosha, kwa pamoja zilitawala kiuchumi sehemu ya kati ya Senegal katika karne za kumi na moja na kumi na mbili. Ushahidi wote unaonyesha kwa uthabiti kwamba baina ya karne ya sita na ya kumi na mbili jimbo hili la kati la mto lilikuwa na shughuli nyingi, (hasa za uvuvi) na nguvu nyingi. Lakini haya yote yanajitokeza kijuu juu tu katika taarifa za maandishi na katika mapokeo simulizi.

Kwa upande wa kusini kidogo, tuna habari zaidi kuhusu ufalme ambao kwa muda mrefu ulikuwa kizani, yaani Djafunu (Zafun-u). Ufalme huu, ambao ulikuwa katika ndagano ya mito Kolombine na Senegal, ulisilimu katika karne ya kumi na moja.

Azuki, ambayo kwa mujibu wa utafiti wa awali, ilikuwa na shughuli nyingi kati ya karne ya kumi mwishoni na katikati ya karne ya kumi na mbili, pengine ilikuwa ni kituo muhimu cha kupangia mikakati katika mfumo huu wa Kisenegali.'

Maisha ya kisiasa ya eneo hili sasa yalianza kuchomoza kutoka kizani, walau katika nadharia tete. Bado ni vigumu kuwa na hakika ni sehemu ipi kati ya Silla, Takrur na Djafunu ilidhibiti zaidi biashara ya dhahabu ambayo yasemekana ilitoka sehemu za kusini zaidi, sehemu ya Kaskazini kabisa ikiwa baina ya Falame na Bafing. Kuimarika kwa Wamoravi kusini mwa sehemu inayojulikana sasa kama Mauritania kulileta athari dhahiri juu ya jografia ya biashara ya dhahabu na katika ushindani uliokuwepo miongoni mwa miji ya kandokando mwa mto Senegal.

Swali la kujiuliza ni iwapo Wamoravi waliwakuta wafalme wa Kiislamu huko kwenye mto Senegal, ambao walikuwa wakikutana na Waberiberi tangu mwanzo wa kusilimishwa kwa eneo hili au iwapo ndio walioanzisha kuongoa miji ya kati ya mto Senegal. Uchunguzi wa kitaalamu wa hivi karibuni kabisa unaonesha kwamba Uislamu ulikitangulia kipindi cha Wamoravi, na huenda ndio uliosababisha kuanguka kwa nasabatawala wa awali wa Takrur ambao ulishikamana sana na 'wapagani' wayeyusha chuma na majusi. Ni dhahiri sasa kwamba Uislamu ulitoa mchango muhimu katika bonde la Senegal katika karne ya kumi na kumi na moja na kwamba maelewano kati ya Wamoravi na watawala Waislamu wengi pengine yalichangia kwenye ushindi wa wapiganaji waliojigubika waliotoka Kaskazini.

Mashariki zaidi, hali haikuwa nzuri sana kwa Wamoravi. Delta ya ndani ya mto Niger ilikuwa eneo la kale la biashara ambalo lilijengwa kabla ya ujio wa Uislamu. Yaelekea kwamba sehemu kubwa ya dhahabu iliyopatikana hadi katika sehemu za misitu ilikusanywa kutoka eneo hili; kufikia karne ya kumi, wafanyabiashara ya dhahabu weusi waliokusanya dhahabu hiyo walikuwa na mawasiliano na Ghana, kwa upande wa Kaskazini, na pengine nyakati fulani fulani, pia na Gao, kwa upande wa mashariki. Wana wa kifalme walioitawala miji miwili hii wafidhibiti mauzo ya dhahabu upande wa Kaskazini. Mtawala wa Ghana hakuwa Muislamu wakati wa kupanuka kwa utawala wa Wamoravi, ingawa alikuwa na uhusiano mzuri kabisa na Waislamu. Waislamu wengi, kama machimbo ya Kumbi Saleh yalivyoonyesha, waliishi katika mji huu uliokuwa na soko, ambapo mtawala wa Ghana aliwakaribisha kwa furaha na pia waliweza kusali kwenye msikiti wenye mnara kuanzia karne ya kumi na kuendelea. Mfumo wote wa Ghana ya ndani na Delta ya Niger ambao uliundwa muda mrefu kabla ya Wamoravi na ambao kwa hakika uliwachukia Wasauhaja, ulitumiwa kufanyia biashara na wafanyabiashara wa Kiifrikiya. Hivyo yaelekea kuliwali kutokea mgongano baina ya Wamoravi na mfumo wa Kighana. Lakini kwa hivi sasa ni vigumu sana

kusema makabiliano haya yalikuwa ya aina gani.

Ili kujibu suali hili, tutahitaji kubainisha aina na viwango vya usilimishaji vilivyofikiwa Sahel wakati mguro wa Wamoravi ulipoanza kukua. Juhudi ya pamoja kubwa ya mwanzo ya kuwasilimisha watu ilikuwa ya watu wa Sahara - yaani Wamoravi, na ilianza karne ya kumi na moja. Katika karne mbili au tatu zilizotangulia, maendeleo ya Uislamu yalikuwa ya kusitasita na yalitangamana na kuwoko kwa wafanyabiashara kutoka Kaskazini na pia kukua kwa miji<sup>6</sup>.

Jamii za mwanzo za Kiislamu huko Awdaghust, Ghana, Tadmekka Gao, na bila ya shaka miji mingine katika mto Senegal, au sehenu za ndani za Delta ya Niger ni za kipindi hiki; ile ladithi maarufu kuhusu kusilimu kwa mfalme wa Mallal labda pia ihusishwe na wakati huu.

Wamoravi walichukua dhima yao kama waleta mabadiliko na walimu wa itikadi ya Kisunni kwa makini sana. Hawakuanzia mwanzo kabisa lakini mabadiliko huko Salaria kusini yaliyotokana na kutamalaki kwao bila shaka yalikuwa nakubwa na yalichanganyika na mapigano ya jumla ya madhehebu ya Kisunni ya karne ya kumi na moja yaliyofuatia ushindi wa Kishia wa karne iliyotangulia. Ni kutokana na usuli huu ndio yawezekana kutathmini mahusiano na Ghana.

Ghana iliingia rasmi kwenye Uislamu mwisho wa karne ya kumi na moja ama kwa njia ya kutamalakiwa au kwa kuongolewa katika Usunni wa Kimaliki. Ushahidi wa kiakiolojia kuhusu maangamizi ya Ghana si kamili, ingawa huko Kumbi Saleh masalia ya kile ambacho pengine ndiyo maangamizi yake yameonckana chini kabisa ardhini, katika kina kipatacho mita tano chini ya ardhi hivi sasa. Vipimo vya msikiti vilibadilika baada ya mwisho wa karne ya kumi na moja na mji mkubwa wa soko katika sehemu hii ulikuwa wazi katika karne ya kumi na tatu na kumi na nne. Viashirio hivi vinaonyesha kwa kiasi fulani kwamba Ghana iliingamizwa na Wamoravi ambao hawakuwa na sababu ya kuwanusuru maadui wao wa Kizanata waliokuwa hapa kuliko wale waliokuwa huko Awdaghust. Lakini uthibitisho kamili bado haujapatikana: na kwa vyovyote vile, kama ilivyokuwa huko Awdaghust, uvamizi kama huo, kama kweli ulitokea, haukusababisha kutoweka kwa mji wa soko, bali kinyume chake. Akiolojia bado ina maswali kadha ya msingi ya kujibu kuhusu jambo hili.

Kama kulikuwa na mapambano, je makao makuu ya kifalme yalifikwa na nini? Makao makuu hayo yaliamishwa kusini zaidi au nayo yalipokea Uislamu? Mahusiano ya baadaye na sehemu ya jirani ya Soso kwa upande wa kusini yalikuwa vipi na ni nani kwa mujibu wa matini ya karne za kumi na nne na kumi na tano walioislinda na kuidhoofisha Ghana? Hivyo, kwa wakati huu, hatima ya 'mfumo wa Ghana' iliyoungana na Delta ya Ndani, kwa kiasi kikubwa, hatuelewi na hili ni jambo la kusikitisha<sup>7</sup>.

Harakati zenye sura za kivita ambazo yawezekana ziliathiri Sahel wakati huo pengine zilikuwa ndiyo sababu ya kukaliwa na kukaliwa tena kwa sehemu muhimu katika eneo la ndani la delta ya Niger na vile vile makazi ya Telleni katika sehemu kongwe za Tolloy katika majabali ya Bandiagara. Baadhi ya waandishi hata wanafikiri kwamba kidogo kidogo mabadiliko yalifika eneo la Chad, lakini jambo hili halielekei kuwa kweli.

Wana wa kifalme wa Gao walikuwa Waislamu tangu nyuma huko katika karne ya kumi. Dalili za uhusiano na Hispania ya Wamoravi, ambao pia ni mgumu kuufafanua, zilijitokeza mwishoni mwa karne ya kumi na moja. Mawe ya makaburi ya kifalme yamepatikana katika

6 Taz. Sura 3 ya juzuu hili.

7 Taz. Sura 14 ya juzuu hili.

kiunga cha Gao-Sane upande wa Kaskazini mwa Gao. Mawe mawili ya zamani kabisa miongoni mwa mawe haya huenda yakawa yamechongwa kutokana na marmar za Kihispania: yalihusiana na wafalme ambao bila shaka walikuwa Waislamu na pengine wa madhehebu ya Kisunni. Kwa wakati huu taarifa juu yao ni ndogo.

Hatujui pia matokeo hahisi ya juhudi za Abu Bakr za kuisilimisha Sahel. Tarehe na mahala pa kifo chake vinahitilafiana sana kulingana na vyanzo. Ni dhahiri maelezo thabiti ya mwisho bado hayajapatikana; na historia ya Wamoravi bado imeficha mapya mengi hata kuhusu mambo ya wa dini; kwa mara ya mwanzo milki ya Kisunni iliyoshikamana ilijitokeza na msimamamo mmoja wa jumla, na kuwa ndiyo mpaka wa dar-es-islam dhidi ya ulimwengu wa watu weusi wenye dini nyngine.

### *Muundo wa eneo lililotanda kutoka Ebro mpaka Senegal - kushindwa kwa Wamoravi*

Uchumi wa sehemu ya Kaskazini ya milki ya Wamoravi tayari ulikuwa ukicendeshwa kwa taratibu za hali ya juu kabla ya kutamalakiwa na Wasanhaja. Kuanzia wakati huu na kuendelea, uchumi huo ulinufaika kutokana na kumiminika kwa dhahabu kutoka Afrika Maghribi. Kwa muda mrefu sana wakati huu, watu wamekuwa wanaandika kwamba utamalaki wa Wamoravi ulivuruga mwambao wa upande wa Maghribi ya Afrika. Kinyume chake, maendeleo ya utafiti katika miaka ya karibuni yameonyesha kwamba maeneo ya Sahel wakati huo yalikuwa yameunganishwa kwa kiwango cha juu na uchumi wa sehemu za Kaskazini. Kuanzishwa au kuimarishwa kwa vituo vipya katika njia zilizoungana baina ya Senegal na Moroko kunaonyesha kwamba sehemu hizi zilitumiwa na misafara mingi. Hivyo mwambao mrefu wa Atlantiki uliunganisha nchi zenye uchumi uhohusiana lazima utazamwe kwa msingi wa mambo yote ya kiuchumi. Hivyo mahitaji ya bidhaa 'kutoka kusini' katika hali yoyote yaliongezeka hadi katikati ya karne ya kumi na mbili. Kudumishwa kwa umoja huu wa kiuchumi kwa hakika, hakukuziwa kuwoko kwa tawala mbili, mmoja huko Marrakesh na mwingine huko Sahel; majeshi mawili, moja kusini, likitegemea ngamia, na jingine likitegemea farasi tu tangu mwisho wa karne ya kumi na moja; na pengine hali mbili tofauti za kisiasa. Lakini kuwoko kwa umoja wa uchumi kunathibitishwa na vyanzo. Moroko ya kusini ilinufaika sana kutokana na ufanisi huu. Al-Idrisi ameelezea kwa ufasaha kuongezeka kwa mali katika Aghmat-Warika, ambayo wakazi wake walikwenda kwenye nchi ya watu weusi na misafara iliyobeba shaba nyekundu, shaba nyeupe, mabulangeti, nguo za sufi, vilemba, majoho, vigae, shanga, vito vya thamani, kombe za lulu, viungo vya kila aina, uturi na chuma kilichonakishiwa. Aghamat haikuwa peke yake katika ufanisi huu wa kiuchumi. Sehemu yote ya milimani ya Moroko ilitoa kiasi kilichoongezeka cha chuma na fedha kwa ajili ya kusafirisha, na katika karne ya kumi na mbili kulikuwa na mapigano hasa kwa ajili ya kudhibiti migodi baina ya wale waliowaunga mkono Wamohadi na wale waliowaunga mkono Wamoravi. Machimbo katika eneo la Chichawa, Maghribi ya Marakesh, yameonesha maisha ya ufujaji katika zama za Wamoravi: mapambo ya aina ya 'stucco' na mapambo nakshi yaliyotiwa rangi yanafaa kulinganishwa na yale mengine yaliyoonekana katika sehemu za Kaskazini na kusini.

Ufanisi wa kiuchumi, ambao kwa hakika ulizifikia baadhi ya jamii za mijini na wale watu waliokuwa karibu na watawala, ni wazi ulichangia maendeleo ya hali ya anasa ambayo wakati mwingine ilikuwa ya mikogo iliyoshutumiwa vikali na Wamohadi. Hakuna mji ambao



13.3 Sarafu za dhahabu za Walmoravi. (Hatimiliki ya picha: Bernard Nantet)

umewahi kutoa masalia muhimu kuliko Marrakesh, mji ambao unaonyesha mpango asilia wa mji wa Wamoravi. Al-Idris anatupa picha ya kuvutia kabisa ya mji huu wakati ulipojengwa, akitaja hasa kasri ya 'Emir wa Waislamu', Ali ben Yusuf ibn Tashfin ambayo ilijulikana kwa jina la *Dar al Hajar* (nyumba ya mawe). Akiolojia imefanya iwezekane kuipata Kasri hii, jengo ambalo lilikuwa 'maajabu ya sanaa ya majenzi' katika eneo hili kwa wakati uliohusika na imefanya pia iwezekane kuiunda tena sehemu ya ramani ya msikiti ya Wamoravi na kufunua kabisa chemchem iliyonakishiwa vizuri kabisa ambayo walipewa wakazi wa hapo kwa ajili ya kutawadhia. Kikomo cha Kaskazini kabisa cha mapambo ya fahari ya Wamoravi kilikuwa huko Hispania, kwenye Ebro, katika Aljaferia huko Saragossa: hakuna kilichobaki hapo sasa isipokuwa sehemu tu za matao.

Marrakesh pia ilikuwa kituo maarufu cha uandishi ambako washairi wa kasri ya mfalme kutoka Hispania waliendeleza shughuli zao zilizoanza chini ya *reyes de taifas* lakini zikavurugwa kutokana na utamalaki wa al-Andalus na Wamoravi na ukali ulioandamana nao awali. Ukali huu wa mwanzo ambao mathalani ulimjaza al-Bakri wasiwasi mkubwa kuhusu Wamoravi mwishowe ulilainika kwa upande wa tabia na vitendo. Hii ilikuwa ndiyo mara ya kwanza kwa utamaduni wa hali ya juu wa Kiislamu kupandikizwa Moroko kwa kiwango kama hicho. Pamoja na utamaduni huu, yalikuja mambo ya anasa na kupenda maisha ya raha sana ambayo yaliwafanya Wamoravi walaumiwe na maadui zao. Lakini ukali wa kisharia wa *wafukaha* walioshirikiana na nasabatawala, ambao mara nyingi ulitofautiana na hali huria ya maisha ya raha huko Marrakesh, ulikuwa bado haujatoweka: ulilazimisha mateso kama ya Usunni wa Kimaliki - jambo ambalo lina umuhimu mkubwa kwa historia ya Uislamu wa Maghribi, ukiwemo Uislamu katika Afrika - lakini pia uliibua chuki pale ulipoyuka kiwango.

Uadui ulioibuka huko Hispania na Moroko kutokana na sera finyu ya *wafukaha* wa Kimaliki na chuki yao dhidi ya fikra zozote mpya lazima ulikuwa mkubwa. Waliyashambulia hasa maandishi ya al-Ghazali, ambayo wakati luo yalikuwa yameingizwa huko Maghribi, na ambayo mitindo yake ya kimafumbo iliwaliza sana *wafukaha*, ambao waliwaunga mkono Wamoravi. Hali katika miongo ya mwisho ya utawala wa Wamoravi iliharibiwa na hatua za ukandamizaji zilizochukuliwa na wanasharia wa Kimaliki ambao waliwaunga mkono wana wa mfalme. Ukandamizaji huu ulizipa nguvu zile lawama zilizoelekezwa kwa nasabatawala, hasa na vuguvugu changa la Wamohadi.

Moja katika sababu za kuanguka mapema kwa nasabatawala wa Wamoravi, ni udhaifu wa utawala wao. Utawala huu ni kama haukuwepo kabisa katika ngazi za chini ambako madaraka yaliendesha kupitia kwa ndugu na wateja. Kwa zaidi ya mara moja vile vitendo viovu vilivyoshutumiwa dhidi ya watawala wa al-Andalus katika miaka ya mwanzo ya uadilifu mara vilichomoza tena, hasa kuhusu utozaji kodi. Ukali ulioonyeshwa katika mambo ya kisharia na katika taratibu za upelelezi hauwezi kuficha ugeugeu fulani wa kidini na uasi uliokuwa ukitokea mara kwa mara. Kile ambacho ndicho kilichokuja kuupeperusha nasabatawala kilianza huko Atlas, na serikali ya Wamoravi haikuweza kufanya lolote isipokuwa kukidhibiti kwa muda mrefu kama ilivyowezekana. Silaha ambayo Yusuf ibn Tashfin alitumia dhidi ya *reyes des taifas* katika mwisho wa karne ya kumi na moja ilitumika dhidi ya Wamoravi ambao sasa walituhumiwa kusababisha madhila, dhuluma, rushwa na ufuska, na pia kutetercka katika dini. Vyombo madhubuti vya dola vya Wamoravi vilishindwa kuhimili mashambulizi ya Wamohadi yaliyokuwa makali na yaliyoandaliwa vyema kutoka katika vituo vyao vya milimani.<sup>8</sup>

8 Taz. Sura 2 ya juzuu la IV.



---

Historia, kwa muda mrefu imewakamia Wamoravi, ambao wameshutumiwa kwa kila kosa linalowezekana, na vile vile kushukiwa kuwaingilia kama 'washenzi' huko Hispania, ambako maridhiano kati ya Waislamu na Waukristo yalifikiwa kwa msingi wa kulazimishwa kujitoa. Walivuruga maslahi mengi mno kwa mashambulio yao kusameheka kwa urahisi, na waliingiza nyuso nyingi mno mpya, zikiwemo nyeusi, kuweza kuepuka chuki na kutoaminika. Litakuwa jambo la kuvutia katika miaka ijayo kufuatilia taratibu za kuirejesha heshima nasaba hii tawala, - kazi ambayo tayari imeanza, na utafutaji wa tathimini ya haki ya dhima yake ya kihistoria.



## *Biashara na njia za biashara katika Afrika Maghribi*

Katika miaka ishirini iliyopita utafiti umebadili kwa kiasi kikubwa msingi wa habari utumiwao katika kulitali somo hili. Matokeo yake ni kwamba takribani kila kazi iliyofanywa hivi karibuni imeyatilia shaka magunduzi yote yaliyopatikana hapo awali na ambayo katika miongo miwili iliyopita yalikuwa yakikubaliwa vivi hivi tu pasi na kusailiwa.

Kuwepo kwa uchumi wa biashara ya ndani ulioegemezwa kwenye ubadilishanaji wa bidhaa za walaji au bidhaa zilizotengenezwa nchini katika Afrika na kwingineko ni jambo ambalo kwa ujumla inakubalika kuwa lilikuwepo tangu zamani; na kwa hakika lipo pia katika kipindi chetu. Hili haliathiri mada ya sura hii moja kwa moja. Uchumi wa biashara ya masafa marefu ambao ulihusisha wafanyabiashara ulitegemea kuwepo katika masoko ya walaji kwa mahitaji ya bidhaa adimu na ghali (kama vile chumvi, kola, dhahabu, ngano, nguo na kupri (shaba) ambazo ilibidi zitoke (kwingineko). Mahitaji mapya ya bidhaa mpya yangeweza kuanzishwa kati ya wafanyabiashara wa masafa marefu kwa kutumia njia za biashara zilizokuwepo. Biashara ya hatari na ya masafa marefu sana iliweza kuanzishwa tu iwapo ilikuwa ya mahitaji makubwa sana.

### *Sahara, Ghuba ambayo imepanuka tangu kipindi cha neolithi*

Biashara ya eneo lote la Sahara haikubakia hivyo hivyo siku zote. Iliinukia, ikakua na ikapata mabadiliko makubwa ambayo twahitaji kuyatalii kwa kadri tuwezavyo.

Ama kuhusu biashara hii karne ya saba hadi karne ya kumi na moja zilikuwa zenye umuhimu mkubwa. Ni katika kipindi hiki ambapo kulikuwa na mahusiano ya mara kwa mara ya uchumi wa Mediterania, ikiwa ni pamoja na mahitajio yake, hasa ya dhahabu, na uchumi wa Sahel ya Sahara na savana ulioiunganisha na ukanda wa msitu uliotumia chumvi lakini ambao haukuizalisha kwa wingi. Lakini kwa muda mrefu sasa kumekuwa na mjadala mrefu kuhusu ni lini hasa maingiliano haya yalianza kuwepo.

Tukiacha sehemu chache adimu ambapo vizingamvua (*isohytes*) vya Kaskazini na kusini vya mm 50 vimekaribiana sana, kulivuka jangwa la Sahara kunahitajia ama kuwepo kwa visima na oasisi za kuaminika au vinginevyo kusafiri kwa njia ya wanyama wasiohitaji maji mengi na kwa kubeba kiasi cha kutosha cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu. Uvukaji huu wa jangwa ni wa hatari na hufanywa tu inapokuwa kuna sababu za kutosha.

Ugunduzi huu, ambao kwao watafiti wote siku hizi wanakubaliana, unaifanya mjadala ya zamani juu ya safari kuu za uvukaji Sahara katika siku za zamani kabisa kuwa zoezi la



kitaaluma tu. Na hata kama hapo baadaye itathibitishwa kwamba safari hizo zilifanyika kweli, kule kuwepo kwa umbali mkubwa kati ya kingo za jangwa hili kulizifanya safari hizi kuwa ngumu au kutowezekana hadi kufikia mwisho wa Kipindi cha Kale<sup>1</sup>.

Katika karne ya tano na ya sita Waberiberi ndio waliotakadamu kujaribu kulivuka jangwa, hasa kutokana na kuenea kwa ngamia. Huyu ndiye mnyama pekee ambaye angewezesha kufanyika kwa misafara mirefu ya kati ya kilomita elfu moja au mbili kati ya kingo mbili za Sahara. Biashara ya masafa marefu, ngumu na nzito kama hii, isingewezekana kufanywa kwa kutumia magari ya farasi (ambayo haisadikiwi tena kuwa yalitumiwa kwa shughuli za kibiashara), farasi (ambao ndio mwanzo walikuwa wameletwa katika Sahara), punda (wanyama wa maeneo haya wa zamani ambao hawakuhitaji chakula kingi) au wale maksai wenye nguvu ambao mwendo wao ulikuwa wa taratibu sana na ambao picha zao zilionekana katika sanaa ya miambani.

Swali jingine lilikuwa ni njia ipi ya biashara itumiwe ili kuepuka hatari. Taabu walizopata waandishi wa Kiarabu wa karne ya kumi na moja na kumi na mbili katika kueleza kwa undani habari za njia za biashara ya eneo lote la Sahara zinaonyesha kabisa kwamba njia zozote za kujibunia tu bila kufuata njia maalumu za misafara zingeweza kuwa za hatari. Wakati mwingine imesemekana pia kuwa kulikuwa na njia ya pwani, lakini utafiti wa hivi karibuni umeonyesha shida na hatari ambazo zingeweza kutokea kwa kutumia njia hii: kati ya latitudo 26° na 24° Kaskazini, eneo la pwani ambalo halikaliki kabisa halionyeshi mabaki ya aina yoyote ya kuwepo kwa binadamu, hata wakati wa kipindi cha neolithi.

Mashariki zaidi, katika eneo ambalo sasa linafahamika kama Mauritania, usafiri ulikuwa rahisi zaidi kwa sababu vizingamvua vya mm 50 vya Kaskazini na kusini vilikaribiana zaidi: hili ndilo eneo ambalo baadaye lilijulikana kama Azuki. Mashariki zaidi ya hapo kulikuwa na bonde la Saura na Kaskazini kulikuwa na Gurara na Tawat, maeneo ambayo baadaye kidogo yaliwavutia sana wanamisafara. Umuhimu wa pekee wa njia hii ulikuwa ni kufanywa kwake kuwa mojawapo ya vituo vya wasafiri vilivyokuwa vikitumiwa sana na misafara kuanzia karne ya ishirini na kuendelea. Aidha kwa upande wa mashariki zaidi ilikuwa lazima kwenda Wargla, katika Mzab, na kuelekea upande wa kusini hadi Adrar des Ifoghas na bonde la Tilemsi ili kupata njia rahisi kama hiyo tuliyotaja hapo juu.

Inaweza kukadiriwa kuwa hatua ya kwanza katika uelekeo wa mahusiano na *Bilad al Sudan* inaanzia katika nusu ya pili ya karne ya nane, japokuwa mahusiano haya hayakuwa yameshamiri mpaka ilipofikia karne ya kumi. Ingawa Waberiberi walikuwa watu wa kwanza kujaribu safari za kuvuka Sahara, kuanzisha kwao biashara za mara kwa mara kulihitaji vivutio vya kiuchumi na nia thabiti ya watu wenyewe; 'mazingira asili' peke yake hayakutosheleza kusababisha kuanzishwa kwa njia za misafara.

Nafasi ya Wagaramante katika kadhia ya biashara mpaka sasa imebakia kuwa jambo lenye ubishi mwingi. Lakini inaelekea kwamba kulikuwa na biashara kati ya Fezzan na Chadi, na inaelekea pia kwamba Kavar iliwauzia watu wa kusini chumvi. Hata hivyo hatujaweza bado kutoa ruwaza ya biashara yoyote ambayo inaweza kuwa ilifanywa na watu waliokuwa wakiishi kusini mwa Chad, ingawa inawezekana kulikuwa na njia toka Chad kwenda Tripolitania iliyotumiwa katika kusafirishia watumwa katika zama za kale.

Kadiri tunavyozidi kuusogelea mto Nili ndivyo mtandao wa njia unavyozidi kuwa wa muda mrefu kwenye mto huo na kwenye njia sambamba nao katika upande wa Maghrib

1 Taz. Sura 20 ya juzuu la II

kwenye mlolongo wa oasisi. Pia kulikuwa na mahusiano ya kimashariki - Maghribi baina ya oasisi hizi na mto. Vizuizi vya Unubi vilifanya iwe vigumu kwa Waislamu wa Misri kuingia Chad moja kwa moja kwa kupitia Darfur. Hali hii iliendelea kuwapo hadi karne ya kumi na nne - hali ambayo ilikuwa na umuhimu mkubwa sana kiuchumi. Njia pekee iliyokuwa wazi ilikuwa ile ya zamani, kuanzia Nili hadi kwenye oasisi ya Siwa. Mbele zaidi njia hii ilipitia oasisi ya Kufra, pengine ikapita Kavar kuanzia mashariki hadi Maghribi, ikipitia al-Kasaba na kufikia Maranda (Marandet) na Gao.

Al-Yakubi anazungumzia kuwepo kwa njia hii katika karne ya tisa kijuujuu, lakini akitumia wakati uliopo. Karne moja baadaye Ibn Hawkal alisema kuwa njia hii iliachwa kwa sababu ilikuwa ya hatari sana. Maelezo ya Ibn Hawkal yanaonyesha msigano mkubwa na maelezo yaliyotangulia. Yeye alichukulia njia ya 'Misri' kuwa njia iliyokuwa inakufa, lakini pia hakutilia maanani mahusiano yaliyokuwepo baina ya maeneo ambapo Waibadi na Wasudan waliishi; yeye alizingatia zaidi njia ya Wafatimi kutoka Sijilmasa hadi Ghana. Tena basi, yeye anasema wazi wazi kuwa njia hii ndiyo iliyokuwa ikitumika sana wakati wa 'kipindi chake.'

Hii yafaa iwe onyo kwetu kwani kila kitu kilichohusu maelezo ya njia hizi ni cha kisiasa na kinatokana na uchaguzi wa mwandishi. Hata hivyo kutozingatia kwa Ibn Hawkal njia ya Misri pengine hakukutokana na masuala ya itikadi na siasa tu bali yawezekana kulitokana na mabadiliko makubwa ya kiuchumi kati ya karne ya tisa na karne ya kumi.

### *Maisha katika ukanda wa Sahel kama yanavyoonyeshwa leo na utafiti wa kiakiolojia*

Utafiti wa hivi karibuni juu ya chuma na shaba katika Afrika Maghribi wenyewe unatosheleza kufanya yatiliwe shaka mawazo mengi yaliyopatikana kuhusu nyakati kabla ya majilio ya Ukristo. Katika kipindi kabla ya safari kuu za kibiashara kuvuka Sahara bidhaa hizi mbili muhimu ziliuzika katika masafa marefu kusini mwa jangwa bila ya msaada kutoka Kaskazini.

Tukiacha athari kutoka ng'ambo ya Sahara, katika karne za sita na saba machimbo ya uvumbuzi yameonyesha kuwa kulikuwa na harakati katika bonde la Senegal na katika nusu ya kusini ya nchi hiyo. Harakati hizo pia zilikuwepo kuanzia sehemu za Nyani hadi Tondidaru, kando ya mabonde ya Niger mpaka kufikia viunga vya nchi ijulikanayo leo kama Nyamey. Maranda, lfe na maeneo mengine katika Ivory Coast pia huonyesha kuwepo kwa harakati kubwa za namna hiyo. Maisha ya jamii yaliyoandamana na shughuli za ufuaji madini, mgawanyo wa kazi na biashara yalikuwa yakiendeshwa katika Sahel kabla ya ishara zozote za kujitokeza kwa biashara kuu ya Sahara. Sasa tunaweza kusema pasi na hofu ya kukosolewa na utafiti wa baadaye, kwamba muundombinu mzima wa makazi na maisha ya kiuchumi katika mabonde ya Senegal na Niger, na bila shaka hata kusini zaidi, ulikwishakuwepo katika karne hizi za giza.'

Tamaduni muhimu za Kisahel sasa zinafululiwa na utafiti; tamaduni ambazo wafanyabiashara kutoka Kaskazini walikutana nazo. Kuhusu vipindi kabla ya karne ya saba sehemu za Tondidaru, Jenne-Jeno na Bandiagara zimetoa matokeo makubwa sana kuhusiana na biashara ya shaba na chuma katika delta ya ndani ya Niger. Eneo la Sintiu Bara, ambako vitu vilivyopatikana huko havijachapishwa kwa ukamilifu bado, limetoa vifaa vya shaba nyeusi vya kuvutia sana. Ama kuhusu karne ya nane na ya tisa, Tegdust imetoa mabaki mengi ya kazi za ufuaji wa madini yaliyochanganyika na shaba, mojawapo ya mali ghafl ambazo

pengine zilitoka Akijujit. Huko umepatikana ushahidi wa mwanzo kabisa wa kiakiolojia wa matumizi ya kalibu ya *cire perdue* (njia mojawapo ya kuyeyushia madini na kuyafanya yawe na umbo maalumu) katika vipindi hivyo vya mwanzo. Hapana shaka kwamba njia hii ya ufuaji madini kienyeji ilikuwa na dhima ya kikanda katika masuala ya uchumi tangu zamani.

Ndiyo maana siku hizi kila kitu kinaonyesha kwamba jamii ambazo watu wa mashariki waliwasiliana nazo kupitia Sabara zilikuwa na mshikamano na mifumo mizuri; zikiwa na miji na vile vile uwezo wa kufanya biashara hata ya masafa marefu. Tena basi kwa upande wa ufanyaji biashara ni muhimu kutambua kwamba mtandao wa biashara ya chumvi pengine ulikuwepo kuanzia kipindi hiki.

### *Hali ilivyokuwa kaskazini mwa Sahara*

Kwa madhumuni ya haja zetu inatosha kutaja tu zile sifa zinazoweza kusemekana kuwa muhimu kwa historia ya uchumi na historia ya mahusiano ya kuvuka Sahara.

Katika nchi ijulikanayo sasa kama Moroko, kuna maeneo mawili yanayotuhusu: eneo la Sus, lililo kati ya Atlas na eneo linaloelekeana na Atlas, ambalo tangu zamani lilikuwa na sifa ya nchi yenye na utajiri; na eneo la Tamdukt, lililojitokeza kama kituo cha mwisho cha njia za kuelekea kuaini. Maeneo mengine yaliongezeka kwenye pande zote mbili za Atlas na katika bonde la Dara hadi kufikia karne ya kumi. Katika upande wa Sahara wa Atlas ya Kati, Sijilmasia ilianza, hasa katika nusu ya pili ya karne ya nane, kuwa kama bandari ya misafara kwa ajili ya mawasiliano na kusini.

Baada ya Waberiberi kutulizwa na hasa katika kipindi cha Waaghlabi, Ifrikiya ilianza kupata umuhimu mkubwa zaidi. Jambo lenye kutuvutia mno hapa katika muktadha wa mawasiliano ya kuvuka Sahara ni kule kuwepo kwa sarafu yao ya dinari. Itabidi kujiuliza kama sehemu kubwa ya dhahabu hii ilitokana na kutamalakiwa kwa Sisilia au kama ililetwa kutoka *Bilad al Sudan* mnamo karne ya tisa, na bado kuna mjadala mkubwa miongoni mwa wanahistoria kuhusu suala hili. Katika mitaala yake juu ya Waibadi, T. Lewicki amesisitiza kwamba kulikuwa na vikwazo vya kiitikadi na kisiasa dhidi ya mipenyo ya Waaghlabi kuelekea kusini. Lakini ingawa Waibadi walihodhi safari katika njia za Sahara, hawakukataa kuwauzia dhahabu magavana wa Kayrawan. Kwa sasa haiwezekani kujua kwa yakini ni mahusiano gani ya kiuchumi yalikuwepo kati ya Ifrikiya na Afrika Maghribi katika karne ya nane na karne ya tisa, au kama Waaghlabi walikuwa na sera thabiti juu ya suala hili. Yaweza tu kuchukuliwa kwamba Waibadi wenyewe walijaribu wakati huo kuandaa mawasiliano ya kawaida kuvuka Sahara. Kuwepo kwa dhahabu Ifrikiya kunadokeza jambo hili na uhakika kwamba kulikuwa na mahusiano baina ya Tahert na Gao hupatia nadhariatete hii mashiko zaidi. Hivyo Tahert pakawa mojawapo ya njia muhimu katika mawasiliano ya kawaida ya mwanzo ya kuvuka Sahara tunazozijua. Mawasiliano haya yalikuwa baina ya miji hii na Gao, siyo Ghana, na itakuwa vema kudadisi ikiwa wafanyabiashara wa Tahert hawakujaribu kupeleka Gao chumvi ambayo watawala wake walihodhi na kisha kuiiza tena.

Hivyo, kwa wakati huu, kuhusu karne ya nane na ya tisa, tunabakiwa tu na nadhariatete juu ya kuanzishwa kwa vile ambavyo baadaye ilikuwa viwe vituo vya mwisho vya Kaskazini vya biashara ya kuvuka Sahara (Tamdukt, Sijilmasia, Tahert, Wargla na miji ya Jarid), na vile vile maandalizi ya awali ya misafara ya kuvuka Sahara. Matukio muhimu ambayo yalisababisha kuwepo kwa biashara za kawaida za kuvuka Sahara yalitokea katika kipindi cha kati ya 850 na 950.

Swali muhimu la kujiuliza ni: je vitu gani vingepatikana kutoka upande mwingine wa jangwa? Kwa upande wa kusini jibu pengine ni vitu vichache sana! Chumvi ingawaje haikuwa nyingi sana ilikuwa ikipatikana kwa kiasi cha kutosha kutokana na mbinu mbalimbali za uzalishaji na vituo vya ukusanyaji na uzalishaji.

Amma kwa hakika, ingawa ni kweli kwamba kulikuwa na tofauti kubwa sana baina ya bei ya chumvi iliyogazwa kutoka Kaskazini na ile iliyokuwa ikiuzwa kwenye eneo la Mediterania, kuna mambo ambayo hayana budi kuwekwa wazi zaidi. Waandishi wengi wa Kiarabu husisitiza umuhimu wa Awlil kama mgodi mkuu wa chumvi kusini mwa Sahara. Chumvi iliyotolewa huko ambayo ilisafirishwa kwa mashua kwenye 'mto Nili' (mto Senegal na mto Niger) ilifika katika sehemu zote za Nchi ya Weusi. Kila kitu katika maelezo ya waandishi hawa kinaonyesha kwamba wafanyabiashara kutoka Kaskazini, ambao awali walikuwa wateja wa Awlil, walipokuwa wanaondoka katika mgodi huu walilazimika kupitia Awdaghust kabla ya kugundua polepole namna ya kufupisha njia hii kwa kutumia akiba ya chumvi iliyowekwa kwenye njia ya Kaskazini - kusini katikati ya Sahara. Halikadhalika, sehemu ya kusini haikuhitaji shaba zaidi (kinyume na fikra iliyokuwepo miaka 20 iliyopita) au chuma ambacho tayari kilikwishakuwa kinazalishwa hapa na pale, lakini kwa kiasi kinacho-tosheleza. Mahitaji yoyote yaliyokuwepo yalikuwa ya kutoka Kaskazini kuliko kusini.

Kuhusu Afrika Maghribi na kipindi chetu mahitaji ya watumwa pengine yametiwa mno chumvi. Claude Cahen alionyesha katika mwaka 1964 kwamba kwa jumla biashara ya watumwa haielekei kama ilileta faida kubwa lakini kuingizwa kwao kutoka nje kulikuwa ni lazima kwa ajili ya ufanisi mkubwa wa uchumi kwa jumla uliohitaji na kuruhusu ajira ya wafanyakazi ambao walipatikana kwa urahisi mno kupitia biashara ya watumwa. Kwa namna hii misafara ya watumwa ilikuwa ya mtiririko thabiti, lakini pengine haikuwa kichocho kikuu cha uchumi; na hivyo haiwezi kutumiwa kueleza biashara ya kuvuka Sahara.

Kwa hivyo tunarejeshwa nyuma kwenye zao ambalo limezungumziwa na waandishi wote wa Kiarabu na ambalo wanahistoria wote wamezingatia, yaani dhahabu. Ulimwengu wa Waislamu, uliokuwa na watumiaji wa kutosha wa dhahabu hasa kuanzia wakati wa mabadiliko mwishoni mwa karne ya saba, ulijiendesha kulingana na utashi mkubwa wa madini haya pembezoni mwake. Sehemu ya Maghribi ya Kiislamu, isipokuwa Ifrikiya iliyokuwa chini ya Waaghlabi, haikutengeneza sarafu za dhahabu kabla ya karne ya kumi. Lakini kuanzia karne hiyo na kuendelea sehemu hiyo ilianza kutumia sarafu za dhahabu kwa wingi. Pia ni katika kipindi hiki ambapo habari kuhusu uzalishaji wa dhahabu katika Afrika zilianza, angalau kwa kiasi fulani, kuwa yakinifu zaidi kijiografia.

Wakati wakiandika habari juu ya dhahabu ya Afrika Maghribi waandishi wengi wa Kiislamu hutumia neno *tibr* ambalo mara nyingi hutafsiriwa kama 'ungaunga wa dhahabu.' Lakini kwa hakika neno hili lina maana ya 'dhahabu ya asili isiyofuliwa wala kutiwa madawa', yaani dhahabu ambayo ni ghafi bado, tofauti na ile ambayo imekwishasafishwa (kwa kiarabu *dhahab*). Ni kwa kuzingatia tu maana hii halisi ya neno *tibr* ndipo tunapoweza kuyafasiri kwa usahihi matini mengi yanayoongelea aina hii ya dhahabu katika Afrika Maghribi.

Katika muktadha wa *Bilad al Sudan*, neno *dhahab* polepole liliachwa na nafasi yake kuchukuliwa na neno *tibr*. Kwa muda mrefu *tibr* huenda ilikuwa na maana ya *dhahabu* ya Afrika Maghribi katika umbo lolote ilimokuwa (yaani kama chembechembe, ungaunga, vibumba au vipande- vipande) na bila kujali asili zake za kiuchumi na kijamii kama dhahabu yenye ubora mahsusi ambayo hata bila kusafishwa ingeweza kutumiwa moja kwa moja kwa

kutengenezea sarafu. Dhahabu hiyo haikuhitaji 'kusafishwa' kwa sababu ilikuwa na taka kidogo sana na haikuwa na mchanganyiko wa aina yoyote ya madini. Ama kwa hakika uchunguzi katika maabara umeonyesha kuwa dhahabu hii ina madini ya fedha na asilimia ndogo ya shaba; na hii asilimia ndogo ya kupri (shaba) ndio hufanya iwezekane kuzitambua dinari zilizotengenezwa kwa dhahabu ya Afrika Maghribi.

Iwapo (kama ambavyo tunafikiri) ni kweli kwamba neno *tibr* (walau kuanzia karne ya kumi na moja na kuendelea) lina maana ya ubora wa dhahabu ya Afrika Maghribi, ambayo iliweza kutumiwa bila kuhitaji kusafishwa au kuchanganywa na madini mengine kwa ajili ya kutengenezea sarafu, basi hii yaweza kueleza ni kwa nini al-Bakr anasema dhahabu hii ndiyo nzuri kuliko zote duniani na vilevile, juhudi kubwa ya watu kuipata. Uchunguzi wa hivi karibuni katika nyaraka kuukuu za Genoa umethibitisha kwamba baada ya karne ya kumi na nne Wagenoa nao walielekea kulitumia neno *tibr* kuonyesha ubora wa dhahabu.

Vyanzo vya Kiarabu vinathibitisha kwamba katika Afrika Maghribi kulikuwepo na dhahabu iliyofuliwa; lakini ni dhahiri wale waliokuwa wakitawala kusini mwa Sahara, wawe Waislamu au la, hawakuwahi hata baada ya mwaka 1050, kutumia dhahabu hii kutengenezea sarafu. Hadi leo hii hakujawahi kupatikana, kuaini mwa jangwa, mabaki yoyote ya chapa ya chuma cha kutengenezea sarafu au mabaki ya kiwanda cha kutengeneza sarafu. Ukweli huu hutufanya tujiulize maswali muhimu sana katika uwanja wa historia ya uchumi. Tukizingatia namna dhahabu hii ilivyokuwa ikizalishwa katika maelfu ya fito zilizozagaa sehemu mbalimbali, je ingewezekana kuwa na matumizi ya moja kwa moja ya dhahabu kutengeneza sarafu huko kusini? Je, dhahabu hii hata kama ingetengenezwa katika sarafu za gramu nne nne, isingekuwa ina thamani kubwa mno kuweza kutumiwa kwa biashara ya ndani tu?

Kaskazini, hasa kuanzia karne ya kumi na kuendelea, utengenezaji sarafu uliokuwa ukifanywa na watawala likawa jambo la kawaida. Biashara ilijitokeza kulingana na mahitaji ya sarafu ya kila mwaka yaliyoamriwa na nasabatawala zilizokuwa zikitengeneza sarafu za dhahabu katika Afrika Kaskazini na baadaye katika Hispania; yaani Waaghlabi katika karne ya tisa; Wafatimi katika karne ya kumi; Waumayya wa Hispania, nao katika karne ya kumi; Wafatimi wa Misri baada ya 970; Waziri wa Ifrikiya na kisha Wamoravi.

Lakini mno ilikuwa hasa pale Wafatimi, Waumayya na kisha Wamoravi, walipoanza kujiingiza katika utengenezaji wa sarafu, kwa kiwango ambacho kitakuwa hakijawahi kutokea katika sehemu za Kiislamu za Maghribi, ndipo umuhimu wa biashara ya kuvuka Sahara ulipoanza kudhihiri. Mahitaji ya utengenezaji wa sarafu Kaskazini kila mwaka hayawezi kukadiriwa kwa usahihi sana, lakini yaweza kufikiriwa kwamba yalibadilika badilika yakikaribia au yakiwa katika kiwango cha juu kabisa cha tani moja. Kwa vyovyote vile, na hata tukitilia maanani mahitaji ya usonara, malimbikizo ya akiba na upoteaji wa sarafu uliotokea katika mwaka mmoja, ni vigumu kufikiria kwamba dhahabu iliyokuwa ikiagizwa kutoka nje ingeweza kuzidi uzito wa tani mbili au kuvuka tatu. Hili si jambo lisilowezekana, kwani ni kazi inayoweza kufanywa na ngamia wa mizigo wapatao 30-40 tu. Taarifa kutoka katika vyanzo vya Kiarabu hutoa picha kwamba tarakimu hizi ni za chini mno na kwamba misafara ilikuwa na ngamia wengi zaidi walau katika safari za kutoka, na idadi ilikuwa ikiongezeka kila siku. Kwa vyovyote vile tunakabiliwa na tatizo kubwa zaidi la kuokosekana uwiano kati ya uzito wa bidhaa ambazo zilikuwa zivushwe jangwani kutoka Kaskazini (na hivyo idadi ya ngamia katika safari ya kutoka) na uzito mdogo zaidi wa bidhaa wakati wa kurudi. Je, kiliwatokea nini ngamia wa ziada? Je, waliwiwa, au waliuzwa Sahel, jambo ambalo lingefanya idadi yao huko iongezeka kwa haraka? Kupungua sana uzito bidhaa kunaonyesha



si tu ushindani mkali wa kudhibiti njia za misafara na jinsi ulinzi wa njia hizi au utekaji nyara misafara ulivyokuwa wa lazima au wa manufaa, bali pia jinsi kila kituo cha mwisho cha Kaskazini cha mzunguko wa dhahabu hii kilivyohitaji kutembelewa mara kwa mara kila mwaka na wanamisafara wa Sahara ili kuweza kulinda hadhi ya sarafu yake. Halikadhalika sasa tunaweza kuelewa kwa nini Mansa Musa alipoleta takriban tani moja ya dhahabu Kairo hapo baadaye bei ya dhahabu ikaathirika vibaya. Itakuwa si jambo la busara kufikiria kwamba dhahabu nyingi sana ilitoka Afrika Maghribi kila mwaka.

Tunaweza pia kufanya makisio ya juujuu ya shughuli zilizowakilishwa na kiasi cha dhahabu kilichoweza kuuzwa nje kila mwaka, kikiongezewa pengine kiasi hicho hicho cha dhahabu kilichobaki, hasa tukikumbuka kwamba shimo moja lilitoa kati ya gramu 2.5 na gramu 5.0 za dhahabu. Hivyo kati ya mashimo 240,000 na 480,000, yalihitaji kuchimbwa kila mwaka yakionyesha mahitaji makubwa ya wafanyakazi. Hata kama tutaongezea kiasi kinachotokana na usafishaji dhahabu, ukweli unabakia kwamba shughuli hii, ambayo ilikuwa ya msimu tu, lazima iliwahusisha mamia ya maelfu ya watu katika Afrika Maghribi pale mahitaji yalipozidi kuwa makubwa na ya hakika.

Jc, ni lini ilipoanza misafara ya biashara ya kawaida ya kila mwaka iliyowauzia dhahabu Waislamu watengeneza sarafu?

Tunaweza kuondoa nusu ya kwanza ya karne ya nane ambayo ilikuwa na ghasia katika sehemu za Kaskazini, wasiwasi katika majaribio ya kulivuka jangwa, na mashambulizi ambayo huenda yalikuwa makubwa lakini yasiyokuwa na athari yoyote. Kwa upande mwingine, biashara ya namna hiyo inafikiriwa kwa dhati, kwa nusu ya pili ya karne ya nane na katika karne ya tisa, wakati Sijilmasa ilipoanzishwa au kuendelezwa. Tahert ikiwa imefikia ufanisi mkubwa, na biashara ya Waibadi ikiwa inakuwa. Yaelekea kwetu kwamba kipindi hiki yawezekana nacho kilikuwa cha biashara ya hatari na uoga bado, inavyodokezwa na matini za al-Yakubi au hata Ibin Hawkal. Machimbo ya Tegdausti, ambayo kwa hakika kubwa ndilo enco la Awdaghust ya kale, yametoa habari muhimu sana kuhusu kipindi hicho hicho, yaani karne ya nane na ya tisa, ambacho habari zijulikanazo juu yake ni kidogo mno. Vitu vilivyoagizwa kutoka Kaskazini vina umuhimu wa pekee, kwani, ingawa havijawa vingi, vinatoa ushahidi kwamba kulikuwa na safari za kuvuka jangwa. Vito vya thamani kubwa na ndogo na vifinyange vilivyong'arishwa vimekwishapati kana huko. Uchunguzi makini wa ithibati bado haujotoa mahitimisho ambayo ni chanya sana, isipokuwa baadhi ya vigae kutoka katika matabaka ya chini ya enco hili ambavyo vina asili ya Ifrikiya. Sasa tunajua pia kwamba vyombo vya kioo vilivuka Sahara. Hapana shaka kwamba tarehe ya tabaka ambako vilipatikana ni ya kabla ya miaka ya 900. Hapana shaka yoyote kwamba vyombo hivi ni ushahidi kamili wa kwanza wa kuwepo kwa mahusiano ya kuvuka Sahara katika karne za nane na tisa.

### *Maendeleo ya biashara ya kuvuka Sahara kuanzia mwaka 900 mpaka 1100*


Katika ulimwengu wa Kiislamu, kama ilivyokuwa katika mapokeo ya Kirumi, utengenezaji wa sarafu ulikuwa ni haki ya watawala ambayo iliwekewa sharia kali sana na watawala hao. Ukiritimba huu katika utengenezaji sarafu haukuhusika kwa namna yoyote ile na uhalali wa sarafu zilizotengenezwa, kwani amana zilizokubaliwa katika ubadilishanaji wa bidhaa zilitegemea makubaliano baina ya pande zilizohusika. Ni dhahiri ilikuwa ni kwa manufaa zaidi kutumia sarafu iliyoaminika kutokana na uhakika wa utengenezwaji wake.

Idadi ya viwanda vya utengenezaji sarafu za dhahabu katika kipindi kabla ya Wafatimi kushika madaraka ya utawala ilikuwa ndogo: kulikuwa na kiwanda kimoja huko Kayrawan kilichokuwa mkononi mwa Waaghlabi na kingine huko Misr-Fustat kilichoendeshwa na Waikhshidi. Katika kipindi hiki dhahabu ilikuwa haijapigwa chapa kwa wingi Hispania wala Kaskazini ya bara la Afrika. Ama kwa hakika Waumayya wa Hispania na Waidrisi wa nehi ambayo sasa yajulikana kama Moroko walitumia njia za kienyeji kupiga chapa *dirham* za madini ya fedha. Sera ya Wafatimi juu ya dhahabu ilibadili sana hali hii ya mambo: karne ya kumi ilikuwa ndiyo mwanzo wa viwanda vya utengenezaji sarafu katika schemu za ulimwengu wa Kiislamu ambako hapo awali hakukuweco na viwanda hivyo; vikiwa chini ya usimamizi mkali wa nasabatawala mbili kinzani, Wafatimi wa Ifrikiya na Waumayya wa Hispania. Wafatimi ndio walikuwa wa kwanza katika ulimwengu wa Kiislamu kuchukua ujasiri wa kupiga chapa ya Khalifa kwenye sarafu ya dhahabu wakishindana na mamlaka yaliyokuwa yakitambuliwa wakati huo, sarafu zao zilinuiwa kuonyesha nguvu na utukufu wa mamlaka mapya. Mahitaji ya Wafatimi ya dhahabu yalichochea na mambo matatu: itikadi, uhalisi wa kisiasa na uhalisi wa kiuchumi. Hivyo utengenezaji wao wa sarafu ulikuwa na umuhimu wa kipekee kabisa kwa historia ya mahusiano kiuchumi ya Kiafrika; yaani ulianzisha vita vya kiitikadi vya sarafu katika maeneo ya Kiislamu ya upande wa Maghribi ambavyo viliendelea hata baada yao.

Makhalifa walijishughulisha sana kutengeneza sarafu zenye ubora wa kiwango cha juu na hivyo kuweka akiba kubwa ya madini ya thamani na kuaminika kimataifa. Baada ya mwaka 953, na hasa baada ya 975, dinari zilizopigwa chapa ya Wafatimi, iwe huko Sijilmasa au Mahdiyya, zilitakiwa sana na wafanyabiashara hata wale wa kutoka sehemu za mbali kama vile Mashariki, kwa sababu ubora wake ulikuwa hauna kifani.

Wafatimi walijitahidi kwa kila hali kutoa sarafu nyingi za dhahabu kulingana na utashi ambao wao wenyewe walisaidia kwa kiasi kikubwa kuanzisha na ambao pengine haukuwa mno wa kiuchumi. Walihangaika kupanga safari za kila mwaka za biashara ya dhahabu kuvuka Sahara kwa namna ambayo ilikuwa haijawahi kutokea. Matokeo ya utafiti uliofanywa Tegdausti yamedhihirisha wazi ukweli huu. Vipimo vya kioo, vyote vikiwa ni vya asili ya Kifatimi, vimegunduliwa, baadhi yake katika mlalo wa kitabaka kiasi kwamba vinesaidia katika kukadiria umri wa eneo hilo. Kuwasili kwake katika eneo hilo kunalingana na kilele cha shughuli za uagizaji bidhaa kutoka nje katika mji huo na vilevile maendeleo yake ya kustajibisha. Kwa kuwa kila mara walipata shida kusafiri kupitia Wargla na Tadmekka - njia ya Waibadi kwenda Afrika ya watu weusi - Wafatimi walifanya njia ya Sijilmasa Ghana kama njia kuu ya kufikia dhahabu ya Afrika ya watu weusi kwa walau karne mbili na kama njia ya kusafirisha sarafu zao za dhahabu na ya kujengea hazina yao ya kivita. Kwa muda wote waliokaa Ifrikiya, baada ya kushindwa kwa Abu Yazid, walipiga chapa sarafu zilizozaminiwa na matajiri.

Mafanikio waliyoyapata mawakala wa Waumayya, baada ya kuondoka kwa Wafatimi kwenda Misri, kuelekezwa kwa dhahabu Hispania au walau upande wa Maghribi ya Maghrib, na kuhamishwa kwa kiwanda cha kutengeneza sarafu cha Sijilmasa kwenda kwa Waumaya, vyote vinaonyesha kwamba hadi kufikia mwongo wa mwisho wa karne ya kumi walionufaika na mfuriko wa dhahabu hawakuwa tena Wafatimi. Vipimo vya mwisho vya Kifatimi ambavyo vimewahi kupatikana Tegdausti sana sana ni vya baada kidogo tu ya mwaka 1000; pengine ni vya mapema zaidi. Hapana shaka kwamba dinari za Kifatimi zilizotengenezwa katika Ifrikiya zilikuwa na dhahabu ya Sudan, lakini hii si kweli tena



**14.3** Utengenezaji sarafu za dhahabu wa Almosavi mueneo ya kutengenezea fedha (J. Devise)

kuhusiana na dinari ambazo hao hao Wafatimi walipiga chapa huku Misri. Badiliko hili lilitokea mnamo mwaka 1047, wakati Waziri na Wafatimi walipotengana.

Kinachosemwa ni kwamba kila kitu kinadokeza kwamba upelekaji wa dhahabu ya Maghribi huko Ifrikiya ulikoma baada ya mwaka 990 na kwamba badiliko hili kubwa la njia za kusafirishia dhahabu lilikuwa na athari kubwa za kiuchumi kwa Ifrikiya.

Hata pale Waumayya wa Kihispania walipokuwa wamekwishachukua cheo cha Makhalifa na kuamua pia kutengeneza sarafu za dhahabu baada ya mwaka 929, sarafu hizo hazikuwa nzuri sana; zilianza kuwa nzuri tu baada ya 987-8, wakati dinari zilizopigwa chapa Sijilmasa zilipoanza kutokea. Lakini utengenezaji sarafu ulibakia hasa katika viwanda vya kutengeneza sarafu vya Kordoba, vilivyokuwa chini ya udhibiti wa moja kwa moja wa mamlaka husika.

Tukio la Waumayya lilikuwa fupi kuliko la Wafatimi, lakini ni dhahiri lilichochea kuendelea kuwepo kwa utashi mkubwa wa uzalishaji wa dhahabu katika Afrika na vile vile kwa misafara ya kuvuka Sahara. *Wareyes de taifas* pia walipiga chapa dhahabu kidogo bila umahiri na kwa matatizo. Lakini unafuu halisi uliletwa baadaye na Wamoravi. Awamu hii ya mwisho ya kipindi chetu pengine ndiyo iliyokuwa ya muhimu zaidi na yenye mafanikio makubwa zaidi katika historia ya mahusiano ya kuvuka Sahara, ingawa kwa namna nyingi ndiyo awamu ambayo haijulikani sana.

Ukitazama ramani (Ramani Na. 14.3) ya mahali ambapo Wamoravi walipiga chapa dhahabu mara moja huonyesha uvumbuzi muhimu. Nusu ya mashariki ya Maghrib, takribani haikuwa na viwanda vyovyote vya kutengeneza sarafu na Tilimsan yenyewe ilikuwa kiwanda kidogo tu. Kwa upande mwingine, nchi ambayo sasa yajulikana kama Moroko, isipokuwa kwa maeneo ya biashara ya kuvuka Sahara (Sijilmasa, Aghmat, na Nul Lamta), ilipiga chapa dhahabu, kama ilivyokuwa pia huko Fez na Marrakesh, miji mikuu, na mji muhimu wa Sala. Kulikuwa na viwanda saba vya kutengeneza sarafu katika sehemu ya Maghribi ya Maghrib na kumi na vinne katika Hispania.

Hapana shaka utengenezaji sarafu ulisitawi sana. Kutoka mwaka 1058 hadi 1088 ulifanyika Afrika, ambako dinari za mwanzo kabisa zilitengenezwa huko Sijilmasa mnamo mwaka 1056-7. Kwa jumla utengenezaji sarafu ulisitawi sana hasa baada ya mwaka 1100.

Wingi na uhakika wa utengenezaji sarafu ambao haukuwa na mshindani hadi kufikia Misri ya Wafatimi (wakati huo wakiwa wamekosa dhahabu kutoka Sudan) ulizifanya dinari za Wamoravi (kwa mara ya kwanza katika eneo la Waislamu la Maghribi) kuwa sarafu yenye nguvu sana kiuchumi, japokuwa haikuwa ikifikia kiwango cha uzuri wa sarafu ya Wafatimi. Maghribi ilisisitiza kupatikana kwa "marabotini"; baada ya mwaka 1070 ulimwengu wa Wafatimi wenyewe ulitaka sana kupata dinari za Wamoravi.

Kama hitimisho kwa matatizo haya ya sarafu, twabakia kujiuliza baadhi ya maswali magumu sana ambayo kwa sasa hayana majibu yakini. Je, dhahabu ya Afrika Maghribi ilisafishwa kabla ya kusafirishwa kwenda Kaskazini? Twaelekea kufikiri kwamba *tibr* haikufanyiwa usafishaji wa aina yoyote, na kwamba ilitumiwa katika viwanda vya kutengeneza sarafu. Sana sana labda ilikuwa ikiyeyushwa huko kusini kuifanya iwe rahisi kusafirisha. Huko Tegdausti tulikuta waya wa dhahabu uliowambwa kwenye mawe ya kuwambia ambayo pia yamegunduliwa. Ni dhahiri waya huo ulikuwa umetengenezwa kwa ajili ya kazi ya sonara au mapambo. Iwapo dhahabu iliyeyushwa huko kusini mwa Sahara, je, hatimaye ilisafirishwa ikiwa katika umbo gani? Wazo kwamba vipande vya dhahabu ama vilivyokuwa vimekatwa tu au vilivyokuwa vimetayarishwa kabisa kwa ajili ya kutengeneza sarafu vilisafirishwa, laelekea kuwa na uzito zaidi kwani kulikuwa hakuna tatizo la kusafisha

madini. Aidha dhahabu hiyo ingeweza kutumiwa pasi kusafishwa, au kuchanganywa na madini mengine bila wasiwasi wowote kuhusu kiwango cha unadhifu wake. Huko Tegdausti tulikuta nusu-vipande vitano vya dhahabu pamoja na vipande vingine vya dhahabu na fedha. Hivyo nusu-vipande vitano vilivyochongwa karibu katikati, vilikuwa vimemiminiwa ama katika tanuri maalumu la kutengenezea au kukalibu madini mchangani au katika chombo maalumu cha kutengenezea vipande maalumu vya dhahabu. Je, vifaa hivi vilikuwa vimekusudiwa kazi ya ufuaji dhahabu mahali hapo au ugawanyaji wa dhahabu hiyo katika maumbo maalumu kwa ajili ya utengenezaji sarafu?

### *Njia za biashara, njia za kusafirisha dhahabu na mawasiliano ya kibiashara kusini mwa jangwa*

Mbali na ushahidi wa kiakiolojia, uchunguzi juu ya uvukaji wa Sahara pia husaidiwa na vyanzo vya kimaandishi vya Kiarabu kutoka Kaskazini, hasa kuanzia karne ya kumi hadi karne ya kumi na mbili. Kati ya vyanzo hivi vya kimaandishi vile vyenye umuhimu mkubwa sana ni zile kazi za al-Bakri na al-Idrisi.

Hebu tusizitazame kulingana na mfuatano baina yake, bali tujaribu kuelewa ni mambo yapi yaliwaathiri wakati walipokuwa wakiandika.

Katika mchoro Na.14.5 tumeonyesha njia kuu saba kati ya *Bilad al-Sudan* na ulimwengu wa Kaskazini zilizonyeshwa na al-Bakri, lakini ambazo karibu zote alizipata kutokana na watoa habari tofauti. Kwa kuwa hakuwa na njia ya kuthibitishia habari alizokuwa akiegemea katika kazi yake, ilibidi azipange moja baada ya nyingine, pasi na njia ya kuzihakikisha, kadri alivyozipata kutoka kwa watoa habari wake.


Njia Na. 1 ilikuwa njia ya 'kifalme' iliyoanzia Tamdult hadi Awdaghust na ambayo kuna taarifa nyingi juu yake. Hakukuwa na njia nyingi za mawasiliano na Awdaghust: ilikuwa safari ya siku kumi na tano kufika Ghana na siku mia moja na kumi kufika Kayrawan; ambapo kuelekea kusini Awdaghust yaelekea ilikuwa mwisho wa njia (*cul de sac*). Kuhusu njia za kutoka Sijilmasa (njia na. 2 kwenye ramani) ambazo zilipita mashariki zaidi zilipotumiwa kutafutia chumvi hasa kutoka Tatintal, hazikuishia Awdaghust bali ziliishia Ghana. Ajabu ni kwamba Awdaghust haikuwa imeunganishwa na ama miji ama kwenye mto Senegal au na Awlil. Kwa sehemu zote haielekei kama ndivyo hali ilivyokuwa, kwani Awdaghust ilikuwa na umuhimu maalumu kwa miji iliyokuwa kwenye mto Senegal, hasa tukizingatia kwamba al-Bakri mwenyewe, kwingineko anaitaja Silla kama mshindani wa Ghana katika biashara ya dhahabu.

Mfumo wa Ghana ulikuwa changamano zaidi na kamilifu. Huko kusini, njia moja ilielekea Ghiyar. Wanahistoria hawajaafikiana juu ya mahala halisi pa majina ya mahali yaliyonukuliwa kwenye njia ya 4. Hata njia ya 5 nayo inaleta ubishani mwingi: wengine husema Kugha ilikuwa Maghribi wengine husema ilikuwa mashariki zaidi.

Eneo la Senegal linaelezwa katika njia ya 3, lakini hata hapa napo maelezo kuhusu mahali halisi na umbali wake haviko wazi sana. Kutoka Kalanbu, mji wa mwisho kutajwa, njia ilielekea 'kusini.' Haya ndiyo yalikuwa makazi ya Wazafku, ambao T. Lewicki anapendekeza wabainishwe kama watu ambao baadaye Yakut anawaita Wazafuni na ambao yeye aliwanasibisha na eneo la Kolombine, Maghribi ya mahali pajulikanapo leo hii kama Diara, na hivyo kuwa mashariki ya miji iliyotajwa na al-Bakri. 'Kusini' zaidi kulikuwa na 'wapagani' wengine. Ama kuhusu njia na. 3, 4 na 5 ujuzi wetu kuhusu Afrika unaathirika vibaya



14.4 Tegdaoust/Awdāghust: Kio cha Wafutimi, karne ya kumi (IMRS, Nouakchott)



*Siku 1 = karibu km 30 kwenye maeneo ya joto*  
Mchoro huu anajaribu kuwa ramani unazingatia maelezo ya mwandishi lakini hauonyeshi maeneo halisi

Namba kwenye mistari zinaonyesha idadi ya siku za safari (isipokuwa ilipoelezwa vinginevyo)

● Sehemu ambayo ilikuwa na visima ambavyo inasemekana vilifukiwa na Abd al-Rahman ibn Habib

0 500 1000 km  
0 500 1000 m

14.5 Mpango wa safari wa Al-Bakri; Sehemu ya magharibi (J. Devisse)

kutokana na kasoro kubwa, kwa madhumuni ya uchambuzi makini, za matumizi ya vyanzo mbalimbali vya habari alivyotumia al-Bakri.

Tukiiacha Ghana kwenye mtandao wa njia za na. 7, tutajikuta mara kadhaa katika matatizo makubwa zaidi ya kufasili: kipande cha mwendo kutoka Ghana kwenda Gao (siku 17) ni kifupi mno, kana kwamba mwandishi alipotoshwa. Aidha kidokezo 'kurejea Kaskazini' kilichotolewa kwenye maelezo ya njia za kuelekea Wargla, Jarid, Ifrikiya, Ghadames na Tripoli, pia chafaa kuzingatiwa. Mtandao huu wa njia ya upande wa mashariki 'kutoka Ghana' unaunda kitu kamili kutoka kituo chake cha mwisho kwa upande wa kusini hadi Kala ya Wabanu Hammad - kwa hivyo taarifa hizi ni za karne ya kumi na moja - na hadi kituo chake cha mwisho kwa upande wa mashariki huko Tripoli. Aidha, kuna uwezekano mkubwa kwamba maelezo haya huwakilisha taarifa zinazoaminika kuhusu karne ya kumi na moja, yaani kabla ya Wamoravi. Al-Bakri anataja njia nyingine sambamba na hii kati ya Tadmekka na Ghadames ambayo ilitumiwa katika safari za kutafuta vito vya thamani ndogo na kama tutakavyoona baadaye, kuna uwezekano mkubwa kwamba njia hii inaweza kubainishwa kikamilifu.

Dinari zilizotumiwa na wakazi wa Tadmekka zilikuwa za 'dhababu tupu' na zilikuwa na sifa maalumu ya kutokuwa na michoro yoyote ile (katika Kiarabu wanasema zilikuwa *sula*). Kwa jinsi al-Bakri anavyoandika, tunaweza kukisia kwamba zilikuwa vipande vipande vilivyotayarishwa kwa madhumuni ya kusafirishwa kwenda Kaskazini lakini ambavyo vilikuwa bado havijapigwa chapa. Katika mtazamo huu *sula* pengine ni kinyume cha *mankush* (enye kukatwa nakshi). Kwa hiyo huku hakukuwa utengenezaji sarafu bali hatua kabla ya hivyo kwani viwanda vyote vya kutengeneza sarafu vilikuwa Kaskazini.

Mbinu, malengo na habari zilizoandikwa na al-Idrisi ni tofauti kabisa zikilinganishwa na zile za yule aliyemtangulia. Yeye aliamua kueleza Afrika kwa kurejea kwenye kiunzi imara cha 'hali ya hewa' (*iklim*) na migawanyo yake midogo midogo. Ingawa naye anaeleza umbali wa maeneo kwa kutumia wingi wa siku kama alivyofanya mtangulizi wake (wakati mwingine akitumia maelezo ya umbali yaliyotolewa na mtangulizi wake, wakati mwingine kutokana na vyanzo vinavyofanana) yeye anazishughulikia taarifa hizo kwa namna tofauti kabisa (Ramani Na.14.6).

Ama kuhusu njia za mashariki, al-Idrisi kwanza anaeleza kitita cha mjiunganiko baina ya maeneo kutoka Mto Niger hadi Mto Nili kwa kuvuka Kawar. Maelezo haya yana taarifa mpya ambazo zinahitaji uchunguzi makini. Sehemu nyingine inashughulikia kwa undani maelezo ya alama za njia (yakiwa yanaonyesha umbali uhiozidishwa mno!) katikati ya Sahara zinazotokea Kaskazini kupitia Ghadames. Mfumo huu wa njia waelekea kuwa huru zaidi kutoka njia ya Tadmekka/Wargla kuliko ilivyo katika maelezo ya al-Bakri. Kwa hiyo kinachovutia zaidi ni ushughulikaji, mnamo karne ya kumi na mbili, wa njia zinazounganisha Niger/Nili na Niger/Chad, na kurejea kwa uhuru zaidi kwa njia ya 'Libya' inayoishia Ghadames na Tripolitania.

Katika upande wa Maghribi uhiunganisho na kazi ya al-Bakri hutoa vidokezo kadhaa muhimu. Kwa mfano, twaona kwamba njia kuu ya meridiani iliyobainishwa na al-Bakri inapotea. Huko Kaskazini, Sijilmasa inachukua nafasi ya Tamdult, labda kwa sababu ya kizuizi cha Wabarghawata kilichoendelea kuwapo katika njia hiyo.

Kwenda kusini, tunaacha kupita Awdaghust na hata Ghana. Jambo kubwa jipya hapa ni kwamba sasa tunakuja moja kwa moja kwenye miji ya Mto Senegal, ingawa kwa matatizo makubwa kutokana na kuvuka Kamnuriyya au Jangwa la Nisar. Miji hii ya kando kando ya



mto, ambako dhahabu ilipatikana, ilihitaji muda wa siku 40 kuifikia. Kutoka Silla au Takrur hadi Sijilmasa kulichukua siku 40; vivyo hivyo kutoka Awlil hadi Sijilmasa, na vilevile kutoka mtoni kwenenda Sijilmasa kupitia Kamnuriyya na Azuki. Hivyo inaweza kuchukuliwa kwamba kulikuwa na njia ya kuanzia Sijilmasa hadi Mto Senegal kupitia Azuki.

Al-Idrisi anasukuma Awdaghust mashariki mno kwa kupafanya pawe safari ya mwezi mzima kutoka Awlil. Njia zilizopaunganisha zilikuwa na umuhimu mdogo karne moja au mbili nyuma. Ingawa ni dhahiri mji huu ulikuwa na umuhimu mdogo kiuchumi kuliko ilivyokuwa miji yenye masoko katika Mto Senegal, uliendelea kuunganishwa na njia ambazo haziwezi kupuuzwa. Al-Idrisi anasema kwamba Awdaghust ulikuwa umbali wa siku kumi na mbili kutoka Ghana; na vivyo hivyo kutoka Barisa, ambayo pia iliwezesha biashara na kusini. Barisa (ambao unafanana na mji wa Y.r.s.ni anaoutaja al-Bakri) ulikuwa muhimu kwa maeneo ya kusini: yaani ulikuwa kituo cha mbele kwa mawasiliano na 'Walamlam' na Wamalal, pia uliunganishwa kwenye mfumo wa Mto Senegal kupitia Takrur. Hivyo, mji huu unakuwa kiungo katika mifumo ya njia za Kaskazini zaidi kupitia miji ya kandokando ya mto na kupitia Awdaghust na Ghana, ingawa katika maelezo yake, al-Bakri hakuwa wazi sana juu ya dhima ya Y.r.s.ni. Hata hivyo, hali ikitazamwa pia kutoka kusini hadi Kaskazini, yaani kuanzia Barisa, umiliki wa Takrur wa eneo katikati ya Bonde la Senegal na udhibiti wake wa biashara wa dhahabu vinachukua upeo mpya na vinalcta mabadiliko katika uwiano uliotokana na mpangilio wa usafirishaji nje dhahabu katika kipindi cha karne moja.


Mfumo wa Ghana umekanganyika zaidi katika maelezo na pia unatoa ukweli zaidi kuhusu umbali; lakini kuna baadhi ya makosa katika data inayohusu njia zilizounganisha sehemu za mashariki, kuelekea Gao na hata kwenye Kuruba ya Niger.

Kwa mujibu wa al-Idrisi, sehemu yote hii ya pili ya "hali ya nchi" ya kwanza, ikiwa ni pamoja na Wawankara na miji iliyoko kwenye Kuruba hadi kufikia Tirakka, ilikuwa chini ya umiliki wa Ghana.

Hivyo, twaweza kudiriki kutoa nadhariatete kwamba kulikuwa na mifumo mikuu miwili iliyoshindana katika kutafuta dhahabu. Mmoja ulikuwa na kitovu chake katika miji iliyokuwa kwenye Mto Senegal na ulikuwa ukiunganishwa na Sijilmasa kupitia Azuki; hii inaakisi moja kwa moja kuinukia kwa Wamoravi na muungano wao na Takrur. Mfumo mwingine, uliotawala nchi zilizokuwa katika Mto Niger, ulimilikiwa na Ghana na uliunganishwa kwa karibu zaidi na Wargla kuliko ilivyokuwa huko nyuma.

Taratibu za safari katika eneo lote la Sahara zilizotolewa na al-Idrisi, na ambazo zinatofautiana na zile za mtangulizi wake, hazitoi kitu chochote kipya ambacho kingetarajiwa baada ya karne mbili za njia zilizounganisha maeneo ya kusini mwa Mto Senegal na Mto Niger. Kuna maelezo mengi yanayoweza kutolewa juu ya jambo hili. Mojawapo, mi kwamba watu weusi hawakuwaruhusu wafanyabiashara kutoka Kaskazini kusafiri sana na kwamba usilimishaji watu, ambao ulifanyika kikweli na ulioenea sana katika Kuruba ya Mto Senegal na katika Gao mwishoni mwa karne ya kumi na moja, ulikuwa ukisitasita huko kusini. Kwa vyovyote vile, al-Idrisi asiegemewe sana zaidi ya mtangulizi wake juu ya maelezo ya maisha ya watu weusi kusini mwa mito hiyo.

Kama tulivyoona tangu mwanzo uwekaji katika ramani wa sehemu za biashara uliuhisishwa sana na sehemu vilipopita vizingamvua: yaani ilibidi pawepo na maji ya kutosha kwa ajili ya wanyama wabebamizigo na kwa ajili ya shughuli zote za maelfu kadhaa ya watu. Kwa bahati mbaya, ujuzi wetu juu ya maendeleo ya mazingira katika ukanda wa Kaskazini bado ni mdogo sana. Aidha kwa bahati mbaya pale linapohusika suala la njia zilizounganisha



14.6 Mpango wa safari wa Al-Idrisi Sehemu ya magharibi (J. Devise)

maeneo ya Sahara utafiti wa kiakiolojia katika sehemu ya Kaskazini ya Afrika umetoa matokeo madogo sana kwa karne ya kumi na kumi na moja, na vilevile kwa karne nyingine mbili zilizotangulia.

Hata hivyo inafurahisha kuona kwamba mambo ni mazuri zaidi upande mwingine wa jangwa. Kuhusu Azuki sasa tunajua kwamba eneo hili lilishuhudia shughuli kubwa mbili: moja katika karne ya kumi hadi kumi na mbili na nyingine katika karne ya tano hadi kumi na saba. Kazi inayoendelea sasa inadokeza kwamba mji mkuu wa Wamoravi uliotajwa katika matini utaweza kutoa maelezo ya kuvutia sana.


Ama kuhusu Awdaghust, matokeo yaliyopatikana yanaonyesha kwamba katika karne za kumi na kumi na moja, eneo hili lilikuwa mji mkubwa sana. Shughuli za kitasnia zilianza hapo katika mazingira yasiyokuwa ya kimji mnamo karne za nane na tisa. Katika karne za tisa na kumi - kwa haraka kiasi lakini bila mabadiliko makubwa ya kitamaduni - eneo hili lilianza kuonekana kama mji, likiwa na mitaa, viwanja, msikiti, majumba ya watu binafsi na kuongezeka kwa vitu vya matumizi ya anasa. Wachimbaji wote wametanabahi ukomo katika mtindo wa maisha ya mji huo mnamo katikati ya karne ya kumi na moja lakini ulianza kuwa na maisha tofauti na bainifu baada ya tarehe hiyo. Awdaghust ulikuwa mji wa wakazi elfu kadhaa ambao ulikuwa na shughuli nyingi sana katika karne ya kumi na karne ya kumi na moja lakini hapana shaka ulipatwa na maafu mnamo katikati ya karne ya kumi na moja. Sababu kubwa za kufifia kwake ziko nje ya mlolongo wa kiunzi cha tarihi zetu na ya upeo wa sura hii.

Machimbo ya Ghana (Kumbi Saleh) pia yametuwezesha kupima muda mrefu ambao eneo hili lilikaliwa; shughuli zilizofanyika kutoka karne ya nane hadi karne ya kumi na tano zinaonekana katika matabaka, moja juu ya jingine, katika unene unaozidi mita 7; pia msikiti muhimu sana umekwishagunduliwa na kuhifadhiwa. Makao makuu ya kifalme anayoyazungumzia al-Bakri nayo bado hayajaonekana. Mpaka sasa vifaa vichache sana vilivyoletwa kutoka Kaskazini vimegunduliwa lakini dalili za kuwepo njia za kuunganisha Awdaghust hazina ubishi.

Sintiu-Bara iko katika eneo la kihistoria lenye kuvutia sana ambako mabaki ya maisha ya zamani katika miji yameonekana, lakini kazi iliyokwishafanyika mpaka sasa haituwezeshi kulihusisha eneo hili na maeneo yale yaliyotajwa na al-Bakri na al-Idrisi. Mabaki ya kazi za ufuaji wa metali zinazorejea nyuma hadi karne ya tano na ya sita yamegunduliwa mahali hapo na vilevile mabaki ya kazi za hali ya juu za ufinyanzi. Hivyo yafaa tuzingatie yale al-Idrisi aliyosema kuhusu Takrur na Barisa, ambako kuhifanyika mawasiliano na wafanyabiashara kutoka Kaskazini.

Mji wa Nyani ulikuwa na maisha machangamfu zaidi katika kipindi kilichofuata. Lakini kwa kipindi kinachotuhusu, hakuna mabaki kamili ya njia zilizounganisha na mifumo ya njia za kuvuka Sahara. Hata hivyo ukweli kwamba mji huo ulikuwepo kwa hakika na kwamba huenda ulifanya biashara ya mazao na maeneo ya jirani yake hufanya mtu adhanie ndio Mallal uliotajwa na al-Bakri.

Uchunguzi huko Jenne-Jeno, ambao umekitwa kwenye elimu makini ya matabaka ardhini na ukadiriaji tarehe, unaelekeza kwenye magunduzi mapya kabisa. Kati ya miaka 400 na 900, tayari kulikuwa na mji katika eneo hili, karibu na sehemu ijulikanayo hii leo kama Jenne (Djenne); mji huu ulikua sana katika kipindi kilichofuata, yaani kuanzia mwaka 900 hadi mwaka 1400. Kwa bahati mbaya kwa sasa matokeo hayo ambayo yana umuhimu mkubwa kwa biashara ya kikanda, hayaathiri mfumo wa njia zilizounganisha maeneo ya Sahara.



14.7 Maeneo ya biashara ya kavuka Sahara, karene ya tisa na kumi na moja (J. Devise)

Mji wa Bhego haujatoa ushuhuda wa kutosha au kuruhusu uundaji wa nadhariatete nyingi. Lakini ukweli kwamba dalili za kale kabisa za shughuli za hapo zinarejea nyuma hadi karne ya pili unaonyesha kwamba haitawezekana kuendelea kukwepa swali kama bidhaa hazikupelekwa huku na huko katika savana karibu na msitu mapema zaidi kuliko ambavyo imekuwa ikifikiriwa.

Matokeo yaliyopatikana hapa na pale kutokana na akiolojia yanaathiri historia ya uchumi na historia ya biashara ya kuvuka Sahara; na ni jambo la kusikitisha kuona kwamba mpaka sasa hakuna taarifa za kutosha kuhusu Gao, Tadmeka, Bilma au hata Air, achilia mbali miji ya Kaskazini mwa Sahara.

Utafiti wote wa hivi karibuni unahitajia kufanyika kwa marekebisho makubwa juu ya historia ya mabadilishano ya kiteknolojia na kibiashara, kwani kutokana na magunduzi ya tafiti hizi, Afrika Maghribi haichukuliwi tena kama sehemu iliyotegemea sehemu za Kaskazini kupitia njia zilizounganisha maeneo ya Sahara.

Vyanzo vya kimaandishi na akiolojia sasa vinatuwezesha kuandaa orodha ya muda ya mazao yaliyovuka Sahara. Kwa bahati mbaya maelezo yanayotolewa na vyanzo vya Kiarabu na yale ya akiolojia huwa kila mara au hata mara nyingi hayakubaliani. Al-Bakri anasema kwamba huko Awdaghust ngano, tende na zabibu viliagizwa nje kwa bei ya juu sana kwa ajili ya wageni wataalamu kutoka Kaskazini, lakini mpaka sasa akiolojia haijaweza kuthibitisha jambo hili. Hata hivyo, al-Bakri anafungua mlango kwa ajili ya utafiti muhimu kuhusu biashara ya tende, ambazo yaelekea zilivuka Sahara mapema sana, na pengine hata na taarifa juu ya jinsi zilivyopandwa. Maeneo yote ya machimbo yanaonyesha ongezeko kubwa katika uingizaji wa bidhaa ambazo ni za nusu-anasa (taa za mafuta za vioo) na za anasa (vikombe, magudulia ya maji, chupa za uturi na vioo vya mapambo) kwa kipindi hiki. Kwa sasa hakuna chochote cha kulingana navyo kimewahi kupatikana, katika kipindi hicho hicho, katika maeneo na kusini zaidi; aidha miji kama Gao, Sintiu-Bara, Nyani au Jenne-Jeno haiwezi kulinganishwa, kwa utajiri, na Tegdausti. Hii ni kweli pia kuhusu zao la kioo, ambalo katika kipindi hicho hicho liliingizwa huko Tegdausti katika maumbo mbalimbali (chupa ndogo ndogo, magudulia ya maji, vikombe na kata za kunywea maji), lakini ambalo upatikanaji wake ni wa nadra sana katika maeneo mengine yaliyokwisha kufanyiwa kazi hadi sasa.

Ili kupata picha kamili ya biashara hii ya bidhaa za anasa ya kuvuka Sahara na ambayo ilihudumia watu wa Afrika Kaskazini walioishi katika Sahel, madini ya fedha lazima nayo yaongezwe kwenye mazao kama ngano, tende, zabibu, vyombo vya mfiyazi na kioo. Madini haya pia yalifanyiwa kazi huko Tegdausti pengine kama ilivyokuwa kuhusu vito vya thamani na vya nusuthamani vilivyozungushwa mbali na Awdaghust.

Kuzungushwa kwa vito vya thamani na vya nusuthamani kulianza kabla ya mwaka 900. Baadaye kukapanuka zaidi kutokana na mahitaji ya soko kubwa la watumiaji wake na asili ya vito hivi inafunza sana.

Ageti (agate) halisi, iliyoipatikana Misri ya Juu ilikuwa adimu. Suala la amazoniti ni muhimu zaidi; na ingawaje hayatajwi na waandishi wa Kiarabu, akiolojia imctoa vipande vingi vya madini haya ambavyo vinavutia sana. Migodi pekek iliyobainishwa mpaka sasa iko umbali mkubwa kutoka Afrika Maghribi, ikiwa huko Kaskazini-mashariki ya Tibesti na huko Fezzan. Katika hali zote ugunduzi wa idadi kubwa ya vipandevipande vya madini haya ya kijani ya kupendeza, katika Afrika Maghribi, huchukulia kwamba kulikuwa na namna fulani ya kuyatoa luko Kaskazini-mashariki na kuyapeleka Maghribi. Utafiti uliofanywa hivi karibuni umeonyesha kuwa kuna mashapo kidogo ya amazoniti katika eneo la Tijikija huko



14.8 *Tegdaoust/Awdāghust*. bakuli la glasi lililokua nye Libde kutoka Ifrīkiya or Egypt (?).  
(Restoration: Mainz Glass Institute, Federal Republic of Germany.) (IMRS, Nouakchott)

Mauritania. Ganeti (garnet) ilitoka Maghrib. Ganeti iliyokatwa vizuri imepatikana huko Tegdausti. Ama kuhusu kito ambacho al-Bakri anakiita *Tasi-s-Samt*, maelezo yake yanaoana na kalisoni (*chalcedony*) zaidi kuliko akiki (*cornelian*). Aidha kalisoni nyingi za kipindi hicho zinapatikana huko Tegdausti. Ama kuhusu kazi ya vito hivi, ambavyo vilikuwa vikipendeka sana huko Afrika Maghribi katika karne ya kumi na ya kumi na moja, ni kwamba vilikuwa vikitumiwa kutengenezwa vito vya thamani kwa kuchanganya metali, mawe na makombe.

Mwisho, pengine yafaa pia kutaja uingizaji wa kauri ambao historia yake katika biashara ya kuvuka Sahara haijulikana vizuri kwetu. Zilijitokeza huko Awdaghust katika takribani karne za tisa na kumi na tunaanza kuona dalili za kuweco kwa biashara yake huko Kaskazini katika karne ya kumi na moja.


Hapana shaka kwamba kwa upande wa Awdaghust bidhaa hizi ziliingizwa kutoka nje kwa ajili ya wateja matajiri wa Kaskazini. Wateja matajiri hawa walipotoweka, baada ya mwaka 1100, bidhaa za anasa nazo zilipotea haraka. Isipokuwa pengine katika hali ya pekee tu yaelekea Awdaghust laikuwa mno kituo cha kuzisambaza tena bidhaa hizi zilizoingizwa kusini kama kituo kwa ajili ya biashara ya thamani kubwa kati ya dhahabu iliyofuliwa na ngozi zilizotengenezwa na kupambwa, ambari kutoka pwani ya Atlantiki, pengine gundi, na bidhaa kutoka Kaskazini, ambazo kati yake ni chumvi tu ndiyo ingeweza kusafirishwa nje tena.

Huenda Awdaghust ilikuwa pia kituo muhimu cha kufulia shaba. Iliagiza mali ghafi kutoka nje na yaelekea iliitumia kutengenezwa michanganyo safi ya madini na kutengenezwa bidhaa za anasa kwa matumizi ya hapo - vito vya thamani na medali - au kwa kusafirisha tena nje. Yawezekana Awdaghust ndiyo ilikuwa chanzo cha waya wa shaba uliotumika kama 'sarafu' huko Ghana.

Haya yote yanaonyesha jinsi ambavyo mahitimisho ya muda ya wakati huu juu ya biashara ya kuvuka Sahara hayana budi kuwa, kwani biashara hiyo ilikuwa ya kubadilikabadilika zaidi, changamano zaidi na yenye kuhitilafiana zaidi kuliko ilivyokuwa ikifikiriwa hapo nyuma. Kwa hiyo, tunaweza kujiuliza kama kweli biashara hii, ambayo hugubikwa katika usemi wa kama biashara ya 'ufahari' ya chumvi na dhahabu, haikuwa ya kubadilikabadilika na ya kuhamahama kutegemea mtindo na uwiano wa nguvu za utawala na vilevile ya uthibiti mdogo kuliko matini na uimara wa njia za biashara vinavyodokezwa; na pia kama kweli biashara hii ilibadilisha mitindo ya maisha na vionjo vya watu katika pande zote mbili za Sahara.

Hebu sasa na turejee kwenye biashara yenyewe ya dhahabu. Af-Bakri anaitolea marejeo bayana kuhusiana na taratibu za safari za biashara. Msafara wa kwanza ulianzia Ghana kwenda Ghiyaru kwa kuvuka kwanza mkono wa 'Nili' na kisha nchi ya Gharntil, ambako hawakuishi Waislamu; hawa walikuwa wameweka makazi Maghribi zaidi katika Yarasna, ambako njia iliishia. Nji ya pili ilitoka Ghana hadi Kugha, huko kusini-Maghribi, ambako kulikuwa na migodi bora ya dhahabu. Sasa tuzieleweje 'nyendo za utafutaji' za wafanyabiashara wa Kiislamu ambazo zinadokezwa na matini ya al-Bakri na ambazo zingewapeleka wafanyabiashara hawa kusini zaidi hadi takribani kuyafikia maeneo haya ya migodi?

Kwa upande wa al-Idrisi, karne moja baadaye, njia mbili kuu za biashara ya dhahabu zilikuwa na utaratibu mzuri zaidi. Njia ya kwanza ilikuwa kama kiungo - kutoka miji iliyokuwa mbali kiasi kwa upande wa Kaskazini kama vile Tadrar, na miji iliyotegemea



14.9 Maeneo yanayozalisha dhahabu Afrika Magharibi (J. Devissé)



kama Barisa na Silla - kati ya wafanyabiashara toka Kaskazini na wafanyabiashara weusi ambao walikuja chini ya Takrur na kusafiri katika sehemu mbalimbali kati ya miji iliyokuwa chini ya uthibiti wake. Hivyo kulikuwa na mfumo wa udhibiti biashara wa weusi - Takrur - katika eneo ambako karne moja kabla hakukuwa na kitu kama hicho, ingawaje al-Bakri tayari alidokeza kwamba wakati huo Silla ilikuwa ikijaribu kushindana na Ghana. Barisa, ncha ya kusini ya mfumo huu, inaweza kuwekwa kwa uwazi katika sehemu ya juu ya Senegal lakini nje ya maeneo ya uchimbaji dhahabu.

Maelezo ya al-Idrisi huviweka vituo vya biashara ya dhahabu mbali zaidi kwa upande wa Kaskazini na wakati huohuo yanapunguza eneo la utafutaji la wafanyabiashara wa Kiislamu waliokuja Afrika ya watu weusi kutoka Kaskazini.

Kisha al-Idrisi anaelezea mfumo wa pili wa soko la dhahabu uliomilikiwa na Ghana. Ncha za kusini kabisa za mfumo huu zilikuwa Gharbil na Ghiyara; hii ya mwisho, ikiwa mwendo wa siku 11 kutoka Ghana, ilikuwa kwenye tao linalopitia Baule, ambalo ni tawi la Mto Senegal, na delta ya ndani ya Niger. Kati ya sehemu hizi yaelekea ni vema kukubali zaidi Baule. Yaelekea pia kwamba Barisa na Ghiyara ndivyo vilivyokuwa vituo vya mbele vya mfumo miwili kuelekea maeneo ya migodi ya Galam na Bambuk. Mashariki zaidi Wawangara walikalia eneo kuowa sana ambako dhahabu ilikuwa nyingi. Viashirio vya al-Idrisi vinadokeza kwamba eneo hili ni sawa na lile la delta ya ndani ya Mto Niger kati ya ncha yake ya kusini kabisa karibu na Bure na eneo linalozunguka Tirakka, lakini hapa hapakuwa katika eneo la migodi ya dhahabu.

Kazi kubwa zaidi kuliko ile iliyokwishafanyika huko nyuma yahitajika juu ya wafanyabiashara weusi waliotajwa na vyanzo, kuanzia al-Bakri. Wafanyabiashara hawa, wajulikanao kama Wabanu Namghmarata, wakati fulani waliwahi kudaiwa kuwa sawa na Wawangh.m.rata na msawidi mmoja; hii ilizua majadiliano muhimu sana, hasa kwa kuwa wafanyabiashara hawa waliuza dhahabu. Hapo baadaye itabidi swala zima la Wawangara, mahali walipoishi na nafasi yao katika uchumi ichunguzwe tena. Mwisho tusisahau kwamba, ingawa hawakutajwa, wafanyabiashara weusi, wamegusiwa habari zao katika maelezo ya al-Bakri na al-Idrisi huko Gharbil, Ghiyara na Barisa, huko Takrur, na huko Ghana na Gao.

Yaweza kuwa ni ujasiri mno kudai kwamba kuna masuluhisho ya mwisho kwa hoja hizi ngumu. Katika enzi ya Ibn Hawkal, maeneo ya mbali ambako weusi waliishi na kupata dhahabu yalichukuliwa kuwa safari ya mwezi mmoja kutoka Ghana. Baadaye tunaona umbali huu ukifupishwa; na katika wakati wa al-Idrisi twafikia jawabu linaloelekea kukubalika. Picha tunayopata ni kwamba wafanyabiashara kutoka Kaskazini hawakufika moja kwa moja kwenye maeneo ya migodi ya dhahabu bali waliwasiliana na wafanyabiashara weusi. Wafanyabiashara hawa wa Kaskazini walirudi nyuma Kaskazini kati ya karne ya kumi na moja na ya kumi na mbili kadri harakati za watu wa Sudan, wawe ni Waislamu au la, dhidi ya shinikizo kwa eneo la Sahel tangu karne ya kumi zilizotolewa na wafanyabiashara kutoka Kaskazini, zilivyo zidi kupata uratibu mzuri zaidi.

### *Athari za kitamaduni za kukua kwa biashara ya kuvuka Sahara*

Ama kuhusu vionjo na vyanzo vya chakula, hakuna badiliko la msingi lililotokea. Kaskazini iliuzwa nje kwa bei kubwa sana bidhaa zake zilizotakiwa na wafanyabiashara 'wageni' waliokuwa wakishi kusini mwa jangwa. Kama bidhaa iliyoweza kusafirishwa, tende zilikuwa na mafanikio ya muda mrefu zaidi kuliko ngano.

Eneo la Sahara halikuwa na shughuli za kilimo isipokuwa kwenye bustani za oasisi. Katika eneo hili, vipande vya nyama ya ngamia iliyokaushwa, maziwa ya ngamia na majani fulani ya mwitu ndivyo vilikuwa chakula kikuu cha watu wa huko ambao hawakuzoea mkate, na ambao walitumia maji kwa uangalifu mkubwa. Nyama ya nyoka ilitumiwa kama chakula cha ziada katika sehemu ambazo walipatikana kwa wingi na ambako maji yalikuwa adimu sana. Vyanzo vilivyopo havisemi chochote kuhusu uwindaji, ingawaje hii lazima ilikuwa njia nyingine kubwa ya kupatia chakula.

Wdaghust ilikuwa sehemu ya jangwa hili, au tuseme ukanda mkame sana, lakini ilikuwa sehemu ya pekee kabisa kwa sababu ya ukanda wake wa chemchemi. Katika karne ya ishirini, kulikuwa na aina mbili za ehakula cha 'matabaka': kile cha watu matajiri, ambao wengi walitoka Kaskazini na ambao walikula ngano, matunda yaliyokaushwa na yale yaliyopatikana mahali hapo (tini na zabibu), nyama ya ng'ombe na nyama ya kondoo, na kile cha mafukara ambao wengi walikuwa weusi, waliotumia zaidi mtama uliolimwa mahali hapo na ambao ulipikwa ugali au kukaangwa kama keki na kutiwa ladha na asali iliyoingizwa kutoka kusini. Katika karne ya kumi na mbili, baada ya wafanyabiashara kutoka Kaskazini kuondoka, pengine baada ya mashambulizi ya Wamoravi, mji ulitumia nyama ya ngamia iliyokaushwa kama chakula kikuu. Yaelekea kuwa kadri mji huu ulivyoendelea kuwepo wakazi wake walijinasibisha na chakula cha mazingira ya hapo.

Kuelekea Maghribi kuvuka Mto Senegal na Mto Niger na kuelekea mashariki katika Kwar kila kitu kuhusu chakula kilikuwa tofauti kabisa. Chakula kikuu kilikuwa mtama (*durra*), ambao ulilimwa kwa wingi, wali, samaki wabichi na wale waliokaushwa kwa moshi au kutiwa chumvi, nyama na maziwa ya ng'ombe, na mara chache nyama na maziwa ya kondoo na mbuzi. Katika eneo hili la kilimo cha mtama kulikuwa na lishe makini kwa kipindi kirefu, chakula bora sana na kilicholingana na mazingira kiasi cha kufanya mabadiliko yoyote kuwa magumu kutokea.

Maeneo haya matatu ya chakula yalikuwa bainifu sana na hivyo kuwa na utengano wa wazi na yaliendelea kubakia hivyo walau hadi karne ya kumi na mbili pamoja na kuwepo kwa mawasiliano. Hivyo haishangazi kwamba maendeleo muhimu sana katika mbinu za kilimo yaliyokuweco Kaskazini hayakufika kabisa kusini ambako mbinu za kilimo, zilizokuwa zikioana vizuri na mazingira zilibakia hivyo hivyo kwa karne nyingi.

Halikadhalika kuingizwa kwa mbinu fulani na vyombo kutoka nje hakukufanya vichukuliwe na tamaduni za kusini. Matanuu yamegunduliwa Tegdausti ambayo yana uwezo wa kuweka joto la kufikia au kuzidi nyuzi joto 100C. Kwa umbo matanuu hayo yanafanana na yale yaliyogunduliwa Sabra Mansuriyya, huko Tunisia. Yaelekea yalikuwa yakitumiwa kutengenezea shanga au kuyeyushia mchanganyiko wa madini ya shaba. Hapana shaka kuwa yalitumiwa katika majaribio ya mara kwa mara ya kutia inapambo ya kung'ara kwenye vyombo vya mfinyazi. Hakuna matanuu ya aina yake yaliyowali kuonekana kwingineko.

Kuingizwa kwa wingi kwa taa za mafuta za ubora wa hali ya juu kulifuatiwa na uigizaji hafifu wa kuzitengeneza mahali hapo. Haijulikani kwa yakini aina ya taa zilizokuwa zikitumiwa huko kusini.

Majilio ya vyombo vya mfinyanzi vilivyorembwa au vilivyong'arishwa yalikuwa na athari ambayo mara nyingi inaonekana kwenye vyombo vinavyotengenezwa mahali hapo. Lakini vyombo hivi vilivyoingizwa kutoka nje havikubadili kwa kiasi kikubwa matokeo ya kazi za ufinyanzi za wenyeji, kazi ambazo mbinu zake za ufundi, mapambo na maumbo yake vilikuwa vya miaka maelfu nyuma. Tukiacha uigizaji wa maumbo na mapambo machache



14. zinazoonyesha nywele, macho - mfano wa sanamu kutoka kwenye kipiūdi kabla ya Uislamu. Sehemu (side view) from the pre-Islām na mdomo zilitengenezwa kwa shina lenye bomba

kutoka nje, eneo la utengenezaji vifinyange la Afrika ya weusi halikutegemea lile la Kaskazini. Wala si eneo la Kaskazini lililolipatia eneo la kusini kionjo makini cha utengenezaji visanamu vya wanyama na binaadamu kutokana na udongo mwekundu (Kielezo na.14. 10).

Kukua kwa njia zilizounganisha maeneo ya Sahara, utashi mkubwa wa dhahabu na ngozi uko Kaskazini na utashi kiasi wa mazao ya Kaskazini (isipokuwa chumvi) huko kusini bengine hakukuleta mabadiliko yoyote makubwa katika utamaduni au namna ya maisha ya watu wa Kaskazini au kusini hadi ilipofika karne ya kumi na mbili.

Mambo hayo yote hayakuwa chanzo cha uhamisho mkubwa wa teknolojia ya msingi- k.m. kuhusiana na metali - ama kwa sababu uhamisho huo ulikwisha- tokea mapema zaidi au kwa sababu sehemu za kusini kwa muda mrefu zilikwishaunda mbinu zake zenyewe za kuzalisha metali. Kuhusu shaba, ambayo ilikuwa imekwishazalishwa huko kusini mwa Sahara kwa walau miaka 1000, wakati njia za kuunganisha maeneo ya Sahara zilipopanuka, tunajua sasa cwamba mbinu za kukalibu metali, - kutengeneza shaba nyeupe zilizomiminwa risasi na za culehemu risasi - zilianzishwa kusini mwa jangwa kati ya karne ya sita na karne ya nane.

Hata hivyo, katika nyanja tatu, uhamisho (wa teknolojia) - na siyo tu kutoka Kaskazini kwenda kusini - pengine ulikuwa na athari kubwa na ya 'kudumu.'

Makala maarufu ya J. Schacht, yaliyoandikwa zainani kabisa yalionyesha, kuhusiana na

usanifu majengo, athari ya mifano ya Waibadi na uvukaji wao wa jangwa. Hizi ni kweli ambazo kwa hakika hazihusiki tu na usanifu majengo. Hata hivyo, itakuwa ni hatari kufasiri kitu kizima kutokana na sehemu ndogo inayofahamika, k.m. kwamba kuingizwa kwa ramani za ujenzi wa misikiti kulikuwa na maana kwamba stadi zote za majenzi pia zilingizwa kutoka Kaskazini.

Lakini watu bado wanaling'ang'ania wazo kwamba usanifu majengo, kama sayansi, uliingizwa huko Sudan na Mansa Musa baada ya safari yake ya hija. Huku ni kukanganya ujenzi wa kumbukumbu fulani, misikiti na sehemu za wazi, na vilevile mipango miji mahususi ya Kiislamu, na sanaa ya kupanga sehemu za kuishi, ambacho ndicho chanzo cha taaluma ya usanifu majengo. Usanifu majengo wa tope umeanza tena kuwa jambo linalohitaji kutazamwa na kufanyiwa uchunguzi makini. Majengo ya zamani kabisa ya Tegdausti yalitumia sana matofali ya kuchoma, na kuta za matofali hayo zilipatikana katika pande zote za jengo. Sanaa ya kujenga kwa tope na pengine matofali ni ya tarehe za kabla ya matumizi makubwa ya njia za kuvuka Sahara. Bara la Afrika liliboea katika mbinu hii ya kutengeneza vifaa vilivyochukuana na mazingira na vya manufaa tangu zamani sana.

Kutokana na usilimishaji wafanyabiashara wa Kiislamu pengine walileta kusini mwa jangwa michoro yao ya nyumba na kwa vyovyote vile, mipango - miji mahususi kwa jiji la Kiislamu. Kwa upande mwingine tunaweza kujiuliza kama baadhi ya teknolojia hazikuvuka Sahara kutoka kusini kwenda Kaskazini. Kwani pale Kasri ya Kimoravi huko Marrakesh ilipochimba kulipatikana ukuta wa mawe uliokuwa na sehemu mbili zilizojengwa na kugawanywa kwa kokoto iliyochanganywa na tope. Kuta zinazofanana na ukuta huu zilipatikana Tegdausti; na yaweza kuulizwa kama kweli Wamoravi hawakutumia mbinu ya Kisahara au Kisahel huko Marrakesh. Hali hii hutokeza pia kuhusiana na mapambo ya ukutani: huko Tegdausti mapambo ya rangi nyeupe na nyekundu, ambayo mpaka sasa hayajalingana na mengine ya aina yake, yalikuwa yameenea sana katika karne ya kumi na karne ya kumi na moja. Yalipakwa juu ya tabaka nyembamba sana ya udongo wa tope. Tunaweza kuyahusisha haya na yale mapambo ya rangi nyekundu na nyeupe yaliyopatikana huko Marrakesh na Chiehawa ambayo ni ya kuanzia kipindi cha Wamoravi. Aidha tunaweza kujiuliza kuhusu chanzo cha mapambo yanayosifika sana huko Walata na Ghadames.

Tatizo jingine la wazi ni lile la kupenya kwa ufumaji na pamba kusini mwa Sahara. Ingawa suala la watu weusi kutovaa nguo linaendelea kutajwa katika matini, lakini kwa kiasi kikubwa hili ni tatizo la mielekeo ya tabia na usuli wa kijamii wa wahariri kuliko ujuzi wa kweli wa mavazi ya weusi. Kwa sasa akiolojia haijatao jibu kuntu. Pia za duara za kusokotea nyuzi zilikuwepo huko Tegdausti tangu zamani sana ingawa ziliongezeka sana tu katika vipindi baada ya karne ya kumi na mbili. Akieleza eneo la miji kwenye Mto Senegal, al-Bakri anasema kwamba huko Silla nguo ndogo za kujifunga kiunoni zilizokuwa zikitengenezwa Tirinka zilitumiwa kama pesa.

Hata hivyo yaonekana kwamba katika karne za kumi na moja na kumi na mbili, nguo za pamba zilikuwa bado ni kitu cha anasa na alama ya tabaka, na uingizaji nguo kutoka Kaskazini uliendelea kwa kiwango kikubwa hadi kufikia karne ya kumi na mbili; lakini suala hili bado liwazi kujadiliwa.

Kwa kadri majengo alivyvo hivi sasa, suala la tatu ni gumu na lisilohitibika zaidi kuliko mawili ya mwanzo. Suala lenyewe ni kama mahitaji ya ghafula ya dhahabu katika karne ya kumi, hayakuwezesha uhamisho wa mfumo wa Kiislamu wa upimaji wa vitu hadi kusini mwa Sahara.

Kuwepo huko Tegdausti kwa mizani yenye uwezo wa kupima vitu vidogo vidogo tangu zamani sana, kuingia kwa mizani ya vioo huko Tegdausti, Gao na Kumbi Saleh, na pengine aina nyingine za mizani katika maeneo mengine, kunatufanya tadokeze jibu la hadhari lakini chanya kiasi, yaani kwamba msingi wa mfumo wa upimaji vitu pengine haukuandamana na utashi wa dhahabu katika karne ya kumi.

Mwisho, hebu tujaribu kutazama matokeo ya ukuaji wa biashara ya kuvuka Sahara kwa nchi zilizohusika.

Huko kusini, ni wazi, ama kwa sababu ya watu kusilimu au kwa sababu ya mahitaji ya kiuchumi ya muundo wa dola, kulitokea kitu fulani (kwa wazi zaidi huko Takrur na Ghana na pengine pia huko Gao na labda kwingineko) ambacho kilimarisha nafasi ya watawala na kuwapa ufahari, nguvu na uhalali.

Huko Kaskazini, Wafatimi, Waumayya na hasa Wamoravi walipata nguvu kutokana na dhahabu iliyoimarisha uhuru na athari yao. Aidha kushamiri kwa sanaa ambayo ilikuwa na ubora wa pekee na asilia kunaweza kusemwa kuwa kulitokana na utajiri ambao dhahabu ililetea falme hizi, na hasa kwa Wamoravi, na mahsuszi zaidi Moroko. Katika kipindi cha karne mbili sehemu za Kiislamu za Maghribi zikawa zimepata sura iliyokuwa muhimu sana.

Historia ya njia zilizounganisha maeneo ya Sahara ni ishara mojawapo nzuri, miongoni mwa nyingine nyingi, ya kuendelea kuhuishwa kwa utafiti juu ya Afrika. Kila ugunduzi una maana ya kupanga upya sura ya picha yenyewe. Katika miongo miwili shaba katika Mauritania na Air imegusa kabisa mfululizo mzima wa ruwaza zilizodumu. Je, kutatokea nini wataalamu watakapoanza kuutazama kwa makini upeo uliokuwepo wakati wa kusafirishwa nje kwa madini ya bati huko Bauchi katika enzi ya kale, au pale uchunguzi makini wa alama kuu nchini baina ya Chad na Nili utakapoonyesha kwamba njia zinazounga mashariki-Maghribi zimepuuzwa kwa kiasi kikubwa mno kwa kuzipendelea zile za Kaskazini-kusini?

Kwa mujibu wa haya yote, tumejaribu kufungua njia za uchunguzi, kuorodhesha vilivyopo na kutokeza njia za utafiti na mada za kufikiriwa kwa makini; badala ya kutoa picha ya 'mwisho' ya kuridhisha juu ya suala hili. Katika miongo mingi ijayo, kumbukumbu ya historia hii itabidi ibomolewe mara kwa mara na kuundwa upya tena kulingana na matokeo ya utafiti ambao hivi sasa uko katika hatua za mwanzo tu kwa yale yanayotarajiwa kufunuliwa.

## Ukanda wa Chad kama njia panda

Ukanda wa Ziwa Chad, ambao ni eneo la Savana, umekuwa ukikaliwa na wafugaji na wakulima tangu kabla ya enzi ya Ukristo. Kwa upande wa Kaskazini, ambako Savana polepole hubadilika kuwa jangwa, Wanomadi ndio walio wengi, ambapo kusini, hususani kwenye kingo za mito inayoingia katika Ziwa Chad, aghalabu hupatikana tamaduni za makazi ya kudumu. Kukauka kwa Sahara na kupungua kwa Ziwa Chad kuliwavuta watu kutoka pande mbalimbali kuja kwenye bonde lake lililokuwa likipungua. Mkusanyiko huo wa watu kutoka maeneo mbalimbali muhimu na majaribio ya watu kujinasibisha na mazingira na hali zinazobadilika ndio usuli wa historia ya eneo hilo.

Haiwezi kuchukuliwa tu kuwa, ukanda wa Ziwa Chad ulikuwa njia panda ya biashara na mahusiano yaliyowanufaisha waliohusika. Tarehe zinazojulikana za msambao wa mbimu za ufuaji chuma zinadokeza kwamba baadhi ya watu walikuwa wametengwa kwa muda mrefu na mikondo mkuu ya uvumbuzi. Mgawanyo mkuu katika jambo hili yaelekea kuwa wa kati ya Maghribi na mashariki kuliko kati ya Kaskazini na kusini. Kusini mwa Air, huko Ekne Wan Aparan, mbinu za uyeyushaji chuma zilikuwa zinajulikana miaka  $540 \pm 90$  kabla ya enzi ya ukristo. Penginepo, mbinu hizo za ufuaji wa chuma zilitumika muda mrefu baadaye. Huko Koro Toro, kati ya Ziwa Chad na Tibesti, kumegunduliwa mabaki ya utamaduni uliotokana na ufuaji chuma. Ukijulikana kama *haddad*, neno la Kiarabu lenye maana ya 'mhunzi' - utamaduni huo ulisitawi tu kati ya karne ya nne na ya nane ya enzi ya ukristo. Kwa mujibu wa tarehe zisizoaminika sana, chuma hakikupatikana kwenye eneo kuu la Daima mpaka baada ya karne ya tano au sita ya enzi ya ukristo, na hadi muda mrefu baadaye mbinu za uyeyushaji chuma zilikuwa hazijaanza kutumika. Ishara hizi chache zinaonyesha kuwa, kabla ya kuanzishwa kwa Kanem, kanda ya Ziwa Chad ilikuwa mashuhuri zaidi kwa inigawanyo yake na viwango visivyolingana vya maendeleo kuliko kwa kipengee chochote kingine cha mwunganisho.

Hatua za mabadiliko ya haraka na makubwa zaelekea zilikuwa zimeanza mnamo katikati ya kikwi cha kwanza cha enzi ya ukristo. Hatua hizo zilivuviwa kwa pembeni na kuingizwa kwa ngamia katika eneo hilo; ama kutoka Afrika Kaskazini au kama inavyoelekea zaidi kutoka bonde la Nili, na kuanza kutumiwa na Wazaghawa na Watubu.

Kati ya Fezzan na Ziwa Chad, hali za kimaumbile zilionyesha dalili njema ya uwezekano wa kuvuka Sahara: msururu wa oasisi ndogondogo na vidimbwi vidogovidogo vya maji na, katikati, oasisi kubwa ya Kawar; vikitoa fursa ya kuwepo njia nzuri kwa misafara. Fursa nyingine ya biashara ilikuwa kati ya eneo hili na bonde la Nili kupitia Darfur na Kordofan na

yaelekea kuwa, katika kipindi cha awali biashara hiyo ilikuwa ya muhimu zaidi. Kwa upande mwingine, kuwapo kwa ufalme wa kale wa Wagaramante katika Fezzan kwa hakika kulikuwa kipengee muhimu katika maandalizi ya biashara ya masafa marefu kwenye mhimili wa Kaskazini-kusini.

Mapema mnamo karne ya saba, njia ya katikati ya Sahara ilikuwa inatumiwa na misafara midogomidogo kutoka Fezzan, kwani mtamálaki mashuhuri wa Kiarabu 'Ukba b. Nafi angepata taabu kupenya hadi Kawar, endapo njia isingekuwa imefunguliwa kabla yake na baadhi ya wafanyabiashara ambao walikuwa Waberiberi au Wazaghawa. Katika nyakati zilizofuata, njia ya katikati ya Sahara ikawa muhimu zaidi, kutokana na kuanzishwa kwa biashara ya kawaida baina ya Ziwa Chad na pwani ya Mediterania kulikotokana na utamalaki wa Kiislamu na usitawi wa dola za Kiislamu huko Afrika Kaskazini na baadaye huko Sahara.

Huko kusini, kuzunguka Ziwa Chad, mfululizo mzima wa mambo, ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa silaha na zana bora na ugunduzi wa njia mpya za kupambana na mazingira yaliyobadilika, yalisababisha uasisi na upanuzi wa mamlaka makubwa ya kisiasa huko Kanem-Bornu.

### *Watu na lugha za kanda za Chadi*

Kabla ya Ibn Said (karne ya kumi na tatu), wanajiografia wengi wa Kiarabu wanawataja Wazaghawa wanapozungumzia Sudan ya kati (jina ambalo linavyotumiwa hapa lina maana sawa na ukanda wa Chad). Hadi karne ya kumi, waandishi wa Kiarabu wanadokeza kuwa Wazaghawa waliitawala Kanem; lakini, al-Idrisi, akiandika mnamo karne ya kumi na mbili, anataja sifa zao zinazodhihirisha asili yao kama Wanomadi halisi. Waandishi wa kisasa mara nyingi wamekuwa hawaitili uzito dhima ya Wazaghawa, ama kwa kuwatazama kama kikundi kidogo tu cha watu wasio muhimu, au kinyume chake, kama watu wa kikundi kikubwa sana, kinachofanana na Watubu wa leo.

Chanzo kikuu cha ndani, kwa jina *Diwan Salatin Barnu* kinataja jina la mbari ambalo haliwezi kuthibitishwa na chanzo chochote cha nje. Wanatarihi wa mfalme walifanya juhudi kubwa ya kuonyesha majina ya mbari ambamo wamtoka mlolongo wa mama-malkia. Tunajua kuwa wafalme wa Kanem waliwaoa wanawake wa Kitomaghra, wa Kikay na wa Kitubu. Mapokeo yaliyoandikwa katika *Diwani* hiyo yanataja miungano iliyofuatana baina ya wafalme wa Kanem na vikundi anuwai vya Wanomadi ambavyo ustadi wao wa kivita uliwasaidia wafalme wa awali kudumisha tawala zao.

Huko mashariki zaidi, baina ya Wazaghawa na Wanuba, al-Idrisi amewaweka Wataju, ambao kuwepo kwao, pengine tangu zama za kale, inaelekea hakukuzingatiwa na waandishi wa awali. Kwa mujibu wa mapokeo simulizi, Wadajo - ambao pengine ndio Wataju - walieta maendeleo ya kwanza ya Darfur kama dola. Katika karne ya kumi na tatu, inaelekea walikuwa wanashinikizwa na Wazaghawa ambao, baada ya kuondolewa madarakani huko Kanem, ni dhaliri walijaribu kurejesha tena mamlaka ya kisiasa yenye mshikamano kwenye ncha ya kusini ya njia kuu ya kuvuka Sahara iliyounganisha kanda ya Darfur na Misri. Kwa hakika, Wadajo walisalimu amri siyo kwa Wazaghawa, bali kwa Watunjur, wakikataa tu usimilishwaji kwa kukimbilia mafichoni. Kinyume na hao, Wazaghawa wenyewe waliweza kudumisha umoja wao wa kimbari, ingawa kwa hakika maeneo yao ya malisho yalikuwa yamepunguzwa inno kutokana na upanuzi wa Wateda-Daza (Watubu).

Katika enzi ya Dunama Dibalami (1210-1248), Wakanem walikuwa bado hawajawafukuza


mababu za Wabuduma kurudi katika visiwa vya Ziwa Chad, na ni vema kufikiria kuwa eneo lililokaliwa na Wakotoko lilitanda kuvuka nchi za udongo wa mfyanzi (*firki*) katika tambarare za matope yaliyolundikwa na Chari ya chini. Bonde la Komadugu Yobe lilikuwa bado limekaliwa na jamii za Wabede (ambao baadaye walisilimishwa na jamii ya Wakanuri au kurejeshwa nyuma hadi kwenye nchi za Wangizim); upande wa pili wa Ziwa Chad, Wakuri (ambao leo hii wamesilimishwa na Wabuduma) bado walikalialia 'ardhi nzuri' kwa upande wa Kaskazini wa kuingilia Bahr-al-Gazal. Kusini mwa ziwa waliishi Wakotoko, wakiwa na jina ambalo linaelekea ni la Wakanembu. Kwa hiyo katika kanda hizo zote, Wakanembu walikwishakuwa watu muhimu katika karne ya kumi na tatu, na inaweza kukubalika kwa urahisi kwamba katika nyakati za awali eneo lililokaliwa na wasemaji wa lugha za Kichad lilieniwa kwenye sehemu kubwa ya Kanem na Bornu.

Kusini mwa Ziwa Chad, Wakanembu walikutana na ustaarabu maarufu wa kale uliosifika kutokana na sanaa yake ya uumbaji sanamu. Wakazi wa tambarare za *firk* waliendeleza uchumi mchanganyiko katika kipindi cha mwanzo kabla ya enzi ya Ukristo, wakati ambapo kilimo kiliendeshwa pamoja na ufugaji na uvuvi. Kipindi cha pili, kilichoanza mwanzoni mwa enzi ya Ukristo, kilibainishwa na uanzishwaji wa mbinu za kufua chuma. Uvumbuzi huo mkubwa uliathiri uzalishaji na uendelezaji wa makazi ya kudumu: ongezeko katika shughuli za kilimo kuzipita kabisa shughuli nyinginezo - kama vile ufugaji na uvuvi. Kutokeza, katika kipindi cha pili, kwa usanifu majengo wa kutumia matofali ya tope, kunadhihirisha kuwa watu walikuwa wameanza kuishi katika makazi ya kudumu. Katika kipindi cha tatu, kilichoanza mwaka +700 hadi 1500, wakazi wa tambarare za *firki* walianza kufaidi na maisha yenye ahueni: vitu anuwai vilivyopatikana kutokana na biashara ya masafa marefu vilionekana kwa mara ya kwanza, mabaki yanapatikana pia ya tasnia ya ufumaji (ya muda mrefu kabla ya Uislamu). Wafyanzi wa Daima walianza kutengeneza magudulia makubwa sana ya udongo, ambayo leo hii wakazi wa kanda hiyo wanayatazama kama ishara bainifu za 'Wasao'. Uvumbuzi mwingine mkuu ulihusu ujenaji ngome. Kuanzishwa kwa majenzi ya ngome kulikuwa dalili za kwanza za tishio kutoka nje ambalo hapo baadaye liliathiri sana maisha ya wakulima wa tambarare za Chari. Tishio hili linaweza kubainishwa mara moja kuwa lilitokana na upanuzi wa Wakanem.

Wakazi wa siku hizi wa tambarare za *firki*, yaani Wakotoko, wanatumia lakabu ya *Sao* au *Soo* katika kuwataja mababu zao. Lakabu hiyo hiyo inatokeza tena na tena katika kila jimbo ambamo Wakanem walichukua nafasi ya wenyeji wa awali na ilitumiwa kwa maana ya wenyeji ambao hawakuweza kukataa kumezwa. Kwa hiyo, usemi 'ustaarabu wa Sao' lazima ulitumika kuelezea utamaduni uliokuwa unajulikana kwa kiasi kikubwa wa wahenga wa Wakotoko - maana inayolingana na matumizi yake ya siku hizi - na pia kuelezea utamaduni wa awali wa Komadugu Yobe na sehemu ya kusini ya Bahr al-Ghazal.

Isimu linganishi hutoa mambo kadhaa ya kuvutia sana. Inakubalika leo hii kuwa lugha za Kichadi zinaunda tawi la familia kuu ya Kiafrika - Kiasia. Mshikamano wa kikundi cha Chad waweza kuelezwa kwa kupitia mabadiliko ya muda mrefu ya mame -lugha katika mazingira ya kijiografia yaliyopendelea mawasiliano na mabadilishano ya kiusimu. Mwanzoni mwa kikwi cha tatu kabla ya enzi ya Ukristo, hali za maisha zilianza kuharibika haraka; na yawezekana kwamba wasemaji walikuwa wamekwishalazimika kukimbilia katika kanda za kusini zaidi. Kadri walivyoingiliana na vikundi vya Waafrika weusi, ndivyo walivyolazimika kupoteza polepole sifa zao za Kisudan-Kimediterrania. Leo hii vikundi anuwai vya wasemaji wa lugha za Kichad vimapatikana kati ya Niger na nyanda za Wadai.





15.1 Vitu vya shaba nyesi kutoka kwenye machimbo ya Houlouf (Kaskazim wa Cameroon (A. Holl)

Kati ya vikundi hivi, Wahausa tu ndio wameanzisha msukumo mpya, ambao matokeo yake ni juhudi za kueneza upya lugha yao.

Familia kuu ya pili ya lugha katika kanda ya Chad ni familia ya Kinilo-Sahara. Lugha ya upande wa Maghribi kabisa katika kikundi hiki ni Kisonghay, ambacho kinazungumzwa kote kandokando ya Mto Niger, toka Jenne hadi Gaya. Kikundi cha pili cha familia ya lugha ya Kinilo-Sahara ni cha lugha za Sahara, yaani (Kizaghawa, Kiteda-Daza na Kikanembu-Kanuri). Leo hii, mawasiliano yote baina ya lugha za Sahara na Kisonghay yamekoma; lakini, maumbo mengi ya kileksikografia yaliyomo katika makundi yote mawili ya lugha yanadokeza kuwa wafugaji wa Kisudan (na pengine wakulima pia) waliozungumza lugha za Kinilo-Sahara walikalia sehemu kubwa ya jimbo kati ya Kuruba kuu ya Mto Niger na milima ya Ennedi. Mwendelezo wa kijiografia wa utaratibu huu wa makazi lazima ulivurugwa na athari ya mchanganyiko wa kukauka kwa Sahara na kusonga mbele kwa Waberiberi wa Kilibya katika karne za mwisho kabla ya enzi ya Kristo. Kwa upande wa mashariki, watu waliozungumza lugha ya mame-Songhay walianzisha lugha ya Kikaw-kaw (Gao), wakati katika kanda wa Ziwa Chad wasemaji wa lugha ya mame-Sahara walitawala Kanem.

### Ufalme wa Wazaghawa

Kutajwa kwa mara ya kwanza kwa Kanem katika vyanzo vya maandishi kunafanywa katika mafini ya al-Yakubi mnamo mwaka 872. Mwishoni mwa karne ya kumi, al-Muhallabi

anatoa maelezo mengi kuhusu mfalme wa Wazaghawa, ambayo yanadhihirisha kuwa mipaka ya ufalme wake ilikuwa sawa na ile ya ufalme wa Kanem. Utawala wa Wazaghawa huko Kanem ulifikia mwisho wake mnamo mwaka 1075, ambapo nasaba tawala mpya, iliyojulikana kama Wasefuwa ilishika madaraka na kuwafurusha Wazaghawa kuelekea mashariki mwa ukanda huoambamo wamcendelea kuishi hadi hii leo.

Al-Yakubi anaeleza kuwa watu mbalimbali wa Afrika Maghribi aliowafahamu 'walimiliki falme zao', baada ya uhamaji wa muda mrefu toka mashariki hadi Maghribi: 'Ufalme wao wa kwanza ulikuwa wa Wazaghawa. Walijikita mahala paitwapo Kanem. Maskani yao ni vibanda vya matete, na hawana miji. Mfalme wao anaitwa Kakura. Miongoni mwa Wazaghawa kuna ukoo uitwao Hawdin: mfalme wao ni Mzaghawa'. Matini hii yaelekea kudokeza kwamba Wazaghawa walikuwa miongoni mwa wakazi wa awali wa Kanem, lakini baadaye, ingawa kulingana na hii haikuwa kweli. Kutajwa kwa Wahwdin' kama ukoo mahsusi miongoni mwa Wazaghawa kunaonyesha kuwa Wazaghawa kamwe hawakuwa watu wa aina moja.

Inaelekea kuwa umwinyi uliotawala, ambao ulitoa mfalme wa Kanem na mfalme wa Hawdin, ulitoa jina lake kwa kundi zima la watu waliokalia nchi zote mbili.

Haiyamkiniki kuwa Kanem ilianzishwa kutokana na uvamizi mkubwa uliofanyika na wahamaji wa vikundi mbalimbali kama wanavyodokezea baadhi ya waandishi. Nadhariatete yenye uhakika zaidi ni kuwa kikundi kidogo cha watu kilisababisha mkinzano mkali katika ukanda ambamo mbinu za kufua chuma zilikuwa zikijulikana tangu karne ya nne ya enzi ya ukristo (utamaduni wa *Haddad*), na ambako kumiliki farasi kulikuwa sio tu alama ya ufahari, bali pia uhakikisho wa nguvu kubwa zaidi za kupigana. Kikiwa na silaha zilizotengenezwa kwa chuma, kikundi hiki aibacho bila shaka kilikuwa cha Wazaghawa - asteaste kiliwatawala wakulima na wafugaji walioishi katika jimbo lililoko kusini-mashariki mwa Kawar, kati ya Ziwa Chadi na Bahr al-Ghazal - ukanda ambao hapo baadaye uliitwa Kanem. Umwinyi wa Kizaghawa ulioshika hatamu haielekei kama ulikuwa umekwishaiibuka Haiyamkiniki kuwa Kanem ilianzishwa kutokana na uvamizi mkubwa uliofanyika na hadi nadhariatete hii, Wazaghawa wote hawakuwa tofauti kimbari na makundi makuu ya wakulima na wafugaji ambao wao waliwatawala mwanzoni. Hivyo ni vema zaidi kuelezea kuibuka kwa Wazaghawa kwa kutazama uasisi na ukuaji wa dola ya Kanem kuliko kudadisi kuwa mbari moja ya awali ya Wazaghawa, ambayo ilikuwa na jinsi moja na iliyotofautiana na makundi mengine katika kanda hiyo, ilitamalaki jumuiya zote za wenyeji, na kwa namna hiyo, kuanzisha dola ya kwanza kubwa kuliko zote iliyowahi kuwepo kati ya Mto Nili na Mto Niger. Taarifa za awali kabisa za Wazaghawa, ambazo zinatolewa na Wabb b. Munabih, zinadokezea kwamba dola ya Kanem ilikuwa imekwisha kuwepo wakati alipoishi mwandishi huyu (takriban mwaka wa 730). Pauka ya Wazaghawa, matini huwataja pia Wanuba, Wazanji, Wafezzani, Wahabasha, Wakhufu na Waberiberi. Kwa mujibu wa ushahidi huu wa awali, Wazaghawa walitofautishwa *hijra*, yaani, mwanzoni mwa karne ya saba. Safari ya kivita ya Ukba b. Nafi huko Kawar katika siku za mwanzoni za utamalaki wa Waarabu inaonyesha umuhimu wa mabadilishano na Wafezzani (warithi wa Wagaramante) na Waberiberi. Ushahidi wote unaonyesha kuwa katika dhana ya Wazaghawa na ile ya Wakanem kuna hakika moja ya kihistoria: kutajwa kwa mara ya kwanza kwa Wazaghawa katika karne ya nane kwa hakika kuaelekea kudokeza kwamba dola kubwa kwenye ncha ya kusini ya njia ya katikati ya Sahara ilikuwa tayari ipo

wakati huo. Tunaweza kuweka tarehe ya kuanza kwa dola ya Kanem muda kidogo kabla ya *hijra*, yaani, mwanzoni mwa karne ya saba. Safari ya kivita ya Ukba b. Nafi huko Kawar katika siku za mwanzoni za utamalaki wa Waarabu inaonyesha umuhimu wa mabadilishano kati ya Kaskazini na kusini katika jimbo hilo. Hapana shaka udhibiti wa mabadilishano hayo ulikuwa mikononi mwa dola ya Kisudan iliyokuwa nje ya maeneo yaliyofikiwa na Waarabu.

Baadhi ya waandishi wanadhani kuwa Wasao ndio walikuwa wakazi wenyeji wa Kanem walioishi katika jumuiya za vijijini - au hata miji midogo iliyozungushiwa ngome - na walikuwa na mifumo ya kitemi tangu zama za zama. Baada ya kushindwa na Wazaghawa Wanomadi, hawa watawala wao wapya walijifunza kutoka kwao miundo ya kisiasa ambayo iliwawezesha kuanzisha dola kubwa.

Hakuna dhana yoyote katika nadharia hii ya uasisi wa Kanem yenye msingi thabiti. Wasao wanatajwa na vyanzo vya maandishi kwa mara ya kwanza mnamo katikati ya karne ya kumi na nne (katika *Diwan*), na wanatajwa pia na waandishi mbalimbali wa karne ya kumi na sita: wakati huo neno 'Sao' lilitumika kuita kundi la watu lililokalia mashariki na kusini-mashariki mwa Ziwa Chad na huenda walikuwa wakisema lugha za Kichad. Ni wakati wa upinzani wao wa muda mrefu dhidi ya upanuzi wa Kanem-Bornu ndipo watu hawa walipoendeleza aina za taratibu za kisiasa na kijamii ambazo ziliwapa sifa yao ya pekee.

Hakuna sababu ya kufikiri kuwa kulikuwapo na mgawanyo dhahiri, hususani katika tabia za kimbari, baina ya Wanomadi na watu wenye makazi ya kudumu, au baina ya wenyeji na wageni, katika zama za Kanem ya kale. Kinyume cha hayo, huenda kuna kiwango fulani cha uhusiano wa kitamaduni baina ya makundi ya wenye makazi ya kudumu na Wanomadi - kama unavyoendelea hadi hii leo kati ya Wakanembu, wenye makazi ya kudumu na Watubu na Wadaza wanomadi - na kama tutaikubali fikra hii, itakuwa rahisi kuelewa jinsi umwinyi kama ule wa Kizaghawa ulivyoweza kuwatawala watu wengine wote bila mgawanyiko baina ya makundi hayo mawili ya watu kudhihirika kwa watazamaji wageni waliokuja baadaye. Maelezo ya Al-Muhallabi yanadokeza ushirikiano wa amani baina ya wakulima na wafugaji, na madaraka ya kuchukua hatua za kushurutisha ni dhahiri yalikuwa mikononi mwa mfalme peke yake. Ufalme wa Wazaghawa hauonyeshwi kama ulikuwa wa watu wa jinsi moja tu. Kinyume na hivyo, mwandishi anaeleza mwanzoni kabisa kuwa ufalme huo una watu wa mataifa mengi (*umam*), ambayo yanadokeza wazi ushirikiano wa mbari mbalimbali ndani ya dola moja. Mwishoni mwa karne ya kumi, ni dhahiri ufalme wa Wazaghawa ulipanuka sana, na haukuwa tena umekomlea tu katika mipaka ya watu waliohusiana wasemao lugha za Sahara. Kwa mfano, Kanem yenyewe iliyokuwa kati ya Ziwa Chad na Bahr al-Ghazal, bado ilikuwa makao makuu ya ufalme huo, lakini watu wengine waliokuwa ukingoni mwake walitawaliwa pia. Haiwezekani kukana kwamba, tangu wakati huo, dola kubwa kuliko zote katikati ya Sudan ilichangia kwa kiasi kikubwa katika maenezi ya lugha za Sahara na usilimisho wa kitamaduni wa majirani zao.

Maendeleo mengine muhimu yaliyotokea wakati huo yalikuwa ongezeko la idadi ya jumuiya zenye makazi ya kudumu pamoja na uanzishaji wa miji midogo. Al-Muhallabi ametaja inajina ya miji miwili, Manan na Tarazaki. Mji wa Manan tunaufahamu pia kutokana na *Diwan*, na Ibn Said anaeleza ya kuwa huo ulikuwa makao makuu ya 'mababu wa kipagani' wa Wasefuwa. Lakini ni katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tatu tu ndipo baadhi ya makazi ya kudumu yaliposhika hatamu. Maendeleo hayo yalitokea sawia na maendeleo ya usilimishaji.

## Maendeleo ya usilimishaji

Imekwishathibitika kuwa Uislamu haukuhusika katika uanzishaji wa Kanem wala katika hatua za mwanzo za ukuaji wake. Huko Kawar, kwenye ncha ya Kaskazini ya Sudan ya kati, Uislamu ulipita tu wakati 'Ukba b. Nafi' alipokwenda huko katika safari ya uvamizi lakini pengine haukuacha athari kubwa. Ni katika karne ya nane tu, wakati Waberiberi wa Fezzan na Kawar waliposilimu kwa wingi, ndipo Uislamu ulipoanza kufika kanda za kusini zaidi.

Kama vile walivyo Waberiberi wengi, wakazi wa Fezzan mwanzoni walikuwa waumini wa madhehebu yaliyokengeuka ya Kiislamu, yaani Uibadi, na hivyo wakaungana na faraka ya Kikhariji, na inawezekana kabisa kuwa aina ya mwanzo ya Uislamu iliyohubiriwa kusini mwa Sahara na wafanyabiashara wa Kiberiberi, kwa hakika, ilikuwa ya Uibadi.

Huko Fezzan, hali ilibadilika katika karne ya kumi, wakati nasabatawala mpya ya Banu Khattab ilipotawala: baada ya tukio hilo, wanajiografia wa Kiarabu hawataji tena imani zilizokengeuka za Waberiberi wa Fezzan, na kuna uwezekano kwamba mabadiliko ya kisiasa yalibadilisha pia mikondo ya imani za kidini.

Mnamo nusu ya pili ya karne ya tisa, Kawar ilikuwa imekwishakaliwa na Waberiberi ambao kazi yao kubwa inaelekea ilikuwa biashara ya watumwa. Watu wengine waliokuwa wanaishi huko huenda walikuwa Wasudan; na hata katika kipindi hicho cha awali yawezekana watu hao walikuwa Watubu, ambao siku hizi wanaishi huko pamoja na Wakanuri. Watumwa wengi ambao waliletwa Fezzan na wafanyabiashara wa Kiberiberi na Kawar bila shaka walitokea Kanem, ambako mfalme wa Wazaghawa aliwafanya watumwa wale miongoni mwa raia wake ambao alipenda kuwafanya hivyo.

Lakini, wakati huo wafalme wa Kanem yaelekea walikuwa wamekwishaanzisha mahusiano ya kibalozi na dola za Kiislamu za Afrika Kaskazini. Vyanzo vilivyopo vinatoa maelezo yafuatayo: katika mwaka wa 992 Ibn Khattab, gavana wa Zawila, alipokea zawadi kutoka nchi mojawapo ya *bilad - al Sudan* ambayo haikutajwa kwa jina, lakini ambayo, kutokana na nafasi ya kijiografia ya Zawila, inawezekana ilikuwa Kanem. Katika mwaka huohuo, sultani kiziri wa Ifrikiya, al-Mansur (984-996), vilevile alipokea zawadi kutoka nchi fulani ya *bilad al-Sudan*, ambayo nayo jina lake halikutajwa. Mnamo mwaka 1031 mmoja katika warithi wake, al Muizz (1016-1062) ahpokea zawadi ya watumwa kutoka kwa *malik al-Sudan* mmoja. Ama kuhusu kipindi cha baadaye, Ibn Khaldun anatumaeleza kuwa wafalme wa Kanem walikuwa wanawasiliana na nasabatawala ya Kihafsid (1228-1347) toka wakati wa kuasisiwa kwake, na hususani anatoa taarifa kuwa katika mwaka 1257 'Mfalme wa Kanem na Bwana wa Bornu' alimpelekea twiga sultani wa Kihafsid, al-Mustansir (1249-1277), ambaye aliwastaajibisha sana watu huko Tunis. Si jambo la kushangaza kuwa mfalme huyo, ambaye alikuwa mmojawapo wa wauzaji wakubwa wa watumwa na ambaye kwa namna alikuwa na ukiritimba katika upatikanaji wao ndani ya nchi yake mwenyewe, alikuwa na uhusiano mzuri na wateja wake wakuu.

Mahusiano ya kibiashara na nchi za Afrika Kaskazini na mawasiliano ya mara kwa mara na wafanyabiashara wa Kiislamu yasingeweza kuendelea kwa muda mrefu pasi kuwezesha Uislamu kupata mashiko ya kutosha miongoni mwa watu walio karibu na mfalme na sehemu fulani za watu. Pengine itakuwa makosa kuangalia maendeleo ya Usilimishaji wa Kanem kana kwamba ulikuwa wa mfululizo pasi kusita. Litakuwa jambo la ajabu iwapo mfalme na mamwinyi wa Kizaghawa hawakujaribu kuzuia harakati ambayo ilitishia kusaliti mfumo wa kiuchumi ambamo walau sehemu ya madaraka yao yalikitwa. Kwa mujibu wa *Diwan*, Arku

b. Bulu (tk.. 1023 1067), mmojawapo wa wafalme wa mwisho wa Kizaghawa, alianzisha makoloni ya watumwa katika oasisi kadhaa za Kawar na hata huko Zayla katika Fezzan ya kusini-kanda ambayo leo ni sehemu ya Libya. Ni jambo linaloeleweka kwamba Arku b. Bulu alilazimika kupanua utawala wake juu ya jumuiya za Kiberiberi za Kawar ili aweze kudhibiti vizuri zaidi amali zao za kibiashara na uhabari wao wa kidini. Tunajua kuwa, katika kipindi hiki, mfalme wa Ghana alikuwa akipanua mamlaka yake juu ya kituo muhimu cha biashara cha Awdaghust, na huenda uunganishaji wa maendeleo hayo haukutokea kwa bahati.

Mrithi wa Arku alikuwa mfalme wa kwanza wa Kiislamu wa Kanem. Jina lake limetajwa katika *Diwan* katika maumbo matatu tofauti: Ladsu, Su (au Sawa) na Hu (au Hawwa) - umbo sahihi bila shaka ni Hu (au Hawwa). Waandishi wa *Diwan*, wakielezea tukio hilo muhimu katika historia ya ukanda wa Chadi, ambalo lilikuwa la mfalme wa Kiislamu kutwaa madaraka ya ufalme wa Kanem, walitosheka na maelezo haya mafupi mno: yeye alitawazwa na Khalifa (*Diwan*, 10). Si namna ya kutawazwa kwake wala umbo la jina la mfalme wa kwanza wa Kiislamu vinakubaliana na nadhariatete ya kuongolewa kwake katika dini. Kinyume chake, kuna uwezekano mkubwa kwamba baada ya kifo cha Arku (huko Zayla), kikundi kilichounga mkono Waislamu katika ukootawala wa zamani kilimhudhurisha mgombea madhubuti kabisa kiliyeweza kumpata. Kwa kuwa hakuna ushahidi mwingine, hatuwezi kukataa uwezekano kuwa kwa hakika Hu (au Hawwa) - kama vile baadhi ya ishara zinavyodokeza - alikuwa mwanamke mwenye jina halisi la Kiislamu la Hawwa. Alitawala kwa miaka minne tu na alirithiwa na 'Abd al - Djalil, ambaye pia alitawala miaka minne. Mfalme aliyefuata, Hummay, alikuwa wa kwanza katika ukootawala mpya, wa Wasefuwa. Utawala mfupi mno wa Hu au Hawwa (c. 1067-1071) na 'Abd al-Jalil (1071-1075) unatofautiana na tawala za wafalme waliotangulia na hiyo inaweza kuchukuliwa kuwa ni dalili ya mgogoro mkubwa: baada ya kipindi kirefu cha kungojea, hatua muhimu ilipofikiwa ya kuongezeka nguvu kwa Uislamu, Waislamu kwanza waliuyumbisha utawala wa zamani na baadaye walisababisha mabadiliko makubwa ya kisiasa.

### *Majilio ya Wasefuwa*

Kwa sadfa ya ajabu mabadiliko ya kinasaba yaliyotokea huko Kanem mnamo mwaka 1075 hayaelezwi kwa kinaganaga katika nyaraka zilizoko. Mwishoni mwa aya ambamo *Diwan* inamzungumzia Abd al-Jalil, kuna kifungu cha kustaajabisha cha maneno ambacho maana yake haijafahamika kwa wanahistoria wengi, nacho husema: 'Hayo ndiyo tuliyoandika kulusu historia ya Banu Duku; sasa tutaendelea kueleza historia ya Banu Hummay, ambao waliutangaza uislamu'. Maelezo haya yamechukuliwa kuwa yanaashiria tu kupokelewa kwa Uislamu na siyo mabadiliko ya nasabatawala - kwa vile waandishi wa *Diwan* wanadokezea katika maelezo baadaye kuwa mfalme aliyefuata alikuwa Hummay, mwanae Abd al-Jalil. Hata hivyo, tumekwishaona hapo awali kuwa Hu (au Hawwa) alikuwa mwislamu, kama alivyokuwa mrithi wake, Abd al-Jalil, na jambo hilo lisingeweza kuwapita wanatarihi. Kwa hiyo, kifungu cha maneno kilichonukuliwa hapo lazima kinahusu jambo tofauti na lile la kuingia kwa Uislamu.

Ni mwandishi wa karne ya kumi na nne, Ibn Fadl Allah al-Umari, ambaye ndiye alipanga mfuatilio wa mtiririko wa matukio ifuatavyo: Wa mwanzo kuleta Uislamu (huko Kanem) alikuwa al-Hadi al-Uthmani ambaye alidai kuwa alikuwa mmojawapo wa vizazi vya Uthman b. Affan. Baada yake (Kanem) ilitakwa na Wayazaniyyuni wa Bani Dhi Yazan'. Ama kwa

hakika Wayazaniyyuni waliotajwa na al-Umari hawakuwa wengine, bali Wasefuwa ambao wamepata jina hilo lao kutokana na jina la Sayf b. Dhi Yazan. Mwandishi ananena kuwa Wasefuwa walishika madaraka baada ya kufika Uislamu.

Ukale wa mapokeo ambao unaficha mabadiliko ya nasabatawala kwa kusisitiza kusilimu unathibitishwa na Ibn Said, ambaye anatoa ushahidi wa awali wa kuwepo kwa nasabatawala iliyodai kutokana na Sayf b. Dhi Yazan huko Kanem:

Sultani wa Kanem ... ni Muhammad b. Jil wa aila ya Sayf b. Dhi Yazan. Mji mkuu wa mababu zake makafiri, kabla hawajasilimu, ulikuwa Manan; kisha mmoja wao, babu wa babu wa babu yake, alisilimu baada ya kuhubiriwa na shekhe mmoja, na baada ya hapo Uislamu ulienea kotekote nchini Kanem.

Kwa hakika, babu wa babu wa babu ya Muhammad b. Jil (=Dunama Dibalami) alikuwa Hummay (tk. 1075-1086) naye, kama tulivyokwishona, hakuwa mfalme wa kwanza wa Kiislamu wa Kanem, na wala haiwezekani kuwa ndio kwanza alikuwa amesilimu. Kipengele kimoja tu katika maelezo haya kinaehusiana moja kwa moja na badiliko la nasaba ni badiliko la makao makuu: ambayo kwanza yalikuwa Manem, na baadaye Njimi.

Mwanajografia mwingine wa Kiarabu, al-Bakri, alipokuwa akiandika katika mwaka 1067-1068, anatueleza mahala pa kuishia katika majilio ya Uislamu huko Kanem na katika badiliko la nasabatawala. (Wakazi wa Kanem) ni Wasudani waabudu sanamu. Inasemekana kuwa katika sehemu hizo kuna ukoo ambao ni kizazi cha Waumayya ambao walikimbilia huko walipokuwa wanateswa na Waabbasi. Wanavaa Kiarabu na kufuata desturi za Waarabu'.

Hatujui kwa hakika maelezo hayo yanahusu kipindi kipi, lakini haiwezi kuwa baada ya 1067-1068. Kwa mujibu wa tarihi inayotokana na *Diwan*, huo ndio mwaka ambao mfalme wa kwanza wa Kiislamu, ambaye alikuwa bado sehemu ya nasabatawala ya kale ya Wazaghawa, alishika madaraka katika ufalme wa Kanem. Ama kuhusu 'Vizazi vya Waumayya' ambao 'walivalia Kiarabu' na kwa hivyo, hawakuwa Waarabu, basi huenda walikuwa kikundi cha Waberiberi ambao walifuata desturi fulani za Waarabu. Kikundi hicho yawezekana kilikuwa kimojawapo eha wale watu ambao hapo baadaye walichangia katika kufanikisha ushindi wa washabiki wa Uislamu katika nasabatawala ya kale kabla ya kujangusha nasabatawala hiyo.

Kutokana na maelezo yaliyotolewa na al-Idrisi (ambaye aliandika katika mwaka 1154) inadhihirika kuwa, katika wakati wake, 'Wakanem' na 'Wazaghawa' walikuwa watu wa mataifa mawili tofauti. Wazaghawa walikuwa hawawatawali tena Wakanem: walipopoteza maslahi yao ya kale, inaelekea Wazaghawa walikuwa wanaishi katika hali mbaya. Wengi wao yaelekea walikuwa Wanomadi. Miji yote miwili ya Manan na Njimi imetajwa, na mji wa Manan yaelekea ulikuwa muhimu zaidi, lakini haijulikani kama ulikuwa mji mkuu wa Kanem au la. Hakuna maelezo yanayotolewa kuhusu hali ya kidini.

Kutokana na yaliyotangulia itadhihirika kuwa badiliko la nasabatawala na majilio ya Wayazaniyyun vilitokea kati ya nyakati za al-Bakri (1067-1068) na al-Idrisi (1154). Wakati huo badiliko la nasaba linaelekea lilisadfiiana na kufukuzwa kwa Wazaghawa kutoka Kanem. Uchanganuzi wa *Diwan* unapunguza muda wa tukio hilo, ambalo ni la muhimu sana katika historia ya Sudan ya kati hadi mwanzoni mwa enzi ya Hummay (tk. 1075- 1086) kwa sababu aliyemtangulia, Abd al-Jalil, alikuwa mfalme wa mwisho wa mlolongo wa *Wabanu-Duku* na Hummay ilikuwa awe wa kwanza katika mlolongo wa *Wabanu Hummay*. Tofauti hii inayoonyeshwa kati ya nasabatawala hizo mbili za kifalme inamaanisha kuwa kulikuwapo

ukatisho mkubwa katika mfululizo wa nasabatawala; haisadifiani na majilio ya Uislamu.

Hao wafalme wanya wa Kanem walikuwa nani? *Diwan* haitoi jibu la swali hilo. Wakati wakimhusisha Hummay kishajara na aliyemtangulia, waandishi wa *Diwan* hawasemi lolote kuhusu jadi yake halisi ya upande wa baba. Lakini, mapokeo ya Kanem na Bornu ambayo yameandikwa katika zama za karibuni kwa jumla yanaeleza kuwa nasabatawala hii mpya ilitokana na Sayf b. Dhi Yazan.


Tunajua kuwa ni katika utawala wa Hummay au wa warithi wake, ndipo ilitokeza *nisba* ya Kisayfu. Sayf ibn Dhi Yazan alikuwa shujaa wa Kiyemeni, ambaye kwa mujibu wa ngano alisaidia kuwaondoa Waethiopia kutoka Yemen katika nusu ya pili ya karne ya sita katika enzi ya ukristo. Na inafahamika kwamba Waberiberi wa Afrika Kaskazini walipenda kudai kuwa ni wazaliwa wa Kiyemeni ili kujitofautisha na Waarabu wa Kiadnani wa Kinajd na Kihjaz. Mwelekeo huu ulikuwa sawa katika uwanja wa shajara na upokeaji wa imani iliyokengeuka ya Kikhariji katika mambo ya kidini.

Hapana shaka kuwa ni Waberiberi ndio walioleta dhana hii ya kishajara katika mazingira ya Waafrika weusi wa Sudan ya kati. Wasingeweza kuwa Wasudan au Waarabu, maana wote wawili hao walikuwa na shajara zilizoheshimika. Lakini kwa upande wa pili, Waberiberi walionea fahari asili yao ya Kiyemeni ya Kihimyari. Mashehe wa Kiislamu wa Kiberiberi ambao walitukuza *nisba* ya Kisayfi bila shaka walivutiwa pia na mlingano wa maana au matumizi kati ya 'Kanem' iliyomaanisha kusini mwa Teda-Daza, na 'Yemen' ambayo mara nyingi katika msimo ilitumika kwa maana ya kusini.

Kinachoweza tu kuelezwa hapa ni kwamba yaelekea Wasefuwa walikuwa watu wa shajara tofauti na watangulizi wao Wazaghawa na kuwa ushikaji wao wa madaraka haukuhusiana na majilio ya Uislamu, kwa sababu Hummay hakuwa mfalme wa kwanza wa Kiislamu wa Kanem. Ingawa hakuna ushahidi thabiti wa kuonyesha kuwa Wasefuwa hawakuwa wa asili ya pale, halikadhalika hakuna ushahidi wowote thabiti wa kusema kwa yakini kuwa wao walikuwa na asili ya pale.

Imedhihirika kuwa usilimishaji wa Sudan ya kati ulianza kwa kuwageuza dini wakazi wa Kavar, ambao baadaye walikuwa ndio watu walioeneza Uislamu katika ufalme wa Wazaghawa. Katika enzi ya Hummay (1075 - 1086), upenyaji wa taratibu wa Uislamu katika sehemu mbalimbali za watu ulikwishaendelea walau kwa karne mbili. Hatimaye mamlaka za kisiasa ziligutuka, maana maendeleo hayo lazima yangedhoofisha mamlaka kamili ya mfalme juu ya raia wake, na papohapo, kusaidia kudhoofisha hadhi ya umwinyi wa Kizaghawa.

Lakini, mwishoni mwa karne ya kumi na moja, Uislamu ulikuwa bado katika mipaka ya wachache waliohusika na mfalme na mamwinyi, na ni baada ya muda mrefu tokea hapo, katika enzi ya Dunama Dibalami (tk.1210-1248) wakati Uislamu ulipokuwa chombo cha sera ya upanuzi, ndipo uliweza kupunguza tofauti kati ya watawala na watawaliwa na kwa njia hiyo kuwa dimi ya umma hasa.



## *Ukanda wa Guinea:*

### *hali ya jumla*

#### *Utangulizi*

Wakati fulani Thurstan Shaw alielezea miaka elfu moja kabla ya + 1000 katika Afrika Maghribi kama 'kikwi sukutu'.<sup>1</sup> Alionyesha ni jinsi gani usukutu (ukimya) huo ulivyoweza kuathiri ujuzi wetu wa historia, kwani wakati huo lazima ndio uliokuwa na vipindi vya awali vilivyokuwa muhimu kwa kuzuka baadaye kwa falme na vituo vya kidini ambavyo tunaweza kuona kuwepo kwao mwishoni mwa kikwi hiyo au mwanzoni mwa kikwi iliyofuata. Katika karni zilizofuata sio tu tunaanza kupata kumbukumbu za kihistoria bali pia kuwa uhusishaji wa kazi za sanaa na asasi za kijamii na kisiasa zilizojeneka katika kiini kimoja, umewavutia wanaakiolojia na wanahistoria wa sanaa. Hata hivyo, lazima tujaribu kuunganisha picha hiyo kwa kadri inavyowezekana; wakati mwingine kazi hii inaweza kuhitaji kurekodi tu data tulizo nazo pasi kuweza kuzifasiri vizuri au kuziweka pamoja katika mpango wa jumla wa hali ya mambo.


#### *Upanuzi wa kilimo*

##### **Maendeleo ya Awali**

Badiliko la hali ya maisha ambalo ni la muhimu sana kwa kipindi chetu ni badiliko kutoka kwenye maisha ambayo msingi wa kuishi ulikuwa kwenye uwindaji, ukusanyaji na uvuvi na kuingia katika maisha yaliotegemea kilimo na ufugaji. Tusilichukulia hadiliko hili kama ni kuachana ghafula na ukale, au kama kitendo kipa kabisa kilichoingizwa ghafla kwenye eneo hili. Yamkini kulikuwapo na 'viwango' vingi vya kilimo na uzalishaji chakula; mwanzoni upandaji mbegu wa kwanza uliopangwa wa nafaka asilia za Kiafrika kusini mwa Sahara huenda ulikuwa mbinu ya kutapatapa ya wavuvi wastakimu na nusu-wastakimu katika kipindi cha ukame kuongezeka. Kutokana na kupungua kwa maeneo ya maji ambamo wangeweza kuvua samaki kiasi kikubwa zaidi cha chakula labda kilipatikana kutokana na nafaka-pori, kuliko ilivyokuwa awali, lakini wakati huohuo nyasi zingezidi kupungua na kutafutiwa mbali zaidi. Kwa hiyo hatua ya kimantiki iliyochukuliwa ilikuwa ni kuotesha nyasi kwa wingi zaidi karibu na makazi ya watu, kwa kupanda mbegu karibu na maziwa na mito iliyokuwa ikianza kukauka. Mwanzoni, upandaji ulichukuliwa kuwa ni hatua ya muda, lakini jinsi muda ulivyozidi kupita ndivyo ulivyozidi kutegemewa. Mara binadamu walipoanza kufululiza katika kuenea nyasi za nafaka, mabadiliko ya kijenetiki yakaanza kutokea ndani mwao.

<sup>1</sup> Taz. Sura 24 ya juzuu hili.





16.1

Kanda ya Guinea sehemu zilizotajwa kwenye matani (T Shaw)

Matokeo yake yakawa ni hatua ya 'kuzifuga' nyasi hizo na kuzifanya ziwe bora zaidi kwa ajili ya kulimwa, kuvunwa na kuliwa.

Mfano mwingine unaotolewa ni ule wa zao-mti muhimu sana la kanda ya Guinea- mchikichi. Kuna hatua ndogondogo tu kati ya ukusanyaji wa kokwa-pori zilizoanguka kutoka mitini, kuchukua hatua ili kuzuia kokwa zote zilizoanguka zisiliwe na wanyama, kukwea mti ili kupata kichane kizima cha kokwa; kuihifadhi miche ya michikichi asilia dhidi ya wanyamapori, moto au magugu; kuwapa watu binafsi au familia haki za kumiliki mti fulani au maeneo ya miti; na mwisho upandaji kwa makusudi mbegu za michikichi. Kwa hivyo, badiliko hilo si lazima liwe la ghafula, bali hata hivyo mahali fulani katika mlolongo huo badiliko limetokea kuanzia kwenye ukusanyaji wa matunda-pori hadi uzalishaji chakula kwa mpango.

### Mazao

Nafaka muhimu kuliko zote katika savana ilikuwa mawelee (*Pennisetum americanum*), aina fulani ya mtama (*Sorghum bicolor*), na aina mbili ya 'fonio' au 'mpunga njaa' (*Digitaria exilis* na *D. iburua*). Katika Futa Jallon, nyasi (*Brachiaria deflexa*) iliotesywa, na mpunga wa Kiafrika (*Oryza glaberrima*) ulikuwa mwingi katika schemu ya Maghribi ya kanda ya Guinea. Katika savana za kusini na misitu ya sehemu ya mashariki, viazi vikuu vya Kiafrika vilivyolimwa vilikuwa ndivyo chakula kikuu, hususani *Dioscorea cayanaensis* na *D. rotundata*. Inawezekana kuwa mchanganyiko wa chakula uliotokana na viazi vikuu na mawese vikijaliziwa na protini kutoka katika samaki, mbuzi, ng'ombe kibushuti na nyama-pori (pamcja na konokono) unaweza kusaidia kuelezea sababu ya kuongezeka kwa idadi ya watu katika Nigeria ya kusini.

### Maradhi

Vilevile ilipofikia karne ya saba kupata jeni ya seli manjali kungeweza kuwa kumeongezeka hadi kwenye viwango vya kuwalinda watu fulani dhidi ya malaria; mwanzoni uanzishaji wa mbimu za kilimo na njia za kuishi uliongeza namna za kupata ugonjwa wa malaria. Mazingira yaliyotokana na kufyeka maeneo ya misitu kwa ajili ya kilimo yalikuwa yanasaidia kueneza malaria: visima vilivyo wazi, na takataka za nyumbani (kama vile vibuyu vilivyotupwa) za kijiji cha kilimo huwa ni mazingira yanayofaa kwa mbu kuzaliana; na paa na pengu za vibanda vilivyozekwa kwa majani huwapatia mbu sehemu zenye giza za kujifichia mchana. Hatujui hasa hasa kuwa ni lini au vipi uzaanaji wa jeni za manjali ulitokea. Kama mtoto akiambukizwa maradhi hayo na wazazi wake, hufa kwa maradhi ya seli manjali kabla ya kubalehe; kama akiupata ugonjwa huo kutoka kwingineko huwa hatarini kufa kwa malaria kabla hajabalehe; lakini, kama atayapata maradhi hayo kutoka kwa mzazi mmoja tu, hatakufa kwa ugonjwa wa seli manjali na huwa na kiasi kikubwa cha kinga dhidi ya malaria. Pale ambapo seli manjali hutokea kwa wingi katika idadi ya watu, mara zote huwa kwenye maeneo yenye malaria kwa wingi. Imehesabiwa kuwa ni lazima ilichukua kiasi cha miaka 1500 kukua na kufikia kiwango kilichorekodiwa katika Nigeria ya Kaskazini mashariki; ukuaji huo huenda ulikuwa wa polepole zaidi katika maeneo yasiyo ya unyevunyevu sana.

### Aina za kilimo na maskani

Kwa hiyo, tunachoweza kutazamia mwanzoni mwa kipindi chetu ni kucnea kwa wakulima wa vijijini. Katika maeneo kadhaa, msongamano wa watu na ekolojia ya eneo viliwezesha kuwepo na makazi ya kudumu, na kucndelea kwa vizazi vingi; katika maeneo mengine, mahitaji ya chakula ya jumuiya yalifikia hali ambapo ilikuwa ni kazi rahisi zaidi kwa kijiji kuhamia kwenye eneo

lisilolimwa, au lile ambalo halikulimwa hivi karibuni. Hivyo, mfumo wa kawaida wa kuacha shamba bila kulilima muda mrefu ulianzishwa. Pale ambapo vijiji vilibakia kwenye sehemu moja kwa vizazi na vizazi na nyumba za tope zikajengwa kwenye magofu ya watangulizi wao kila baada ya miaka kumi mpaka ishirini, usawa wa ardhi ya kijiji hicho uliunuka juu ya maeneo yaliyokizunguka na kufanya vichuguu. Vichuguu kama hivyo vinaanza kutambuliwa na wanaakiolojia na vichache kati ya hivyo vimekwishachimbuliwa, lakini haiwezekani kupata maelezo kamili kwa kuchimba eneo moja tu.

Aina nyingine ya eneo la kijiji haionekani kwa urahisi; eneo hilo linaweza kutambuliwa tu kutokana na mtawanyiko wa vigae unaoonekana juu ya ardhi, wakati pale penye mimea eneo hilo halionekani. Hiyo ndiyo sababu tunajua machache zaidi kuhusu vijiji vya awali vya kilimo visivyodumu kuliko tunavyojua kuhusu maeneo yaliyokaliwa na wawindaji na waokotezaji wa Enzi ya Baadaye ya Mawe, ambao walikuwa na tabia ya kurudi mara kwa mara kwenye majabali na mapango ya kujisetiria. Mapango na majabali ya kujisetiria kama hayo aghalabu yalitumiwa kwa muda na wakulima wa baadaye wenye kutumia chuma, kwa ajili ya kujihifadhi au kama makao ya kufaa wakati wa shughuli za kilimo, lakini mara chache tu sehemu hizo zilifanywa kuwa mastakimu ya kudumu. Tofauti na mapango ya namna hii ni mapango ya Tellem ya genge la Bandiagara huko Mali, ambapo vifaa vya kiakiolojia na vya viunzi vilivyopatikana mapangoni vimechunguzwa kwa makini. Wadogoni wanaoishi hapo hivi sasa wanaelezea masalia hayo kuwa yanahusiana na 'Watellem'. Tarehe za radiokaboni zinaashiria kuwa ukaaji wa 'Watellem' mapangoni humo ulianza mwishoni kabisa mwa kipindi tunachokizungumzia na uliendelea kwa muda wa karne mbili au tatu. 'Watellem' mwanzoni walidhaniwa kuwa walihamia mashariki katika Burkina Faso ya sasa na kuwa ndio ni mababu wa Wakurumba wa leo walioko huko. Hata hivyo, uchunguzi wa anthropolojia ya maumbile ya Wakurumba na ya viunzi vya Watellem unaashiria kuwa watu hao wanahitilafiana kijeni.

### *Upanuzi wa Metalujia*

Katika sehemu kadhaa za eneo hilo, uyeyushaji wa chuma tayari ulikwishakuwa unafanyika kwa miaka elfu moja. Tarehe za radiokaboni za eneo la 'utamaduni wa Nok' wa Tuga zinaashiria kuwa uyeyushaji chuma ulikuwa unaendelea huko tangu karne ya nne kabla ya enzi ya Ukristo; katika eneo la Hani, huko Ghana, tarehe za radiokaboni inaashiria karne ya pili ya enzi ya Ukristo. Tarehe za radiokaboni katika karne ya saba zinahusishwa na makalibu ya uyeyushaji chuma huko Nigeria kutoka chini ya kilima cha Dala huko Kano na katika bonde la Kubanni karibu na Zaria. Eneo hili, ambalo liko karibu na chanzo kizuri cha matapo ya lateriti, lilibaki kuwa kituo cha kimapokeo cha uyeyushaji chuma kwa muda wa karne kadha. Kusini mwa Mto Niger kikundi cha makalibu ya kuyeyushia chuma yaliyochimbuliwa huko Ufe ljummo yalianzia katika karne za tisa na kumi na mbili na yaliishia karne ya kumi na nne.

Mbali na makalibu halisi ya kuyeyushia chuma, maeneo kadhaa ya makazi hivi sasa yanaonyesha matumizi ya chuma tangu mwanzo wa enzi ya ukristo, na mengi zaidi ilipofikia katikati ya kikwi cha kwanza. Vichuguu vya makazi ya watu katika sehemu za bonde la Mto Niger zilizofurikishwa na ziwa Kainji na katika bonde lililokuwa karibu la Kaduna vinaonekana ni vya tarehe - 130, + 100 na + 200. Tarehe za awali kabisa za makazi yaliyodhaniwa kuwa ni makao makuu ya Mali huko Nyani, na ya Ife, ni za karne ya sita halikadhalika na tarehe za awali kabisa ambazo pia zilipatikana za matumizi ya chuma katika eneo la Benue (makutano ya Mayo-Kebbi huko Kameruni). Katika eneo la Daima, Kaskazini - mashariki mwa Nigeria kusini mwa ziwa Chad,

tarehe inayokisiwa ni ya mapema zaidi kidogo. Baadhi ya vichuguu-simbi vya Kasamansi vilikuwa vikilundikana tangu mwanzoni mwa kipindi chetu kutokana na tabia za watu waliotumia chuma kukusanya chakula; utafiti umedokezea kuwa ni wahenga wa wakazi wa siku hizi, Wadiola, ambao ndio waliishi katika eneo hilo. Inaelekea kuwa vichuguu-simbi vya Dioron Boumak katika delta ya Saloum huko Senegal vilianza kwenye miaka ya mwisho ya karne ya nane, na kuzidisha matumizi ya rasilmali zitokanazo na shaza kuanzia karne ya kumi na moja.

Yamkini kuenea kwa teknolojia ya chuma hakukuwa kwa namna moja. Ingawa teknolojia hiyo ilikuwa inafahamika huko Taruga karne kadha kabla ya enzi ya Ukristo, haikutumika kwingineko katika eneo la Guinea mpaka baada ya miaka elfu moja au zaidi. Katika kipindi hiki, lazima ilikuwapo mifano mingi ya watu wenye teknolojia ya Enzi ya Baadaye ya Mawe walioishi si mbali sana na watu waliokuwa wakitumia chuma. Mfano wa hali ya aina hii unaweza kuonekana Kaskazini mwa Sierra Leone. Kambai, sehemu ya juu kabisa, yenye zana za chuma, mavi ya chuma na vigea iliotoa tarehe za radiokaboni kwenye karne ya saba na ya nane, wakati huko Yagala teknolojia ya Enzi ya Mawe ya Nyuma iliendelea hadi karne ya kumi na moja. Hatutapata picha sahihi ya kihistoria ya kuenea kwa matumizi ya chuma Afrika Magharibi mpaka tuwe na maeneo mengi yaliyochimbwa na yaliyopewa tarehe za vipindi vinavyohusika katika maeneo wakilishi mbalimbali.

Licha ya hali hii ya kutokuwa na uwiano wa ueneaji wa ujuzi wa ufuaji chuma, tunaweza kuchukulia kuwa hadi mwanzoni mwa kipindi chetu ujuzi huu ulikuwa umeenea sana; ilipofikia mwisho wa kipindi hiki, lazima kulikuwa na vijishehemu vichache vya teknolojia ya Enzi ya Mawe vilivyobakia, ingawa inayumkinika kuwa baadhi ya zana za mawe zilicndelea kutumika.

## Biashara ya Ndani

Hapana shaka mojawapo ya matokeo muhimu ya ueneaji wa chuma ilikuwa ni ongezeko la ustadi wa uzalishaji wa mazao ya kilimo. Majembe ya chuma na zana za kufyeka mapori vilisaidia kuleta ziada ya mazao ya kilimo ambayo yanatoa nafasi zaidi ya mgawanyo wa kazi, kumakinikia kazi za ufundi, na hatimaye maendeleo ya miji na ugharimiaji makazi ya wafalme na makuhani. Kwa upande mwingine, kungekuwa kumejitokeza mifumo ya ndani ya ubadilishaji bidhaa kutokana na ziada mahususi na kazi za ufundi. Eneo la mtoni lingeweza kubadilisha samaki wakavu kwa nafaka iliyolimwa mbali na mto; wanyama-pori waliowindwa na kukamatwa katika savana wangeweza kubadilishwa kwa vyakula vipatikanavyo misituni tu. Eneo linaloyeyusha chuma lingeweza kuuzia bidhaa za chuma kwa vyungu vilivyofinyangwa kutoka mahala penye udongo mzuri wa mfinyanzi. Pole pole mtandao huo ungekuwa na mazao ya sehemu moja yangeweza kusafiri, pengine kupitia kwa watu wa kati kadhaa, mpaka sehemu za mbali sana. Mifumo hiyo ya mabadilishano ya ndani inaweza kuwa muhimu katika ukujaji wa mamlaka unganifu, kwa sababu mara utajiri wa ziada uliotokana na biashara ya masafa marefu unapoingizwa humo, unampa nguvu kubwa chifu ambaye ndiye anayedhibiti bidhaa zinazobadilishwa kwa kiasi kikubwa kuliko ilivyokuwa hapo awali. Bila shaka hilo lilikuwa mojawapo ya mambo muhimu yaliyokuwa yakiendelea katika kipindi chetu katika Guinea, kwa kadri mikondo ya biashara za kuvuka Sahara ilivyoanza kutumia mifumo ya ubadilishaji iliyokwisha kuwepo. Upanuzi kama huo wa mtandao wa kibishara usingesababisha kuachwa kwa mifumo ya ubadilishanaji iliyopo ndani; kwani ukuzaji wa mbinu za biashara unaelekea zaidi kuwa wa kuongezea kuliko wa kimfuatano.

Kama ambavyo maendeleo ya mifumo ya kilimo na ya uyeyushaji chuma hayakuwa sawa kila mahali, ni vivyo hivyo bila shaka yalivyokuwa maendeleo ya mitandao ya ubadilishanaji. Pale ambapo mifumo ya ubadilishanaji haikuwa imeendelea vizuri, pangukuwa na ukosefu wa kichocheo

kimojawapo cha kuyaweka mamlaka chini ya kiini kimoja na uundaji dola, na kwa hivyo kusaidia kuhifadhi jamii nyingi za Afrika Maghribi zisizo na taifa. Mitaala ya biashara katika Afrika Maghribi imekuwa na tabia ya kuzingatia zaidi kwenye biashara ya nje, lakini ubadilishanaji wa mazao asilia kati ya kanda mbalimbali za kielekolojia za Afrika Maghribi unaelekea ulianza zamani sana.

### Biashara ya Nje

Ushahidi mmojawapo wa kuisimua wa ukusanyikaji wa aina fulani ya utajiri, na, yamkini, ukiandamana na kiasi fulani cha uelekezaji katika sehemu moja wa mamlaka ya kijamii na kisiasa, unaoonekana katika minara mikubwa ya Senegambia<sup>2</sup>.

Ni jambo la kuvutia kujaribu kukisia ni kitu gani kilichowezesha ugeuzaji wa kiasi kikubwa hivyo cha juhudi za wanadamu kuelekezwa katika kuchonga, kusafirisha na kujenga maelfu ya nguzo hizo za mawe. Kwa vile nguzo hizo zimechongwa kutoka kwenye mabonge ya mawe yaliyojaa chuma, basi inadhaniwa kuwa minara hiyo ilijengwa na watu waliotajirika kutokana na kuyeyusha chuma na kuziua kwa jumuiya zilizokuwa jirani. Huenda hivyo ndivyo mambo yalivyokuwa, lakini kama ni hivyo, majoko ya kuyeyusha chuma bado hayajagunduliwa tena zaidi ya maeneo ya maskani ya wajenzi wa minara ya mawe. Pendekezo jingine linaloeleza sababu za kuwapa minara hiyo ya mawe ya Senegambia linaona sehemu ilipokuwa minara hiyo kuwa ni sehemu nzuri ya kuweza kuwapatia wakaaji wa eneo hilo nafasi ya kuweza kudhibiti biashara ya dhahabu kutoka kwenye migodi ya dhahabu ya Bure na Bambuk. Iwapo tarehe hiyo ya karne ya nane ni sahihi, basi inaelekea tarehe hii ni ya mapema kidogo kuweza kufikiria kwamba biashara ya Waarabu kuelekea upande wa Kaskazini ndiyo iliyosababisha ujenzi wa minara hiyo. Iwapo minara ya Senegambia imejengwa kabla ya kudhibiti biashara ya Waarabu na kuwa kuwapa kwake kumesababishwa na usafirishaji Kaskazini wa dhahabu, pengine ni muhimu tuwafikirie Waberiberi wa jangwani kuwa ndio waliokuwa watu wa kati katika biashara ya Afrika Kaskazini ya Ubizenti.

Kaskazini mwa eneo la minara ya mawe na kwenye bonde la Senegal ni eneo la vichuguu vikubwa, baadhi yake vikiwa vimetoa vifinyange vinavyolingana na vile vilivyotoka katika minara hiyo ya mawe. Kuna mkusanyiko mkubwa wa vitu vilivyotoka makaburini, zikiwemo shanga za dhahabu na za akiki, vito vya dhahabu na shaba na silaha za chuma; vyombo vya shaba vilivyotengenezwa na mafundi wa Kimoroko vinaashiria uhusiano wa ubadilishanaji na Kaskazini. Ingawa sasa kuna tarehe ya radiokaboni ya karne ya nane ya mojawapo ya vichuguu vilivyo kusini zaidi, vingi vya vichungu hivyo vinahesabika kuwa ni vya karne ya kumi. Kadhalika, vichuguu vingine vingi vimechimbuliwa katika bonde la Mto Niger ya juu, chini ya Segu; huko Kaga, mwanzoni mwa kuruba kuu ya Niger, kichuguu kimoja kinachohusishwa na mawe yaliyo wima kimekisiwa kuwa ni cha miaka ya + 1000. Katika eneo hilo hilo la kuruba ya kati ya Mto Niger, huenda minara ya Tondidaru ni ya tarehe za kipindi kilekile cha jumla, nayo huashiria kuwapa kwa biashara ya dhahabu iliyosafirishwa kuja chini kwenye Mto Niger kutoka kwenye migodi ya dhahabu ya Bure. Ukuaji wa Kumbi Saleh kama kituo cha kukusanyia dhahabu kwa ajili ya biashara ya kuvuka Sahara unianza sio baada ya karne ya nane. Pengine miji yote miwili ya Kumbi Saleh na Awdaghust ilikuwa vituo vya kukusanyia dhahabu itokayo migodi ya Bambuk na pengine ilikuwa ni uandalizi bora wa njia zao za biashara ambao ulisababisha kufifia kwa umuhimu wa jumuiya za kijamii na kisiasa ambazo mpaka hapo zilikuwa zikichukua dhahabu mbali zaidi upande wa Maghribi.

Katika Sura ya 14, kuwepo kwa uhusiano wa moja kwa moja ulioanza mapema kati ya Misri na

2 Kuhusu mgawanyo, ukubwa, tarehe, na kazi yake taz. Sura 18 ya juzuu hili.

Sudan ya Maghribi kulitajwa. Huenda tunaweza kupata uthibitisho wa njia hii ya awali katika tarehe tatu za rdiokaboni za karne za sita, saba na kumi kutoka kwenye eneo la Marandet, huko Air. Hapa pana lundo la taka ambapo pameonekana kalibu 42,500, ambazo zinawakilisha shughuli za maskani ya mafundi. Wanahistoria hawakubaliani juu ya metali iliyokuwa ikifuliwa hapo, kukiwepo na madai kinzani kuhusu dhahabu. Ni muhimu kujifunza zaidi kuhusu Marandet, kuthibitisha na kupunguza makadirio ya tarehe na, fauka ya hayo yote, kuwa na fununu kuhusu chanzo cha malighafi iliyokuwa inatumika, mahali zilikopelekwa bidhaa zilizokwishatengenezwa, utambuzi wa mafundi na udhibiti wa kisiasa na kibiasara wa muundo wa biashara hiyo. Iwapo dhahabu ilikuwa inachimbuliwa huko Marandet, basi malighafi ingekuwa imeshafika mbali sana kutoka Bambuk na Bure na kufika nusu ya njia kuelekea Misri. Ama kuhusu vyanzo vya kupri (shaba), kwa muda mrefu watafiti wamekuwa wakijaribu kuhusisha 'Takedda' iliyowasifiwa na Ibn Battuta katika karne ya kumi na nne kuwa ndiyo chanzo chake. Mojawapo ya maeneo hayo ilikuwa Azelik (kilometa 150 Kaskazini-Maghribi kutoka Marandet) ambapo magofu na mtawanyiko mkubwa wa mavi ya chuma unadhahirisha umuhimu wake wa awali kama eneo la kufulia shaba. Lakini imegundulika kwamba hapakuwa na mashapo ya kutosha ya shaba ya kuweza kutumika, na kwamba ni lazima ilikuwa shaba kutoka nje ambayo inafuliwa hapo Azelik, shaba ambayo tarehe zake za radiokaboni (karne ya kumi na mbili na kumi na sita) ni za baadaye kuliko zile za Marandet.

Kuna ushahidi wa kutosha kutoka kwa waandishi wa Kiarabu unaonyesha kuwa shaba ilikuwa bidhaa nje muhimu katika ukanda wa Guinea. Ilikuwa ikitumika kama sarafu kauka Takedda na Kanem kwenye karne ya kumi na nne. Msafara uliokuwa unakwenda kusini ambao inaelekea ulipata matatizo katika Majabat al-kuhra huko Mauritania mapema mnamo karne ya kumi na mbili ulikuwa umechukua shehena ya fito 2000 za shaba nyeupe na ukazitupa baharini kupunguza uzito. Dhahabu ilikuwa bidhaa kuu iliyotamaniwa huko Afrika Maghribi na wafanyabiashara wa kuvuka Sahara, lakini pia kulikuwa na bidhaa nyingine za thamani na zenye kuleta faida kubwa zilizopatikana, hususan pembe za ndovu na watumwa katika maeneo ambayo hayakuwa na dhahabu, kama vile sehemu ya mashariki ya eneo la Guinea.

### *Mwanzo wa Uunganifishaji (Mamlaka Kuu)*

*Igbo-Ukwu* iko kiasi cha kilometa 35 kusini-mashariki mwa Onitsha, mji ambao muundo wake wa kisiasa ulikuwa umeathiriwa na Benin. Vitu kadha vya shaba nyeusi viligunduliwa hapa na maeneo matatu yaliyopakana yaligunduliwa. La kwanza lilikuwa bohari au hekalu, ambamo mliwekwa mavazi ya kifalme na vitu vya ibada. La pili lilikuwa kaburi la mbao la mtu maarufu, na la tatu lilikuwa shimo la kutupia vitu vilivyotumika katika sherehe. Katika bohari mlikuwemo vipande vikubwa, takriban sabini, vya shaba na shaba nyeusi na vitu vidogovidogo karibu mia tano. Kaburini mlikuwa na vipande kumi na tisa vikubwa na thelathini na viwili vidogo; jaani mlikuwamo vipande kumi na vitatu vikubwa na themanini na saba vidogo. Bcharini mlikuwa na shanga zaidi ya 60,000 na zaidi ya 100,000 katika kaburi. Bila shaka vitu hivyo havikuwa vya matumizi ya watu wa kawaida ya kila siku, na jinsi yule mtu aliyelazwa kaburini alivyotukuzwa inaonyesha hadhi kubwa aliyokuwa nayo juu ya wengine katika jumuiya. Hadhi hii huenda ni ile aliyokuwa anapewa mwenye cheo cha juu zaidi (*Ozo*) katika mfumo wa Waigbo wa kupata cheo; au pengine cheo hicho kilikuwa cha *ezenri* 'falme-kuhani' mwenyewe, ambaye hadi miaka ya mwanzoni mwa karne hii, alikuwa na mamlaka makuu katika tambiko na dini, ingawa siyo ya kisiasa, kwenye sehemu kubwa za Uigbo. Sehemu muhimu kabisa ya kazi yake ilikuwa inahusiana na zao la viazi vikuu na rutuba ya ardhi, katika kuondoa machafuzi ya taratibu za ibada baada ya miiko kuvunjwa na katika kusuluhisha

migogoro. Katika jumuiya za wakulima lilikuwa ni jambo muhimu kutenga vitu na watu mahususi ambao dhima yao ilikuwa ni kulinda rutuba ya ardhi. Uwekaji katika mamlaka kuu amali za jamii na nguvu za kisiasa kwa kawaida huhusiana sana na utaratibu huu ulioelezwa na inawezekana ulikuwa ni sehemu muhimu ya maendeleo ya falme nyinginezo za Guinea na asasi unganifu.

Huko Igbo-Ukwu hapakuwa na bidhaa maarufu zilizoagizwa kutoka nje, isipokuwa metali kwa ajili za sanamu na shanga za kioo. Mitindo ya sanamu ya hapa ni tofauti kabisa na ile ya Ife na Benin na ni ya kipekee; hivyo, inakuwa vigumu kutumia hoja ya mitindo kukadiria umri wake. Katika sampuli moja, tarehe za radiokaboni zimedhibirisha kipindi cha tangu karne ya nane hadi ya kumi na moja; hata hivyo, zingine ziliingia katika kipindi cha mwisho wa karne ya kumi na nne na mwanzoni mwa karne ya kumi na tano; tarehe hizi ni sawa na tarehe za sanamu mojawapo tu iliyoichimuliwa iliyoanana na zile zitokazo Igbo-Ukwu. Kuaminika kwa tarehe za awali za radiokaboni za Igbo-Ukwu kumekuwa kukisailiwa, lakini mara nyingi kutokana na misingi isiyo sahihi.

Kwa vile kupatikana shaba huko Nigeria ni kudogo, tarehe katika karne ya kumi na moja au kabla yake inamaanisha kuwa shaba iliagizwa kwa njia ya barabara kutoka Kaskazini. Nigeria Mashariki haikuwa na dhahabu ya kusafirisha nje, kwa hiyo bidhaa hizi za anasa pengine zililipiwa kwa pembe za ndovu na watumwa. Baadhi wamepinga kuwa hakuna mahali popote pengine hadi kusini ya Afrika Maghribi ambapo pamepatikana ushahidi wa kuwepo kwa biashara ya masafa-marefu katika kipindi kinachodokezwa na tarehe za radiokaboni. Hii ni hoja ya kuheshimiwa, lakini inafaa ikumbukwe kuwa njia za awali kuliko zote ambazo kwazo Waarabu walipata dhahabu kutoka Sudan ya Maghribi ziliunganisha Ghana ya kale na Misri kupitia al-Wahat, oasisi za Kharja na Dakhla. Ni wakati tu njia hii ilipoanza kuwa ya hatari baada ya katikati ya karne ya tisa ndipo njia ya Maghribi kutoka Maghrib ikaanzishwa. Kulikuwapo 'njia-ya-pembe-za ndovu' katika nyakati za mwishoni mwa Warumi na Wabizenti kutoka Tripoli hadi eneo la Ziwa Chad kwenye njia fupi kabisa ya kuvukia Sahara na inaelekea kuwa Waarabu pia waliitumia njia hiyo. Kuna ushahidi wa kutosha, siyo tu wa ya biashara kwa jumla kwenye Sahara katika kipindi ambamo ugunduzi wa Igbo-Ukwu umepewa tarehe za radiokaboni, bali pia wa biashara ya shaba. Uwezekano ambao inastahili pia kutiliwa maanani na kuhakikishwa kwa uchunguzi wa siku za mbele ni ule wa kuwa shaba ilitoka katika kanda zenye metali katika bonde la Mto Niari, Kaskazini kidogo mwa mkondo wa chini wa Mto Zaire (Kongo).

Pengine inawezekana kuunga mkono wazo la kuwa kuenea kwa biashara ya kuvuka Sahara hadi ilipofikia karne ya kumi na moja kilikwisha fika kusini, kulingana na tarehe mbili za radiokaboni zilizopatikana kutoka Nyarko katika Begho, huko Ghana, ambapo baadaye palikuwa kituo kikuu cha kukusanyia dhahabu kutoka Asante na ambayo ilisafirishwa Kaskazini hadi Jenne.

## Ife


Ingawa kilele cha utamaduni wa Ife kiko nje ya kipindi chetu - kuanzia katikati ya karne ya kumi na mbili hadi katikati ya karne ya kumi na tano - shurti tuelewe kuwa ukuzaji wa asasi za mamlaka kuu za kidini na kisiasa, zenye utajiri wa kutosha wa kulinda uzalishaji mkubwa wa kisanaa haufanyiki katika siku moja. Kwa vile hatua hii ya mwanzo imo katika kipindi chetu, inastahili izingatiwe. Suala hili la 'usitawi wa Ife' linahusiana na suala pana zaidi, lile la asili ya ujengaji miji wa Kiyoruba kwa jumla, suala ambalo limewatatanisha waandishi kadhaa.

Tunaweza kuchukulia kuwa katika kikwi cha kwanza cha enzi wa ukristo, maeneo ya misitu ya Nigeria yalizidi kulowewa na watu waliolima viazi vikuu na michikichi. Kwa muda wa vizazi thelathini, ufyekaji mapori na ukulima ulifanywa kwa ufanisi zaidi kutokana na matumizi ya zana za



**16.2** Machumbo ya Igbo-Ukwu  
Tume ya Taifa ya Maabo ya Kale aa Makumbusho,  
Lagos)  
Sanamu ndogo ya kichwa chenye jebeli ya shaba nyuma

*Fovu la shaba la chini alivewekwa pua ya  
nguzo ya shaba nyekundu*





*Bakuli la shaba la ditara (urefu wa sm 20)*



*Bakuli la shaba likiwa wima (urefu sma 27.5)*

kimetali zilizotengenezwa kutokana na chuma kilichozaalishwa nchini.

Yaonekana watu hawa walikuwa na sifa tatu. Mosi, wakulima wote waliojenga maskani katika nyakati za kabla ya sayansi walihisi kuwa kama sehemu ya ada zao za kilimo ni lazima wachukue hatua kuhakikisha kuwa ardhi inakirwa na rutuba na uzalishaji wa mazao yao unakuwa mzuri. Inaaminiwa kuwa vitu hivyo vinategemea nia njema ya kudra. Watu wa kawaida wanaweza wasijiamini kuwa wanao uwezo wa kuzimudu nguvu hizo zenye hatari au wanakuwa na hofu kufanya hivyo; kwa hiyo, walitosheka kuwakilishwa na wataalamu waliolipwa ada ambao hawaogopi kama wao na ambao wanadai kuwa wana ujuzi wa kitaalamu unaohitajika. Hivyo, madhehebu na makuhani ni mambo muhimu katika maisha ya jumuiya yao.

Pili, kwa kawaida kuna wakazi wote ongezeko la watu. Ongezeko hilo halitokei hivi hivi tu na kwa kawaida huenda polepole, lakini linatokea; huenda kukawa na athari hasi kwa sababu ya miaka ya ukame na maradhi, lakini watoto huzaliwa mara nyingi zaidi kuliko wanavyokufa. Kuongezeka huku kwa watu kwenyewe kuna athari desturi za ukulima na kuzirekebisha zikaelekea kwenye matumizi bora ya kanda za kiekolojia.

Tatu, matumizi haya yenye ufanisi ya maliasili huenda yalisababisha kumakinikia maeneo maalumu mbalimbali ya kiekolojia, pamoja na ubadilishanaji wa mazao kati yao. Jambo hili hupendelea kuwepo mgawanyo wa kishughuli na utegemeaji wa kiuchumi na kufanya sehemu za jamii zilizokaribiana kijiografia kutegemeana. Hapo baadaye litatolewa wazo kuwa huenda Ife ilichukua nafasi mahsusi katika mtaandao wa mabadilishano.

Hali tofauti zinaelekea zilikuwapo Maghribi mwa Niger zikilinganishwa na zile za mashariki, ambako wakulima wa Kiigbo walijihisi wako salama kiasi cha kuweza kuishi katika maskani yaliyotawanyika katika ardhi waliyoilima. Mahandaki ya kujihami yaliyokuwa yamezagaa katika nchi ya Waado na Wayoruba yanaashiria, kwa sababu ambazo tunaweza kuzikisia tu, kuwa Maghribi mwa Niger mahitaji ya kujihami yaliwafanya wakulima waishi karibukaribu pamoja vijijini. Hivyo, mfumo wa kijamii ulitokeza miongoni mwa wasemaji wa Kiyoruba na Kiedo ulikuwa tofauti na ule wa Kiigbo. Kwa vile watu wa koo tafauti walikuwa wakiishi pamoja, madai ya jirani yalianza kuleta ushindani na hatimaye kuyapita yale ya ndugu. Mahitaji ya kidugu yalitishia mshikamano wa vijiji katika hoja zake za kujihami, na athari za kiufarakano za majukumu haya ziliipukwa kwa kuzipa baadhi ya nasaba shughuli kadhaa katika maisha ya jumuiya, kama vile kumteua chifu, kiongozi wa vita, mwanahistoria, msemi na kuhani. Uongozi huo ulielekea kujijenga na kuwa mamlaka ya kudumu. Kwa upande wake, mamlaka ya kudumu yanapokuzwa katika kiwango kikubwa, huhitaji wasaidizi na tabaka ya waendeshaji ili kusaidia kuendeleza shughuli zake. Au tunepindua mambo? Je yawezekana kwamba Wayoruba walikuwa wamekwishaendeleza mfumo wa jamii wa kimsonge ambao kwao sehemu kubwa ya matunda ya uzalishaji ilikuwa mikononi mwa walio kileleni au kwenye tabaka za juu za hatamu ya kijamii? Je mfumo huo ndio ulielekea kushadidisha na kuongeza uhasama kati ya wanajumuiya kauka kudhibiti matunda ya uzalishaji na pengene hata ardhi na nyenzo za uzalishaji?

Lau kama ni haja za kujihami ndizo zilizowaweka pamoja kauka vijiji wakulima waliotawanyika, basi kulikuwa na kitisho cha aina gani? Je msongano wa watu ulikuwa umefikia kiwango cha kusababisha kushindania umiliki wa ardhi iliyopo ya kulima kiasi kwamba jumuiya moja ilitishia jumuiya nyingine? Au tishio hilo lilitokea nje kwa sababu ya uluwa wa kibiashara na wa kijeshi wa majimbo ya kibiashara yaliyoko Kaskazini, yaani majimbo ya Mali na Songhay? Mojawapo ya tatizo letu ni kuwa hatuelewi ni lini mahandaki ya Uyoruba yalijengwa. Mbali na ukuta wa ndani wa Benin wa karne ya kumi na nne na kumi na tano, mifumo mingi ya mahandaki katika eneo la wasemaji wa Kiedo inaelekea ilitokana na watu wenyewe na inaelekea zaidi kuwa

ilikuwa mipaka. Kwa hakika, pengine, mahandaki ya kujihami hayakuanza kujengwa huko Uyoruba hadi vitisho vya nje vilipoanza kushtadi kama hali ilivyokuwa baada ya mwaka wa 1100: kwenye kilele chake, utamalaki wa Mali ulienea hadi Mto Niger na kufika masafa ya kilometa 100 tu Kaskazini ya nchi ya Wayoruba. Tunaweza kuwazia tu jinsi shinikizo hilo lilivyotokea mwanzoni, lakini inavyoelekea zaidi ni kuwa chanzo hasa kilikuwa cha mahitaji ya watumwa. Usakaji watumwa ulikuwa muhimu zaidi katika sehemu ya kati kuliko Maghribi ya Sudan kwa sababu Sudan ya kati haikuwa na dhahabu. Mfumo wa ubadilishanaji ambamo vitu kama samli kutoka savana ya Kaskazini iliuzwa katika maeneo ya misitu kwa kubadilishana na mazao kama vile kola, huenda ulikuwa wa kale zaidi kuliko biashara yoyote ya masafa marefu. Punde tu mfumo huo wa ubadilishanaji ulipositawi, maeneo ya Kaskazini yalijikuta na nafasi ya kubadilishana bidhaa zilizotoka mbali zaidi, na jambo hili lilichochea usafirishaji nje wa bidhaa za ziada kutoka kusini.

Kwa upande mmoja tukichukulia haja ya kuwa na madhehebu na makuhani kuwahudumia watu kama wataalamu wao katika mambo ya uendeshaji wa kikudra wa kilimo, na kwa upande wa pili, haja ya kurasimisha mipango ya ugawaji tena maliasili, matokeo yake huwa utokeaji wa aina fulani ya kitovu cha maadhimisho. Pale panapokuwa na maendeleo kuelekea kwenye mfumo wa ubadilishanaji, wataalamu kama hao huzidi kuonekana wamestakimu kwenye vifundo vya mifumo hiyo. Kuhani anatarajia kulipwa kwa ajili ya huduma zake, pengine moja kwa moja, pengine kwa matambiko, na mara nyingi ikiwa mchanganyiko wa vyote viwili. Katika hali hii kukatokeza kitovu cha maadhimisho, ambamo asasi zilizoratibiwa na hekalu na ikulu, na ziara na *alafin* au *oba*, zinatokeza kuwa ndizo asasi thabiti zaidi za ugawaji tena wa maliasili. Kuna ushahidi kidogo zaidi kuwa *oni* wa Ife alijishughulisha na biashara kuliko alivyofanya *oba* wa Benin: na sababu yake inaweza kuwa kuanguka hapo baadaye kwa utamalaki wa kibiashara wa Ife katika karne ya kumi na tano na kumi na sita. *Oba* wa Benin alishika biashara zote za watu binafsi nje ya Benin na yeye peke yake ndiye aliyemiliki bidhaa muhimu za biashara - watumwa, ngozi za chui, pilipiliimanga, michikichi, marijani naembe. Lakini, wimbo mmojawapo wa *Ife oriki*, au nyimbo za tambiko, wa Kiyoruba, unatupa kidokezo: unamtaja Oduduwa, shujaa mwasisi na *oni* wa kwanza wa Ife, kama alikuwa mfanyabiashara aliyetajirika kutokana na kusafirisha nje kola zilizozalishwa pale na ambaye aliagiza farasi kutoka Kaskazini.

Ife iliyoko kwenye ardhi yenye rutuba ilifikika kwa urahisi kutoka savana Kaskazini, na pwani kusini. Hivyo tunaweza kuona jinsi Ife ilivyoweza kukua na kugetika kuwa kitovu cha maadhimisho ambamo *oni* alionekana kuwa ndiye mtu mtakatifu, akikirimiwa kwa hongo na kodi za biashara ya mahala pale, na kuwa kiongozi kutokana na hadhi kubwa aliyokuwa nayo katika mfumo wa kidini. Uanzishaji wa mamlaka kuu ya kiada na kikudra ya aina hiyo ulimpa uwezo wa kunufaika binafsi kiuchumi na madaraka halisi ya kisiasa. Kwa hivyo, wakati mahitaji ya kibiashara kutoka Kaskazini yalipoanza kujitokeza, Ife ilikuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kufaidika nayo. Wale waliotaka watumwa walianza kuwanunua kutoka mamlaka yaliyoasisiwa ya maeneo hayo. Wafanyabiashara ya watumwa wa baadaye wa Bahari ya Atlantiki waliyaona hayohayo kwenye ukingo wa pwani wa nsitu. Utumwa wa kibiashara uliongezewa kwenye utumwa wa nyumbani na biashara hiyo kaongeza utajiri na madaraka ya *oni* na wasaidizi wake, ambao nao waliendelea na kutononoka zaidi mfumo ulivyokua. Pale ambapo biashara ya nje iliingia katika jamii za Kiafrika zisizokuwa na idhaa za kusafirisha nje kama vile dhahabu, lakini ambapo madaraka makuu ya kisiasa alikwishanzishwa, watumwa ndio walikuwa bidhaa dhahiri ya kusafirisha nje. Makisio ya chini ana ya idadi ya watumwa waliosafirishwa nje kupitia Sahara hadi Afrika Kaskazini katika nusu ya wanza karne ya kumi na tisa ni 10,000 kwa mwaka<sup>3</sup> na biashara hiyo ilikuwa ikiendelea kwa

karne nyingi. Hata kama idadi ya watumwa ilikuwa ndogo zaidi wakati wa uluwa wa Ife, biashara hiyo huenda ilikuwa ndiyo chanzo kikuu cha utajiri wa Ife. Yawezekana watumwa waliouzwa kwa wafanyabiashara wa Kaskazini walilipiwa kwa chumvi, lakini jinsi uhusiano wa kibiashara ulivyositawi na kusaidia kuongeza utajiri na madaraka ya *oni*, ndivyo bidhaa nyinginezo za anasa zilivyoongezwa kwenye vitu vilivyoagizwa kutoka Kaskazini, na bidhaa nyinginezo za asili za kubadilishana navyo. Shaba na shaba nyeupe, nguo, shanga, bangili, panga na farasi viliongezwa katika bidhaa ghali zilizoagizwa. Katikati ya karne ya kumi na mbili al-Idrisi pia anataja viungo, manukato na zana zilizoundwa kwa chuma kuwa bidhaa zilizosafirishwa kutoka Moroko ya kusini kwenda nchi ya watu weusi. Hatujui vipi sanaa za kukalibu shaba nyeupe na utengenezaji wa shanga za vigae zilianzishwa. Vyovyote vile 'utumwa' utakavyofasilwa, kuuona kama msingi muhimu wa mfumo wa kiuchumi na wa kijamii ulioichomoza sanaa ya Ife, hakuuondoi katika sanaa hiyo; utumwa ndio uliokuwa nguzo ya usanii wa Ugiriki ya kale na siye hatuwashutumu Wayunani kwa hayo. Shaba nyekundu na nyeupe ilibidi zilipiwe kwa njia fulani, kwa sababu hakuna shaba huko Nigeria na kuna masimulizi mengi ya Waarabu kuhusu usafirishaji wake nje kwenda Afrika ya Maghribi kupitia njia za misafara zilizopita inwambao kutoka Kaskazini, kama ilivyokwishaelezwa kuhusu Igbo-Ukwu. Vitu vingine vya anasa vilivyokuwa adimu yaelekea vilikuwa ghali. Huenda biasbara ya kola ina historia kongwe na kuwa kola na pembe zilisaidia kulipia gharama; lakini ni vigumu kufikiria kuwa kulikuwapo bidhaa nyingine kuu zaidi, kuliko watumwa, za kusafirisha nje. Wazo kuwa biashara ilikuwa shughuli muhimu katika kusitawisha dola ya Ife halimaanishi kuwa ufalme huo ulitegemea watu walioshughulikia biashara. Lakini, punde tu biashara ya nje inapoleta utajiri na ziada katika mfumo wa ndani wa mabadilishano, basi utajiri huongeza sana madaraka ya machifu ambao hudhibiti ugawaji wake.

Kuna vidokezo kadhaa kuhusu athari za kutoka Kaskazini - mapokeo kwamba Obatala, mwumbaji wa wanaadamu, alikuwa 'mweupe'; mbinu ya kukalibu sufuri iliyotumika, na vilevile kuwepo kwa kikundi cha 'Tsoede' cha sanamu za shaba nycusi kwenye Mto Niger. Nafasi yao kwenye mpaka wa Kaskazini wa nchi ya Wayoruba inaweza ikahesabiwa kuwa inaashiria umuhimu wa mwelekeo huu wa msafara.

Vidokezo vinginevyo vya uhusiano wa Kaskazini vimedaiwa katika sanaa nakshi za Ife kongwe. Athari hii imeonekana katika matumizi ya ruwaza za *kigilochi* na *kiwaridi*, katika nyumba za aina ya *impluvia* ambazo zinafuata mpango ulcule wa nyumba za Kirumi; na katika mabaraza yaliyotengenezwa kwa vigae vinavyofanana na nakshi za vyanzake.

Huenda ufanano huo ulikuwa wa sadfa, na vitu vingi huenda vilitokea huria; vidokezo hivi vya uhusiano na ulimwengu ulioko mbali sana na nchi ya Wayoruba havithibitishi kuwa sanaa za Ife hazikuwa zao wenyewe. Inaelekea ukalibu-shaba na utengenezaji-shanga ulikuwa fursa ya mfalme. Huenda shanga zilihusiana na utengenezaji wa mataji ya shanga kwa ajili ya wafalme kumi na sita wa Kiyoruba walioistahiki kuyavaa kutokana na mamlaka waliyopewa kutoka Ife.

Chanzo cha kilele cha Ife kongwe katika karne ya kumi na mbili kinaweza kulingana na tarhe ya kufika katika nchi ya Yoruba kwa mahitaji yale ya kibiashara kutoka Kaskazini ambayo Ife iliweza kufaidika nayo. Huenda himaya ya Mali ilikuwa mbali mno kuweza kuchochea hayo, na tunapaswa kuangalia dola za mwanzoni za Kihausa, ambazo uchumi ulikuwa ni kipengee muhimu kauka kusitawi kwake. Tunajua kuwa hapo baadaye *Zazzau* ilijihusisha na usakaji wa watumwa upande wa kusini, na pengine mji ambao uliachwa na Turunku ulikuwa na nafasi hiyo katika kipindi cha awali. Mji huo uko kilometa 300 tu kutoka Mto Niger huko Tada. Kwa bahati mbaya, bado tuna taarifa kidogo sana za kiakiolojia kuhusu dola za mwanzo mwanzo za Kihausa, na eneo la Turunku bado halijachambulwa.



## *Ukanda wa Guinea watu waishio kati ya Mlima Kameruni na Cote d'ivoire*

### *Isimu na historia ya mwanzo*

Ushahidi wa kiakiolojia unaonyesha kwamba maelfu ya miaka iliyopita schemu za pwani na msituni za Guinea ya Chini zinazokaliwa na watu watumiao lugha ya Kikwa na lugha ya Kibenue-Kikongo zilikuwa zikikaliwa na wakulima; na kabla ya hapo zilikalifiwa na wawindaji. Ingawa ushahidi wa kiakiolojia na wa kiisimu hudokeza kuwepo kwa uhusiano wa kimaumbile na kitamaduni baina ya wakazi wa mwanzo na waliopo katika maenco hayo, hii leo uhusiano huo bado haujabainishwa kikamilifu. Udhihirishaji wa jambo hili ni wa lazima hasa inapokuwa baadhi ya wakazi wa maenco haya wana visaasili mbalimbali juu ya asili yao ambavyo huelekea kuonyesha kwamba walifika katika makazi yao hayo ya sasa hivi karibuni tu.

Sehemu kubwa ya ukanda wa msitu wa Afrika Maghribi, yaani eneo linalotanda umbali wa zaidi ya kilomita 1600 kutoka katikati ya Liberia hadi kuvuka Niger ya Chini, imekaliwa na watu wasemao lugha nyingi zenye kuhusiana, zikiwa na mifanano ya ndani kimsamiati na kimuundo. Hizi ndizo zile lugha za makundi madogo ya Kikwa na Kibenue-Kikongo ambayo nayo yako chini ya kundi kubwa la Kiniger-Kikongo.

Katika ukanda wa kati lugha muhimu za kundi dogo la *Kikwa* ni Kiakan (Kitwi, Kifanti n.k.) na Kiguang, ambazo ziko kwa wingi katika Ghana na Cote d'Ivoire; Kiga na Kiadangbe (Dangme), ambazo ziko kusini mwa Ghana; na Kiewe ambacho kiko zaidi katika Togo na Benin, na pia husemwa katika schemu za kusini-mashariki ya Ghana. Watu wa kundi dogo la *Kikwa* katika Guinea ya Chini ni Wayoruba-Waigala, kundi la Wanupe (ikiwa ni pamoja na Wanupe, Wagbari, Waigbirra na Wagade), Waedo, kundi la Waidoma (ikiwa ni pamoja na Waidoma, Waagatu na Waiyala), Waigbo na Waijo. Wazungunzaji wa lugha za Kibenue-Kikongo wanapatikana Kaskazini na kandokando ya mto Cross nao ni pamoja na Waibibio, Waefik na vijikundi vya Waekoi, na Wativ pia.

Isimu linganishi inadokeza kwamba lugha za *Kivolta-Kikomoe* (kijikundi cha Kiakan) ni kijikundi azali cha vijikundi vya kundi dogo la *Kikwa*; kwamba mabaki ya lugha za Togo ni tofauti na vijikundi vya Kiewe na Kiga-Kiadangme; na kwamha vikundi vya *Kiakan*, *Kiewe*, Kiguang na Kiga-Kiadangme huunda kikundi ambacho hakikuhusiana sana na vijikundi vya lugha za kundi dogo la *Kikwa* la Nigeria kusini.

Makutano ya Niger-Benue yamekuwa yakichukuliwa kuwa kitovu ama cha asili au cha mtawanyiko wa watu wa mashariki wazungunzao lugha za *Kikwa*. Wazo kwamba mgawanyiko baina ya vijikundi vikubwa vya *Kikwa* ni wa zamani sana limehitimishwa kutokana na mitaala ya uvumbuzi katika glotokronolojia. Imethibitishwa kuwa kwa kawaida lugha za *Kikwa* ni tofauti sana



na zinaachana na lugha nyingi zinazozizunguka. Ama kwa hakika yawezekana kwamba lugha hizo ni mabaki ya lugha-azali zilizokuwa zimezagaa sana.

Yaelekea pia kwamba hakuna mpaka wa wazi baina ya baadhi ya lugha za *Kikwa* (k.m. Kiigbo) na lugha za *Kibenué-Kicross* kama vile Kiibibo, Kiefik na Kikele. Kuna baadhi ya lugha za *Kibenué-Kikongo* (kama vile Kijunkun) ambazo hazina mifumo ya ngeli, wakati kuna baadhi ya lugha za *Kikwa* (k.m. Kidogama na Kiedo) ambazo zina mifumo ya ngeli. Kwa upande mwingine, yaelekea kwamba lugha za Kiigbo na Kiefik baada ya kuwa na mgusano wa karibu na wa muda mrefu zingeweza kuwa zimekopa maneno, moja kutoka kwa nyenziye, bila kujijua, hata katika msamiati wa msingi.

Ushahidi wa kihistoria-kijiografia unaashiria zaidi kwamba msitu ambao tayari ulikuwa umekaliwa na watu ulikuwa kizuizi cha watu wa baadaye kuingia. Kupenya huko kulipotokea hakukuwa katika mtindo wa uhamaji wa makundi makubwa makubwa ya watu, bali ulikuwa wa makundi madogomadogo ambayo hata kama yalileta athari za kitamaduni, yalimezwa kiisimu, na pengine hata kuchanganyika na wenyeji wa pale.

### *Gold Coast kati ya mwaka 600 na mwaka 1100*

Kipindi cha kuanzia karne ya saba hadi karne 000 ya kumi na moja kilikuwa na athari dhahiri ya maendeleo; kilikuwa ni kipindi cha mpito kati ya mfumo wa vijiji wa kipindi kabla ya historia uliotangulia karne ya saba kwa upande mmoja, na mfumo wa miji, biashara, teknolojia za hali ya juu za mwaka 1200 na baadaye, kwa upande mwingine. Udhahiri wa kutokueleweka kwa kipindi cha miaka 600 - 1100 hautokani na kutokuwepo na matukio yoyote katika kipindi hicho (kwani kipindi cha mwanzo cha historia ya awali, yaani kuanzia 1500 mpaka + 500, kina nyaraka nyingi za kimaandishi kutoka sehemu mbalimbali za nchi) bali unatokana na wanazuoni kutokitia maanani kipindi hiki, pamoja na hali yenyewe ya utafiti.

Inawezekana kwamba baadhi au lugha zote za Mame-Akan, Mame-Guan na Mame-Ga/Dangme zilikuwa zikitumika katika kikwi cha kwanza kabla ya enzi ya Ukristo. Kutokana na uwiano uliopo wa mitaala ya kiisimu juu ya Baule, Agni, Bia na Akan, pamoja na kiakiolojia, inaanza kuonekana (ingawa bado inahitaji kuthibitishwa) kwamba Mame-Akan ilitokea katika mazingira ya msitu na savana, ikawa imetanda katika sehemu za kati na kusini mwa Cote d'Ivoire na Gold Coast; na kwamba changamano ya Kintampo<sup>1</sup> ambayo maeneo yake sasa yameainishwa katika nchi zote mbili inaweza kuwa ni kisawe cha kiakiolojia cha wazungumzaji wa Mame-Akan ambao walijinasibisha na ekolojia yao na ambao hawakuwa na mipaka ya nchi kama iliyopo sasa baina ya Cote d'Ivoire na Ghana.

Wakati miguro midogomidogo ya watu, biashara na mahusiano ya kitamaduni ni sifa za kawaida katika mabadiliko ya jamii nyingi, jambo ambalo hatuna budi kulitambua hivyo, fikra za zamani kwamba kulikuwa na uhamaji wa makundi makubwa makubwa ya watu toka sehemu moja hadi sehemu nyingine ni mtazamo usiosadikika sana (labda kwa sehemu chache tu) katika kuzieleza asili za tamaduni na mbari mbalimbali. Kwa hiyo mawazo ya zamani kuhusu asili ya uhamaji wa Waakan kutoka Misri au Ghana ya Kale, na nadharia ya asili ya Kig-Kidangme kutoka Dahomey/Nigeria si yakini sana iwapo tutatumia vigezo vya kiisimu na kiakiolojia.

Mojawapo ya minara muhimu kabisa katika mabadiliko ya kitamaduni ya watu wa Gold Coast

1 Kuhusu changamano ya Kintampo Taz. Sura 24. juzuu 11.

ni kuanzishwa na kuendelezwa kwa teknolojia ya chuma. Ushahidi wa mwanzo kabisa wa teknolojia hii unatoka Begho (+105-255) na Abam, Bono Manso (+290-350). Machimbo katika maeneo haya yametoa magofu ya matanuu, taka za chuma, vyombo vya mfinyanzi na mkaa kwa ajili ya ukadiriaji tarehe.

### Nchi ya Akan

Pango la mawe la Amuowi karibu na Bono Manso lina tarehe (+370-510) ambayo inakitanguha kidogo kipindi tukizungumziaheo. Lakini tarehe hii inalingana na tarehe ya kuyeyusha chuma huko Abam, Bono Manso. Ushahidi wa vyombo vya mfinyanzi na ukadiriaji tarehe kutoka machimbo ya Amuowi vinadokeza kwamba kuanzia takribani karne ya sita Wabrong wa eneo la Bono Manso walikuwa wanaanzisha makazi ya kudumu ambayo baadaye yangukuwa mame-miji na baadaye tena kuwa makazi ya miji hasa katika Bono Manso.

Eneo la Bonoso lina tarehe ya zamani kabisa ambayo inaangukia kabisa katika kipindi hiki tukizungumziacho. Machimbo yaliyofanywa pale yameonyesha kuwepo hapo kwa tasnia ya uyeyushaji chuma yenye taka za chuma, zana za chuma na vyombo vya mfinyanzi vilivyopambwa kwa alama za chanuo. Eneo hili la machimbo limekadiriwa umri kwa radiokaboni na kuonyesha kwamba shughuli hizo zilifanyika katika kipindi cha miaka 660-1085.

Eneo la tatu la Wabrong ambalo pia ni la kipindi hiki tukizungumziacho ni lile la makazi ya mame-miji huko Begho. Nyarko, kiunga cha Begho, ambacho kimekadiriwa umri kwa radiokaboni kuwa cha miaka 965-1125, kimetanda eneo la zaidi ya kilometa moja ya mraba. Vitu vyote vilivyopatikana katika eneo hili la machimbo vinaakisi hali ya jumla iliyokuwepo katika kipindi cha miaka 600 - 1100, yaani kumakinika kwa watu katika kazi za mikono na teknolojia, umame-miji na pengine kuanza kwa tasnia ya pembe za ndovu na biashara ya nje. Kanda ya Brong yaelekea ndiyo lilikuwa eneo la Akan lililotakadamu katika mabadiliko ya kilimo cha Enzi ya Chuma, utengenezaji madini, umiji, ujengaji wa taifa na biashara ya masafa marefu.


Maeneo ya Asante na Wassa yanajulikana sana kwa machimbo yake yaliyo juu ya vilina; sehemu hizi za vilima ndizo zilizopendelewa sana kwa makazi ya Enzi ya Chuma katika kipindi kati ya mwanzo wa enzi ya Ukristo na 1500. Kati ya machimbo haya yote yale yaliyosifika sana ni Nkukoa Buoha (karibu na Kumasi), Bekwai, Kwapong, Obuasi Monkey Hill, Nsuta, Tarkwa, Ntirikurom na Odumparara Bepo. Yaelekea kuwa maeneo haya yalikuwa makazi ya vijiji vyenye maboma. Ushahidi wa teknolojia ya chuma iliyokuwa ikitumika katika changamano hii unaonyesha sifa ya uwekaji-msingi ya kipindi hiki ukiwa kama matayarisho kwa tukio kubwa la ujenzi wa miji, ujengaji wa taifa na biashara ya masafa marefu yaliyohibitika huko Adanse, Denkyira na Asante.

Eneo la Akyem Manso na Akwatia linafahamika kwa ngome zake za udongo. Maeneo kadhaa yaliyojengewa ngome yamechimbuliwa kaika jitihada za kujaribu kuthibitisha nadhariatete mbili ambazo zimewahi kutolewa kuhusu matumizi yake. Nadhariatete ya kwanza yasema kwamba ngome hizo ziliukiliwa kuwa kama njia ya kujilhami (ulinzi); nadhariatete ya pili yasema kwamba ngome hizo ziliukiliwa kuwa kuta za kuzunguka makambi yaliyojengwa na kutuniwa katika shughuli za kuchimbia dhahabu katika mashapo ya Bonde la Birim. Yaelekea kwamba ile dhana ya mwanzo ya 'ulinzi' inakubalika kuliko ile ya 'kuta za makambi ya wafanyakazi.'


### Guan

Mapokeo simulizi hueleza kwamba katika karibu mwaka 1200 watamakani wa Kiguan ambao walikuwa wakimiliki mbuga za Afram walianzisha makao yao makuu Ganebofo, mahali ambapo nasabatawala ya Atara ili watawala Waguan wa mbuga za Afram. Kituo cha biashara kilianzishwa





17.2 Ujuzi wa wenye mchoro wa karne ya kumi hadi ya kumi na moja kutoka maceo ya Nyatko ya mji wa Inshara wa Begho, Jamburi ya Ghoma (J. Anquandah).



**17.3** Vatu vya Utamshini Tana na Kiarabhi wa Kocambo kutoka - 1500 hadi - 500 haka Njokou (1) na be na Kuniisi, Jambura ya Ghama. Kuchoto vilaa vya kutengeneza vyangu, kati na kulia - vyangu vilivyopigwa mitaani

Juafo Abotan, mahali ambapo walifanya biashara motomoto ya pembe za ndovu, kola, ng'ombe, chumvi na watumwa na ukanda wa Sudan. Machimbo kadhaa yamekwishafanywa katika pango la Bosumpira na kwenye mapango ya miamba huko Apreku, Tetewabuo, na Akyekyemabuo. Machimbo haya yakisaidiwa na ukadiriaji tarehe kwa njia ya radiokaboni yanaonyesha kwamba mnamo miaka ya 1000-1300, genge la Kwahu liliehukuliwa na wawindaji maarufu, wavuvi, wachungaji na wagama mawcse ambao walitengeza vyombo vya ufinyanzi "vilivyong'arishwa kwa moshi."

Eneo la Dawu na Awukugua linatambulika kwa miinuko mingi ambayo ni dalili ya milundikano ya mashapo yaliyokuwa yakiwekwa na wenyeji wa hapo katika miaka mingi na vipindi virefu sana. Ingawa tarehe za majalala makuu ni za baadaye kidogo kuliko kipindi tunachozungumzia sasa, mazingira ya utamaduni yanayohusishwa na miinuko inayopatikana kila sehemu katika Akuapem hudokeza taratibu za kuweka misingi zilizoshitadi sana katika miji ya sasa ya Waguan wa Akuapem Hill.

### Waga na Wadangme

Akiolojia na isimu-ethnolojia ya magcge ya Akkra huashiria kwamba watu wa Ga na Dangme wanaweza kuwa wametamakani katika eneo hili kwa kipindi cha takribani kikwi moja au viwili. Maeneo kadha ya machimbo kama vile Gbegbe, Little Akkra, Pampram na Lólôvô, ingawa bado hayajakadiriwa umri, yana magofu ya makazi yaliyo na vyombo vingi vya mfinyanzi visivyohusiana na bidhaa zilizoagizwa Ulaya vikidokezea kwamba ni vya kipindi kabla ya 1400; wakati ambapo Ladoku na Shai, yalikuwa makazi ya vijiji vingi vya kipindi cha 600-1400. Kati ya 1000-1300 wakazi wenyeji wa Dangme, katika maeneo ya Pampram, Dawhenya na Shai, walikuwa wakianza kuingia katika mtindo wa maisha uliotegemea kilichopatikana (k.v. kutokana na ufugaji, uvuvi, utengenezaji chumvi na kilimo cha mahindi ya Guinea katika matungazi) na walikuwa na mfumo wa utawala uliokitwa kwenye maongozi ya Mungu, ambao baadaye ulipeleka katika kuanzishwa kwa miji-pacha ya Shai na Ladoku. Mfumo huu wa utawala, vilevile ulikuwa na ustaarabu uliosifika kwa sayansi ya miti shamba, miziki ya *Klama* iliyojaa mithali na falsafa, na mfumo wa utawala uliokitwa kwenye misingi ya mchanganyiko wa uongozi wa Mungu na mfalme.

### Makazi miji

Ushahidi uliopo unaonyesha kuwepo kwa aina mbili kuu za makazi miji katika Ghana ya kabla ya majilio ya wazungu. Hizi zilikuwa ni vituo vya biashara kama vile Begho na miji mikuu ya taifa kama vile Bono Manso. Uhamaji na biashara ya masafa marefu vilikuwa vitu muhimu katika ukuaji wa miji hiyo. Kabla ya majilio ya Wamande eneo la Jakpawuase lilikuwa na watu wengi na lilikuwa na sehemu kubwa za makazi ambazo zilikwishaanzisha mtandao wa biashara ya ndani na ubadilishanaji wa bidhaa.

Kazi iliyofanywa katika Begho imedhihirisha kwamba utamaduni wa mji huu kwa kiasi kikubwa ulikuwa ni ule wa Kibrong; kulikuwa pia na ushahidi wa athari kubwa kutoka nje. Sehemu kubwa kabisa, ambayo ndiyo ile ya Wabrong, ina mamia kadhaa ya vilima vidogo vidogo katika eneo la zaidi ya kilometa moja kwa urefu. Sehemu nyingine zimetengana kwa umbali wa kilometa moja au mbili katikati yake kukiwa kumechomoza udongo mwekundu ambapo yasemekana ndipo palipokuwa sehemu ya soko.

Awamu ya maisha ya kimiji htko Begho ilitanguliwa na awamu ya maisha ya kilimo na ufugaji ya tarehe zinazorejea nyuma hadi miaka 3500 iliyopita. Ushahidi kutokana na vimfyange unadokeza kwamba kabla ya kipindi cha katikati ya kikwi cha pili (hasa katika karne za kumi na moja na kumi

ufalme mtukufu ilikuwa na dhima muhimu katika uendelezaji wake ilikuwa ni ile ya Benin na Nri.

Katika nchi ya Yoruba kuna masanamu mengi sana yaliyokatwa nakshi katika mawe. Masanamu hayo yanatofautiana kimtindo na yale ya Ife yaliyotumia shaba nyeupe na udongo wa kuchoma; ingawa yote yanapatikana katika eneo la maili sitini kuzunguka Ife katika msitu wa kati wa Yoruba. Katika vichaka vitakatifu vya Ife kuna sanamu za Wanegro zilizochongwa katika miamba migumu kwa mtindo wa maumbile asili. Sanamu maarufu kabisa kati ya hizi ziko katika vichaka vya Idena na Ore pamoja na sanamu ya mwanamke aliyepiga magoti, katika kichaka kingine kilicho jirani, iliyochoongwa katika jiwe-sabuni (steatite).

Kwingineko, hukohuko Ife, kuna mawe kadhaa yaliyochoongwa. Kati ya haya lenye kuvutia zaidi ni lile la nguzo ya mwamba mgumu lenye kimo cha futi 18 na lijulikanalo kama *Opa Oranmiyan* - yaani fimbo ya Oranmiyan - aliyekuwa mmojawapo kati ya watoto wa Oduduwa, muasisi wa Oyo. Katika soko kuu kuna jiwe la *Opa Ogun* - (fimbo ya Ogun,) mungu wa vita na chuma - lenye kimo cha futi sita lililochongwa kama rungu lenye umbo la mche duara.

Huko Eshure katika nchi ya Ekiti kuna michongo yenye kulandana, kama zile sanamu za mawe za Apa Ipetu ambazo zinashabihiana katika mkao, vidani, bangili za mikono na uvaaji wa nguo; lakini sanamu hizi zimechongwa kwa mtindo makini zaidi.

Mbali na zile za Eshure, sanamu za mawe ambazo zaonyesha uhusiano na mapokeo ya Ife zapatikana katika maeneo mengine ndani ya maili 30 kuzunguka Ife. Haya ni maeneo kama vile Kuta, lililo Maghribi; Ikirun, lililo Kaskazini, na Effon, lililo Kaskazini- Maghribi.

Kundi kubwa kuliko yote la sanamu za mawe katika nchi ya Yoruba liko katika mji wa Igbomina huko Esie; ambalo nao bado limo ndani ya msitu ingawa sura ya savana inaonekana maili chache tu kuelekea Kaskazini. Sanamu za mawe kwa hakika ni masafu ya kazi na shughuli za watu waliotangulia. Sanamu hizi za watu ambazo zajulikana kama *Ere* ni zaidi ya 800 kwa idadi na zinaonekana zilichongwa kwa kutumia jiwe sabuni. Sanamu ambazo ni kamili kwa kawaida zina urefu wa sentimeta(sm) 60 kwenda juu ingawa zinatofautiana kwa ukubwa kutoka sm 20 hadi sm. 130. Mapokeo yamehusisha sanamu hizi na watu waliokaa katika eneo hilo hapo zamani na ambao walitamalakiwa na Oyo. Walikuwa ni watu wa msituni waliokuwa katika kitende cha utamaduni wa Ife, ambacho athari yake inaweza kuonekana katika maumbile kadhaa yanayojitokeza- zatokeza katika sanamu hizo.

Sanamu za Ife za udongo wa kuchoma na za shaba nyeupe ambazo zimekadiriwa kuwa za karne ya kumi na moja na ya kumi na mbili, kwa hakika zilichongwa kama mapambo ya heshima ya ufalme wa kale wa *oni* (mfalme) wa Ife kama ilivyokuwa pia kuhusiana na vibago vizuri vya mawe ya kwatzi na nguzo za miamba migumu. Kutokea kwa zaidi ya sanamu 800 za Esie na vilemba vyenye urembo mwingi na mapambo mengine na kule kukaa kwao kwenye vibago kunadokeza kwamba nazo zinadhihirisha ufalme.

Ni muhimu kujua kuna viungo gani, kama vipo, vya kikronolojia au vinginevyo, baina ya sanamu zilizochongwa kwa mawe na yale mapokeo ya sanamu za udongo wa kuchoma na za shaba nyeusi; na vilevile uhusiano gani upo baina ya haya mapokeo ya uchongaji sanamu kwa kutumia mawe na yale yapatikanayo katika sehemu nyingine za Afrika Maghribi.

Willet, katika kazi yake juu ya sanaa ya Ife, amegundua sifa nyingi za jumla za uchongaji sanamu wa Ife zinazofanana na zile za Nok. Anadokeza pia kwamba maumbile asilia ya masikio ya sanamu za watu wa Ife yangeweza kutupa msingi wa kuwepo kwa mtindo huru wa kuifasili Benin. Ushahidi huu na mwingine unaofanana nao, yeye huchukulia kuonyesha miunganiko inayovuka kitambo cha muda na nafasi na wa mwendeleo wa mapokeo ya kisanaa katika Afrika Maghribi kwa zaidi ya vikwi viwili.

na mbili), makazi karibu na Begho (na katika awamu yake kabla ya kuwa miji) yalikuwa zaidi ni ya kundi la Wabono, wazawa wa hapo mahali. Kadri muda ulivyozidi kupita ndivyo pia mji livyozidi kukua kutoka katika msingi wa Kibrong (Kiakan) na kuingiza Wavolta na Wamande ambao walikuwa wakifanya shughuli mbalimbali.

Begho ilikuwepo kama kituo cha biashara kuanzia karne ya kumi na moja lakini haikufikia kilele cha ustawi wake hadi karne ya kumi na nne. Wakati huo yaelekea mji huo ulikuwa na viwanja takribani 500 na wakazi elfu tano. Mji huu ulikuwa umegawanyika katika sehemu kuu tano; sehemu kubwa kuliko zote ikiwa na upana wa nusu kilometa. Maeneo yao ya kulima yalikuwa mashambani, nje kabisa ya miji.

Kuna taarifa ndogo sana kuhusu aina ya jamii iliyoishi hapo wakati huo; labda twaweza tu kukisia kutokana na mitaala juu ya maisha ya kimapokeo ya baadaye ya Waakan. Hata hivyo mapokeo haya yanaonyesha kuwepo kwa watumwa wa nyumbani na mfumo ulioshamiri wa koo.

Kama makazi mengine mengi ya kale, haijulikani wazi jinsi Bono Manso ulivyoanzishwa. Kukua na umuhimu wake vilitokana zaidi na kuunganishwa kwa temi ndogondogo zilizokuwepo katika maeneo ya jirani, mwishoni mwa kikwi cha kwanza, na kuzifanya taifa moja. Bono Manso haukuwa mji wa kale kabisa miongoni mwa vijiji vikubwa na miji katika eneo hili, bali ulikuwa mji wa kwanza kushika hatamu juu ya makazi mengine yote kutokana na kuwa kwake mji wa wafalme wa Kibono.

Uchunguzi wa kiakiolojia umeonyesha kuwa kulikuwa na walau maeneo matano ya tasnia ya kazi za chuma. Moja kati ya maeneo haya ni la karne ya nne ya enzi ya Ukristo, lakini mengine pengine ni ya awamu ya ujenzi miji. Bono Manso ilikuwa katika eneo ambapo savana na msitu vilikutana, na ambapo, katika medani ya kikanda, bidhaa za savana ziliweza kubadilishwa kwa bidhaa za kutoka msituni. Eneo hili pia ndilo lilikuwa kikomo cha kusini kabisa kwa wanyama wabeba mizigo kufika bila kuathirika na magonjwa; na kwa hiyo pakawa eneo muhimu sana la kubadilishana bidhaa za kigeni kwa zile zilizotoka maeneo ya kusini zaidi. Eneo ambapo Bono Manso ilijengwa halikuwa tu chanzo cha dhahabu ya mitoni, ambayo ilitafutwa sana na wafanyabiashara wa Mande, bali pia lilikuwa ni chanzo cha kola.

Kinyume na Begho, hakuna ushahidi wowote unaonyesha kuwepo kwa sehemu ya makazi ya wageni. Hii ina maana kwamba watu wa Bono walikuwa wa asili moja zaidi kuliko wale wa Begho. Mamlaka kuu ya Bono pia yalidhibiti kikamilifu shughuli za kibiashara ambapo htuko Begho yaelekea shughuli za kibiashara zilikuwa zimezidi zile za kisiasa.

### *Nchi ya Yoruba kati ya mwaka 600 na mwaka 1100*


Katika nchi ya Yoruba utafiti wa kiakiolojia mpaka sasa umeishia Ife na Oyo tu; na hata katika hizi sehemu mbili ni awamu ya miji ya Ife tu ndiyo ya tarehe ya kipindi chetu.

Mji wa kimapokeo ya Kiyoruba ulikuwa na viwanja kadha na kila kiwanja kilikuwa nyumba zilizojengwa kuzunguka nyuga kadhaa za ukubwa mbalimbali. Hata hivyo kulikuwa na tofauti muhimu kati ya miji mbalimbali zikiwa zinaakisia tofauti za kihistoria na kiekolojia.

Wanahistoria kadhaa wamewahi kudokeza kwamba mojawapo ya vichocheo muhimu sana katika ukuaji wa miji pengine ilikuwa ni kuasisiwa kwa ufalme mtukufu. Ingawa mbimu hasa ya mweneo wake haijulikani yaonekana kuwa ndiyo pengine ilitoa msukumo wa nguvu katika ukuzaji wa maumbo ya miji. Hata hivyo, miji ya Kiyoruba ilikuwa matokeo ya miunganiko midogomidogo iliyochochewa na migawanyiko ya kitabaka ndani ya jamii badala ya mwendelezo wa ruwaza za mifano na mipangilio zilizokwishakuwepo kwingineko. Lakini mifumo ya dola ambamo dhana ya



**17.4** Kichwa cha Terra cotta kutoka kwense mwili, labda wa malkia, uliochambuliwa huko Ita Yemoo, Ite Uretu 23.1 cm. (Photo: copyright Frank Willett)



**17.5** Kichwa cha Terracotta kilichokutwa pembeni mwa barabara ya Ife wata, Ije Urefu 22.5 sm  
(Frank Willett)

Yaonekana Wayoruba hutupa kianzio cha kimantiki cha mitaala ya watu wa pwani na bara walioishi katika Guinea ya Chini. Dhima yao kubwa inadhahirika zaidi tunapochunguza miguro ya watu wa mwanzo kabisa huko kusini mwa Nigeria. Ni dhahiri kulikuwepo kwanza msambao wa kundi la Wayoruba-Waigala Maghribi na kuelekea kusini wakitokea katika sehemu yao ya asili huko Kaskazini-mashariki. Pili, mapokeo ya Waigala yanahusisha kuenea kwao mashariki ya ukingo wa Niger na miguro kuelekea mashariki dhidi ya Waidoma, na kusini dhidi ya watu wasemao Kiigbo. Tatu, nafasi ya Waitsekiri katika sehemu ya kusini-Maghribi ya delta ya Niger inaonyesha kwamba kuenea kwa kundi hili la Wayoruba kunaweza kuwa kumetokea kabla ya kuenea kwa wasemaji wa Kiedo kuelekea pwani.

Uvamizi wa mapema wa delta ya Niger uliofanywa na Waijo pia unadhahirika. Mguro huu wa kuelekea kusini yaonekana ulifuatiwa baadaye kwanza na mguro wa Waedo kuelekea kusini na kisha kupinda mashariki; pili, ulifuatiwa na kuenea kwa jumla kwa Waigbo katika uelekeo wa kusini hadi kufikia nyanda za juu Maghribi ya Niger; na tatu, ulifuatiwa na kusogea kwa Waigbo kwenye pwani ya delta ya mashariki ambako kulikuwa bado kukifanyika wakati wa maendeleo ya biashara ya utumwa.

Mpaka sasa Ife ndiyo makazi ya zamani kabisa ya Wayoruba yanayofahamika. Schemu hii ilitawaliwa na *onis* ambaye aliathiri eneo kubwa kwa nguvu za kiroho kwa kipindi kirefu sana. Ife pia ilikuwa kama kituo cha kutawanyikia na kupelekea kuanzishwa kwa Oyo na miji mingine mitano mikubwa ya Kiyoruba; na vilevile kama mahali ulipoondolewa ukoo tawala wa hapo awali huko Benin mnamo karne ya kumi na nne na kumi na tano. Ife pia yasemwa kwamba ilianzishwa na kikundi cha wavamizi kilichokuja na silaha za chuma, ambacho kilitamakani miongoni mwa wenyeji wa mahali hapo walioitwa Waigbo.

Kati ya karne ya saba na karne ya kumi na moja Ife, ilikuwa ikistawi kitamaduni na kisiasa. Baadhi ya sanamu za shaba nyeusi kwa hakika zimepewa tarehe ya katikati ya karne ya kumi na moja na inawezekana kwamba baadhi ya sanaa za udongo wa kuchoma ni za zamani zaidi kuliko hizo za shaba nyeusi.

Tunaweza kubainisha vipindi vikuu vitatu kuka kukua na kuendelea kwa Ife. Wakati wa awamu ya mwanzo kabisa inayopewa tarehe ya mwaka-350, Ife ilikuwa vitongoji kumi na vitatu tu vilivyotawanyika na ambavyo vilikalikiwa na wanavijiji wakulima. Awamu nyingine kuu ilikuwa ni kuasisiwa kwa Ife ya kipindi cha historia cha kati, ikiwa na muundo mzuri zaidi wa kijamii. Haijulikani wazi kama ukuaji huu wa mji na mabadiliko ya kijamii vilitokana na makubaliano huru ya jamii zenyewe au kama vilitokana na amri ya nguvu kutoka nje; wala hatujui kwa yakini matukio haya yalitokea lini. Hata hivyo, yaelekea kwamba walau baadhi ya maendeleo haya ya mwanzo na muhimu ya Ife yalitokea pengine kati ya karne ya saba na karne ya kumi na moja. Ni dhahiri pia kwamba ni mnamo kipindi hiki ndipo ruwaza ya barabara, ilivyo hadi hii leo, kwenda Edo, Old Oyo na kupitia Ilesha hadi Benin, ilipoanzishwa.

Mapokeo ya sanamu za maumbile asili huko Ife nayo ni ya kipindi cha walau mwaka 960 ± 130. Utengenezaji wa shanga za kioo zilizokuwa makini pia ulikuwepo Ife na Benin. Vyombo vya mfinyazi vya nyumbani vilivyotengenezwa Ife vyaelekea kuwa makini zaidi kuliko vile vilivyotengenezwa Nok; hasa kwa kuwa vile vya Ife vilikuwa na mapambo ya aina mbalimbali na ukataji nakshi, ung'arishaji, upakaji rangi na alama nyingine za kukatwa mapambo.

## Benin

Uchimbuzi wa Graham Connah umeonyesha kuwa kuta za Benin ni masega ya kazi za udongo



yaliyojengwa katika mistari kuwekea mipaka na siyo kama ngome za kujilinda. Haya yanadokeza kuwa jiji la Benin, kama ilivyokuwa Ife, linaweza kuwa limetokana na vikundi vidogo vidogo vingi, kila kimoja kikiwa kinamtii *oba* (mfalme) lakini kikiwa na mashamba yake, yaliyozungukwa na ukingo na mtaro wake. Jiji hilo lilizungukwa na ukuta wa ndani kabisa ambao haukujengwa kabla ya karne ya kumi na nne na yaelekea zaidi kwamba ulijengwa katikati ya karne ya kumi na tano.

Kwa upande mwingine, ukuta wa nje umechukuliwa kimapokeo kuwa kazi ya *oba* Oguola mnamo mwishoni mwa karne ya kumi na tatu; na kwa hakika ushahidi wa kiakiolojia unathibitisha kwamba ukuta huu una umri mkubwa zaidi kuliko ule wa ndani. Ushahidi kutokana na mabaki ya sanaa pamoja na mapokeo simulizi pia vyatoa mwanga juu ya kipindi hiki cha historia ya Benin. Sanaa za nyumbani, ikiwa ni pamoja na uchongaji miti, zilianza katika enzi ya Ere, ambaye alikuwa Ogisos wa pili wa ukoo tawala uliotangulia huu wa sasa, na ambaye yaelekea alianza kutawala kati ya 900 na 980. Huyu Ere ndiye asemekanaye kuwa alianzisha mapambo mengi ya kifalme na alama mbalimbali; na vilevile alianzisha vyama vya wachongaji na mafuzdi seremala. Iwapo hii ni sahihi, basi yaweza kuwa na maana kwamba jamii ya Benin wakati wa Ere ilikuwa imefikia hatua ambapo ilikuwa lazima kuanzisha rasmi vyama vya wasanii na mafundi. Imani kwa wahenga iliashiriwa na uchongaji wa vichwa vya miti ambavyo vilitumiwa katika muktadha wa ukumbusho. Kwa hiyo tabia ya kutengeneza vichwa vya ukumbusho yaweza kusemewa kuwa ilikuwepo miaka 350 au 450 kabla ya usubishaji wa shaba nyeupe – ambao ni kazi ya enzi ya utawala wa Oguola. Ingawa hatuwezi kuwa na hakika ni lini mfuatano wa vichwa vya shaba nyeusi ulianza Benin, tukio hili laweza kuwekwa kwenye robo ya kwanza ya karne ya kumi na nne.

Yaweza kuchukuliwa kwamba sanaa ya uchongaji ilikwishaanzishwa kabla ya unasabatawala wa Ogiso kushika madaraka ya utawala. Hivyo msingi ulikuwa umekwishawekwa wa uanzishaji wa matengenezo ya vichwa vya shaba nyeusi kwa ajili ya ukumbusho wa wafalme waliopita. Ingawa teknolojia ya kazi za shaba nyeusi ilianzishwa Benin katika kipindi cha utawala wa Oguola, lakini mapokeo yaliyopo yanaeleza kwamba kazi za sanaa ya shaba nyeusi zilipelekwa Benin kutoka Ife kabla ya utawala wake. Hakuna anayejua jambo hili lilitokea muda gani kabla ya utawala wa Uguola.

Ushahidi wa kiisimu unadokeza kwamba Waedo wamekuwepo hapo walipo hii leo kwa muda wa takribani miaka elfu nne. Kwa sehemu kubwa ya kipindi hiki, vijiji ndivyo vilivyounda kitengo cha kisiasa, ambako ruwaza muhimu ya madaraka ilijengwa na vyama vya wanaume wa marika. Kilichosababisha kutokea kwa mfumo mpya wa utaratibu wa kisiasa badala ya ule uliokuwepo zamani bado hakijulikani. Baadhi ya wanazuoni wamedokeza kwamba utaratibu huu mpya ulitokana na kujipenyeza katika jamii hii kwa mfumo wa zamani zaidi wa nchi ya Yoruba, ambayo ilikuwa jirani, na ambako kwa muda wa miaka mingi kulikuwa na utaratibu wa kitovu kimoja cha shughuli za kisiasa au ufalme. Wengine wamedokeza kwamba utaratibu huu uliokana na ukuaji huru wa vitengo vikubwa zaidi vya kisiasa katika eneo hili.

Awamu hii ya mwanzo ilifuatwa na kipindi cha "kujichambua" miongoni mwa miji ya awali ambayo ilihusisha ushindani mkali wa kisiasa. Katika kipindi hiki cha ushindani miongoni mwa temi mbalimbali (tk. 1170), na kutokana na ushindani huo, nasaba tawala ya kigeni kutoka nchi ya Yoruba ilingizwa Benin. Nasabatawala huu mpya ulianzisha utaratibu ambao kwao Benin ilijitokeza kama makazi makubwa ya kimji katika eneo hilo.

### *Igbo-Ukwu na "ufalme" wa Nri*

Mkusanyiko wa kale kabisa wa shaba nyeusi ya Kinigeria, umechimbwa katika nchi ya Igbo



17.6 Machimbo ya Igbo-Ukuvu. ▲ Chungu chenye kamba za Shaba nyensi na kishukio chake (nyuma na kushoto) kwenye Ghala la mavazi rasmi (vipimo: futi 1 urefu). ▲ Chombo cha Chungu kilichopambwa sana kutoka kwenye mashimo ya Igbo-Ukuvu (urefu: sm 40.6).



mashariki mwa Niger. Takribani sanamu 100 za shaba nyeusi zilionekana huko Igbo-Ukwu (Kaskazini mwa nchi ya Igbo) na huko Ezira, kilometa 24 mashariki mwa Igbo-Ukwu. Miongoni mwa vitu hivi vilivyopatikana kuna vitu kadhaa ambavyo vinaelezwa kama vichwa vya fimbo, sanamu za binadamu, meno ya tembo, vitu vilivyotengenezwa kwa shaba nyeusi vikiwa vinaonyesha nzi, wadudu warukao, mayai ya panzi, na vichwa vya wanyama kama vile chui, tembo, kondoo dume, tumbili, konokono na chatu. Idadi kubwa ya shaba nyeusi hizi ni ndogondogo isipokuwa baadhi ya vyombo vyenye kipenyo cha sm. 40; na sanamu za binadamu ni chache, ikiwa ni pamoja na kichwa cha Kianus (chenye nyuso mbili), pambo la kuning'inia usoni, mpanda farasi na sanamu za sehemu za mbele kwenye madhabahu. Eneo hilo limekadiriwa kuwa wa umri wa karne ya tisa, na hivyo kuwa la kale zaidi kuliko Ife, ambayo imekuwa ikichukuliwa kuwa mwanzo wa mapokeo makuu ya Nigeria katika kazi za metali. Vitu vyote vilivyopatikana Igbo-Ukwu, ikiwa ni pamoja na udongo wa mfinyanzi, kioo, vifaa vya kisanii vya chuma na shaba, pengine ni vifaa alivyoziikwa navyo mtawala wa zamani wa Kiigbo aliyetamalaki Igbo Kaskazini na maeneo ya mbele yake.

M.A. Onwuejogwu amejaribu kuunda mfumo wa utaratibu wa kisiasa-kijamii wa watu wa Nri kuanzia nyakati za kale kabisa zijulikanazo hadi kufikia karne ya kumi na nane. Hitimisho lake kubwa ni kwamba Wanri wa Igbo-Ukwu na maeneo jirani walikuwa wameanzisha mfumo wa dola ulidumishwa na kusimikwa kwa mbinu za ibada kwa ishara.

Ushahidi wote uliopo unadokeza kuanzishwa kwa utawala wa Nri katika nchi ya Igbo tangu karne ya tisa. Ujengaji makoloni na upantaji wa ufalme wa Nri uliwezekana kutokana na kuwapeleka watu wa Nri katika makazi mengine ambako utii wa watu wa sehemu hizo kwa *Eze Nri* (rafalme) ulipatikana kwa kula kiapo. Amri ya *Eze Nri* ilitekelezwa si kwa kupitia nguvu za majeshi, bali kwa viziuzi vya matambiko na usirisiri. Mamlaka yote yalikuwa mikononi mwa mtawala (*Eze Nri*) na utii katika himaya yake ulidumishwa na makuhani wazungukaji ambao waliondoa chuki katika nyoyo za watu na kuwapa watu haki za uongozi. Ingawa hii leo hakuna mabaki yoyote ya nguvu za *Eze Nri*, jamii zenye koo bora zinaendelea kuwa na nafasi kubwa katika maamuzi mbalimbali, japokuwa kuna vyombo vya kitaifa na kiserikali.

Athari ya Nri ilienea kuvuka eneo lake la kiini huko Waigbo Kaskazini hadi makazi ya Wa-Igbo kwenye ukingo wa Maghribi wa Niger na kwenye jamii zilizokuwa zimeathirika na utawala wa kihistoria wa Benin katika Niger ya chini.

Kuna mifanano michache baina ya utaji subu wa shaba nyeusi wa Kiigbo-Ukwu, Kiufe na Kibenin; kama vile utumiaji wa sanaa ya uchongaji wa maumbo ya kichwa cha kondoo dume na kichwa cha tembo; lakini pengine hivi vitu si muhimu katika maswala ya historia ya sanaa. Uchanganuzi wa mambo pia umeonyesha kwamba sanamu nyingi za Niger ya chini zinafanana na zile za shaba nyeusi za Igbo-Ukwu ambapo zile za Benin karibu zote ni za shaba nyeupe ambayo madini ya zinki yaliyomo ndani yake yalizidi kuongezeka kadri muda ulivyoendelea kupita.

Magunduzi haya yote yanaelekea kuunga mkono madai ya William Fagg kwamba kulikuwa na vikundi vikuu viwili vya mitindo ya kazi za madini huko Afrika Maghribi, yaani kikundi cha Ife/Benin na kile cha Yoruba ya leo katika sehemu ya kati ya Nigeria; vikiwa vimepakana na mapokeo yaliyotumia nyuzi nyembamba za nta au gundi katika kutengeneza vifaa vyao. Inaelekea kwamba mapokeo ya Ife/Benin yalipenya katika eneo la mapokeo makongwe na bayana. Inawezekana pia kwamba desturi za ufuaji chuma huko Igbo-Ukwu zilikuwa tofauti na zile za ufuaji chuma za Ife/Benin na Nok.

Machimbo ya Iuko Igbo-Ukwu yanaonyesha dhahiri kwamba kazi za chuma kusini-mashariki mwa Nigeria ni za tarehe ya walau karne ya tisa, na kuna kila sababu ya kuonyesha kwamba kazi

hizo zilikuwa kongwe zaidi. Vitovu vingine vya kazi za madini miongoni mwa Waigbo ni vile vya wayeyusha chuma wa Kiabiriba, na wafua vyuma na shaba nyeusi waliokuwa karibu na mwinuko wa Okigwe-Arochuku, na wahunzi wa Nkwerre katika sehemu ya kusini ya kanda hii.

Haikuwa dhahiri mahusiano ya kiwakati/kitamaduni yalivyo baina ya Ife na Igbo-Ukwu, ingawa Willett anafikiri kwamba inawezekana Ife ni ya tarehe ya zamani zaidi kuliko ijulikanavyo hii leo na inaweza ikawa karibu zaidi na Nok kuliko ushahidi wa sasa (karne ya kumi na kumi na mbili) unavyodokeza. Ama kwa hakika, iwapo shanga za Ife ni sawa na zile za "akori" za pwani ya Guinea, basi inawezekana kabisa kwamba shanga za kioo za Igbo-Akwu zilitengenezwa huko Ife. Ikiwa hivyo ndivyo, ina maana kwamba tarehe ya utamaduni wa Ife ni sawa na walau ile ya vitu vilivyopatikana Igbo-Ukwu (karne ya tisa).

Vitu vya shaba nyeusi na shanga vinaakisitaji utajiri wa uchumi na usanii wa hali ya juu wa wachonga sanamu za shaba nyeusi. Aidha vitu hivyo pia vinaonyesha ni kwa kiwango gani eneo hili lilikuwa sehemu ya mfumo wa biashara ya kimataifa. Kwa mujibu wa Thurston Shaw, mali ghafi ya kutengeneza shaba, yaani shaba nyekundu na shaba nyeusi iliyotiwa risasi, viliagizwa kutoka migodi ya shaba ya Tekedda na mbali zaidi huko Sahara. Hata hivyo, inavutia pia kuona kwamba vitu kama hivyo vilipatikana huko Abakaliki na Kalabar, na yawezekana kabisa kuwa vilitoka huko.

Tamaduni yakiniifu za Igbo-Ukwu, Ife na Benin ya kale mara nyingi huchukuliwa kwamba ndizo ziwakilishazo hatua ya juu kabisa ya maendeleo ya Enzi ya Chuma katika eneo hili. Machimbo yanadhihirisha watu wenye zana za vyuma na silaha za kuweza kuufanya msitu utoe utajiri mkubwa na matumizi ya fikra za ujenzi miji na utaratibu wa kijamii na kisiasa kwa mafanikio makubwa. Zaidi ya hayo, huenda walikuwa katika mahusiano ya kibiashara na ulimwengu wa Kiislamu na inawezekana walipata au hawakupata maarifa ya sanaa ya zamani ya kusubisha metali kwa kutumia nta kwa njia hiyo.

## Akwanshi

Katika sehemu ya Kaskazini ya bonde la Mto Cross kuna ushahidi wa urithi wa sanaa ya pekee ya sanamu za mawe zijulikanazo kama *akwanshi*. Sanamu hizi zaonekana kuwa kazi za wahenga wa kundi la Wabantu wa Kiekoi waliokuwa wakiishi Kaskazini - hasa watu wa Nta, Nselle, Nnam, Abanyom nba Akagu.

Uchongaji mawe magumu kuwakilisha sura ya binadamu unatokea tu katika eneo dogo la chini ya kilometa za mraba 1,000 kwenye ukingo wa kulia wa Mto Cross. Hapa, mnamo mwaka 1961 na 1962, P. Allison aligundua mawe 295 ambayo yalikuwa yamechongwa kwa ustadi wa aina tofautitofauti kuwakilisha sura ya binadamu. Mawe haya ya sanamu yanapatikana katika maeneo makuu ishirini na sita (26) katika ardhii iliyokaliwa na makundi madogo sita ya mbari ya Waekoi yaliyokuwa huru hapo awali. Sanamu zilizo nyingi zaidi na zilizochongwa kwa ustadi mkubwa zaidi hupatikana katika nchi ya Wanta (sanamu 50), Wanselle (90) na Wannam (94). Sanamu hizi zilichongwa kwa kutumia aina ya mawe meusi magumu (basalt), ambapo zile za Abanyom na Akagu zimechongwa kwa kutumia aina ya chokaa ngumu. Watu wa Nta na Nselle huita mawe yao Akwanshi, yaani "wafu waliozikwa."

Watu wa *Akwanshi* huzungumza aina mbalimbali zenye kuhusiana za lugha ya Wabantu wa Kiekoi. Katika nyakati za hivi karibuni mambo ya kila jumuiya yalikuwa yakiiongozwa na wazee ambao chini yao vijana wa kiume walipangwa kwa makundi ya marika. Kulikuwa pia na *Ntoon*, au watemi makasisi ambao kazi yao kubwa ilikuwa ni shughuli za kidini na maadhimisho. Mawanda ya mamlaka ya *Ntoon* yalitofautiana kutoka kijiji kimoja hadi kwenye kikundi chote.

Allison alijaribu kuunda upya shajara ya wamakuhani wa *Ntoon* katika Wanta kwani aliambiwa, kwa sababu thabiti, kwamba *Akwanshi* zilikuwa ukumbusho wa waanzilishi wa ufalme huo. Yaelekea kwamba hapo awali watu wa huko walikuwa katika ufalme mmoja mkubwa kama walivyokuwa watu wa Bini na wale wa nchi ya Yoruba. Majenzi ya *Akwanshi* za mazishi kubwa na za zamani yanaashiria kuwepo kwa mifumo mikubwa na madhubuti ya kijamii-kisiasa yenye kiutovu kimoja na iliyokuwa na wafanyakazi wa kutosha.

Asili za *Akwanshi* zaweza kuwa popote kati ya karne mbili au tatu za mwisho za kikwi cha kwanza cha enzi ya Ukristo na karne za kwanza mbili au tatu za kikwi cha pili, yaani karibu wakati mmoja na Igbo-Ukwu. Yaelekea kutokea kwa biashara ya watumwa ya kuvuka bahari ya Atlantiki kulikuwa na athari mbaya juu ya dola hii.

### *Biashara ya awali*

Kama tulivyokwishaona, makundi mengi ya Wakan, Waewe, Waga-Adangme, Wayoruba, Waedo, Waigbo na mengine yanayohusiana nayo kama yajulikavyo hii leo yalikuwa yamekwishakalia karibu sehemu zilezile za Guinea ya Chini mnamo karne ya kumi na moja na karne ya kumi na mbili, na pengine mapema zaidi. Wayoruba, basa wakati huo, walikuwa wamekwishakuwa wakazi wa mjini inavyotubitishwa na ushahidi wa machimbo ya miji kama Ife, Oyo ya Zamani na Ileshe. Hali ilikuwa hivyo pia kwa Waedo inavyoakisiwa na machimbo huko Benin. Schemu nyingine kama Igo-Ukwu katika Nigeria na Bono Manso katika Ghana zilianzisha mifumo ya kidola ya hali ya juu zaidi.

Miji hii ilibainishwa na makazi mengine kwa misingi ya ukubwa wake, vilivyomo ndani yake, muundo wa jamii, na katika taratibu na shughuli zake. Kadri muda ulivyozidi kusonga mbele, miji hii ilikua na kuwa na shughuli na kazi mbalimbali za ufundi maalumu ikazalisha bidhaa kuzidi kiasi kilichohitajika kwa matumizi ya ndani, na vilevile ikawa na masoko makubwa katika maeneo muhimu kibiashara na katika umbali maalumu kutegemea maliasili ilizozitegemea kwa ufanisi wake.

Kutokana na ukubwa na uchangamano zaidi wa kijamii, kiuchumi na mfumo wa kisiasa wa baadhi ya miji, haukupita muda wakazi wake wakaanza kuwa na mgawanyiko katika utiifu wao kwa watawala, wakati ambapo vijiji vilikuwa na umoja zaidi chini ya mtemi mmoja, baraza moja na uzoefu wa aina moja wa shughuli za kilimo. Ama kwa hakika, kufikiwa kwa kiwango muhimu cha teknolojia na maarifa ya kuwawezesha kuhimili idadi kubwa ya watu, na pia viwango vya juu vya uyakinifu katika shughuli za kiuchumi, tulivyokwishaeleza hapo juu, lazima vilihimiza kuwepo kwa biashara ya masafa marefu ya aina mbalimbali.

Miongoni mwa jumuiya nyingi za awali zilikuwa zikijihusisha na kilimo, mashoka ya mawe yaliyong'arishwa vizuri (huko Ghana wakiyaita *nyame akume*) yaliuzwa katika masafa ya mamia ya kilometa. Mashoka ya mawe ya kijani kutoka eneo la Bibiani yanapatkana katika sehemu kubwa ya Ghana kusini. Mawe ya kuparua ya utamaduni wa Kintamp ambayo yametoa ushahidi wa kale kabisa wa shughuli za kilimo - katika Ghana (kwenye miaka ya 1500) yalitengenezwa kutokana na mawe ya chokaa ambayo yaliuzwa sehemu mbalimbali, kwani aina hiyo ya mawe imeonekana kwenye tambarare za Akkra na Ghana Kaskazini. Huko Kumasi, "kiwanda" cha mashoka ya mawe ya kusagwa kimechimbuliwa. Huko Rim, karibu na Wahiguya, tabaka za enzi ya neolithi/Enzi ya Mawe ya Baadaye zinahusishwa na maeneo ya viwanda vya mashoka. Eneo hili yaelekea lilikuwa kituo kikuu, kikiuza mashoka kwa maeneo ambayo hayakuwa na mali ghafi. Kwa vyovyote vile umbali mkubwa uliogubikwa na mtawanyiko wa mashoka ya mawe-kijani na mawe ya kuparua vinaonyesha kuwepo zaidi kwa biashara ya masafa marefu, kuliko kuwapo kwa mabadilishano ya ndani tu.

Kuna ushahidi wa biashara ya ndani kwa ndani ya vyombo vya mfinyanzi huko Ghana kulingana na utambuzi wa udongo wa mfinyanzi katika vyungu ambao ni wa kigeni katika maeneo ambako vyungu hivyo vilipatikana. Vyombo kadhaa kati ya vile vilivyojibainisha sana huko New Buipe vilitengenezwa kwa udongo wa mfinyanzi uliotoka umbali ufikia kilometa 100 kutoka eneo vilipofinyangwa. Vyungu kutoka eneo la juu la Ghana vilizwa katika eneo la kaskazini, ambako ufinyanzi mdogo sana ulifanywa.

Kuanza kwa biashara ya masafa marefu katika Afrika Maghribi kunahusiana na utafutaji wa mawe na udongo wa mfinyanzi vilivyotajwa hapo juu, na vilevile metali. Yaelekea ni busara kufikiria kuwepo, tangu Enzi ya Mwanzo ya Mawe, kwa mfumo changamano, na ulioenea sana, wa biashara ya masafa marefu iliyotokea kwenye vituo vichache vya kati vilivyokuwa katika maeneo maalumu ya kiekolojia na kuunganisha watu wa pwani na wakulima wa bara kwa upande mmoja, na vilevile watu wa kusini na wafugaji wa kaskazini, kwa upande mwingine.

### Hitimisho

Kuwepo kwa ufundi wa aina mbalimbali kulikothibitishwa kunadhihirisha kwamba kulikuwepo na teknolojia ya hali ya juu, ulimbikizaji mali, asasi ya uongozi wa kimila na kushiriki katika biashara. Yawezekana kiasi kikubwa cha shaba iliyopatikana katika machimbo ndiyo ilivyokuwa ikitumika kama fedha halali ya biashara. Shaba iliyotumika katika kutengeneza sanamu ilikuwa ya asili ya kuvuka Sahara wakati ambapo shanga nyingi zilizopatikana huenda zilitengenezwa India na baadhi labda zilitengenezwa Venise, ingawa kipindi cha miaka ya + 900 chaelekea ni mapema mno kufikiria kuwepo kwa mawasiliano na bandari ya Italia. Sehemu za karibu zaidi ambazo zafikiriwa kuwa pengine ndiko shaba ilikotoka ziko katika eneo la Azelik (Takedda) huko Air na Nioro huko Mali. Wingi wa vyombo vya shaba huko Nigeria kusini kabla ya + 1300 waashiria kwamba kulikuwepo na biashara ya mawanda mapana na pengine ilikuwepo kwa miaka takribani 500 kabla ya tarehe hiyo.

Biashara ya masafa marefu katika bidhaa za anasa zilizokuwa zikitegemea matabaka ya kijamii pengine ilikuwepo hata nje ya masoko ya nchini. Katika baadhi ya sehemu biashara ya kawaida iliendelezwa katika vitu maalumu kama vile chumvi, nguo, metali, shanga, vyombo vya mfinyanzi na zana za mawe kuanzia enzi ya neolithi/Enzi ya Mwanzo ya Mawe. Hata hizo biashara za kikanda zinaweza kuwa hazikuanzisha masoko mapya kabisa bali zinaweza kuwa zimcanzisha tu mawasiliano ya kawaida zaidi kati ya masoko yaliyokuwepo lakini ambayo mawasiliano yake hayakuwa ya vipindi. Kwa mfano, biashara ya kikanda katika zao la chumvi ni ya tarehe ya nyuma kabisa ya kufikia walau mwishoni mwa Enzi ya Chuma na ilikuwa ikianzia Sahara hadi Sudan na pwani hadi msituni. Sehemu kubwa za delta ya Niger ni za vinamasi na chumvichumvi mno kuwezesha kuwepo kwa kilimo kingi, lakini kwa upande mwingine sehemu za bara hazina mashapo ya chumvi. Kwa hiyo maeneo yote mawili yalinufaika kwa kubadilishana chumvi na samaki wakavu kwa bidhaa za ziada za kilimo na wanyama.

Biashara ya kanda katika zao la shanga imeonyesha zaidi uelekeo wa kimashariki-Maghribi kuliko wa kiKaskazini-kusini. Aina moja ya shanga ambayo haijawahi kutambuliwa kwa makini lakini ambayo imekuwemo katika harakati za biashara ya masafa marefu kwenye Ghuba ya Guinea ni ile iliyoitwa *akori*.

Mitandao ya biashara ya kikanda pia ilianzishwa kwenye vituo vya viwanda vye nguo. Vituo hivi vya viwanda vya nguo vilikwishafikia ubora wa hali ya juu katika eneo la utamaduni wa Igbo-

Ukwu na vikaendelea kuwapo hadi nyakati za hivi karibuni. Kwa mfano, katika karne ya kumi na sita watu wa Benin walitumia aina ya nguo zilizofanana na zile zilizopatikana huko Igbo-Ukwu. Hata hivyo mitandao muhimu kabisa ya biashara ya kikanda katika bara ya Igbo kuanzia enzi za Igbo-Ukwu ilikuwa ni ile ya chuma na metali nyingine na pengine ilihusisha pia wafuametali watembezi.

---



18

## *Watu wa Guinea ya juu: kati ya Cote d' Ivoire na Kasmansi*

### *Mfumo wa Kiisimu na wa Kimbari*

Wakazi wa jimbo la Guinea ya Juu wanatokana na vikundi vidogo vya lugha kuu tatu za familia ya Kiniger-Kikongo: Kimande, Kiatlantiki Maghribi na Kikwa.

#### **Kimande**


Kundi ambalo linafahamika na limejienga zaidi kati ya haya ni life la Kimande – ambalo lina lugha karibu 25 zinazoanzia Busa huko Nigeria hadi Gambia upande wa Maghribi, na kuanzia Soninke kwa upande wa Kaskazini hadi Vai-Kono kwa upande wa kusini. Lugha zote za Kimande zimegawanyika katika makundi mawili - kundi la Kaskazini (au Kaskazini-Maghribi) na kusini (au kusini mashariki). Kiwango cha uhusiano baina ya kila moja ya lugha hizo kinaeleweka. Kikundi cha kusini-Maghribi katika kundi la Kaskazini- Maghribi kinajumuisha lugha kama vile Kimende, Kikpelle na Kiloma ambazo zinazungumzwa Sierra Leone, Liberia na Guinea; ilihali kikundi cha Kaskazini cha kundi hilo hilo kinajumuisha Kisoninke, Kimandenka (Kibambara, Kimalinka, Kidyula n.k.),

Kisoso-Yalunke, Kivai-Kono na lugha nyinginezo. Hadi hivi karibuni kundi la kusini lilihukuliwa kuwa na vikundi vidogo viwili tofauti - cha kusini kinachojumuisha Kimano na lugha chache nyingine ndogo ndogo huko Liberia na Cote d'Ivoire, na cha mashariki ambacho kilijumuisha kiasi fulani cha lugha ndogo zilizotawanyika (Kibusa, Kibisa, Kisamo) na kusambaa huko Burkina Faso, Benin ya Kaskazini na Maghribi ya Nigeria. Lakini hivi sasa inethibitishwa kuwa vikundi hivi vidogo vinahusiana sana na kwa misingi hiyo vinaunda kundi moja tu.

Kimandenka kina sifa tatu za pekee. Sifa hizo ni idadi kubwa ya wazungumzaji wa lugha hii, ukubwa wa eneo lake, na mshikamano wa watu wake. Eneo la wazungumzaji wa Kimande lilikuwa chimbuko la madola ya mwanzo ya Sudan Maghribi, ambayo kati yake ya awali kabisa ni dola la Ghana, ambalo lilisitawi zaidi ya miaka elfu moja iliyopita. Kulingana na mapokeo simulizi, kupantika kwa Kimande hadi Gambia kulitokea wakati wa utawala wa Sundiata mnamo karne ya kumi na tatu, na makazi ya biashara upande wa kusini yalianzia karne ya kumi na nne, kama sio mapema zaidi.

Mtawanyiko wa kijografia wa watu wanaozungumza Kimande unaweza kupata maelezo mbalimbali ya kihistoria. Kwa vile idadi kubwa ya Wamande inawakilishwa na Wamandenka tu, kwa muda mrefu ilishikiliwa kuwa asili ya Wamande wote ilikuwa katika eneo la Senegal-Niger ya Juu katika nchi ya Mali ya hivi sasa. Ilifikiriwa pia kuwa wazungumzaji wengine wote wa lugha za 256





18.1 Lugha za Afrika Magharibi (zilizoamshwa kwa urahisi na lugha kuu kadhaa kuonyeshwa).

(B. W. Andah)

Kimande walikuwa vizalia waliotokana na mfululizo wa makundi makundi ya kutoka kitovu hiki cha asili. Hii inaelekea kuwa kweli hasa kwa uhamaji wa baadaye wa watu (ambao pia unafahamika kama mtawanyiko wa pili wa Wamande), ambao ulielekezwa zaidi upande wa kusini na Maghribi.

Kwa upande mwingine, inaweza kufikiriwa kinadharia kuwa Wamande (au Mame-Mande) walianza kuhama makazi yao ya kabla ya historia iliyoandikwa, huko karibu na Ziwa Chad na baada ya kuvuka Mto Niger, waliendelea kwa kufuata zaidi mwelekeo wa Maghribi au kusini Maghribi. Uhamaji huu lazima ulitokea kabla ya ule wa Gur (uhamaji wa Volta) na wa watu wanaozungumza Kikwa. Mapokeo simulizi ya Wabisa (Wabusanse) na Wamossi-Dagomba yanaeleza kuwa Wabisa walikuwa kwenye makazi yao ya hivi sasa muda mrefu kabla ya kuanzishwa kwa tawala za baadaye. Mapokeo ya Wabusa (huko Nigeria) yanasimulia kuwa walikuja kutoka mashariki.

Yote haya yanaashiria kuwa watu wanaozungumza Kimande ambao sasa wanaishi katika nchi za Burkina Faso, Benin na Nigeria si vizalia wa mashariki kabisa waliotokana na upanuzi wa Wamande unaoanzia Maghribi, bali ni Wamande waliobaki nyuma baada ya uhamaji wa Wamande wa kusini kutoka mashariki hadi kusini Maghribi, kama unavyoonyeshwa na uhusiano wao wa karibu kiisimu.

Kwa upande wa kiunzi cha kikronolojia (mfuatano wa miaka), Welmens alipendekeza kuwa lugha za Kimande zinawakilisha lugha zilizojitenga mapema sana na lugha za Kiniger-Kikongo, akikadiri kuwa mchepuko huu huenda ulitokea kama mwaka - wa 3300; kutengana baina ya Wamande wa kusini na wale wa Kaskazini-Maghribi pengine kungetokea kama mwaka wa 1600. Hata hivyo, kwa vile tarehe hizi zimekitwa kwenye glotokronolojia ambayo mbinu zake zinazidi kushambuliwa na wanaisimu wengi, lazima zikubaliwe kwa tahadhari kubwa.

Hata hivyo, hapana shaka kuwa sehemu kadhaa za Liberia na Cote d'Ivoire, katika kipindi kinachozungumziwa, zilikuwa tayari zimekaliwa na watu wanaozungumza lugha za Kimande wa kundi la kusini. Wamande wengine (Wavai, Wakono, Wamende, Wasoso, Wakpelle/ Waguerze, Waloma/Watoma n.k.) walihamia upande wa pwani katika karne tano au sita tu zilizopita na uhamaji wao umeelezewa katika Juzuu lifuatalo<sup>1</sup>.

### **Kiatlantiki Maghribi**

Tofauti na uhusiano wa ndani wa kundi dogo la Wamande, kundi la Kiatlantiki Maghribi lilikuwa kwa kiasi fulani tofauti zaidi, likiyameza makundi madogo yaliyokuwa maarufu kihistoria na kipindi muhimu cha ukuaji wa lugha kama ilivyokuwa kwa lugha za Kimel.

Kundi la Kiatlantiki Maghribi ni kundi lenye lugha tofauti zinazozungumzwa kwenye eneo la pwani linaloanzia kwenye mpaka wa Senegal na Mauritania upande wa Kaskazini-Maghribi hadi kwenye mpaka wa Sierra Leone na Liberia upande wa kusini-mashariki. Lugha ya pekee ambayo ni tofauti ni ile ya Kipular (au Kifulfude), lugha inayozungumzwa na watu wa mbuga za savana kuanzia Senegal Kaskazini hadi Kameruni ya kaskazini na eneo la Chad. Tofauti kabisa na Kipular, nyingi miongoni mwa lugha za Kiatlantiki Maghribi zinazungumzwa na idadi ndogo ya watu na ambao mara nyingi wametawanyika. Idadi ya wazungumzaji wengi ni 200,000 na zaidi (k.m. Wadyula na Wakisi) na baadhi zilikuwa na wazungumzaji wachache wanaofikia mamia kadhaa (k.m. Wakobiana). Licha ya sifa fulani za kimaumbo zenye kufanana kama vile mfumo wa ngeli na viambishi vinavyonyambulisha vitenzi, hakuna kitu kingine kikubwa kinachopambanua kundi hili zima kwa namna nyingine iliyo dhahiri zaidi. Japokuwa kundi hili ni dogo kwa idadi ya

1 Taz. juzuu la IV, Sura 12.

wazungumzaji, sifa hizi ni dhahiri vya kutosha kukiri kuwa hili ni kundi moja japokuwa mahusiano yake ya kijenetiki ni mapana sana. Kikwa Kundi la kwa huishi katika ukanda wenye upana wa karibu wastani wa km 320 na urefu wa karibu km 2,240 kandokando ya pwani ya Afrika Maghribi kuanzia Monrovia nchini Liberia kwa upande wa Maghribi, kupitia Cote d'Ivoire, Ghana, Togo na eneo kati ya Benin na mashariki ya delta ya Mto Niger. Lugha nne muhimu zaidi za kundi la Kikwa kufuatana na idadi ya wazungumzaji ni (1) Kiakan, (Kitwi, Kifanti), ambacho kinazungumzwa sana Ghana, (2) Kiewe, lugha inayozungumzwa zaidi Togo na Dohomey na inayozungumzwa pia kusini-mashariki mwa Ghana; (3) Kiyoruba, kinachozungumzwa zaidi Nigeria ya Maghribi; na (4) Kiigbo, kinachozungumzwa zaidi Nigeria mashariki; zote zikiwa ni lugha za kisilabi na zenye toni ya kimuziki<sup>2</sup>. Uchunguzi wa makini unaonyesha kuwa sehemu kubwa ya ukanda wa msitu wa Afrika Maghribi, zaidi ya maili elfu moja kutoka Liberia ya kati hadi kupita Niger ya chini huko Nigeria, imekaliwa na watu wanaozungumza lugha nyingi zinazohusiana, lugha ambazo zina mambo mengi sana ya kimsamiati na kimuundo yanayofanana. Iwapo sifa hizi zinaakisi mame-lugha moja, basi ushahidi wa kiisimu unaashiria hapa kuwepo kwa mwendelezo wa kitamaduni wa mapema sana kwenye sehemu kubwa ya ukanda huu wa msitu, na kutofautiana kulikofuatia tangu kipindi cha mapema zaidi lakini ambacho hakifahamiki.


Ushahidi wa kihistoria na kijiografia unaonyesha kuwa msitu huo haukuwa rahisi kwa watu waliokuja baadaye kuupenya, na wakati ilipowezekana kuupenya ni makundi madogo tu ya wahamaji yaliyoweza kufanya hivyo. Upenyaji huo ulifanywa na makundi madogo madogo ambayo, hata kama yalileta athari za kutosha za kitamaduni, yalimezwa kiisimu na wenyeji. Ni katika maeneo ya Maghribi ya mbali tu ndipo wakazi wa Kaskazini walipopenya kwa wingi, wakianzisha tawala za wapiganaji kama zile za Wamende wa Sierra Leone, ambazo ziliipeleka lugha ya Kimande hadi pwani.

### *Dhima ya Kundi la Kimande*

Mada kuu katika kuichambua historia ya jimbo hili ni ile ya mgongano baina ya desturi mbili za kitamaduni zilizowakilishwa na watangulizi wa wazungumzaji wa Kimele wa pwani na kundi lililokuwa likipanuka la wazungumzaji Kimande kutoka bara.

Enco hili lilikuwa na mipaka mingi ya uhamiaji, uongezekaji wa idadi ya watu na ushindani baina ya makundi kadri watu kutoka bara walivyozidi kuingia kwenye misitu ya tambarare za pwani wakitafuta ardhi na biashara. Hapana shaka pia kuwa kupenya kwa makundi yanayozungumza Kimande kutoka mashariki kulikuwa ni jambo kubwa lililochangia katika uhamaji huu.

Hata hivyo, matatizo ya kimisingi yanabakia kuhusu historia ya kijamii na kitamaduni ya eneo hili kabla ya karne ya kumi na tano na hasa mwishoni mwa kikwi cha kwanza na mwanzoni mwa kikwi cha pili. Kwa mfano haeleweki iwapo uvamizi wa Wamane ulifanyika kwenye karne ya kumi na nne, kumi na tano au kumi na sita. Pia kuna kutokukubaliana kuhusu namna uvamizi huo ulivyofanyika na athari zake kwa wenyeji. Je, vilikuwa ni vita vya muda mfupi vilivyoishia kwa wavamizi kusimilishwa na wenyeji au uhamaji wa watu wengi ambao ulikuwa na matokeo dhahiri na ambayo wakati mwingine yalikuwa na athari mbaya kwa makundi ya asili? Kwa mfano, Rodney na Lamp wanahusisha uvamizi huu na uharibifu wa stadi za Wasape (ambao wanajumuisha Wabulom, Watemne, Walimba, Wabaga na Wanalu ambao hivi leo wanafahamika kama wazungumzaji wa lugha za Kimele) ambao walikuwa na sifa kubwa kama wasanii na mafundi wa



18.2 Uhamaji wa idadi ya watu eneo la Gambia ya Jim (B. W. Andhi)

kazi za mikono. Kwa upande mwingine, 'Wamane' wanafikiriwa pia kuwa walichangia stadi nyingi mpya, kama vile uhunzi, ufumaji na mbinu za vita. Livingstone alieleza kuwa wazungunzaji wa Kimande wa mwanzo kabisa kuhamia Maghribi (ambao uhamiaji wao yeye aliuweka kwenye karne ya kumi na nne) walikuwa hasa wawindaji na wapiganaji; na kwamba makundi yaliyofuatia ya wahamaji wa Kimande yalianzisha kilimo cha mpunga, pamoja na zana za chuma kwa ajili ya kilimo kwenye maeneo ya msitu kwa kutumia mbinu ya kukata na kuchoma msitu. Huenda matukio haya yalianzia kwenye ukingo wa nyanda za juu za Guinea na kisha kusambaa polepole kati ya watu wa misitu ya nyanda za chini. Maoni ambayo bado yameenea ni yale ya kuwa watu hawa wa pwani hawakuwa wakijishughulisha zaidi na kilimo au ufuaji chuma hadi watu wanaozungumza Kimande walipofika na kuishi nao, hali ambayo ilitokea, si muda mrefu sana, mnamo karne ya kumi na sita.

Upande mwingine wa hoja hii unayafuatilia majilio ya Wamande kuwa yanarudi nyuma zaidi kiwakati na kuwa yana msukumo wa ustaarabu zaidi, hasa kwa vile wanahusishwa na uanzishaji wa kilimo, ufuaji chuma, aina za kimaendeleo za mifumo ya kijamii na kisiasa pamoja na biashara ya masafa marefu. Pamoja na haya yote, kulikuwa na mifumo tata zaidi ya kiuchumi na taratibu za kiufundi.

Kuanzia pwani kuelekea bara yanaonekana kwanza masalia ya watu wa asili. Huko Sierra Leone watu hawa ni Wabullom, ambao wanahusiana sana na Wakisi na Wakrim. Lugha zote tatu zinahusiana. Kandokando ya mpaka wa Liberia ya sasa wanaishi Wagola, ambao wanazungumza mojawapo ya lugha za Kimel za kusini kama hao wengine.

Baadaye kidogo walikuja Wabaga na Watemne ambao wana uhusiano wa karibu. Watu hawa walikuwa wakizunguma lugha ya Kimel cha Kaskazini na kuanzisha makazi yao bara nje kidogo kutoka pwani. Hawa Watemne pamoja na Wanalu,

Walanduma na Wakokoli walio Kaskazini zaidi, wanaelekea kuwakilisha tabaka la pili la baadaye na wameitwa "watu wa kabla ya Wamandinga." Kwa hivyo Watemne, Wakisi, Walimba, Wabaga na Walanduma wote walikuwa wakazi wa mwanzo wa Futa Jallon. Mwishoni waliposambazwa na Wasoso wanaozungumza Kimande mnamo karne ya kumi na tatu, walielekea kwenda Maghribi na kusini ili kutwaa ardhi yenye rutuba zaidi inayokaribia pwani. Wakati Wasoso walipoanza kujitokeza walielekea upande wa pwani kila walivyozidi kuongezeka. Wabaga, Walanduma na Watemne inawezekana walikuwa watu wamoja hadi Wasoso walipowasambaratisha. Wabaga ambao sasa wanaishi Guinea wanamezwa polepole na Wasoso. Wenzao huko Sierra Leone, Watemne, wamebakia na jina lao na wenyewe wamewameza baadhi ya Wabullom wa pwani, pamoja na Waloko, Wakoranko, Wafulbe na hata Wasoso walioko bara mbali na pwani.

Kwa kutilia mkazo vipengele vya kiuchumi, kiekolojia na muundo wa kijamii, Murdock aliligawanya eneo hilo katika sehemu mbili: (1) Senegambia inayowakilisha sehemu kubwa ya wazungunzaji wa lugha za Kiatlantiki Maghribi, wakipambanuliwa kwa mfumo wa nasaba ya kukeni, kuenca sana kwa mazao ya Kisudan mapema sana na mazingira ya kisavana, uhusiano mzuri wa kiutamaduni na uvamizi kutoka Sudan na (2) ukanda unaoanzia pwani ya Guinea hadi kukaribia Mto Sassandra wanamoishi watu wanaoitwa Wakru na Wamande wa 'pambizoni' ambao kihistoria na kijamii wanahusiana sana, ingawa wanazungumza lahaja nyingi za lugha za Kimande, Kikwa (Kikru) na Kiatlantiki Maghribi (Kimel).

Mtazamo mwingine na ambao unaridhisha zaidi ni ule unaodai kuwa uhunzi na kilimo vilikuwa vimeanzishwa kikamilifu kauka schemu za Guinea ya Juu kabla ya majilio ya Wamandingo. Fikra hii ilielezea tu kuongezeka kwa vipengele vya Kisudan kwenye mfumo wa wenyewe ya kilimo, na wa kijamii-kisiasa.

Mchakato wa mahusiano ya kiutamaduni ulikuwa ukiendelea kauka enco hili kwa karne

kadhaa, muda mrefu kabla ya uvamizi maarufu wa Wamane, na maingiliano ya aina hiyo yalihusu uhamaji na mwingiliano wa watu wa lugha na tamaduni tofauti kwenda kwenye eneo la misitu ya pwani ambapo watu wachache waliishi. Vikundi vingi vya kiisimu thnolojia ambavyo vilielezwa tu kwenye kumbukumbu za Wazungu kati ya mwaka 1440 na 1700 huko pwani vingali bado vipo hadi leo katika hali ile ile, ingawa makao yake na ukubwa wa eneo lake vinaweza kuwa vimebadilika kwa kiasi fulani. Hii haimaanishi kuwa vikundi vya kisasa ambavyo vinafanana kwa majina yake, lugha au makazi na vile vya zamani, ndivyo vizazi vya asili au vizalia vya kiutamaduni vilivyotokana na tamaduni za jamii mbalimbali za zamani, kwani eneo hili limepita katika mabadiliko makubwa kwa karne nyingi.

## Senegambia

Katika eneo la Senegambia ushahidi wa kiakiolojia unaonyesha kuwa maeneo ya Loudia na Wolof katika Kasamanse ya chini yalikalikiwa tangu zama za kikwi cha kwanza kabla ya enzi ya Ukristo. Inaelekea kuwa watu walikuja kutokea mashariki, hasa kwa vile ufundi wao wa kupamba vigae umefanana, k.m. mistari ya mvingo ya kimawimbi, ikiwa ni pamoja na vifinyage vya enzi ya zana za mawe vilivyosambaa kote kuanzia Cape Verde hadi Algeria ya kusini, na hata zaidi ya hapo hadi Afrika ya Kati.

Wakazi hawa wa pwani hatimaye waliiga maisha ya pwani, kama ilivyodhihirishwa na kuwepo kwa mabaki ya konokono. Watu hawa walikwishaanza kulima mpunga-maji kati ya -200 na +200. Mabadiliko haya mapya na makubwa yaliingizwa na walowezi wanya pengine wahenga wa Wadiola, ambao walikuja kutokea kusini na kuwaondoa wakazi wa awali ambao kwa kiasi fulani walikuwa wachache.

Katika awamu ya tatu muhimu ya uvamizi wao walifuga kondoo na mbuzi; ng'ombe waliendelea kuwepo, na samaki walikuwa chakula cha kawaida kwao.

Katika awamu ya nne na ya mwisho, mifugo miwili ilifugwa nayo ni nguruwe na mbwa. Ufinyanzi vyungu ulielekea kuwa sawa na ule wa kipindi kilichotangulia. Ushahidi wa kiakiolojia unaonyesha hasa kuwa Wadyula walikuja kukalia mabonde yote ya matope ya mito kati ya delta ya mto Kasmansi na Sondrugu katika kipindi cha awamu tatu za baadaye.

Licha ya Kasamansi, maeneo ya mto Senegal unapoingilia baharini karibu na St. Louis na delta ya Sine-Salum (Joal, Gandoul na Bandiala) nayo yalikuwa yamekaliwa katika kipindi hicho kama si mapema zaidi. Machimbo ya hivi karibuni yameonyesha vitu vya Enzi ya Chuma (majembe, koja na hangili pamoja na vyombo vya udongo). Kuna mambo ya jumla yanayofanana ya vifinyage vya maeneo ya Kasamansi na St. Lous. Huko Kasamanse na Cape Verde mbinu za mapambo ya neolithi pia zinaendelea kuwepo hadi mwanzo wa Enzi ya Chuma.

Ushahidi wa kiisimu unaonyesha kuwa mahali ambapo Wadyula wa zamani walitawanyikia kulikuwa ni upande wa kusini, kwenye eneo la pwani ya Guinea Bissau, ambapo wanaishi pia Wamandyak na Wabalante, ambao wote wanahusiana kiisimu na Wadyula. Kama walivyokuwa Wadyula, watu hawa pia ni walimaji wa mpunga maji na hutumia sepeto maalum la mkono litwalo *kayando*.

Sifa nyingi zilizo dhahiri za utamaduni wa Wadyula tayari zilikuwepo kuanzia kwenye kipindi cha pili na kuendelea. Makundi kadhaa yaliishi kwenye vigongo vya mchanga au karibu na mabonde ya matope ya mito, kama wanavyoishi sasa. Majaa yao yana vipande vya vyombo vya udongo na takataka nyingine ambazo zinafanana na vitu vya utamaduni wa Wadyula wa leo.

Zaidi ya miaka themanini hivi iliyopita, majengo kadhaa makubwa ya miduara ya mawe

yaliyogunduliwa katika eneo la Senegambia, Kaskazini mwa mto Gambia, katika eneo la zaidi ya kilomita za mraba 30,000 kuanzia Fara-fenni, kiasi cha kilomita 360 kutoka mwanzo wa mto, hadi mashariki karibu na Tambakunda, katika mto Senegal. Megalithi minara mikubwa ya mawe ya zamani zaidi yanayofahamika safu za mawe yaliyosimama wima na matofali ya ngegu ambayo idadi yake ni kuanzia manane hadi ishirini na manne, na kimo chake kinafikia mita nne. Mkusanyiko mkubwa wa mawe uliopo Diallumbere una miduara hamsini na nne, kila miduara ukiwa na mapana ya mita nane. Miduara hiyo kwa kawaida huwa miwili miwili au mitatu mitatu. Mawe yote katika miduara wowote ule yana ukubwa uliolingana. Kimo chao ni kuanzia mita moja hadi mbili. Kwa umbo, mawe hayo kwa jumla ni mihimili ya duara. Miduara mingi ina jozi za mawe yaliyoelekezwa mashariki yake, na wakati mwingine kuna mawe makubwa yaliyokatwa yenye umbo la herufi Y.

Sanamu hizi ni za mava. Safu za miduara inayopakana zilikuwa ni makaburi ya koo za wafalme na makuhani, ilihali makundi madogo yalikuwa yale ya watemi au makuhani wenyeji wa sehemu hizo. Mwelekeo wa mashariki wa jwe lenye umbo la herufi Y na jozi za mawe unaweza kuashiria kuabudu jua.

Vifinyange vya kutoka kwenye mawe haya vinaelekea kufanana na vile vilivyopatikana kwenye vichuguu vya Rao na Sine, katika maeneo ya Saheli. Mpaka sasa, zaidi ya vichuguu 4,000 vimekwishagunduliwa, baadhi yavyo vikiwa na kimo cha mita tano na hata mita arobaini. Vichuguu vilivyochimbuliwa vinaonyesha makaburi mengi pamoja na mkuku wa bidhaa zinazotiwa makaburini ikiwa ni pamoja na dhahabu na makoja, silaha za cbuma, vito vya dhahabu na kupri na kwenye kaburi moja, dhahabu ya kuvaliwa kifuari. Inawezekana kukadiria tarehe ya kuanza kutumika kwa chuma, vito na vifaa vingine vya kuzikia katika eneo hili kuwa ni kwenye kipindi baina ya karne ya nne hadi ya sita ya enzi ya Ukristo. Hata hivyo moja [za kuvaliwa] zimetokea kwenye maeneo yaliyofuata baada ya karne ya kumi na moja na zinaonyesha kuwepo mzunguko wa vitu hivi pengine kutokea bonde la mto Nili.

Kutokana na yaliyoelezwa juu ni dhahiri kuwa kulikuwa na majngiliano na mahusiano baina ya Sudan Maghribi na Senegambia katika kipindi hiki cha wajenga megalithi. Uthabiti wa ushahidi uliopo unaonyesha kuwa megalithi na mafanikio ya kijamii na kitamaduni yanayohusiana nazo vilikuwa ni kazi ya wahenga wa watu wanaoishi katika eneo hilo hivi leo - hasa Wamande, Wawolof na Wafulbe. Kwa jinsi inavyofahamika, ni Wadyula tu ambao waliishi hapo wakati miduara hiyo ilipojengwa. Hata hivyo, ukweli kuwa vifinyange vilivyopatikana kwenye majengo kadhaa (k.m. Wassu) vinatofautiana sana na vile vilivyopatikana kwingine (k.m. Fara-fenni) unaweza kuashiria kuwa makundi mengi ya kimbari, ambayo yalikuwa na tamaduni zilizofanana, yalikusika katika mazishi haya. Zaidi ya hayo, aina tofauti za mitindo kwenye uchongaji wa mawe zinaelezea maendeleo ya muda mrefu.

### *Guinea Sierra Leone Liberia*

Huko Sierra Leone, binadamu anaelekea kuwa aliweza kuyafikia kwa urahisi mapango na makazi ya majabali yaliyokuwa kwenye eneo la nyanda za juu upande wa Kaskazini-mashariki. Machimbo ya huko Kamabai na Yagala (makazi ya majabali yaliyo umbali usiozidi kilomita 320 Kaskazini ya Cape Mount) na huko Yengema yalionyesha awamu za kutumia chuma katika maki za baadaye, kuanzia mapema karne ya saba au ya nane, ingawa zana za mawe ziliendelea kutumika hadi pengine karne ya kumi na nne. Sehemu kubwa za kuyeyushia chuma ziko Kaskazini-mashariki mwa Sierra Leone kwenye nchi ya Koranko, lakini kwa bahati mbaya haifahamiki ni wakati gani shughuli hii ilifanyika.

Maki za karibuni zaidi za Kamabai zimepewa tarehe za kati ya karne ya sita hadi ya tisa na ya

sita hadi ya kumi. Vifinyange kutoka kwenye sehemu hizi vilikuwa tofauti sana na vile vilivyopatikana kutoka kwenye maeneo madogo zaidi kuzunguka Koidu na Bo ya Kaskazini-mashariki. Katika sehemu moja kalibu inayong'aa kidogo na kalibu ambayo inaelekea kuwa ya kutengenezea shaba nyeupe vilipatikana. Kazi za kisanii za chuma zilipatikana kwa pamoja kutoka kwenye eneo moja la aina hiyo zikiwa na zana za mawe zilizochongwa. Viwanda vilivyofanana au hata kuwa sawasawa kabisa na vile vya Yengeman ya chini na ya kati ya pango la Yengema vilinea katika majimbo ya mashariki na kusini.

Ni inahiri kuwa kulikuwa na mahusiano baina ya watu wa msituni na wale wa sehemu za savana katika sehemu hii ya Guinea ya Juu kuanzia mapema sana. Biashara ilikuwa muhimu hasa kama njia mojawapo ya mahusiano na kuingiliana/mashirikiano. Hata hivyo, tofauti na mawazo ya baadhi ya watu, kuna ushahidi wa kushamiri kwa ustaarabu katika maeneo ya msitu tangu zama za kale. Miongoni mwake ni michoro ya kale katika mawe laini ilivyopatikana huko Sierra Leone na Liberia na kufahamika kama *nomoli* na *pomdo*, na megalihi ambazo zimetajwa hapo awali. Baadhi ya wanazuoni wamesema kuwa desturi zote karibu zilikuwa za wakati mmoja na ule wa kuanzishwa kwa chuma, ikimaanisha kuwa chuma na desturi hizi vililetwa kwenye maeneo ya msitu.

Iwapo vifinyange na uhunzi uliingizwa katika eneo la msitu au la, eneo kati ya Senegal na Cote d'Ivoire lilionyesha sifa za kuwepo kwa mfumo kabambe wa utawala muda mrefu kabla ya historia iliyoandikwa. Sifa hizi hazikuwa na uhusiano na ustaarabu wa eneo la Niger ya kati.

Vyombo vya udongo vya "Enzi ya Mwanzo ya Chuma" katika msitu wa Liberia vinafanana sana na vyombo vya udongo vya Enzi ya Mwanzo ya Chuma kutoka sehemu nyingine za Afrika Maghribi. Kwa mfano, vyombo vilivyotiwa chapa vilivyopatikana katika machimbo huko Mali, Senegal na Ghana vinaonyesha mifanano mahsusi katika utengenezaji wake na vyombo vingine vya aina hiyo.

Vyombo vya udongo vilivyopatikana Liberia vinaweza kuwekwa katika makundi tofauti ambayo yanaelekea kuwa na maana kwenye uchambuzi wa kiutamaduni. Kuhusu vitu vya kiethnografia, vyombo vya Wamandingo-Walomo-Wakpelle-Wamano vinafanana kiasi kwamba vinaweza kuunda jadi ndogo yenye uhusiano wa kijenetiki. Huu kwa hakika ni mwendelezo wa tabia changamano na zenye kutofautiana za vyombo vya Wamandingo na zilizo za kawaida sana za vyombo vya Wamano. Kwa upande wa violezo na maumbo ya vyombo Wamandigo ndio wanaingiza tofauti kubwa na zilizo changamano zaidi kuliko Wamano. Hii inakubaliana na nafasi changamano ya kiutamaduni ya Wamandingo, Wamande wa asili na wengine wajulikanao kama Wamande wa pembeni.

Mifano inayofahamika ya *pomtan* na *nomoli*, majina ambayo mara nyingi hutumiwa kwa aina tofauti za michoro ya mawe, imeorodheshwa kwa maelfu na inepatikana kwenye eneo kuanzia kisiwa cha Sherbro hadi kwenye nchi ya Kisi ya Guinea na kutoka Liberia Maghribi kuelekea Maghribi hadi nchi ya Temne. Kuwepo kwa vinyago kunaelekea kutapaka kiasi katika eneo lote, ingawa kuna tofauti kubwa za kimtindo baina ya *pomtan* (umoja, *pomda*) za Kisi na *nomoli* zilizo Sierra Leone. Enco hili limekaliwa na wakulima wanaolima mpunga kama zao kuu, lakini ambao wanatokana na makundi mawili tofauti kilugha, Wakisi kwa upande wa Kaskazini, na Wabullom - Sherbro kwa upande wa pwani wanazungumza lugha za kundi moja, lakini wanatofautiana kimsingi na lugha ya Wamande na Wakono ambao wanaishi kwenye eneo linalowate-nganisha.

Baadhi ya wanazuoni wamedai kuwa *nomoli* za kwanza zilitengenezwa kwa kuiga sanamu za udongo za Sudan Maghribi, utamaduni wa kutengeneza *nomoli* ukiwa umeletwa kutoka Sudan Maghribi wakati ambao vyombo maalum vya udongo na chuma vilipoonekana kwa mara ya kwanza huko Kamabai kwenye karne ya sita na ya saba hivi. Wazo hili halitili maanani ukweli kuwa



sanamu za miti zilizofanana sana na vitu vya mawe (na sio vya mfinyanzi) zipo katika eneo hili, na kuwa ujuzi uliotakiwa kutengenezea sanamu za mawe inawezekana kuwa unepatikana kwa kutumia miti kwanza.

Idadi kubwa ya sanamu zilitengenezwa kwa ulanga au mawe laini, na chache zaidi zilitengenezwa kwa aina ya mawe ya *klorit* au *amfiboliti* na chache zaidi kwenye mawe magumu kama vile matale, *deleriti* na *jiwemchanga*. Kuwepo kochokocho kwa sanamu hizi na kuenea kwake katika eneo kubwa pamoja na ukweli kuwa mawe na miti vilitumika badala ya mfinyanzi, pamoja na aina tofauti za mitindo, vinaashiria kuwa vitu hivi vilitokea humo humo na wala sio utamaduni uliotoka nje, utamaduni ambao ulishamiri katika hali hizi tofauti ili kukubahana hasa na shinikizo na tofauti za utamaduni wa asili na ekolojia. Kutokana na ushahidi uliopo, inakuwa na mantiki zaidi kukubali kuwa *nomoli* zilikuwa ni mafanikio binafsi ya watu ambao walikuwa wakiishi katika eneo hili kwa muda mrefu. Pia kuna uwezekano kuwa utamaduni huu wa sanaa ulipelekwa upande wa Kaskazini kutoka kusini ambako ndiko kwenye chimbuko lake. Vile vile inawezekana kuwa si kwa bahati tu kwamba utamaduni wa sanamu za mawe uko katika sehemu nyingine nyingi za eneo la Guinea, kama vile Esie luko Yoruba, na *akwanshi* miongoni mwa Waekoi wa eneo la mto Cross.

Idadi kubwa ya sanamu za aina zote zinawakilisha umbo la mwanamume, ingawa tupu zake za mbele zilionyeshwa kwa nadra sana. *Nomoli* halisi kwa kawaida ina urefu kati ya inchi sita na nane na *pomdo* kati ya inchi tatu na sita; ingawa mifano michache ya urefu wa zaidi ya inchi kumi na mbili imekusanywa kwenye sehemu zote za eneo hili. Aina chache za umbo la tunguu la mwanamke pia zipo. Mwisho sanamu nzuri za maumbo ya binadamu wa jinsia zote zinapatikana, ingawa za wanaume ndio nyingi zaidi. Sanamu hizi zinaonyesha kwa kiasi kikubwa vilemba au ukaya, koja na urembo wa nembo za mwili. Sanamu na makundi yaliyo dhahiri zaidi yanatokea kwa uchache katika makusanyo yaliyofanywa katika nchi ya Kisi huko Guinea na labda yanatoka hasa Kisi ya kusini ya Sierra Leone na nchi ya Kono.

Imani maarufu katika eneo lote hili ni ile isemayo kuwa vinyago vina asili takatifu, ingawa wazee wa Kikisi wanakubali kuwa *pomtan* zilitengenezwa na mababu zao zamani sana na kila wakati ni kielelezo cha mhenga maalum. Kwa upande mwingine, miongoni mwa Wamande, *nomoli* zinahusishwa sana na wamiliki ardhi wa zamani, na sio na wahenga wao.

Kwa hakika ushahidi wa kiisimu unaelekea kuonyesha kuwa kuanzia takribani miaka 2,500 iliyopita, eneo la Sierra Leone ya kusini na Liberia Kaskazini, na sehemu ya Guinea inayopakana nayo lilikaliwa na watu wanaozungunza Kimel, ambao labda walikuwa wakijipania na kuwameza Wakwa. Takribani wakati huo huo, lugha za kundi la Kimande zilikuwa zikisambaa kuanzia ndani ya nchi ya eneo la mpaka wa Mali na Guinea na zilikuwa zinaanza kutofautiana. Tawi moja la Wamande, wahenga wa Wakono-Vai, Wakoranko, Wamalinke na wengine lilielekea Kaskazini na hatimaye kusambaa sana huko Sudan. Baadaye, tawi la Wakono-Vai lilisambaa kuelekea kusini Maghribi, likiwa tanga Wakisi na Wagola kutoka kwa wazungunzaji wa lugha nyingine za Kimel. Hatimaye, na katika miaka ya hivi karibuni sana - kikundi kingine cha kundi la Wamande, ambacho tayari kilikuwa kimejidhihirisha kuwa kundi la pekee, kilielekea Kaskazini Maghribi, kikiwagawa Wakisi kutoka kwa Wagola kama walikuwa bado hawajatenganishwa, na kuwavuka Wakono-Vai. Msukumo huu wa kuelekea Kaskazini Maghribi wa kundi la Wamande (wanaofahamika kama Mande Loko) hatimaye uligawanywa na uvamizi uliokuwa ukielekea mashariki wa watu wanaozungunza Kitemne Kaskazini ya eneo hili.

Kuna ushahidi mdogo kuhusu uhusiano wa moja kwa moja kati ya uhamiaji wa Wavai (ambao wanazungunza lugha ya Kimande cha Kaskazini) kuelekea pwani na ule wa Waligbi walioelekea mashariki ya Cote d'Ivoire; licha ya kufanana kwa lugha zao. Uwezekano mkubwa ni kuwa Wavai

walingia Sierra Leone ya hivi leo pamoja na Wakono na inaelekea kuwa Wakono na Wawai, pamoja na wazungunzaji wa lugha ya 'Kidama' ambayo hivi sasa imepotea, waliunda kundi lililoendelea kutoka Sierra Leone ya mashariki hadi baharini, na kuwatenga Wagola na Wakisi kutoka kwa wazungunzaji wengine wa Kimel.

Kulingana na uchunguzi wa hivi karibuni, makundi ya watu wanaozungunza Kimande cha Kaskazini hayakufika kwenye maeneo ya msituni ghafla, bali yalilingia taratibu yakiwa katika makundi madogo madogo; pia inafikiriwa kwa sasa kuwa hali hii lazima ilitokea mapema zaidi kuliko ilivyokuwa inadhaniwa hapo mwanzo. Dhima ya biashara ya masafa marefu katika kuchochea maendeleo muhimu ya kijamii na kisiasa, pamoja na athari ambazo zinaweza kuwa zimetokea kutokana na washiriki wakuu wa biashara hiyo, kama vile Wawai, yaelekea kuwa muhimu. Hivi sasa inakubaliwa kuwa kuna uwezekano mkubwa kwamba Wawai walikuja Liberia karne nyingi kabla ya karne ya kumi na tano. Maendeleo ya ustaarabu wa Wakono-Vai yalikuwa ni ya polepole yakirutubishwa na ustaarabu kutoka pande tofauti na katika nyakati tofauti. Uhamaji wa Wawai na Wakono haukuwa ni uvamizi wa ghafla uliokadiriwa kuwa ulitokea mnamo karne ya kumi na tano au kumi na sita kwani matukio ya kihistoria yanayochukua miongo au karne hayawezi kuelezwa kwa tukio moja tu la vita au kitendo cha kiongozi mmoja. Vivyo hivyo, njia mpya za biashara zinaanzishwa, hasa kwa mabadiliko ya polepole, na sio utamalaki wa ghafla wa kijeshi.

Tunachohusika nacho hapa hasa ni kuhama kwa watu kwa sababu za kisiasa au kiuchumi katika kipindi cha zaidi ya karne nyingi. Matokeo yake yalikuwa ni kurekebisha idadi ya watu kwa njia ya kuoana, kubadilisha miundo ya kijamii na kupanuka au kufifia kwa lugha. Idadi ya wazungunzaji wa Kivai iliongezeka kutokana na kuoana na wenyeji - sio tu na wazungunzaji wa Kimel bali pia Wadie ambao, kutokana na taarifa za karne ya kumi na sita, walikuwa wakiishi katika eneo kubwa la pwani. Kwa hivyo Wawai hawakuwa wakionekana kama wageni hasa.

Kutokana na hali hiyo, inaelekea kulikuwa na maingiliano ya mapema sana baina ya watu wa Kisudan na wale wa msitu wa Guinea; maingiliano ambayo yalisababisha uhamaji wa watu wa Kisudan kama vile Wasoninke na Wamande kuhama kuelekea kusini na mashariki hadi kwenye sehemu za maeneo ya nyanda za misitu. Hata hivyo kuna wasiwasi mkubwa iwapo hawa walikuja katika makundi makubwa kiasi cha kuweza kuwaondoa wenyeji. Ama kwa hakika inara nyingi wenyeji hawakuwa tu wawindaji na wakusanyaji au wavuvi wa Kikwa kama ambavyo mara nyingi imedaiwa. Wala siyo kweh kuwa utamaduni wa wenyeji hao na wahamiaji kwa kawaida ulikuwa umedumaa au hata kurudi nyuma, kutokana na kujitenga kwao na watu wengine, na kutokuwa na ekolojia inayofaa. Ukweli wa kihistoria unadhihirisha kuendelea kuingiliana kwingi kwa makundi yaliyoishi katika eneo hili, na kusababisha marekebisho dhahiri katika eneo hili.

Kulikuwa na uhusiano wa namna fulani wa baina ya makabila, lugha na tamaduni za aina mbalimbali. Hata hivyo uhusiano huu haukuwa wa karibu au wa mara kwa mara kama ilivyoielezwa na waandishi kadhaa. Watu wa pwani ambao waliishi mbalimbali kama vile Wawolof, Wasereer, Wadyula, Wanalu, Watemme, Wakisi na Wagola wanaweza kuwa wawakilishi wa wakazi wa zamani sana wa eneo hili lakini hawa hawakuwa na utamaduni wa msituni wa 'zama za kale' wa kundi asili la Wanegro ambalo lingesemekana liliishi katika eneo lote la Afrika Maghribi kwenye nyakati za kale sana kabla ya historia iliyoandikwa. Hata hao watu wanaozungunza lugha ya Kikwa ya kusini mashariki ya Liberia na Maghribi ya Cote d'Ivoire hawakuwa wa kale zaidi ya wengine katika makundi haya. Kusema kweli, ushahidi mwingi wa akiolojia na mwingine wa aina hiyo uliopo mpaka sasa unaonyesha wazi kuwa kilimo, dola kubwa zenye mamlaka, vyama vya kazi na matabaka ya kurithi, majeshi na mifumo ya biashara na masoko, vilikuwa mambo muhimu katika maisha ya wengi wa watu hawa mnda mrefu kabla ya uvamizi na athari za mwanzo za Wasudan

hazijaitokeza, na hasa tuseme kati ya karne ya saba na ya kumi na moja.

Ushahidi wa akiolojia na wa ethnolojia pia unaonyesha kuwa mpunga ulikuwa ndio zao muhimu na lililolimwa sana pwani ya Atlantiki Maghribi kuliko pamba, uwele au mtama; mazao ambayo watetezi wa mwanzo wa eneo la Sudan wanaelekea kuyapa msisitizo usiostahili na ambayo yanaweza kuwa yameletwa na wahamiaji kutoka Kaskazini au kupitia kwenye mahusiano yao na watu wa Kaskazini.

Liberia ya kusini na Cote d'Ivoire ya Maghribi inaelekea kuwa kitovu cha mgawanyiko mkubwa wa tamaduni hizi za kilimo. Mto Bandama, ambao unawagawa Wabaule na Wakru, ndio pia mpaka wa Kaskazini zaidi wa kilimo cha viazi vikuu. Iwapo viazi vikuu vinalimwa Kaskazini mwa mpaka huu, uvunaji wake hauhusishwi na matambiko mengi yanayofanywa na Waagni na watu wengine wanaozungumza Kikwa kwa upande wa kusini zaidi.

Japokuwa Kaskazini mwa mto Saint-Paul na upande wa mashariki kandokando ya eneo la msitu, mpunga unaendelea kuwa zao muhimu la kilimo kabambe kwa watu wote wa eneo la kati la Atlantiki ya Maghribi, mazao muhimu ya Sudan kama vile mtama, pamba na uwele yaliingia kidogo sana Maghribi hadi kufikia mpaka wa Guinea na Liberia. Mazao haya hayakuenea kusini zaidi ya nchi za Watemme, Wamande Wakaronko na Wakono wa Siera Leone. Katika jimbo la Kaskazini Maghribi la Liberia, mazao haya hayalimwi na Wade, Wagola na Wakpelle wa Maghribi, isipokuwa pale ambapo Wamandingo wamekaa katika nyakati za hivi karibuni au pale ambapo athari hii incafhamika kuwa imekuwepo kwa muda mrefu uliopita.

### *Hitimisho*

Maarifa yetu ya sasa kuhusu historia ya eneo la Guinea ya Juu katika kipindi kilichozungumziwa katika Juzuu hili yanaweza kuchukuliwa kama yasiyoridhisha. Tulichoonyesha hapa ni juhudi za mwanzo za kukusanya na kujadili taarifa zilizopo za uchunguzi wa kiakiolojia na kisimu ambazo zimefanywa katika eneo hili mpaka sasa. Lakini bado kuna mapengo zaidi kuliko ukweli thabiti katika maarifa tuliyonayo, na tunashughulikia zaidi mawazo ambayo yanahitaji ithibati zaidi. Hali hii inadai mikakati maridhawa zaidi ya uchunguzi iliyokitwa kwenye kuwahusisha wataalamu kutoka kwenye fani mbalimbali. Hata hivyo jambo lenye umuhimu huo huo, ni kuwa na mkabala mpya na usio na tashwishi ambao utatuwezesha kuona historia ya watu wa Guinea ya Juu kwa namna inayowaonyesha sio tu kama watu walioathiriwa kutoka nje, iwe ni kutoka Kaskazini au baadaye kutoka kusini, bali kama washiriki halisi katika mwenendo wa historia.

Ramani ya Ethiopia ya karne ya saba isingeweza kuwa na umbo lililo thabiti. Katika ramani hiyo kungekuwa na idadi ndogo ya miji na maeneo yaliyotajwa na Kosmas Indikopleustes katika kitabu chake cha *Christian Topography (Topografia ya Ukristo)* kilichoandikwa katikati ya karne ya sita. Kitabu hiki kinatupa taarifa sahihi kuhusu maeneo yanayopakana na Nili, Bahari ya Shamu na Bahari ya Hindi. Kinatuambia, kwa mfano, kuwa 'kutoka Aksum hadi kwenye nchi ya ubani inayoitwa Berbera, katika mwambao wa pwani mbali na Sasou, ambayo ni eneo la mbali kabisa la Ethiopia, ni safari ya siku arobaini.'

Kosmas pia aliandika kuhusu mamia ya wafanyabiashara ambao walisafiri katika eneo zima wakifanya biashara ya ng'ombe, chumvi na chuma kwa kubadilishana na vipande vya dhahabu. Pia walifanya biashara ya viungo, ubani na mdalasini. Miji mikubwa ya wakati huo ilikuwa Aksum na bandari yake ya Adulis. Hatuna sababu ya kufikiria kuwa hali ilikuwa tofauti mnamo karne ya saba. Baada ya kufikia ustawi wake katika karne iliyotangulia, ufalme wa Aksum ulikuwa inara kabisa. Mwanzoni mwa karne ya nane Khalifa wa nasabatawala ya Umayya ahamuru picha za wafalme wanne wa dunia zichorwe katika kuta za jumba lake la kifalme huko Kusayr Amra, nchini Jordan. Hizi zilikuwa ni tawala za Hispania ya Kivisigoth, Ubizenti, Uajemi na Aksum. Hii inathibitisha umuhimu wao, hata kama Khalifa anadai kuwa alizishinda tawala hizi.

### *Kuanguka kwa ufalme wa Aksum*

Ufalme wa Aksum ulifurahia kipindi cha ufahari wa pekee wakati wa enzi za Ezana mnamo karne ya nne. Utajiri wao ulitokana na ng'ombe, kilimo na zaidi ya vyote biashara, na hasa biashara ya pembe. Ufalme uliendelea kuimarisha uhusiano wa biashara na sehemu nyingi katika Bahari ya Hindi kupitia bandari yake ya Adulis.

Biashara hiyo ilitoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi ya nchi za kutokana na shughuli mbalimbali za kibiashara miji mingi ilikua.

Mapema karne ya tatu, umuhimu wa biashara ulisababisha uanzishaji wa sarafu na kutokana na sarafu hizo tumepata majina ya wafalme ishirini kwa kipindi chote cha ufalme wa Aksum na ambao wengi wao, kuanzia Endybis hadi Hataz, wasingeweza kujulikana.

Mwanzo wa karne ya saba ulileta mabadiliko katika ufalme wa Aksum. Kipindi kingime kilianza, kile cha kuporomoka kwa ufalme, kipindi ambacho ushahidi wake wa maandishi ni nadra sana, ingawaje haimaanishi kwamba haupo. Miji ya Aksum iliendelea kukua kwa kipindi ambacho hakikufahamika. Sarafu zilizopatikana maeneo ambapo miji ya Aksum, Matara na Adulis ilijengwa,



zinataja majina ya wafalme waliotawala karne ya saba na sehemu ya karne ya nane: Ella-Gabaz, Anaeb, Armah, Yathlia, Za Ya-Abiyo, La Madhen, Wazena, Ghersem na Hataza. Vichwa vya wafalme katika sarafu hizi vimezungushiwa maandishi katika lugha ya Ki-ge'ez ambayo hadi leo inatumika kama lugha ya ibada.

Mnamo mwaka wa 615, wakati wa utawala wa mfalme Armah, au huenda katika utawala wa baba yake, Ella-Tsaham, tukio muhimu lilitokea. Baadhi ya wafuasi wa Muhammad ambao maisha yao yalikuwa yakitishiwa walikimbilia katika ikulu ya Aksum ambako walipokelewa vizuri. Machifu wa Maka, maadui wa mtume, walipoomba wakimbizi hao warudishwe, mfalme aliyakataa maombi yao, akitilia maanani kuwa dini ya wageni hao ilikuwa ikifanana na imani ya Kiukristo ambayo alikuwa akiamini. Zaidi ya hayo kamuni ya ukarimu ilibidi ifuatwe.

Karne ya saba ilishuhudia kuanza na kukua kwa dini ya Kiislam na kuenea kwake taratibu kandokando ya Bahari ya Shamu. Maelewano mazuri baina ya Waislam wa kwanza na ufalme wa Aksum yalidumu kwa muda mfupi na mara migongano ilianza. Waaksum walishambulia pwani ya Uarabu, hali ambayo iliwafanya Waislamu kujibu mashambulizi. Katika karne ya nane, Waislamu walivikalia Visiwa vya Dahlak vilivyokuwa sehemu ya ufalme wa Aksum. Bandari ya Aksum ya Adulis ilibomolewa katika karne ya nane hivi na kusababisha shughuli zote za biashara ambazo hadi wakati huo zilikuwa zikiendesha na mfalme wa Aksum zisimamishwe kabisa. Hata hivyo historia haiutumii lolote kuhusu matukio yaliyokuwako bara ya nchi hii.

## Wabeja

Sababu mojawapo zilizofanya ufalme wa Aksum kufifia karne ya saba na kuendelea, na kutoweka kwake mnamo karne ya nane, ilikuwa ni kuvamiwa kwa maeneo ya Ethiopia Kaskazini na Wabeja. Moja wapo ya makundi ya Wabeja yaliyokuwa na nguvu sana, Wazanafiji, liliuvamia uwanda wa juu wa Eritrea kupitia bonde la Barka.

Katika vipindi vya nyuma Wabeja walikwishajiunga katika 'falme' kadhaa wakiwa wamekalia eneo kubwa kuanzia Aksum hadi Misri ya Juu. Wabeja (au Wabega) wanatajwa kwa mara ya kwanza katika maandishi kwenye mawe kuanzia karne ya tatu, ambayo yaliandikwa na mfalme wa Aksum na kunakiliwa na Cosmas katika karne ya sita. Kutwaliwa kwa Ethiopia Kaskazini na Wabeja-ndipo tukapata jina la sasa Begemder (nchi ya Wabeja) - bila shaka kulitokana na likweli kwamba kwa kiasi fulani mamlaka ya Aksum yalikwishafifia, tena basi kuanzia wakati huo Wabeja wakaongeza shinikizo ili kuharakisha kuporomoka kwa utawala wa Waaksum.

Kuanzia karne ya tisa hadi karne ya kumi na moja vyanzo peke yake vinavyohusu Wabeja ni waandishi wa Kiarabu, wa kwanza akiwa al-Yakubi (ambaye alifariki mnamo mwaka 897) na wa pili akiwa Ibn Hawkal akifuatiwa na al-Uswani. Kuanzia katika eneo karibu na Nili, al-Yakubi anaorodhesha na kuonyesha mahala pa 'falme' tano za Wabeja — falme zikianzia Nili kuelekea kwenye bahari kisha kuelekea tena kusini. Ufalme wa kwanza, uliokuwa karibu zaidi na nchi ya Kiislamu ya Aswan, ulikuwa *Nakis*; ufalme ambao ulikaliwa na mbari ndogondogo kadhaa ambazo majina yake yameorodheshwa lakini hayajasimbuliwa bado. Mbari hizi ziliishi karibu na ufalme wa pili uliojulikana kama *Baklin* au *Taflin*, katika Sahel ya Eritrea, nyanda za juu za Rora na bonde la kati la mto Barakat. Mashariki mwa *Baklin* waliishi *Wabazin* ambao kizazi chao huenda ni Wakunama wa leo, ambao huitwa *Bazen* na majirani zao. Ufalme wa *Jarin* ulitanda kuanzia Badi (Massawa) hadi nchi ya *Baklin* kuelekea Barakati. Kundi la mwisho lilikuwa la *Wakataa*, ambao eneo lao lilianza Badi hadi Faykun au Fankun. Hawa *Wakataa* walikuwa Waukristo na wakajiona wanaathiriwa na *Wanajashi*. Wafanyabiashara Waarabu walifanya biashara na hawa watu na



19.2 Sarafu ya Mfalme Armah, karne ya saba ya enzi ya Kikristo. (Wizara ya Utamaduni, Ethiopia)

19.3 Kitabu cha Injili cha Abba-Guerima kikionyesha picha ya Mt. Mark (karne ya kumi na moja). (Wizara ya Utamaduni, Ethiopia)



polepole waliwabadilisha dini na kuwa Waislamu.

Huko Eritrea na Tigre ya Kaskazini, bado kuna mapokeo yanayowakumbuka hawa watu wa zamani katika majina ya kiasili ya *Warom* na *Wabalaw* (mara nyingine *Wabelew Kelew*, hasa katika Kichimezana). Majina ya mahali pia yanaonyesha kuwepo kwa watu hao, hasa Wabelew ambao katika karne tano au sita zilizopita waliongezeka umaarufu wao hadi sehemu za pwani. Wabeni Amer ambao siku hizi huishi kwa kuhamama Kaskazini ya Eritrea na Sudan ni vizalia vya Wabeja wa awali.

Kutokana na shinikizo la wapenda vita wa Kibeja, wafalme wa Aksum na watu mashuhuri waliondoka Aksum kwenda kusini zaidi ambako kulikuwa hakuna hatari ya wavamizi. Kama ilivyoelezwa hapo mwanzo, mwanzoni mwa karne ya saba hali ya kisiasa katika Bahari ya Shamu ilibadilika kabisa. Dola ya Wabizenti, ambayo pia ilikuwa inatishiwa na wavamizi wa Uajemi ilirudi nyuma. Waajemi waliongezeka na wakaanzisba vituo pwani ya Afrika.

Ethiopia ilishirikiana na Ubizenti ambayo nguvu zake zilikuwa zimefifia. Kidogo kidogo, Waarabu waliwarudisha Wabizenti nyuma. Huko Misri walipata ushindi mkubwa na huko Ethiopia, warithi wa Armah walitengwa. Nchi ikawa katika giza kuu, ikaachwa na miaka kidogo tu ya historia.

Hakuna maandiko yaliyovumbuliwa katika kipindi hiki cha karne ya saba na ya nane, licha ya yale yasiyosomeka vizuri kwenye taji moja huko Aksum. Maandishi hayo ni ya Kige'ez na yaelekea ni ya kipindi cha baadaye. Yanataja mtu mmoja *Hadani Danel* (aliyejifanya mtawala?) ambaye alimuasi mfalme wake na kumzuia asiingie katika jiji lake.

### *Mwanzo wa Kikwi cha Pili*

Mnamo nusu ya pili ya karne ya kumi, kulikuwa na idadi kadhaa ya matukio muhimu yaliyoathiri maisha ya nchi.

*Historia Ya Maaskofu Wakuu* inamtaja malkia mmoja wa *Banu al-Hamwiva* kutoka kusini aliyewavamia Waaksum na kunaribu makanisa. Alimwondoa mfalme ambaye aliomba msaada kwa Askofu wa Kikhufu, Kosmas, kupitia kwa mfalme wa Wanubi Djirdjis/George, akimwomba atume askofu mkuu katika sehemu hiyo. Kama tujuavyo dayosisi ya Aksum ilikuwa ineshikiliwa na kasisi wa Kikhufu kutoka Aleksandria toka karne ya nne. Katika karne ya tano, Ethiopia ilishikilia imani ya Kimonofista kwa kufuata ibada ya Misri.

Alipoondolewa madarakani, huyo mfalme mwenye bahati mbaya, alikimbilia Shoa akifikiria kwamba yaliyompata ni adhabu aliyopewa na Mungu kutokana na kufukuzwa kwa askofu. Baada ya Mfalme wa Nubia, Jirjis, kuingilia, uongozi wa kidini ulimchagua mtu mmoja Abba Daniel kuwa Askofu wa Aksum. Kabla ya kuchukua madaraka yake, mfalme ambaye tangu 970 mpaka 980 alikuwa bado akipigana na malkia katili, alikufa.

Takribani katika kipindi hicho hicho, Ibn Hawkal aliandika (c.977) kuhusu mambo yaliyokuwa yakitokea Ethiopia. Kuhusu nchi ya Waabyssinia imekuwa ikitawaliwa, kwa muda mrefu sasa, na mwanamke. Alimwua mfalme wa Abyssinia aliyejulikana kwa cheo cha *Hadani*. Tangu wakati huo ametawala kikamilifu katika nchi yake na sehemu zilizoizunguka ardhi ya *Hadani* kusini mwa Abyssinia.

Maelezo ya kimapokeo yanapingana kuhusu maelezo juu ya malkia huyu. Wengine wanasema alikuwa malkia wa Wafalasha (Wayahudi wa Ethiopia) na ni binti wa chifu Gideon. Wengine wanasema alikuwa mjukuu wa mfalme Wedem-Asfere, na wengine wanasema alikuwa binti aliyejulikana kama Mesobe-Work wa mfalme wa mwisho wa Aksum aliyetiwa Delnaad.

Conti Rossini anapendekeza kuwa neno *Al-Hamwiva* katika cheo cha malkia lisomeke kama *Al-Damut*, ambalo linaweza kuashiria eneo la Damot kusini na kusini masbariki mwa *Blue Nili*



kama ndiyo nchi yake ya asili. Matukio haya, yanaweza kutafsiriwa kama ni ukinzani wa mbari ndogo ndani ya Ethiopia dhidi ya upanuzi wa wafalme Waukristo wa Aksum kuingia sehemu ya kusini ya nchi.

Historia za Ethiopia kuhusu kipindi hiki cha giza zina mifuatano ya shajara za kifalme. Nyingi ya hizi zinapatikana katika *Tarihi za Utawala wa Mfalme Menelik* zilizoandikwa mwanzoni mwa karne ya ishirini na mtu mashuhuri wa kanisa aliyetwa Neboure-Id Guebre Sellasie, lakini jedwali hilo la urithi wa utawala kutoka karne ya sita ni wazi kwamba haliwezi kuthibitishwa. Lilitayarishwa baadaye kabisa ingawaje bado linaweza kuwa na kiasi fulani cha ukweli ndani yake.

Taarifa nyingine za mapokeo zinasema kwamba mfalme wa mwisho, Delnaad, huenda alikimbilia katika nchi za kusini na kwamba binti yake aliolewa na mtoto wa mfalme kutoka Bugena, eneo lililo karibu na Lasta. Watu hawa waliotoka Lasta ambao walikuwa na nafasi muhimu sana katika historia ya baadaye ya Ethiopia walitokana na wakazi wa awali, Waagaw, ambao kwa karne nyingi walikuwa wakiishi kusini Maghribi mwa nchi.

Kisa cha Messobe-Work, aliyolewa na Mera Takle Haymanot, mfalme wa kwanza wa nasabatawala mpya ya Zague, kufuatana na shajara ya mapokeo, ni taarifa iliyohamasishwa ya visa vilivyotokea kweli. Tukiacha kama ilivyo, baada ya usitawi wa enzi ya Aksum nasabatawala hii mpya iliiondoshwa nasaba tawala ya zamani ya ukoo wa Ezania na kuanzisha utawala wake katikati ya Ethiopia.

Baada ya uharibifu mkubwa, nasabatawala mpya iliweka mfumo wake yenyewe wa kifalme baada ya kujiimarisha katika majimbo ya kati. Hata hivyo iliendeleza mapokeo mengi na amali za kiutamaduni za Aksum. Utawala huu mpya ulifikia kilele cha ustawi katika karne ya kumi na mbili hadi kumi na tatu kama ilivyothibitishwa na wafalme wakuu wa nasabatawala ya Zague ambapo Lalibela ndiye anayekuwa maarufu zaidi.

## Maandishi

Maandishi ya Ethiopia ni ya Kibiblia na yenye asili ya Kiukristo. Kutoka karne ya nne, lugha ya Kige'ez ilitawala katika makao ya mfalme na katika makanisa. Tafasiri ambazo zimeshika nafasi kubwa katika maandishi haya zimeandikwa katika lugha hiyo.

Vitabu vya kwanza vilikuwa tafsiri ya Biblia, ambavyo vilifasiriwa katika makao ya watawa yaliyoanzishwa mwishoni mwa karne ya tano na kuendelea. Agano Jipya lilifasiriwa kutoka maandishi yaliyoidhinishwa na askofu wa Antiokia na makasisi wa Kimonofista wa Shamu waliokimbilia Ethiopia katika karne ya tano na ya sita.

Mintaarufu Agano la Kale, Waethiopia pia walifasiri vitabu vingi vilivyofikiwa na makanisa mengine kuwa havikubaliki. Hivi ni pamoja na *Kitabu cha Enoki*, *Kitabu cha Jubilee*, *Kupaa kwa Isaya*, *Mchungaji wa Hermas* na *Ufunuo wa Esdras*. Ni vizuri kukumbuka kuwa vitabu hivi visivyokubalika vimetufikia katika ukamilifu wake vikiwa vimeandikwa katika lugha ya Kige'ez peke yake. Ni vichache sana vilivyokuwa katika lugha nyingine. Katika kipindi hicho cha giza Ethiopia ilitoa mchango muhimu katika maandishi ya dunia.

Orodha ya tafsiri inayo pia makala ndogo za Kimjili kama vile *Qerillos*, mtayarishaji akiwa Mtakatifu Cyril wa Aleksandria; *Utawala wa Pachomius*, Mtakatifu Pachomius akiwa mwanzilishi wa utawa wa mashariki, na *Physiologos*, mkusanyo wa ngano za wanyama, mimea na mawe zikihitimishwa na maadili.

Matini zote hizi zilifasiriwa kabla ya karne ya saba, lakini matini nyingine zilinakiliwa katika kipindi kinachochunguzwa. Katika kipindi hicho – tokea karne ya saba, hadi ya kumi na moja – Ukristo uliendelea kueneza ushawishi wake kupitia utawa, ambao pengine ndilo jambo muhimu katika historia ya kipindi hiki cha giza.

Kutokana na ukweli kwamba hakuna kazi asilia iliyopatikana ya kipindi hicho haimaanishi kuwa karne hizo zote hazikuwa na shughuli za kisomi. Kusema kweli inaelekea kuwa mbegu zilipandwa ambazo mavuno yake yalipatikana katika kazi za fasihi katika karne ya kumi na nne na ambazo E. Cerulli anasema kwa usahihi kwamba: 'kupevuka kwa sanaa ya maandishi haya kunadhahirisha kukomaa kwa fasihi; na matumizi bora ya lugha yanamaanisha kuwa si uwanja ambao ungeweza kueleweka kwa haraka bila kipindi kirefu cha mapokeo.'

### *Usanifu majenzi na sanaa*

Kwa mujibu wa mapokeo mengi, nyumba za watawa za kwanza huko Kaskazini ya nchi hii zilianzishwa katika karne ya tano na sita.

'Watakatifu tisa' (*Teseatu Kidusan*) ambao wanaaminika kuwa walitoka Ubizenti wanaonekana kuwa ndio walikuwa waasisi wa maisha ya kitawa halisi. Waliishi katika sehemu za mbali na miji katika eneo la Aksum. Msingi mmojawapo wa kale kabisa unapatikana mashariki ya Adwa katika mwamba ulio juu katika milima ya Tigre, unaoitwa Debre-Damo. Kanisa ambalo hivi karibuni limerekebisha na kujengwa upya lilijengwa hapo zamani sana. Wataalamu wanalikadiria kuwa lilijengwa karne ya kumi, lakini mapokeo yanaamini kuwa kanisa la kwanza Debra-Damo lilijengwa katika karne ya sita kwa pendekezo la mfalme Gebra-Masqal, mwana wa Kaleb.

Mbimu ya ujenzi inafanana na ile ya usanifu majenzi wa Aksum ambapo mawe na miti vinatumika pamoja. Milango na madirisha yana vizingiti vya aina moja kama inavyoonekana kwa mfano katika jengo kubwa la Aksum ambapo nguzo nene zinajitokeza nje na sehemu kadhaa hujitokeza katika mtindo wa Aksum.

Ingawaje kanisa hili lilikuwa la kwanza kuonyesha jinsi majengo yaliyojengwa katika karne ya kumi yalivyokuwa yanafanana, huu siyo mfano pekee wa usanifu majenzi wa kipindi hiki. Uchimbuaaji wa majengo ya zamani uliofanywa katika miaka 1970 ulionyesha makanisa mengine Kaskazini mwa Ethiopia ambapo ushahidi wa kiakiolojia unayahusisha na Aksum ya zama za kale ilipokuwa ikiporomoka. Makanisa yaliyotajwa hapa kama ushahidi wa kipengele hiki cha kihistoria ni yale ya Zarema, Agowo na Berakit.

Kanisa la Zarema lililo mashariki ya Atsbi, kwa upande wa mashariki wa mlima wa Tigre, ni la mtakatifu George (Kadus Ghiorghis) na huenda ni mabaki ya miaka ya baadaye ya majengo yenye umbo la mraba na safu za nguzo za enzi ya Aksum. Mapambo katika dari za mbao zilizo juu ya bwalo yanavutia sana katika usanifu na ufundi uliotumika. Kazi hii ya kutia nakshi inatokana na mapambo ya kisanana ya Mediterania ya karne za saba na nane hasa kutoka kwa Wakhufu wa Misri. Kazi hii haina athari yoyote ya mapambo ya Kiislamu. Tarehe ya asili ya kanisa la Zarema-Ghiorghis ni baina ya karne ya tisa au kumi.

Kanisa la Agowo linapatikana katika eneo hilo hilo. Ni kanisa dogo la mawe na miti lililojengwa kwenye mteremko chini ya mwamba. Kama ilivyo katika majengo ya Aksum, kuta zinaonyesha nguzo nene na dari ya kati ina mbao nyembamba ambazo hazikupambwa kama zile za Debre-Damo. Kanisa hili lina jina la Tcherqos (Cyriac). Sehemu kongwe sana za kanisa hili huenda zilijengwa karne ya kumi na moja lakini lilifanyiwa matengenezo katika miaka ya baadaye.

Makanisa ya Debre-Damo, Zarema-Ghiorghis na Agowo-Tcherqos ni makanisa yenye majengo ya kawaida, na yanatofautiana na idadi kubwa ya makanisa ya mapangoni yanayopatikana Kaskazini mwa Ethiopia ambako Ukristo una historia ndefu sana. Makanisa haya yalianzishwa katika kipindi kinachozungunziwa, na yana uhusiano mkubwa na usanifu majenzi wa Aksum na baadhi yake yamejengwa vizuri sana.

Makanisa mengi yanapatikana katika maeneo ya Guerealta, Kaskazini mwa Makele. Makanisa mengine yanapatikana katika wilaya za jirani za Tembien, Amba Senayt na Atsbi. Jumla ya makanisa 120 ya mawe yameorodheshwa katika eneo hili. Miongoni mwa yale ya zamani sana ni Degum-Sellassie huko Guerealta, ambalo linafikiriwa kuwa lilijengwa mnamo karne ya kumi. Ushahidi mwingine wa kiakiolojia unakadiria kuwa makanisa haya huenda yalijengwa karne mbili nyuma.

Kilomita kama ishirini kutoka Degum-Sellassie kuna kanisa la Maryam wa Berakit. Hili ni mfano bora wa sanaa ya miamba ya Waethiopia. Limetengenezwa kwa kuchimba mwamba katikati ya ufa na linaaminika kuwa ni mwamba ulio sawa na kanisa la pekee la Aksum. Umbo lake linaweza kufananishwa na jengo la kanisa la Debre-Damo.

Hakuna shaka kwamba kitu cha kwanza kinachomvutia mtu aonapo kanisa la aina hii ni ule ulusiano wake na aina ya ujenzi wa Aksum. Maeneo haya mawili yako karibu kijografia na kuna mabaki ya Aksum. Kisha, katika ujenzi, kuna maumbo mengi ambayo yanafanana na mapokeo ya Aksum, kama vile udogo wa viwango vya uwiano; ile plani ya kanisa inayofanana na makanisa madogo ya karne ya sita na saba katika Enda-Tchergos karibu na Aksum huko Matara Tokonda na Kohayto, dari bapa, nguzo na vichwa vya nguzo. Mambo haya yanaonyesha kuwa kanisa kama lile la Berakit lazima litakuwa limejengwa katika miaka inayokaribia kipindi cha Aksum.

Katika majengo mengi ya zamani, pamoja na tuliyoyazungumzia katika sura hii, nakshi inapatikana hasa katika dari na sehemu za juu za nguzo.

Katika kanisa la Debre-Damo, mapambo ya nakshi yanawakilisha hasa wanyama kama vile simba, swala, pundamilia, nyoka, ngamia, tembo, nyati, mbuzi, punda, twiga na chui. Pia wanyama wa kubuni, majani na maumbo ya kijiometria. Msalaba mara nyingi huwa katika ukizungukwa na ubunifu mchanganyiko na vitanga vya mikono. Wasanii wa zamani walijua aina tofauti za mapambo yaliyotumika katika nchi za Mediterania pamoja na Misri ya Wakhufu. Kanisa la Zarema-Ghiorghis ni moja ya majengo ya zamani yaliyopambwa sana Kaskazini mwa Ethiopia.

Hakuna picha za kuchora ukutani katika makanisa haya wakati wa sasa. Tunaweza kujiuliza kama michoro kama hiyo ilikuwa inatumika kupamba kuta wakati wa zamani, kama ilivyo kwa makanisa ya sasa kama lile la Beta Maryama lililoko Lalibela, lakini kuta za makanisa ya zamani sana yanayojulikana hazionyeshi ishara yoyote ya mapambo. Udogo wa kuta za ke uliacha nafasi ndogo sana ya kuchora mapambo. Hata hivyo, inawezekana kuwa mapambo hayo yalikuwepo wakati fulani. Kwa kweli yapo maelezo ya mtu aliyeshuhudia mapambo haya kama yalivyonukuliwa na al-Tabari juu ya mwanamke katika msafara wa Muhammad aliyekwenda Aksum katika karne ya saba ambaye aliporudi Medina, alikumbuka kwa furaha michoro ya ukutani katika makanisa. Hata hivyo hakuna mchoro, wala dalili yake iliyobaki ya zamani hizo.

Mintarafu miswada, vitabu vingi vya zamani vilijulikana kuwa vilifasiriwa katika karne ya tano na ya sita na kuendelea, lakini ni vigumu kusema kwa usahihi kama miswada hii ilikuwa imepambwa kwa rangi, kwani hakuna hata mmoja ambao ulinusuika uhaifu wa wakati huo, licha ya injili mbili nzuri zilizohifadhiwa katika nyumba ya watawa ya zamani ya Abba-Garma karibu na Adwa huko Tigre (taz. 19.3 uk...). Rangi zilizopamba baadhi ya ktrasa za muswada huu zinafanana na zile za sanaa ya Kibizenti ya Shamu.

20

## *Mahusiano ya Ethiopia na nchi za Kiislamu*

Mahusiano ambayo toka zama za kale yaliwaunganisha watu wa pwani mbili za Bahari ya Shamu, Waarabu na Waethiopia<sup>1</sup> yalianza kubadilika tokea kuibuka kwa Uislamu, kwani baada ya hapo yalianza kutazamwa kama mahusiano kati ya Waukristo na Waislamu.

Mapokeo yaliyokusanywa katika wasifu wa Mtume Muhammad huonyesha matukio mbalimbali katika historia ya mahusiano ya Uislamu wa mwanzo na Ethiopia, muhimu mno miongoni mwake ikiwa kuhama kwa Jafar ibn Abi Talib, binamu wa Muhammad na ndugu ya Khalifa wa baadaye, Ali ibn Talib, ambaye alikwenda kwenye makao ya Negus na Waislamu wengine ili kuepuka uhasama wa Makurayshi. Kulingana na mapokeo fulani, alifaulu kumwingiza katika Uislamu *negus* (=mfalme wa Ethiopia) ambaye hakuidhihirisha imani yake katika Uislamu kwa kuchelea kuchukiwa na watu aliowatawala ambao walikuwa Waukristo.

Kitendo hiki cha Jafar ndicho pengine baadaye kilichochea wana wa wafalme mbalimbali na viongozi wa Ethiopia na Somalia kudai kuwa walikuwa wazawa wa jamaa ya Abi Talib, kama tutakavyoona hapo baadaye.

Mapokeo mengine mengi, kwa jumla, hurejelea Bilal wa Ethiopia<sup>2</sup> na mapendeleo ya Mtume kwake na watu wa asili moja na yake, kama usemavyo usemi: 'yule amkaribishiaye Muethiopia mume au mke nyumbani mwake, huleta baraka za Mungu humo.'

Mapenzi haya kwa Waethiopia yaliubua pia maandishi fulani ya fasihi ya Kiarabu. Kuna kazi kama ile ya Ibin al-Jawzi (aliyefariki mwaka 1200) yenye mada ya mbwembwe 'kumulika giza juu ya sifa za Waethiopia weusi' (*Tanwir al-ghabash fi fadl as-Sudan wa l-Habash*). Mmisri mwanahistoria aliyebobea al-Suyuti (aliyefariki mwaka 1505) naye aliandika kijitabu maalum chenye mada 'Kuimuliwa kwa hadhi ya Waethiopia' (*Raf Shan al-Hubshan*) ambacho baadaye kilifupishwa katika kitabu chake kingine 'Maua ya viti vya enzi katika historia ya Waethiopia' (*Azhar al-urush fi akhbar al-Hubush*). Kazi nyingine ya namna hii ni "Zari ya rangi juu ya sifa njema za Waethiopia" (*Al-Tiraz al-mankush fi mahasin al-Hubush*) iliyoandikwa mwaka 1583 na Muhammad ibn Abd al-Baki al-Bukhari al-Makki.

Ilikuwa ni mtindo kuingiza katika kazi hizi sura moja au kadhaa ya maneno ya Kiethiopia ambayo yanafikiwa kuwa yapo katika Ufunuo, yaani katika Kurani tukufu na pia katika hadithi za Mtume, maelezo ya kimapokeo ya matendo na misemo ya Mtume (*hadithi*).

1 Taz. Sura ya 16 ya Juzuu II

2 Taz. Sura ya 4 ya juzuu hili

## *Makazi ya Waislamu katika visiwa vya Dahlak*

Mahusiano kati ya dola ya Kiislamu ya mwanzo na Ethiopia mara nyingi hayakuwa ya kirafiki. Katika karne ya saba yote, Bahari ya Shamu ilikuwa mikononi mwa Ethiopia kikamilifu na Waislamu walipata nguvu polepole tu. Mnamo mwaka 702 Waethiopia walishambulia Hijaz kwa mara ya mwisho na meli zao zikashikilia Jidda kwa muda mfupi. Kama hatua ya kulipiza kisasi kwa kitendo hiki, Waarabu waliteka na kuharibu Adulis na kutwaa Visiwa vya Dahlak kwenye Ghuha ya Masawa vinavyotazamana na Adulis. Visiwa hivi viliwapa fursa ya kudhibiti njia ya baharini ya Ethiopia, ambayo ilikuwa mojawapo ya rasilmali kubwa ya dola ya Aksum. Tokea nusu ya pili ya karne ya nane, hayatajwi tena mashambulizi ya baharini ya Waethiopia wala shughuli zao za baharini kwa jumla. Yaelekea, Waarabu walilivunja jeshi la majini la Waethiopia, ambalo linatokea tena tu katika karne ya kumi na nne.

Katika karne hizi, Waislamu walidhibiti kwa ukamilifu biashara ya majini katika Bahari ya Shamu, kitendo ambacho kilizidi kuitenga Ethiopia.

Kukaliwa kwa Dahlak kulifanyika mapema katika kipindi cha Kimayya na visiwa hivi vilitumiwa pia kama mahali pa wakimbizi wa kisiasa. Baadaye, chini ya Waabbasi, visiwa hivi vilitumika kama kituo cha kuhakikisha usalama wa safari za mahujaji kwenda katika sehemu Takatifu, kutokana na kutapaka kwa maharamia katika Bahari ya Shamu wakati huo.

Mwanzoni mwa karne ya kumi, jimbo huru la Kiislamu lilianzishwa katika Visiwa vya Dahlak. Dola hii ilikuwa na dhima muhimu katika historia ya kiuchumi ya Ethiopia na pia katika kueneza Uislamu kwenye eneo hili<sup>3</sup>

Kuhusu Usultani wa Dahlak na pia kiwango cha utamaduni wa Kiislamu cha wakazi wake, kuna hazina kubwa ya nyaraka zikiwa katika umbo la nakshi za Kiarabu zaidi ya 200 zilizopatikana katika kisiwa kikuu, Dahlak Kabir. Nakshi ya zamani kuliko zote miongoni mwake ni ile ya mwaka 911 na ya karibu mno ni ya mwaka 1539.

Pamoja na nyaraka hizi zinazodhihirisha kuendelea kuwepo kwa Waarabu, mapokeo yaliyoenea sana katika upwa wa Afrika toka ghuba ya Masawa hadi Jibuti nayo yasipuuzwe. Mapokeo haya yanaonyesha kwamba *Wafur* (Waajemi) ndio waliojenga majengo ya kumbukumbu ambayo kwa jumla yalikuwa matangi makubwa ya kukusanyia maji na ambayo mabaki yake bado yanaonekana katika Dahlak Kabir na Adal. Hü huweza kuwa ushahidi wa kuwepo kwa wafanyabiashara wa Kiajemi katika upwa wa Afrika, au yaweza kuwa uthibitisho wa kuajiriwa kwa wahandisi wa Kiajemi katika kujenga majengo haya; tukizingatia sifa kubwa waliyojipatia katika shughuli za hifadhi na ugavi maji.

### *Dola za Kiislamu za kusini mwa Ethiopia*

Pwani ya Afrika ya Bahari ya Shamu ilidumisha kazi yake ya toka zamani kama njia ya kwenda India, ingawa kwa wakati huu kwa kufuata mfumo wa kiuchumi wa nchi za Kiislamu. Punde tu wafanyabiashara wa Kiislamu walisonga mbele kutoka pwani hadi katika maeneo ya jirani ya Ethiopia wakitafuta bidhaa kwa ajili ya biashara.

Japokuwa dola ya Kiukristo ya Aksum ilizua kuenea sana kwa Uislamu Kaskazini, maendeleo yake kusini mwa Ethiopia yalikuwa tofauti sana. Hapa pia Uislamu ulianzia baharini ukifuata njia asilia kutoka Ghuba ya Jibuti kupitia bonde la mto Hawash hadi kwenye

maeneo yenye utajiri mkubwa ya kusini na Maghribi ya nyanda za juu za Ethiopia. Kwa mara nyingine tena kuenea kwa Uislamu kukawa kumefuata njia za biashara; na mpaka leo hii neno *naggadie* ambalo kwa Kiamhara lina maana ya 'mfanyabiashara' linatumika kwa maana ya 'Muislamu' katika lugha ya Waoromo (Wagalla) wa kusini mwa Ethiopia.

Watu mbalimbali wa kusini mwa Ethiopia, kutoka upwa wa Bahari ya Shamu na Ghuba ya Aden hadi Blue Nili, waluingizwa katika Uislamu. Matokeo yake, kuliundwa sultani mbalimbali za Kiislamu zilizotawaliwa na watu waliorithiana kiukoo ambao walidai kuwa na asili ya Kiarabu, wakati ambapo wananchi wenyewe walikuwa Waethiopia na pengine wa koo za Wakushi wa Wasidama.

Usultani wa kwanza miongoni mwa sultani hizi ulikuwa ule wa Damut, ambao mamlaka yake yalifika hadi Ifat. Si rahisi kuonyesha kwa hakika mahali ulipokuwa usultani huu, kwa sababu leo hii Damut ni eneo lililo Kaskazini mwa Blue Nili na kusini mwa Gojam. Yaclekea kwamba Damut mwanzoni lilikuwa jina la nchi kusini-Maghribi mwa Ethiopia katika sehemu karibu kabisa na Blue Nili. Punde tu ilishambuliwa na kutekwa na mfalme (*negus*) wa Ethiopia ya Waukristo; kisha wakazi wake waitwao Walasma wakahamia mashariki zaidi na kukaa Ifat, walikoundia usultani mwingine.

Usultani wa Shoa, ambao katika wakati wake ulikuwa na ushawishi mkubwa katika eneo la Kiislamu la kusini mwa Ethiopia, ulijumuisha walau ukanda wa mashariki wa Shoa ya leo. Eneo hili lilitawaliwa na nasabatawala wa masultani waliodai kuwa wazawa wa nasabatawala maarufu wa Banu Makhzum wa Maka. Majina ya masultani hudhihirisha matumizi ya lugha ya Kisemiti ya Ethiopia.

Nasabatawala wa Makhzum ulitawala Shoa tangu mwaka 896-7 na viongozi wake walirithiana kwa karne nne hadi mwaka 1285, wakati sultani wake wa mwisho na familia yake walipoondolewa madarakani na kuuawa na sultani wa Ifat. Miongoni mwa majina ya masultani wa Makhzum yaliyohifadhiwa ni vema kuzingatia yale yanayoelekea kuwa na sifa maalum kama vile Girangazi, lenye maana 'bwana wa kuogofya,' ambapo Dil-ganis yaweza kufasiriwa kama 'nyati mshindi' na Harb-arad lenye maana ya 'tishio la mikuki; yote haya yanawiana na majina ya kawaida ya kifalme katika Ethiopia ya Kiukristo. Yafaa kumtaja Mfalme Sayfa Arad 'tishio la inajambia.'

Yafaa izingatiwe pia kwamba inaelekea wanawake nao walikuwa na unuhimu fulani katika mfumo wa madaraka wa kisiasa kwenye usultani wa Shoa; hii yalingana na mila ya Ethiopia zaidi kuliko ilivyo kwa upande wa vyeo rasmi katika nchi nyingine za Kiislamu.

Historia ya ndani ya Shoa, inavyojidhihirisha katika *Chronological Repertory*, ina mfululizo wa mapambano kati ya viongozi mbalimbali, na kwa nje mfululizo wa mashambulizi na vita dhidi ya nchi jirani za Kiislamu, hasa dhidi ya Ifat. Lakini imeandikwa pia kwamba mnamo mwaka 1278 Sultani Dil-marrah alishindwa na kuondolewa madarakani na maadui wa ndani na kukimbilia kwa mfalme wa Ethiopia ya Kiukristo. Huu ni ushahidi muhimu wa kihistoria unaohititisha kwamba kuimarika kwa Ethiopia ya Kiukristo chini ya utawala wa Wasulemani wa kwanza kulianza kuathiri usultani wa Shoa ulioanza kudhoofika kutokana na mapambano ya vikundi tofauti.

Hatimaye usultani wa Shoa ulipoteza uhuru wake kutokana na kitendo cha usultani jirani wa Ifat. Mwishoni mwa mgogoro wa wenyewe kwa wenyewe ulioikumba Shoa ya Kiislamu tangu mwaka 1276 hadi 1280, usultani wa Ifat ulilingilia kati moja kwa moja katika mambo ya dola ya Shoa iliyokwishadhoofika; ukaikalia sehemu ya katikati ya Shoa na kukomesha

maeneo yenye utajiri mkubwa ya kusini na Maghribi ya nyanda za juu za Ethiopia. Kwa mara nyingine tena kuenea kwa Uislamu kukawa kumefuata njia za biashara; na mpaka leo hii neno *naggadie* ambalo kwa Kiamhara lina maana ya 'mfanyabiashara' linatumika kwa maana ya 'Muislamu' katika lugha ya Waoromo (Wagalla) wa kusini mwa Ethiopia.

Watu mbalimbali wa kusini mwa Ethiopia, kutoka upwa wa Bahari ya Shamu na Ghuba ya Aden hadi Blue Nili, waliingizwa katika Uislamu. Matokeo yake, kuliundwa sultani mbalimbali za Kiislamu zilizotawaliwa na watu waliorithiana kiukoo ambao walidai kuwa na asili ya Kiarabu, wakati ambapo wananchi wenyewe walikuwa Waethiopia na pengine wa koo za Wakushi wa Wasidama.

Usultani wa kwanza miongoni mwa sultani hizi ulikuwa ule wa Damut, ambao mamlaka yake yalifika hadi Ifat. Si rahisi kuonyesha kwa hakika mahali ulipokuwa usultani huu, kwa sababu leo hii Damut ni eneo lililo Kaskazini mwa Blue Nili na kusini mwa Gojam. Yaelekea kwamba Damut mwanzoni lilikuwa jina la nchi kusini-Maghribi mwa Ethiopia katika sehemu karibu kabisa na Blue Nili. Punde tu ilishambuliwa na kutekwa na mfalme (*negus*) wa Ethiopia ya Waukristo; kisha wakazi wake waitwao Walasma wakahamia mashariki zaidi na kukaa Ifat, walikoundia usultani mwingine.

Usultani wa Shoa, ambao katika wakati wake ulikuwa na ushawishi mkubwa katika eneo la Kiislamu la kusini mwa Ethiopia, ulijumuisha walau ukanda wa mashariki wa Shoa ya leo. Eneo hili lilitawaliwa na nasabatawala wa masultani waliodai kuwa wazawa wa nasabatawala maarufu wa Banu Makhzum wa Maka. Majina ya masultani hudhibirisha matumizi ya lugha ya Kifemiti ya Ethiopia.

Nasabatawala wa Makhzum ulitawala Shoa tangu mwaka 896-7 na viongozi wake walirithiana kwa karne nne hadi mwaka 1285, wakati sultani wake wa mwisho na familia yake walipoondolewa madarakani na kuuawa na sultani wa Ifat. Miongoni mwa majina ya masultani wa Makhzum yaliyohifadhiwa ni vema kuzingatia yale yanayoelekea kuwa na sifa maalum kama vile Giramgazi, lenye maana 'bwana wa kuogofya,' ambapo Dil-gamis yaweza kufasiriwa kama 'nyati mshindi' na Harb-arad lenye maana ya 'tishio la mikuki; yote haya yanawiana na majina ya kawaida ya kifalme katika Ethiopia ya Kiukristo. Yafaa kumtaja Mfalme Sayfa Arad 'tishio la majambia.'

Yafaa izingatiwe pia kwamba inaelekea wanawake nao walikuwa na umuhimu fulani katika mfumo wa madaraka ya kisiasa kwenye usultani wa Shoa; hii yalingana na mila ya Ethiopia zaidi kuliko ilivyo kwa upande wa vyeo rasmi katika nchi nyingine za Kiislamu.

Historia ya ndani ya Shoa, inavyojidhibirisha katika *Chronological Repertory*, ina mfululizo wa mapambano kati ya viongozi mbalimbali, na kwa nje mfululizo wa mashambulizi na vita dhidi ya nchi jirani za Kiislamu, hasa dhidi ya Ifat. Lakini imeandikwa pia kwamba mnamo mwaka 1278 Sultani Dil-marrah alishindwa na kuondolewa madarakani na maadui wa ndani na kukimbilia kwa mfalme wa Ethiopia ya Kiukristo. Huu ni ushahidi muhimu wa kihistoria unaohititisha kwamba kuimarika kwa Ethiopia ya Kiukristo chini ya utawala wa Wasulemani wa kwanza kulianza kuathiri usultani wa Shoa ulioanza kudhoofika kutokana na mapambano ya vikundi tofauti.

Hatimaye usultani wa Shoa ulipoteza uhuru wake kutokana na kitendo cha usultani jirani wa Ifat. Mwisloni mwa mgogoro wa wenyewe kwa wenyewe ulioikumba Shoa ya Kiislamu tangu mwaka 1276 hadi 1280, usultani wa Ifat ulimngilia kati moja kwa moja katika mambo ya dola ya Shoa iliyokwishadhoofika; ukaikalia sehemu ya katikati ya Shoa na kukomesha utawala wa Shoa.

Kwa kuwa njia ya biashara ya bonde la Nili ilikuwa imefungwa kwa Ethiopia ya Kikristo na kwa vile njia ya bahari kwenda India ilipunguzwa kabisa umuhimu wake kutokana na kuimarika na kupanuka kwa utawala thabiti wa Kiislamu, ufalme huu wa Kiukristo ulilazimika

kujipania upande wa kusini kuelekea katikati ya nyanda za juu za Ethiopia. Hatua ya kwanza ilikuwa kuhamisha makao makuu kutoka Aksum hadi eneo la kati la Lasta, na kisha, baada ya nasabatawala wa Kisulemani kujimarisha katika ufalme, waliyahamisha tena hadi mpakani mwa Shoa, ambayo kwa wakati huo ilikuwa dola ya Kiislamu; nyumba ya Watawa ya Mtakatifu Stefano iliyo katika Ziwa Hayq ilikuwa ikitambuliwa kama kituo cha dini ya Kiukristo kabla nayo haijahamishiwa Absbo (Babra-Barkan) ndani kabisa mwa Shoa iliyotekwa. Matukio haya yalifanya Ethiopia ya Kiukristo kutia shinikizo kubwa kwa dola ya Kiislamu kusini mwa Ethiopia, ambazo kwa hali hiyo nazo zilikuwa hatarini.

### *Usultani wa Ifat*

Usultani wa Ifat uliushinda ule wa Shoa katika mamlaka juu ya Uislamu kusini mwa Ethiopia ulitawaliwa na nasabatawala ulioitwa Walasma. Waasisi wake waliingia Ifat mwanzoni kama wakimbizi kutoka dola ya kale ya Kiislamu ya Damut, na nasabatawala huo ulijivunia asili ya mbali ya Uarabu

Tarehe ya mwanzo kutajwa kwenye '*History of the Walasma*' (Historia ya Walasma) ni ile ya miaka 1376-7; lakini taarifa za wakati huohuo mmoja katika *Tarihi* za Ethiopia na pia za wanahistoria wa Kiarabu huwchezsha kukadiria kuanzishwa kwa nasabatawala wa Walasma wa Ifat mwishoni mwa karne ya kumi na mbili.

Sabr al-din, wa kipindi kimoja na Mfalme Amda Seyon (1314-44), naye huzungumziwa kwenye *Tarihi* za Ethiopia kama mtawala wa Kiislamu muhimu kuliko wote kusini akiitwa 'Mfalme wa Mapagani' (*Negusa elwan*). Hii huthibitisha mamlaka Ifat iliyokuwa nayo katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na nne baada ya kuanguka kwa usultani wa Shoa. Zaidi ya hayo, taarifa mbili muhimu za kihistoria pia zimetolewa na *Tarihi* za Ethiopia juu ya sultani Sabr al-din. Ya kwenda ni kwamba kutumiwa kwa neno *kat* (mirungi) na Waislamu wa Ethiopia kumerekodiwa kwa mara ya kwanza. Mirungi (*kat* kwa Kiarabu na *chat* kwa Kiamhara) ni mmea (*Catha edulis*) ambao majani yake husisimua kidogo. Matumizi ya mirungi huko Ethiopia ni sifa halisi ya Waislamu.

Baada ya kuwashinda Waislamu, mtawala wa Kiukristo ahitaka kutumia ushindi huu kuanzisha jeshi katika nchi iliyotekwa, lakini alikabiliwa na upinzani kutoka kwa askari wake. Baada ya kupata ushindi na nyara, walitaka kurudi nyumbani na kufurahia matunda yake na hawakuelewa haja ya ukaliaji wa kudumu wa nchi ya adui. Ukweli huu wa kisaikolojia ni wa kuvutia kwa sababu tutakuta tukio la namna hii hii karne mbili baadaye (katika karne ya kumi na sita), wakati huu wakiwa ni askari wa Kiislamu wa *Imamu Ahmed ibn Ibrahim*, ambao nao hawakupendelea kutamalaki daima nchi ya watu waliohindwa.

Kusonga mbele kuelekea kusini kwa nasabatawala mpya wa Kisulemani na upanuzi wa Ifat ya Kiislamu kuelekea Shoa vilielekea kuleta mapambano kati ya dola hizo mbili. Mkabala wa kwanza tulio nao katika maandishi upo katika *tarihi* ya Mfalme Amda Seyon I ambapo kiongozi wa Ethiopia anasema kwamba mwanzoni mwa utawala wake, ahinshinda Sultani Hakk al-din wa Ifat na kumwua Darader, mwana mfalme wa Kiislamu, ndugu wa Hakk al-din. Yafaa kusema hapa kwamba kitabu cha Kiarabu cha *History of the Walasma* (Historia ya Walasma) hakimtaji Hakk al-din wala vita vyake, lakini kwa kuwa mwandishi wa Kiislamu wa *tarihi* anahusisha mwanzo wa mapambano ya Waukristo na Sultan Hakk al-din II, aliyetawala toka mwaka 1376 hadi mwaka 1386 (karne nyingi baada ya Hakk al-din I) pengine haya ni makosa ya mwandishi au ya chanzo alichopatia habari hizi.



Hata hivyo, vita vya kwanza vilivyo na kumbukumbu nzuri za kimaandishi kati ya Ethiopia na Ifat ni vile vilivyopiganwa mwaka 1332 wakati wa utawala wa Negus (Mfalme) Amda Seyon I na wa Sultani Sabr al-din I. Sabr al-din alishambulia majeshi ya mfalme wa Ethiopia ambaye alikuwa amekwishaingia Shoa, lakini akashindwa. Halafu *negus* akamteua Jamal al-din, ndugu wa Sabr al-din kama sultani wa Ifat, lakini kwa sababu ya chanzo batili cha uwezo wake, alishindwa kudhihirisha madaraka yake na punde tu baadaye aliondolewa kwa harakati kubwa za Waislamu zilizochochewa na mechochezi wa Kiislamu Kadhi Saleh. Mchochezi huyu wa Kiislamu aliweza kuunda umoja wa wanamfalme wa Kiislamu, lakini *negus* kwa mara nyingine aliwashinda maadui wake. Ushindi wake uliingiza enzi mpya miongoni mwa dola hafifu za Kiislamu za kusini, kwa sababu toka wakati huo na kuendelea mamlaka yalitoka Ifat hadi kwa usultani wa Adal, ingawa nguvu ilibakia mikononi mwa nasabatawala wa Walasma. Katika karne mbili (karne ya kumi na tatu na ya kumi na nne) kituo cha siasa cha Uislamu wa Ethiopia kiliamishwa mara tatu, kila wakati katika mwelekeo wa Maghribi-mashariki kuelekea ukiongoni mwa nyanda za juu: kutoka Damut hadi Shoa, kutoka Shoa hadi Ifat na kutoka Ifat hadi Adal.

Ushindi wa Negus Amda Seyon dhidi ya Waislamu uliwachochea viongozi waliofuata kufanya mfululizo wa mashambulizi ya kijeshi kusini. Kwa hivyo Negus Dawit I (1382-1411) alimshinda na kumuua Sultani Hakk al-din II vitani na mrithi wake, Negus Yehaq alimshinda Sultani Saad al-din, mrithi wa Hakk al-din II na kusonga mbele kuelekea bahari hadi kufikia Zayla. Sultani Saad al-din, aliyeshindwa katika vita dhidi ya Waukristo mnamo mwake 1415, akafanywa shujaa wa upinzani wa Kiislamu dhidi ya *manegus* wavamizi, na tangu wakati huo na kuendelea, schemu ya kusini ya Kiislamu iliyokuwa imebakia huru iliitwa 'nchi ya Sa ad al-din' (barr Saad al-din).


Usultani wa Adal, wakati huu ukiwa unaongoza Uislamu wa Ethiopia, ulirejea katika hali nzuri baada ya kupita miongo kadhaa. Baada ya hapo kukawa na jaribio kubwa la kutaka kuivamia Shoa ambayo haikuwa tu sehemu ya Waukristo bali pia makao ya *manegus*. Jeshi la Waislamu liliongozwa na Sultani Shihab al-din Ahmed Badlay. Baada ya mafanikio ya mwanzo, Badlay alishindwa na Negus Zarea Yakob katika vita vikubwa huko Egubba mnamo Desemba 29, 1445, na sultani huyo aliuawa vitani. *Negus* alilifuatia jeshi la Waislamu hadi Mto Hawash na kuteka nyara nyingi zilizoathaminiwa na Waethiopia Waukristo. Hii ilikuwa kwa sababu mahusiano ya kibiashara ambayo usultani wa Adal ulikuwa nayo na nchi za nje yaliuwezesha kupata vitu vingi vya anasa ambavyo Waethiopia Waukristo, ambao mahusiano yao na nchi za kigeni yalikuwa hayakupanuka, walikuwa hawawezi kupipata.

Baada ya vita vya Egubba, masultani wa Adal, ambako nasabatawala wa Walasma, masultani wa awali wa Ifat, uliendelea kutawala, walianzisha makao yao makuu Dakar ukingoni mwa tambarare za mashariki. Miaka michache baadaye, Negus Eskender alifanya mashambulizi, akaingia Adal na kuteka na kuuharibu mji mkuu huu. Hata hivyo wakati wa kurudi nchini kwake Shao, jeshi la Waukristo lilishambuliwa ghafla mnamo mwaka 1475 na sultani wa Adal, Shams al-din ibn Muhammad; Negus Eskender alishindwa na kuuawa vitani. Lakini Waislamu hawakufuatia ushindi huu, kwa sababu Adal ilivurugwa na kufanywa maskini na mapambano ya maemiri mbalimbali waliokuwa wakigomba mamlaka.

Kisha mji mkuu ulihamishwa tena kuelekea mashariki hadi Aussa kwenye tambarare, mpaka Sultani Abu Bakr ibn Muhammad ibn Azhar al-din hatimaye alipohamisha makao makuu toka Adal hadi Harar mnamo mwaka 1520. Kwa hivyo alianzisha nasabatawala wa maemiri wa Harar ambao toka wakati huo na kuendelea uliitwa uemiri wa Harar. Sababu

ilikuwa kwamba Sultani Muhammad ibn Abu Bakar ibn Azhar al-din, ambaye alihamishia makao makuu kusini kwa ajili ya usalama, alikuwa na mamlaka makubwa kwa jina tu, kwani katika kiti cha enzi aliwaweka wanamfalme wa ukoo wa Walasma ambao aliwaachia cheo cha usultani. Kwa kufanya hivi aliepuka kulaumiwa kuchukua cheo kisicho chake akawa na madaraka kidogo tu ya nasabatawala wa zamani kwa sababu zake mwenyewe. Warithi wake nao walifanya hivyo hivyo, hadi nasabatawala wa Walasma ulipotoweka kabisa katika mazingira yasiyoeleweka.

Usultani mpya wa Harar nao punde tu ulivurugwa na migogoro ya wenyewe kwa wenyewe; na hali hii iliendelea hadi alipotokea mtu mmoja mwenye nguvu kwa jina *Imam Ahmed ibn Ibrahim*, ambaye alichukua madaraka na kujitwalia mamlaka yote.



## *Pwani ya Afrika Mashariki na visiwa vya Ngazija*


### *Utangulizi*

Sura hii inajaribu kutathmini tena historia ya Pwani ya Afrika Mashariki na Visiwa vya Ngazija kati ya karne ya saba na karne ya ishirini. Tathmini hii inafanywa katika hali ya kurekebisha picha mbaya iliyoonyeshwa na wanahistoria na/au wanaakiolojia wa mkondo wa mawazo ya kikoloni ambao kwa kiasi fulani walielezea historia ya wafanyabiashara wa kigeni na wakoloni waliohusika na kufanywa kuwa wao ndio walioleta ustaarabu wa pwani. Dhima ya wageni katika historia ya zamani ya pwani ya Afrika Mashariki haiwezi kukataliwa, kwani ni jambo moja kuwa sehemu ya mchakato wa mabadiliko, na ni jambo jingine kabisa kudai kuwa wewe ndiye uliyesababisha mchakato huo. Uchunguzi wa hivi sasa, kidogokidogo lakini kwa uthabiti zaidi, unaanza kuonyesha wazi kabisa kuwa historia ya pwani ya Afrika Mashariki ni historia ya wenyeji wa Afrika na maingiliano yao na mazingira.

### *Akiolojia vyanzo*


Ingawa kazi ya kiakiolojia katika eneo hili bado iko katika hatua za mwanzo, tayari ushahidi wa kutosha umepatikana kuthibitisha kuwepo kwa makazi ya binadamu kwa muda mrefu katika sehemu nyingi za Afrika Mashariki. Ushahidi uliopo mwingi sana ni ule wa makazi ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma na Enzi zilizofuatia. Kwanza kabisa ni eneo la Kwale lililochimbuliwa katika miaka ya kati ya 1960 ambako kuhpatikana aina mbalimbali za vyombo vya udongo, mavi ya chuma, zana, n.k., vyote hivyo vikithibitisha kuwepo hapa kwa watu wa Enzi ya Chuma katika robo ya kwanza ya kikwa cha kwanza ya enzi ya Ukristo. Vifaa na vyombo vya utamaduni vya kipindi hicho hicho pia vimechimbuliwa na vingine kupatikana juu ya ardhii tu katika maeneo kadhaa katika sehemu za kati na pwani ya Tanzania na Kenya. Baadhi tu ya maeneo hayo ni kama vile milima ya Usambara, milima iliyoko kusini mwa Upare na katika makazi ya kaya ya Mijikenda.

Kwa mfano, katika eneo la Gedi, aina ya vyombo maalum vilivyopambwa vya karne ya kumi na mbili vilichimbuliwa kutoka katika tabaka lililo chini ya msingi wa mji. Mapambo na mitindo yake hapana shaka ni ya Kiafrika, lakini mabaki ya vipande hivyo yametajwa kuwa ni ya Waoromo na siyo ya Wabantu au Waswahili kwa misingi ya ushahidi hasi. Huko Unguja Ukuu na Manda, kumegunduliwa makazi ya tokea karne ya tisa. Hata hivyo, Chittick anasema kuwa vyombo vya Kiislamu vyenye rangi ya bluu ndivyo vilivyokuwa vikiagizwa



**21.1** Machunbo ya Manda

**21.2** Msikiti wa Shrazi ya Kale wa Domani Anouan, Visiwa vya Comoro (karne ya kumi na moja)  
(H. T. Wright, P. Vénin)



zaidi ya vingine lakini hakuna takwimu zozote zilizotolewa ili kuweza kulinganishwa na vyombo vilivyotengenezwa katika sehemu hizo.

Mjini Kilwa, kipindi cha karne ya tisa hadi ya kumi na mbili kilichotangulia nasabatawala wa Kishirazi kilikuwa na vyombo vya utamaduni vya namna moja ikiwa ni pamoja na mavi ya chuma kama ushahidi wa uweyushaji chuma, utengenezaji shanga, vyombo vya udongo na mabaki ya samaki. Ingawa Chittick anadai kuwa Kilwa haikuwa na wakazi wenyeji tarihi zinaonyesha bila ya shaka kuwa watu wa Kilwa kwa wakati huo walikuwa wenyeji watupu. Vyombo vya rangi nyekundu vya aina hiyo vimepatikana katika maeneo mengine ya pwani kama Unguja Ukuu na Manda. Ukweli kwamba hakuna taarifa ya vyombo hivyo vya udongo iliyowahi kupatikana bara haina maana kwamba mbinu hii ya ubunifu isingeweza kutokea katika miji ya pwani tu.

Aina mbili za vyombo vya udongo vya kienyeji katika kipindi hiki ni: 1. vyungu vya kupikia vyenye umbo kama mfuko vikiwa na mapambo ya nakshi katika mzingo au pembeni mwake, na

2. vyombo vyele vya udongo vilivyochoywa. Vyombo vya udongo vilivyoingizwa kutoka nje ni vile vyenye mapambo ya rangi na pia vyombo vya udongo kutoka Uajemi vilivyopakwa rangi ya bati. Ugunduzi mwingine wa kiakiolojia katika kipindi hiki ni pamoja na visu, vigumba vya mishale, ndoana, mirija, ncha za chuma, misumari na shanga za madini. Kama ilivyokuwa Manda, shanga za kioo hazionekani kabla ya karne ya kumi.

Huko Unguja Ukuu katika Kisiwa cha Zanzibar, vyombo vya udongo vya zamani kabisa vimeainishwa kuwepo katika karne ya kumi au katika kipindi sawa kabisa na kipindi ambacho vyombo hivyo vilikuwepo Manda. Ingawa inasemekana kuwa mji wa Gedi ulianzishwa katika karne ya kumi na mbili na kwa hiyo uko nje ya kipindi ambacho kinashughulikiwa katika juzuu hili, inaraghibisha kuona kuwa kiasi cha vigaye vya vyombo vya udongo vya kienyeji vilizidi kiasi cha vigae vya vyombo vya udongo vilivyoagizwa kutoka nje. Vyombo vya udongo vya kienyeji vilivyokuwepo wakati huo havikung'arishwa, vilikuwa na nakshi za mistarimistari, vilibonyea kidogo, havikupambwapambwa sana kwa rangi. Chapa ya Kiafrika yaani, vyombo vilivyopambwa kwa vituta vituta na mabakuli yenye umbo la nusu mvingo ya tokea zamani kabisa ni dhahiri kabisa kuwa ni vya Kiafrika; aina hii inafanana na vyombo vya udongo kutoka katika maeneo ya Afrika ya Kati ya Zimbabwe na Mapungubwe.

Vyungu vya kupikia vilivyopambwa kwa nakshi za kucha za vidole, ambavyo bado vinafinyangwa hadi hivi leo na Wagiriama, viligunduliwa Gedi. Aina hii maalum ya mapambo inachukuliwa kama ni mtindo wa Wanyika, tofauti na mapambo ya nakshi yaliyokuwa yakitumiwa na Waswahili.

Ushahidi wa kiakiolojia katika pwani yote ya Mashariki unaonyesha dhahiri pasi na shaka yoyote kuwa kulikuwa na wenyeji waliokuwa na ustaarabu wao kabla ya majilio ya Waarabu. Baada ya kufika kwao, ufundi wao wa kutengeneza vyombo vya udongo ulififishwa na ufundi wa kigeni, ambao ulitumika badaŵa yake. Matokeo yake ni kwamba vyombo kutoka nje ya nchi vikiwa ni pamoja na vyombo vya udongo vyenye rangi ya bluu na kijani (vya Waislamu); vyombo vya udongo vyenye rangi ya njano na nyeusi; na *celadon* ya buluu na nyeupe (China), vilikuwa vingi kuliko vile vya asili baada ya kuanzishwa kwa mji wa Gedi.

## Vyanzo vya Maandishi

Ushahidi wa kiakiolojia ulitolewa hapo awali kuhusu kuwepo kwa makazi ya asili katika eneo hili katika kipindi hicho umethibitishwa zaidi na vyanzo vya maandishi. Idadi kubwa zaidi ya

vyanzo hivyo imeandikwa na waandishi wa Kiarabu lakini pia kuna sehemu ya maelezo yaliyotolewa katika maandishi ya Kichina. Wingi wa matini yaliyoandikwa katika lugha ya Kiarabu ndio uliosababisha pwani ya mashariki kwa muda mrefu ifikiriwe kuwa koloni la Kiarabu na Kiajemi au kiambatio cha utamaduni wa himaya kubwa ya Kiislamu ambapo wenyeji walichangia kiasi kidogo sana. Hata hivyo, usomaji wa makini wa kazi muhimu kabisa za Kiarabu na ufafanuzi wake usiopendelea upande mmoja utaonyesha picha tofauti na ile iliyoonyeshwa katika mkondo wa awali wa historiografia.

Waarabu waliwaita wakazi wa Mashariki mwa Afrika, kusini mwa mto Juba, *al-Zanj* au *al-Zinj*, jina ambalo etimolojia yake haifahamiki vizuri. Baadhi ya maneno ya *Kizanj* yaliyonukuliwa na waandishi wa Kiarabu yanaonyesha wazi chanzo chao katika Kibantu; jina la Mungu *makujulu* linafanana na jina la Kibantu *mkulu* (mtu mkubwa), takriri yake *Mkulunkulu* ikionyesha hadhi au ukubwa wa mtu. Neno linalokaribiana sana na hili la zamani ni lile la Kizulu *unkulunkulu*. Maneno mengine yaliyohifadhiwa ni *wafimi*, neno ambalo kwa Kiswahili ni *wafalme* (umoja, *mfalme*) - wafalme au machifu; *inbila*, linalotokana na neno la Kibantu *mpela* - lenye maana ya kifaru; au *makwanju*, ambalo kwa Kiswahili ni *mkwaju* - mti unaozaa ukwaju (*Tamarindus indica*).

Katika kipindi hiki hakuna mahali popote katika maandishi ya Waarabu panapoonyesha makazi makubwa au makoloni ya wahamiaji kutoka katika nchi za Kiislamu. Pwani inaelezwa kuwa ilikaliwa na watu; na umuhimu zaidi ilitawaliwa na wenyeji wa sehemu hizo. Al-Masudi, ambaye aliitembelea pwani hii mnamo mwaka 916, alisisitiza tabia za watu wasiokuwa Waislam wa eneo la Zanj, na hadithi iliyojulikana sana ya Buzurg ibn Shahrriyar kuhusu kutekwa nyara kwa mfalme wa Zanj kulikofanywa na Waarabu wafanyabiashara ya watumwa kunatoa ushahidi wa ziada wa maendeleo huria ya Wabantu walioishi pwani. Hata katika maandishi ya al-Idrisi ambayo ni ya baadaye zaidi (1165), tunapata taswira ya kuwa nguvu ya kisiasa katika makazi yote ya pwani ilikuwa mikononi mwa Waafrika waliokuwa wanaishi katika sehemu hiyo ya pwani.

Kwa upande mwingine, vyanzo vyote vya maandishi ya Kiarabu vinazungumzia kukua kwa biashara kati ya pwani ya Afrika Mashariki na nchi (ardhi) zinazozunguka Bahari ya Hindi na kuwasili mara kwa mara kwa wafanyabiashara wa Kiarabu, Kiajemi na Kihindi. Maingiliano haya hayakuwa mapya, kwani katika kipindi kilichotangulia maandishi wa Kiyunani na Kirumi walikwisha kuueleza uhusiano wa kibiashara baina ya eneo hili na sehemu nyingine zilizopakana na Bahari ya Hindi<sup>1</sup>.

Kuhusu kuwepo kwa idadi kubwa ya watu wenye asili ya Kiarabu na Kiajemi katika makazi ya pwani na kufikiriwa kwao kuwa wao ndio walioyaanzisha, katika kipindi hiki kuna ishara moja na hata hiyo ishara moja pia ina utata mkubwa. Al-Masudi anatumia kuwa kisiwa cha Kanbalu (Pemba) kilikaliwa na Waislamu, ingawa lugha yao ni ya Kizanj, na kueleza kuwa Waislamu walikiteka kisiwa hicho na kuwafanya wenyeji wake kuwa wafungwa. Hakuna mahali ambapo mwandishi anasisitiza kuwa Waislamu hawa walikuwa Waarabu au Waajemi; lugha yao inaonyesha kuwapo kwa wasemaji wa Kibantu waliosilimishwa. Kwa vyovyote vile, visiwa hivyo vilikwishakaliwa na Wazanj kabla ya utamalaki wa Waislamu.

## Mapokeo Simulizi

Chanzo kikuu cha tatu ni mapokeo simulizi yaliyohifadhiwa katika tarihi za wenyeji wa Pate, Lamu, Kilwa na miji mingine. Kumbukumbu nyingi kati ya hizi zilikuwa zimeandikwa ama kwa Kiswahili au kwa Kiarabu mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Maelezo ya *Tarihi za Kihwa* yamo katika kitabu cha Joao de Barros, *Decadas da Asia* cha karne ya kumi na sita na hivyo kuwa karibu kabisa na kipindi kilichopita. Katika mapokeo haya mengi, jaribio

linafanywa ili kuweka uhusiano baina ya nasabatawala au tabaka la watawala na baadhi ya watu mashuhuri na/au miji ya historia ya Mashariki ya Kati. Huu ni mwelekeo wa kawaida katika mapokeo ya karibu jamii zote za Kiislamu za Kiafrika.<sup>2</sup>

Ingawa mapokeo simulizi mengi si ya kuaminika sana kutokana na ukale wa kipindi tunachokizungumzia hapa, hata hivyo ndicho chanzo cha historia ya koo tatu za Mombasa (*Taifa tatu*) Wachangamwe, Wakilindini na Watangana – ambao mapokeo yao yanadai kwamba wao walikuwa wazawa wa eneo hilo hadi utawala wao ulipopinduliwa na watawala wa Kishirazi katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tatu.

Wanahistoria wengi wametumia vyanzo hivi tu katika kutoa historia ya kuenea na kuhamia kwa watu na mawazo katika pwani ya Afrika; matokeo ya mchanganyiko huo yakiwa kwamba historia na ustaarabu wa pwani ni vitu vya kigeni.

Kwa hivyo ni muhimu kuipitia tena historia kwa kutumia mkabala mpya ambao unayaainisha mambo ya wenyeji katika mwanzo wa ustaarabu wa pwani ya Afrika Mashariki na kuonyesha kwamba ustaarabu huo ni wa watu wa asili waliokuwa wakiishi sehemu hiyo na uliendelea kulingana na mazingira ya eneo lenyewe. Kauli hii haikatai kuwepo kwa vipengee vya ustaarabu wa kigeni vilivyojitokeza hapa na pale kwani hatushughuliki na utamaduni uliofungwa.

## Watu wa Pwani

Wanajiografia wa Kiarabu waliigawanya pwani ya Mashariki katika sehemu kuu tatu: nchi ya Wabarbar (*Bilad - al-Barbar*) iliyokuwa Kaskazini; nchi ya Zanj (*Bilad al - Zanj*) iliyokuwapo kati ya mto Webi Shebele na sehemu ya pwani iliyokuwa inatazamana na Zanzibar, na sehemu ya Sofala (*Ard au Bilad Sufala*) iliyokuwa kusini. Iwapo nchi ya ajabu ya Wak-Wak ambayo mahali pake panatatanisha itawekwa kusini zaidi katika bara la Afrika, au iwapo eneo hilo ni nchi ya Bukini, ni vigumu kuamua kutokana na mkanganyiko wa maelezo yaliyopo.

Kuna uwezekano mkubwa kuwa neno *Barbar* lilitumiwa na Waarabu kuwaita Wasomali na watu wengine waliokuwa wanazungumza Kikushiti waliokuwa wanaishi katika Pembe ya Afrika. Istilahi hiyo tayari ilikwishatumiwa katika *Periplus* na Klaudius Ptolemy na Kosmas kwa maana hiyo hiyo. Kuna ushahidi wa kutosha wa kuonyesha kwamba kundi la watu waliokuwa wanazungumza lugha ya Kibantu liliishi katika eneo hilo hadi mto Webi Shebele. Makundi yanayozungumza lugha za Kibantu kama vile Washidla, Washabeli, Wadube na Waelayi bado yanaishi katika sehemu ya chini ya mto Webi Shebele; na kundi linalojulikana kama Wagosha bado lipo Kaskazini mwa mto Juba. Kwa upande mwingine, inaonekana kuwa mapema kabisa mnamo karne ya kumi na ya kumi na moja Wasomali waliingia katika ukanda wa pwani katika eneo baina ya Mogadishu na Brava; na katikati ya karne ya kumi na mbili tayari al-Idrisi alikwishavumbua vijiji hamsini vya Wahawiya, kundi la Kisomali ukingoni mwa mto ambao jina lake halikutajwa, pengine mto huu ni ule mto Webi Shebele.

Inaonekana kuwa nchi ya Wazanj ndiyo iliyowavutia sana kuliko sehemu nyingine zote za pwani. Sababu kubwa ilikuwa ni biashara kubwa iliyokuwa ikifanyika baina ya Zanj na nchi nyingine zilizopakana na Bahari ya Hindi. Maelezo yaliyotolewa na waandishi wa Kiarabu yanadhihirisha pasi na shaka yoyote kuwa watu waliokuwa wanaishi pwani walikuwa ni weusi. Waandishi walioishi kabla ya karne ya kumi na mbili hawakufahamu sehemu yoyote ya pwani kwa jina ila tu makazi yaliyokuwa katika visiwa. Licha ya Kanbalu (ambayo

2 Taz. Sura 4 ya juzuu hili.

inawezekana kuwa ni Kisiwa cha Pemba), mji ambao ulitembelewa na al-Masudi, ni jina moja tu jingine lililotajwa na mwandishi wa zamani: al-Jahiz (alikufa mwaka 869) ambaye aliigawa Zanj katika sehemu mbili, *Kanbalu* na *Lunjuva*, neno ambalo ni dhahiri kuwa ni matamshi mabaya ya neno la Kibantu lenye maana ya Zanzibar - Unguja. Mwandishi huyohuyo pia anahusisha maelezo yanayovutia sana na ambayo hayapatikani mahali pengine kuhusu misafara ya baharini iliyoongozwa na Mwana Mfalme wa Oman ambayo pengine iliwasili eneo la Zanj mwishoni mwa karne ya saba na ikaangamizwa na wenyeji wa pale.

Kusini ya nchi ya Zanj palianza nchi ya Sofala iliyoitwa na Warabu *Sufala al-Zanj* (Sofala ya Zanj) ili kuitofautisha na Sofala ya India iliyo karibu na Bombay. Kwa kuwa Sofala ya Afrika ilikuwa maarufu sana kwa dhalabu, ilijulikana pia kama *Sufala al-dhabab* (Sofala yenye dhahabu) au *Sufala al-tibr* (Sofala yenye mchanga wa dhahabu). Nchi hii ilichukuwa sehemu yote ya pwani kati ya Pangani na Msumbiji. Watu wa Sofala walikuwa na udugu na watu wa Zanj na walikuwa na uhusiano wa kibiashara na wafanyabiashara kutoka katika nchi za Kiarabu na India. Nchi hiyo ilikuwa kituo cha mwisho cha misafara ya baharini kwani hakuna meli iliyodiriki kwenda mbali kutokana na hatari ambazo zingeweza kutokea kutokana na kuabiri katika bahari isiyokuwa na ramani. Kauli ya Al-Biruni (1050) kuwa mbele zaidi ya Sofala Bahari ya Hindi iliungana na bahari ya Maghribi (Atlantiki) ni ya kufurahisha.

Hadi kufika karne ya tisa, miji mingi ya pwani ya Afrika Mashariki ilikaliwa na Waswahili. Kiwango cha utajiri kilitofautiana kutoka mji mmoja hadi mwingine, kutegemeana na uongozi wao wa kijamii na shughuli za kiuchumi. Miji michache sana ilikuwa imejengwa kwa mawe katika hatua za awali, lakini kadri makazi hayo yalivyositawi, matokeo yake yalikuwa ni ujenzi wa nyumba za mawe. Nyumba za miji ya Kilwa na Mafia, kama ilivyoonyeshwa na machimbo ya kiakiolojia, zilijengwa kwa udongo na fito. Miji hiyo ilikuwa na uchumi uliokitwa katika uvuvi wa samaki, ufinyanzi na bidhaa zilizotengenezwa kwa chuma, na kwa kiwango kidogo, biashara ya ndani.

## Muundo wa jamii

Miji ya pwani kila mara ilikuwa ikijitawala yenyewe na kwa jumla ikijitegemea; uhusiano wa mji mmoja na mwingine ukifuata ruwaza mbalimbali za ushirikiano na uadui. Mara kwa mara Kilwa, Pate na Mombasa zilifanikiwa kupata utawala usio dhahiri wakati zilipokuwa na nguvu za kutoza kodi watu wengine.

Katika nchi za Benadir zilizokuwa katika pwani ya Somalia, inaelekea kuwa mwanzoni mamlaka yalikuwa ni ya baraza la wakuu wa koo mbalimbali kama ilivyokuwa Mogadishu, Brava na Siyu, mmojawapo akijulikana kama wa kwanza kati ya wote. Lakini miji mingi ya pwani iliwapa mamlaka maichifu ambao wakati mwingine walikuwa wahamiaji wa Kiarabu au wa Kiajemi waliokubalika kwa hiari, kama ilivyokuwa katika Pate, pengine kwa sababu walikuwa nje ya koo zilizokuwa zinashindania madaraka.

Mchanganyiko wa wenyeji na wahamiaji ulisababisha mchanganyiko wa watu wa mataifa mbalimbali na jamii yenye uchumi maalum. Hali hii ilisababisha ruwaza ya tabia ya kutofautiana kiuchumi-kijamii na kuundwa kwa tabaka za kijamii, kukiwa na makundi kadha kila moja likiishi katika *mtaa* wake. Makundi hayo mbalimbali ya mitaa yalikuwa na mpangilio wa kimsonge kundi moja dhidi ya kundi jingine.



## Lugha ya Kiswahili

Makazi ya pwani au miji midogo ilikusanya watu tofauti, wengi wao wakiwa ni Wabantu, hali ambayo iliwezesha kukua kwa Kiswahili.

Neno *Swahili* linatokana na neno la Kiarabu *sahil* (wingi *sawahil*) — likiwa na maana ya pwani – na lilitumika kwa mara ya kwanza kwa eneo linaloanzia Mogadishu hadi Lamu. Lugha ya Kiswahili (kwa tafsiri ya 'lugha ya pwani') ilikua baadaye baada ya kuingizwa maneno ya kuazimwa ya Kiarabu na Kiajemi kulikoenda sambamba na kuwasilimisha watu wa pwani. Kwa hivyo, itakuwa ni sahihi, hasa kabla ya karne ya kumi na tatu, kuzungumza kuhusu *mame-Kiswahili* kama lugha ya Kibantu ambayo ndio msingi ambao kwao lugha ya Kiswahili ilikuzwa. Inaelekea kuwa lugha ya Kiswahili kwanza ilishamiri katika eneo lililo Kaskazini mwa delta ya mto Tana katika pwani ya Somalia na kuenea kuelekea kusini. Kauli hii inalingana na ruwaza ya makazi, kwani hadi mwaka 1300, kulikuwa na makazi takribani ishirini Kaskazini mwa mto Tana; kusini mwa mto huu kukiwa na miji ya Mombasa, Malindi, Zanzibar, Pemba, Kilwa na mingineyo michache. Miji hii ilikistawisha Kiswahili na kukifanya kikue, ambapo uhamaji uliofuatia kutoka katika eneo chimbuko la Kiswahili ulieneza lugha hii.

Uchanganuzi wa lugha umedhihirisha wazi kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu yenye uhusiano wa karibu na lugha za Kipokomo na Kimijikenda ambazo mwanzoni zilikuwa zikizungumzwa katika pwani ya Somalia na pwani ya Kaskazini mwa Kenya. Inaelekea kuwa Kiswahili kimeanzia katika eneo hili na kuwa watu waliokuwa wanazungumza lugha zenye nasaba ya Kimijikenda, Kipomoko na Kiswahili waligawanyika na lugha zao ziligawanyika katika lahaja tofauti na mwishowe kuwa lugha tofauti.

Kadiri biashara ilivyozidi kuwa muhimu na maingiliano na wafanyabiashara wa Kiislamu kuongezeka, idadi ya maneno ya Kiarabu na Kiajemi na hati ya Kiarabu vikaingizwa katika Kiswahili. Katika karne ya tisa, lugha ilienea pwani, ikiwa imeletwa na wafanyabiashara kutoka nchi ya Somalia na Kaskazini mwa Kenya ambao walianzisha makao yao mapya na kuingiliana na jamii ambamo walikaa na kuwezesha taratibu kuchukuliwa kwa dini ya Kiislamu kuwa dini ya tabaka tawala na tabaka la wafanyabiashara.

Mtazamo huu ni kinyume kabisa na hoja iliyotolewa na baadhi ya wanahistoria, ambao walisema kuwa utamaduni wa Kiswahili una vipengee vingi vya Kiarabu, kwamba lugha hiyo inatumia maandishi ya Kiarabu na kuwa misikiti na majengo ya mawe yamejengwa katika mitindo ya Kiarabu. Mtazamo huu ulikuwa ni wa kimweneo zaidi kwani ulichukulia kwamba ubunifu wa kiutamaduni na maendeleo ya kihistoria katika Afrika ya Mashariki unaweza kutoka nje ya nchi tu. Uchunguzi uliofanywa hivi karibuni kuhusu utamaduni wa Kiswahili na jamii umeonyesha kuwa vipengee vya Kiafrika ni vingi zaidi kuliko maelezo yale yaliyotolewa ambayo yalijikita zaidi katika hoja za kimweneo:

- (1) Muundo wa sarufi ya Kiswahili na sehemu kubwa ya msamiati vinakaribiana sana na lugha za Kimijikenda na Kipokomo wakati ambapo fasihi yake inaakisi kanuni za mpangilio wa masimulizi ya Kiafrika.
- (2) Mambo ya utamaduni wa Waswahili hayana ulinganifu na yale ya Uarabuni wala Uajemi. Mtindo wa Waswahili wa kujenga kwa kutumia mawe hauna vifani makimi vya kutosha ambavyo vinatuwezesha kufikia hitimisho la kuwa chanzo chake kiko Mashariki ya Karibu. Mtindo huo uliendelea kutokana na mtindo wa ujenzi wa kutumia udongo na

fito ambao ulienea pwani kutokana na kuongezeka kwa uchumi na tofauti za kiuchumi na kijamii.

- (3) Hata Uislamu wa pwani una mabaki ya dini za kiasili za Kiafrika ambazo imani yake imejikita katika mizimu na kupunga pepo, kuabudu wahenga, uchawi na uramali, vyote vikienda sambamba na imani balisi ya mapokeo ya kisharia.

Japokuwa Uislamu ulifika sehemu ya Kaskazini ya pwani ya Afrika Mashariki katika karne ya nane na sehemu ya kusini kabla ya karne ya kumi na moja, ilikuwa ni mpaka katika miaka ya 1400 ndipo ustaarabu wa Kiislamu wa pwani ulipojitokeza ambao baadaye ulijulikana kama *Shirazi*. Kwa muda mrefu, dini ya Kiislamu ilienezwa na wahamiaji kutoka Uarabuni na Uajemi ambao waliishi katika miji ya pwani. Japokuwa wataalamu hawakundeleva shughuli ya kuwabadilisha watu dini kwa kiasi kikubwa, baadhi ya wafuasi wao pamoja na Waafrika waliopenda kufanya biashara na wageni waliikubali dini ya Kiislamu kama dini yao.<sup>3</sup> Kwa jumla inakubaliwa kwamba dini ya Kiislamu ilienezwa visiwani kabla ya kuenezwa bara.

Shughuli ya kueneza dini inahusishwa sana na tatizo la Washirazi. Mapokeo simulizi na tarihi za karibuni zilizoandikwa kwa Kiswahili zinasisitiza kuwa baadhi ya wafanyabiashara kutoka Ghuba ya Uajemi, hasa kutoka Siraf, bandari ya mji maarufu wa Shirazi, walikuja Afrika Mashariki katika karne ya tisa na ya kumi. Maelezo mengine kutoka Kilwa yanaonyesha uwezekano wa kuwaliwa sehemu ya Kaskazini ya pwani (pwani ya Benadir) na kufanywa koloni na Wakarmatia wenye madhehebu ya Kishia<sup>4</sup>, ambao kituo cha utawala wao kilikuwa katika jimbo la al-Ahsa la Uarabuni, linalopakana na Ghuba ya Uajemi. Mapokeo hayo yanadai kuwepo kwa uhusiano baina ya jimbo la Kikarmatia la al-Ahsa na kuanzishwa kwa madola ya Mogadishu, Brava, Marka na pengine pia ya visiwa vya Lamu na Zanzibar. Halikadhalika yanadai kuwa Kilwa ilianzishwa katika kipindi hichohicho (cha karne ya kumi) kama ilivyokuwa kwa miji ya Benadir, lakini miji hii ilianzishwa miaka mia mbili mapema zaidi kuliko miji ya Kilwa, Sofala na ile iliyoko katika Visiwa vya Ngazija.

Washirazi wamesifiwa kwa kuleta usanifu majenzi wa hali ya juu wa kutumia mawe, matumizi ya chokaa na saruji, useremala, usokotaji nyuzi za pamba pamoja na sayansi nyingine ikiwa ni pamoja na kalenda ya Waajemi inayotumia jua pamoja na aina mbalimbali za matunda. Hata hivyo, hii leo inadaiwa kuwa Washirazi hawakuleta hayo yote, bali maendeleo yake yalichapuzwa na usitawi ulioletwa na biashara. Bila shaka, baadhi ya miti ya matunda lazima itakuwa imeletwa na Waarabu na Waajemi, lakini ufundi wa ujenzi wa kutumia mawe na useremala ulifahamika pwani hata kabla ya kuja kwa Washirazi.

Mapokeo simulizi kuhusiana na athari za Waajemi katika pwani ya Benadir yanasaidiwa na maandishi ya karne ya kumi na tatu yenye majina ya Kiajemi, lakini kwa upande mwingine, kuna ushahidi mdogo sana wa shughuli za Waajemi kusini mwa pwani ya Somalia. Hata hivyo, kuna dalili kuwa tangu mwaka 1100 wa enzi ya Ukristo na kuendelea, kundi la wafanyabiashara, wengi wao wakiwa wametokana na kuoana kati ya vizazi vya Waarabu na Waajemi na wenyeji wa pwani ya Benadir, walianza kuhamia kusini na kuchukua pamoja nao utamaduni wa Kiislamu wa Waarabu na kuupeleka katika Visiwa vya Zanzibar, Pemba, Kilwa, na Mafia. Visiwa hivi pamoja na miji ya Ozi, Mafiudi na Mombasa vilibaki kuwa vya

3 Taz. Sura 3 ya juzuu hili.

4 Taz. Sura 7 ya juzuu hili.

Kishirazi, ingawa viliendelea kugeuzwa kuwa vya Kibantu hadi baada ya kutamalaki Wareno.

### *Shughuli za Kiuchumi*

Katika hali za kiuchumi, jamii ya pwani iliendelea kuwa na maisha ya mjini na vijijini ikiwa na watu walioishi kutokana na kilimo. Bila shaka kulikuwepo pia na wafugaji hasa Kaskazini mwa pwani ya Benadir. Lakini wengi wa Waswahili, hasa wale waliokuwa wakiishi katika makazi madogo au ya wastani walikuwa wakulima. Katika vyanzo vya Kiarabu tunaona maelezo ya mabaki kuhusu mazao na tamaduni. Inaonekana kuwa mazao makuu yalikuwa mtama (*dhurra*), na pia viazi vikuu ambavyo kwa jina la kienyeji vililitwa *al-kirari*, jina ambalo lilithibitishwa na al-Masudi. Zao jingine lililolimwa na Wazanj lilikuwa *al-rasan*, ambalo limeainishwa kama *coleus*. Chakula cha watu wa pwani kilikuwa ni pamoja na ndizi, nazi, mchele na ukwaju, na katika sehemu nyingine hata zabibu, na pia umetajwa muwa kama mmea.

Uchunguzi wa kiakiolojia huko Kilwa umeonyesha kuwa zao pekee la nafaka lililolimwa lilikuwa mtama kama unavyoonyesha ushahidi wa mbegu zilizozingizwa karboni. Hakuna vyombo vyovyote vya kusaga nafaka vilivyopatikana katika kipindi cha mwanzo lakini katika kipindi kinachofuata, mawe yanayozunguka pia yalitumika kama ilivyo sasa, lakini vyombo hivyo vingewa kutoweka katika *kumbukumbu za kiakiolojia*.

Jumua za pwani zilijihusisha pia na shughuli za baharini kama vile uvuvi, uundaji na mitumbwi na usafiri baharini. Waandishi wengi wa Kiarabu wanasisitiza kuhusu Wazanj kuwa ni walaji wa samaki na kuongeza kuwa kwa kufanya hivyo meno yao yalionekana kuwa makali sana. Katika pwani watu waliendesha shughuli za uvuvi kikamilifu lakini ni sehemu chache ambazo zinatajwa kuwa shughuli ya aina hii ilikuwa ndiyo kazi kuu ya kujipatia kipato. Kwa mfano, huko Malindi wakazi wake walisafirisha nje sehemu ya samaki waliowavua. Katika baadhi ya visiwa, watu walikusanya kombe, konokono, n.k. kwa ajili ya kutengeneza mapambo lakini si kwa chakula. Katika mji wa Sofala watu walizamia baharini kutafuta lulu.

Japokuwa uundaji wa mitumbwi na usafiri wa majini ni vitu viwili ambavyo haviwezi kutenganishwa, waandishi wa Kiarabu hawasemi chochote kuhusu kipengele hiki cha hali ya maisha ya Waswahili. Buzurg ibn Shahriyar ndiye pekee anayeitaja mitumbwi mingi (*zawarik*) ambayo ilizunguka meli za Waarabu karibu ya pwani ya Sofala. Mwandishi huyohuyo ameandika kuwa kati ya manahodha wa meli katika Bahari ya Hindi walikuwemo Wazanj; hii inaonyesha kuwa Wabantu wa mashariki walikuwa na ujuzi si tu wa kusafiri pwani bali pia na ule wa kuabiri baharini mbali na pwani. Matumizi ya mtumbwi uliojulikana kama *dau la mtepe* katika karne ya kwanza kwenye pwani ya Benadir na sehemu ambayo hivi sasa inajulikana kama pwani ya Tanzania yameelezwa wazi katika *Periplus*. Mtumbwi ulioshonwa (*mtepe*) na ule mtumbwi mdogo zaidi, *dau la mtepe*, imekuwa ikitumiwa katika kusafiri baharini kwa muda mrefu, ingawa hivi sasa imepotea, isipokuwa kwa mifano michache ambavyo ipo katika makumbusho. Asili ya mitumbwi hii inatatanisha. Kiisimu, ingeonekana kuwa asili ya *mtepe* ilikuwa Afrika Mashariki lakini muundo na mjengo wake unaonyesha kuwa *mtepe* ulifanana na mtumbwi wa Kihindi, *mtepe* ukiwa umegeuzwa kidogo ili ufanane na muundo wa Kiarabu-Kiajemi.

Wakati kuna uhakika kwamba kulikuwepo na ufugaji Kaskazini mwa mto Juba tokea zamani, hali ya mambo ilivyo huko kusini mwa mto haifahamiki sana. Kwa upande mmoja, al-Masudi anatoa taarifa ya kutumika kwa ng'ombe na Wazanj kwa inadhumuni ya kivita, kwa

mfano maksai mwenye shogi na hatamu, wakati ambapo Buzurg anataja kondoo na wanyama wengine wafugwao. Kwa upande mwingine, al-Idrisi anasisitiza kutokuwepo kwa wanyama wabebao mizigo au ng'omhe wafugwao na watu katika pwani ya Afrika Mashariki; na waandishi wa Kiarabu vilevile hawasemi chochote kuhusu suala hili la ufugaji. Kama inavyofahamika, sehemu za pwani ya Afrika Mashariki hivi sasa zimejaa mbung'o na hivyo kufanya mazingira yasiwe ya kufaa. Hii haina maana kwamba hakuna hata sehemu moja ambayo ilikuwa haina mbung'o hapo zamani kuwezesha ufugaji ufanyike.

Ingawa uwindaji ulikuwa ni sehemu ya uchumi, kuna ushahidi mdogo sana kuhusu jambo hilo. Waandishi wa Kiarabu walivutiwa zaidi na uwindaji wa tembo, wakati kulikuwa na wanyama wengine waliowindwa kama vile chui, simba na nyani. Wanyama wengi waliuawa kwa madhumuni ya biashara ya nje (pembe za tembo, ngozi) na ingawa hakikutajwa chochote kuhusu uwindaji uliofanywa kwa ajili ya chakula, ni dhahiri kwamba nyama ya wanyama waliouawa (tembo) iliwa.

Kati ya madini, hapana shaka dhahahu ndiyo iliyowavutia waandishi wa Kiarabu; na Sofala ndiyo sehemu iliyochukuliwa kama mojawapo ya maeneo maarufu yenye dhahabu nyingi ambayo yamepata kufahamika ulimwenguni kote. Ingawa al-Idrisi aliandika kuhusu miji ya pwani ya Jasta na Daghuta (ambayo bado haijabainishwa lakini inafikiwa kuwepo mahali fulani katika pwani ya Msumbiji) kama sehemu zilikopatikana dhahabu, ni dhahiri kutokana na vyanzo vyote vya maandishi kuwa machimbo makubwa ya dhahabu yalikuwa katika sehemu za bara ya nchi ya Sofala, na miji ya pwani ilikuwa kama bandari tu za kusafirishia bidhaa hizo. Al-Biruni anaeleza kuwa dhahabu katika nchi ya Sofala ilipatikana katika namna ya nafaka. Aina kama hiyo ya dhahabu imegunduliwa katika machimbo ya kiakiolojia ya Zimbabwe.

Ushahidi mkubwa wa uchimbaji wa madini ya chuma umetolewa na al-Idrisi, ambaye alieleza kuwa vituo vikuu vya uzalishaji chuma vilikuwa Malindi na Mombasa upande wa Kaskazini na Jantama na Dandama katika upande wa kusini. Chuma ni mojawapo ya bidhaa muhimu zilizosafirishwa nje ya nchi ya sehemu hizi na madini hayo yalikuwa ndio tegemeo kuu la mapato. Ingawaje hakuna sababu ya kutilia mashaka ukweli wa al-Idrisi, lakini maelezo yake yanaleta matatizo kwa kuwa hakuna matanuri makubwa ya kuyeyushia chuma ambayo yamepatikana karibu na Mombasa na Malindi. Utafiti zaidi wa kiakiolojia unahitajika katika kufafanua tatizo hili muhimu.

### *Shughuli za Kibiashara*

Pwani ya Mashariki ni mojawapo ya maeneo machache kusini ya jangwa la Sahara yaliyoanza mapema uhusiano wa muda mrefu wa biashara na sehemu nyingine za dunia. Kuanzishwa kwa soko lililokuwa linapanuka katika nchi za Kiislamu kulileta uwezekano mpya wa biashara ya kusafirisha nje bidhaa za miji ya pwani. Kutokana na shughuli hizi za biashara, sio tu kwamba biashara ilipanuka bali pia bidhaa nyingine mpya ziliongezewa katika zile za asili na kwa hivyo hali hiyo ikawa imechangia katika kuifanyia miji ya pwani imakinikie biashara za aina mbalimbali. Katika karne ya tisa na ya kumi, vituo kadhaa vya biashara vya pwani kama vile Mogadishu, Marka, Brava, Mombasa, Manda na Unguja Ukuu, vilianzishwa na kupanuliwa. Hata hivyo, kabla ya karne ya kumi na moja, inaelekea miji peke yake iliyokuwa maarufu ilikuwa Manda katika visiwa vya Lamu na Kanbalu (Pemba). Miji mingine ilipata umaarufu katika siku za baadaye tu. Bidhaa za

biashara zilizowavutia wageni katika miji ya pwani zilikuwa nyingi na za aina mbalimbali, lakini muhimu zaidi zilikuwa pembe za ndovu, magamba ya kobe, gundi, ubani, viungo, dhahabu, chuma, ngozi za wanyama na watumwa.

Baadhi ya bidhaa hizi zilifika China mapema zaidi: ambari, mafuta ya storaksi, magamba ya kobe, damu ya nyoka (mchanganyiko wa *Dracanea schizantha* na *D. scinnabari*), na 'aloe' (utomvu wa mti). Kumbukumbu za Wachina pia zinataja kuwa wakazi weusi kutoka Kuumr Zangi (Zanzibar) walishawishiwa kwa chakula na kisha wakakamatwa. Waarabu kutoka Oman pia waliwashawishi watoto kwa kuwapa tende kisha wakawachukua na kuwaingiza katika utumwa. Hadithi inayojulikana sana iliyosimuliwa na Buzurg ibn Shahriyar kuhusu kumteka nyara mfalme wa Zanj inaonyesha aina nyingine ya kuwapata watumwa.

Kwa hivyo tunakuja kwenye tatizo la biashara ya watumwa. Hakuna ushahidi wa moja kwa moja katika vyanzo vya maandishi kati ya karne ya saba na karne ya kumi na mbili kuhusu biashara ya watumwa katika pwani ya Afrika Mashariki. Matukio yaliyotajwa yanaonyesha kuwa watumwa walipatikana kwa kukamatwa au kuwaiba wenyeji kuliko kuwanunua. Njia hii haikufaa tena hapo baadaye na iliweza kutumika mara chache na hivyo ingewezesha kupatikana kwa idadi ndogo ya watumwa. Kuendelea kutumika kwake kuliambsha chuki kwa watu wa pwani na ilikuwa na athari isiyofaa katika maendeleo ya uhusiano wa kawaida na kibiashara.

Kwa upande mwingine, uajiri wa watu wengi waliojulikana kama watumwa wa Zanj katika kazi za umwagiliaji maji katika Irak ya chini ambao, katika karne ya tisa, ulisababisha mgomo wa watumwa ujulikanao sana, unaonyesha kuwa kulikuwa na usafirishaji wa mara kwa mara wa watumwa kutoka Afrika Mashariki hadi nchi za Kiislamu<sup>55</sup>.

Mkinzano huu ulio dhahiri unaweza kufafanuliwa kwa maelezo: ingawa watumwa weusi kusini mwa Irak walikuwa ni watu kutoka sehemu tofauti, tuseme kutoka Ethiopia, pembe ya Afrika na sehemu nyingine za Afrika, hata kama kulikuwa na kiasi kidogo cha watu wa Afrika Mashariki, kwa sababu zisizo dhahiri, kwa pamoja waliitwa 'Wazanji.' Hii haina maana kuwa hakukuwa kabisa na biashara kama hiyo, lakini kiasi chake hakikuwa kikubwa; kwani kiasi hicho kingekuwa kikubwa jambo hilo litudhahiri katika kumbukumbu za maandishi wa Kiarabu ambao walikuwa wakitoa maelezo ya kina ya bidhaa zote zilizoingizwa au kupelekwa nje ya nchi. Lakini katika maelezo yao hayo swala la watumwa halijitokezi.

Usafirishaji nje wa dhahabu kutoka sehemu za kusini ulianza katika karne ya kumi, lakini al-Idrisi katika karne ya kumi na mbili alidhani kwamba chuma ndiyo iliyokuwa bidhaa kuu iliyosafirishwa nje na miji mingi ya pwani. Pwani ya Benadir ilijulikana kwa usafirishaji wake wa ubani, manukato na mafuta mazuri kama vile 'balsam' na manemane.

Kwa upande wa bidhaa zilizotoka nje, bidhaa kuu zilizotajwa katika maandishi ya Waarabu na Wachina zilikuwa vyombo vya udongo (vya Kiislamu na Kichina), nguo, shanga na kioo. Hadi kufikia mwaka 1100, wahamiaji kutoka kusini mwa Asia ambao waliwasili Kaskazini mwa Bukumi na Ngazija karne chache mapema walikuwa wakisafirisha vyombo vya aina ya sabuniwiwe kwenda Kilwa, Manda na kwingineko.

Bidhaa ya kwanza kabisa kati ya vifaa vya udongo iliyoagizwa kutoka nje ni ile ya vyombo vya Kiislamu vya udongo vyenye mapambo ya rangirangi, ambavyo vimepakwa rangi nyeupe katika sehemu za pembeni. Bidhaa kuu zilizoagizwa, hasa tukichukulia mfano wa Gedi, zilikuwa vyombo ya udongo vyenye rangi za bluu na kijani, seladoni ya rangi ya

njano na nyeusi na vyombo vya udongo vya rangi ya buluu na nyeupe kutoka China. Katika karne ya kumi na moja, bidhaa zilizosafirishwa nje kutoka China zilikuwa dhahabu, fedha, shaba, hariri na vyombo vya udongo. Sarafu za Kichina zimepatikana katika sehemu zote za pwani na ziliendelea kufika Afrika Mashariki hadi karne ya kumi na tatu.

Suala la uhusiano wa mapema baina ya miji ya pwani na bara bado limebaki kuwa tatizo muhimu. Ni jambo lisiloeleweka kwamba hakukuwa na mashirikiano kabisa, lakini hakuna ushahidi wowote uliopatikana. Kwa hali kama hii uchunguzi wa kiakiolojia unahitajika kupata ukweli wa mambo. Sehemu pekee ambayo ilikuwa ikifanya biashara na bara inaonekana ilikuwa ni pwani ya Sofala; dhahabu ambayo ilikuwa inasafirishwa nje ya nchi hii ilikuwa inatoka nchi ambayo hivi sasa inaitwa Zimbabwe. Hata hivyo itakuwa mapema mno kuhitimisha kwamba watu wa pwani walijaribu kuingia mbali bara mapema kiasi hiki.

Pengine hakukuwapo na biashara ya masafa marefu kama neno lenyewe linavyoamaanisha. Tunachoweza kufikiria zaidi ni kwamba bidhaa zilizotoka mbali sana zilikuwa zikihadilishwa mali kwa mali kutoka watu wa jamii moja hadi jamii nyingine kuliko kufanywa katika misafara kama ilivyokuwa katika karne ya kumi na tisa. Uhusiano huu wa kibiashara haukuacha ushahidi wowote wa kudumu, vyombo vya udongo vilivyotengenezwa pwani havifanani na vile vya bara.

### Hitimisho

Katika kipindi hiki tunachokijadili, pwani ya Mashariki ilishuhudia kuanza kwa michakato mbalimbali ya kihistoria ambayo ilikuja hutumiwa kikamilifu baada tu ya karne ya kumi na mbili. Pengine ilikuwa ni wakati huu ambapo misingi ya kitamaduni ya Waafrika iliwekwa, misingi ambayo kwayo utajiri wa utamaduni wa Waswahili ulijengeka baadaye. Maendeleo ya kisiasa na ya kihistoria ya watu wa pwani wanaozungumza lugha za Kibantu yalianza kuathiriwa na kuzuka kwa biashara ya kimataifa katika Bahari ya Hindi. Mwanzoni, athari hiyo ilionekana zaidi katika uwanja wa kiuchumi wakati baadhi ya miji ya pwani ilipojihusisha zaidi na biashara ya nje; polepole, siasa, utamaduni na dini vilienezwa na kanuni zilizoletwa na wahamiaji kutoka katika nchi za Kiislami. Eneo la kwanza lililotokea kupata athari za kigeni lilikuwa katika sehemu ya Kaskazini mwa mto Juba. Kutoka pale, katika karne zilizofuata, mawimbi mapya ya wahamiaji yalibeba vipengee vya utamaduni mchanganyiko kuelekea kuaini. Wakati huohuo, wahamiaji wote, ambao hawakuwa wengi, walipitia katika mchakato wa kufanywa Wabantu. Matokeo muhimu ya mchakato huu wa kubadilishana na kuoana baina ya watu kutoka nje na wenyeji ni lugha ya Kiswahili na utamaduni wa Waswahili ambao uliunganisha vipengee vya Kiafrika na vile vyenye asili ya nchi za Mashariki.

---

### *Miguro ya Watu*

Kwa jumla karne ya saba hadi ya kumi na moja zinaonekana kuwa ni kipindi cha uimarishaji wa mielekeo iliyowekwa awali katika bara la Afrika Mashariki. Hii haina maana kwamba kipindi hiki hakikuwa na mabadiliko; ueneaji upya wa mbari ulitokea, ukiibadilisha ramani ya kiisimu na kuweka changamoto mpya zilizopaswa kushughulikiwa na jumua zilizokuwepo.

Makundi makubwa mawili ya watu yaliyokuwepo mwanzoni mwa karne ya saba yalikuwa ya Wakushi wa Kusini na Wabantu. Makundi ya Wasudan wa Kati, Wanilo na Wakhoisani ndiyo yalikuwa muhimu ijapokuwa hayakuwa na watu wengi walioshiriki katika matukio ya katikati mwa kikwi cha kwanza.

Wakushi wa Kusini wa kwanza walioishi Kaskazini mwa Kenya katika kikwi cha tatu kabla ya enzi yetu wanaweza kuchukuliwa kuwa ndio waanzilishi wa kile kitwacho mapokeo ya wafugaji wa Kiniolithi wa eneo la Savana la Afrika Mashariki. Tokea walipohamia kwenye eneo hilo, Wakushi wa Kusini walifuga ng'ombe na mifugo mingine michache ikiwa ni pamoja na punda, lakini pia walilima nafaka, wakitumia mbinu za umwagiliaji maji na samadi katika kuongeza mapato yao.

Wakushi wa Kusini wa kikwi cha kwanza cha enzi yetu walitofautiana sana. Ukingoni mwa mto Tana na katika sehemu za ndani karibu na pwani ya Kenya kuliishi Wadahalo, nusu wakulima na nusu waokotezaji chakula na wawindaji. Kundi lingine linalokumbukwa katika mapokeo simulizi kwa jina la Wambisha liliishi katika milima ya Taita. Katika Eneo linalozunguka mlima Kilimanjaro na kuelekea kusini hadi katika mbuga za Wamasai waliishi wasemaji wa Kiasa cha Kale; na katika sehemu za kati za Tanzania yaliishi makundi ya zamani yaliyohusiana ya Wakwadza wa Kale na Wairinga. Wengi kati ya Wakushi wa Kusini wa Bonde la Ufa wa karne ya saba huenda walikuwa ni wafugaji. Wengine, hasa wale walio katika eneo linalozunguka mlima Kilimanjaro, nailima ya Taita na kingo za Bonde la Ufa walitumia muda wao mwingi katika kilimo.

Jumua nyingine muhimu za Wakushi wa Kusini wa kipindi hicho zilizungunza lugha za Kimbugu. Kundi moja la Wakushi wa Kirinyaga liliwatangulia wakazi wa Kibantu wa mlima Kenya, ambapo kundi la pili la Kimbugu, Wamaa wa Kale, lilikuwa likiishi Kaskazini Mashariki mwa Tanzania, ambako hali ya kiekoloji iliruhusu ufugaji wa ng'ombe wengi.

Upantakaji wa Wakushi wa Kusini katika vikwi vitatu vya mwisho kabla ya enzi yetu ulikwihazijumuisha kikamilifu jumua nyingi za Wakhoisan. Jamii nyingine zimeendelea kuishi kama wawindaji-waokotezaji, wakushi pamoja na Wakushi wazalishaji chakula, lakini wakisema lugha za wakazi waliokuwa wanaishi hapo. Hata hivyo, katika mipaka ya maeneo ya Wakushi wa





Kusini ya Tanzania ya kati, makundi mawili ya Wakhoisan yameweza kushikilia na kuendeleza lugha zao hadi hivi sasa. Wahadza waliendelea kuishi kama kikundi karibu na ziwa Eyasi katika maeneo ambayo hayakufaa sana kwa kilimo na pia hayakuwa mwafaka kwa ufugaji kwa sababu ya kuwepo na mbug'o wengi. Lakini pengine hata nao walikuwa wameathiriwa vikubwa kiutamaduni na watu jirani wa Bonde la Ufa mnamo karne ya saba ya enzi yetu. Jumua nyingine ya Wasandawe iliishi kwa kilimo na hivyo kupata msingi wa kiuchumi wa kushindana na wazalishaji chakula wengine. Mwanzo wa Wasandawe kuingia katika uzalishaji chakula unaweza kuwa mapema katika kipindi cha karne ya saba hadi ya kumi na moja.

Changamoto ya mwanzo dhidi ya umaarufu wa Wakushi wa Kusini ilitoka, kwa Wanilo wa Kusini ambao walianza kuhama kuelekea kusini, nje ya maeneo ya mipaka ya Uganda-Sudan katikati mwa kikwi cha kwanza kabla ya enzi ya Ukristo; na wanatambuliwa kama watu walioleta mapokeo ya kiakiolojia ya Ementeita. Hadi kufikia karne ya saba, kulikwishatokea vizazi viwili vya Wanilo wa awali wa Kusini, Wakalenjini wa kwanza walitokea Kaskazini mwa Mau, na Watato ambao ndio chimbuko la Wadadoga, kusini mwa milima hiyo.

Lakini changamoto kubwa zaidi ililetwa na ueneaji wa Wabantu katika Afrika Mashariki. Baadhi ya wahamiaji wapya walikwenda kwenye maeneo ya pwani ya kusini mwa Kenya na maeneo mengine ya milima ya Kaskazini-mashariki mwa Tanzania, hasa kwenye safu za milima ya Upare na Ngulu. Hawa ndio walioleta ufinyanzi wa Kwale.

Awamu ya pili ya miguro ya awali ya Wabantu katika pwani ya Afrika Mashariki ilikuwa ni ile ya watu wa pwani ya Kaskazini-mashariki, pengine kufikia au kabla ya katikati mwa kikwi cha kwanza cha enzi ya Ukristo. Hadi kufikia karne ya saba, pengine jumua za pwani ya Kaskazini mashariki zilienea kutoka kwenye lango la mto Tana hadi bara, karibu na Dar es Salaam ya leo nchini Tanzania.

Makazi kadhaa ya Wabantu yaliishia kusini mwa Afrika Mashariki. Watu wa Kilombero walikwisha-tamakani katika au jirani na bonde la Kilombero wengine wakatamakani kusini zaidi, katika miinuko ya Songea na kusini mwa Ruvuma. Makazi mengine yalifanyika katika ncha ya Kaskazini ya Ziwa Nyasa.

Makazi ya mwisho ya Wabantu wa awali yaliyojulikana katika Afrika Mashariki yalikuwa kandokando mwa ufuko wa Maghribi wa Ziwa Viktoria. Makazi ya ghuba ya Wami, yaliyokaliwa na watengenezaji wa vyombo vya Urewe pengine yalikuwa ndiyo kituo ambamo zilianza jamii za baadaye za Kiluyia-Gisu. Makazi ya pili, yaliyokaliwa na jamii za watengenezaji wa vyombo vya udongo vya Kilelesu huenda yalidumu kwa muda mfupi tu.

Hivyo, hadi karne ya saba jumua za wakulima wa Kibantu ziliweza kupatikana katika sehemu mbalimbali na kugawanyika katika makundi mbalimbali yasiyo na idadi sawa ya watu. Sifa jumuiya ya mgawanyiko huu ni uwiano wa makazi ya Wabantu na maeneo yenye zaidi ya milimita za mvua kati ya 900 na 1000 kwa mwaka. Inaelekea Wabantu wa awali walihamia kwenye maeneo yaliyofanana na ya kule walikotoka: maeneo yenye misitu yanayopata mvua ya kutosha kwa kilimo cha viazi vikuu. Kilichoyafanya maeneo yenye unyevunyevu yavutie zaidi ni kuwa inawezekana kwamba yalikuwa hayajatumia kabisa au yalikuwa yametumiwa kidogo na wazalishaji vyakula wa Kikushi wa Kusini na Wanilo. Kwenye pwani ya Afrika Mashariki maeneo mengi yalikuwa na mbug'o na hivyo hayakuwavutia wafugaji wa ng'ombe wa Wakushi na Wanilo. Kusini mwa Tanzania, makazi ya Wabantu yalikuwa katika maeneo ambayo halikadhalika hayakufaa kwa ufugaji, na hivyo yakawa hayajaingiliwa na ueneaji wa Wakushi wa Kusini. Katika mengi ya maeneo haya makundi ya wawindaji wa waokotezaji yalikuwepo, lakini, kama waokotezaji vyakula, walikuwa katika hali ya kutonufaika katika kushindania rasimili na wazalishaji vyakula waliokuwa

wakiingia katika eneo hilo. Wawindaji na waokotezaji pengine walimezwa na kuingizwa katika jumua za Kibantu zilizojidukiza kabla ya kupita karne nyingi isipokuwa tu katika misitu ya nyanda za juu yenye baridi.

Tofauti moja inayojitokeza katika ruwaza ya makazi ya Wabantu ilikuwa ni uhamiaji wa watengenezaji wa vyombo vya Lelesu katika sehemu kame za katikati mwa Tanzania. Kama jamii hii iliweza kuishi kama jamii pekee katika vipindi vilivyofuata, ilipaswa kufanya mabadiliko ya haraka na makubwa ya kuweza kujikimu kufuatana na mazingira, ikibadilika kabisa na kujikita katika kilimo cha nafaka. Hakuna ushahidi wa kuwahusisha Walelesu na jamii yoyote iliyofuata na iliyokuwa inazungumza lugha ya Kibantu; hivyo historia hii yenye utata haiwezi kuzingatiwa kwa hivi sasa.

Bonde kubwa linaloanzia mto Tana hadi bonde la Shebelle nchini Somalia, tayari lilikuwa makazi ya Wasomali na Warendille kwa karne kadhaa. Ueneaji wao katika maeneo haya ulifanyika kwa kuwaathiri si tu wawindaji-waokotezaji wenye lugha isiyo na msimamo wa uhakika, bali pia jumua za wafugaji wa Kidahalo. Lakini, hadi karne ya saba, maeneo ya mito Shebelle na Juba yalikuwa na watu waliokuwa wanazungumza Kisomali.

Yakiwa ni maeneo makame kabisa ya Afrika ya Mashariki, maeneo ya Kaskazini-mashariki, hadi karne ya saba, yamekuwa kitovu cha kutokea kwa aina mpya ya ufugaji ambayo ngamia walichukuwa nafasi ya ng'ombe kama chakula kikuu cha nyama. Pamoja na hayo yote kulikuwa pia na maendeleo mapya ya kijamii - ruwaza ya maisha ya kinomadi - ambayo hayakuwepo katika sehemu za kusini zaidi za Afrika Mashariki. Mabadiliko haya yalifanyika zaidi miongoni mwa Warendille wa awali ambao walikuwa wakiishi katika maeneo makame zaidi na miongoni mwa baadhi ya wazungunzaji wa lugha ya Kisomali. Wengine waliishi katika sehemu zenye maji ambapo ng'ombe wangeweza kujichunga wenyewe pamoja na ngamia; kwa jamii za kikulima ukingoni mwa mito ya Juba na Shebelle, ng'ombe walikuwa wanyama wenye manufaa zaidi.

### *Michakato ya Kimbari*

Kudumu kwa mielekeo iliyokwishaanzishwa kati ya karne ya saba hadi ya kumi na moja katika karne sita za kwanza za zama zetu kunaweza kuelezwa katika hali mbalimbali.

Katika mtazamo wa kijiografia, kwa sehemu kubwa jamii mbalimbali zinazozungumza lugha za Kibantu zilibakia katika mipaka ya kiekolojia ya maeneo ya makazi yao ya awali; ingawaje ziliendelea kutumia kikamilifu utajiri uliomo katika maeneo hayo labda kwa kufyeka zaidi misitu na kutapakaa katika maeneo yanayofaa kulimwa nje ya maeneo ya nyanda za juu. Ushahidi wa kiisimu pia umeonyesha ongezeko la kuwaingiza katika utamaduni wa Kibantu watu wasiozungumza lugha za Kibantu katika maeneo kadhaa.

Hitilafu na tofauti baina ya jamii za Kibantu pia ziliendelea kukua. Mwanzoni mwa enzi yetu, Wabantu wote wa Afrika Mashariki walizungumza lahaja za lugha moja ya mashariki mwa Afrika. Hadi kufikia karne ya kumi na moja, mchakato wa kutofautiana ulikwishaendelea hadi kuwezesha idadi kubwa ya lugha kubainishwa: lugha ya pwani ya Kaskazini mashariki yenye makundi matatu ya lahaja (Seuta, Sabaki na Ruvu); lugha ya Kitakama ya Wabantu wanaoishi kusini mwa Ziwa Viktoria; lugha mame ya Kigusii-Kikurya ya mwambao wa kusini-mashariki ya ziwa; lugha mame ya Kiluyia-Kigisu ya mwambao wa Kaskazini-mashariki ya ziwa: mame - Kithagisu ambayo pengine ni lugha ya watengenezaji wa vyombo vya Gatung'ang'a katika Mlima Kenya; mame Kitaita-Kichaga inayozungunzwa na waumbaji wa vyombo vya Maore Kaskazini mwa Upare, Kilimanjaro na Taita; na lugha nyingi za kusini zaidi mwa Tanzania. Mgawanyiko wa kwanza wa

kundi la Wataita-Wachaga ulihusu mguro wa kikundi kidogo cha watu katika milima ya Taita mwishoni mwa kikwi cha kwanza; lahaja yao ya Kitaita-Kichaga ikakua kuwa lugha ya sasa ya Kisaghala. Kipindi kilichofuatia cha mguro kutoka Upare ya Kaskazini hadi Taita kilileta lahaja ya pili ya Kitaita-Kichaga ambayo ni chanzo cha Kidawida cha sasa katika eneo hilo. Wakazi waliobaki wa Kitaita-Kichaga wa Upare Kaskazini wakazaa mame-Kichaga, lugha ambayo vizazi vyake vilikuwa kitovu cha mpangilio mpya wa kiuchumi na kijamii wa mkoa wa Kilimanjaro katika karne zilizofuata.

Nyika na nyanda zilizoimuka zilikalwiwa na wazungumzaji wa lugha za Kinilo na Kikushi. Jamii ya Wadadoga pengine ilijitokeza katika karne hizi kama jamii iliyopata riziki kutokana na ufugaji katika maeneo ya kutoka upande wa Maghribi wa Bonde la Ufa la kusini mwa Kenya hadi Kaskazini na kati ya mabonde ya Wamasai wa Tanzania. Katika eneo la kati la Maasai, Wadadoga waliishi pamoja na jumua ya wawindaji- waokotezaji ambao walidumisha lugha ya Kiasa hadi wakati huu. Jamii moja ya Wabantu iliyozaa Wasonjo inaonyesha kuwa ilipata sehemu nzuri katikati mwa eneo linalozungumza lugha ya Kitato kwani lugha ya Kisonjo ya sasa ina maneno ya kigeni yasemekanayo kuwa yalitokana na maingiliano yao ya awali na Wadadoga.

Jamii ya mame-Kalenjini ilikuwa ni mojawapo ya Wanilo wa kusini ambao waliishi Kaskazini mwa Mau. Kukua kwa jamii karne nyingi kabla ya mwaka 1000 kwa muda mrefu kuliwajumuisha pia Wakushi wa Kusini. Inaonyesha kuwa kipengee muhimu cha Kibantu pia kiliingizwa kupitia kwa wanaume waliokuwa wanazungumza lugha ya Kikalenjini waliowao wanawake waliokuwa wanazungumza lugha ya awali ya Kiluyia-Kigisu. Kuanzia takriban mwaka 1000 wazungumzaji wa Mame-Kalenjini waliendelea kuenea katika eneo kubwa na jipya, kutoka Mlima Elgon Kaskazini Maghribi hadi safu ya Nyandarua ya kusini na maeneo ya Bonde la Ufa ya kati na kusini mwa Kenya. Ueneaji mwingine wa Wakalenjini ulifanyika Maghribi hadi katika sehemu ambazo hivi leo zinakaliwa na watu wanaozungumza Kiluyia, kusini mwa Mlima Elgon, ambako hapo awali ziliishi jumua za Wabantu na Wakushi.

Tukio kubwa lililokuwa tofauti na mielekeo hii ni kutokea kwa kipengee kipya cha kimbari katika eneo la kati la Afrika Mashariki la Maa-Ongamo. Kutoka katika sehemu yao ya awali karibu na milima ya Lotuko ya kusini zaidi mwa Sudan, jumua ya mame-Maa-Ongamo ilisambaa kusini kwenye maeneo ya Baringo na Laikipia upande wa Kaskazini na Kaskazini-Maghribi mwa Mlima Kenya mnamo karne ya nane ya enzi yetu. Ueneaji wao wa awali kuelekea kusini uliwajumuisha Wabaz wengi, Wakushi wa Mashariki wa uwanda wa chini ambao hapo awali walilikalia bonde la Turkana. Kusini mwa Baringo na Laikipia, jumua zilizoishi sehemu hizo hapo awali pengine zilikuwa zinazungumza lugha za Wanilo na Wakushi wa kusini. Wakitokea katika eneo la Mlima Kenya walikokuwa wakiishi, wazungumzaji wa mame-Maa-Ongamo waligawanyika katika makundi mawili: Wamaa halisi waliishi katika bonde la Baringo na Laikipia na waliendelea kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na jirani zao wa Wakalenjini wa kusini na Maghribi; Waongamo wa Kale walienea kusini na kuishi katika nyanda za Milima ya Upare na Kilimanjaro.

### *Shughuli za kiuchumi*

Katika uchumi, ruwaza ya shughuli iliyokwishawekwa katika kipindi kilichotangulia ilikwamisha mielekeo ya mabadiliko.

Kuliendelea kuwepo uhusiano mkubwa baina ya mbari na aina ya uzalishaji chakula. Wanilo wa kusini walihamia Maghribi mwa Kenya miaka elfu moja kabla, wakiwa ni wafugaji na pia kwa kiasi fulani wakilima nafaka. Mikakati ya kujikimu kwao haikuweza kubadilika hata ilipofika

mwishoni mwa mwaka 1000. Katika hali hiyo ya uchumi ni dhahiri kwamba Wanilo waligombea ardhi na Wakushi wa kusini ambao walikuwa wafugaji. Kufanikiwa kwa ueneaji wa Wanilo wa kusini mara nyingi kulikuwa na maana ya kumezwa kwa mbari za Wakushi zilizokuwa zikiishi sehemu hiyo.

Jamii zilizokuwa zinazungumza lugha za Kibantu zilikuwa zinaendesha kilimo cha upandaji mimea kwa sababu mazao waliyolima hayakutokana na mbegu bali sehemu ya mimea wenyewe ambao hupandwa ardhini. Pia walipanda mbegu za mazao mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwele na, katika maeneo ya milima, ulezi; na wakati mwingine walifuga ng'ombe. Hata hivyo, hadi mwishoni mwa kikwi cha kwanza, aina mbalimbali za viazi vikuu ziliendelea kuwa chanzo cha chakula kikuu kwa Wabantu karibu kila mahali. Mazao ya awali kabisa ya bara la kusini mashariki la Asia ikiwa ni pamoja na magimbi ya Kiasia, 'taro', na ndizi yatakuwa yalipendelewa sana kuliwa na jamii zilizozunguma lugha za Kibantu; sababu kuu ikiwa ni hali ya hewa na kuzoea kwao kilimo cha kupanda mimea.

Kulikuwepo na vighairi kadhaa vya mieleleko hii. Wasonjo, kwa kiasi kikubwa walitumia kilimo cha umwagiliaji maji na mboji katika kulima aina mbalimbali za vyakula katika ardhi finyu. Aina ya kilimo waliyoitumia pengine ilikuwa ni ile iliyopendelewa na Wakushi wa Kusini na kufuata kwao aina hiyo ya maisha kunaweza kurudi nyuma hadi miaka 1000. Katika baadhi ya sehemu za Tanzania katika kipindi cha miaka 600-1100, ziliweza kupatikana jamii za Kibantu ambazo zilitegemea kwa kiasi kikubwa nafaka na mazao mengine yanayotokana na mbegu kuliko viazi vikuu. Mojawapo ya jamii hizo ilikuwa ni ile ya Ruvu ya Maghribi ambayo ilihamia katika sehemu zilizoinuka na kame, hasa eneo la Ukagulu lililofaa kwa ufugaji na ulimaji wa mazao ya nafaka.

Maarifa kuhusu ulimaji wa migomba yalienea vizuri sehemu ya bara katika nusu ya pili ya kikwi cha kwanza kupitia ukanda wa Upare hadi Mlima Kenya. Ilikuwa ni katika milima ya Upare ambapo kipindi komavu cha mpito cha kilimo cha upandikizaji katika nyanda za juu kilitokea mwanzoni mwa kikwi hicho. Kundi la Wadawida, ambalo lilitoka katika mame-Wachaga na kuihama Upare Kaskazini na kwenda kuishi katika milima ya Taita Jabda kwenye karne ya kumi au kumi na moja liliendelea kutumia viazi vikuu kama zao kuu.

Mwelekeo wa kutumia teknolojia ya zana za chuma badala ya zile za mawe uliendelea katika kipindi cha karne ya saba hadi karne ya kumi na moja. Yaelekea metali ziliingia katika bara la Afrika Mashariki kutoka pande mbili mwanzoni mwa kipindi hiki, kutokea Maghribi au Kaskazini Maghribi na kutokea pwani ya mashariki. Jamii za Kibantu mara nyingi zilikuwa ni pamoja na wahunzi na utaalamu wa uhunzi unaonyesha kuenea mapema zaidi Kaskazini mwa Mlima Elgon hadi maeneo ya Wanilo wa kusini Maghribi mwa Bonde la Ufa. Kaskazini mwa Tanzania, baadhi ya Wakushi wanaonekana kuwa walikifahamu chuma tangu kipindi cha ujio wa Wabantu. Kufahamu kwao metali inawezekana kumetokea pwani ya Bahari ya Hindi ambako wafanyabiashara kutoka Mashariki ya Karibu walikuwa wakifanya biashara ya kubadilisha chuma katika kipindi cha si zaidi ya karne ya kwanza au ya pili. Ni katika kipindi cha karne za nane na kumi ndipo ambapo utumiaji wa vifaa vya Kielmenteita ulipopotea, wakati ambao wahamiaji wanya wanaotumia chuma, Wamaa-Ongamo, walipotaka watu wafahamu kuwepo kwao. Hadi mwaka 1100 vifaa vya mawe vilikuwa vichache sana kila mahali katika sehemu ya bara ya Afrika Mashariki isipokuwa pengine kaulika sehemu kame ambapo wawindaji-waokotezaji walibaki kwa karne kadhaa zaidi.

Kwa wakati mwingi na mahali pengi kati ya mwaka 600 na 1100, biashara ilikuwa ni shughuli ambayo ilifanywa kufidia mahitaji machache. Ruwaza fulani ya mabadilishano iliyojitokeza mara kwa mara ilikuwepo: kwa mfano, usafirishaji nje wa madini ya obsidi kutoka katika maeneo ya Kenya ya kati ambako ilikuwa inatumiwa kutengeneza mabapa ya mawe ya Elmenteita hadi

mwishoni mwa karne za nane na tisa na biashara ya magamba ya kauri huko bara kutoka pwani ya mashariki. Lakini ubadilishanaji huo ulitoka kwenye jumua moja hadi jumua iliyo karibu bila ya ubebaji mizigo wa kwenda umbali mrefu na bila kuwepo masoko wala wafanyabiashara wa kudumu.

Uhunzi ndiyo taaluma moja pekee iliyokuwepo katika karne ya saba. Uhunzi haikuwa kazi iliyopatikana katika kila sehemu iliyoko bara ya Afrika Mashariki; hivyo jamii nyingi zilinunua chuma. Hii ina maana kwamba ni kwa kiasi kidogo sana waliweza kuyeyusha chuma na hata kukifua hadi baada ya karne zilizofuata.

Katika karne za nane na tisa, tofauti za ufinyanzi wa kimbari kwa kiasi fulani zilitoweka katika maeneo ya kati ya Kenya yaliyokaliwa na Wanilo wa kusini na wavamizi wa jumua za Wamaa-Ongamo. Baada ya hapo, aina moja tu ya ufinyanzi, ya vyombo vya Laneti, ilianza kutumika na makundi mengi yanayozungunza lugha za Kinilo. Ufinyanzi vyungu ulianza kuwa kazi maalum iliyofanywa na wawindaji-waokotezaji wa Ufa na Mau.

Yawezekana biashara ya ufinyanzi ilikuwepo pia kati ya Upare Kaskazini na Kilimanjaro, wakazi wakiwa ni jamii za Kibantu na pengine wanunuzi wakiwa Waasa wa Kale. Ufinyanzi vyungu Upareni miongoni mwa wawindaji wa Bonde la Ufa ulikuwa kazi ya muda na hivyo kuifanya hii kuwa kazi maalumu kusingesababisha kuanzishwa mara moja kwa masoko ya kudumu; bali kulivezesha kuanzishwa, katika maeneo kadhaa ya Afrika Mashariki ya kati, vituo maalum ambapo watu wangekwenda kupata bidhaa walizolutaji. Kati ya Kilimanjaro na Upare Kaskazini, eneo lililokuwa maarufu kwa chuma na vyungu, mchakato huo ungefikia hatua kubwa zaidi hadi kuanzishwa kwa masoko halisi ya kudumu ilipofikia mwanzoni mwa kikwi cha pili.

### *Taratibu za maisha kijamii*

Tabia ya jumla ya jamii za sehemu ya bara ya Afrika Mashariki kuanzia karne ya saba hadi ya kumi na moja ilikuwa ni kiwango kidogo cha maeneo ya makazi na ya kisiasa. Hapakuwepo na msingi wa kiuchumi wenye uwezo wa kubimili tawala kubwa.

Jamii za Wakushi wa kusini zilijengwa na koo nyingi zilizokuwa zikijitegemea kila moja ikiwa na kiongozi alyictambulika. Miongoni mwa wakazi wa Kibantu wa awali ruwaka ileile ya koo zilizoongozwa na machifu wa kurithi ilijitokeza. Uchifu wa ukoo kwa Wabantu ulikuwa ni wadhifa mkubwa wa kisiasa, ukiwa na majukumu katika maeneo mengi ya maisha ya jumua wakati ambapo kiongozi wa ukoo wa Kikushi kimsingi alihusika na ugawaji wa ardhi.

Miongoni mwa mame-Wachaga kulizuka nafasi mpya ya uchifu ambapo chifu hakuwa mtawala wa ukoo mmoja tu bali alitawala eneo lililokaliwa na watu wenye muungano wa koo tofauti. Hali hii inaonyesha kutokea wakati mmoja na ule wa kilimo eha upandikizaji katika sehemu za nyanda za juu. Inaweza kuchukuliwa kuwa mfumo huu wa kilimo cha upandikizaji uliwanufaisha Wachaga wa awali na hivyo kutoa msukumo wa kuenea kwa Wachaga. Wajibu wa chifu ulikuwa ni kuwatia katika kundi moja watu wa mbari mbalimbali na hivyo kuunda muungano wa koo mbalimbali.

Hata hivyo, kiwango kikubwa cha ushirikiano wa kisiasa na kijamii pengine kilifikiwa na Wanilo wa kusini na Wamaa-Ongamo. Vyombo vya marika vya jumua hizi viliwakusanya vijana wote kutoka nyumba za jirani katika eneo kubwa sana. Kwa kuwa katika makundi ya rika moja, vijana kutoka sehemu za mbali walipata misingi ya kushirikiana katika kuwavamia watu wengine wakiwa bado vijana na kuweza kulinda amani katika kukua kwao. Kuwa na vyombo vya aina hiyo pengine kunasaidia kuelezea kwa nini lugha ya Kinilo na utambulisho wake wa kimbari hapo baadaye vilivapiku Wakushi wa kusini. Kulipotokea kutoelewana au wakati yalipotokea matatizo ya

baa la njaa Wanilo walikuwa na kundi kubwa la watu ambalo lingeliweza kuwapa msaada waliouomba.

Kwa hali hii, kutokomea kwa utaratibu wa marika miongoni mwa Wabantu wengi wa Mashariki mwa Afrika pamoja na tohara kunakuwa ni jambo la kuvutia (kiutafiti). Katika maeneo ya bara, wakazi wa awali wa Kibantu waliwatahiri vijana wao wa kiume na kuwaweka katika makundi ya marika. Lakini jamii za Kibantu kusini mwa Tanzania (ambazo zilihifadhi utamaduni wa zamani ambao ulipotea katika sehemu za Kaskazini kama vile uhusiano wa kindugu kwa kufuata upande wa mama na uchifu wa ukoo), ziliacha kuwatia tohara na kuwaweka pamoja vijana wenye rika moja pengine mapema zaidi katika historia zao. Tohara iliendelea kuwepo pale tu zilipokuwepo jamii za jirani za Wakushi na Wanilo wa kusini ambao pia walikuwa na utamaduni huo. Wakati mwingine, athari hii ilikuwa na nguvu sana hasa katika kipindi cha kuanzia karne ya saba hadi ya kumi na moja. Mfano mmojawapo ni mifumo ya vizazi ya Wathagisu wa Mlima Kenya ambapo msukumo wa namna fulani kutoka kwa Wanilo wa kusini wakati wa mame-Wathagisu lazima uzingatiwe. Mfano wa pili dhahiri ni ule wa Wachaga ambao mawazo yao wa marika yanaonyesha mchango mkubwa wa Wamaa-Ongamo, pengine hasa kutoka kwa Waongamo wa Kale wakati wa kipindi cha mame-Wachaga mwanzoni mwa kikwi hiki. Kitu kinachoweza kuonyesha hapa ni kuwa, vikundi vya marika havikuhitajika sana katika sehemu za kusini ambako wawindaji na waokotezaji wachache tu ndio walikubali kutamakani kwa Wabantu. Hata hivyo Kaskazini zaidi, kuigiza mifumo ya Kinilo pengine kulitoa mbinu mpya zinazofaa za kuziingiza jamii zisizo za Kibantu katika jamii za Kibantu na za kukabiliana na shinikizo za kuenea upya kwa Wanilo mwishoni mwa kikwi cha kwanza na mwanzoni mwa kikwi cha pili.

### *Mifumo ya kidini*

Kati ya mifumo mikuu miwili ya kidini, watu wengi walifuata ama mfumo mmoja au mwingine.

Sehemu kubwa ya bara ya nchi ya Kenya na kusini hadi Tanzania ya kati kulikuwa na imani ya Mungu mmoja iliyoainishwa kisitari na anga. Katika dini hii, kuwepo kwa maovu kulieleweka kuwa kunatokana na uamuzi au adhabu ya Mungu. Habari za dini za watu waliokuwa wanazungumza Kikushi wakati mwingine ziliongezea imani kwa pepo wachache walioweza kuleta madhara, na baadhi ya Wakushi wa kusini mwa Ufa walikuwa na sitiari ya kimbingu iliyo tofauti, ikiunganisha uungu na jua kuliko anga kwa jumla. Aina hii ya dini iliyotokea hapo baadaye ilikuwa ikifuatwa hapo zamani kwa karne kadhaa na wahenga wa Kinilo wa Kusini wa Watato na Wakalenjini wa awali.

Katika nusu ya kusini ya sehemu ya bara la Afrika Mashariki, kulikuwepo na aina nyingine ya dini. Ikiwa imeenezwa na wakazi wa Kibantu, dini hii ilikuwa na kanuni za imani zilizoonyesha kuwepo kwa mungu muumbaji lakini mafundisho yake ya kidini yalielekezwa kwa mababu. Mara nyingi uovu ulihesabiwa kuwa na chanzo katika chuki na husuda ya binadamu; waganga wa jadi na walozi.

Sehemu ya kati ya bara la Afrika Mashariki, ambapo dini zote mbili zilifuatwa, mwelekeo wa miaka 2000 iliyopita ulikuwa ni katika kupatanisha vipengee vya falsafa mbili. Maghribi mwa Kenya, dhana ya mababu kuwa ni sehemu kuu ya kuabudia ilitoweka, pengine kutoka kwa Watuyia-Gisu wa awali kuelekea mashariki hadi kwa Wakalenjin wa awali katika zama zile, na dhana ya uchawi imekuwa ni sehemu ya maelezo ya Wakalenjini kuhusu uovu wa tangu mwishoni mwa kikwi cha kwanza. Kaskazini mwa Upare na maeneo yanayozunguka Kilimanjaro, sitiari ya mungu jua ilikuwepo katika mawazo ya kidini ya mame-Wachaga mwanzoni mwa kikwi cha pili.

Hali ya mame-Wachaga kuwajumuisha Waasa pia iliongeza dhana za mungu za Wakushi wa kusini zilizowathamini kikamilifu mababu, hali iliyotokana na sehemu ya Ubuntu ya Wachaga.

### *Hitimisho*

Ingawa Hitimisho nusu ya kikwi ya kati ya mwaka 600 hadi 1100 haikuwa ni kipindi cha mabadiliko makubwa, bado kilikuwa ni kipindi kilichokuwa na mabadiliko machache katika sehemu mbalimbali za eneo kubwa. Kutofautiana katika uchumi wa ndani kuliendelea kufuata migawanyo iliyokwisha kuwekwa ya kimbari na kijiografia. Kilimo cha upandikizaji na ulimaji kidogo wa nafaka vilifanywa na Wabantu, wakati ambapo ulimaji nafaka pamoja na ufugaji vilifanywa na Wanilo na Wakushi. Yawezekana kwamba wawindaji-waokotezaji wa Kikhoisani walikuwa bado wamezikalia sehemu za Maghribi na kusini Maghribi mwa Tanzania. Wakati huohuo mabadilishano ya tamaduni miongoni mwa jamii lilikuwa ni jambo dhahiri; mwanzo wa kubobelea katika aina moja au nyingine ya uchumi ulionekana katika baadhi ya sehemu; na mara kadhaa kulitokea mchanganyiko mpya wa watu. Tukio kubwa zaidi, kucbanganyika kwa Wanilo, Wakushi wa kusini na Wabantu katika mame-Wachaga kuliunda jamii mpya ambayo ilijumuisha mawazo ya msingi na tabia kutoka katika kila moja ya historia za tamaduni tatu.

Sifa ya kipindi hicho ilikuwa ni ya kutengwa kwa sehemu ya bara ya Afrika Mashariki kutokana na mfululizo wa mabadiliko yaliyoshamiri katika Bahari ya Hindi. Mazao machache kama vile ndizi kutoka Indonesia yalienea sehemu za bara katika kipindi cha kabla ya karne ya saba lakini kilimo chenyewe hakikuathiriwa kwa vyovyote na Bahari ya Hindi.

Haionyeshwi kabisa kuwa biashara ilifanywa hadi ndani kabisa mwa Afrika Mashariki. Kauri chache sana zilifika huko, zikipitia katika njia ya mabadilishano ya kiwango kidogo kutoka katika jumuiia moja hadi nyingine; lakini sehemu ya bara ya Afrika Mashariki haikuwa na kitu chochote cha maana kwa bishara ya Bahari ya Hindi, kitu ambacho hakikuwepo pia katika kilomita chache za ukingo wa Bahari. Watu walioishi bara waliweza kujipatia mahitaji yao katika kipindi chote na kwa karne nyingi zilizofuata.

Jambo lingine kuu, ambalo ni la muhimu lakini lisiloonekana wazi katika sehemu ya bara la Afrika Mashariki, linaweza kuwa limejitokeza katika nusu ya pili ya kikwi cha kwanza. Matumizi makubwa ya ardhi katika kilimo yaliyofanywa na Wabantu wa kipindi hicho yanaonyesha kuwa maeneo ya Wabantu yalikuwisha kuwa ni maeneo yenye watu wengi. Katika kikwi cha pili, maeneo hayo yalikuwa hifadhi kuu ya watu ambayo ilikuwa kitovu cha miguro ya watu na mfululizo wa mabadiliko makuu.

# 23

## Afrika ya Kati Hadi kaskazini ya Mto Zambezi

### Mwanzo wa Enzi ya Chuma

Hadi kufikia mwanzo wa kipindi kinacho-shughulikiwa katika sura hii, karibu sehemu yote inayohusika ilikuwa inakaliwa na watu wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma, wengi wao inawezekana walikuwa wanazungumza lugha za Kibantu. Katika maeneo mengi, mabaki ya watu walioishi mapema zaidi na wenye teknolojia tofauti waliendelea kuishi sambamba na watu wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma ambao inawezekana walitofautiana kilugha. Utamaduni wa kusini mwa msitu wa ikweta kote unajulikana kwa jina la tasnia changamani ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma, na imegawanywa katika mkondo wa mashariki na mkondo wa Maghribi. Kwa kufuata msingi wa aina ya vyombo vya ufinyanzi, kuna makundi kadha, kulingana na maeneo ya kijiografia, katika kila mkondo. Kila kundi limepewa jina kufuatia mahali ambapo ufinyanzi unaohusishwa nalo uligunduliwa kwanza na kufafanuliwa. Kuna ulinganifu wa namna fulani kati ya mchakato wa upanuzi na kronolojia inayohusiana na mikondo hii, kwa upande mmoja, na kwa uundaji wa mtawanyiko wa lugha za Kibantu, kwa upande mwingine. Mikondo yote miwili inaonekana, angalau kwa upande fulani, kuwa imetoka katika makazi ya Urewe katika eneo la maziwa katika kikwi cha mwisho cha kabla ya enzi yetu.

Kupanuka kwa mkondo wa mashariki inawezekana kulianza kwenye karne ya pili ya enzi yetu pamoja na mwanzo wa mapokeo ya vyombo vya Kwale katika maeneo ya pwani ya Kenya na Tanzania; mtandao wake mkuu kuelekea kusini ulikuwa haujafikiwa mpaka karne ya nne, wakati ambapo utamaduni wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma ulipofika katika sehemu nyingi za mashariki ya Afrika chini ya ikweta kuelekea kusini hadi Transvaal na kusini mwa Msumbiji. Ni wakati huu ambapo makazi ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma ya mkondo wa mashariki yalipofanyika katika maeneo ya mashariki kabisa ya sehemu hii, yaani, katika Malawi na sehemu za Zambia ambazo ziko mashariki mwa mto Luangwa. Upanuzi wa baadaye wa mkondo wa mashariki, kuanzia kwenye kituo cha kusini mwa mto Zambezi, katika nchi ya sasa ya Zimbabwe, ulitokea kwenye karne ya sita, lakini uliathiri sehemu ndogo kabisa ya eneo linalohusika -eneo la maporomoko ya Viktoria kusini kabisa mwa Zambia.

Imekisiwa kwamba mkondo wa Maghribi ulijitokeza kwenye mwanzo wa enzi ya Ukristo, katika eneo la kusini mwa Kongo ya chini, kufuatia mwingiliano wa makundi mawili tofauti yaliyokuwa yanazungumza lugha za Kibantu. Moja kati yao yaelekea lilipenya katika misitu ya ikweta na kuingia kusini kutoka kwenye chanzo asilia cha lugha ya Kibantu katika nchi ya sasa ya Kameruni. Yawezekana imewakilishwa katika rekodi za kiekiojia katika kile kiitwacho neolithi ya Kileopold '(Leopoldian neolithic)' ya koneo ya Chini.





23.1 Tamaduni za kiakiolojia Afrika mashariki na kusini • (D. W. Phillipson)

Kundi la pili la wazungumzaji wa Kibantu laelekea, kama lile la mkondo wa mashariki, kutokana na makazi ya Urewa, katika eneo la maziwa. Yamkini kabisa ilikuwa ni kutokana na kupanuka huku kuelekea kusini na Maghribi katika kingo za msitu ambapo ufugaji wa ng'ombe na kondoo, kilimo cha nafaka, na pengine maarifa ya mbinu za kutengeneza madini, vilipoletwa kwenye savana ya kusini-Maghribi. Maendeleo haya yanaweza kuwa ndiyo yalisababisha upanuzi wa utamaduni wa Enzi ya Chuma kutoka nchi ya Kongo kuelekea kusini, kupitia Angola hadi Kaskazini mwa Namibia, yakiamana na lugha ya awali iliyozaa lugha za Kibantu za leo kama vile Kimundu na Kiherero. Eneo pekee la kiakiolojia ambalo tarehe yake inajulikana na ambalo linaweza kusemwa kuwa ni matokeo ya awamu ya mapema ya upanuzi huu ni Benfika; eneo lililo kwenye pwani ya Atlantiki karibu na Luanda ambapo vyombo vya ufinyanzi vinavyofanana sana na vile vya Enzi ya Mwanzo ya Chuma katika maeneo mengine ya mkondo wa Maghribi vinatokea katika karne ya pili ya enzi ya ukristo.

Aidha, baadhi ya mambo ya utamaduni wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma, yaani maarifa ya ufinyanzi na ufugaji wa kondoo na ng'ombe yaelekea kuwa yaliwafikia wasemaji wa Kikhoisan wa Namibia ya kusini na Cape ya Maghribi – mbali zaidi ya mpaka wa kusini wa upenyezi wa Wabantu – kwenye karne ya pili au ya tatu ya Enzi ya ukristo. Kwa kuwa ni vigumu kufikiria chanzo kingine cha magunduzi haya mbali na mkondo wa Maghribi wa enzi ya Mwanzo ya Chuma, tarehe yake inaweza kufasiliwa kama *teminus antequem* (kipindi cha mwisho) kwa huo upanuzi wa kuelekea Angola.

Dokezo la hapo juu halipingani na mahitimisho ya wanaisimu-linganishi wa lugha za Kibantu kama ambavyo linavyoweza kutumiwa katika kuunda misingi ya kihistoria ya maendeleo ya lugha za Kibantu. Kiini cha kusambaa kwa mkondo wa Maghribi kutoka nchi ya Kongo kuelekea kusini mwa sehemu za chini za mto Kongo kinaweza kukubahana na kiini cha pili cha kusambaa kwa lugha za Kibantu ambacho kimekwika katika eneo hili kufuatana na uchunguzi nipa wa kiisimu. Lugha za Kibantu zilienea moja kwa moja kuelekea kusini kuanzia kwenye asili yake ya Kameruni kufuatia ama njia ya pwani au njia ya mto hadi sehemu ambayo sasa ni Kongo ya Chini. Yaelekea huu ulikuwa ni mguro tofauti kabisa na ule ambao ulileta lugha nyingine ya Kibantu Kaskazini karibu na kingo za msitu katika eneo la maziwa. Lugha za Kibantu ambazo zimeanza kutumika hivi karibuni kusini mwa msitu wa ikweta zote zaelekea kutoka, moja kwa moja au kwa namna fulani, kwenye kiini cha mtawanyiko karibu na Kongo ya Chini. Hatua ya kwanza ya mtawanyiko kutoka kwenye kiini hiki yaelekea ndiyo iliyoleta lugha azali zilizozaa kundi la nyanda za juu za Maghribi, lugha ambazo zinazungumzwa sasa katika nyanda ya juu ya Angola na kusini hadi Kaskazini mwa Namibia.

### *Mkondo wa maghribi wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma*

Kikronolojia, tasnia ya mwanzo kabisa katika tasnia za kipindi cha kabla ya kuandikwa kwa historia ni ile ya Kongo ya Chini, ambayo imekuwa ikijulikana kama 'Neolithi ya Kileopold' (Leopoldian neolithic). Vyombo vya mulula huu vya ufinyanzi vina shingo na vimetiwa nakshi kwa mifuo ya madoido. Hakuna masaha ya kazi za chuma yaliyohusishwa na ufinyanzi huu, badala yake kuna 'mashoka' mengi ya mawe. Yaliyogunduliwa kuhusu ufundi huu yanajulikana kutoka sehemu ya Kinshasa kwa upande wa kusini mwa Malebo (Stanley) Pool, na kutoka hapo kuelekea Maghribi karibu na pwani ya Bahari ya Atlantiki hasa katika mapango na mawe ya kujihifadhi katika jimbo la Kongo ya Chini. Hakuna dalili ya ufundi huu iliyoandikwa katika maeneo ya Kaskazini mwa Angola. Uchunguzi huu, pamoja na kuonekana ghafla kwa zana za mawe katika sehemu ya eneo


ambako kupatikana kwake ni adimu sana, na pia kuonekana kwa tasnia kama hizo Kaskazini mwa msitu, katika Afrika ya Maghribi na kisiwa cha Fernando Po, yote haya yanadhahirisha kwamba 'neolithi ya Kileopold' ililetwa Kongo ya Chini kutoka hasa Kaskazini.

Katika sehemu nyingine za Kongo ya Chini ambazo zinaweza kukisiwa kuwa za tarehe ya baada ya vyombo vya 'kineolithi' vilivyotajwa hapo juu, vyombo vingi tofauti vya ufinyanzi viligunduliwa na ambavyo vinaonyesha mfanano mkubwa na vile vya Enzi ya Chuma ya Mwanzo katika maeneo ya mashariki zaidi. Hasa, mshabaha kati ya vyombo hivi na vile vya Urewe, hususani vile vya kutoka pango la Dimba karibu na Mbanza Ngungu, unaonekana kuwa wa karibu kuliko ilivyo katika 'Neolithi ya Kileopold.' Kusini zaidi, kama tulivyoona hapo juu, vifinyange vya Benfika pia vinaonyesha mshabaha mkubwa na vile vya Enzi ya Mwanzo ya Chuma: vinakisiwa kuwa ni vya karne ya pili ya enzi yetu, na hii inaweza kuwa pia ndiyo tarehe ya vyombo vya Kongo ya Chini.

Taarifa tulizonazo juu ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma katika maeneo ya ndani zaidi ya Angola na katika sehemu jirani ya Kasai ya Kongo ni ndogo kabisa. Karibu na Tshikapa, jirani na mpaka wa kusini wa Kasai, uchimbaji wa madini katika bonde la Lupembe ulitoa karibu vyombo vinne vya ufinyanzi ambavyo vilikuwa karibu kukamilika na ambavyo haingekuwa makosa kuviweka katika kundi moja na vile vya Urewe katika enco la maziwa. Kusini kidogo tu, ukivuka mpaka wa Angola, makusanyo madogo mawili ya vyombo vya ufinyanzi kutoka sehemu ya Dundo yamepatikana na yanakisiwa kuwa ya kipindi cha robo ya mwisho ya kikwi cha kwanza cha enzi ya Ukristo. Masalia ya vyombo vya ufinyanzi yanatofautiana sana na yale ya Tshikapa (yanayokisiwa kuwa ya zamani zaidi). Lakini, hata hivyo, yanaonyesha sifa kadhaa za Enzi ya Mwanzo ya Chuma na sifa ambazo zimeendelea katika ufinyanzi wa enzi hizi Kaskazini mwa Angola. Hadi kufikia karne ya saba au ya nane, kiasi kikubwa cha makazi ya Enzi ya Chuma kilikwishafanyika huko Feti la Choya, karibu na makutano ya mito ya Kunene na Kunyongauna. Kaskazini kabisa mwa Namibia, huko Kapako karibu na mwisho wa Maghribi katika ukanda wa Kaprivi, eneo lenye mabaki ya kazi za uhunzi wa chuana limetoa vyombo vya ufinyanzi vinavyohusiana na vyombo vya Enzi ya Mwanzo ya Chuma katika mkondo wa Maghribi, hasa vya kutoka Kapwirimbwe.


Ujuzi wetu wa kiakiolojia juu ya mkondo wa Maghribi wa enzi ya Mwanzo ya Chuma kwa mapana na marefu unatokana na bonde la chini la Upemba katika Lualaba ya chini huko Shaba. Makazi ya awali kabisa ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma yako Kamilamba, na yamekadiriwa kuwa ya karne ya sita au ya saba hivi ya Enzi ya Ukristo. Ufinyanzi unaonyesha uhusiano wa karibu sana na ufinyanzi wa vyombo vya wakati huohuo vya huko Zambia ya Maghribi. Kwenye karne ya kumi, au nyuma kidogo, matumizi ya mfululizo wa makaburi yenye maeneo makubwa makubwa yalianza, inatumizi ambayo yamegunduliwa katika nyakati kadhaa katika miaka ishirini iliyopita. Maarufu kuliko yote ni lile la Sanga kwenye Ziwa Kisale. Makaburi ya Sanga yanaonekana kuendelea kutumika hadi kwenye karne ya kumi na saba au ya kumi na nane, lakini katika kipindi hiki aina ya ufinyanzi unaohusiana na makaburi hayo unaonekana kuwa na mizizi ya mapokeo ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma.

Maiti walikuwa wanalazwa kwa kunyooshwa au kupindwa kidogo pamoja na vitu vingi vya kuweka kaburini. Vitu vilivyotumika mara nyingi vilikuwa vyombo vya ufinyanzi vya kabla ya mwaka wa 1300 wa Enzi ya Ukristo. Vyombo vilitengenezwa kwa mtindo wa Kisafia, vikifuatwa na vile vinavyosemekana kuwa vya mapokeo ya Kabambi. Vyombo vya metali pia vilikuwapo kwa wingi, ikiwa ni pamoja na mapambo mazuri yaliyotengenezwa kwa shaba kama vile mikufu, bangili na mikanda iliyosukwa na vidari. Chuma kinawakilishwa zaidi na majembe na mashoka kuliko silaha: kulikuwa pia na kiasi kikubwa cha kengele zenye ndimi. Mikuo ya shaba yenye umbo la



23.2 Kaburi kutoka kwenye kipindi cha Kisaham (karne ya kumi hadi ya kumi na nne), eneo la Sanga (P. de Maret, Makumbusho ya Kifalme ya Afrika ya Kati)

23.3 Vyungu na bangili za pembe za ndovu kutoka Sanga



msalaba ya ukubwa mbalimbali ilikuwa ya kawaida sana katika makaburi ya Kabambi, lakini adimu kwa makaburi ya Kisali; kuna ushahidi kwamba mikuo hii huenda ilitumika kama pesa.

Kama kilometa 140 Kaskazini mwa ukanda wa Lualaba kuna eneo la Katoto, mahali ambapo pana makaburi mengine ambayo kwa namna nyingi yanafanana na yale ya bonde la Upemba. Ufinyanzi ni ule wa mapokeo ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma, ingawa una uhusiano mkubwa na vyombo vya Urewe na ufinyanzi wa Maghribi mwa Zambia kuliko ulivyo ufinyanzi wa Kasali. Inawezekana kwamba Katoto huenda ikatokea kuwa ya zamani zaidi kuliko makaburi ya Sanga.

Lakini, makazi ya Lualaba yanaonyesha utajiri yakinifu na teknolojia ya hali ya juu iliyokuwa imefikwa katika eneo hili tangu mwanzoni mwa kikwi hiki. Kulikuwepo na kiasi kikubwa cha msongamano wa watu wakati huu kutokana na kuwepo kwa mashapo mengi ya madini katika ukanda wa shaba. Eneo hili la uchimbaji madini lilivuta mahusiano ya kibiashara katika eneo kubwa la watu wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma ingawa uchimbaji madini ulibakia kuwa wa kiwango kidogo. Mfuatano huu ni wa maana sana na unavutia kwa kuwa unatokea katika eneo ambamo napokeo simulizi yanakiweka kiini au chanzo cha ufalme wa Luba ambao unakisiwa kuwa asili ya falme nyingi za maeneo ya savana ya kati.

Makazi mengi ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma yameonekana katika tikanda wa shaba na yanadaiwa kuwa katika kundi la Chondwe, lililopewa jina hilo kufuatia eneo lililo kilomita 45 kusini nwa Ndola. Bangili za shaba zilipatikana Chondwe kwenye maki ya tarehe ya kati ya karne ya sita ya karne ya nane za enzi yetu; ufundi wa vitu vya aina hiyo uliotumika kuremba vyungu unaashiria pana kuwa utumiaji wa shaba huenda unarudi nyuma hadi katika kipindi cha makazi ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma katika eneo hili, kwenye mwanzo wa karne ya sita.

Masalia ya aina za ufinyanzi wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma yanayoonekana hapa na pale katika maeneo kadhaa siyo ya mapokeo ya ufinyanzi wa kiasili wa kundi la Chondwe bali wa maeneo ya mbali, kwa mfano - bonde la kati la Zambezi na kusini Malawi. Matokeo haya yanaweza kufasiliwa kama ushahidi wa maingiliano baina ya makundi. Maingiliano hayo yalifanywa na watu waliokuwa wakisafiri kutoka mbali kwenda kwenye maeneo yaliyokuwa yakizalisha shaba, kwa ajili ya kupata madini. Kwa kuwa kuna kila sababu ya kuamini kwamba wakati wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma katika eneo hili la Afrika ufinyanzi ulikuwa kazi ya wanaume, inawezekana kwamba ufinyanzi wa kigeni uliotajwa hapo juu ulifanywa na wasafiri hawa: kwa hiyo hakuna haja ya kufikiri kwamba familia nzima zilisafiri kwenda kwenye maeneo ya uchimbaji madini kwa ajili ya kutafuta metali, au kwamba vitu vinavyovunjika kama vyungu navyo vilikuwa bidhaa za biashara katika maeneo ya masafa marefu.

Kuelekea Maghribi mwa ukanda muhimu wa shaba kwenye milima kati ya mto Zambezi/Kongo karibu na Solwezi, eneo la uchimbaji madini la Kansashi la kipindi cha awali limegunduliwa hivi karibuni. Hapa, makazi ya mwanzo ya Enzi ya Chuma kwenye karne ya tano yanahusishwa na ushahidi wa kazi za shaba. Ufinyanzi ni tofauti na ule wa kundi la Chondwe na unachangia sifa na vyombo vilivyoonekana kuzagaa katika mahali pengi na nchi ya Mchanga ya Kalahari, Maghribi mwa Zambia. Hapa, maeneo yenye habari nyingi ni yale ya Sioma kwenye sehemu ya juu ya mto Zambezi, mahali ambapo si mbali sana na kusini mwa uwanda wa mafuriko wa Barotse na Lubusi katika wilaya ya Kaoma. Makazi ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma yanayohusishwa na kazi za chuma na (kufuatia michoro ya bangili kwenye vyombo vya ufinyanzi) shaba yalithibitishwa kuwa ya karne ya sita, kama siyo ya mwisho wa karne ya tano. Katika maeneo yaliyofanyiwa utafiti ni karibu na bonde la mto Zambezi tu ambako kuliwezesha mgawanyo wa eneo kufanywa kwa kiwango cha kueleweka.

Maeneo mengine pekee ya Zambia yanayoweza kuingizwa tu katika makazi ya ukanda wa

Maghribi ni nyanda za juu za Lusaka na Jimbo la Kusini ambako maeneo ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma yameelekezwa katika makundi ya Kapwirimbwe na Kalundu, katika mfuatano huo. Ufinyanzi wa kundi la mwanzo ambako makazi ya muda mfupi yanakadiriwa kuwa ya karne ya tano, unaonyesha kufanana sana na kundi la Chondwe katika ukanda wa shaba. Masalia mengi ya daga (matope yaliyogandamana) yaelekea kuwa mabaki ya matanuri ya kuyeyushia chuma: inaelekea kazi ya kufua chuma ilikuwa inafanywa kwa kiwango kikubwa ndani au karibu na kijiji, lakini shaba haikuweko.

Awamu za baadaye za kundi la Kapwirimbwe zinajulikana sana katika eneo la Barabara ya Twickenham katika kitongoji cha Lusaka. Kwenye kipindi kati ya karne ya tisa na mwanzoni mwa karne ya kumi na mbili, ufinyanzi ulikuwa ukitumia urembeshaji wa vyombo ambao ni mwendelezo wa mapokeo yaleyale ya huko Kapwirimbwe. Mbuzi walikuwa wanafugwa, na uwindaji wa nyama pori ulikuweko. Uhunzi ulikuweko kwa kiasi kikubwa lakini uhunzi wa shaba ulijitokeza tu katika Barabara ya Twickenham kwenye awamu ya mwisho ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma. Huko Kapwirimbwe na Barabara ya Twickenham kuligunduliwa mabakuli ya udongo yenye vitundu, ambayo inakisiwa kwamba pengine yalikuwa yanatumika katika utayarishaji wa chumvi.

Kiwango cha mwanzo cha kundi la Kapwirimbwe si rahisi kuthibitishwa lakini ufinyanzi unaofanana nacho uligunduliwa kuanzia sehemu za mbali Maghribi kabisa kufikia Pango la Mumbwa na katika eneo la Chirundu la boude la mto Zambezi. "Ufinyanzi wa mapokeo ya Sinoa" wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma katika Wilaya za Lomagundi na Urungwe huko Zimbabwe unafanana sana na ule wa Kapwirimbwe na Barabara ya Twickenham kiasi kwamba nao pia unachukuliwa kuwa katika kundi hilo moja. Maeneo haya ni tofauti kabisa na mengine ya wakati huo nchini Zimbabwe na yana umuhimu maalumu kama viwakilishi vya mkondo wa Maghribi wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma ambao haujabainishwa kusini mwa mto Zambezi.

Katika Jimbo la Kusini au uwanda wa juu wa Batoka kusini mwa mto Kafue, makazi ya kwanza ya kundi la Kalundu huenda yalikuwepo kabla ya mwisho wa karne ya nne. Ufinyanzi na mambo mengi ya kitamaduni vinachangia sifa nyingi na yale ya kundi la Kapwirimbwe. Huko Kalundu Mound karibu na Kalowo, wanyama wa kufugwa (ng'ombe, mbuzi/kondoo) wafichukua uwiano wa chini ya mbili ya tano ya mifupa iliyofukuliwa, jambo linaloashiria kwamba uwindaji ulichukua sehemu kubwa ya uchumi.

### *Mkondo wa mashariki wa enzi ya mwanzo ya chuma*

Nchini Malawi na mashariki ya Zambia, tasnia za Enzi ya Mwanzo ya Chuma zinajibainisha wazi. Zinawekwa chini ya mkondo wa mashariki na zinaelekea kuwa zimetokana moja kwa moja na makazi ya kundi la Urewe katika eneo la maziwa.

Tunaweza kubainisha namna mbili zenye kuhusiana katika Enzi ya Mwanzo ya Chuma huko Malawi: kundi la Mwabulambo lililoko Kaskazini, lililopata jina kutokana na mto Lufilya, na huko kusini - kundi la Nkope, lililopata jina kutokana na sehemu ya Maghribi ya Ziwa Malawi, Kaskazini mwa Mangochi. Hali na mahali pa mipaka ya kijiografia kati ya makundi haya mawili havijulikani vizuri. Mtawanyiko wa vyombo vya Nkope unaendelea kuelekea Maghribi hadi sehemu kubwa ya kusini mashariki mwa Zambia, wakati kusambaa kwake katika sehemu jirani za Msumbiji kunadhihirishwa na vyombo vilivyokusanywa na Carl Wiese katika mwaka wa 1907. Tarehe zilizokadiriwa kwa kutumia radio karboni kwa maeneo ya Malawi ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma zinaonyesha kwamba ustawi wake ulianza mapema katika karne ya nne ya Enzi ya Ukristo; takwimu zimeonyesha pia kwamba yawezekana kundi la Mwabulambo lilianzishwa mapema kidogo

kuliko kundi la mwanzo la kusini.

Alama za nyumba za miti na udongo (miti na udongo wa kukandika) zilihifadhiwa kwenye kilima cha Phopo karibu na Ziwa Kazuni. Mavi ya chuma na masalia ya vifaa na vyombo vya chuma vimepatikana katika maeneo kadhaa, kama vile Nanyangu, katika wilaya ya Ncheu na katika safu ya milima ya Zomba. Kwa upande mwingine, shaba haikugunduliwa. Shanga za koa ziligunduliwa pamoja na vyombo vya Nkope katika shimo la ghala kwenye mkondo wa Phwadze katika wilaya ya Chikwawa. Shanga hizo zinakisiwa kuwepo katika karne ya tano au ya sita ya enzi ya Ukristo. Kitu pekee cha Enzi ya Mwanzo ya Chuma kilichoonekana mwambao wa Malawi ni kipande cha ushanga wa kauri kutoka katika eneo la Nkope kwenye mkondo wa Namichimba, Mwanya.

Ni lazima sasa tuangalie Enzi ya Mwanzo ya Chuma katika sehemu ya Maporomoko ya Viktoria kusini mwa Zambia. Kundi hili limepewa jina la Dambwa. Kundi hili limeenea kwenye bonde la mto Zambezi kuanzia eneo la Chirundu kuelekea juu hadi karibu na Sioma, na kusini angalau kufikia eneo la Wankie huko Zimbabwe. Hapana shaka kwamba kundi la Dambwa lilitokana na kupanuka kwa mkondo wa mashariki wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma kuelekea Kaskazini Maghribi kuanzia nyanda za juu za Zimbabwe. Kilele cha kundi la Dambwa katika sehemu ya Maporomoko ya Viktoria kilikuwa hakijafikiwa hadi kwenye karne ya sita ya Enzi ya Ukristo. Hii ilikuwa muda kitambo baada ya kutokea kwa makazi ya mkondo wa mashariki katika maeneo ya umbali kidogo tu upande wa Kaskazini.

Mahali palipojulikana sana pa kundi la Dambwa ni Kumadzulo, ambapo palikaliwa kati ya karne ya tano na ya saba, na makazi ya Dambwa yalifanyika baadaye kidogo. Kwenye maeneo ya kundi la Dambwa imegunduliwa mifupa ya ng'ombe na mifugo mingine mbali na ile ya wanyamapori. Alama za nyumba huko Kumadzulo zinafasiliwa kuwa mabaki ya nyumba ndogo za mstatili za miti na udongo. Maingiliano na pwani ya mashariki kibishara yalikuwisha kuwapo tangu karne ya saba kama inavyodhihirishwa na vipande vya bilauri vilivyopatikana katika masalia ya nyumba huko Kumadzulo pamoja na shanga za kauri zilizopatikana katika eneo jirani la Shamba la Chundu. Lakini shanga za vioo hazipatikani katika Enzi ya Mwanzo ya Chuma katika sehemu hii. Zana za chuma zilizokuwa zinatengenezwa huko ni pamoja na majembe, mashoka, visu, ncha za mikuki na vyembe vya mishale. Pia mkuo wa shaba na bangili viligunduliwa vikiashiria kuwepo kwa biashara baina ya sehemu zilizokuwa zinatoa staba kama vile Hook ya mto Kafue au jimbo la Wankie la Zimbabwe.

Machimbo ya Shamba la Chundu yametoa mwanga kuhusu utamaduni wa kuzika katika Enzi ya Mwanzo ya Chuma, utamaduni ambao unaweza kulinganishwa na ule uliokuwepo kwenye makaburi ya Lualaba ya juu tuliyokwisha elezea hapo awali. Maiti walizikwa katika makaburi membamba na mafupi yaliyofanana na mashimo, na mashimo ya namna hiyo hiyo yalichimbwa pembeni kwa ajili ya kuwekea vitu vya kuzikwa navyo. Vitu hivi mara nyingi vilikuwa ni jozi za vifaa vya ufinyanzi, ikiwa ni pamoja na chombo kilichofunikwa cha kuwekea vitu na vifaa vya marehemu kama majembe ya chuma, mashoka, bangili za shanga au chuma, shanga za kauri au za koa. Eneo la Shamba la Chundu linakisiwa kuwa la kwenye karne ya nane ya Enzi ya Ukristo.

### *Kipindi cha mpito kati ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma na Enzi ya Baadaye ya Chuma*

Katika sehemu nyingi za Afrika kunakozungunzwa lugha za Kibantu wanaakiolojia hawakujishughulisha sana na Enzi ya Baadaye ya Chuma ukilinganisha na Enzi ya Mwanzo ya

Chuma. Matokeo yake ni kwamba walau kwa kipindi hiki kinachohusika, kipindi ambacho kabla yake mapokeo simulizi huwa chanzo muhimu cha kihistoria, karne zinazofuata mwaka takriban 1,000 hazijulikani kabisa katika historia ya Afrika ya Kati. Lakini, pamoja na kukosekana kwa taarifa nyingi muhimu sura imeanza kujitokeza ya kuachana na utamaduni wa ufinyanzi katika maeneo mengi kuanzia mwanzoni mwa karne ya kumi na moja ya Enzi ya Ukristo. Moja ya maeneo machache ambapo utamaduni huo uliendelezwa katika kipindi hiki ni kusini mwa Zambia.

Taarifa za kiakilojia zinazohusika hapa zinahusu tasnia ya Kalomo ambayo ilitokana na awamu ya baadaye ya mfuatano wa kundi la Dambwa la eneo la Maporomoko ya Viktoria. Kwa hiyo kuelekea mwishoni mwa karne ya kumi na moja, ya enzi yetu mafundi wanaelekea walikwishaanzi kuaambaa Kaskazini na Kaskazini magharibi kuelekea nyanda za juu za Batoka ambako ufinyanz wao ulichukua nafasi ya ule wa kundi la Kalundu la Enzi ya Mwanzo ya Chuma. Sura nzuri ya tasnia ya Kalomo, kwa ujumla, inapatikana Isamu Pati, Maghribi mwa Kalomo, mahali ambapo hakukuwa na makazi ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma.

Inaelekea uhunzi ulifanywa na wakazi wa Kalomo kwenye kiwango cha chini kuliko watangulizi wao wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma. Ingawa mashoka na majembe yamepatikana, lakini ni adimi sana; visu, nyembe na ncha za mikuki na nyembe za mishale ndivyo vitu pekee vilivyopatikana kwa wingi. Shaba ilitumiwa kutengeneza bangili. Kuna ushahidi kuwa kulikuwa na kilimo cha mtama lakini inaonekana kwamba katika karne za mwanzo za Enzi ya Baadaye ya Chuma uchumi ulikuwa unategemea sana ufugaji wa wanyama, hasa ng'ombe. Kupatikana kwa shanga za vioo, kauri na ko kunaonyesha kuwa kulikuwepo na mawasiliano ya kibiashara zaidi na pwani ya mashariki kuliko ilivyokuwa kabla.

Kwenye nusu ya pili ya karne ya kumi na moja, tasnia ya Kalomo, kwenye nyanda za juu za Batoka, ilipoteza nafasi yake ghafla na kuehukuliwa na tasnia tofauti iliyojulikana kama Kangili iliyoenea kuelekea kusini na ambayo yaelekea ilianzia katika au karibu na bonde la chini la miti Kafue. Tasnia ya Kangila ilisambaa pia hadi eneo la Maporomoko ya Viktoria ambako kukutana kwake na tasnia ya Kalomo kulikadiriwa tarehe, huko Sinde, kuwa miaka mia moja baada ya tukio linalofanana nalo kwenye nyanda za juu: kuehelewa huku kwa muda kunaweza kuchukuliwa kama matokeo ya kusambaa polepole kuelekea kusini kwa tasnia ya Kangila. Machimbo yalifanywa katika maeneo mawili tu - Sebanzi, karibu na Monze na Ingombe Ilede, karibu na makutano ya miti Zambezi na Kafue. Katika Ingombe Ilede makazi huenda yalianza katika karne ya saba au ya nane huko Sebanzi yawezekana makazi yalifanyika baadaye. Ufinyanzi wa hapa unaweza kuchukuliwa kuwa ndio uliokuwa kitovu cha ule uliopatikana kwenye nyanda za juu za Kangila, karibu na Mazabika. Kijiji cha Kangila chenyewe kilikaliwa kwa muda mfupi karibu kwenye karne ya kumi na tano ya Enzi ya Ukristo. Kwa hiyo kinawakilisha awamu ya mwisho ya tasnia, ambayo imepewajina lake.

Nje ya Jimbo la Kusini, ufinyanzi uliozaga sana wa Enzi ya Baadaye ya Chuma inayotambuliki huko Zambia ni ule wa mapokeo ya Luangwa. Mtandao wake unachukua Zambia yote hadi Kaskazini na mashariki ya mlolongo unaotokea Kafue ya chini hadi Lubumbashi, na unaendelea pia hadi sehemu za karibu za Kongo, Malawi, Msumbiji na Zimbabwe. Kwa hiyo, mapokeo ya Luangwa yanatokea katika maeneo ambamo Enzi ya Mwanzo ya Chuma ilikuwa sehemu ya makundi ya Kalambo, Nkope, Chondwe na Kapwirimbwe; sehemu ambazo zinawakilisha mikondo yote miwili ya mashariki na Maghribi. Mapokeo haya yanajitokeza kwanza katika karne ya kumi na moja ya Enzi ya Ukristo na yanajitofautisha kabisa na mapokeo ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma yaliyotangulia. Katika sehemu yake yote ya msambao mapokeo ya ufinyanzi wa Luangwa yamedumishwa hadi nyakati za sasa na watu kama vile Wabemba, Wachewa, Wansenga na



Walunda wa Kaskazini.

Kuna tofauti kubwa sana kati ya ufinyanzi wa mapokeo ya Luangwa na ule uliotangulia wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma, na hapajawa na dalili za maendeleo ya taratibu toka ufinyanzi mmoja hadi mwingine. Hata hivyo, vyombo vya Enzi ya Mwanzo ya Chuma ambavyo vinakaribiana na vya mapokeo ya Luangwa ni vile vya mapokeo ya kundi la Chondwe. Inaelekea chanzo cha mapokeo ya Luangwa kinakaribiana sana na ufinyanzi wa kundi la Chondwe kuliko kundi lolote la Enzi ya Mwanzo ya Chuma linalojulikana hadi sasa. Labda mwanzo wa mapokeo ya Luangwa ulisababishwa na uhamaji kwa wingi wa watu ambao ulifanywa na familia nzima kutoka sehemu ya Kaskazini au Kaskazini-Maghribi mwa Zambia/ukanda wa Shaba. Kama ufinyanzi wa Luangwa ilikuwa kazi ya wanawake (kama ilivyo sasa), kutoka kwake ghafla kunaweza kufasiliwa kuwa ufinyanzi wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma ulikuwa unafanywa na wanaume.

Hali kama hii inajitokeza sasa katika Malawi, vyombo vya Nkope vikibadilishwa, kwenye miaka ya 1000 ya Enzi ya Ukristo, na vile vilivyopewa jina la Kapeni Hill katika Wilaya ya Ncheu. Karibu na wakati huohuo vyombo vya Mwamasapa vilichukua nafasi ya vyombo vya Mwabulambo kama sifa ya namna ya ufinyanzi katika sehemu ya Kaskazini ya nchi. Aina hizi mbili za vyombo vya Enzi ya Baadaye ya Chuma katika Malawi zinahusiana kwa kiwango fulani na zile za asili ya Luangwa. Nyumba za miti na tope zimechiriwa kuwepo kwake katika baadhi ya maeneo na nyumba zisizo za kudumu zenye umbo la mzinga wa nyuki. Vyombo vya chuma, na wakati mwingine vyombo vya shaba, vilitumika katika kipindi chote hiki. Shanga za kioo zilizoagizwa, ambazo zilikuwa adimu mwanzoni, zilizidi kuonekana kwa wingi. Mbegu za mtama zimepatikana katika ufinyanzi wa Mamasapa, ambapo mifupa ya ng'ombe inaonekana kwa wingi katika maeneo kadhaa ya Enzi ya Baadaye ya Chuma; vitu ambavyo vimesambaa kwa wingi katika Malawi.

Maghribi mwa eneo lililokuwa na mapokeo ya tasnia za Luangwa kuna kiwango kikubwa cha kuendeleza ufundi huo kuanzia ufinyanzi wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma hadi ufinyanzi wa kikwi cha sasa. Kwa mfano, katika wilaya za Mongu, Kabompo, Zambezi, Mwinilunga na Kaoma Maghribi mwa Zambia, mapokeo ya leo ya ufinyanzi, ambayo yameitwa mapokeo ya Lungwebungu, yanaonyesha kuwa na sifa za kufanana sana na yale ya Enzi ya Mwanzo ya Chuma, kama ilivyoonekana katika eneo la Lubusi hapo juu. Hakuna ushahidi wa kuwepo mwachano mkubwa katika rekodi za kiakiolojia mapema katika kikwi cha sasa kama ilivyokuwa katika kipindi kinachofuata Enzi ya Mwanzo ya Chuma katika upande wa mashariki. Katika sehemu inayokaliwa sasa na Wakaonde, aina nyingine ya ufinyanzi kati ya karne ya kumi na moja na kumi na tatu ilipatikana katika maeneo ya Kamusongolwa na Kansanshi.

## *Hitimisho*

Sasa ni lazima kuachana na hoja za kiakiolojia tupu ili kuchunguza maana na umuhimu wa maoni haya kihistoria.

Jambo la kwanza kuwekewa mkazo ni ukubwa wa kiwango cha mfungamano wa Enzi ya Mwanzo ya Chuma/Enzi ya Baadaye ya Chuma katika sehemu ya Maghribi ya Afrika ya Kati tofauti na hali ilivyo mashariki. Kinachovutia ni kwamba mgawanyo huu wa mashariki/Maghribi hauambatani na migawanyo ya mbari za sehemu hii, kama inavyofikiriwa katika mapokeo simulizi. Kwa mfano, watu wanaodai kwamba asili zao ni dola za Lunda na Luba wanapatikana katika maeneo yote mawili, mashariki na Maghribi. Zaidi ya hayo, kuna makundi yanayoiwa Lunda yanayofanya, kwa upande mmoja, ufinyanzi wa Luangwa (Kazembe ya Lunda katika bonde la Luapula) na, kwa upande mwingine, ule wa mapokeo ya Lungwebungu unaotokana na Enzi ya

Mwanzo ya Chuma (Lunda ya Maghribi ya Kaskazini-Maghribi mwa Zambia). Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba kuanzishwa kwa Enzi ya Baadaye ya Chuma na kutokea jamii-jenzi zake zifahamikazo vilikuwa ni vitu viwili tofauti kabisa. Hii inathibitishwa na vidokezi vya kikronolojia vitokanavyo na mafafanuzi ya hivi sasa kabisa ya mapokeo simulizi ambavyo vinayapeleka maendeleo ya kisiasa yaliyoanzisha himaya ya Luba kwenye umbali wa karne ya kumi na nne au kumi na tatu, tarehe ambayo bado ni ya karibu kuliko iliyotolewa na akiolojia kwa mwanzo wa Enzi ya Baadaye ya Chuma.

Tunapolinganisha taarifa za kiakiolojia na zile za kiisimu, ndipo tuwezapo kupendekeza uwiano wenye maana. Hapo juu tulivutwa na nadharia juu ya kundi la lugha za Kibantu za Mwinuko wa Maghribi; kundi ambalo linatokana na mtawanyiko wa kundi asilia karibu na Kongo ya Chini. Baada ya kuanzishwa, lugha hizi za Mwinuko wa Maghribi zilitoa zenyewe kiini cha mtawanyiko cha tatu katika eneo la Shaba. Kiini hiki ndicho ambacho wanaisimu wengi wanakichukulia kuwa chanzo cha mtawanyiko mkubwa wa mwisho wa lugha za Kibantu, ambao ulisababisha kujitokeza kwa lugha zinazokaribiana sana kwenye eneo lote la nusu ya mashariki ya Afrika ya Kibantu zinazoitwa kundi la Mwinuko wa Mashariki. Kuna misingi ya kuhusisha kuanzishwa kwa tasnia za Enzi ya Baadaye ya Chuma katika maeneo ya mashariki na usambaaji wa watu waliokuwa wakisema lugha za nchi ya Mwinuko wa Mashariki. Kuendelea kwa lugha za zamani na zinazozidi kuhitilafiana za Maghribi kunalingana na kiwango kikubwa cha kuendelea kwa Enzi ya Mwanzo ya Chuma/Enzi ya Baadaye ya Chuma katika Maghribi. Mtawanyo wa kijiografia wa lugha za nchi ya Mwinuko wa Mashariki unakubaliana na eneo ambamo tofauti iliyojidhihirisha katika mfuatano wa kiakiolojia ilitokea mwanzoni mwa Enzi ya Baadaye ya Chuma.

Hü ndiyo picha itolewayo na akiolojia na isimu katika kuelezea juu ya Afrika ya Kati kuanzia karne ya saba hadi karne ya kumi na moja ya Enzi ya Ukristo. Katika eneo hili lote katika Enzi ya Baadaye ya Chuma kulikuwa na watu, labda Wabantu, kuanzia mwanzo wa kipindi hiki, ingawa katika sehemu nyingi watu waliokuwa wakitumia zana za mawe katika kuwinda na kuokoteza chakula waliendelea kuwepo; mara nyingi walikuwa wakitegemeana na jirani zao wakulima. Ni dhahiri kwamba zilikuwa jamii za wakulima wadogo wadogo, bila mfumo maalumu wa kiutawala. Lakini, kuelekea mwishoni mwa kikwi cha kwanza tunaanza kuona ongezeko la mali, shughuli za kibiashara na kuongezeka kwa watu katika eneo la Lualaba ya juu. Ni katika sehemu hii ya jumla ambako kwenye karne ya kumi na moja ulianza mchakato wa mtawanyiko wa watu ambao ulizaa utamaduni wa Enzi ya Baadaye ya Chuma katika sehemu kubwa ya mashariki mwa Afrika ya Kati. Hivyo ilitokea idadi ya watu ambayo kutokana nayo kulianzishwa jamii za Enzi ya Baadaye ya Chuma.

---



---

## *Kusini mwa Afrika hadi kusini ya mto Zambezi*

### *Miguro ya kimbari na mifumo ya utamaduni: 700-1000*

Wataalamu wa akiolojia wa Kusini mwa Afrika hutumia mtindo wa vyombo vya ufinyanzi kuchunguza miguro ya watu wa Enzi ya Chuma kwa sababu vitu vya mitindo mbalimbali huonyesha mpaka wa utawanyikaji wa makundi ya mbari kufuatana na wakati na maenco. Hii ni kwa sababu:

(1) mtindo wa vyombo vya kauri hubuniwa na kuenezwa katika makundi ya watu; (2) kurithishwa kwa mitindo kwa kiasi fulani lazima kufanywe kwa kupitia mawasiliano ya mdomo, na (3) madhali watengenezaji na watumiaji wa mitindo ni watu wa aina moja, ueneaji wa mitindo lazima pia uwe unawakilisha kundi la watu wanaozungunza lugha moja.

Katika misingi hiyo lugha zilizozungumzwa na watu wa Enzi ya Chuma katika Afrika ya Kati na Kusini mwa Afrika zinaweza kuainishwa kuwa zote zilitokana na familia ya Wabantu. Kwa kuwa kazi za ufinyanzi za mwanzoni mwa Enzi ya Chuma katika eneo hili zinahusu mtindo mmoja changamani na kwa kuwa mmoja wa mitindo hiyo unaweza kufuatiliwa moja kwa moja hadi mtindo wa ufinyanzi wa sasa wa Washona, uendeleaji huu wa ufinyanzi unatosha kuonyesha kwamba kuna kiungo kati ya makundi ya Enzi ya Chuma na lugha za Kibantu.

Hadi kufikia mwaka 700 makundi kadhaa ya Wabantu yaliishi Kusini mwa Afrika. Kundi moja, ambalo limepewa jina kutokana na mji wa sasa wa Sinoa ni hivi karibuni tu limevuka mto Zambezi lakini mababu wa makundi mengine wamekuwa katika eneo la kawaida tokea mwanzo wa Enzi ya Chuma. Eneo ambalo tunajiluisisha nalo ni kusini Maghribi mwa eneo la Wamatabele, mashariki ya kati ya Botswana na Kaskazini mwa Transvaal, lililokaliwa hasa na Wazhizo. Walilikalia eneo hili kwa muda mwingine wa miaka 250 kabla ya wageni wapya wanaojulikana kama Wakopye wa Leopard hawajaingia kusini Maghribi mwa Zimbabwe. Mguro huu wa baadaye wa kimbari unathibitishwa na kutokuwepo mwendeleo mkubwa wa mtindo wa ufinyanzi kati ya Wazhizo na kundi la Wakopye wa Leopard la karne ya kumi. Kutokuendelea huku kwa mtindo wa ufinyanzi kunatokea wakati mmoja na ongezeko la mara tatu katika makazi ya Wazhizo ya baadaye yaitwayo Toutswe, huko Botswana. Ni dhahiri kwamba Wazhizo wengi waliamua kuondoka katika eneo hilo kuliko kujiunga na kundi jipya la Wakopye wa Leopard.

Baadhi ya wanaakiolojia wanaamini kuwa ueneaji wa Wakopye wa Leopard mnamo miaka ya 1000 ulikuwa sehemu ya ueneaji wa wazungumzaji wa Kibantu kutoka Afrika ya Kati kuvuka bara kubwa. Hata hivyo, ufinyanzi wa kauri wa Wakopye wa Leopard la uhusiano wa karibu na mitindo ya miaka ilcile ya Zambia na Malawi. Badala yake Kopye ya Leopard inaunda awamu ya tatu katika mfululizo wa mitindo ambayo inajumuisha pamoja ufinyanzi wa karne ya nane-tisa wa Klingbeil na ufinyanzi wa aina hiyo wa karne ya tano hadi tisa wa Transvaal ya kati. Zaidi ya haya,

kubadiliwa kwa Wazhizo wa kusini Maghribi ya Zimbabwe na Wakopye wa Leopard na tena kubadiliwa kwa watu wa Maxton Kaskazini mwa Zimbabwe katika karne ya kumi na moja na kundi linalohusiana na Wakopye wa Leopard linalojulikana kama Gumanye (zamani lilijulikana kama Zimbabwe Kipindi II na Zimbabwe ya Chini) kunaonyesha kuwa watu hawa Wakopye wa Leopard walihamia Kaskazini kupitia mto Limpopo na siyo kusini kupitia mto Zambezi.

Kopye ya Leopard na Gumanye ni sehemu ya mfululizo wa ufinyanzi wa kauri uliotajwa hapo awali unaohusisha lugha ya Kibantu na watu wa Enzi ya Chuma. Hivyo basi walikuwa ni mababu wa Washona wa siku hizi.


Mahali na aina ya maeneo ya Enzi ya Chuma na vyombo vinavyohusiana nayo vinaonyesha kuwa watu hawa walikuwa wakulima na wafugaji. Makazi mengi ya awali kabisa ya Enzi ya Chuma yalikuwa katika sehemu ambazo zilikuwa na ukaribu wa kupata maji, kuni, ardhi yenye rutuba kwa ajili ya kulima na malisho ya mifugo pia. Kwa upande mwingine, wafugaji walipendelea nyanda za majani kama vile Kalahari, wakati wawindaji-waokotezaji hapo awali waliishi karibu katika kila sehemu. Makazi ya Enzi ya Chuma yalikuwa kama ya kudumu tukilinganisha na kambi zisizo za kudumu za wafugaji na wawindaji-waokotezaji. Hali na vitu vya kisanaa katika makazi ambayo nusu ni ya kudumu ni pamoja na ghala za mashimo, ghala za vibanda vilivyoinuliwa, mawe ya kusagia, majembe ya chuma; vyote vikionyesha teknolojia iliyotokana na ukulima wa nafaka. Baadhi ya mazao halisi pia yamepatikana katika maeneo ya Enzi ya Chuma: uwele wenye karboni umepatikana Zhizo, Toutswe na Kopye ya Leopard. Wakati huo huo ulezi (*Eleusine*) na mtama (*Penisetum*) umegunduliwa Kopye ya Leopard, na jamii nyingi za kunde zinajulikana kutoka Sinoa na maeneo ya Kopye ya Leopard.

Kipengee cha ufugaji ni sehemu iliyothibitishwa katika kumbukumbu za kiakiolojia za karne ya saba mpaka kumi na moja, kwani mifupa ya mifugo (mbuzi na kondoo) na ng'ombe vimepatikana katika kila sehemu za Enzi ya Chuma zinazojulikana hadi sasa. Hata hivyo hadi hivi karibuni ilikuwa ikifikiriwa kuwa Wakopye wa Leopard ndio walikuwa watu wa kwanza Kusini mwa Afrika kuanza kufuga ng'ombe kwa wingi. Hii ilikuwa inatokana na imani kwamba kulikuwepo na aina mbili tofauti za uchumi wakati wa Enzi ya Chuma: Enzi ya Mwanzo ya Chuma iliyojikita katika kilimo na Enzi ya Baadaye ya Chuma iliyojikita katika ufugaji wa ng'ombe. Hata hivyo uchunguzi wa hivi karibu unabatilisha mgawanyo huo.


Uchunguzi mpana katika ukingo wa mashariki mwa Kalahari nchini Botswana ulionyesha kuwa maeneo yote ya Wazhizo ya karne ya nane na tisa na ya Watoutswe ya karne ya kumi na kumi na moja yana sifa za mashapo yenye maki nene ya mavi ya ng'ombe. Iliyoy ni kwamba Wazhizo ukingoni mwa Kalahari walifuga ng'ombe wengi zaidi kuliko ndugu zao Wazhizo wa mashariki. Tofauti za kiuchumi kati ya jamii za Enzi ya Chuma yaelekea zilitokana zaidi na uamuzi wa makusudi kabisa wa kutumia mazingira na nafasi za kisiasa kuliko mapokeo ya kihistoria na kitamaduni. Utafiti wa hivi karibuni umeonyesha pia kwamba karibu watu wote wa Enzi ya Chuma walikuwa na mtazamo mmoja kuhusu ng'ombe, bila kujali kuwa walifuga ng'ombe wengi au la.

Inawezekana kutumia mpangilio wa nafasi kuonyesha mfumo wa utamaduni wa makundi ya Enzi ya Chuma kwa sababu matumizi ya nafasi hutegemea utamaduni wa jamii: kila jamii inagawanya nafasi ya mazingira yake katika sehemu mbalimbali ambapo kiasi tu cha shughuli za kitamaduni huruhusiwa.

Utamaduni huu wa Kibantu wa ufugaji ng'ombe unapambanuliwa na kikoa cha amali zinazohusiana kuhusu dhima ya kisiasa ya wanaume, wema na ukarimu wa pepo wa mababu na dhima ya kati ya ng'ombe. Ng'ombe huingizwa katika miliki ya wanaume: ng'ombe ndiyo njia kuu



24.1 Makabila na utamani kusini mwa Afrika kari ya 950 na 1000. (T. N. Huffman)



**24.2** Mjumo wa utamaduni wa ng'ombe wa Wabantu: nyumba kuu kwa konyada ipo juu na nyuma ya uwanja wa wanaume; na zizi la ng'ombe ina ghala za nafaka (P) na makoburi (G). Viduara vidogo vimaonvesha ghala za nafaka za kila nyumba  
(T. N. Huffman)

ya kupatia mali na ndio msingi wa kupata wake na watoto wengi, mafanikio, hadhi na madaraka. Hivyo, nyumba ya mwanaume inakuwa katikati ya makazi ndani au karibu na zizi la ng'ombe la jumbe. Jumbe na watu wengine muhimu huzikwa katika sehemu hiyo. Vibanda vya wake wa mtu hujengwa kuzunguka sehemu hiyo ya katikati kufuatana na mfumo wa hadhi unaojionyesha kupitia matumizi ya nafasi ya kushoto na kulia. Kwa upande mwingine mielekeo ya mambo ya kilimwengu na shughuli za mambo ya kidini huamua ni kipi kitakuwa katika nafasi ya mbele au ya nyuma. Mbele ya nyumba na anakazi hupangwa mambo ya kilimwengu wakati ambapo sehemu ya nyum a huwekwa kwa ajili ya mambo ya siri na mambo ya kidini. Kwa kuwa mpishano wa mambo ya kidunia na yale ya kidini umepangwa takribani katika pembemraba na yale yanayohusiana na hadhi, mtu muhimu kuliko wote huwekwa nyuma ya makazi katika sehemu yenye usalama. Iwapo sehemu ya mbele ya makazi inatazama mteremko, umuhimu wa hadhi na taratibu za dini pia utadhihirishwa na mwimo.

Ruwaza hii ya kawaida inahusu vikundi vingi tofauti vya kimbari vya Kusini mwa Afrika, lakini haipo miongoni mwa Wabantu wanaofuata utaratibu wa kukeni waliopo Afrika ya Kati, ambao hufuga ng'ombe wachache sana, na wala haipo miongoni mwa wafugaji wasiozungunza Kibantu wa Afrika ya Mashariki. Badala yake, ruwaza hii inajitokeza miongoni mwa Wabantu wanaofuata utaratibu wa kuumeni ambao hubadilisha ng'ombe ili kupata wake. Kuwepo kwa ruwaza hii kwenye rekodi za kiakiolojia ni ushahidi tosha wa mfumo wa awali wa kipekee wa Kibantu unaohusu siasa na ng'ombe.

Kwa kutumia ushahidi wa namna hii utamaduni wa Wabantu wa ufugaji ng'ombe huko Kusini mwa Afrika unaweza kufuatiliwa nyuma kuanzia enzi za historia na kurudi moja kwa moja hadi karne ya saba. Sifa za uchunguzi wa kuyakinisha za ruwaza za maeneo zimeainisha makazi ya kuta za mawe ya karne ya kumi na nane, ambayo yanahusishwa na Wandebele wa Transvaal ya Kaskazini; makazi ya kuta za mawe ya karne ya kumi na sita hadi kumi na nane, ambayo yanahusishwa na wasemaji wa Kisotho-Tswana; Moloko (jina la kiakiolojia la tasnia ya ufinyanzi ya Wasotho-Tswana) ya karne ya kumi na nne hadi kumi na sita ambayo haikuwa na kuta za mawe; maeneo ya Woolandale ya karne ya kumi na mbili hadi kumi na nne; makazi ya Wazhizo ya karne ya kumi hadi kumi na mbili, ikiwa ni pamoja na yale yanayodhihirika kuwa makundi madogo ya akina yakhe. Sifa hizi za uchunguzi wa kuyakinisha zinaonyesha kwamba katika Enzi ya Mwanzo ya Chuma Wazhizo walikuwa na mielekeo ya msingi kuhusu ng'ombe sawa na ile ya Wanguni wa kipindi cha historia. Wakati huo huo uchunguzi umeonyesha kuwa ufugaji na kilimo vilikuwa vipengee vya mfumo mmoja vilivyokamilishana: hapakuwa na aina tofauti za kiuchumi baina ya Enzi ya Mwanzo na Enzi ya Baadaye ya Chuma.

Kuelewa kwetu utamaduni wa Kibantu wa ufugaji ng'ombe kunaweza kutumiwa kufasili matukio na mabadiliko muhimu ambayo yalitokea katika eneo la Shashi-Limpopo. Kiasi cha ukubwa wa makazi ya utamaduni wa Kibantu wa ufugaji ng'ombe ni matokeo ya moja kwa moja ya nguvu ya kisiasa. Makazi makubwa zaidi yanaashiria umuhimu au nguvu ya mtawala aliyekuwapo. Mpaka sasa makazi ya Wazhizo yaliyo makubwa zaidi na yenye umuhimu mkubwa wa kisiasa kuliko sehemu nyingine yoyote ni yale ya Shiroda (*Schroda*), kusini-mashariki ya mpaka wa leo kati ya Zimbabwe, Botswana na Afrika ya Kusini. Makazi makubwa kabisa ya Wakopye wa Leopard yanayo-Julikana ni K2, karibu kilometa sita kusini-Maghrabi ya mji mkuu wa mwanzo wa Wazhizo.

Wakati fulani K2 ilifikiriwa kuwa ni makazi ya Wakhoisan zaidi kuliko Wabantu. Lakini uchambuzi wa hivi karibuni umeonyesha kuwa watu wa K2 walitokana na Wanegro, kama zilivyofanya jamii za Wakopye wa Leopard na za Eiland, ikiwa ni pamoja na Wazhizo na Washiroda. Fasili hii iliyo tofauti sana ya Enzi ya Chuma ni matokeo ya makusanyo-linganishi

mazuri zaidi, na njia nzuri zaidi za uchambuzi. Ushahidi unaotokana na mifupa sasa unajaliza ule wa mtindo wa ufinyanzi wa kauri na mpangilio wa makazi na inaonyesha kuwa watu wa K2 na Shiroda walikuwa Wanegro.

Watu wa K2 na wa Shiroda huenda walivutiwa kwenda sehemu za Shashi-Limpopo kwa sababu ya mazingira mazuri ya ufugaji na kilimo. Kwa kuongezea tu, pori la Mopani kati ya mito hiyo miwili ni nchi yenye tembo wengi na pembe za tembo zingeweza kupatikana kwa urahisi; hata hivi leo eneo hilo lina pembe nyingi. Zaidi ya hayo mito inayobomoa miamba ya mashariki ya dhahabu huko Zimbabwe huingia katika makutano ya mto Shashi na Limpopo na kwa hiyo ingewezekeza kupata dhahabu katika ujirani wa Shiroda na K2.

### *Biashara na siasa: 1000-1075*

Ushahidi wa kiakiolojia kuhusu maingiliano kati ya wafanyabiashara wa pwani na watu wa Enzi ya Chuma katika eneo la Shashi-Limpopo uko wazi. Kwa kweli Shiroda ya karne ya kumi na tisa ndilo eneo la awali kabisa Kusini mwa Afrika kutoa idadi kubwa ya shanga za vioo na pembe za ndovu; K2 imetoa pembe za ndovu na shanga za vioo zaidi kuliko makazi mengi ya wakati huo huo yakikusanywa pamoja. Aidha wanaakiolojia nchini Msumbiji hivi karibuni wamegundua kituo cha biashara pwani kilichotumika karne ya nane hadi ya kumi na mbili ambacho huenda ndiyo kilitoa kwanza shanga za vioo kwa Shiroda na kisha K2.

Uchunguzi wa uwanda wa pwani katika eneo la Ras ya Vilanculos na visiwa vya Bazaruto umegundua maeneo yenye ufinyanzi wa Kiajemi na vioo vya Kiislamu. Uchimbuzi wa awali katika moja ya maenco haya, yaani hapo Chibucne, uligundua mabaki ya karne ya nane na tisa ya vyombo vya vioo vinavyong'aa na visivyong'aa kama vile vya vipindi vya awali vya Kilwa na Manda. Machimbo haya ya awali ya Enzi ya Chuma pia yalitoa shanga za vioo vya njano, kijani na buhuu kama zile za Shiroda na K2. Eneo la Vilanculos linaonyesha kuwa lilikuwa na vituo vya awali kabisa vya biashara kusini-mashariki mwa Afrika, na eneo la Shashi-Limpopo linaonyesha kuwa lilikuwa moja kati ya maenco ya kwanza ya Kusini mwa Afrika kujihusisha na mfumo wa biashara wa Bahari ya Hindi.

Tunajua kutokana na vyanzo vingine kuwa shanga za vioo, nguo na vyombo vya ufinyanzi vinavyong'ara vililetwa Kusini mwa Afrika kutoka Uchina na Mashariki ya Kati kwa kubadilishana na dhahabu na pembe. Jambo muhimu ni kuwa bidhaa zilizoingizwa zilikuwa tofauti na utajiri wa asilia wa ng'ombe angalau kwa namna moja.

Katika uchumi wa kimapokeo wa Zhizo na Kopye ya Leopard, kila mara ng'ombe walikuwa katika umiliki wa mzunguko ili kuimarisha mfumo huo. Matajiri waliwakopesha masikini ng'ombe, na matajiri kwa masikini walibadilisha ng'ombe na wake. Kwa hiyo utajiri wa kimapokeo usingeweza kukiritimbwa bila kuharibu mfumo wenyewe. Kwa upande mwingine, mgawanyo wa dhahabu, pembe za ndovu, shanga za kioo na nguo viliweza kumilikiwa na watu wachache bila kuudhoofisha uchumi kwa sababu bidhaa hizi ziliweza kuhifadhiwa bila matatizo. Kwa kuwa bidhaa za biashara ziliagizwa kutoka nje kwa wingi watawala wa kijadi walitokea kuwa matajiri sana. Katika mfumo wa kimapokeo utajiri na nguvu ya kisiasa vilikwenda pamoja kwa kuwa, mbali na sababu nyingine, kadri chifu alivyozidi kua wake wengi na kutoa mikopo mingi kwa masikini, ndivyo alivyozidi kupata marafiki wengi na ndivyo alivyozidi kutiwa na raia zake. Kwa mujibu wa hati za baadaye za Wareno, baadhi ya bidhaa za biashara zilitumiwa kwa kulipia mahari, ndiyo kusema bidhaa hizi zilipofasiliwa katika muktadha wa amali za jamii utajiri wa biashara pia uliongezwa nguvu ya kisiasa.



Watu wa Kopye ya Leopard walipohamia eneo la Shashi-Limpopo pengine waliondoa biashara pembe za ndovu kutoka Shiroda kabla utajiri wa biashara haujaiathiri sana jamii ya Wazhizo. ata hivyo, ongezeko la ajabu la nguvu za kisiasa walizopata watawala wa K2 linaakisika katika aratibu wa utumiaji maeneo. Mwanzoni K2 ilikuwa na utaratibu kama wa Shiroda: nyumba ya yifu ilizungukwa na vijumba vidogo vidogo na mazizi yake. Lakini hadi kufikia mwaka 1020 zizi la g'ombe (pamoja na mavi ya ng'ombe) la chifu likawa kubwa kiasi cha kumeza zizi la ng'ombe ilokuwa jirani. Karibu wakati huo huo ng'ombe waliondolewa katika eneo la kati. Kutolewa huku wa ng'ombe katika eneo la kati kulikuwa ndiyo badiliko la kwanza katika mpangilio wa maeneo utika utamaduni wa Kibantu wa ufugaji ng'ombe; nako kukawa na athari ya moja kwa moja ya ongezeko la shughuli za kisiasa na mabadiliko yaliyohusiana nazo katika thamani ya kiuchumi ya g'ombe.

Hadi kufikia mwaka 1075 bonde mwinuko ambamo ndimo K2 ilimokuwa likawa metamakaniwa kabisa. Machimbo ya hivi karibuni na ukadiraji tarehe kwa kutumia radiokaboni imeonyesha kuwa uachaji ghafla wa K2 wakati huu ulitokea sawia na ongezeko la papo kwa papo watu wa K2 katika eneo la Kilima cha Mapungubwe, umbali wa chini ya kilometa moja. Kwa jwa kulikuwa na nafasi zaidi ya makazi katika eneo la Mapungubwe, hatutakuwa tunakwenda ibali sana tukifikiria kuwa mji mkuu ulihamishiwa hapo ili kupata nafasi zaidi kwa ajili ya ongezeko watu. Yawezekana kwamba uwanja wa asili wa duara chini ya Kilima cha Mapungubwe ndio lichukua eneo la nyumba mpya ya chifu kwa sababu hili ndilo eneo kubwa peke yake lilokuwa atikati ya mji ambalo halina mabaki ya makazi. Kutokuwepo mavi ya ng'ombe mahali popote atika eneo hili kunaonyesha kuwa zizi halikujengwa karibu na nyumba ya mtawala; hii ikiwa na ana kwamba mabadiliko ya mpangilio wa maeneo yaliyofanyika katika K2 yaliendelezwa Mapungubwe. Mabadiliko ya baadaye ya mpangilio wa maeneo yanaonyesha kwamba asili ya utamaduni wa Zimbabwe ilikuwa ni mahala hapa na siyo pale ilipo Zimbabwe Kuu yenyewe.

### *Mapungubwe, mji mkuu wa kwanza wa Zimbabwe: 1075 - 1220*

Taratibu wa utamaduni wa Zimbabwe unatofautiana kwa njia nyingi na ule mtindo wa Kibantu wa fugaji wa ng'ombe. Mfalme aliishi katika boma lililozungushiwa mawe mlimani juu siyo chini ya ulima; watu bora walizikwa mlimani, siyo chini kwenye zizi; wake wa mfalme waliishi katika maeneo yao na siyo pamoja na mfalme, na watu mashuhuri walikuwa na makazi ya fahari katika iunga vya miji mikuu. Haya yote, pamoja na sifa nyingine, yalitokea kwa mara ya kwanza Mapungubwe.

Wakati mji mkuu ulipowekwa Mapungubwe, chifu na mali yake alihamia mlimani juu ya eneo ke. Uhamaji huo kutoka katika mwinuko kwenda mlimani ni wa kwanza Kusini mwa Afrika katika ipindi cha kabla ya kuandikwa kwa historia na unaonyesha kuwa viongozi walitengana kabisa na pia wao na ni dalili za kwanza za muundo wa matabaka.

Muda mfupi baada ya kuhama kutoka K2 kwenda Mapungubwe, mtindo wa ufinyanzi wa K2 lianza kubadilika. Wengine wanaweza kusema kuwa mabadiliko haya yalikuwa ishara ya kutokea wa watu wapya lakini yawezekana kuwa yalisababishwa na kuzuka kwa wafinyazi wa kudumu waliotokana na ongezeko la watu na kuzuka kwa matabaka.

Ushahidi mwingine wa kisanaa unaonyesha kuwepo kwa maingiliano na wafanyabiashara wa wani. Mashine za kufuma zinajitokeza miaka ya 1100 Mapungubwe. Kwa vile ufumaji wa pamba likuwa tayari ukifanyika katika miji ya Waswahili kwa wakati huu, mashine za kufuma katika Mapungubwe, ambazo ni za kwanza kabisa zinazojulikana bara, zinaashiria mwanzo wa ufumaji wa

wafanyabiashara wa pwani na pengine kuanza kwa stadi nyingine ya kiufundi.


Mwanzoni mwa biashara, dhahabu ilikuwa ni njia ya kupata utajiri kuliko kuwa ndiyo ukwasi wenyewe, lakini mnamo 1150 vyombo vya dhahabu vilikuwa vikitengenezwa nchini humo, vifaa maalumu kama vile sanamu za vifaru na fimbo ya kifalme iliyotengenezwa kutokana na vibambo vyembamba vya dhahabu vilivyopigiliwa katika sehemu ya katikati ya fimbo vilipatikana katika makaburi ya watu bora katika kilima cha mfalme. Hii ni mara ya kwanza dhahabu kutumika kama alama ya hadhi Kusini mwa Afrika na hivyo ushahidi wa awali kuonyesha kuwa dhahabu ilikuwa na thamani yake katika sehemu hizi.

Wakati huu utaratibu wa Mapungubwe wa nafasi ulibadilishwa katika sulubu mpya ambapo kuta za mawe ziliweka mipaka ya maeneo muhimu. Nyumba moja ya kuta za mawe ilionekana karibu na baraza chini ya mlima. Makazi haya bila shaka yalikuwa ya diwani mkuu, mtu ambaye katika utamaduni wa Zimbabwe alitayarisha mashauri yote ya baraza na mipango ya kuonana na mfalme. Ngazi kuu iliongoza kutoka eneo hili kupitia kijia chembamba mpaka juu ya mlima: matundu mawili katika mawe ya udongo laini huenda yalikuwa na vipandio vya mbao, na ufupi na urefu wa kuta ulikuwa ni alama ya upeo wa juu wa njia. Matundu zaidi mlimani huenda yaliegemewa na wigo uliozunguka mlima na kuongoza watu upande wa kulia wa makaburi. Upande wa kulia vibanda vingi vilijengwa mbele ya nusu duara ya ukuta wa mawe ulio mvingo ambao ulizingira vibanda kadhaa. Seladoni adimu ya Kichina katika vibanda hivi pamoja na ukuta wa mawe vyaonyesha kuwa mfalme aliishi hapo. Vibanda vilivyoko upande mwingine vimeonyesha kuwepo kwa mawe ya kusagia kutoka mlimani, na hivyo kuonyesha kuwa huenda vilikalifiwa na wake wa mfalme. Hivyo basi mtindo mpya ulijumuisha mpambanuo kati ya makazi ya wake wa mfalme na yale ya mfalme na watumishi wake.

Mtawanyiko wa takataka zinazotokana na kazi za kiuchumi unaonyesha kuwa watu wengi walikaa upande wa Maghribi wa ukuta, lakini familia chache zilikaa uwanda wa juu nje ya mji. Katika sulubu za ufugaji wa ng'ombe wa Kibantu, wanaume waliokuwa wanagombania uchifu, kama vile ndugu, wajomba na watu wengine mashuhuri katika koo, kwa kawaida waliishi nje ya mzingo wa ulinzi uliofanywa na wafuasi wa karibu wa chifu. Kwa kiuwa mashindano kama haya yangeweza kuwepo Mapungubwe, inawezekana kuwa majumba ya fahari kuzunguka ukingo wa mji yalikalifiwa na watu maarufu. Nyumba hizi muhimu ni sawa na makazi ya watu bora wa mlimani; mbali kidogo kutoka Mapungubwe: kwa mfano Little Muck, umbali wa km 13, Mmangwa, km 40 Maghribi; Kilima cha Mapela, km 85 na Kilima cha Macena km 96 Kaskazini mashariki. Makazi haya tofauti yametoa ushahidi kamili wa kiakiolojia katika mifano mitatu ya urasimu wa kisiasa: maeneo ya uwanda wa chini huenda yalikalifiwa na watu wa kawaida; kilima kidogo huenda kilikalifiwa na viongozi wa wilaya; na makao makuu ya Mapungubwe ndipo penye hatamu za utawala. Makazi ya walio bora nje ya mji huenda yalikuwa miji ya nyumba za viongozi wa wilaya. Hivyo basi, muundo wa tabaka katika jamii ya Mapungubwe unajidhihirisha katika mgawanyiko wa makazi ya utaratibu wa kuishi katika makao makuu.

Mkururo wa mabadiliko kutoka K2 mpaka Mapungubwe na mambo yanayolingana kati ya Mapungubwe na Zimbabwe Kuu yanaonyesha kuwa utamaduni wa Zimbabwe ulitokana na utamaduni wa Kibantu wa ufugaji ng'ombe wa eneo la Shashi-Limpopo. Kutokana na hali hii Mapungubwe yaweza kuchukuliwa kuwa ndio uliokuwa mji mkuu wa kwanza wa Zimbabwe.

Mkururo huu pia unadhihirisha dhima za dini na ng'ombe katika kuendeleza utamaduni wa Zimbabwe. Baadhi ya wanahistoria wanaamini kuwa Wambire walikwenda kusini na kuvuka mtc Zambezi na kuendeleza ufalme wa Zimbabwe kupitia uwezo wa dini yao kabla ya kuanzishwa kwa biashara ya dhahabu na watu wa pwani. Ushahidi wa kiakiolojia upo wazi kwamba mguro muhimu



## *Bukini*

Historia ya Bukini kabla ya + 1000 na wakati mwingine hata kabla ya + 1500, imeonekana kutokuwa na uhakika na yenye ukinzani mwingi kutokana na nadhariatete zilizotolewa kw muda mrefu bila kufikia makubaliano ya jumla. Vyanzo vya maandishi vilivyotambulish kisiwa hicho vinaturejesha nyuma mpaka karne ya kumi na mbili, na utaalamu wa kiakioloji umetokea hivi karibuni mno kiasi kwamba umeshindwa kutupa matokea ya kihistoria katik misingi inayokubalika. Matumizi ya vyanzo ambavyo si vya Kimalagasi, tokea maandishi y G. Ferrand, yameishia katika kazi zilizoandikwa kwa lugha ya Kiarabu tu.

Hivyo basi, tumejaribu kutumia vyanzo vya masimulizi vya aina zote ambavyo vinapatikana sasa Bukini. Vimeweza kudumu katika mazingira tofauti. Wakati mwingine, has kwa upande wa kusini mashariki, vimejumuishwa katika hati zilizoandikwa kwa Kiarabu eh Kimalagasi (Volan Onjatsy au Sorabe); wakati mwingine vimepatikana katika umbo la mabak ambayo ni vigumu kuyafasiri; katika vyanzo ambavyo vimebadilishwabadilishwa sana; n wakati mwingine vimetumika katika kafara ambazo bado zinafanywa mpaka leo na mwishu vimesambaa sana katika vyanzo ambavyo muktadha wake haueleweki vizuri.

Kama ilivyo katika sehemu nyingi, vyanzo hivi vinahitaji njia mahususi za kufuata. Kw mfano, kwa upande wa Bukini isimu huchukua nafasi muhimu sana katika kupata taarifa z kihistoria kutokana na simulizi. Ulinganifu mkubwa uliopo kati ya lugha ya Kimalagasi unaotokana na msingi wa umoja wa Kiaustronesia, unafanya iwezekane siyo tu kutambua kw urahisi maneno ya mkopo kutoka lugha nyingine na kuweza kuyapanga kikronolojia katik historia ya utamaduni wa nchi hiyo, bali pia kuchunguza mapokeo yoyote yaliyoingizw kwenye Kimalagasi.

### *Visakale vya "majitu" kama chanzo cha taarifa*


Kuna taarifa ambazo hazijawekwa pamoja kuhusu "majitu", miongoni mwa "majitu" hay yaliyo muhimu ni kama vile Darafify, Darofipy na Darafely Fatrapaitan(ana). Masimuliz yaliyokamilika na yaliyo sahihi ni yale ya ngano ya Darafify yaliyo katika muswada wa sorab uliohifadhiwa kule Oslo na kuhaririwa mwaka 1982 na Ludwig Munthe. Mchanganuo wak unatuwezesha kugundua baadhi ya mazingira ya kisiasa na kijamii ya kurithishwa kwake n kutokana nayo tunaweza kupata amali muhimu za taarifa ya kihistoria. Taarifa ya kwanza iliy wazi inapatikana kutokana na majina ya 'majitu' tuliyotaja: majina haya yanatokana n mehangananyiko wa maneno ya Kiaustronesia, Kisanskriti na Kiajemi, na yote yanahusiana r

wa kimbari ulikuwa kutokea kusini na kwamba masuala ya kafara yaliyowazunguka wafalme wa Zimbabwe, yalikwenda sambamba na, siyo kwamba yalitangulia, biashara ya nje na maendeleo ya nguvu za kisiasa. Hivyo basi, nguvu za dini mpya hazingeweza kuwa ndizo chanzo cha utamaduni wa Zimbabwe.

Wataalam wengine wa historia ya Afrika wanaamini kuwa utamaduni wa Zimbabwe ulikua kutokana na umilikaji ng'ombe na mikakati ya malisho katika maeneo makubwa. Imetolewa hoja kwamba kwa vile mifugo iliongezeka, dhana ya mali binafsi iliegemea kwa kuwa na ng'ombe. Kwa kuwa mikakati ya malisho bora ya mifugo hii mingi ilikuwa mzingo wa mapito ya ubinadamu, kufuatana na nadharia hii tete, ilikuwa muhimu kudhibiti malisho ya mbali na hali hiyo ikalazimisha kuendelezwa kwa madaraka ya kisiasa mahali pamoja. Hoja ya kwanza dhidi ya fasili hii ni kwamba mifugo ya ng'ombe haikuongezeka ghafla kabla ya kuendelezwa utamaduni wa Zimbabwe, kwani mashapo makubwa ya mavi ya ng'ombe na utaratibu wa makazi ya Wazhizo ya karne ya saba vinaonyesha kuwa jamii za kufuga ng'ombe zilikuwepo angalau miaka mia nne kabla ya kuanzishwa kwa Mapungubwe. Hoja yangu ya pili kuhusu fasili hiyo inahusu mzingo wa mpito wa ubinadamu. Hifadhi nyingi zilizokaliwa na watu wa kawaida na mashapo mengi ya kinyesi cha ng'ombe katika eneo la Mapungubwe ni kinyume cha uwezekano wa kuwepo na miguro mingi ya ng'ombe na watu katika malisho ya mbali kwa vile mabaki yanayoonekana yanaonyesha kuwa makazi haya yalikuwa ya kudumu kama yale ya jumuiya za Enzi ya Mwanzo ya Chuma.

Muhimu zaidi kuliko makosa haya ni mkanganyiko kati ya uunganifu wa kisiasa na mabadiliko ya kisiasa. Jamii mbalimbali za wafuga ng'ombe Kusini mwa Afrika zilikuwa na mamlaka mahali pamoja kama vile Wabamangwato, Wamatebele, Wazulu na Waswazi na bado jamii hizi zilikuwa na amali za kitamaduni kama jamii nyingi za Wabantu wa Kusini, na hivyo, makazi yao yalikuwa bado yakifuata utaratibu wa misingi kama ile ya K2 na Shiroda. Hivyo basi ni dhahiri kuwa utajiri wa kibinafsi wa ng'ombe unawezekana kuwa ulikuwa ni wa lazima katika mabadiliko ya Zimbabwe akini haukujitosheleza peke yake.

Hivyo, si ng'ombe wala nadhariatete ya dini inafafanua data za sasa. Nadhariatete ya biashara imilifu, kwa upande inwingine, inadhihirisha kuwepo kwa muda mrefu wa ufugaji wa ng'ombe kabla ya kukua kwa Mapungubwe, na kisha marekebisho yake na kuendelea na utamaduni wa ufugaji ng'ombe wa Wabantu katika sehemu nyingine Kusini mwa Afrika. Kama sura hii livoonyesha, mageuzi ya K2 na Mapungubwe yaliyoleta utamaduni wa Zimbabwe yalikuwa ni natokeo ya kuongezeka kwa nguvu za kisiasa kulikosababishwa na kuwepo kwa biashara ya hababu na pembe.



25.1 Madagascar na Comoro . (B. Domenichini-Ramiaramanana)

biashara ya viungo, manukato na dawa za mitishamba. Hivyo basi, yanarejelea kipindi cha maingiliano baina ya Bukini na maeneo ya Bahari ya Hindi kabla ya Uislamu na kupendekeza nadhariatete kuwa mashariki na sehemu za kusini mashariki ya kisiwa hicho cha Bukini zilishiriki katika shughuli za biashara katika Bahari ya Hindi kabla ya karne ya saba.

Daraffify, Darofipy, Darafely Fatrapaitan(ana) yametokana na maneno ya kawaida ambayo bado yanatumika katika Kimalagasi na tunahitaji kuchunguza jinsi yanavyotumika. Fi/m/py/fify yanahusiana na chakula, vipodozi na madawa. Aina hii ya mwisho ya bidhaa ilikuwa ni pamoja na bidhaa zinazotokana na wanyama zilizoletwa zaidi kutoka Murex na hasa za Murex trunculus, ambazo bado zinatumiwa, katika hali ya ungaunga, kusini Maghribi. Kwa upande mwingine, ni mazao ya mboga yanayotokana na miti midogo (magamba na utomvu wa Haematodendron au Mauloutchia), lakini huenda pia kutoka katika mzizi wa mazao mengine ya mimea. Hali kadhalika katika kundi la fi/m/py/fify kulikuwa na aina tofauti ya pilipili mwitu (Piper borbonese DC) ambayo sasa yajulikana kama 'pilipili nyekundu-nyeupe' (Piper pyriofolium Vahl na Piper pachyphyllum). Mwisho kabisa kulikuwa na 'benjamin' (Fatra au Sytrax benzoin Dryander) ambayo inakumbukwa kwa jina la Fatrapaitan (ana) kubwa lakini ambayo haionyeshi kuwa ndiyo iliyokuwa zao muhimu la kusini-mashariki ya Bukini lililokuwa likisafirishwa nje, kwani yaonekana kutokana na jina hili kipimo cha 'benjamin' (fatra) kilikuwa ni zawadi ya mnunuzi baada ya mauzo kumalizika (paitanana). Zao kuu pengine lilikuwa fimpy ambalo wataalamu wa elimu-mimea wamebaini kuwepo kwake kwa wingi kusini mashariki mwa Bukini.

Kuna mazao mengine pia ambayo yanajitokeza katika vyanzo vya 'Mzunguko wa Daraffify,' lakini majina yake hayakutumika kama yalivyotumika yale ya awali kuwaita majitu. Majina yao halisi (ha)ramy' (Canarium Bukiniense; C. boivini na C. multiflorum Engler) leo yanajulikana kama 'uvumba wa Bukini' au 'uvumba mweupe wa Kiafrika.'

Isimu inaonyesha kuwa kuna uhusiano wa kirazini kati ya majina ya wahusika katika 'visakale' ambao hurejea katika historia dhahania ya zamani na mimea pamoja na mazao ya thamani ya Bukini, hasa katika sehemu za mashariki za kisiwa hiki. Tunahitaji kujua kama haya tunayoyataja juu juu tu kupitia ngano yana ukweli halisi wa kihistoria, na kama inawezekana kuyaweka katika kronolojia na iwapo kronolojia hiyo inaingia vizuri katika kronolojia ya biashara katika Bahari ya Hindi. Kwa upande mwingine, tunahitaji kudhibirisha, kwa uwezekano wa kikronolojia, historia ya uhusiano wa madaraka kati ya makundi ya kipindi cha kale cha kisiwa hiki.

Majina ambayo tumeyataja hivi punde ni magumu kutumia kihistoria. Kila moja ni mkusanyiko wa ishara na sio majina binafsi ya mashujaa wa kihistoria. Wakati tunazungumzia 'Daraffify,' 'Darofipy' na mengine, tunakuwa tunazungumzia matukio mengi ya kihistoria katika kisiwa hiki ambayo huenda yalikuwepo kabla ya karne ya kumi na moja. Lakini pia yanaelezea juu ya kundi maalumu katika kipindi maalumu cha historia yake, kwa mfano lilipojaribu kuzalisha na kuuza nje mazao fulani fulani; wakati mwingine, au katika mazingira mengine, kikundi kile kile huenda kilikuwa na jina jingine.

Huenda itakuwa vigumu kuhitimisha kwa haraka moja kwa moja, kwa misingi ya sifa chache, ambazo haziwezi kupingwa kihistoria, zinazopatikana katika 'mzunguko wa Daraffify' na ambazo zinahusiana na historia ya ndani ya kisiwa, kuwa historia ya Bukini inawcza kuandikwa kutegemea sifa hizo. Sifa hizo ni sehemu muhimu sana katika kuelezea historia ya Bukini. Lakini hawa 'Daraffify' waliokuja kutoka Kaskazini mashariki, na ambao inasemekana walliamua kukimbia, katika kipindi ambacho ni vigumu kuelezea, kutoka katika maeneo yao ya

mapokeo ya ufugaji wa ng'ombe, ambayo simulizi zinasisitiza kuwa yalikuwa yao, walikuwa watu gani? Inasemekana walijishughulisha, ama kwa hiari au kwa nguvu, na biashara kutegemea mahali na hali ilivyokuwa (mara ngapi? kwa kiwango gani?), biashara ambayo inaweza kuwa ilihusu uchukuzi (kwa kutumia walanguzi wa Kiaustronesia (?) au wa Kiajemi?) wa bidhaa kutoka pwani ya mashariki ya Bukini na kuzipeleka katika ulimwengu wa Kaskazini ambako zilikuwa zikihitajika.

Eneo ambalo kundi shupavu la Darafify lilipotaka kujinyakulia ukiritimba wa biashara liliingilia linaainishwa kwa ufynyū zaidi, siyo tu na sehemu ambako matukio hayo yalirekodiwa, bali pia na sehemu mafanikio ya kundi hilo bado yanaonekana na karibu yote haya yanahusiana na kazi za machimbo ya mawe na utengenezaji bidhaa. Eneo hili, ingawa linaendelea mpaka Mahafale kusini Maghribi, lilianza Kaskazini kabisa ya kisiwa hiki hadi katika bonde la Matatana(na). Eneo lote la mwambao wa mashariki wa kisiwa cha Bukini ambalo ni tajiri katika manukato, viungo vya chakula, marashi na madawa ya miti shamba, na jinsi vitu hivi vilivyopatikana (uzalishaji na uuzaji) pia vinajitokeza wazi kutokana na kuyafasiri majina halisi.

## Akiolojia

Woto wa sasa wa Bukini kwa kawaida hufikiriwa kuwa matokeo ya shughuli za binadamu. Kupotea kwa baadhi ya wanyama ambako kunakisiwa kulitokea mwanzoni mwa kikwi cha sasa (komba wakubwa, mbuni wakubwa au Aepyornis, mamba wakubwa, kobe wakubwa, viboko wafupi, n.k.) kunaonyesha kuwa kulikuwa tayari na mabadiliko katika misitu. Pia lazima ikumbukwe kuwa katika baadhi ya maeneo kutoka katika enzi yetu (Lamboharana, +730 + 80; Taolambiby, +900 + 150; na Ambasambazimba, +915 + 50), masalia ya tasnia za binadamu yamepatikana pamoja na mabaki ya wanyama hawa.

Upandaji wa spishi za thamani na uzoeshaji mazingira mageni wa mimea mipya, bila shaka, ulifanywa kabla ya uharibifu wa misitu uliosababishwa na watu wa utamaduni wa misitu au pengine na watu waliokuwa wakitangatanga wakitafuta ardhi ya kulima, ambao kwa kawaida walikuwa waangalifu wasiharibu udongo na hali ya awali ya mimea. Utafiti wa kiakiolojia umegundua eneo moja tu ambalo linaenda nyuma zaidi ya kipindi kinachozungumziwa sasa (Saradrano, eneo la wavuvi kusini Maghribi, +490 + 90), lakini kwa upande mwingine, umeonyesha baadhi ya mambo yanayojitokeza katika kipindi kinachozungumziwa. Maeneo haya yamedhihirisha wazi baadhi ya taarifa zilizofasiriwa kutokana na simulizi ambazo nazo zinaleta uwezekano wa kupata ufafanuzi bora zaidi kutokana na uchambuzi na utafiti.

Kwenye eneo la Kaskazini ambako mapokeo yanaonyesha kuwa ndilo lilikuwa eneo asilia la Wadarafify, katikati ya Bobaomby na Daraina, chini ya ghuba, inapatikana Irodo, ambalo ndilo jina la kijiji kilichopo leo katika mto unaoingia baharini kupitia ghuba hiyo. Kwa vile hakuna uhakika wa uchanganuzi, hakuna uthibitisho au kukataa uvunaji wa dara na mimea mingine ya biashara inayokumbukwa kama Daraina, ('zao lililotoa dara''mahali penye dara nyingi').

Maeneo matatu wa pwani ambayo yamefanyiwa uchunguzi yamebainisha watu wenye utamaduni sawa ambao, kwa mujibu wa maelezo ya Verin, unaji-pambanua kwa mitindo ya ufynyanzi (vyungu, magudulia na mabakuli yenye miguu), matumizi ya kloriti-shisti (vyungu na mabakuli) na utumiaji wa Pyrazus palustris. Eneo hili, ambalo lilikuwa linatumika mpaka

katikati ya karne ya kumi na tano, lilikuwa tayari likitumika katika karne ya tisa au labda ya nane. Katika zama za awali, wavuvi walijua kufua chuma na vioo walikuwa na uhusiano na maeneo ya biashara ya Kiajemi - Kiarabu. Kati ya makombe ya pwani (*Pyrazus palustris*, *Ostrea mytolooides*, Turbo, n.k.), bila shaka kwa ajili ya chakula na kazi za ufundi (vijiko vilitengenzwa kutokana na Turbo), kunapatikana, ingawa kwa kiasi kidogo, *Murex* inayotoa fimpy, manukato ambayo bado yanatakikana leo na Waislamu wa Kihindi huko Bukini, na ambayo jina lake linapatikana kama tulivyoona katika jina la Darafify.

Maeneo mengine ambayo kwa kiasi fulani yamo katika kipindi tunachozungumzia yanaweza kupatikana kusini zaidi ya kisiwa katika eneo la sasa la Antandroy. Haya yamo katika makundi mawili kwenye kingo za mto Manambovo: lile la eneo la Talaky ambalo linachukua pande zote za mahali ambapo mto unaingia baharini; na lile la eneo la Andranosoa ambalo sehemu yake inakaliwa na Manda (n-d) - Refilahatra katika makutano ya mto Manambovo na mto Andranosoa. Kwenye vikundi hivi viwili tunaweza kuongeza mto wa juu zaidi wa eneo la Andoro, unaochanganya Mahirane na Ambonifanane, kundi ambalo halijapewa tarehe maalumu lakini lina utamaduni ule ule wa maeneo yenye udongo laini na ngome za mawe kama Manda (n-d) Refilahatra-Andranosoa na linarudi nyuma hadi kwenye kipindi ambacho, katika sehemu zilizokaliwa, spishi mbalimbali za mabaki ya mifupa bado zinaweza kupatikana.

Kama ilivyo kwa vyanzo vya maandishi, vyanzo vya simulizi, ikiwa ni pamoja na mzunguko wa Darafify, havisemi lolote kuhusu maeneo haya, ambayo watu wake wametoweka bila kuacha alama zozote, ambayo wakazi wake wa sasa hawajui lolote kuhusu wahenga wao wa zamani za kale. Ukadiriaji umri kwa kutumia radiokaboni unaonyesha kipindi cha + 940 mpaka + 1310 kuwa ndiyo mpaka ya mwisho, pamoja na uwezekano wa karne ya kumi na moja.

Hata kama huenda kusini kulikwishaathiriwa na mwanzo wa ukame katika kipindi hiki, ni lazima kulikuwa na hali ya hewa tofauti katika karne ya kumi hadi kumi na moja. Eneo lenye misitu lilileta uwezekano wa kujiingiza katika uchumi uliojicgemeza, kwa kiasi fulani, katika ufuaji shaba na chuma; na mashapo ya metali hizi yameonekana, lakini tofauti na mashapo ya shaba katika eneo la Bemarivo lililopo Kaskazini, alama za uchimbaji wake wa kale zimeonekana. Hata hivyo, shaba, ambazo katika kipindi cha baadaye zilikuwa na thamani zaidi, zilisababisha utengenezaji wa bangili za vangovango zenye duara iliyovunjika ambazo zimepatikana Irodo, mahali mbali, nazo bado zinaitwa kwa jina la haba hata kama zimetengenezwa kwa fedha. Hapo tena uhusiano wa kisisimu unajitokeza. Cham haban na vuru saban vinamaanisha shaba katika Kiastronesia; katika Kimalagasi na Kingazija neno saba bado linatumwa kwa maana ya shaba hadi leo. Katika Kiswahili shaba maana yake ni 'copper' kwa lugha ya Kiingereza.

Chuma kilichimbwa kwa wingi sana. Hapa chuma hakionyeshi kilichimbwa wakati huo huo, kwa kuwa matumizi mapya ya chuma kilichotumiwa zamani, kama ethnografia inavyohibitisha, hayatoshi kuelezea tofauti kati ya machimbo mengi ya vyuma (majivu na makaa na mavi ya chuma) na kutokuwepo vitu vya chuma, na kama inavyoonyesha maeneo ya kipindi hicho yalitoa ureinbo wa wanawake (Andranosoa), chusa na ndoana (Talaky). Hapa inaweza kuongezwa - katika nchi ambayo kuwepo kwa zana za mawe hakujahakikishwa - alama za mapanga na visu zinazopatikana katika mifupa (Andoro na Andranosoa). Ni wazi kuwa bidhaa zilizoyeyushwa zilipelekwa nje kupitia Talaky, ambayo maendeleo yake, kama si msingi wake, yanaonyesha uhusiano wake kutokana na shughuli zake kama njia muhimu ya



bahari ambayo ilitumika kusafirisha shehena hizo kutoka sehemu ya bara ambako kulikuwa na bidhaa nyingine mbali ya zile za kuyeyushwa.

Ugunduzi wa mabaki mengi ya mifupa ya wanyama wadogo huko Andaro unaashiria kuwa wanyama wadogo waliljwa kwa wingi. Hili halihusiani sana na vionjo vya chakula vya wakazi, bali na haja ya kuchinja wanyama hawa kabla ngozi (*daro*) yao laijaharibika zaidi kwa miiba. Huenda ngozi ya kondoo ilikuwa ni-bidhaa ya pili kwa umuhimu kusafirishwa nje. Na inawezekana kuwa ziada kubwa ya nyama iliyopatikana ilitiwa chumvi na kukaushwa kwa kutumia mbinu za kuhifadhi ambazo zinajulikana kuwa zilikuwepo wakati huo. Nyama hii iliyohifadhiwa bila shaka ndiyo iliyokuwa bidhaa ya tatu muhimu kusafirishwa nje. Lakini, kama vyombo vya usafirishaji baharini vilikuwa vingi, basi huenda nyama hii ilitumiwa zaidi na mabaharia. Pia inawezekana kuwa nyingine ilitumiwa na watu wa palepale.

Licha ya kondoo, watu hao yaelekea pia wafuga ng'ombe na mbuzi kwa idadi ndogo, mifugo ambayo ulaji wake unathibitishwa na mabaki ya vyakula, ambayo pia yanaonyesha ulaji wa wanyama wa kuwinda (mifupa ya ndege, aina ya nungunungu, na panya wadogo wadogo) na uvuvi (mifupa ya samaki, kucha za kaa, magamba ya makombe). Kuhusu mimea ya chakula, ambayo haitajwi katika historia ya mapokeo na ambayo haina ushahidi wa kiakolojia, hapana shaka ilijumuisha mimea ya awali kabisa iliyolimwa kisiwani na ambayo ilikuwa tayari katika eneo hilo, kama vile viazi vikuu na mazao mengine ya aina hii, ambayo yangeweza kuokotezwa msituni kama inavyofanyika hadi sasa.

Sehemu ndogo sana ya Talaky iliyochunguzwa, kwenye ukingo wa mashariki, imeonyesha kijiji kimoja tu cha wavuvi; vyombo vya matumizi ya kila siku ni vipande sahili tu na haviwezi kulinganishwa na vile vya maeneo ya bara. Ufynyanzi wa hapa una dalili za matumizi ya grafiti bila dalili zozote za wazi za utumiaji wa vyombo hivyo kama ule uliopatikana nje ya Bukini (ufynyanzi wa kale na wa zama hizo) isipokuwa tu baadhi ya ufynyanzi wa Afrika Mashariki (mapokeo ya Lelesu) na Kusini mwa Afrika (mapokeo ya Gokomere-Ziwa-Zhizo) kwa upande mmoja, na ule wa mapokeo ya Sa-huynh-Kalanay (hasa katika Champa ya kale), katika eneo la Austronesia, kwa upande mwingine. Aidha kuwepo katika sehemu za juu za Manambovo kwa vipimo vya mawe ya kloriti-shasti na ufynyanzi wa kuigiza mawe, mazao ya bahari na vitu vya kutoka nje (kutoka Uarabuni na ufynyanzi wa nje ambao haujapewa tarehe kamili, vipuli vya pembe za ndovu kutoka Afrika au Asia) ni uthibitisho kamili kuwa Talaky, ambapo vitu vyote vilipitia, hayakuwa makazi ya wavuvi wa aina ya Sarodrano. Ukweli kwamba Talaky inachukua eneo pana unaonyesha kuwa uvuvi mkubwa ulikuwa unafanywa ambao bidhaa zake lazima zilikuwa zinahifadhiwa na kuuzwa kama ilivyokuwa ikiuzwa nyama ya kondoo. Hata hivyo, haya yote yanahitaji uthibitisho.

Utafiti zaidi, hususani wa maeneo yaliyo karibu na unapoingia mto baharini, na juu zaidi unakotokea mto, katika sehemu zinazofaa kwa shughuli za kiuchumi (kwenye mabonde), bila shaka utawezesha kusuka upya maisha ya kiuchumi na kijamii ya Bukini nzima katika kipindi hiki muhimu cha historia ya kiekolojia na kisiasa. Data kutokana na akiolojia, kama ilivyo sasa, zikiungana na data za kiethnografia na za mapokeo, tayari zinaonyesha kuwepo kwa umoja wa utamaduni na vifaa ambavyo vinajionyesha katika dhana ya ustaarabu wa leo wa Kimalagasi na vile vile katika maumbo ya vifaa vya utamaduni wa kipindi kinachozungumziwa sasa. Baadhi ya vyombo hivyo, hasa vyombo vya udongo kutoka nje, vinathibitisha wazi kuwa baadhi ya vikundi vya Kimalagasi vilikuwa schcmu ya mtandao wa kimahusiano ulioifika katika maeneo ya mbali ambayo uchunguzi wa kimapokeo haukuwahi kuyaonyesha, kwa mfano nchi zilizopakana na Bahari ya Uchina ya Kusini, kwa upande mmoja, na nchi

zinazopakana na Mlangobahari wa Msumbiji, kwa upande mwingine. Hii inalazimu kuendeleza uchunguzi katika maeneo haya 'mapya' ili kukusanya data zinazoweza kutoa mwanga kuhusu historia ya Bukini.

### *Bukini katika muktadha wa kimataifa*

Kutokana na data kuntu za kimapokeo na pia data za wazi za kiakiolojia, eneo la Bukini tayari limekwishatoa, katika kipindi kinacho-zungumziwa, dalili mbalimbali za uhusiano na maeneo mengi ya nchi za nje. Baadhi ya maeneo hayo yamegusiwa tu, ambapo mengine yametiliwa mkazo. Lakini kutokana na mapengo yaliyopo sasa katika kumbukumbu, hakuna fasiri yoyote ya maana inayoweza kufanywa sasa kutoka katika kumbukumbu hizo, iwe ni kuhusu hali halisi ya uhusiano wa kisiwa na maeneo hayo ya nje au kuhusu kiwango cha uhusiano huo. Dalili zinazopatikana kutokana na uchunguzi wa vyanzo vya simulizi na akiolojia zinawezesha kutupilia mbali nadhariatete ya kronolojia fupi ambayo imeweka kutamakani kwa watu wa Bukini mwishoni mwa kikwi cha kwanza. Hakuna shaka tena kuwa binadamu alikuwepo Bukini, hasa katika maeneo ambayo uchunguzi wa hivi karibuni umetoa taarifa mpya, muda mrefu kabla ya +1000. Kipindi cha kutoka karne ya saba mpaka karne ya kumi na moja, bila kujali yasiyofahamika sasa, lazima kisikubalike tena katika historia ya Bukini kuwa ndio mwanzo wa kutamakani kwa watu. Wakati umefika wa kutupilia mbali kabisa mijadala yote inayotokana na uchache wa taarifa tulizonazo kuhusu Austronesia katika historia ya Bukini. Kwa hakika, kisiwa kinaonekana kilikuwepo kwenye muktadha mpana wa kibahari.

Historia ya ubaharia katika Bahari ya Hindi bado hajaandikwa; kwa sasa kuna uchunguzi kidogo tu na hivyo ni vigumu kuiunganisha mitalaa iliyopo na kupata taarifa nzima inayoaminika. Upanuzi wa vyombo vya baharini uliofanywa na Waarabu-Waislamu kutoka karne ya kumi na moja na kuendelea huenda ukawa umepiku umuhimu wa watu wengine na sehemu nyingine katika ubaharia wa mwanzo kabisa. Kuna haja ya kuzingatia zaidi maendeleo yaliyofikiwa katika karne ya kwanza ya enzi ya Ukristo, katika mbinu za usafiri za wale ambao Wachina, katika kikwi cha kwanza, waliwatambua kwa jina la Kunlun, ambao kati yao Waaustronesia huenda walikuwa ndio wengi. Waaustronesia hawa walikuwa wa kwanza kujulikana kuwa wajenzi wa mashua kubwa za kushona zilizokuwa zikitegemewa kusafiria katika bahari kubwa, ambazo waandishi wa Kichina wa karne ya tatu hadi ya tisa walikuwa wakiziita kun-lun bo, wakizieleza kama meli zenye matanga ya kushona zenye urefu wa mita 50 na uwezo wa kubeba abiria kati ya 500 hadi 1000 na shehena kati ya tani 250 hadi 1000. Ingawaje majahazi na ngalawa huenda viliendelea kuwasafirisha wahamiaji wa Kiau-stronesia kwenda Bukini, mwishoni mwa kikwi cha kwanza, sasa haikubaliki (kwa kipindi baada ya au kabla ya karne ya tatu) kuunganisha tarehe za kutamakani kwa watu kisiwani Bukini na uwezo wa vyombo vya baharini.

Endapo itakubalika kuwa Waaustronesia walikuwa wa kwanza kusafiri baharini kuelekea Bukini (ambayo kutamakani kwao, lugha na utamaduni vinaonyesha dalili zao-hoja ambayo imejitokeza katika uchunguzi wa hivi karibuni), kuna sababu nzuri ya kuchunguza nadhariatete kuwa kisiwa hicho kilibadilika na kujungiza katika mfumo wa biashara wa ukanda au eneo moja kubwa, biashara ambayo ilianzisha mahitaji ya aina mbalimbali za bidhaa zenye thamani. Mbao, gundi, marashi na viungo, kutoka zama za kale, viliuzwa kwa njia ya ukusanyaji katika kisiwa hiki; na hasa tangawizi, ambayo inaonyesha kuwa ilikuwa moja kati ya bidhaa zilizoleta faida sana na ambazo ukusanyaji wake unatokana na mbinu za Champa ya kale.

Nadharia tete hii inagongana na mawazo yaliyopokelewa na ina vipengee ambavyo bado havijakamilika sambamba na vingine ambavyo vimekwishathibitika. Kwanza inajikita katika uwezekano wa Waaustronesia kushiriki katika usafirishaji wa binadamu na bidhaa Maghribi mwa Bahari ya Hindi, mwanzoni mwa kikwi cha kwanza. Kuna ushahidi mwingi wa hapa na pale unaopendekeza uwezekano wa kuwepo kwa 'vyombo vya watu weusi,' kun-lun-bo karibu na Afrika; marejeo katika Periplus (Mwongozo wa Bahari ya Hindi) kuhusu mitumbwi ya kusukwa ya pwani ya Azania na mitumbwi ya kushonwa yenye usukani mmoja huenda ilikuwa ni ya Wacham ambao walikuwepo katika bahari ya Shamu katika karne ya sita. Ukulima wa migomba kutoka Asia ya kusini mashariki katika Afrika Mashariki, usafirishaji wa mafuta ya nazi kupitia Rhapta wakati wa Periplus, kuwepo kwa tembo wa vita waliopandwa na Wasere katika jeshi la Ethiopia kabla ya karne ya tatu, kushiriki kwa wafanyabiashara wa baharini wa Kicham katika biashara ya watumwa ya Zanj kwenda Asia na Mashariki ya Kati, na kutambua umoja na uzito katika ulimwengu wa watu weusi uliosema na al-Jahiz kuhusu Wazanj ni sababu miongoni mwa sababu nyingi zinazothibitisha ukale na uimara wa maingiliano.

Msururu wa pili wa sababu unahusiana na nafasi iliyochukuliwa na Bukini katika safari za mitumbwi ya Kiaustronesia kuelekea upande wa Maghribi. Miller anafikiri kujiunga kwa kisiwa hiki katika biashara hii kulitokea mapema sana; inaelekea kuwa, tukichukua ushahidi wa vyanzo vya simulizi na akiolojia, Bukini haikuwa tu, kama Miller anavyoamini, kisetiri cha kudumisha siri za biashara kuhusu nchi ya mdalasini na aina nyingine za viungo ambayo kwa makosa ilifikiriwa kuwa ilikuwepo kwenye Pembe ya Afrika. Pwani ya mashariki ya Bukini ilikuwa bado tajiri katika bidhaa kadhaa muhimu za biashara ya kimataifa ya kale na Enzi za Kati, na, zaidi ya hapo, ilikuwa na faida ya kuwa karibu na njia kuu za kutokea nje na hasa bandari za Afrika zilizopeleka bidhaa Misri na kupitia Misri kwenda nchi za Mediterania. Hakuna shaka kuwa pwani ya mashariki ya Bukini ilitoa bidhaa zake katika kipindi kinachozungumziwa sasa. Ukosekano wa baadhi ya mimea yenye umuhimu sana wa kitamaduni kama *Calophyllum inophyllum* katika pwani ya Afrika, unatulazimisha tuamini kuwa Bukini, ambako mmea huu upo, ilitembelewa mapema zaidi na Waaustronesia kuliko Afrika Mashariki.

Haya yote uliyoeleza hapo juu, yanahusu kipindi kilichotangulia kile kilichozungumziwa katika juzuu hili. Kwa vile tunaamini kuwa katika kipindi hiki cha mbali Bukini ilikuwa inashiriki sana katika biashara ya Bahari ya Hindi, hatua inayofuata ni kujaribu kufuata ngazi za kushiriki huku, kati ya karne ya saba na ya kumi na moja.

Baada ya ushindi wa Arabia ya Kusini (570), Uajemi ya Wasassanid ilifanikiwa kwa kiasi fulani kuchukua hiba ya watu wa Arabia ya Kusini katika biashara ya Bahari Hindi, pamoja na Bahari ya Shamu. Katika karne iliyofuata Uajemi kwa kiasi fulani ilijiunga katika sera ya upanuzi wa ulimwengu wa Uislamu wa Kiarabu ambao ushindi wao dhidi ya Misri (641-642) ulikamilisha unyakuzi wa umiliki wa njia za biashara za Maghribi wa Waarabu na Waajemi.

Ujirekebishaji wa mwanzo wa Bukini katika mabadiliko haya ulihusu kujiingiza katika uhusiano na waingizaji bidhaa kutoka nje wa Kiajemi, ambao unaonyesha jinsi athari zao zinavyoonekana kupitia data zilizotolewa na udongo wa Bukini. Lakini, kiasi kidogo cha mabadiliko katika washiriki na mwingiliano wa misafara ya bara, ambayo ilisababisha siyo tu kupungua kwa biashara ya ubani bali pia katika bidhaa nyingine zilizoanza kushindana na zile za kutoka Uarabuni, pia huenda kilizuia biashara ya mdalasini ambao ulikuwa tayari upo katika mashindano na ule uliotoka Sri Lanka. Na pengine tunaweza kusema kuwa watu wa al-Kumr (Ngazija na Bukini) walipoivamia Aden kwa kutumia mitumbwi yao, mwishoni mwa

karne ya saba na mwanzoni mwa karne ya nane lilikuwa ni jaribio lililofanikiwa kiasi katika jitihada za kuirudisha hali ya awali. Baadhi yao walikwi-shaifanya Aden kuwa bandari yao, ambako walianzia safari zao kila msimu, 'wakasafiri pamoja katika msimu wa pepo' na walifaulu kuanzisha njia ya moja kwa moja ya kusafiri kati ya nchi yao ya asili na Arabia ya Kusini. Hivyo basi, walikuwa na uwezo wa kushindana na washindani wao, kwa vile wasafiri wa baharini wa Kiarabu na Kiajemi, ambao wanaonekana hawakujua habari za Ngazija na Bukini mpaka karne ya kumi - na wakaja kuwajua vema katika karne ya kumi na mbili tu - waliendelea kupata bidhaa za Bukini katika pwani ya Afrika Mashariki, ambayo waliweza kuifikia kwa njia ya bahari.

Ni vigumu kuwa na uhakika wa hali halisi ya biashara katika karne ya tisa. Katika karne hii na zile zilizofuata safari za wasafiri wa baharini wa 'Kimalagasi' huenda mara kwa mara ziliishia Aden. Uelewano wao wa muda mrefu na nchi za Kiarabu uliwafanya baadhi ya Wamalagasi waingie dini ya Kiislamu, na si ajabu iwapo baadhi ya safari kutoka al-Kumr hadi Aden na mlango wa kuingilia Ghuba ya Uajemi zilikuwa hatimaye sehemu ya mfumo ya biashara ya Kiarabu na Kiajemi. Wasafiri baharini wa Kimalagasi waliosilimishwa waliwaonyesha mabaharia wa Onan na Siraf njia ya kusafiri moja kwa moja mpaka Kaskazini mwa Bukini ambako hadi hii leo makazi ya kale sana yanaweza yakaonekana huko Onjatsy na pia katika kisiwa cha Kanbalu. Ni mwanzoni mwa karne ya kumi ambapo ushidani kati ya Wamalagasi na Waarabu na Waajemi ulitoweka. Hii ilitokea wakati ambapo, wakitumia nafasi ya mauaji ya Waislamu huko Canton (878) na ukuaji wa nguvu za Srivijaya, ulimwengu wa Kun-lun, kupitia kuimiliki milango bahari, ulikuwa ndiyo mwanzo tu umepata faida zaidi dhidi ya washindani wao wanajeshi (Waarabu,-Waajemi na Wahindi, kwa upande mmoja, na Wachina, kwa upande mwingine).

Udhibiti huu wa milango bahari ulifanikisha kuifanya rasi ya Malaka, katika falme ya Srivijaya, kuwa kituo maalum cha meli zinazokwenda na kutoka Uchina. Kwa wakati huu Uchina ilikuwa tayari ni moja kati ya masoko makubwa, na biashara kubwa ya nchi zote za kusini Maghribi mwa Bahari ya Hindi nje ya Mediterania iliigeukia rasi ya Malaka. Bukini, ambayo sehemu yake ya mashariki iliendelea kuwa katika mzunguko wa Kun-lun, ilishiriki katika biashara hii. Katika tukio la mashambulizi ya Kanbalu, (945), wakati mwingine inakubalika kuwa washambuliaji walioitwa Wakwak-Wak, kutokana na taarifa za Kiarabu, walitokea Bukini. Maelezo ya shambulio hili yaliyotolewa na Ibn Lakis katika kitabu cha *The Marvels of India* yanakubalika kuwa ni kamilifu; safari hiyo ilikuwa inatafuta Zanj ili kuchukua watumwa na bidhaa ambazo zilikuwa na manufaa kwa nchi yao na kwa Uchina (pembe, magamba ya kobe, ngozi za chui na ambari).

Hata hivyo, ingawa uharamia wa baharini na unyang'anyi ulikuwa ni kitu cha kawaida katika kipindi hiki, safari iliyokuwa na 'vyombo vya bahari elfu moja' ya watu waliotokea kusini kuja kushambulia Kanbalu haikuwa tu inaongozwa na Wamalagasi kutoka pwani ya mashariki bali pia iliwajumuisha Wawak-Wak kutoka Mashariki ya Mbali. Safari yao katika eneo hili la kusini kabisa isingeweza kuwa ilisababishwa na mahitaji ya bidhaa ambazo wangeweza kuwaachia marafiki zao wa Bukini kuzitunza na ambazo pia zilikuwa nyingi sana huko kwao na ndizo walizozifanya biashara kwa karne nyingi na Uchina. Kila kitu kinaonyesha kuwa kilichokuwa cha muhimu kwa hawa Wakun-lun au Wawak-Wak ni kupinga Waislamu kuelekea kusini (wakiungwa mkono na Wamalagasi waliosilimishwa) na kulinda machimbo ya dhahabu na madini mengine yasiingiliwe na Waislamu hao. Huenda inaweza kukubalika kuwa chuma katika Bukini ya kusini, bidhaa ambayo ilikuwa inalindwa sana na

wale waliokuwa wakūchimba, yawezekana yenyewe ndiyo iliyokuwa ikigombaniwa ili kuendeleza ukiritimba.

Safari kama zile za 945 zaonyesha kuwa zilipunguza kuja kwa jeshi la maji la Kiislamu kusini kwa muda mrefu. Hata hivyo, ufanano wa ulimwengu wa Wakun-lun ulikuwa tayari umeathiriwa na uongofu wa dini ya Kiislamu. Inawezekana kuwa ilikuwa wakati huu ambapo uhamiaji kama vile wa Zafi (n-d) Raminia uliondoka kutoka pwani ya Bahari ya Shamu. Wakati huohuo, kisiwa hiki kilianza kukuza uhusiano wake na Afrika ya Mashariki ambayo ingeweza kuwa tofauti lakini ambayo pia ilikuwa imesilimishwa, pengine kikipeleka huko bidhaa za kloriti-shisti kilichoizalisha, kama bidhaa zilizokuwa zikiingia Kilwa kutokea karne ya kumi na kuendelea zinavyoashiria.

Tathmini hii mpya ya mahusiano ya kiuchumi na kibahari kati ya Bukini na ulimwengu wa Wakun-lun, kwa upande mmoja, na kati ya kisiwa hiki na Uarabu-Uajemi, kwa upande mwingine, inaleta maswali mapya kuhusiana na maisha ya kisiwani. Uchunguzi unaokubaliana, wa tofauti ya karne sita, wa Hudud al-Alam (karne ya kumi) na Adimirali Sidi Ali Celebi (karne ya kumi na sita) unaonyesha kuwa miundo ya kisiasa na kijamii ya zamani, ya sehemu za kusini ilikaidi kabisa athari mpya. Hii itawasukuma wanahistoria kuangalia upya swala la 'athari za Waarabu,' ambazo zinaonyesha zinctumiwa sana katika jaribio la kueleza sura mbalimbali za utamaduni wa kale wa Bukini. Hata hivyo, uchunguzi kama huu unahusiana zaidi na utafiti wa vipindi baada ya karne ya kumi na moja. Mabadiliko makubwa katika mtazamo unaotakiwa ni lazima yawe ya matokeo ya kuleta pamoja vyanzo vya taarifa vyote vilivyopo sasa ili kuwezesha kuandika historia ya kipindi cha karne ya saba hadi kumi na moja; kuna mengi zaidi ya kufikiria, wakati mapengo mengi ambayo bado yamo kwenye nyaraka za kipindi hiki pamoja na kiwango cha kutokukijua kipindi cha awali, bado tunavikumbuka. Hoja ya msingi, kwa wakati wa usoni, huenda isiwepo zaidi katika kutambua kuwa kipindi hiki kilikuwa muhimu katika historia ya kale ya kisiwa hiki na katika kukubali mambo ambayo yanaonekana kuwa yameshathibitishwa kihistoria kuliko katika kuthibitisha kitaalamu na kukubali umuhimu wa kategoria mbalimbali za vyanzo vya habari na haja ya kuvitumia vyanzo vyote katika mfumo ulio sahihi pia.

# 26

## *Diaspora ya Waafrika katika Bara la Asia*

### *Utangulizi*

Ingawaje kuwapo kwa Waafrika nje ya bara lao ni jambo ambalo limethibitishwa tangu zama za zama, ilikuwa tu katika kipindi hiki kinachoja- diliwa ambapo umuhimu wa nafasi yao katika nyanja mbalimbali za shughuli za binadamu katika nchi za Kiislamu, za Mashariki ya Kati, Bara Hindi, Visiwa vidogo vya Malay na Mashariki ya Mbali, ulipozidi kutiliwa maanani. Kwa bahati mbaya, habari tulizopata kuhusu jambo hili bado ni chache na zimetawanyika sana katika maandishi tofautitofauti na katika kazi za utafiti zilizoandikwa kwa lugha mbali mbali na hasa lugha za Kiasia.

Fauka ya hayo, hapajafanyika uchunguzi wowote wa kitaaluma kuhusu kuwepo kwa Waafrika barani Asia. Kwa hiyo sura hii ni jitihada ya mwanzo ya kujaribu kukusanya habari zilizopo juu ya uhusiano wa zamani kati ya Afrika na Uarabuni na pia juu ya mambo ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni yaliyopelekea kuwepo kwa Waafrika katika maeneo hayo yaliyotajwa.

### *Watu weusi Arabuni kabla ya Uislamu*

Ujirani uliopo kati ya Afrika na Uarabuni na uhusiano wao wa karne nyingi kwa kupitia Bahari ya Shamu, umesababisha kuwapo kwa Waafrika wengi Uarabuni, tangu zamani. Waafrika hao, wake kwa waume, waliokuwa wa asili mbali mbali lakini zaidi kutoka Ethiopia, Somalia, Nubia na pwani ya Mashariki, walikuja hapo kwa sababu mbali mbali, lakini sana sana kama watumwa. Kwa upande mwingine, idadi kubwa ya askari wa Kiethiopia walibakia Arabuni ya kusini baada ya kutamalakiwa katika vita vya karne ya sita<sup>1</sup> na baada ya miaka kupita wakamezwa katika taifa la Waarabu ambao walikuwa wengi.

Vyanzo vya habari vya Arabuni vimehifadhi simulizi za hapa na pale kuhusu kuwepo kwa watu wenye asili ya Kiafrika Arabuni kabla ya majilio ya Uislamu.

Washairi kadhaa wa enzi za kabla ya Uislamu (Jahiliya) walijulikana kwa ujumla kama Aghribat al-Arab (makunguru wa Waarabu) kwa ajili ya rangi yao nyeusi waliyoirithi kutoka kwa mama zao. Waliokuwa mashuhuri zaidi kati yao walikuwa Antara b. Shaddad, Khufaf ibn Nadba na Sulayk b. al-Sulaka. Huyu aliyetajwa mwisho alikuwa mmoja wa Wasaalik, kundi lililojulikana sana la askari wanyang'anyi waliosifika sana kwa ushujaa na heshima yao

<sup>1</sup> Taz. Sura 16 ya Juzuu II.

ijapokuwa walitenda vitendo vya unyang'anyi. Hata hivyo, aliyetukuka sana alikuwa Antara (au Antar) aliyekuwa wa mbari ya Waabs, ambaye alizaliwa na kijakazi wa Abyssinia aliyetewa Zabiba.

Alisifika kwa nguvu na ujasiri wake na hapo basi akawapatia utukufu watu wa ukoo wake. Baadaye alichiliwa huru kutoka utumwani na akawa mtu mheshimiwa sana katika mbari yake. Ushairi wake juu ya mapambano yake mengi ya kivita, mabadiliko na visa vyake vya mapenzi, ndio uliosifika sana, kama sanaa bora zaidi za ushairi wa *Jahiliya* na hivyo kumhakikishia mshairi huyo sifa za kudumu milele. Matendo yake ya ushujaa ndiyo yalikuja kuwa kiini cha maudhui ya nganopendwa za mapenzi zilizoitwa *Sirat Antar* (Hadithi ya Antar) katika enzi iliyofuata ya Uislam. Baadaye alijitokeza kama shujaa wa taifa la Kiarabu.

Katika mji wa biashara wa Maka, ulinzi na uhifadhi wa misafara ya mji ulikabidhiwa kikosi cha mamluki waliojulikana kama *Wahabish*, jina linalochukuliwa kuwa na uhusiano na jina lililotumiwa na Waarabu kutaja watu kutoka Ethiopia - *al-Habash*. Ingawa inaonekana kwamba Waethiopia ndio waliokuwa kiini cha kundi hilo, lakini lilikuwa pia na watumwa wengine wa Kiafrika na Waarabu wanomadi. Umuhimu wao kama kiini hasa cha jeshi la mji huo ni jambo linalothibitishwa katika vyanzo vingi vya habari vya Kiarabu ambamo ustadi wa kiaskari, nidhamu na ushujaa wa hawa 'askari mamluki wa Kiafrika', unasisitizwa mara kwa mara.

### *Watu Weusi katika msafara wa Muhammad*

Katika habari za kimapokeo, inasemekana kwamba, kati ya waongofu wa kwanza katika dini ya Kiislamu huko Maka, ni idadi kubwa ya watumwa, wengine wao wakiwa wenye asili ya Kiafrika. Katika mafundisho ya dini yaliyohubiriwa na Muhammad, watu hawa waliokuwa na hadhi duni katika jamii waliuona uwezekano wa kupata kuheshimika kama binadamu, na kujiunga na jumua mpya ambapo mtu alithaminiwa hasa kutokana na uzingatifu wake wa dini na matendo yake ya uchaji Mungu na wala sio tu kutokana na umuhimu wake katika jamii au asili yake.

Mmoja kati ya waongofu wa kwanza kama hao aliitwa Ammar ibn Yasir ambaye mama yake aliyetwa Sumayya alikuwa mtumwa wa Kiafrika; huyu Ammar alishiriki katika uhamaji wa kwanza kwenda Ethiopia, na baadaye alishiriki katika shughuli zote za kidini za Mtume. Khalifa Umar (634-43) alimteua kuwa gavana wa Kufa, cheo kimojawapo kati ya vyeo muhimu katika utawala mpya wa awali wa Kiislamu. Hali kadhalika alikuwa mmoja wa wahubiri wa *hadith* (yaani maelezo ya matendo na misemo ya Muhammad).

Mtu aliyejulikana sana kati ya wale wafuasi wengi wa mwanzomwanzo kabisa, walioandamana na Mtume, aliitwa Bilal b. Rabah, ambaye alikuwa mtumwa wa Kihabeshi. Kabla Khalifa Abu Bakr hajamnunia na baadaye kumpa uhuru wake, mtu huyu alidhulumiwa na kuteswa na bwana wake kwa ajili ya kusadiki sana mambo ya dini. Alikuwa muadhini wa kwanza (mtu awaitaye watu kuswali) katika dini ya Kiislamu na akashiriki katika harakati za mwanzomwanzo za kueneza Uislam, ikiwa ni pamoja na zile zilizofanyika Syria, ambako alikufa kutokana na ugonjwa wa tauni, katika mji wa Damasko mnamo mwaka wa 640.

Mwongofu mwingine wa mwanzomwanzo aliyejiunga na Uislam, na aliyetoa mchango mkubwa katika shughuli za vita alikuwa al-Mikdad b. Amr al-Aswad. Alikuwa mmojawapo kati ya masahaba wa mwanzo wa Muhammad na kumsaidia Mtume katika vita vyake vyote alivyopigana. Akiwa Mwislamu pekee aliyepigana akiwa amepanda farasi, wakati wa vita vya Badr, alipewa jina la heshima la *Faris-al-Islamr* (yaani jasiri wa Uislam). Watumwa

waliozingatia Uislamu walipewa uhuru kutoka utumwani na hapo basi wakawa mawalii au wafuasi wa Mtume na Waislamu wengine mashuhuri.

Kati ya jumuiya ya kwanza ya Kiislamu, walikuwamo wanawake weusi kadha wa kadha, ambao walikuwa wamekamblewa kutoka utumwani, kama vile Umm Ayman Baraka, ambaye alimtunza na kumlea Mtume alipokuwa mtoto, na huyu mama alikuwa mmoja kati ya watu walioheshimiwa katika jamaa yake; Fudda, ambaye alikuwa mtumishi aliyejariwa na binti ya Mtume, na Nabaa ambaye alikuwa kijakazi wa mjomba wa Muhammad, Abu Talib, ambaye ndiye aliyepata sifa ya kueneza hadithi ya safari ya usiku ya Muhammad isra'a kwenda Jerusalem.

Miaka mitano baada ya kutangazwa kwa dini ya Kiislamu (615), Waislamu wengi walikimbilia nchi jirani, Ethiopia, ili kuepokana na kuuawa na Wakurayshi kwa ajili ya imani yao katika mji wa Maka. Ukaribisho wa ukarimu waliopewa na Negus (*Najashi* katika simulizi za Kiarabu) pamoja na baraza lake, ulileta kipindi cha uhusiano mzuri kati ya jumuiya hizo mbili zenye dini tofauti. Haya yalijitokeza katika mapokeo<sup>2</sup> ya awali ya Kiislamu.

### *Waafrika katika jamii ya Kiislamu*

Kurani ambayo ndiyo maandishi ya hali ya juu ya Uislamu sharti yawe ndiyo chanzo cha majadiliano yoyote juu ya mienendo na mielekeo ya Kiislamu kuhusu taifa na rangi, walakini, kwa kweli, kuna vifungu viwili tu katika Kurani ambavyo vinahusiana na swala hilo moja kwa moja. Kifungu cha kwanza kati ya hivi kinapatikana katika sura ya XXX aya ya 22, ambacho kinasema, 'Miongoni mwa ishara za Mwenyezi Mungu kuna uumbaji wa mbingu na dunia na namna mbali mbali za lugha na rangi zenu.' Tofauti baina ya lugha na rangi zimetajwa hapa kama ishara mojawapo ya enzi na uwezo wa Muumba wa kufanya mambo mengi kwa namna nyingi.

Kifungu kingine, cha sura ya XLIX, aya ya 13, kiko dhahiri zaidi: 'Enyi wanadamu tumewaumba kutokana na mume na mke na tumewafanya muwe katika sehemu na mbari ili kwamba mje kajuana. Aliye bora zaidi kati yenu mbele ya macho ya Mwenyezi Mungu ni yule aliyemchaji kuliko wote, kwa sababu Mwenyezi Mungu ni mwenye ujuzi wote na anaona yote'.

Kulingana na hayo, mtu haoni ubaguzi wowote wa kitaifa au rangi katika Kurani na hamna hata udokezi wowote wa kuwemo kwake. Hata hivyo, vifungu hivyo vilivyotajwa hapo juu, vinaonyesha utambuzi wa kuweco tofauti, kwani katika lile dondoo la pili kuna msisitizo zaidi wa uchaji wa Mwenyezi Mungu kuliko wa asili ya kuzaliwa.

Kadiri Uislamu ulivyoenea, Waislamu, hasa wale wa asili ya Kiarabu, waliingiliana zaidi na Waafrika wa aina mbali mbali kuliko pale mwanzo. Kutokana na vyanzo vya Kiarabu wakazi wa Afrika ya tropiki wanagawanywa katika makundi manne makuu: *Wasudan*, *Wahabesha*, *Wazanj* na *Wanuba*.

Jina *as-Sudan* (wingi wa neno *al-aswad*, yaani, 'weusi') ni la ujumla sana, na linatumika kuwaelezea watu wote wenye rangi nyeusi bila kufikiria nchi zao za asili. Mara nyingine, hata Wahindi, Wachina na watu wengine kutoka Asia, walijumuishwa katika kundi hili. Kwa mtazamo finyu, jinsi miaka ilivyopita, jina Wasudan lilikuja kumaanisha Waafrika weusi wanaoishi kusini mwa Maghrib, yaani wakazi wa *Bilad al-Sudan* ('nchi ya watu weusi') hasa.

2 Taz. Sura 19 na 20 ya juzuu hili.



Kuhusu *Wahabasha* (Waethiopia), kwa vile nchi yao iko karibu zaidi na Arabuni, na pia kwa ajili ya kushirikiana kwao na Muhammad katika siku zake za mwanzoni, wao walikuwa kundi lililojulikana zaidi kati ya Waafrika. Hata hivyo, waandishi wengine walilitumia jina hili kuwa na maana pana zaidi; waliwahesabu hata watu waliokuwa wakiishi mbali sana kama vile Niger au sehemu za kusini mwa Misri kuwa Wahabasha.

*Wazanji* au (*Wazinj*) ni jina linalotumiwa zaidi kwa wale watu wanaozungumza lugha za Kibantu kutoka pwani ya Mashariki ambao, tangu nyakati za kabla ya Uislamu, waliitwa kama watumwa huko Arabuni, Persia, na Mesopotamia. Hata hivyo, jina hilo nalo, baada ya muda mfupi, likawa na maana ya 'weusi' kwa jumla.

Wanuba walijulikana na Waarabu baada ya Misri kushindwa vitani, walakini, si ajabu kuwa jina hilo pia lilimaanisha Waafrika wote waliotoka sehemu za kusini mwa Nubia yenyewe, yaani, Wanilo na wale wa Mashariki ya Sudan waliozungumza Kisudan, waliokuja katika nchi zilizotawaliwa na Khalifa, kutokana na uamuzi wa Wanuba.

### *Biashara ya Watumwa*

Waarabu hawakuwa waanzilishi wa biashara hii ya watumwa ya Waafrika weusi. Kuchukuliwa mateka na kufanywa watumwa kwa Wanubi na Waafrika wengine, kulifanyika tangu enzi za Firauni, kama inavyodhihirishwa na sanaa nyingi za Kimisri zionyeshazo hali ya kuwepo watumwa katika nyakati hizo. Watumwa weusi walipatikana pia katika enzi za tawala za Kiyunani na Kirumi.

Mara tu baada ya kipindi cha ushindi wa Uislamu kwisha, hakukuwa na raia yeyote kati ya wale waliolindwa (*dhimmi*), kama vile Wayahudi, Waukristo au Wazoroasta, ambaye angeweza kutiwa utumwani tena. Ililazimu watumwa watafutwe mahali pengine, kutoka nchi za karibu au za mbali, au wapatikane kwa njia ya uvamizi; lakini sana kwa kununuliwa kutoka kwa jamii zilizokuwa dhaifu na zisizo na umoja, ambazo hazikuwa na uwezo wa kujikinga wakati wa mashambulizi. Sehemu maalumu katika Afrika ambapo watumwa waliweza kupatikana zilikuwa zile ambamo watu weusi waliishi, yaani pwani ya mashariki, Nubia, Ethiopia na pia Sudan ya Maghribi na kati.

Sharia ya Kiislamu inatambua hali mbili tu za utumwa wa halali, yaani utumwa wa ruzaliwa, na ule wa kutekwa mateka katika vita.

Katika hali ya kwanza, mtumwa anatambuliwa kama mtu aliyezaliwa na wazazi ambao ni watumwa. Pindi mtoto anapozaliwa, anatwaa hadhi ya mamake, yaani mtumwa au mtu huru. Walakini, mtoto anayezaliwa na mwanamume ambaye yu huru na mjakazi ambaye ni mtumwa vake, anahesabika kama aliyezaliwa huru.

Hata hivyo, kuzaliwa utumwani kusingeweza kutosheleza upatikanaji wa daima wa watumwa, kwani idadi ya watumwa ilizidi kupungua kadri watoto walivyozidi kuzaliwa huru, utokana na utaratibu wa halali wa unyumba na watumwa wengi kuachiliwa huru. Hivyo basi, uendelea kuwepo kwa utumwa katika lilimwengu wa Kiislamu kulitegemea mchango wa kila nara kutoka janibu za mbali au karibu, kwa njia ya kuwakamata moja kwa moja mateka atika vita, au kwa kusingizia kuwa wametekwa kutoka nchi za kigeni (*dar-al harb*) kwenye ita vitakatifu. Hatujui habari zote zinazohusu namna taratibu za biashara ya watumwa ilivyoendeshwa katika eneo la Waislamu, wa enzi hizo. Walakini, tunaewa kutokana na jambo fulani yanayojitokeza.

Masoko ya watumwa yalipatikana katika miji yote muhimu katika milki ya Kiislamu yote. atika karne ya tisa, baadhi ya masoko haya kwa kawaida yalikuwa katika malango ya njia za

kibiashara za kimataifa na hivyo yakawa kama vituo vya usambazaji. Masoko ya Bukhara, Samarkand, Nishapur, Rayy, Balkh na Marw, yalikuwa ndio vituo vya mwisho vya kupokea misafara ya watumwa wa Kislav na wa Kituruki. Zabid, Aden, Basra, Pezzan, Zawilla na Tripoli vilikuwa ni vituo ambavyo watumwa weusi walipitishiwa. Masoko mengine yalikuwa katika miji au maeneo ambapo huduma za watumwa zilitumiwa. Nayo yalikuwa Baghdad, Samarra, Kairo, Kordova na Maka.

Masoko ya watumwa yalikuwa chini ya amri kali ya serikali ili kuwalinda wanunuzi kutokana na uendeshaji biashara ya dhuluma. Wafanyabiashara ya watumwa, waliojulikana kama waingizaji bidhaa (*Jallab*), au wauzaji ng'ombe (nakhkhas) walibezwa kutokana na kazi yao na kuhusudiwa kwa ajili ya utajiri wao.

Bei za watumwa zilitegemea asili zao, jinsia, umri, hali ya afya, na uwezo mbalimbali. Katika Oman mtwana mzuri mweusi, angaliweza kununuliwa kwa dinari kati ya 25 hadi 30. Kafur wa Abyssinia, ambaye baadaye alikuwa mtawala wa Misri (mnamo 945 hadi 966) yasemekana alikuwa amenunuliwa kwa kiasi duni cha dinari 18.

Hata hivyo, watumwa ambao walikuwa wamejaaliwa vipawa visivyo vya kawaida waliuzwa kwa bei za juu kupindukia. Wasichana waliofungwa kucheza ngoma waliuzwa kwa bei za kati ya dinari 1,000 hadi 2,000, na mwimbaji mmoja wa kike aliuzwa kwa jamii fulani ya kingwana, katika mwaka wa 912, kwa bei ya dinari 13,000

### *Ajira na hali za kijamii*

Kutokuwepo kwa visa vya ubaguzi wa kitaifa au wa rangi katika mambo yanayozingatiwa na Uislamu, kuhakikishiwa haki za kisharia na upendeleo katika shughuli mbalimbali za ustawi wa maisha, visitufanye tukapata picha ya kupendeza kwamba hali ya kijamii ya watumwa ilikuwa nzuri sana katika karne za mwanzo za Uislamu. Katika maisha ya kila siku na katika mahusiano halisi ya maisha, kulikuwapo na ubaguzi kila mahali, ingawaje ubaguzi huu haukufanyiwa Waafrika pekee.

Fasili ya mwanzo ya kudhalilishwa kwa mtu mweusi katika siku hizo ilikuwa imeegemezwa kwenye hadithi ya Biblia, ya jinsi Ham, mmoja wa wana wa Nuhu, alivyolaaniwa na kupewa rangi nyeusi kwa ajili ya 'dhambi' zake. Laana ya weusi iliyofungamana na utumwa, ilirithishwa vizazi vyote vya watu weusi waliotokana na uzao wa Ham. Maelezo haya, ambayo yalikuwa maarufu sana miongoni mwa weledi wa kusimulia ngano na hekaya na hata baadhi ya wanazuoni, kwa ujumla hayajakubalika. Al-Hamdani aliyakataa kata kata, mapokeo haya, ambayo aliamini kuwa yalitokana na Wayahudi, kutokana na mafunzo ya kurani ya kifungu cha (IV:164) 'Kila roho itavuna kwa jasho lake na hakuna hata moja itakayobebeshwa mzigo wa nyingine'. Na anahitimisha kwa kurejelea athari za kimazingira: 'Weusi, weupe au wekundu wa rangi ya ngozi ya mwanadamu hautokani na chochote zaidi ya hali ya hewa ya nchi anamoishi.'

Ibn Khaldun pia anatupilia mbali mawazo ya laana ya urithi:

Ikiwa Torati inasema ya kuwa Nuhu ahimlaani mwanawe Ham, haelezi juu ya rangi ya mtoto huyo. Laana hiyo iliwafanya tu wana wa Ham kuwa watumwa wa wazao wa ndugu zake. Kufungamanisha rangi nyeusi na laana ya Ham kunamaanisha kutojua ukweli hasa wa athari za joto na baridi juu ya tabia ya nchi na viumbe vilivyomo.

Watumwa weusi walitumiwa kwa shughuli mbali mbali katika jamii za Kiislamu za kale, hasa kama watumishi, masuria na matowashi mafundi, wasaidizi katika biashara, wafanyakazi

katika sekta mbalimbali za kiserikali na majeshi. Mchango wao katika kujenga msingi wa kiuchumi, kisiasa na kijamii katika mataifa ya Kiislamu katika enzi ya kati ulikuwa mkubwa.

'Wazanj' ndio waliohesabika kuwa duni kabisa katika matabaka ya kijamii, zaidi wakiwa watumwa kutoka Afrika ya Mashariki. Katika maeneo makubwa ya tambarare ya chumvi ya Mesopotamia ya Chini, watumwa hawa walifanyishwa kazi ngumu, katika makundi makundi ya idadi za watu kati ya 500 na 5,000, ya kuchimba na kuondoa udongo wa juu wa chumvichumvi (*sebakhy*) hadi kuufikia ule wa rutuba ulioweza kutumiwa kwa kilimo. Hali ya maisha ya watumwa hawa katika maeneo haya na mazingira ambamo walifanyia kazi na kuishi yalikuwa mabaya sana. Hawakupewa chakula cha kutosha na aghlabu walishambuliwa na malaria na magonjwa mengine. Hali hii pamoja na mateso makubwa walivyoyapata kutoka kwa wanyapara wao, ilikuwa chanzo cha chuki isiyokwisha ambayo ilisababisha maasi ya mara kwa mara.

Hata hivyo, kazi hasa walizozifanya watumwa wengi zilikuwa ni utumishi wa nyumbani na za jeshi, ambazo hali zake kimaisha zilivumilika zaidi. Katika jamii nyingi, za kitajiri au zenye maisha ya kawaida, kazi za nyumbani zilifanywa na mtumwa mmoja au zaidi wakiwemo wale watumwa walioachiliwa huru. Hawa walikuwa wapishi, watumishi, mayaya, mabawabu, wabeba maji na wengine. Katika nyumba za matajiri, wajakazi waliokuwa na vipawa walipatiwa nafasi ya kuvikua na kuwa waimbaji, wanamuziki, wacheza ngoma na washairi, na kwa namna hiyo wakaweza kuwaghibiwa mabwana zao katika kuwatumbuiza.

Kushirikiana kimwili kwa wanaume wa Kiarabu na wanawake weusi ni jambo lililokuwako hata kabla ya enzi za Uislamu; aghlabu wanawake hao walikuwa Wanubi au Wasudan. Uhusiano huu ulikuwa wa kisuria na wala haukuwa wa ndoa kamili. Katika enzi za Waumayya na Waabbasi hili lilikuwa jambo la kawaida katika kila tabaka ya jamii. Washairi wengi wa Kiarabu waliwapenda wajakazi wao weusi wakautukuza uadilifu na haiba zao.

Maandishi maarufu ya tangu karne ya tisa ya al-Jahiz yaliyotetea watu weusi dhidi ya wachongezi wao, yanaonyesha wazi wazi jinsi watu weusi na watu weupe walivyozoea kuishi pamoja katika daraja mbalimbali za kijamii hasa mjini Basra. Zaidi ya hayo, mwandishi huyo huyo anatoka mifano mingi ya huruma waliyofanyiwa watu kutoka Afrika na visiwa vya Bahari ya Hindi, walau hadi kufikia wakati ambapo palipotokea maasi ya Kizanj ambayo yalisababisha mabadiliko mengi katika mielekeo na mitazamo ya watu.

Mfumo wa uhusiano wa masuria na bwana zao, uliopendelewa na taratibu za Kiislamu, ulisababisha mwingiliano wa mataifa uliokuwa chanzo muhimu katika wenyeji wa mijini na wa shamba.

Ingawa kulikuwa na mmiminiko mfululizo wa watu wenye asili ya Kiafrika kuja katika nchi za Kiislamu, kumezwa kwao kwa urahisi katika jamii za Kiislamu kumeacha athari za viwango mbali mbali katika eneo hili, likilinganishwa na sehemu nyingine ambazo vilevile zimekuwa na Waafrika wengi walioenda huko. Mojawapo kati ya matokeo dhahiri ya jinsi Uafrika ulivyomezeka katika Uarabu ni kwamba hamna makundi makubwa ya watu ambao wana tofauti za uasili ambao wana historia na mila za kipekee kama vile ilivyo katika nchi za Amerika.

Katika matabaka ya juu ya jamii za zama za Kiislamu, kuwafanya masuria vijakazi wenye asili ya Kiafrika lilikuwa ni jambo la kawaida sana. Wana wa wafalme na makhalifa kadhaa walikuwa na asili ya uhotara waliourithi kutoka kwa mama zao. Kijakazi mmoja wa Kisudan, aliyekuwa suria wa al-Zahir, ndiye alimzaa Khalifa wa Wafatimi, al-Mustansir. Alikuwa mwanamke mashuhuri na alitawala Misri baada ya kifo cha al-Zahir, wakati ambapo mwanace alikuwa na umri mdogo wa kutoweza kutawala.

Matowashi watwana walijaa katika majumba ya wakuu na watukufu wa nchi, sana sana walitumiwa kama walinzi wa nyumba walimowekwa wanawake. Wengine wao waliwahi kupata vyeo vikubwa na kutekeleza wajibu muhimu katika shughuli za serikali katika enzi za kati. Jambo hili linadhihirika kwa mifano mingi. Towashi mweusi Kafur al-Ikshidi (966) aliyeinukia na kupata cheo cha kuwa mtawala wa Misri na Muflih – 'mweusi' na aliyependwa sana na Khalifa al-Radi (kf. 940), alipewa jukumu la kuunda sera za serikali. Towashi mwingine mweusi ambaye alikuwa msimamizi wa nyumba ya mwana wa mfalme Adud al-Dawlah (982) ndiye aliyekuwa mtu pekee aliyeweza kujiaminisha kwa bwana wake dhalimu, aliyekuwa na tabia ya kumshuku kila mtu; kujiaminisha huku kwake kulihusudiwa na wote.

Jukumu la uaskari-jeshi lililotekelezwa na watumwa lilikuwa ni dhihirisho kubwa la ustaarabu wa Kiislamu na lilikuwa na athari nyingi zisizotazamiwa katika sera za serikali nyingi za Kiislamu nchini na nje.

Askari jeshi weusi wanaonekana mara kwa mara mwanzoni mwa nyakati za Waabbasi na baada ya maasi ya watumwa nchini Irak, ambamo watu weusi walionyesha ujuzi mkubwa wa kuogofya, wa kijeshi, wengi wakaandikwa kazi ya uaskari. Tayari chini ya uongozi wa Khalifa wa Waabbasi Al-Alamin (kf. 813) kiliundwa kikosi maalumu cha walinzi wa Kiethiopia, waliojulikana kama 'makunguru'. Katika mapigano makali ya kupigania utawala katika enzi ya al-Muktadir (kf. 932) kiasi cha askari weusi 7,000 walikuwa wakipigana katika upande wa kundi la Khalifa.

Ahmad ibn Tulun (kf. 844), aliyekuwa gavana wa Misri na baadaye kuwa mtawala wa nchi hiyo, aliunda kikosi kikubwa cha askari jeshi waliokuwa watumwa weusi, hasa wa asili ya Kinubi. Alipokufa, katika milki yake aliyoiacha mlikuwamo askari 24,000 weupe (mamluiki) na 45,000 weusi.

Majeshi ya askari weusi yalikuwa sehemu muhimu ya wanajeshi wa Wafatimi. Wadhifa wao ulizidi kuwa mkubwa katika enzi ya al-Mustansir (1035 - 94) kwa ajili ya kuungwa mkono na mama ya Khalifa aliyekuwa mjakazi wa Kisudan. Walipofikia kilele cha umaarufu wao, walikuwa na idadi ya askari 50,000.

## Maasi ya Wazanj

Mara kwa mara Wazanj walizusha vita dhidi ya Khalifa wakati wa karne ya saba na ya nane, lakini maasi haya yalizimwa kwa urahisi na majeshi ya kawaida.

Walakini, maasi ya Wazanj ya mwaka 869 ndiyo yaliyokuwa makubwa zaidi kati ya yote yaliyofanywa na watumwa weusi katika enzi za kati za Kiislamu. Maasi haya yaliendelea kwa zaidi ya miaka kumi na minne na yalipitia misimu miwili ya (869 - 879) na (879 - 883). Msimu wa kwanza ulikuwa wa kukuzua na kueneza juhudi zao na ulikuwa wa mafanikio makubwa kwa waasi hao. Msimu wa pili ulikuwa wa mapigano ya muda mrefu dhidi ya majeshi bora na kusababisha maanguko ya serikali ya Kizanji. Maeneo ya mapambano yalikuwa yale ya nyanda za chini za Mesopotamia na kusini mwa Uajemi.

Kiongozi wa uasi huu alikuwa Mwarabu, aliyeitwa Ali b. Muhammad, aliyejulikana sana kama *Sahib al-Zanj* (yaani Bwana wa Zanj). Hapo mwanzo Ali alidai kuwa mzaliwa wa ukoo wa Ali, ili ahalalisha uasi huo na kutaka kuungwa mkono. Hata hivyo hakuwa mfuasi wa imani ya Kishia bali alikuwa mfuasi wa Kikhariji, imani ambayo mafundisho yake ya kidini ya kuzingatia usawa wa binadamu yaliruhusu hata Waethiopia kufikia cheo cha Ukhalifa.

Maasi hayo yalianza kama utesi wa kitabaka, kati ya watumwa Wazanji waliodhulumiwa na mabwana wao. Walakini baadaye vikawa vita vikali vya wazi wazi dhidi ya Khalifa. Kwa hivyo basi yakawa ni mapambano ya kisiasa na mapigano ya kijamii na wala sio vita baina ya watu wa mataifa mbali mbali.

Jeshi la Wazanji linakadiriwa kuwa na askari wengi kuliko majeshi ya Khalifa ambao nguvu zao zilisemekana kutokana na idadi ya askari 50,000 hasa mwanzoni mwa vita. Walakini majeshi ya Khalifa yalikuwa na zana bora zaidi na vile vile walilishwa vyema na kila wakati waliongezewa nguvu na majeshi mapya yaliyokuja kujiunga nao.

Wafuasi wa Ali b. Muhammad walikuwa katika vikundi maalum vifuatavyo:

- (1) *Wazanji*: ambao hawakuzungumza lugha za Kiarabu; hawa walikuwa watumwa kutoka Afrika ya Mashariki na waliwasiliana na kiongozi wao kupitia kwa wakalimani.
- (2) *Wakarmatiyya*: Hii ni jamii ya watumwa wa Kiafrika ambao hawakubainika waziwazi kama ni wa kundi gani, lakini inaaminika kuwa walikuwa wa asili ya Kisudan na walizungumza Kiarabu. Hawakuwa na uhusiano wowote na chama cha Karamita.
- (3) *Wanuba*: Hawa walikuwa ni mchanganyiko wa Wanubi na Wanilo; wao pia walikuwa wakizungumza Kiarabu.
- (4) *Wafuratiyya*: Hawa walikuwa watumwa wa asili tofauti tofauti ambao waliishi kwenye kingo za sehemu ya chini ya mto Yufrati, kusini mwa mji wa Wasit. Wao walitofautiana sana na Wazanji na waliweza kuongea Kiarabu.
- (5) *Washuridjiyya*: Hawa walikuwa ni vibarua (*Wakassahin*) walioajiriwa katika vinamasi vya chumvi vya nyanda za chini za Mesopotamia. Katika kundi hili vile vile walikuwamo watu ambao hawakuwa watumwa na pia watumwa ambao walikuwa wameachiliwa huru; na pia wengine ambao walikuwa wameajiriwa katika mashamba ya mitende na miwa.
- (6) Kundi la mwisho lilikuwa la mabedui walioishi katika wilaya za kusini mwa Wasit.

Vikosi vya waasi viliongezeka kutokana na wanajeshi wengi wa Khalifa kutoroka na kujiunga nao. Hatudhamiriri kutoa habari zote za mapambano mbalimbali (katika maelezo haya) ya uasi wa Wazanji bali tunatoa tu muhtasari wa yale matukio muhimu ya mapambano hayo.

Mnamo mwaka wa 870, majeshi ya Kizanj yaliteka bandari iliyokuwa imestawi ya al-Ubulla na kuiharibu. Kuangukia inikononi mwa adui kwa bandari hii kuliwatisha sana wakazi wa Kiajemi wa mji wa bandari ya Abbadan na kuwafanya wasalimu amri. Jambo hili liliwafungulia Wazanji njia ya kuuvamia mkoa jirani wa Khuzistan katika mwaka huo huo. Wazanji walijitawaza wenyewe na kujifanya mabwana wa Jubba na mji mkuu wa al-Ahwaz.

Mwaka uliofuata wa (871) ulishuhudia kukaliwa na kutekwa kwa Basra, bandari kuu ya Irak. Huu ndio uliokuwa ushindi mkubwa sana wa Wazanji na pigo kubwa sana kwa Khalifa wa Waabbasi. Maafa haya ya kutisha yaliyoikumba Basra yalikuwambukwa kwa muda mrefu na vizazi vilivyofuata.

Vikosi vya Wazanji vilifuata katika mashambulizi yake na kuhodhi kuelekea Kaskazini na kuendelea kuteka na kuhodhi miji waliyoipitia ya Wasit (877-78), Numaniya (878) na Jardjaraya, umbali wa maili sabini kutoka Baghdad. Huu ndio uliokuwa upeo wa upanuzi kuelekea Kaskazini.

Kati ya 881-883, Mfalme mtawala wa Waabbasi, al-Muwaffak, alifanya ushambulizi dhidi ya majeshi hayo na kuyasukumia kusini na baadaye akaweza kuyawekea vikwazo vya kiuchumi katika mji wao mkuu wa al-Mukhtara.

Katika mwaka wa 883 baada ya mazingira haya ya miaka mitatu, mji huo ulishindwa katika shambulio na kiongozi wa maasi pamoja na wengi wa makamanda wake wakauawa.

Hapana shaka ya kuwa maasi haya ya muda mrefu yaliithiri sana hali ya uchumi, siasa na jamii katika ulimwengu wote wa Kiislamu. Wakati huo huo yaliwafanya Waislamu kuwa na chuki zaidi kwa Afrika na Waafrika kwa ujumla. Uletaji wa watumwa wa Kizanj uliwekewa mipaka au ukawa chini ya usimamizi mkali. Matokeo mengine yalikuwa ni kuenea sana kwa sifa mbaya za watu weusi katika nchi za Kiislamu.

### *Dhima ya kitamaduni*

Waafrika walichangia, kwa kiasi kikubwa, katika nyanja za utamaduni kama washairi, waandishi, wanamuziki, na wataalamu wa sayansi za Kiislamu.

Katika enzi za Ukhaliifa wa Waumaya na Waabbasi, walikuwepo washairi maarufu kadhaa weusi. Diwani ya mmojawapo wa washairi hao Irar b. Amr (mwanzoni mwa karne ya nane) aliyekuwa mwana wa kijakazi mweusi, imehifadhiwa kwa vizazi vyote vya siku za baadaye katika Kitab al-Aghani na Hamasa. Mshairi mwingine mweusi aliyekuwa na kipawa cha kipekee na ufasaha wa kusema katika kipindi hiki alitwa al-Haykatan. Hata hivyo aliyesifika zaidi na maarufu kwa washairi wote hao alikuwa Abu Mihjan (alikuwa mwaka 726-7). Alizaliwa huko Hijaz na wazazi wa Kiethiopia. Katika ujana wake alifanya kazi ya kuongoza ngamia.

Katika miaka ya mwanzo ya utawala wa ukoo wa Waabbasi, mshairi mmoja mweusi Abu Dulama (aliyekufa t. 778) alisifika kwa ucheshi wake, visa vya kuchekesha, maarifa yake ya fasihi kwa jumla na kipawa cha ushairi.

Mtangulizi mkuu hasa aliyewakilisha sanaa za Kiarabu za kiriwaya alikuwa Amr b. Bahr al-Jahiz (mwenye macho yaliyotokeza/mkodoa macho) wa Basra (alikuwa mwaka wa 868-9) ambako aliishi hadi akafikia umri wa miaka 96. Babu yake alikuwa mweusi na mwendesha ngamia. Ingawaje alikuwa na kilema kama inavyoonyeshwa katika jina lake la bandia, al-Jahiz, alikuwa na akili tambuzi na moyo wa busara.

Alikuwa na elimu ya maarifa mengi na alikuwa mwandishi mwenye ujuzi wote aliyesanii kazi nyingi juu ya takriban tanzu zote za elimu. Halikadhalika alikuwa maarufu kama mtu aliyekuwa mwanafalsafa huru na alitunga hotuba juu ya kanuni za dini. Madhehebu ya Mutazili yaliitwa 'al-Jahiziya' kwa heshima ya ukumbusho wake.

Vile vile Waafrika walikuwa bora katika sanaa za kimuziki na baadhi ya Waafrika stadi katika elimu ya muziki waliitawala medani ya muziki katika karne mbili za mwanzo za enzi ya Kiislamu. Mwanamuziki wa kwanza na aliyekuwa maarufu zaidi wa enzi hiyo alikuwa mtu mweusi aliyetwa Abu Uthman Said ibn Misjah (alifariki t. 715). Hamu yake ya kujifunza stadi za muziki wa kigeni zilimpeleka Ajemi na Syria. Aliporejea Hijaz alileta kwa mara ya kwanza nyimbo za Kibizenti na za Kiajemi katika uimbaji wa nyimbo za Kiarabu. Alitambuliwa kama mmoja wa waimbaji wanne wakuu wa muda huo maalumu.

Mwimbaji mwingine mweusi aliyetukuka alikuwa ni Abu Abbad Mabad ibn Wahb (aliyefariki 743); sanaa yake ilimtunza jina la heshima la 'Mfalme wa waimbaji wa Kimedina.' Kati ya wanafunzi wake alikuwamo pia Sallama al-Kass, mwanamke chotara, mwimbaji aliyependwa sana na Khalifa Yazid b. Abd al-Malik. Wanamuziki na waimbaji wengi weusi walitukuzwa nyakati za makhalifa wa Kiabbasi.

Habari za Kiarabu juu ya maisha ya watu zinataja Waafrika kadhaa waliohusika na mapokeo na vilevile wataalamu wa dini. Aliyejulikana sana kati yao alikuwa mawla mweusi,

Abu Abd Allah Said ibn Jubayr ibn Hisham (alikufa mwaka wa 712) aliyekuwa mtaalamu wa ibada za hija, mfaanuzi wa Kurani, sharia za utawala na masuala ya utaratibu wa sala. Ubingwa wa mtu mweusi mwingine, Abu Ata b. Rabah (alikufa mwaka 733-4) juu ya mapokeo ulienea na kukubalika mahali pengi na mamlaka ya mufti huko Maka yalikuwa juu yake. Wa kwanza kujitambulisha mwenyewe katika nyanja za hadith na fikih katika sehemu za Kiislamu za Misri alikuwa Yazid b. Abi Habib (aliyekufa mwaka 745) aliyekuwa mtoto wa mateka wa vita wa Kinubi. Mtawa mashuhuri na daktari mkuu wa sufi alikuwa towashi mweusi Abu'l-Hassan al-Baghdadi, aliyejulikana zaidi kwa jina la Khayr al-Nassaj (aliyekufa mwaka 934). Alifanya kazi ya kufuma hariri kabla ya kupewa uhuru wake na bwana wake.

### *Waafrika katika Nchi za Bara Hindi, Kusini mwa Asia na Uchina*

Kuna ushahidi haba unaonyesha kuwepo kwa Waafrika nchini India katika wakati huu. Kama alivyosema J. Burton Page, 'kuna habari chache sana kuhusu idadi, hadhi na dhima ya Waethiopia katika nyakati za awali sana za Kiislamu.' Kuna uwezekano kuwa uchunguzi wa dhati wa hifadhi za kitaifa za Kihindi na vilevile wa utajiri uliomo katika fasihi zilizoandikwa kwa lugha nyingi za kienyeji zilizoko hasa katika sehemu za kusini na Maghribi ya bara hili, ungetupatia mambo mengi ya hakika. Kwa hivi sasa tuko katika hali nzuri zaidi kuhusu habari tulizo nazo juu ya kuwepo kwa watumwa weusi wa Kiafrika katika Indonesia na Uchina.

Watumwa weusi wa Kiafrika walijulikana katika visiwa vya Malay tangu zamani za nyakati za kwanza za karne ya nane na walijulikana kwa ujumla kama Wazanji.

Katika hadithi ya utawala wa ukoo wa kifalme wa T'ang wa Uchina katika matukio ya 724 kuna habari za makaribisho ya ubalozi uliotumwa na mtawala wa milki ya Srivijaya iliyopo Palembang katika Sumatra. Mwanamwali wa Kizanj alitolewa kama ushuru pamoja na bidhaa nyingine za kigeni. Hili halikuwa tukio la kipekee, kwani tangu kati ya mwaka 813 na 818 milki nyingine ya Kiindonesia, ile ya taifa la Kijava la Kalinga, lilipeleka ujumbe mara tatu kwa baraza la mfalme wa T'ang, Hsien Tsung. Katika vitu vingine vya tunu vilivyotolewa kama zawadi ilikuwa ni pamoja na vijana kadhaa wa Kizanj, wasichana kwa wavulana. Pia, imeandikwa katika hadithi ya utawala wa ukoo wa ufalme wa Sung, kuwa mnamo mwaka 976, mfanyabiashara mmoja wa Kiarabu alimleta katika baraza la mfalme, mtumwa wa K'un Lun aliyekuwa na macho yaliyoingia ndani sana, na mwili mweusi.'

Vijana na wanawali hawa weusi walikuwa ni sehemu tu ya kundi kubwa la watumwa wa Kiafrika walioletwa na wafanyabiashara wa Kiarabu katika jimbo hili. Katika mwaka wa 1178 afisa wa Kichina alionyesha kutanabahi kwake juu ya uingizwaji huu wa watumwa wa Kiafrika. Akiandika juu ya sehemu isiyobainika ya pwani ya Afrika Mashariki ambayo aliita '*Kun-lun Ts'eng-chi*' alieleza juu ya watu wasiostaarabika, waliokuwa na miili yenye weusi wa kung'aa na nywele za kipilipili ambao walikamatwa baada ya kushawishiwa kwa vyakula. Aliendelea kueleza kuwa, maelfu ya watu hawa weusi yaliuzwa kama 'watumwa wa kigeni.'

Ilionekana kwamba sehemu fulani ya biashara hii ya binadamu hawa ilisafirishwa kwa meli za wafanyabiashara wa Kiarabu hadi Uchina, kupitia visiwa vya Malay. Mji wa Kanton ndio uliokuwa bandari kuu ya kupokea na kuwasambaza watumwa.

Halikadhalika kuna ushahidi wa kazi walizozifanya watumwa wa Kiafrika katika nyanja za kijamii na kiuchumi. Masimulizi ya matukio ya Kichina yanataja ya kuwa hao 'watumwa wa kishetani' walitumiwa melini kama kalafati kuziba sehemu zenye nyufa ambamo maji ya bahari yangaliweza kupenyeza na kuingia melini, kwani wao walikuwa waogeleaji hodari ambao hawakuyafunga macho yao walipokuwa ndani ya maji. Yamkini kuwa lilikuwa ni

jambo la kawaida kwa watumwa hao kutumiwa kama watumishi wa nyumbani na matabaka ya kitajiri ya watu walioishi katika miji mikubwa. Akitumia maelezo kutoka vyanzo bora vya maandishi ya Kichina G. Ferrand, alieleza juu ya dhima yao kama wanamuziki katika milki za Kisumatra za Srivijaya (*san-fo-ts'i*).

Kuwepo kwa Waafrika pote pote ulimwenguni chanzo chake sio katika uhamisho wa nguvu wa watu wengi kwenda bara za Amerika. Imeonekana ya kuwa tayari tangu karne ya saba hadi ya tisa ya enzi ya Ukristo idadi kubwa za Waafrika zilikuwapo katika sehemu nyingi za bara la Asia na Waafrika hao walikuwa na mamlaka muhimu mbali mbali katika jamii wakichangia sana kuendeleza nyanja za uchumi, siasa na ustaarabu.

Inasikitisha ya kuwa, ingawa mkumbo wa Afrika katika bara la Asia una umuhimu wa kihistoria, bado habari zenyewe hazijakamilika; nazo zinatokana na vyanzo vya habari visivyo vya Kiafrika. Ili kupata habari kamili, kuna haja ya haraka ya kutafiti jinsi Waafrika walivyojiona katika kuhusiana kwao na wenyeji wa nchi hizo za kigeni walimohamia.



---

## *Mahusiano kati ya kanda mbalimbali za Afrika*

27

Kipindi kuanzia karne ya saba hadi kufikia karne ya kumi na moja kilikuwa cha ustawi mkubwa wa mahusiano kati ya maeneo tofauti tofauti ya Afrika. Ukweli kwamba ustawi huu ulitokea sawia na kuenea kwa Uislamu uliwafanya waandishi wengine kusema kuwa ilikuwa ni kutamalaki kwa Waarabu na usilimishaji vilivyoitoa Afrika ya tropiki katika upweke wake na kuiunganisha tena na nchi nyingine za ulimwengu. Licha ya mapengo makubwa yaliyomo katika vyanzo vya habari, taarifa zinazopatikana kwa hivi sasa zinathibitisha usemi wa C. Coquery -Vidrovitch kuwa mojawapo ya tabia za jamii za Kiafrika ni kuwa hata mara moja hazikujitenga na watu wengine. Bara la Afrika limekumbwa na manbo mawili makubwa: kuhama kwa watu na biashara kubwa za masafa marefu. Maandishi ya E.W. Bovill, C.A. Diop na T. Obenga na wengineo, yameonyesha nguvu za mahusiano kati ya nchi za Kaskazini na kusini mwa Sahara tangu zama za zama<sup>1</sup>. Licha ya maelezo haya lazima ifahamike kuwa kuunganishwa kwa sehemu fulani za Afrika kwenye milki ya Kiarabu kulitoa nguvu mpya katika mahusiano baina ya Waafrika<sup>2</sup>. Athari za Kiarabu na za Kiislamu zilisababisha mabadiliko; moja baada ya jingine, katika eneo lote barani, na yakawa ndiyo chanzo cha ustawi wa Maghrib, Misri na watu wa Sahara tangu karne ya nane na kuendelea<sup>3</sup>. Kwingineko athari hizo zilikuwa kama jambo la kigeni tu kutoka nje ambalo umuhimu wake ulikuwa wa ngazi tofauti tofauti kulingana na maeneo ya kijiografia kuhusiana na njia zilizotumiwa na Waislamu katika kupenyeza nchi hizo.<sup>4</sup>

### *Kustawi kwa biashara kati ya nchi mbalimbali*

Kutamalaki kwa Waarabu hakukuleta tu mabadiliko makuu katika mipaka ya kijiografia katika ulimwengu wa Mediterania ambao ulitawaliwa, kati ya karne ya saba na ya kumi na moja, na utawala wa Kiislamu, lakini pia kuliipa biashara ya kimataifa nguvu ya ajabu, hasa baada ya kuanguka kwa milki hiyo. Licha ya michafuko ambayo daima ilikuwa sifa kubwa ya utawala wa dola hiyo, ulimwengu wa Kiislamu ulibaki kuwa chimbuko pekee la biashara ya ulimwengu hadi karne ya kumi na tatu.

1 Taz. Juzuu II Sura 20 na 22

2 Kuhusu utanuzi wa Kiislamu Taz. Sura 2 na 3 ya juzuu hili.

3 Taz. Sura 7 hadi 12 katika juzuu hili.

4 Taz. Sura 19 mpaka 21 ya juzuu hili.



27.1 Uhusiano kati ya sehemu tofauti za Afrika kuanzia karne ya saba hadi ya kumi na moja (A. Bathily)

Biashara kati ya nchi za Kiafrika, wakati wa kipindi hiki kinachojadiliwa, ilikuwa na sifa tatu muhimu:

- (1) Maendeleo katika njia za mawasiliano.
- (2) Upanuzi wa ushirikiano wa kibiashara.
- (3) Kuongezeka kwa kiwango cha biashara.


Kwa kuimarisha mahusiano ya kudumu kati ya Afrika ya Kaskazini na Asia ya Maghribi, utamalaki wa Kiarabu ulilicta mazingira ya kufaa ya matumizi makubwa ya ngamia.

Ijapokuwa ngamia walikwisha kuwepo Afrika ya Kaskazini kwa karne kadhaa, kuenea kwa matumizi yake kama mnyama wa kubeba mizigo katika biashara ya kuvuka Sahara kulianzishwa katika enzi ya Uislamu na kuendelea. Ndiyo maana nchini Moroko, kuchanganya kizazi cha ngamia mwenye nundu mbili wa Asia ya kati na yule mwenye nundu moja wa asili ya Kiarabu kwa kutumia taratibu maalumu za uteuzi, kukazalisha aina mbili za ngamia. Aina ya kwanza ni ngamia aendae polepole lakini mwenye nguvu za kubeba mizigo mizito ambaye alitumika kwa biashara; aina ya pili ni ngamia mwenye mbio na mwepesi zaidi ambaye alitumiwa kwa kuwabeba wajumbe wa kupeleka habari (mehari).

Sahara Maghribi pia ilisifika kwa uzalishaji wa ngamia. Kwa mujibu wa maelezo ya al-Bakri, mfalme wa Sanhaja alikuwa na ngamia wa uzao bora zaidi ya 100,000 kwa ajili ya jeshi lake. Idadi ya ngamia waliokuwa wakifanya misafara mbali mbali kati ya Sudan, Maghrib na Misri katika mwaka mzima ilikuwa kwa maelfu<sup>5</sup>.

Jambo jingine la manufaa lililotokana na upanuzi wa Uislamu ni kwamba ulichochea usafiri wa baharini. Makundi mengi ya merikebu zenye nguvu yaliundwa na yakawawezesha wafanyabiashara wa Kiislamu kudumisha biashara kati ya Afrika Mashariki na nchi za Bahari ya Hindi, Bahari ya Shamu na Mediterania. Bandari kubwa zenye guda za kuundia merikebu zilianzishwa katika Maghrib kama vile Tunis (karne ya nane), Bijaya (Bougie) na Mahdiyya (915), Algiers (946), Oran (902) na Arzila (karne ya kumi). Nchini Misri, bandari ya kale ya Aleksandria ilifufuliwa tena. Ilikuwa kati ya karne ya nane na ya kumi na moja ambapo mifano hasa ya vyombo vikubwa vya biashara vya bahari ya Mediterania vilivyokuwa na muundo wa milingoti iliypambwa kwa matanga ya pembe tatu, vilipoanza kuundwa chini ya ulinzi wa majeshi ya wanamaji ya Kiislamu. Kiufundi, muundo wa meli hizi ulikuwa umetokana na muundo wa meli za kibiashara za zamani za Mediterania na miundo ya meli za Bahari ya Hindi. Siku nyingi kabla ya kubuniwa kwa dira na vifaa vingine vya usafiri wa majini, ilikuwa ni kawaida ya wanamaji wa Kiislamu kusafiri baharini kwa masafa marefu kwa kutumia mbinu iliyoitwa, 'Sidereal rose,' yaani kwa kuusoma mkao wa nyota na sayari nyingine.

Kati ya karne ya saba na ya kumi na moja, biashara kati ya nchi mbalimbali barani ilikuwa imeshamiri sana. Ishara ya wazi iliyobainisha maendeleo ya shughuli hizi za kiuchumi ilikuwa ni kuzuka na kukua kwa mji. Katika mwaka wa takriban 757 soko la zamani katika Tafilalet lilikua na kuwa mji wa Sijilmasa, na kisha kuwa kituo muhimu cha biashara za kuvuka Sahara. Kayrawan, ambao baadaye ulichukua nafasi ya mji wa kale wa Karteji, pia ulianzishwa. Katikati ya karne ya nane, kulianzishwa mji wa Tahert katika Maghrib ya kati, na mnamo mwaka wa 800 Waidrisi waliustawisha mji wa Fez. Chini ya utawala wa Wafatimi, mji



27.2 Kutoka kambi moja hadi nyingine: njia za kila mwaka za wachungaji katika eneo la Sahel; la Mali (Karibu na Gumbu ya Sahel) (C. Meillassoux)

wa Kairo ndio uliokuwa egemeo kwa Uislamu maeneo ya Maghribi, Mashariki na Afrika kusini mwa Sahara. Maghribi mwa Sahara, mji wa Awdaghust ukawa soko lililounga Afrika ya weusi na Barbary kama vile ulivyokuwa mji wa Zawila katika Sahara ya kati. Njia ambazo zilitumika sana au kidogo kulingana na hali ya kisiasa ziliunganisha masoko haya na mengine yaliyokuwa kusini mwa Sahara. Hivyo, Ghana/Kumbi, mji mkuu wa milki ya Ghana/Wagadu, Silla na Barisa katika mto Senegal na Kaw-Kaw katika mto Niger, iliunganisha ulimwengu wa Kiislamu na sehemu za savana na zile za msitu wa Afrika Maghribi. Katika pwani ya Afrika Mashariki, wafanyabiashara wa Kiislamu walifanya makao katika miji ya biashara kama vile Mogadishu, Barawa, Malindi, Mombasa, Kilwa na Sofala katika bara na vile vile katika visiwa vya Pate, Kanbalu (Pemba), Kizimkazi (Zanzibar), n.k.<sup>6</sup>

Kukua upya kwa miji kulikotokea tangu karne ya saba na kuendelea kulisababisha kupanuka kwa njia za biashara na vile vile kukaharakisha kuunganisha shughuli za kiuchumi kati ya eneo na eneo au nchi na nchi.

6 Taz. Sura 21 ya juzuu hili.

Bidhaa zilizofanyiwa biashara zaidi wakati huo ziko katika makundi manne yafuatayo:

- (1) Malighafi.
- (2) Bidhaa za vyakula.
- (3) Bidhaa za anasa (kwa matumizi ya nyumbani).
- (4) Bidhaa za anasa nyinginezo.

Malighafi muhimu zaidi zilikuwa chuma, kitani, pamba, gundi na nili. Chuma kutoka milki ya Ghana kiliuzwa katika nchi nyingine za Afrika Maghribi. Tunajua kwa uhakika kuwa Afrika Mashariki iliuzia India chuma. Katika Maghrib, machimbo yaliyokuwa Sabta na Oran na katika eneo la kati ya Sale na Marrakesh yalikuwa bado yakichimbuliwa katika karne ya kumi na moja.

Biashara ya kitani, pamba, gundi na nili inahusishwa na maendeleo ya viwanda vya nguo. Kitani iliwahi kupandwa Maghrib na pamba nayo ilipandwa katika sehemu kadha wa kadha (mfano: kandokando ya mto wa Senegal, Ethiopia, Maghrib, n.k.). Gundi, ambayo ilitumiwa katika hatua ya mwisho ya kutengeneza vitambaa vya nguo, ilitoka kwenye misitu ya miti ya gundi ya Sahara Maghribi au Kordofan. Mnili, ambao labda una asili ya Kihindi, ulipandwa katika Maghrib tangu karne ya kumi na moja, na kutoka hapo, nili iliuzwa Sudan Maghribi.

### Bidhaa za vyakula

Biashara ya ugawaji wa bidhaa za vyakula ilikuwa ya kwanza kwa ukubwa katika biashara baina ya nchi mbalimbali za Kiafrika. Ngano iliyotolewa Maghrib ilisafirishwa kwa misafara kupitia Sijilmasa hadi Sahara Maghribi na Sudan. Ingawaje kulikuwa na soko kubwa nyumbani, bado Misri iliuzwa nafaka ya ziada kwenda Libya na Nubia kwa kutumia misafara, na kwenda Sirenaika kwa inashua.

Mtama wa aina mbali mbali, mchele, na siagi ya shea kutoka Sudan Maghribi na halzeti kutoka Maghrib viliuzwa pande zote. Samaki wa kukaushwa kwa moshi kutoka pwani na katika nchi zenye mito mikubwa walisafirishwa bara. Biashara ya chumvi ilikuwa sehemu kubwa ya biashara ya bidhaa za chakula. Chumvi ya mawe kutoka Sahara na chumvi ya baharini zilishindania biashara huko bara, lakini bado hazikutosheleza mahitaji makubwa yaliyokuwepo kama inavyohibitishwa na hali ya juu ya thamani ya bidhaa hii, ambayo kulingana na Ibn Hawkal ingeweza kufikia dinari 200 hadi 300 kwa mzigo mmoja wa ngamia.

### Bidhaa za anasa za nyumbani

Bidhaa hizi zilikuwa hasa ni watumwa na farasi. Habari kutoka Uarabuni zasisitiza umuhimu wa biashara ya watumwa weusi iliyofanywa na wafanyabishara wa Kiislamu, ingawa, kwa kweli biashara hii ilifanywa katika pande zote mbili. Katika baraza za kifalme za Sudan kulikuwapo na watumwa wa Kiarabu na wa Kiberiberi, na bila shaka vile vile watumwa wa asili ya kizungu. Ni yamkini ku sema kuwa kuongezeka kwa uchumi na mambo yaliyofungamana nao (kama vile maendeleo ya miji na fahari za maisha ya kifalme) kulisababisha mahitaji makubwa ya watumishi.

Hata hivyo, kutoa makadirio ya idadi ya watumwa waliouzwa kutoka Afrika ya weusi kwa ulimwengu wa Kiislamu, kama R. Mauny na T. Lewicki walivyofanya, ni jambo la hatari sana. Mwandishi wa kwanza anaamini kuwa idadi ya Waafrika weusi waliouzwa nje ya Afrika ni kama 20,000 kwa mwaka mmoja, au kama milioni mbili hivi kwa karne nzima katika enzi

Bidhaa zilizofanyiwa biashara zaidi wakati huo ziko katika makundi manne yafuatayo:

- (1) Malighafi.
- (2) Bidhaa za vyakula.
- (3) Bidhaa za anasa (kwa matumizi ya nyumbani).
- (4) Bidhaa za anasa nyinginezo.

Malighafi muhimu zaidi zilikuwa chuma, kitani, pamba, gundi na nili. Chuma kutoka milki ya Ghana kiliuzwa katika nchi nyingine za Afrika Maghribi. Tunajua kwa uhakika kuwa Afrika Mashariki iliuzia India chuma. Katika Maghrib, machimbo yaliyokuwa Sabta na Oran na katika eneo la kati ya Sale na Marrakesh yalikuwa bado yakichimbuliwa katika karne ya kumi na moja.

Biashara ya kitani, pamba, gundi na nili inahusishwa na maendeleo ya viwanda vya nguo. Kitani iliwa kupandwa Maghrib na pamba nayo ilipandwa katika sehemu kadha wa kadha (mifano: kandokando ya mto wa Senegal, Ethiopia, Maghrib, n.k.). Gundi, ambayo ilitumiwa katika hatua ya mwisho ya kutengeneza vitambaa vya nguo, ilitoka kwenye misitu ya miti ya gundi ya Sahara Maghribi au Kordofan. Mnili, ambao labda una asili ya Kihindi, ulipandwa katika Maghrib tangu karne ya kumi na moja, na kutoka hapo, nili iliuzwa Sudan Maghribi.

### Bidhaa za vyakula

Biashara ya ugawaji wa bidhaa za vyakula ilikuwa ya kwanza kwa ukubwa katika biashara baina ya nchi mbalimbali za Kiafrika. Ngano iliyotolewa Maghrib ilisafirishwa kwa misafara kupitia Sijilmasa hadi Sahara Maghribi na Sudan. Ingawaje kulikuwa na soko kubwa nyumbani, bado Misri iliua nafaka ya ziada kwenda Libya na Nubia kwa kutumia misafara, na kwenda Sirenaika kwa mashua.

Mtama wa aina mbali mbali, mchele, na siagi ya shea kutoka Sudan Maghribi na halzeti kutoka Maghrib vilizwa pande zote. Samaki wa kukaushwa kwa moshi kutoka pwani na katika nchi zenye mito mikubwa walisafirishwa bara. Biashara ya chumvi ilikuwa sehemu kubwa ya biashara ya bidhaa za chakula. Chumvi ya mawe kutoka Sahara na chumvi ya baharini zilislindania biashara huko bara, lakini bado hazikutosheleza mahitaji makubwa yaliyokuwepo kama inavyohibitishwa na hali ya juu ya thamani ya bidhaa hii, ambayo kulingana na Ibn Hawkal ingeweza kufikia dinari 200 hadi 300 kwa mzungu mmoja wa ngamia.

### Bidhaa za anasa za nyumbani

Bidhaa hizi zilikuwa hasa ni watumwa na farasi. Habari kutoka Uarabuni zasisitiza umuhimu wa biashara ya watumwa weusi iliyofanywa na wafanyabishara wa Kiislamu, ingawa, kwa kweli biashara hii ilifanywa katika pande zote mbili. Katika baraza za kifalme za Sudan kulikuwapo na watumwa wa Kiarabu na wa Kiberiberi, na bila shaka vile vile watumwa wa asili ya kizungu. Ni yamkini kusema kuwa kuongezeka kwa uchumi na mambo yaliyofungamana nao (kama vile maendeleo ya miji na fahari za maisha ya kifalme) kulisababisha mahitaji makubwa ya watumishi.

Hata hivyo, kutoa makadirio ya idadi ya watumwa waliouzwa kutoka Afrika ya weusi kwa ulimwengu wa Kiislamu, kama R. Mauny na T. Lewicki walivyofanya, ni jambo la hatari sana. Mwandishi wa kwanza anaamini kuwa idadi ya Waafrika weusi waliouzwa nje ya Afrika ni kama 20,000 kwa mwaka mmoja, au kama milioni mbili hivi kwa karne nzima katika enzi.

ya kati. Yule wa pili anaamini kwamba watumwa milioni 12 hadi 16 weusi walipitia katika mji wa Kairo katika karne ya kumi na sita pekee. Ni wazi kwamba makadirio kama haya yametiliwa chumvi kupindukia. Kuna sababu zisizopungua tatu zinazoeleza kwa nini biashara hii ilikuwa na idadi ndogo kuliko zile tulizopewa.

- (1) Hali duni ya uchumi wa Waislamu katika kipindi hiki, ambayo haingeweza kuchukua kiasi kama hicho cha watumwa. Tukiachia kando Wazanji (yaani watumwa weusi) kutoka nyanda za chini za Irak<sup>7</sup> kihistoria hakuna kundi kubwa lolote la watu weusi kutoka kusini mwa Sahara lililokuwako mahali popote Uarabuni.
- (2) Gharama kubwa za watumwa kutokana na hatari zilizokuwepo katika kuvuka jangwa, zisingeruhusu kuyavusha makundi makubwa ya watumwa. Aidha ni muhimu kukumbuka.
- (3) Kabla ya vita vya kidini, Waislamu walipata watumwa kutoka sehemu mbili: Ulaya ya kati na Mashariki (Waslav), na Tirkestan<sup>8</sup>. Watumwa weusi walithaminiwa hasa kwa madhumuni ya kutumiwa kama watumishi wa nyumbani - matouwashi, masuria, walezi, wanyonyeshaji, wapishi, n.k. Vizalia vya masuria na walezi hawa waliingizwa katika jamii za Kiislamu kama wananchi halisi.

Kutokana na maendeleo ya biashara kati ya Afrika ya weusi na ulimwengu wa Kiislamu, farasi wa Kiarabu waliongezeka katika nchi za savana ambamo kutokuwemo kwa malale kuliwezesha kuendelea kuishi kwao. Biashara ya farasi wa Kiarabu (*barbs*) ilisababisha kupotea kwa aina ya farasi wadogo wa kimo, wa kienyeji, ambao walikuwa wakitajwa hadi kufikia karne ya kumi na moja. Nchi za Numidia na Nubia, punde si punde zikachagua kufuga farasi wa Kiberiberi ambao waliwauza Sudan Maghribi na kati.

### Bidhaa za anasa

Bidhaa za anasa zilikuwa hasa vitambaa vya nguo, vito vya thamani, lulu na pembe za ndovu. Maandishi ya wakati huo yanasisitiza hasa kustawi kwa ufundi wa nguo katika Maghrib na Misri. Bidhaa za hariri kutoka Gabes na bidhaa za sufi kutoka Kayrawan ziliuzwa kwa thamani kubwa katika masoko yote. Awdaghust iliua nguo zilizotiwa rangi nyekundu na samawati nao mji wa Taranka katika sehemu za katikati za mto wa Senegal ulijulikana kwa shuka zake za pamba (shakkiyyat) ambazo zilipelekwa na wafanyabiashara nchi za Kaskazini na nchi nyingine jirani. Mabadiliko ya kijamii (maendeleo ya miji, kutajirika kwa matabaka yaliyokuwa na inamlaka ya utawala, kutokana na biashara ya kigeni, kuongezeka kwa watu) yalikuwa chanzo cha kupanuka kwa ufundi wa nguo katika nyanja zote.

Kuhusu madini ya thamani, dhahabu ndiyo iliyochukua nafasi ya kwanza. Katika kipindi hiki tunachojihusisha nacho, kulikuwa na sehemu nyingi za utoaji wa dhahabu, ambazo, kwa kiasi kisicholingana, ziliziuzia sehemu nyingine za bara hili na masoko mengine ya kigeni. Masoko yaliyouziwa bidhaa hii, tukianza na soko kubwa hadi soko dogo, ni kama ifuatavyo:

- (1) Bambuk/Galam na Bure katika Afrika Maghribi
- (2) Kusini mwa Afrika.
- (3) Nubia.

7 Taz. Sura 26 ya juzuu hili.

8 Taz. Sura 1 ya juzuu hili.

Shaba ilitumiwa kama malighafi katika kutengeneza vitu vya sanaa na vinginevyo vya anasa. Ilipokatwa katika umbo la pete ilitumiwa kama pesa katika sehemu fulani (k.m. Silla katika mto Senegal). Kwa kweli biashara ya shaba ilifanywa sana katika nchi zilizoizalisha (Katanga, Aïr, na Sahara Maghribi), nchi za Kiyoruba na Kaskazini mwa Afrika ambako ukuaji wa sanaa uliongeza mahitaji yake<sup>9</sup>

Kusini mwa Maghrib na Sudan ya kati zilisifika sana kwa utoaji wa lulu na vito vya thamani (ageti, amazoniti, n.k.). Nchi ya Beja iliyo katikati ya Bahari ya Shamu na mto Nili ilikuwa na machinbo ya vito na zumaradi, vito ambavyo vilichimbwa na Waislamu.

### Usambazaji wa ufundi

Biashara na safari za watu za shughuli hizo, ndiyo mambo yaliyokuwa chanzo cha usambazaji wa ufundi. Maarifa tuliyonayo sasa yanaashiria kuwa kulikuwa na tanzu tano zilizopata mafanikio na kisha kuenea katika bara, yaami:

- (1) Uchimbaji na usafishaji madini
- (2) Ukulima
- (3) kazi za mikono
- (4) Mbinu za biashara
- (5) Maarifa ya kivita.

### Uchimbaji na usafishaji madini

Uchimbaji na usafirishaji madini ulikuwa ukisitawi vyema katika sehemu zote. Katika nchi za Kiislamu za magharibi, majaribio yalifanywa ya kuendeleza maarifa ya kuchuja madini kutoka kwenye mawe yenye madini. Katika sehemu za Hispania zilizokuwa za Kiislamu, njia mpya ilitumiwa ya kutenganisha taka na azuriti na inawezekana kuwa mbinu hii ilitumika pia katika Maghrib. Mjadala juu ya kusambaa kwa matumizi ya chuma katika Afrika bado unaendelea, lakini maandiko ya L.M. Diop kwamba wenyeji ndio chanzo halisi cha ufujaji chuma yanaelekea kukubalika zaidi kuliko nadhariatete zinazodai usambaaji wa ufundi huo kutoka nje ambazo zinashikiliwa na wanahistoria wengi. Kwa vyovyote vile, sasa imethibitika kuwa watu wengi wa Afrika walitoka katika enzi ya Mawe na kuingia enzi ya Chuma mnamo kikwi cha kwanza cha enzi ya Ukristo. Mabadiliko ya kijamii yaliyoendelea polepole barani labda ndiyo yaliyoleta juhudi za dhata na pengine kuboreshwa kwa ufundi wa kutengeneza metali.

### Kilimo

Kuhusu kilimo, wakati huu unabainishwa na kuenea kwa mbinu fulani za ukulima na ukuzaji wa mazao mapya. Katika Maghrib na oasisi za Sahara, kwa mfano, mbinu mpya ya kumwagilia iliyotumia foggara au mifereji ya inawe ilitumiwa. Hü ilileta uwezekano wa kuanzisha na kueneza ukuzaji wa mazao mapya kama vile mpunga, pamba na miwa.

Sehemu ya ukulima ya Gangara (Assaba katika Mauritania) iliyokuwa na makonde yaliyopigwa matuta na kuzungushiwa nyua za kuta, magofu yake yangali yapo hadi leo hii na bila shaka ni ya tangu kipindi cha Wamoravi.

Chini ya mwamko mpya wa biashara kati ya nchi mbali mbali, mimea au aina mpya za mimea hiyo hiyo zilisambazwa nje ya mahali pake pa asili. Aina nyingine za mpunga wa asili



ya Asia zilisambaa hadi oasisi za Misri na kusini mwa Moroko. Mtama, ambao asili yake ni sehemu ya Afrika kusini mwa Sahara, ulilimwa katika Misri ya Juu, Sirenaika, Algeria na hata katika Shamu na kusini mwa Ulaya.

Mtende, ambao asili yake ni Mesopotamia na Ghuba ya Uajemi, ulionekana Misri tangu enzi za Farao, lakini kilimo chake kilizidishwa kati ya karne ya saba na ya kumi na moja. Kusini mwa Tunisia na Maghribi mwa Sahara zilikuwa sehemu muhimu sana za mitende. Jamii za wafanyabiashara wa Kiislamu na Kiyahudi ndizo zilizoleta maboga kama matikiti, matango, n.k., katika Sudan (Ghana na Kanem) ambayo yalipandwa katika mabustani. Ukuzaji wa migomba na minazi ulihusishwa na ueneaji wa biashara ya Bahari ya Hindi.

### Maarifa ya ufundi

Kuna habari chache zaidi kuhusu njia zilizotumika katika kusambaza maarifa ya ufundi. Mambo mawili yapaswa kutajwa. Kwa taarifa za al-Bakr, Sfaks, mji uliokuwa mashuhuri kwa mashuka yake, ulipata mbinu za kulainisha vitambaa kutoka kwa watu wa mji wa Aleksandria.

Utengenezaji wa karatasi kutokana na kitani, na halafu kutoka kwenye pamba kwa kutumia maarifa kutoka Uchina, ni jambo ambalo lilileta mapinduzi halisi kuanzia inwishoni mwa karne ya kumi na kuendelea. Wakati ngozi za wanyama na mafunjo, vifaa ambavyo hadi wakati huo vilitumiwa kuhawilisha matini, havikutosheleza kusambaza elimu kwa wote, karatasi rahisi zilizotengenezwa kwa kutumia mbinu mpya zilileta mwamko mpya wa shughuli za kisomi<sup>10</sup>

### Mbinu za biashara

Maendeleo ya biashara yalisababisha utumiaji wa njia za hali ya juu za malipo. Sifa kubwa sana katika maendeleo haya ni hatua kubwa ya utumiaji wa pesa katika shughuli za kiuchumi za kikanda. Wakati ambapo mfumo wa pesa katika Maghrib ulifungamanishwa na ule wa ulimwengu wa Kiislamu (ambao ulitumia dinari ya dhahabu), kulikuwa na aina mbalimbali za mifumo ya pesa katika sehemu nyingine barani: kombe za aina aina zikiwemo kauri (Cypraea moneta) kutoka Visiwa vya Maldive, pete za shaba, vinoo vya sabuni na vipande vya vitambaa vya nguo vilitumika sawia kwa madhumuni ya kufanya biashara.

Katika ulimwengu wa Kiislamu, mbinu za biashara ziliendelezwa sana. Wafanyabiashara wa huko tayari walitumia hawala na hati za kulipia fedha (suftaja) na ahadi za kulipa (shakk) au hundi. Wafanyabiashara waliojishughulisha na biashara za kuvuka jangwa la Sahara walifanya mtandao wenye ufanisi wa juu wa biashara, uliokitwa ama kwenye msingi wa familia au kampuni za pamoja, wakiwa na washiriki waliowasiliana nao katika kila mahali muhimu. Walifanya biashara na nchi zilizokuwa nje ya miliki ya Uislamu kwa msaada wa watu wa kati (wakalimani) walioajiriwa katika vituo muhimu kama vile Ghana/Kumbi. "Biashara bubu" iliyotajwa katika tarhi kadha wa kadha baada ya Herodotus yaclekea, kama alivyoonyesha Paulo Farias, kuwa mojawapo ya ngano ambazo hazifi kwa urahisi.

### Maarifa ya kivita

Katika savana ya Sudan, ongezeko la uagizaji farasi wa Kiarabu na ukuaji wa ufuaji wa metali, kwa upande mmoja, na maendeleo ya ndani ya jamii katika sehemu hiyo, kwa upande mwingine, vilileta mabadiliko makubwa katika maarifa ya kivita. Vitani, askari jeshi wapanda

10 Kubusu swala hili Ling. Sura I ya juzuu bili.

farasi wakawa muhimu zaidi kuliko askari wa miguu. Muundo wa zana za kivita vile vile ulibadilika. Uta na mshale ambazo ndizo zana zilizofikiriwa kama za kawaida na ambazo zilitumiwa sana na jamii zilizozingatia usawa wa binadamu wote, punde zikaachwa na badala yake zikatumika zana za chuma ambazo zilihitaji matengenezo ya ufundi wa hali ya juu zaidi kulingana na hali ya jamii za siku hizo. Utengenezaji wa ngao nao vilevile ulipata maendeleo mapya katika nyakati hizo. Kwa hiyo, ngao zilizoitwa Lamta, zilizotengenezwa na mbari moja ya Sahara, ambayo pia ilijulikana kwa jina hilo, zikawa mashuhuri sana hadi nchi za Maghrib. Kutokana na usafiri wa haraka zaidi (kwa kutumia farasi na ngamia) na silaha kufanywa bora zaidi, vita vikachukua nafasi muhimu sana katika kukua kijamii kwa jamii za Kiafrika.

### *Sifa za msingi za maendeleo ya jamii za Kiafrika kuanzia karne ya saba hadi karne ya kumi na moja*

Sifa tatu muhimu zilitawala mabadiliko ya kijamii katika kipindi hiki:

- (1) Uhamaji wa makundi makubwa ya watu.
- (2) Mchapuko katika kuleta tofauti za kijamii kutokana na mgawanyo wa kazi.
- (3) Kutokea kwa mapambano ya kitabaka, kama ilivyodhihirika katika maasi na vita vya wenyewe kwa wenyewe katika nchi kadhaa.

#### **Miguro ya Watu**

Uhamaji wa makundi makubwa ya watu ulibadilisha sana makazi ya wenyeji barani. Vyovyote itakavyosemwa kuhusu uhamaji wa Wabantu, miguro ya watu hao kuvuka Afrika ya Kati, Mashariki na Kusini iliendelea katika kipindi hiki kinachotuhusu<sup>11</sup>. Kustawi kwa biashara ya kuvuka Sahara kulikuwa chanzo cha makundi mengi ya Kiberiberi kupenya zaidi ndani ya Sahara. Nguvu za wageni hawa pengine ndizo zilizosababisha uhamaji kwa wingi wa baadhi ya watu weusi kama vile Mame-Wolof na Wasereer kutoka Tagant (Mauritania) kwenda kusini Maghribi (Senegal Maghribi). Wasonike Dyula (wafanyabiashara) wa Ghana ambao walikuwa wafanyabiashara wa kati katika biashara ya kuvuka Sahara, walianza vituo kadhaa vya biashara katika mto Niger na vijito vyake. Idadi ya watu katika pwani ya mashariki ya bara na kisiwa cha Bukini iliongezeka sana kwa ajili ya ujio wa makundi makubwa ya wahamiaji kutoka Uarabuni, Bara Hindi, Asia Maghribi na Indonesia<sup>12</sup>.

#### **Tofauti za kijamii**

Mehapuko wa tofauti za kijamii ulitokana na mgawanyo wa hali ya juu wa ufanyaji kazi. Sifa muhimu katika jambo hili ilikuwa ni kuibuka kwa tabaka la wafanyabiashara wa kati weledi katika Maghrib na Sudan, ambao walifanya biashara katika nchi mbalimbali. Wafanyabiashara hawa waliweza kuvuka mipaka ya asili zao (baadhi yao walikuwa Waberiberi, Waarabu, Wayahudi na weusi) na kuunda tabaka moja halisi lililotambua na kuzingatia maslahi yake.

Kuhusu koo za watawala wa kijeshi ambazo zilikuwa na mamlaka ya kisiasa, biashara ya kigeni iliawazeshwa kujipatia madaraka zaidi (zana za vita na farasi, kwa upande wa nchi za Sudan, na dhahabu, kwa upande wa miliki za Kiislamu), ambayo yalielekea kuimarisha mamlaka katika kuwatawala raia wa kawaida. Matokeo ya jumla ya maendeleo ya biashara

11 Taz. Sura 6 ya juzuu hili

12 Taz. Sura 21 hadi 25 ya juzuu hili.

yalikuwa ni kusababisha kuvunjika kwa muundo wa kijamii uliojengeka kwa misingi ya udugu na kuleta utaratibu mpya wa kijamii uliokitwa kwenye misingi ya umilikaji wa njia za uchumi (ardhi katika nchi za Maghrib) na biashara. Tafsiri ya hivi karibuni ya hekaya ya Sundiata, mtawala mashuhuri wa Kimandingo aliyeishi katika karne ya kumi na tatu inadokeza kuwa safari za kuteka watumwa za wana wa kifalme wa Malinke, wakishirikiana na wafanyabiashara wa Kisonike, zilikuwa chanzo cha kuanzishwa kwa miliki ya Mali.

Walakini biashara siyo iliyokuwa sababu ya kushawishi uanzishaji wa madola hayo. Biashara iliharakisha tu mipango ya uundaji kwa kufuatia mivuvumko iliyokuwemo tayari ndani ya jamii hizi, ambayo ilikuwa imefikia upeo wa kupevuka ambao ilizivezesha kukabiliana vizuri na athari za kigeni kutoka nje ya nchi zao. Na hasa uzalishaji wa mazao ya ziada kutokana na uzalishaji ulioboreshwa ndio uliokuwa msingi wa kufanya biashara na jamii za kigeni. Ndiyo kusema kwamba mambo yaliyotokea wakati huu katika jamii yalikuwa matokeo ya mabadiliko ya uzalishaji na usambazaji wa bidhaa. Kupanuka kwa Uislamu kulitokana na mwingiliano kati ya mageuzi ya kiuchumi na mabadiliko ya kijamii yaliyotatanisha takriban nchi zote za Kiafrika, hasa nchi za Maghrib, Misri, Sahara, Afrika Mashariki na Sudan ya kati na ya Maghribi. Penginepo, Uislamu na kanuni zake za kiulimwengu ulitoa mafundisho yanayofafanua migongano ya kimaslahi kati ya jamii mbali mbali. Ndiyo maana chama cha Kikharji, maasi ya Abu Yazid, na vyama vingine vya ukombozi vilivyoleta ghasia katika nchi za Maghrib wakati huo, viliwakilisha, katika mtazamo wa kijamii, kukataliwa kwa utaratibu uliokuwapo, na zaidi ya hayo, azma ya kukomesha dhuluma katika jamii.

### Mapambano ya kitabaka

Kuendelea kwa mapambano ya kitabaka, na migongano ya kijamii kwa ujumla, vilitokea katika uzito tofauti kulingana na hali halisi ilivyokuwa katika eneo lililohusika, na kiwango cha kutawaliwa na kudhulumwa kilichokuwepo katika kila kundi la jamii. Kuhusu Maghrib, C.A. Julien, A. Laroui na, kwa kiasi fulani, G. Marçais wamechanganua maasi na vyama vya upinzani vya kipindi hiki kama matukio katika mapambano ya kijamii.

Katika nchi za Wasudan, hali hii si wazi sana. Walakini kuanguka kwa utawala wa Ghana/Wagadu mwishoni mwa karne ya kumi na moja ndilo lililokuwa tukio la mwisho katika hali nzima ya kuharibika kwa mambo ya ndani. Kulingana na nadhariatete yetu, uozo huu ulisababishwa na vita kati ya makundi mawili katika tabaka la kifalme la Ghana: moja la Kiislamu na lililoungana na wafanyabiashara, na lingine la wafuasi wa dini ya kienejeji na lililoungana na jamii za vijijini. Kisha mifarakano ya ndani ikazidishwa na migongano mikali baina ya umma kwa ujumla na tabaka tawala. Vyovyote tutakavyoichukulia nadhariatete hii, lililo wazi ni kwamba biashara kati ya mataifa ya Kiafrika ilileta athari za ukinzani katika makundi ya kijamii ya bara hili. Katika sehemu nyingine biashara hii ilileta muungano wa kisiasa (dola za Kimoravi na Kitimi na baadaye Mali na Songhay); katika sehemu nyingine, ilileta kuanguka kwa miundo ya dola iliyorithiwa kutoka vipindi vya nyuma (dola ya Ghana na dola ya Kiukristo ya Ethiopia).

# 28

## *Afrika kuanzia karne ya saba hadi karne ya kumi na moja: karne tano za ujenzi*

### *Utangulizi*

Kumekuwa na majaribio mengi ya kutafuta mielekeo ya jumla ya kubainishia mageuko ya bara hili katika kipindi baina ya karne ya saba na karne ya kumi na moja. Lakini hakuna hata moja kati ya majaribio hayo ambalo huweza kutiwa maanani; iwe tunalifikiria bara lote zima au sehemu tu. Si katika kuenca kwa Uislamu, ambako kunajitokeza sana Kaskazini mwa ikweta, wala katika kile ambacho kimeitwa Enzi ya Pili ya Chuma (ambayo tutarejea kwayo baadaye) ambamo tunaweza kupata vielelezo vya rejea visivyo na ubishi.

Kutokana na uchunguzi huu mdogo hatuna budi kuwa na hadhari: utafiti unazidi kusonga mbele kwa kasi na kila moja ya magunduzi yake hutufanya tuyasaili mambo yote ambayo hapo nyuma tumekuwa tukiyachukulia kuwa yakini. Hii inaonyesha jinsi ambavyo mahitimisho ambayo hii leo yaweza kufanywa kutokana na uchanganuzi wa karne hizi tano yalivyo ya muda tu na yasivyo ya hakika. Lakini bado ni muhimu kwa watafiti na wasomaji kuyasoma na kuyatafakari kwa sababu katika karne hizi tano, na kwa mara ya kwanza kwa wazi kabisa, imewezekana kufuatilia mfululizo wa maendeleo ya aina hiyo hiyo katika bara lote.

Karne hizi zilishuhudia kukua kwa aina mbalimbali za uchumi, miundo ya kijamii-kisiasa na uwakilishi wa watu; mambo ambayo ndiyo yaliyokuwa chanzo cha miguro ya kihistoria iliyotokezea baadaye. Katika karne hizi maendeleo ya polepole yalianza kutokea, jambo ambalo linatonyesha kwa nini baadaye kulitokea mafanikio mengi.

Sifa ya kwanza kubwa na ya jumla ni kuanzishwa kwa maeneo ya makazi ambako uzalishaji wa bidhaa za kilimo ulikuwa ndiyo kazi muhimu ya watu. Maendeleo ya teknolojia mbalimhali ni sifa ya pili kubwa. Maendeleo haya yalilusisha matumizi bora ya maliasili, mgawanyo wa kazi na kuenea kwa ubadilishanaji wa bidhaa. Kwa mwanahistoria uchangamani wa tawala mbalimbali za kisiasa ndilo jambo lilitokezalo katika kipindi liki; wakati huo huo kulianza kutokea uwakilishi wa pamoja, dini, itikadi na njia mbalimbali za kujieleza na kujibainisha kitamaduni ili kuhakikisha kuwa vitu hivyo vinaendelea kuwepo na kurithishwa kwa vizazi vya baadaye.

### *Upangaji wa maeneo ya makazi*

Ukaaji wa watu katika maeneo ulitokana na uhusiano mpya kati ya watu na mazingira ambao hulazimika kutokea kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa ya nchi, kuongezeka kwa idadi

ya watu na uchangamani wa kijamii. Katika Afrika, kama ilivyo katika mabara mengine, kuongezeka kwa idadi ya watu ambako kunawiana na kuongezeka kwa idadi ya wafanyakazi waliitajikao katika uzalishaji wa mazao ya chakula, ndiko kunafanya mkakati mkubwa wa kudumisha uhai. Utafiti wa mabadiliko haya katika kipindi hiki ndio mwanzo tu umeanza; hata hivyo, kule ambako utafiti wa kiakiolojia umefanyika, imedhihirika umuhimu wa utafutaji wa chakula na faida ya kuwepo kwa aina mbalimbali za vyakula.

### *Afrika ya Kati na ya Kusini*

Kwa hakika usambaaaji wa Wabantu ulifikia mwisho kwenye karne ya sita hivi<sup>1</sup>. Kuanzia wakati huo na kuendelea sehemu kubwa ya bara hili, kule ambako tabia ya nchi iliruhusu kilimo, ikakaliwa na wakulima. Katika misitu ya Afrika ya Kati mbinu ya kulima kwa kufyeka mashamba kila mwaka ikaanzishwa. Kukalimwa viazi vikuu, migomba na mboga. Lakini kilimo cha mazao ya chakula kilikua kipengele kimojawapo tu kwani utegaji wanyama na uchumaji matunda zilibakia njia muhimu sana za kupatia chakula. Kusini mwa msitu, katika maeneo ya mbuga yaliyojaa mbung'o, mfumo wa kilimo ulikuwa wa kulima mashamba mawili kwa mwaka; shamba moja lililofyekwa msituni na jingine katika mbuga. Nafaka ndiyo iliyochukua nafasi kubwa zaidi, na shughuli zikakamilishwa zaidi na uwindaji kuliko utegaji. Katika sehemu za mashariki na kusini-mashariki ya Afrika, uzalishaji wa chakula ulikitwa kwenye ufugaji, na kilimo kikawa ni eha mtama na ulezi. Ufugaji ulifanyika kwa wingi katika maeneo yenye ukame zaidi: Botswana, Uganda Kaskazini na Sudan, kusini na maeneo ya Kenya yanayopakana nayo. Hadi kufikia mwaka 600 maisha kamili ya ufugaji wa ng'ombe yalikuwa yakipatikana tu katika Pembe ya Afrika, katika Sahel, pambazoni mwa Sahara na labda katika eneo lianzialo kusini mwa Sudani, mashariki ya White Nili hadi kufikia katikati ya Tanzania. Lakini, kuanzia karne ya tisa aina mpya ya uchumi ya kusini-mashariki ya Afrika ilianza kujitokeza Botswana na kuelekea zaidi katika ufugaji wa ng'ombe. Ilichukua karne kadhaa kufikia mfumo kamili wa ufugaji ambao baadaye uliwawezesha Wakhoi-Khoi kuyachukua maeneo yote yaliyokuwa mazuri kwa ufugaji katika Namibia na Cape Province.

### *Afrika ya Mashariki*

Katika Afrika ya Mashariki, upanuzi wa ufugaji huenda ulitokana na kuingizwa kwa aina mpya ya ng'ombe, yaani Zebu (mwenye nundu) na Sanga. Aina hizi zilikuwako katika Nubia ya Kiukristo zamani lakini katika kanda ya White Nili na Pembe ya Afrika zimpatikana tu baada ya mwaka 1200. Ng'ombe aina ya Sanga, ambayo imapatikana kuanzia sehemu hizi hadi kufikia Afrika Kusini, ambako ilizaa aina nyingine, ni ya zamani zaidi kuliko Zebu. Inawezekana aina hiyo ilianza kuenea katika kipindi tukishughulikiacho sasa na yawezekana pia kwamba kwa kiasi fulani ilihusika na kusambaa kwa Wakhoi-Khoi. Hata hivyo swala hili linahitaji utafiti zaidi. Aina hii ya ng'ombe pengine ilikuwa na nafasi fulani katika kuimukia kwa wafugaji katika kanda ya Maziwa Makuu kulikotokea katika kipindi tukichunguzacho na pengine ilisababisha matumizi zaidi ya ardhi kame katika Afrika Mashariki. Afrika

1 Taz. Sura 6 ya juzuu hili.

kusini-Maghribi, ambayo ni kame mno kwa kilimo, haikupata mabadiliko makubwa ingawa ufugaji wa wanyama wa jamii ya kandoo ulikuwepo mwanzoni mwa enzi ya Ukristo.

### *Afrika Maghribi*

Afrika Maghribi ilipitia mageuko ambayo yanaweza kulinganishwa na kutofautishwa na yale ya sehemu nyingine. Yawezekana kuongezeka kwa watu tayari kulikuwa kumeanza kuandamana na uharibifu wa msitu. Dalili kidogo zilizoko Sierra Leone na Liberia zinatufanya tufikirie kwamba wakulima ndio waliokuwa watu wa kwanza kutamakani kanda huu; katika misitu ya Niger kufika kwa wakulima katika maeneo hayo kuna ushahidi halisi wa kimaandishi.

Katika sehemu kavu zaidi za mbuga na katika kanda ya Sahel hali ya hewa ya nchi yalikuwa ikibadilikabadilika kwa muda wa karne kadhaa. Matokeo yake yakawa kuhamahama kwa watu taratibu toka Kaskazini-Maghribi au kusini katika harakati za kuweka maskani na kulima mimea. Watu hao walifuata mvua na milima iliyotakikana kwa ajili ya kilimo halisi, katika maeneo ambayo hayakuwa na akiba ya maji yaliyotokana na mabonde ya mito. Uchangamano wa aina za makazi katika ghuba ya Senegal na Niger polepole unaanza kudhihiri. Maeneo haya mawili ya nchi kavu, ambayo yamezungukwa na mito, yalikuwisha kuwa maeneo yenye idadi kubwa ya watu, na uchangamano wa kiuchumi wa hali ya juu wa kabla ya enzi ya Ukristo.

Sahel ni eneo la ufugaji. Chakula kikuu ni maziwa pamoja na majani na pia uwindaji wa wanyama na ndege. Katika sehemu hizi kilimo kinawezekana tu katika maeneo ambayo kina cha usawa wa maji kinaruhusu uchoaji wa maji na umwagiliaji. Uvuvi ambao ulikuwepo katika enzi za Kineolithi ulikwishatoweka sehemu zote; kutokana na hali kama hiyo chakula kikuu (samaki) cha wakazi wa huko kilichokuwa kikipatikana kwa wingi kikawa hakipatikani tena. Pengine hamu ya 'kutaka kuonja samaki' ndiyo uliyosababisha watu katika eneo la Sahel kimunua ng'onda au samaki wa kukaushwa kwa moshi kutoka kusini. Uagizaji vitu kutoka nje likawa jambo la lazima pale mahitaji fulani ya kiuchumi yalipowalazimisha watu waishi katika mazingira ambamo mahitaji hayo hayakupatikana.

Mabonde yalikuwa maeneo ya miundo changamani, mahali ambapo pengine watu waligombea ardhi; kadri idadi ya wakazi ilivyoongezeka kukatokea mgawanyo wa kazi na uanzishaji wa mfumo wa mamlaka. Katika karne ya saba wavuvi walikuwa wakikausha samaki kwa jua, au pengine kwa kutumia moshi, na kuwasafirisha nje. Mito na maziwa vilikuwa na aina nyingine nyingi za vyakula kama vile kasa, chaza, kamba, konokono; nyama ya kiboko na mamba.

Kilometa chache tu kutoka kwenye maeneo mazuri ya mabonde ya mito zinajitokeza aina mbalimbali makini za kilimo; tunaona utumiaji maji kwa uangalifu na matumizi bora ya mimea yote iliyo ya muhimu katika maisha. Kwa kiasi kikubwa yaelekea kwamba kati ya karne ya saba na karne ya tisa teknolojia nyingi bora za matumizi ya udongo zilianza kuchukua miundo na taratibu maalumu.

Maeneo yaliyo Kaskazini ya mito polepole yakageuzwa kuwa maeneo ya malisho ya mifugo. Kuna uwezekano mkubwa kwamba kusambaa kwa Wafulani katika maeneo haya kutoka sehemu ambayo hii leo yajulikana kama Senegal kulianza katika karne ya kumi na moja au pengine mapema zaidi; yawezekana pia kuwa kusambaa kwao huku kulikusiana na kupatikana kwa ng'ombe wa aina ya Zebu.

## *Sahara*

Katika vikwi viwili au vitatu vilivyopita, Sahara na kingo zake za Kaskazini na kusini polepole zilikwishaanza kuhamwa na wakazi wake kadri mazingira ya huko ya asili yalivyozidi kuishiwa uwezo wa kuwapatia chakula cha kutosha. Kuletwa kwa ngamia katika maeneo haya kuanzia karne ya tatu kulileta mapinduzi katika usafirishaji wa chakula na katika usafiri kwa ujumla.

Oasisi zikawa vituo vya misafara ya usafirishaji uliotumia wanyama ambayo ilizitumia njia zote zilizokuwa na visima vingi. Matumizi ya ngamia yaliwawezesha watu kusafirisha mizigo mizito katika umbali mkubwa sana, jambo ambalo halina budi kutiliwa maanani tunapozungumzia kuinukia kwa mahusiano ya kuvuka Sahara ambayo yalipata vuvumko kubwa mnamo mwisho wa enzi ya Wabizenti.

Watu wa Sahara, ambao wengi wao walizungumza Kiberiberi, wakalitamalaki jangwa na wakawa kwa namna fulani wamechukua nafasi mpya na kubwa zaidi katika sehemu hiyo. Hii ikatokea wakati mmoja na kuongezeka kwa mahitaji ya dhahabu kwa ajili ya mataifa ya Kiislamu yaliyokuwa Kaskazini; katika karne ya kumi na ya kumi na moja hali hii ikaipa Sahara umuhimu wa kihistoria ambao ulikuwa haujawahi kupatikana kwa muda mrefu.

## *Afrika ya Kaskazini*

Uhusiano baina ya wakazi wa miji na sehemu za mashambani, pamoja na migomo na makinzani yao ndiyo ijulikanayo zaidi kuliko mfumo wa jamii hizi zalishi. Kwa mfano, sana sana tunaweza kugusia tu kwamba Wabarghawata wa Moroko walikuwa na uchumi uliotokana na ngano ambayo waliweza kuisafirisha nje; kwamba Sus ilikuwa ikizalisha miwa katika karne ya tisa; na kwamba Ifrikiya ilikuwa kanda iliyozalisha mazao ambayo yalikusudiwa kusafirishwa nje kwa njia ya bahari.

Katika bonde la Nili ambako kulikwishakuwa na mfumo maalumu wa maisha kwa muda mrefu, hakuna lolote kubwa la kuweza kutaja. Huko Misri tatizo la chakula halikuwa tena la uzalishaji tu bali lilikuwa la utumiaji kwa wingi wa mazao katika miji: kulisha idadi kubwa ya watu wa mji kama Kairo, ambao ulikuwa na laki kadhaa za wakazi katika karne ya kumi na moja, kulileta matatizo makubwa zaidi kuliko yale yaliyokuwa katika jamii zote za Afrika ya watu weusi zilizokuwa na wazalishaji na walaji. Lilikuwa ni swala la kitaifa lililohitajia kuanzishwa kwa sera ya uzalishaji mali, fedha na uingizaji bidhaa nchini; kwa sababu hii swala hili linakuwa nje ya mchanganuotete huu tuufanyao kwa sehemu nyingine za Afrika.

Nubia Kaskazini ilishiriki katika uchumi wa Misri, ingawa ilitamalakiwa na kudhibitiwa kikamilifu na mfalme wa Kiukristo katika Dunkula, lakini kusini mwa poromoko la pili kulikuwa na ulimwengu mpya wa uchumi. Mbele ya maporomoko ya mwisho katika ufalme wa Alwa kulikuwa na ukanda mwingine ambako hakukuwa na mitende au zabibu bali kulikuwa na mtama mweupe ambao unafanana na mchele na ambao wakazi wa huko hutumia kutengenezea mikate na pombe. Nyama pia ilikuwako kwa wingi kutokana na makundi makubwa sana ya ng'ombe.

## *Miguro ya jamii za Kiafrika*

Kuanzia karne ya saba hadi karne ya kumi na moja miguro ya jamii za Kiafrika kwa kawaida ilielekezwa katika kujiweka sawa na mazingira na kuboresha uzalishaji chakula ili kukidhi

mahitaji yaliyokuwa yameongezeka. Ongezeko la kawaida la idadi ya watu, japokuwa lilikuwa la polepole na ingawa hatujui kiwango chake, liliandamana na kudhoofika zaidi kwa uhusiano wa wakazi na mazingira katika maeneo mengi. Mambo haya mawili yalisababisha mijongeo ya polepole ya watu, kama vile mguro kinyume kutoka Transvaal kuelekea Zimbabwe; mguro ambao yaelekea ulianza katika karne ya nane au ya tisa. Mguro huu waelekea kuhusiana na ongezeko kubwa la idadi ya watu. Hali ni hiyo hiyo katika delta ya ndani ya Niger ambako miinuko juu ya tambarare za mafuriko ilitamkaniwa katika karne ya kumi na moja; maeneo ambayo huko nyuma yalikuwa hayajawahi kukaliwa na watu. Katika eneo hili hata mabadiliko kidogo tu ya hali ya hewa ya nehi pengine yaliweza kusababisha ongezeko kubwa la watu au, kinyume chake, kuleta ubora zaidi wa maisha japo ya muda mfupi.

Hapana shaka kwamba mbinu mpya za uzalishaji mali zilileta mabadiliko ya kijamii. Tunaweza kusema kwamba maendeleo hasa ya kuviunganisha vikundi mbalimbali kuwa jamii zenye mshikamano yalianza katika kipindi hiki. Kwa hakika hiki kilikuwa kipindi cha watu kuunganika na kuwa wamoja, kipindi cha kuchanganyika kwa vikundi vya zamani na kuwa vikundi vikubwa zaidi, na kipindi cha kuingiliana kwa lugha zenye kukaribiana.

Katika msitu wa Afrika ya Kati wawindaji walibakia na maumbo yao ya kimbilikimo lakini waliishi maisha ya kuelewana na wakulima, wakatimia lugha zao na 'wakamezwa' kijamii na kiutamaduni na kuwa 'chotara' katika makundi makubwa makubwa. Katika Zimbabwe na Zambia kufikia karne ya kumi na moja wenyeji wa asili 'walikwishamezwa' kabisa. 'Umezwaji' huu unakuwa na kasi ndogo zaidi mashariki mwa Angola na maeneo ya Zambia yahyo jirani: wawindaji-wakusanyaji polepole walirudi nyuma kadri ongezeko la watu lilivyozidi kuathiri idadi ya wanyamapori. Waliendelea kuishi kusini mwa Angola katika maeneo ambako wakulima wa Kibantu hawakuweza kupenya.

Katika Afrika Maghribi tayari jamii changamani zilikwishatamkani katika kanda za misitu na misitu midogo. Mpangilio wake wa nafasi ukakusanya pamoja wawindaji, wakusanyaji na wakulima katika jamii ambazo zilikuwa changamani zaidi. Katika maeneo ya mito uzalishaji wa mazao ulileta ziada ambazo zilifanya biashara baina ya sehemu hizo na sehemu ambazo hazikuwa mbali sana ianze; halikadhalika mgawanyo wa kazi kati ya wazalishaji mahsusi wa mazao ukajitokeza zaidi. Muundo wa utawala sasa ukawa changamani zaidi.

Katika vikundi kama hivi vya wakazi ambao walikuwa wakishi katika mazingira bora zaidi mpaka kuongezeka kwa watu kulipowafanya wagawike katika makundi madogomadogo, jamii za Kiafrika ziligundua teknolojia mpya katika uzalishaji wa chakula na shughuli nyingine. Kutafuta hali bora za maisha likawa lengo dhahiri: akiolojia ya viumbe waliokuwa wakishi katika tope haijatupa habari za kutosheleza kama unavyotegemea. Ingawa baadhi ya waandishi hufikiri kwamba chokaa ilitumika tu Nyani baada ya kuletwa huko na Waislamu, hapana shaka udongo wa kawaida ulitumika kukandikia nyumba za miti kuanzia zama za karne ya sita (ling. kwa mfano nyumba za udongo huko Jenne- Jeno kabla ya mahusiano yao na watu wa Kaskazini). Ingawa nyumba zilizojengwa kwa matofahi huko Tegdausti na Kumbi Saleh zilitokea wakati mmoja na inahusiano yao na nchi za Kiislamu, wanaakiolojia wana hakika kwamba ujenzi huo haukutimia teknolojia ngeni.

### *Mbinu za ufundi na kwa nini hazina budi kuchunguzwa*

Mojawapo ya mahitaji muhimu sana katika historia ya Afrika na akiolojia ni uchunguzi makini



na wa kina wa mabadiliko ya shughuli za ufundi na mazingira yaliyoyachochea. Ufinyanzi, metali na ufumaji vyaweza kuchukuliwa kama mfano wa uchunguzi wa mambo haya ambao unaweza kuchangia katika historia ya bara hili, ingawa uchunguzi wake haujakamilika.


## Ufinyanzi

Imekuwa ni mazoea, hasa katika mashariki na kusini mwa Afrika, kuzipa majina aina za ufinyanzi kwa kufuata eneo kuu ambapo aina hizo ziligunduliwa; zikikadiriwa umri wa wachimbaji zikiwa katika hali ya kuridhisha zinaweza kutumiwa kama viashirio vya kihistorolojia. Kazi za ufinyanzi, ziwe zimetazamwa kwa ubora au wingi wake, zimekuwa ni kiashirio cha idadi ya watu waliokuwepo na kiwango cha hali ya uchumi wao (biashara na eneo ambamo vitu hivyo vilienea), kazi hizo pia zimetumiwa kama kiashirio cha utamaduni. Mlolongo wa ugunduzi uliofanywa na akiolojia katika miaka ya hivi karibuni ni kielelezo cha mambo ambayo akiolojia ya ufinyanzi wa Kiafrika inaweza kutupatia: vijisanamu vya binadamu vilivyotengenezwa kwa udongo wa mfinyanzi vilivyopatikana huko Ife na Owo, vikiwa vinafuatia vile vya Nok; vile vijisanamu vya aina hiyo hiyo vilivyopatikana huko Niger ya juu; vielelezo ambavyo vinaanza kujitokeza katika Niger; mitindo adimu lakini yenye kuvutia ambayo imepatikana katika machimbo ya Mauritania; mtindo wa kusakafia vyumba na nyufa kwa kutumia vipande vya vyombo vya mfinyanzi (vyungu, n.k.) - vyote hivi ni katika jumla ya vipengele vya kushangaza vya magunduzi yanayozidi kupatikana.


Ufinyanzi wa Kopye ya Leopard kipengere kimojawapo katika uundaji wa jamii changamani inayoelekea katika ujengaji wa taifa kwenye miaka ya 900<sup>2</sup>. Kinyume na hali hii, kutokea kwa ufinyanzi wa Kisali katika karne ya nane huko Sanga hakukuandamana na hali yoyote ya namna hiyo; ama kwa hakika yaelekea kwamba kutokea kwa ufinyanzi huo ni dalili ya kuinukia kwa aina mpya ya wakulima-wavuvi. Katika karne hiyo hiyo au iliyofuata aina mpya ya ufinyanzi katika Rwanda yaweza kuwa dalili ya badiliko dogo tu ingawa ndio ulikuwa mwanzo wa kuacha kumakinikia matanuri ya kuyeyushia vyuma. Lakini hii pia yaweza kuwa ishara ya mageuzi makubwa yaliyotokana na kutokea kwa wafugaji maalumu katika jamii.

## Metali

Dhahabu ya Afrika kwa muda mrefu imekuwa ikijengewa visaasili na uchawi fulani wa kihistoria. Leo hii walau tunajua habari kidogo juu yake na sasa tunaanza kuondokana na mawazo ya kufikirika na kuanza kutoa tathmini zenye ushahidi. Nchi ambayo leo hii inajulikana kama Zimbabwe ilisifika zaidi katika kipindi hiki; eneo la mwisho lililokuwa likizalisha bidhaa hii baada ya Unubi na Afrika Maghribi. Katika kanda hii iliyotajwa mwisho, ni dhahiri kwamba dhahabu iliyopatikana katika tope za mito ilianza kutumiwa kabla ya mwaka 600 ingawa pengine ilikuwa kwa matumizi ya nyumbani tu. Kiasi chake kilikuwa kidogo tu na haiyamkiniki kuwa ilipatikana kwa uchimbaji migodi. Baada ya kuanzishwa kwa mataifa ya Kiislamu mahitaji yakaongezeka; na katika kipindi chote tukichunguzacho sasa usafirishaji nje wa dhahabu uliongezeka sana. Ni vigumu sana kuaema kwa yakini kwamba kabla ya karne ya kumi ilikuwepo teknolojia maalumu ya uchimbaji madini hata kwa upande wa Nubia. Yaelekea kwamba njia ya kuchuja dhahabu kutoka katika tope, ambayo ilikuwa imeenea sana, kwa kipindi kirefu ilitosheleza haja. Leo hii imedhihirika kwamba dhahabu



**28.1** *Sanamu zilizotolewa kwenye eneo la Jamhuri ya Niger ya juu sasa katika karne ya sita na ya kumi. Mjano wa uvumbuzi uliofanvika 1983 (B. Gado, Mkurugenzi wa Taasisi ya Uchunguzi ya Sayansi za Jamii, Namexy)*



28.2 Baraza ya vitae vya vyungu : kona ya uwanya ilivochimbuliwa huko Ita Yemoo, Ije. Vipimo vipo kwenye futu

kutoka kanda za misitu ya Afrika Maghribi kufikia mwaka wa c. 1100 tayari ilikwishaanza kusafikirishwa Kaskazini. Ushahidi wa kimaandishi unadhihirisha wazi kwamba tayari migodi ilikuwa ikichimbwa katika karne ya nne. Akiolojia pia imetoa ushahidi wa jambo hili katika Uwanda wa Juu wa Zimbabwe, lakini haliwi jambo la kushangaza kufikiria kwamba uchimbaji migodi tayari ulikwishaanza kufanyika katika karne ya kumi. Uyeyushaji metali ulikuwa katika maeneo ambako mbale za chuma zilitumika<sup>3</sup>; pengine ingekuwa ni kutozingatia mambo kama tungesema kwamba ufundi wa dhahabu haukuwepo katika maeneo ambako ilizalishwa. Yawezekana kwamba ufundi wa temsi, ambao ulikuwa umesambaa sana katika Andalusia na Afrika Kaskazini mapema kwenye karne ya kumi, ulifika kusini kutokea katika maeneo hayo. Mapambo ya temsi ya dhahabu yamewahi kupatikana Tegdausti na ufundi wa temsi ulitumika kwa vyombo vyenye michanganyiko ya shaba katika Igbo-Ukwu, huko Nigeria. Dhahabu ya Afrika kwa muda mrefu imekuwa ikijengewa visaasili na uchawi fulani wa kihistoria. Leo hii walau tunajua habari kidogo juu yake na sasa tunaanza kuondokana na mawazo ya kufikirika na kuanza kutoa tathmini zenye ushahidi. Nchi ambayo leo hii inajulikana kama Zimbabwe ilisifika zaidi katika kipindi hiki; eneo la mwisho lililokuwa likizalisha bidhaa baada ya Unubi na Afrika Magharibi. Katika kanda hii iliyotajwa mwisho ni dhahiri kwamba dhahabu iliyopatikana katika tope za mito ilianza kutumiwa kabla ya mwaka 600 ingawa pengine ilikuwa kwa matumizi ya nyumbani tu. Kiasi chake kilikuwa kidogo tu na haiyamkiniki kuwa ilipatikana kwa uchimbaji migodi. Baada ya kuanzishwa kwa mataifa ya Kiislamu mahitaji yakaongezeka; na katika kipindi chote tukichunguzacho sasa usafirishaji nje wa dhahabu uliongezeka sana. Ni vigumu sana kusema kwa yakini kwamba kabla ya karne ya kumi ilikuwepo teknolojia maalumu ya uchimbaji madini hata kwa upande wa Nubia. Yaelekea kwamba njia ya kuchuja dhahabu kutoka katika tope, ambayo ilikuwa imeenea sana, kwa kipindi kirefu ilitosheleza haja. Leo hii imedhihirika kwamba dhahabu kutoka kanda za misitu ya Afrika Magharibi kufikia mwaka wa c. 1100 tayari ilikwishaanza kusafikirishwa kaskazini. Ushahidi wa kimaandishi unadhihirisha wazi kwamba tayari migodi ilikuwa ikichimbwa katika karne ya nne. Akiolojia pia imetoa ushahidi wa jambo hili katika Uwanda wa Juu wa Zimbabwe, lakini haliwi jambo la kushangaza kufikiria kwamba uchimbaji migodi tayari ulikwishaanza kufanyika katika karne ya kumi. Uyeyushaji metali ulikuwa katika maeneo ambako mbale za chuma zilitumika; pengine ingekuwa ni kutozingatia mambo kama tungesema kwamba ufundi wa dhahabu halikuwepo katika maeneo ambako ilizalishwa. Yawezekana kwamba ufundi wa temsi, ambao ulikuwa umesambaa sana katika Andalusia na Afrika Kaskazini mapema kwenye karne ya kumi, ulifika kusini kutokea katika maeneo hayo. Mapambo ya temsi ya dhahabu yamewahi kupatikana Tegdaoust na ufundi wa temsi ulitumika kwa vyombo vyenye michanganyiko ya shaba katika Igbo-Ukwu, huko Nigeria. Dhahabu ya Afrika kwa muda mrefu imekuwa ikijengewa visaasili na uchawi fulani wa kihistoria. Leo hii walau tunajua habari kidogo juu yake na sasa tunaanza kuondokana na mawazo ya kufikirika na kusnza kutoa tathmini zenye ushahidi. Nchi ambayo leo hii inajulikana kama Zimbabwe ilisifika zaidi katika kipindi hiki; eneo la mwisho lililokuwa likizalisha bidhaa baada ya Unubi na Afrika Magharibi. Katika kanda hii iliyotajwa mwisho ni dhahiri kwamba dhahabu iliyopatikana katika tope za mito ilianza kutumiwa kabla ya mwaka 600 ingawa pengine ilikuwa kwa matumizi ya nyumbani tu. Kiasi chake kilikuwa kidogo tu na haiyamkiniki kuwa ilipatikana kwa uchimbaji migodi. Baada ya kuanzishwa kwa mataifa ya Kiislamu mahitaji

3 Taz. Sura 14 ya juzuu hili.

yakaongezeka; na katika kipindi chote tukichunguzacho sasa usafirishaji nje wa dhahabu uliongezeka sana. Ni vigumu sana kusema kwa yakini kwamba kabla ya karne ya kumi ilikuwepo teknolojia maalumu ya uchimbaji madini hata kwa upande wa Nubia. Yaelekea kwamba njia ya kuchuja dhahabu kutoka katika tope, ambayo ilikuwa imeenea sana, kwa kipindi kirefu ilitosheleza haja. Leo hii imedhihirika kwamba dhahabu kutoka kanda za misitu ya Afrika Magharibi kufikia mwaka wa c. 1100 tayari ilikwishaanza kusafikirishwa kaskazini. Ushahidi wa kimaandishi unadhihirisha wazi kwamba tayari migodi ilikuwa ikichimbwa katika karne ya nne. Akiolojia pia imetoa ushahidi wa jambo hili katika Uwanda wa Juu wa Zimbabwe, lakini haliwi jambo la kushangaza kufikiria kwamba uchimbaji migodi tayari ulikwishaanza kufanyika katika karne ya kumi. Uyeyushaji metali ulikuwa katika maeneo ambako mbale za chuma zilitumika; pengine ingekuwa ni kutozingatia mambo kama tungesema kwamba ufundi wa dhahabu haukuwepo katika maeneo ambako ilizalishwa. Yawezekana kwamba ufundi wa temsi, ambao ulikuwa umesambaa sana katika Andalusia na Afrika Kaskazini mapema kwenye karne ya kumi, ulifika kusini kutokea katika maeneo hayo. Mapambo ya temsi ya dhahabu yamewahi kupatikana Tegdaoust na ufundi wa temsi ulitumika kwa vyombo vyenye michanganyiko ya shaba katika Igbo-Ukwu, huko Nigeria. Dhahabu ya Afrika kwa muda mrefu imekuwa ikijengewa visaasili na uchawi fulani wa kinistoria. Leo hii walau tunajua habari kidogo juu yake na sasa tunaanza kuondokana na mawazo ya kufikirika na kuanza kutoa tathmini zenye ushahidi. Nchi ambayo leo hii inajulikana kama Zimbabwe ilisifika zaidi katika kipindi hiki; eneo la mwisho lililokuwa likizalisha bidhaa baada ya Unubi na Afrika Magharibi. Katika kanda hii iliyotajwa mwisho ni dhahiri kwamba dhahabu iliyopatikana katika tope za mito ilianza kutumiwa kabla ya mwaka 600 ingawa pengine ilikuwa kwa matumizi ya nyumbani tu. Kiasi chake kilikuwa kidogo tu na haiyamkiniki kuwa ilipatikana kwa uchimbaji migodi. Baada ya kuanzishwa kwa mataifa ya Kiislamu mahitaji yakaongezeka; na katika kipindi chote tukichunguzacho sasa usafirishaji nje wa dhahabu uliongezeka sana. Ni vigumu sana kusema kwa yakini kwamba kabla ya karne ya kumi ilikuwepo teknolojia maalumu ya uchimbaji madini hata kwa upande wa Nubia. Yaelekea kwamba njia ya kuchuja dhahabu kutoka katika tope, ambayo ilikuwa imeenea sana, kwa kipindi kirefu ilitosheleza haja. Leo hii imedhihirika kwamba dhahabu kutoka kanda za misitu ya Afrika Magharibi kufikia mwaka wa c. 1100 tayari ilikwishaanza kusafikirishwa kaskazini. Ushahidi wa kimaandishi unadhihirisha wazi kwamba tayari migodi ilikuwa ikichimbwa katika karne ya nne. Akiolojia pia imetoa ushahidi wa jambo hili katika uwanda wa Juu wa Zimbabwe, lakini haliwi jambo la kushangaza kufikiria kwamba uchimbaji migodi tayari ulikwishaanza kufanyika katika karne ya kumi. Uyeyushaji metali ulikuwa katika maeneo ambako mbale za chuma zilitumika; pengine ingekuwa ni kutozingatia mambo kama tungesema kwamba ufundi wa dhahabu haukuwepo katika maeneo ambako ilizalishwa. Yawezekana kwamba ufundi wa temsi, ambao ulikuwa umesambaa sana katika Andalusia na Afrika Kaskazini mapema kwenye karne ya kumi, ulifika kusini kutokea katika maeneo hayo. Mapambo ya temsi ya dhahabu yamewahi kupatikana Tegdaust na ufundi wa temsi ulitumika kwa vyombo vyenye michanganyiko ya shaba katika Igbo-Ukwu, huko Nigeria.

Kusini mwa Sahara shaba ilipendwa zaidi kuliko dhahabu na ikatumiwa kama mali ghafi ya vyombo vya anasa. Maeneo ambako mali ghafi ilizalishwa na metali ikayeyushwa yalikuwa mengi zaidi katika karne ya saba na katika sehemu nyingi mapema zaidi ya hapo kuliko ilivyofikiwa hapo nyuma. Mauritania, Niger (Aïr), ukanda wa shaba (Kongo na Zambia) na Transvaal (Phalaborwa) zilikuwa zinazalisha na kusafirisha nje shaba katika karne zote


zizungumziwazo katika juzuu hili. Hapana shaka kwamba biashara hii ya metali ilitoa shaba na aloi ya kupri Kaskazini kwenda kusini mwa Sahara. Hata hivyo picha tuliyonayo hii leo juu ya biashara hii ni changamani zaidi kuliko ilivyokuwa ikifahamika hapo nyuma; leo hii haikubaliki tena kwamba bidhaa na ufundi wa matumizi ya metali hizi vyote vilitoka Kaskazini. Huko Afrika ya Kati shaba ilitumika kama fedha halali kuanzia mwaka 900, na huko Transvaal mgodi wa Phalaborwa ulikuwa ukizalisha metali hii, na wala haukuwa mgodi huo tu.

Ufundi wa uchimbaji inaelekea ulikuwa ule tu wa uchimbaji wa mashimo na mapango; mifumo ya mapango yenye vina ilikuwa adimu katika kupata shaba na dhahabu. Ufundi wa kusuba shaba nyeusi ulikuwako Mauritania na Air miaka ya enzi ya Ukristo; na ulikuwako katika ukanda wa shaba katika karne ya tano na ya sita. Kalibu ya nta imewahi kupatikana katika machimbo ya Tegdausti (Mauritania); tarehe yake ni kuanzia karne ya nane na ya tisa. Michakato iliyotumika katika kazi za metali mbalimbali imegunduliwa huko Igbo-Ukwu, ambako ulimbo ujulikanao kama '*euphorbia latex*' ulichukua nafasi ya nta. Sasa imethibitika kuwa ufuaji metali ya shaba na aloi zake tayari ulikuwa ukifanywa kwa uhodari mkubwa katika Afrika ya tropiki mnamo karne za sita, saba na nane. Ufuaji metali na kukalibu kwa kutumia kiolezo cha udongo na nta vyote vilitumiwa kwa kutegemea aina ya metali: shaba zilizotokana na zebaki na risasi ziliwakilisha aina mbalimbali za metali kwa ajili ya utengenezaji wa vitu mbalimbali; hata kulehemu kulitumiwa pia katika metali zilizokuwepo.

Kuwepo kwa metalujia (ufuaji metali) ya shaba ya kiwango cha juu kabisa tangu zama za kale ni jambo ambalo hii leo halina budi kukubalika, kinyume na mawazo yaliyokuwepo hapo nyuma. Hali ilivyokuwa kwa upande wa metali hii haikutofautiana na chuma. Historia ya teknolojia ya metali hii bado haijulikani sana ingawa kumekuwa na mitaala mingi juu ya baadhi ya maeneo ya metalujia huko Afrika Maghribi na Mashariki na huko Phalaborwa. Yawezekana aina mbalimbali za chuma zilitengenezwa lakini hatujui ni kwa kiasi gani uzalishaji chuma ulidhibitwa, wala hatujui jinsi michakato mbalimbali, tangu hatua ya uchimbaji hadi mwisho wa kitu kamili ilivyotokea na kuendelea, kuanzia ujenzi wa matanuri. Ramani ya mgawanyo wa aina mbalimbali za matanuri na zana (mivuo, nyundo, mipondeo, fuawe, mawe ya kuchorea, n.k.) pamoja na fueli na njia za kuvitumia, yote haya yaonyesha kuwa kulikuwa na teknolojia ya hali ya juu katika zama hizo. Tunaona kwamba kulikuwa na chuma katika maeneo mbalimbali kuanzia karne ya saba na kuendelea, na kwamba madini haya yalitumiwa kama malighafi ya kutengeneza zana (mashoka, majembe ya kulimia, n.k.), silaha (sime, mikuki, vyembe vya mishare, ncha za chusa na visu), vyombo vingine mbalimbali (mikasi, sindano) na mapambo (vidani, bangili na pete). Kwa kiasi fulani data za kiethnografia zinatufanya tujiulize maswali kadhaa: Chuma kilikuwa na matumizi gani? Umuhimu wake hasa ulikuwa nini? Kilihusiana vipi na shaba na vitu vingine vya thamani au vito au bidhaa nyingine za kubadilishana eneo kwa eneo na kipindi kwa kipindi? Hapana shaka kwamba historia ya metalujia ya chuma na matumizi ya bidhaa zake kwa upande fulani itabadili vikubwa fasili zote zilizokuwepo hapo nyuma.


## Nguo

Huko Misri na Nubia kumekuwepo na ufumaji kwa muda wa vikwi kadhaa. Baada ya mwanzo wa enzi ya Ukristo, ufundi wa Kikhufu ulifikia kilele ambacho hakikuwahi kuvukwa baadaye. Lakini pamba kama malighafi kilikuwa kitu kilichokuja baadaye tu. Pengine mmea huu uliletwa nchim kutoka Meroe. Majadiliano yaliyopo yanahusu maendeleo ya ufumaji,



28.3 *Widant na shanga za kioo kutoka kwenye chumba zha kuzikia huko Igbo -Ukwu; shanga kutoka Igbo Richard.*

▼ *Shanga za kioo kutoka kwenye bohari ya mavazi rasmi Katika Igbo-Ukwu*



hasa kwa kutumia pamba, kusini mwa Sahara. Pamba ilikuwepo vijijini katika kuruba ya mto Senagal katika karne ya kumi na mbili; nguo zilizofumwa kwa miyaa zimewahi kupatikana huko Tellem na yakadiriwa kuwa ni za karne kati ya kumi na kumi na moja. Ni muhimu kutaja kwamba ufumaji wa pamba ulikuwa umeenea Ethiopia, na mapema kabisa kwenye miaka ya t. 900 ulikuwako huko kusini mwa Msumbiji na Mapungubwe. Katika karne ya tisa na kumi tayari pamba ilikuwa ikilimwa na kufumwa katika Afrika ya tropiki. Ufumaji huu ulihitajia vitu viwili muhimu sana; mashine za kufumia zenye kuzunguka ili kuruhusu mizunguko na mitandi. Mashine nyingi za kufumia zenye kuzunguka zilizogunduliwa na kutambuliwa bila shaka zilikuwepo kwa wingi katika karne za kumi na tatu na kumi na nne; katika karne za nyuma zilikuwa chache sana, kwa kadri tufahamavyo hii leo. Kwa upande wa mitandi, imedhihirika kwamba ile ya Msumbiji na ile ya Afrika Maghribi ni tofauti. Katika karne zilizofuatia ufumaji na uuzaji wa nguo vikawa vitu muhimu sana kiuchumi. Kwa hiyo ni muhimu kujua mianzo ya shughuli hii ambayo kusema kweli haikuleta tu bidhaa mpya za nguo lakini pia ilileta hali ya watu kujitofautisha kijamii pamoja na kuwepo kwa vitu vya kubadilishana na kuhodhi.

Katika Afrika kusini mwa Sahara siyo pamba tu iliyofumwa. Rafia (chane) za mivumo na mimea ya aina yake hutoa nyuzi ambazo zilifumwa. Kule ambako aina hii ya miti huota, huko Afrika Maghribi na Kati, nyuzi hufumwa kwenye mtandi mpana uliokaa wima au ulalo na utari mkubwa mmoja. Si ajabu kwamba mtandi huu ni wa zamani zaidi kuliko ule wa Afrika Magharibi, na inawezekana pia kuwa ni wa miaka ya karibuni zaidi. Nguo za rafia zilikuwa na umuhimu mkubwa sana katika Afrika ya Kati ambako ufundi wa kuzipamba ulikuwa wa hali ya juu sana kabla hata ya karne ya kumi na sita, na ambako miraba ya rafia ilitumika kama pesa. Katika kanda ya msitu utengenezaji wa nguo za magome ya miti ambayo yalipondwapondwa ulikuwa wa hali ya juu sana. Katika mbuga za savana ngozi ndizo zilizotumika kama nguo. Maelezo haya yote yanapingana na wazo kwamba ufumaji wa nguo za pamba ulisambaa kutokana na athari ya Uislamu iliyotokana na haja ya kupiga vita kwenda uchi. Mtazamo huu wa fikra unashindwa kuleta mslawasha mkubwa tunapozingatia ukweli kwamba aina nyingine za mavazi zilikuwepo pia.

## Chumvi

Katika mazao yote ambayo yaelekea yaliongezeka kwa wingi katika kipindi hiki tukichunguzacho, chumvi inachukua nafasi ya pekee kabisa. Chumvi ilipatikana katika machimbo ya chumvi ya Sahel, Ethiopia na Afrika Mashariki, ikiwa katika umbo la mnara wa jiwe-la-chumvi. Chumvi hiyo ilipatikana pia kwa kukausha (kwa jua) maji ya bahari au mabwawa, kwa kukusanya mashapo, kama ilivyokuwa katika bonde la chini la Sine-Salum huko Senegal, na kwa kutumia mbinu za hali ya juu kabisa zilizotumia majivu ya mmea uitwao '*xerophilous*'; usindikaji wa chumvi kutokana na mmea huu ulifanywa kwa kugema utomvu wake. Hata hivyo chumvi ya bahari au ya Sahara ilikuwa bora kiasi kwamba ilisafirishwa masafa marefu; katika baadhi ya maeneo, hasa Ethiopia, katika vipindi fulani fulani chumvi ilitumiwa kama fedha halali. Chumvi ilikuwa bidhaa iliyowapatia watu wa pwani pato kubwa zaidi kuliko samaki wabichi au waliokaushwa na pia kombe. Waliitumia chumvi kubadilishia bidhaa za aina mbalimbali walizohitaji. Si rahisi kufikiria uwezekano wa watu kutamakani katika maeneo ya chumvi ya delta ya Niger - na pengine hii ilitokea katika kipindi tukichunguzacho bila ya kupatikana kwa vyakula na zana kutoka bara; lakini





28.4 *Uzalishaji chumvi* - Walata: Msafara wa Wasebhra wa Idjul (Mauritania), wakiwa wemebeba mizigo ya minata ya chumvi, Bernard Nântet)

kutokana na zao hili la chumvi wakazi hawa waliweza kupata chakula na mahitaji hayo bila matatizo yoyote. Halikadhalika wakazi wa Sahara walipata nafaka waliyohitaji kwa kubadilishana na watu wa Sahel, wao wakawapa chumvi kutoka katika migodi yao na badili yake wakapata nafaka. Kwa hiyo, mfano huu wa chumvi unatuchukua toka kwenye masuala ya kuzingatia teknolojia hadi kwenye mgawanyo wa mahiasili usiosawa na biashara inayotokana nao.

### *Aina mbalimbali za biashara*

Kufanya biashara kwa njia ya kubadilishana bidhaa, katika maeneo makubwa au madogo, kuliendelea kwa muda mrefu, hususani kwa bidhaa muhimu kama vile chumvi au chuma, vito

vya thamani, na mapambo pia; vitu ambavyo wakati mwingine vilisafirishwa masafa marefu.

Katika karne tano tunazozichunguza, biashara ilindelea sana, kilele chake kikiwa ni biashara ya kuvuka jangwa la Sahara. Kabla ya kuanza kwa kipindi hicho, kulikuwako tayari biashara ya ndani ambayo, bila shaka ilihusiana na bonde la Nili na Afrika Kaskazini, na hasa kufuata kiungo cha Ziwa Chad, Kawar na Fezzan. Lakini ukweli unabaki kwamba tangu mwaka 800 biashara hii iliongezeka sana. Mfumo wa zamani wa Sahara ambao ulihusu upelekaji dhahabu na vyakula Kaskazini ili kuvibadilisha na chumvi kutoka jangwani na bidhaa za viwandani kutoka Kaskazini, ulijengeka katika kipindi hiki<sup>4</sup>. Biashara hii ilifika mbali. Katika karne ya tisa, ilipeleka maelfu ya shanga huko Igbo-Ukwu, kituo ambacho kilikuwa ni kiungo cha bahari upande wa kusini. Katika mwaka 1100 biashara ilifika katika kingo za misitu katika eneo ambalo baadaye lilitwa Gold Coast. Kupanuka kwa biashara kuvuka jangwa la Sahara kulikuwa na athari katika maendeleo ya asasi za kidola huko kaskazini kuanzia Moroko mpaka Misri, kati ya karne ya nane na karne ya kumi na moja. Hali kadhalika kusini, kati ya Atlantiki na Ziwa Chad katika karne hizo hizo.

Dhima ya Ethiopia katika biashara ya kimataifa ilififishwa na mabadiliko makubwa katika misafara mikubwa ya Bahari ya Hindi kati ya karne ya sita na karne ya nane. Kinyume na hali hiyo, pwani ya Afrika Mashariki ilipata umaarufu zaidi. Katika karne ya nane kulikuwa na dalili za uingizaji wa biashara kutoka pwani za Somalia mpaka zile za kusini mwa Msumbiji<sup>5</sup>. Dhahabu, pembe, mbao na watumwa vilisafirishwa nje pamoja na bidhaa nyingine za anasa, ambapo bidhaa zilizoingizwa zilikuwa ni pamoja na baadhi ya vitu vya anasa, kama vile shanga na nguo. Ijapokuwa haya yalikuwa ni mabadilishano yasiyowiana, lakini bado yaliyapa msukumo maendeleo ya mawasiliano ya ndani. Katika jimbo la Limpopo biashara hii iliongezea kasi au kuimarisha uundaji wa maeneo makubwa ya kisiasa.

Hata hivyo, ukuaji wa kiuchumi na upanuzi wa kibiashara kwa jumla haukulingana katika jamii zote za bara la Afrika. Afrika ya Kaskazini ilikuwa kwenye kitovu cha uchumi wa ulimwengu na teknolojia za huko ziliendelea kutoka dunia moja ya Kiislamu hadi nyingine, kama vile ilivyokuwa katika kuenea kwa upandaji wa miwa au mitende. Misri, Tunisia, na miji mikubwa ya Kiislamu katika Moroko ilikuwa vituo maarufu vya viwanda vilivyopeleka zaidi bidhaa zao Afrika Magharibi. Afrika Mashariki ilihusiana na uchumi wa ulimwengu wa Kiislamu, China, India na Indonesia<sup>6</sup> kwa namna changamani.

Kwa upande mwingine, kulikuwa na maeneo ambayo yaliathiriwa kidogo sana au pengine hayakuathiriwa kabisa na biashara ya kimataifa. Afrika ya Kusini na ya Kati ni mifano inayoonyesha hali hii, ijapokuwa katika Afrika ya Kati kulianzishwa ukanda wa kibiashara uliokuwa na kituo chake katika ukanda wa shaba na kuwa na uhusiano usio wa moja kwa moja na Bahari ya Hindi kabla ya mwaka 1100. Biashara ilihusu kubadilishana bidhaa kutoka sehemu tofauti na kutoka kwenye machimbo ya chumvi. Kwa kuzingatia vipindi vilivyofuata baadaye tunaweza kusema chumvi na chuma, samaki na nguo za rafia, mafuta ya mawese na mbafu,

na mbao zilizotiwa rangi nyekundu ni bidhaa zilizotumika katika mabadilishano. Kwa ujumla misafara ilitokea kaskazini kuelekea kusini, ikizivuka kanda za kiekolojia.

Maeneo ya mrima ya Afrika Mashariki yanaendelea kuwa tatizo. Hakuna dalili za bidhaa

4 Taz. Sura 11, 12, 14., 15 na 27 ya juzuu hili.

5 Taz. Sura 21 na 24 ya juzuu hili.

6 Taz. Sura 1 na 21 ya juzuu hili.

kutoka nje zinazoonekana huko na kwa jinsi hiyo imehitimishwa kuwa hapakuwa na uhusiano wa kibiashara kati ya sehemu za mrima na pwani inayopakana nazo. Hata hivyo, ni vigumu kuamini kuwa ilikuwa hivyo. Huenda bidhaa zilizoingia zilikuwa ni chumvi na nguo, na zilizopelekwa nje zilikuwa ni pembe na ngozi. Uhusiano na biashara ya kimataifa ulikuwa si wa moja kwa moja.

Katika Ethiopia, biashara baina ya majimbo inaelekea iliendelea, na yamkini ilienea kufuata uhamisho wa makao makuu ya ufalme kwenda Lasta. Kusini mwa Ethiopia, hususani Shoa, kulianzishwa uhusiano na sehemu za nje na kituo cha wafanya biashara wa Kiislamu waliosafirisha bidhaa nje kupitia pwani ya 'pembe'<sup>7</sup>. Falme za Kiukristo za Nili zilifanya biashara na Waislamu ambao waliyapatia mahakama ya Kinubia na matabaka ya nasaba bora bidhaa za kutoka Mediteraniaaaaa - nguo, mvinyo, nafaka - kwa kubadilishana na watumwa. Mahitaji ya watumwa yalisababisha kuanza kwa uhusiano na eneo la bonde la Chad na majimbo yaliyo kusini ya Nubia.

Kwa jumla, hali ya bara ilikuwa mpya ikilinganishwa na kipindi kilichopita. Kujumuika kwa Sahara, Afrika Magharibi, pwani ya mashariki na sehemu za Zimbabwe na Transvaal na kuwa katika mfumo mmoja wa biashara ya kibara lilikuwa jambo jipya kama yalivyokuwa maendeleo ya vituo vya biashara za kanda. Ilikuwa ni vigumu kukosekana mfumo wa biashara, angalau wa kikanda, ijapokuwa hali kama hiyo iliwezekana katika maeneo machache kama vile Namibia na jimbo la Cape, misitu ya Liberia (na labda maeneo ya jirani), mrima wa Afrika Mashariki na baadhi ya maeneo ya savana kati ya Kameroun na White Nili. Msukumo wa biashara ulikuwa ni zao la kwanza la kuanzisha makazi na urekebishaji wa mifumo ya uzalishaji mali. Kwa hiyo kipindi hiki kinawakilisha mwanzo ambao kwao uchumi na biashara uliendelea kwa nguvu zaidi na uchangamano kati ya mwaka 1100 na 1500. Vituo vya kanda viliendelea na kuunganika, ijapokuwa katika hali ya chini, vikilinganishwa na maeneo ya biashara ya kimataifa. Na kufikia mwaka 1500 hivi yamkini hapakuwa na eneo lolote katika bara ambalo bado lilibaki nje ya kanda ya kibiashara.

## *Jamii na mamlaka*

Historia ya kijamii ya bara la Afrika bado inahitaji kuandikwa, hasa kuhusu kipindi kinachotuhusu. Hatujui lolote kabisa kuhusu maisha ya wakati huo, mipango kuhusu udugu na kuishi na kufanya kazi pamoja. Hata historia ya asasi zilizounda mahusiano haya, kama vile familia, jamaa, kaya, ndoa na makundi ya kazi, haijulikani.

Mgawanyo wa kazi na matokeo yake ndivyo vinavyoonekana zaidi. Kati ya karne ya saba na ya kumi na moja, palikuwa na maendeleo makubwa yaliyosababisha jamii kugawika katika matabaka. Mafarakano makubwa ya hali za kiuchumi na kijamii - matabaka yalijitokeza katika kipindi hiki, ijapokuwa hatujui kwa hakika jinsi mahusiano baina ya matabaka yalivyofanya kazi. Katika Afrika ya Kaskazini, Nubia na Ethiopia, tunaona mamwinyi ambao ardhi waliyokuwa nayo bila kujali waliipataje, inakuwa ndio msingi wa nguvu yao. Katika Afrika ya Kaskazini umwinyi huu ulizingiwa na wateja (*mawali*) wengi, pamoja na watumwa, watumishi, wafanyakazi au askari wapiganaji. Mamwinyi hawa walikuwa na nguvu ya kutosha hata mara nyingine kuweza kuwafanya maafisa wa serikali

7 Taz. Sura 20 ya juzuu hili.

wawanyenyekee. Inawezekana kuwa kwa namna fulani hali ilikuwa vivyo hivyo katika Nubia au Ethiopia.

Kusini zaidi mambo si wazi sana, wachunguzi wangali katika majadiliano makali kuhusu kuwoko kwa matabaka yaliyo wazi katika kipindi hiki. Majadiliano makali zaidi yanahusu kuwoko kwa matabaka ya kiamali kama yale ambayo zyalikuwoko katika maeneo fulani ya Afrika katika karne za baadaye. Uchunguzi wa hivi karibuni sana wa huko Afrika ya Maghribi unaelekea kudai kuwa matabaka ya kiamali ni ya hivi karibuni tu, wala si ya zamani za kale.

Katika Afrika ya Kati hali ilitofautiana na ile ya Kaskazini na Maghribi mwa bara. Katika maeneo ya Ikweta kulikuwa na dalili za mgawanyo wa kazi. Watu walioishi misituni pengine walijihusisha na vikundi vya wawindaji (hususani Wambilikimo) kwa kupatia chakula (kama mizizi, mihogo, viazi n.k.) na vifaa vya chuma, ili kubadilishana na nyama na asali. Kutegemeana huku kulisababisha ongezeko kubwa la ziada ya vyakula. Inadhaniwa kuwa hali hii haikuwepo kabla ya vyakula vya mizizi (mihogo, viazi) kuwa ni zao la msingi au kabla ya kipindi ambapo ongezeko la wakulima lilikuwa kubwa kiasi cha kuwabughudhi wawindaji. Mpango huu ulikuwa tofauti kabisa na ule wa uhusiano wa kawaida wa kibiashara baina ya wakulima wa misituni na wavuvi waliowapatia samaki, vyungu na chumvi kwa kubadilishana na vyakula vya mbogamboga.

Mahali ambayo mabadiliko yasiyokoma ya maendeleo ya kijamii yanaonekana vizuri ni mijini. Historia ya mwenendo wa ukuaji wa miji inafanyiwa marekebisho makubwa. Tangu zamani ilidhaniwa kuwa inahusiana na athari za Uislamu tu, kutokana na ukweli kwamba Waislamu walikuwa ni waanzilishi wakubwa wa miji kila mahali walipoishi. Lakini mafungu mengi ya miji yalikuwepo hata kabla ya Uislamu: hii imejidhihirisha sana Jenne-Jeno na kusini-mashariki mwa bara vile vile<sup>8</sup>. Mifano hii ni ya wazi zaidi kuliko ile inayohusu miji ambamo makazi ya Waislamu yalikuwa na dhima iliyoonekana waziwazi, kama vile Kumbi Salch, Tegdausti na Nyani. Itafaa sana kwa hali ya baadaye ya utafiti juu ya ukuaji wa miji ikiwa kazi bora zilizofanywa huko Ife, Igbo-Ukwu, Benin, Begho na Kong, zitafuatiliwa na kuendelezwa.

Vivyo hivyo, utafiti kuhusu Nyarko, pambazoni mwa maeneo ya dhahabu yaliyoko katika misitu ya Ghana ya sasa, sehemu ambayo tayari ilikuwa ni mji mwanzoni mwa karne ya kumi na moja, sharti uendelezwe. Inawezekana kuwa miji mingine mikongwe au vituo vya miji ambavyo vilijengwa katika kipindi hicho vitavumbuliwa.

Kinyume na madai ambayo yamefanywa na kazi nyingi za kiethnografia, Afrika Maghribi haikuwa ni mkusanyiko wa vijiji vilivyoletwa pamoja na makundi ya mbari yenye tamaduni na lugha tofauti za vijijini ambazo, licha ya kuishi pua na mdomo, hazikuweza kuathiriana. Baada tu ya kujitokeza, miji ikawa vituo vya kiutamaduni na ikaathiri maeneo makubwa yaliyoizunguka. Tofauti changamani za kiutamaduni na kijamii zilijitokeza kabla ya karne ya kumi na moja na hali hii ndiyo inayoaridhia kuingiliana kwa lugha kama vile Kimandingo, Kiyoruba na Kihausa.

Maswali mapya katika mkabala huo huo yanaweza kuulizwa kuhusu vituo vya biashara katika pwani ya Mashariki na Bukini, msingi wake wa Uafrika na Umalagasi na nafasi ya wafanyabiashara wa Kiislamu katika maendeleo yake<sup>9</sup>. Tayari imeanza kudadisiwa iwapo

8 Taz. Sura 24 ya juzuu hili.

9 Taz. Sura 21 na 25 ya juzuu hili.

utamaduni wa Kiswahili haukuwa ustaarabu wa kimji tangu mwanzo. Majadiliano bado kabisa yanaendelea. Vituo vya biashara vilivyokuwa katika nchi ambayo sasa ni Msumbiji vilikuwa ni viungo vya mawasiliano na bonde la Limpopo na vilichangia, ijapokuwa si moja kwa moja, katika ujenzi wa mji wa kwanza huko Mapungubwe. Mji huu ulikuwa pia ni kituo cha kiutawala ambacho kilikuwa ni hatua ya kwanza katika maendeleo ambayo yalikuja kuijenga Zimbabwe katika karne ya kumi na tatu<sup>10</sup> Uzingatifu wa namna hiyo hiyo pia ufanywe kuhusu eneo la Kaskazini mwa bara juu ya ujenzi wa miji muhimu ambayo kwayo utafiti kidogo sana umefanywa. Ingawa mathalan, maendeleo ya Fez, Kayrawan, Marrakesh na Rabat, yanaeleweka sana, kumefanyika utafiti kidogo sana kuhusu Sijilmasa, Tahert au Sadrata na eneo lote la Mzab, Ghadames, au juu ya miji ya Misri na Nubia ya bonde la Kati la Nili.

Baada ya kipindi kifupi cha umoja wa kinadharia chini ya utawala wa makhalifa wa mashariki, kulifuatia mfarakano wa kisiasa katika Afrika ya Kaskazini ainbao ulikuwa muhimu sana kwa hali ya baadaye. Himaya mpya zilianzishwa katika Misri na nchi ambayo sasa ni Tunisia; vilevile kuzunguka miji muhimu kama vile Fez, Tahert na Sijilmasa. Himaya hizo zilizidi kuimarika katika karne ya tisa na ya kumi. Hasa hasa zilitumia dhahabu ya Afrika Maghribi katika kuhakiki ubora wa sarafu yao. Polepole jambo moja lilianza kuonekana: msingi wa eneo la watawala wa kurithishana wa Kiislamu, hususani katika Tunisia, Misri na kisha, katika karne ya kumi na moja, katika Moroko ya Wamoravi, ulikuwa na dalili za kuimarika na kudumu. Himaya za Kiislamu, zikiwa na uamilifu na utawala wake zilianzishwa katika kipindi hiki. Hata hivyo, utawala ulibadilikabadilika na matukio kama vile maasi ya Abu Yazid au uvamizi wa Hilal au mashambulizi yaliyofanywa na Waukristo kutoka Sisilia mara kwa mara yaliuyumbisha udhibiti wa eneo hili.

Katika Afrika Maghribi mpango wa madola yamkini ulianza kabla ya mwaka 600, ijapokuwa uhanza kujulikana katika kipindi ambacho kimetaliwa hapa. Gao, Ghana na Kanem zinajulikana sana sasa, lakini kuna sehemu nyingine nyingi ambazo hazijafanyiwa utafiti wa kutosha hadi sasa na ambazo kwazo kuweko kwa mamlaka ya dola katika kipindi hicho si jambo la kutilia mashaka tena. Uchache wa habari umewafanya wataalam wengi waamini kwamba himaya za Kiafrika hazikuwa zaidi ya 'milki za kichifu' zisizo na utaratibu wowote dhahiri wa kiinchi; lakini hapana budi kujiuliza kuwa: je, ni sahihi kuliangalia suala la lfe kwa namna hiyo? je, tuamini kuwa mamlaka ya Sumaoro Kante, wa Soso, ambaye alikuwa akipigana na Ghana na *Mansaya* za Wamande hadi alipoangushwa na Sundiata katika karne ya kumi na tatu hayakuwa ni ya kidola bado? Na je, kulikuwa kukitendeka nini baina ya Wahausa na Wayoruba?

Katika Afrika Kaskazini-mashariki kipindi hiki kilishuhudia kilele cha falme za Kiukristo zilizoundwa katika karne ya sita, hususani katika schemu tatu za Nubia ambazo mafanikio yake ya kiuchumi na kitamaduni yalikuwa bado yanaonekana katika karne ya kumi na moja. Ethiopia ilikuwa katika hali mbaya zaidi, lakini ufalme ulijirekebisha wenyewe baada ya anguko la Aksum luko Lasta, katika karne ya kumi na moja. Wakati huo huo mamlaka kadhaa za Kiislamu zilianzishwa mashariki na Maghribi hadi kufikia maziwa ya Ethiopia<sup>11</sup>.

Utaratibu wa mamlaka tawala ya miji unaelekea kuwa ndio uliotumika katika pwani ya Mashariki. Katika nchi ambayo sasa ni Zimbabwe, kuliundwa dola katika karne ya kumi nyenye makao yake makuu Mapungubwe. Katika Afrika ya Kati au katika sehemu za mrima za

10 Taz. Sura 24 ya juzuu hili.

11 Taz. Sura 20 ya juzuu hili.

Afrika Mashariki, hapajaonekana bado dalili za maendeleo makubwa ya kinchi. Hata hivyo, inaweza kusemwa kuwa huko Sanga data zinaonyesha kuwepo kwa mabadiliko ya polepole kuelekea kwenye uchifu, mabadiliko ambayo yalionyesha kuimarika kuelekea mwishoni mwa karne ya kumi.

Nje ya maendeleo haya hatuna ushahidi wa moja kwa moja kuhusu suala la aina nyingine za utaratibu wa kisiasa. Katika mashariki na kusini mashariki ya Afrika, utaratibu wa kuhudumia makazi unaelekea kuonyesha namna fulani ya uongozi wa pamoja uliofanywa na viongozi wa makundi makubwa katika msingi wa itikadi ya udugu. Katika hali hiyo, hakukuwa na utawala wa kurithishana kinasaba, mfumo wa matabaka wala tofauti kubwa za kimaisha. Ukweli kwamba tunashughulika na sehemu zenye mkusanyiko wa majengo unadokeza uwezekano wa kuwepo kwa serikali ya pamoja. Data huenda inaonyesha vilevile kwamba eneo ambalo lilidhibitiwa kwa namna hii lilikuwa ni dogo, lililolingana labda na kijiji. Kwa jumla, mifano ya namna hiyo hiyo inaweza kupatikana katika kanda za misitu ya Afrika Maghribi.

### *Uwakilishi wa pamoja: dini, itikadi, Sanaa*

Sehemu kubwa ya bara la Afrika iligawika katika dini mbili zenye imani juu ya Mungu mmoja. Moja - uislam - ilikuwa ikiendelea kupanuka kati ya karne ya saba na ya kumi na moja, wakati ambapo nyingine ilipotea katika eneo zima la Afrika ya Kaskazini ambako ilikuwa imeanzishwa katika kipindi cha Warumi, na kuendelea kubaki katika Nubia na Ethiopia tu, ijapokuwa sehemu kubwa ya idadi ndogo ya Waukristo iliendelea kuwepo Misri<sup>12</sup>. Lieha ya warevu wao na kwa hakika walikuwa na majumba mengi ya watawa wakristo hawa, waliendelea kuishi bila kuwa na uhusiano na ulimwengu wa nje.

Athari ya Uislamu, dini na utamaduni, ambavyo vilienea kutoka Asia hadi Atlantiki na kuwatenga kwa muda mrefu watu weusi wa Afrika na watu walioko Kaskazini mwa Mediteraniai, ilipata nguvu zaidi na zaidi. Katika karne ya kumi, umoja wake ulitishiwa sana na ushindi wa muda wa imani ya Kifatimi-Kishia iliyoenea katika Afrika ya Kiislamu. Lakini katika karne ya kumi na moja majilio ya imani ya Kisunni yenye msingi wake katika sharia ya Kimaliki yalitokea. Kidogo kidogo kawaida za Kiislamu zilizipiku namna kongwe za kiutamaduni katika maeneo yaliyosilimishwa. Kwa jumla, inaweza kukisiwa kuwa hali hii ilifanyika katika eneo zima la Kaskazini mwa bara hadi kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na moja. Kulikuwa na majaribio ya namna hiyo katika Sahel na Pwani ya Mashariki, lakini katika sehemu hizi mbili, ushindi wa hakika wa kiutamaduni wa Uislamu ulikuja tu katika kipindi kilichofuata<sup>13</sup>.

Kwa wanahistoria ingekuwa ni muhimu zaidi kujua kulikuwa na dini gani ya Kiafrika wakati huo. Tunaweza tu kufafanua vipande vidogo vya habari tulivyonavyo kwa msaada wa zile habari zinazohusu vipindi vya hivi karibuni. Kuna mazungumzo mengi kuhusu 'waleta-mvua', kuhusu 'hirizi', kuhusu 'kusbudu mizimu', kuhusu 'sanamu', kuhusu 'uchawi'. Mkabala wa namna hii unaficha tu ujinga wetu; unasisitiza maendeleo ya mambo na kufutilia mbali suala la ukuo. Hapa tunakabiliana tena na pengo kubwa la utafiti kuhusu Afrika ya kale.

12 Taz. Sura 3 na 4 ya juzuu hili.

13 Taz. Sura 3,4 na 10 ya juzuu hili.

Mawazo ambayo yako kwenye tamaduni kuhusu mamlaka ambayo kwayo zinakabidhi uongozi wa jamii yanahusiana na itikadi tawala na miundo ya kiuchumi. Dini ziliweka mamlaka yote katika uelekeo wa kumtumikia Mungu na kwamba yeye ndiye mwenye kutoa mamlaka. Hata kama maimamu wa Tahert hawakufanana na wale wa Kifatimi, hata kama hawa wa pili walijiona kuwa karibu zaidi na Mungu kuliko maamiri wa Aghlabi au wana wa kifalme wa Idris, himaya zote hizi zilitawala katika jina la Mungu na Kurani. Hali ilikuwa ni hiyo hiyo katika uhusiano na Mungu kwa upande wa wafalme wa Nubia na Manegusi (watawala) wa Ethiopia.

Hali ilikuwa tofauti katika sehemu za Afrika ambazo zilibaki na uaminifu kwa dini yao na miundo yao ya kijamii na kiuchumi. Kuchipuka kwa madola makubwa kulisababisha kuzuka kwa dhana maalum ya mamlaka iliyoitwa kwa makosa 'ufalme mtakatifu'. Mwenye mamlaka alikuwa 'mtakatifu', yaani aliheshimiwa kwa kadiri alivyotimiza masharti ya sharia za kibinadamu zilizomhusisha na kundi (tabaka) lake, na pia aliogopwa na aliweza hata kukiuka tamrini za kawaida za maisha ya kijamii. Mfano unaotolewa sana kuhusu ukiukaji wa taratibu hizi za kimila ni uzinzi baina ya maharimu. Mtu huyo alikuwa na sauti juu ya mazingira na uzazi, juu ya mvua na maji, juu ya chakula, juu ya amani katika jamii, juu ya maisha ya jumuiya. Kwa makubaliano yasiyo na swali alikuwa na nguvu zilizokubaliwa kimya kimya, za kiungu zilizotokana na wadhifa wake au zilizopatikana kwa njia ya wingi wa dawa za kujikaga. Mama-malkia au dada za mfalme au hata mke wake walikuwa na dhima kubwa katika matambiko. Mfalme alitakiwa kutokuwa na kasoro ya kimaumbile, alitakiwa kutokuona damu au maiti. Alipaswa kutoonekana kwa watu na hivyo alijificha uso wake, akiwasiliana na wengine kwa njia ya wajumbe maalumu. Alikuwa peke yake na alitakiwa asionekane akinywa. Aliposhindwa vibaya mno katika kutimiza wajibu wake, hususani akiwa kama mwangalizi wa mavuno kwa kutokana na ubinadamu wake au kwa kuzidisha kiwango cha madaraka yake, aliweza kukabiliwa na kifo. Bila shaka hapa ndipo penye tofauti kubwa muhimu katika uendeshaji wa mamlaka kwa kulinganisha na ulimwengu wa Mediterania.

Kufanana baina ya mamlaka ya kisiasa ya Kiafrika aghalabu kulielezwa wakati uliopita kwa namna inayoshabihiana na chimbuko moja la Kifarao. Leo kuna msisitizo zaidi juu ya ukale na chimbuko lenye Uafrika la baadhi ya kaida za mamlaka haya ya kisiasa na uhusiano wake na ardhi, uwindaji, na mvua. Pia inaelekea kuwa mamlaka hizi ziliigana baadhi ya kaida zao zilizokuwa nzuri na zile za kuvutia; namna fulani ya kufanana ilitokana na kuigana na kubadilishana huku.

Itikadi ya kitawala (kitemi) yamkini ilihusishwa na uanzishaji wa ufalme huko Mapungubwe. Mfalme alikuwa mganga wa mvua aliyedhibiti mvua. Jambo hili lilikuwa nyeti, hususani katika nchi ambayo ilikuwa na mvua ya kubadililikabadilika na ambapo mazao yote yalitegemea mvua hiyo. Lakimi hatujui lolote kabisa juu ya mambo mengine yanayohusu itikadi hii.

Uchangamano wa vipengele vya mamlaka unajionyesha wazi katika kipindi kinachozungumziwa. Katika majimbo ambayo biashara ilikuwa ni kitu muhimu, mamlaka hayakuwa kimya kuhusu namna ya kuidhibiti; kwa mfano, yasingekuwa kimya kuhusu usonara wa dhahabu, shaba au chuma. Hivyo vipengele vya mamlaka vilijitokeza kwa namna ambayo haikuweko baina ya jamii ya wawindaji na wakusanyaji au katika kikundi cha kawaida cha wakulima.

Kwa jinsi hiyo hatimaye, historia ya mamlaka ya kisiasa katika Afrika na kwingineko inaelekea kuhusishwa zaidi na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii kuliko (kuhusishwa) na

itikadi. Ilipokuwa hapana budi, itikadi iliunda sababu na matambiko ambayo yalihatijika kwa ajili ya utengamano na uhalali wa viongozi. Kulitokea nini pale ambapo uhalali wa namna mbili ulikinzana ndani ya mtu huyohuyo, kama vile uhalali wa mfalme ambaye ni muumini wa Allah na uhalali wa ubingwa wa ufuaji chuma wenye kuhusishwa na waasisi wa kale wa kijasusi. Mamlaka ya kisiasa ya Kiafrika yalikalibiwa na mikinzano, wasiwasi, uchaguzi na mabadiliko ya taratibu kama ilivyokuwa katika maeneo mengine ya dunia. Jambo ambalo huenda ni la kushangaza zaidi ni wepesi wa kubadilika kwa kiitikadi ambao ulipunguza mikinzano na migogoro, na hasa kama madai ya Ukristo na Uislamu hayakuingizwa hapo.

Dini na itikadi zinajibu suala la kiutamaduni. Kazi za sanaa ni kielelezo cha suala hilo. Katika kiwango hiki, tofauti inawekwa kati ya makundi mawili ya jadi zinazotofautiana: jadi ya *oikumeni* na jadi ya sanaa za kijimbo.

Ulimwengu wa Kiislamu unaiweka sanaa chini ya maisha ya jumuiya ya Kiislamu. Kimsingi, matukio (ya kawaida) ya pamoja ni yale yafanywayo mahali ambapo jumuiya hukutana kusali na kutimiza masuala mengine ya imani. Msikiti uko katika kitovu cha ufundi wa ujenzi wa Kiislamu. Humo imo mitindo ambayo inatambulika mara moja na kila himaya ilipenda kuweka muhuri wake (wa kumbukumbu) katika msikiti wake. Katika suala hili Watulunidi wa Fustat, Waaghalabi wa Kayrawan, Wafatimi wa Mahdiyya au Kairo, Wamoravi wa Moroko au Hispania hawakuwa na tofauti. Lakini juu ya tofauti ndogondogo zilizokuwapo, msikiti ulibainisha umoja wa *umma* wa Kiislamu.

Katika karne hizi, umwinyi wa kiserikali, vita au biashara viliendelea mwonjo wa starehe ambayo inajibainisha waziwazi katika uzalishaji wa mavazi, pembe na miti iliyochongwa, utengenezaji wa vifinyange vitu vya kioo au mawe, na wakati mwingine michoro ya kutani. Katika uwanja huu, kama ilivyo katika uwanja wa ujenzi, kubadilishana maarifa kulitoka bara moja hadi jingine kufuatana na maendeleo ya mitindo.

Sanaa za Nubia na Ethiopia ambazo zilikuwa zimejitosheleza zaidi, ijapokuwa zilikuwa bado zinaazima kutoka kwenye bonde la Mediteraniaia, zimetajwa katika juzuu hili. Nafasi inayoshikiliwa na michoro ya kutani katika sanaa ya Kiukristo inatofautiana kabisa na kawaida za Kiislamu. Athari ndogo za moja juu ya nyingine - za sanaa ya Kiislamu juu ya sanaa ya Kiukristo, na kinyume chake, ni suala la kusionzwa. Ni ushahidi wa kinyume kwamba mitindo haikuenea moja kwa moja, bali ilifuatana na nguvu za kidini na kisiasa.

Kwa muda mrefu ilifikiriwa na kuandikwa kwamba hakuna sanaa za kuonekana za Kiafrika zilizobaki kusini mwa Sahara, baada ya miti-kifaa kilichodhaniwa kuwa bora kwa ajili ya kujieleza kisanaa kutostahimili uharibifu mbalimbali. Ugunduzi wa hivi karibuni umeliuliza upya swali hilo. Sanaa ya uchoraji wa maumbo katika vyombo vya udongo huko Nok, vyombo ambavyo viliendelea kutengenezwa kwa muda wa takribani kikwi kimoja tangu karne ya saba kabla ya enzi ya Ukristo, vilibainisha mara moja kina cha historia katika ukongwe wa sanaa ya Kiafrika. Kisha kulikuwa na mwelekeo wa kwenda moja kwa moja kwenye kazi za Ife katika karne ya kumi na mbili, wakati huo Ife ikionekana kama ni matokeo ya Nok. Kosa lilikuwa katika kuamini kwamba kulikuwa na kiasi kidogo tu cha sanaa katika kipindi baina ya matukio haya mawili, na kwamba kazi ya utengenezaji wa vyombo vya udongo ilikuwa Nigeria tu. Leo hii inafahamika kwamba Nok haikuwa ni jumuiya iliyojitenga, na kwamba vyombo vya udongo vyenye sanaa ya maumbo vilionekana hata nje ya eneo hilo. Na pia katika kipindi chetu sanaa ya utengenezaji wa sanamu za udongo iliendelezwa, na imeonekana kutoka Tegdausti hadi Jenne-Jeno katika Niger, kusini mwa Ziwa Chad na bila shaka sehemu nyingine, hususani Igbo-Ukwu. Katika hali ya sasa ya utafiti, inawezekana



kuzungumzia jadi ya eneo la juu ya Niger iliyojipambanua si katika sanaa ya vyombo vya udongo tu, bali pia katika vyombo vidogo vidogo vya ehuma. Katika mwaka 1100 hivi, vilionekana pia vyombo ya miti huko Bandiagara. Inawezekana kuwa vifaa vingi vya miti vilichongwa katika kipindi hiki lakini vimepotea.

Katika Afrika Maghribi yote, kulikuwa na sanaa ya ufinyanzi wa maumbo kwa kutumia udongo wa mfinyanzi uliochomwa. Utengenezaji huu pamoja na ufundi unaohusiana uliendelea kwa karne nyingi na inaelekea uhanza kabla ya karne ya saba. Inafaa pia kutajwa, ijapokuwa kwa kugusia tu, hali bora sana ya sanaa ya vyombo vya udongo vilivyoonyesha kuwa ni vya karne ya sita. Hivyo vinaweza kuchukuliwa kama ni ushahidi wa utamaduni uliosainbaa katika eneo pana la kijiografia.

Katika Afrika ya Kati vifaa vya miti vimegunduliwa. Kifaa kimojawapo ni namna ya juso la kofia (helmeti) inayowakilisha mnyama na kingine ni kichwa juu ya chungu; vyote viwili ni vya karne ya kumi, mwishoni. Vinaonyesha kuwa angalau kulikuwa na jadi ya uchongaji huko Angola. Katika Afrika Mashariki vijiumbo vichache vya ng'ombe vinavyosadikiwa kuwa ni vya kipindi hiki vinatoka White Nili na kuna vijiumbo vya watu kutoka Uganda. Katika Afrika ya Kusini kipindi cha majuso ya udongo katika Transvaal kilikwisha mwaka wa 800 hivi. Huenda kuna uhusiano hapa na baadhi ya vifaa vilivyopambwa kwa dhahabu vilivyopatikana Mapungubwe. Vifaa hivi, yamkini ni vitangulizi vya sanamu za nawe zilizotengenezwa baadaye katika Zimbabwe. Kwingineko katika kipindi chetu, kulikuwa na vijisanamu vya ng'ombe vya udongo wa mfinyanzi na vya wanyama wengine wa kufugwa, vikiwemo vya kike, katika sehemu za mapokeo ya 'Kopye ya Leopard'. Vitu hivi vinapatikana pia katika sehemu za kale za Zimbabwe (Gokomere). Katika Zambia ya kati (Kalomo), vijisanamu vya namna hiyo hiyo vya kipindi kinachochunguzwa hapa vinatofautiana sana kimitindo na vile vya Zimbabwe. Mwisho, isisahaulike kuwa utajiri mkubwa wa sanaa ya miambani katika Zimbabwe ulififia katika karne ya kumi na moja, ijapokuwa sanaa ya namna hiyo yenye mitindo isiyo changamani iliendelea kuwepo katika Namibia na Afrika ya Kusini, ambayo yamkini ilikuwa ni kazi ya Wasan.


Kutapakaa kwa maeneo ya mitindo mbalimbali ya sanaa hakujawa wazi bado na tuna habari za juu juu tu kuhusu dhima ya kazi hizi na madhumuni yake. Hata hivyo, inategemewa kwamba siku moja baadhi ya mapengo yatazibwa na kwamba tutaweza kuunda upya historia ya sanaa za kimapokeo za kanda mbalimbali.

## *Hitimisho*

Karne tano za kujiimarisha kwa jamii, kujiwekea misingi ya maendeleo katika maana pana kabisa ya neno hilo; karne tano ambazo zimedhihirishwa na namna bora zaidi ya matumizi ya mazingira na majilio ya Uislamu ambao, baada ya muda mrefu, ulibadilisha taratibu zilizokuwepo hapo nyuma. Karne tano za maendeleo yasiyowiana, ambamo baadhi ya maeneo ya bara hili yanajitokeza wazi katika kivuli cha vyanzo vya kimaandishi na kutuwezesha kuunda upya, kutokana na kazi za uvumilivu na ubunifu wa kimbinu, mabadiliko yanayotokea ya kiufundi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa. Karne tano ambamo pia baadhi ya maeneo yamebakia katika hali ya kutoeleweka vizuri, jambo ambalo linaonyesha kwamba hatujafanya kazi ya kutosha. Ni wazi kwamba katika kipindi hiki Afrika ya Kati ilikuwa ikijishughulisha na uundaji wa utaratibu wa kijamii-kisiasa: hali hii tunaweza kuihisi takribani kila mahali, lakini mara nyingi, ushahidi tuliona hautoshelezi.

Mchunguzi wa mambo wa mwaka ya 600 asingeweza kufikiria Afrika ingekuwa katika umbo ganikunako mwakaa 1100, japo kwa mtazamo mpana sana. Lakini mchunguzi wa mambo wa mwaka ya 1100 angeweza walau kukisia kwa mapana sana jinsi ambavyo hali ya watu katika bara hili ingekuwa katika mwaka wa 1500; na kwa upande wa utamaduni angeweza kukisia hali yake hata kufikia miaka ya 1990. Na huo ndio umuhimu hasa wa karne tano za ujenzi wa jamii ya bara hili ambazo zimcelezwa katika juzuu hili.

---



## Bibliografia

---

- Abdalla, A.M (mh.) (1964), *Studies in Ancient Languages of the Sudan*: (Khartoum: University Press).
- Abun-Nasr, J.M. (1971), *A History of the Maghrib* (Cambridge: Cambridge University Press).
- Abu Salih (1969), *The Churches and Monasteries of Egypt and some Neighbouring Countries*, tafs. B.T. Evetts na A.J. Butler. (Oxford: Clarendon Press, Reprint).
- Adams, W. Y. (1977), *Nubia - Corridor to Africa* (London: Allen Lane)
- Ahmad, A. (1975), *A History of Islamic Sicily* (Edinburgh: Edinburgh University Press)
- Alayi, J. F. A. na Crowder, M. (wah.) (1976), *History of West Africa* (London: Longman)
- Allison, P. (1968), *African Stone Sculpture* (London: Lund Humphries)
- Anquandaha, J. (1982), *Rediscovering Ghana's Past* (London: Longman)
- Arkell, A. J. (1961) *A History of the Sudan from the Earliest Times to 1820*, (London: Athlone Press)
- Armstrong, R. G. (1964), *The Study of West African Language* (Ibadan: Ibadani University)
- Arnold, T.W (1913), *The Preaching of Islam: A History of the Propagation of the Muslim Faith*, (London: Constable)
- Barreteau, D. (wah.) (1978), *Inventaire des études linguistiques sur les pays d'Afrique Noire d'expression française* (Paris: SELAF)
- Barth, H. (1857-9), *Travels and Discoveries in North and Central Africa* (New York: Harper. Reprint: London 1965)
- Beale, P.O. (1966), *The Anglo-Gambian Stone Circles Expedition 1964/65* (Bathurst: Government Printer)
- Biohaku, S. O. (1955), *The Origin of the Yorubas* (Lugard Lectures), (Lagos: Government Printer)
- Biobaku, S.O. (mh.) (1973), *Sources of Yoruba History* (Oxford: Clarendon Press - Oxford Studies in African Affairs)
- Bleek, W. H. I. (1862-9), *A Comparative Grammar of South African Languages* (Cape Town: Juta/London: Trubner)
- Bosch Vila, J. (1956), *Los Almoravidos* (Tetuan)
- Boulnois, J. na Hama, B. (1954), *L'Empire de Gao* (Paris: A. Maisonneuve)
- Bouquiaux, L. na Hyman, L. (Wah.) (1980), *L'Expansion Bantoue* (Paris: SELAF)
- Bovill, E. W. (1933) *Caravans of the Old Sahara* (Oxford: Oxford University Press)

- Bovill, E. W. (1958), *The Golden Trade of the Moors* (Oxford: Oxford University Press)
- Bryan, M.A. (1959), *The Bantu Language of Africa* (London: International African Institute)
- Bulliet, R.W. (1975) *The Camel and the Wheel* (Cambridge, Mass.: Harvard University Press)
- Buxton, D.R. (1971) 'The rock-hewn and other medieval churches of Tigre Province, Ethiopia', *Archaeologia (London)*, 103, uk. 33 - 100
- Cahen, C. (1971), *Les Peuples musulmans dans l'histoire médiévale* (Damascus: Institut Français de Damas)
- Cahen, C. (1983), *Orient et Occident au temps des croisades* (Paris: Augier)
- Camps, G. (1980), *Berbères, aux marges de l'histoire* (Paris: Editions des Hesperides)
- Carbou H. (1912), *La Région du Tchad et du Ouadaï* (Paris: Leroux)
- Chapelle, J. (1982). *Nomades noirs du Sahara: les Toubous* (Paris: L'Harmattan)
- Chavane, B. (1985), *Villages anciens du Takrur. Recherches archéologiques dans la vallée moyenne du Sénégal* (Paris: Karthala)
- Chittick, H.N. (1974), *Kilwa: an Islamic Trading City on the East African Coast* (Juz. 2). (Nairobi: British Institute in Eastern Africa)
- Christophe, L. A. (1977), *Campagne internationale de l'Unesco pour la sauvegarde des sites et monuments de Nubie. Bibliographie* (Paris: Unesco)
- Clark, J. D. (1968) *Further Paelaeo-anthropological Studies in Northern Lunda* (Lisbon: Publicacoes cult. Co. Diam. Angola, 78)
- Clark, J. D. (1970), *The Prehistory of Africa* (London: Thames and Hudson)
- Clarke, S. (1912), *Christian Antiquities in the Nile Valley: a contribution towards the Study of the Ancient Churches* (Oxford: Clarendon Press)
- Cline, W. (1937), *Mining and Metallurgy in Negro Africa* (McNasha: The American Anthropologist - General Series in Anthropology, no.5)
- Collett, D.P. (1979), *The archaeology of the stone walled settlements in eastern Transvaal, South Africa* (Johannesburg: Tasnifu; Chuo Kikuu cha Witwatersrand)
- Connah, G. (1975), *The Archaeology of Benin* (Oxford: Clarendon Press)
- Connah, G. (1981), *Three Thousand Years in Africa. Man and his Environment in the Lake Chad Region of Nigeria* (Cambridge: Cambridge University Press)
- Conti Rossini, C. (1928), *Storia d'Etiopia*, Juz.1. (Bergamo: Istituto Italiano d'Arti Grafiche)
- Cosmas, Indicopleustes (1968), *Topographie chretienne*, (taf). Wanda Wolska-Conus, (Paris: Le Cerf)
- Coulon, C. (1983), *Les Musulmans et le pouvoir en Afrique noire* (Paris: Karthala)
- Crabb, D. (1965), *Ekoid Bantu Languages of Ogoja* (London: Oxford University Press)
- Dachraoui, F (1981), *Le Califat fatimide du Maghreb. Histoire politique et institutions* (Tunis: Societe tunisienne d'edition)
- Dahl, O. C. (1951) *Malgache et Manjaan. Une comparaison linguistique* (Oslo: Egede-Instituttet)
- Dalby, D. (nh.) (1970), *Language and History in Africa* (London: Cass/New York: Africana Publ. Co.)
- Dark, P. J. C. (1973), *An Introduction to Benin Art and Technology* (Oxford: Clarendon Press)

- Deschamps, H. (mh.) (1970-1), *Histoire générale de l'Afrique noire* (Paris: Presses Universitaires de France)
- Deschamps, H. (1972), *Histoire de Madagascar* (Paris: Berger Levrault)
- Devic, L. M. (1983), *Le Pays des Zandjs ou la côte orientale d'Afrique au Moyen âge* (Paris: Hachette)
- Diagne, P. (1967), *Pouvoir politique traditionnel en Afrique occidentale* (Paris: Présence Africaine)
- Diehl, C. (1896), *L'Afrique byzantine* (Paris: Leroux)
- Diop, C.A. (1960), *L'Afrique noire précoloniale* (Paris: Présence Africaine)
- Diop, C. A. (1967), *Antériorité des civilisations négres: Mythe ou vérité historique?* (Paris: Présence Africaine)
- Domenichini-Ramiaramanana, B. (1976), *Le Malgache, Essai de description sommaire* (Paris) linguistiques africaines)
- Domenichini-Ramiaramanana, B na Domenichini, J.P. (1984), *Les Premiers Temps de l'histoire malgache, Nouvelle définition d'un champ de recherche* (Antananarivo)
- Doresse, J. (1971), *Histoire sommaire de la Corne orientale de l'Afrique* (Paris: Geuthner)
- Dozy, R. (1874), *Geschichte der Mauren in Spanien bis zur Eroberung Andalusiens durch die Almoraviden (711-1110)* (Leipzig: Grunow)
- Duby, G. (1978), *L'Atlas historique* (Paris: Larousse)
- Effah-Gyamfi, K. (1975), *Traditional History of the Borno State: an Archaeological Approach* (Legon)
- Egharevba, J. (1960), *A Short History of Benin*, (Ibadan: Ibadan University Press)
- Ehret, C. (1971), *Southern Niloitic History: Linguistic Approaches to the Study of the Past* (Evanston: Northwestern University Press)
- Ehret, C. (1974), *Ethiopians and East Africa: the Problems of Contacts* (Nairobi: East African Publishing House – Nairobi Historical Studies 3)
- Ehret, C. (1980), *The Historical reconstruction of Southern Cushitic Phonology and Vocabulary* (Berlin: Reimer – Kölner – Beiträge zur Afrikanistik 5)
- Ehret, C. na Posnansky, M. (wah.) (1982), *The Archaeological and Linguistic Reconstruction of African history* (Berkeley, Los Angeles and London: University of California Press)
- Epsterin, H. (1971), *The Origins of the Domestic Animals in Africa* (New York: Africana Publishing)
- Ervedosa, C. (1980), *Arqueologia Angolana* (Luanda: Ministério da educacao Nacional)
- Fagan, B.M. (1967), *Iron Age Cultures in Zambia, I: Kalomo and Kangila* (London: Chatto na Windus)
- Fagan, B.M, Phillipson, . W. na Daniels, S.G. H. (wah.) (1967-9), *Iron Age Cultures in Zambia* (London: Chatto na Windus)
- Fage, J. D. (1969) *A History of West Africa*, 4<sup>th</sup> edn. (Cambridge: Cambridge University Press)
- Fage, J.D. (mh.) (1978), *The Cambridge History of Africa*, Vol.II, c. 500 BC – AD 1050 (Cambridge: Cambridge University Press)
- Fage J. D na Oliver, R. A. (1970), *Papers in African Prehistory* (Cambridge: Cambridge University Press)

- Fagg, W. na List, H. (1963) *Nigerian Images* (London: P Lund Humphries/New York: Praeger)
- Fahmy, A.M (1950), *Muslimu Sea-power in the Eastern Mediterranean from the Seventh to the Tenth century AD* (London)
- Filesi, T. (1970), *China and Africa in the Middle Ages* (Lodon: F. Cass)
- Fisher, A, G. B. na Fisher, H. J. (1970), *Slavery and Muslim Society in Africa* (London: Hurst)
- Forde, D na Jones, G.I. (1950), *The Ibo and Ibibio Speaking Peoples of South-Eastern Nigeria* (London International African Institute)
- Fourché, L. (mh.) (1937), *Mapungubwe: Ancient Bantu Civilization on the Limpopo* (Cambridge: Cambridge University Press)
- Fraser, D na Cole, H.M. (1972), *African Art and Leadership* (Madison: Wisconsin University Press)
- Freeman-Greenville, G.S.P. (1962), *The Medieval History of the Tanganyika Coast* (Oxford: Oxford University Press)
- Freeman-Greenville, G. S. P. (1962), *The East African Coast: Select Documents from the 1<sup>st</sup> to the earlier 19<sup>th</sup> century* (Oxford: Clarendon Press)
- Gallais, J. (1984), *Hommes du Sahel, Espace, Temps et Pouvoirs* (Paris: Flammarion)
- Galloway, A. (1959), *The Skeleta; Remains of Bambandyanalo* (Mh). P.V. Tobias. (Johannesburg: University of the Witwatersrand Press)
- Gardner, G. A (1963), *Mapungubwe*, Juz II. (retoria: J.L. van Schaik)
- Garlake, P. S. (1973), *Great Zimbabwe* (London: Thames na Hudson)
- Gartkiewicz, P. M. (1982), 'An introduction to the history of Nubian church architecture', NC, I
- Gautier, E. F. (1937), *Le Passé de l'Afrique du Nord. Les siècles obscurs* (Paris: Payot)
- Gemery, H. A. na Hogendorn, J. (wah.) (1979), *The Uncommon Market: Essays in the Economic History of the Atlantic Slave Trade* (New York: Academic Press)
- Goiterin, S. D. (1967), *A Mediterranean Society Juz I, Economic Foundations* (Berkeley na Los Angeles: University of California Press.
- Golvin, L. (1957), *Le Maghreb central à l'époque des Zirides* (Paris)
- Goody, J. (1974), *Technology, Tradition and the State in Africa*, (Oxford: Oxford University Press)
- Gray, J. (1962), *History of Zanzibar from the Middle Ages to 1856* (London: Oxford University Press)
- Greenberg, J. H. (1955), *Studies in African Linguistic Classification* (New Haven: The Compass Publishing Co.)
- Greenberg, J. H. (1966) *The Languages of Africa* (The Hague: Mouton)
- Grottanelli, V. L. (1955), *Pescatori dell'Oceano Indiano* (Rome: Cremonse)
- Guidi, I. (1932), *Storia della letteratura etiopica* (Rome: Istituto per Oriente)
- Guthrie, M. (1967-71), *Comparative Bantu* (Farnborough: Gregg)
- Guthrie, M. (1948), *The Classification of the Bantu Language* (London; Oxford University Press)
- Hama, B. (1967), *Recherche sur l'histoire des Touaregs sahariens et soudanais* (Paris: Présence Africaine)

